

SIRI ZA MAOMBI



SIRI ZA MAOMBI

RohoYaUnabii.Org

2026 Edition
New Jersey, Marekani
Enendeni Mtandaoni Kote

Uhamishoni Ughaibuni Mtandaoni Majumbani

YALIYOMO

SURA YA 1.....	11
MUNGU ANATUALIKA TUOMBE.....	11
SURA YA 2.....	20
UHITAJI WETU WA MAOMBI.....	20
SURA YA 3.....	34
MUNGU HUSIKIA MAOMBI.....	34
SURA YA 4.....	39
MAOMBI NA USHINDI WA NAFSI.....	39
SURA YA 5.....	45
AHADI ZA MUNGU KUHUSU MAOMBI.....	45
SURA YA 6.....	50
MAOMBI YA IMANI.....	50
SURA YA 7.....	60
MAOMBI NA UTII.....	60
SURA YA 8.....	65
MAOMBI YALETAYO USHINDI.....	65
SURA YA 9.....	76
NGUVU YA MAOMBI.....	76
SURA YA 10.....	83
SABABU ZA KUOMBA.....	83
SURA YA 11.....	88
MAOMBI YALIYOJIBIWA.....	88
SURA YA 12.....	106
MAOMBI NA UAMSHO.....	106
SURA YA 13.....	111
WANAUME NA WANAWAKE WA MAOMBI.....	111
SURA YA 14.....	139
SALA YA KILA SIKU.....	139
SURA YA 15.....	149
MFANO WA YESU KATIKA MAOMBI.....	149

SURA YA 16.....	158
MAOMBI YA FARAGHA.....	158
SURA YA 17.....	168
MAOMBI KATIKA MZUNGUKO WA NYUMBANI.....	168
SURA YA 18.....	175
MAOMBI NA IBADA.....	175
SURA YA 19.....	183
MTAZAMO KATIKA MAOMBI.....	183
SURA YA 20.....	192
KUOMBA KATIKA JINA LA YESU.....	192
SURA YA 21.....	196
MWONGOZO WA BWANA KUPITIA MAOMBI.....	196
SURA YA 22.....	201
MAOMBI KWA AJILI YA WAGONJWA.....	201
SURA YA 23.....	210
MAOMBI KWA AJILI YA MSAMAHA.....	210
SURA YA 24.....	214
MAOMBI YA KUOMBEA WENGINE- MAOMBEZI.....	214
SURA YA 25.....	221
MALAIKA NA MAOMBI.....	221
SURA YA 26.....	227
MAOMBI BANDIA.....	227
SURA YA 27.....	233
SHETANI NA MAOMBI.....	233
SURA YA 28.....	239
MAOMBI KATIKA SIKU ZA MWISHO.....	239
SURA YA 29.....	244
FURSA YA MAOMBI -UPENDELEO WA MAOMBI.....	244
SURA YA 30.....	253
SALA YA BWANA.....	253
SURA YA 31.....	266
KUOMBA ILI KUTOA.....	266
SURA YA 32.....	275

'Maelfu ya watu wataoongoka kwenye ile Kweli, katika saa ya kumi na moja, AMBAO wataupata na kuukubali Ukweli wa injili na Neno la Mungu na KUHUIISHWA KWA harakati za Roho wa Mungu.—EGW'88 755 (1890). – {PrSw 212.2}.' Unabii huu unatimia, Maelfu ya watu duniani kote wanamwamini Mwenyezi Mungu na kubatizwa kwa siku moja, kwa wazi au kwa faragha, kupitia Machapisho Mtandaoni, Uhamishoni, Ughaibuni na Majumbani. Kazi ya Mungu haina mipaka, na hakuna anayeweza kuifanya mwenyewe, hata awe tajiri sana. Watu walioajiriwa, wasiojiajiri kwa kujikimu kimaisha, na wafanya biashara, kwa pamoja wataimaliza kazi hii. Tafsiri zetu ni kama Wikipedia, ukitaka kuongeza ladha, bila kupoteza maana, wewe boresha tu, ila usipoteze kabisa ujumbe na maana iliyokusudiwa. Kila Shuhuda imehaririwa mara tano, binafsi nimepitia mara tatu. Tumeweka Pointers (2Tsw 45.5) na kadhalika ili ujihakikishie mwenyewe na kutafsiri kwa ubora zaidi unapotaka. Sw inawakilisha, Kiswahili ambacho kinazidi kupanuka na kuwa moja za lugha za Wakristo wengi duniani. Ikiwa umemsaidia mtu mmoja kumjua Mungu, maisha yako hukuishi bure! Tunamshukuru sana Mungu kwa msaada Wake toka mwanzo. Tunawashukuru wasomaji, wanamaombezi, wadhamini, watafsiri, wahariri, washauri, wahakiki, marafiki, wajoli, ndugu katika safari ya kwenda mbinguni. Siku moja tutashangilia pamoja tutakapoona mavuno!

Watafsiri, Waombezi, Wahariri, Washauri, Wataalamu wa Teknolojia, na wengine wote

Grace Momadi-Masaka-Jersey, Marekani
 Niwaeli Mburuja-Kilimanjaro, Tanzania
 Daniel Masaka-Kisii, Kenya
 Cindy Tustch-Washington, Marekani
 Mbusi na Kwandu Mpagalushu- Tanzania
 Innocent Wayoga -Mbweni, Tanzania
 Paul Masaka-New Jersey, Marekani
 David Masaka-Pennsylvania, Marekani
 Sharon Ondieki -Nairobi, Kenya
 John Mugane-Boston, Marekani

Filbert Kalokaza-Katavi, Tanzania
 Michael Sokupa-Afrika ya Kusini
 Gerard Nyafanga- Shirati, Tanzania
 Ezekiel Ojwang-Tarime, Tanzania
 Pendo Makori-Momadi-Kibaha, Tanzania
 Judi Mmari Mugane-Siha, Tanzania
 Sandra Barron-Kentucky, Marekani.
 Kikundi cha Mbaki/Ngulus cha Maombi,
 Women Prayer Warriors of TAUS- US
 Musa Budodi-Shinyanga, Tanzania

Mpendwa Msomaji

Hitaji letu kuu katika huduma hii ya Machapisho Uhamishoni ni Roho Mtakatifu na kisha Maombi yako msomaji. Kumbuka pia huduma zingine za machapisho kwa kila lugha, taifa na jamaa. Toka mtambo wa kuchapa ubuniwe kule Ujerumani mwaka 1456 na Johannes Gutenberg, Neno la Mungu limefikia mabilioni, ila bado kuna makundi 6000 hayajafikiwa, angalia Joshugaproject.org na habari za '1040 window' Sambaza Biblia popote ndiyo kauli mbiu ya muumini, Sambaza Neno la Mungu kote. Jiunge nasi katika kuandika vitabu vya kuboresha watu, kutafsiri, kuhakiki, na kuhariri.

Ombi letu, usibadilishe chochote, tuite kama kuna kosa! Sasa umefika wakati wa kuandika vitabu ambavyo vinaendana na muktadha wa rasilimali, mazingira na utamaduni wetu, kwani ulimwengu wa Kikristo sasa umehamia Afrika na Amerika ya Kusini, ila hapa Kwetu Afrika Mashariki, nasit umekuwa wazito kuandika kuhusiana na Mada mbalimbali ambazo zinaendana na mazingira yetu kwenye mada za afya, lishe, mahusiano kati ya wazazi au ndoa, kilimo na mazao yake, kulea na kukuza watoto, aina za biashara zinazoendelea, hali ya kisiasa na muumini, utendaji wa kufikia watu na kujenga makanisa, nyimbo zetu na noti zake, haya yote tunayasoma na kuyaiga kwenye vitabu vya magharibi na ni mema tu, ila kama ulimwengu wa Kikristo umehamia kwetu, tunabidishwa pia kuwa waandishi kwasababu tunajua hali yetu katika kufikia wengine au kuboresha afya na jamii kuliko mtu mwingine.

Kwanini nyimbo zetu nzuri zenye ujumbe mzito zisichaguliwe kwa makini, nyimbo zilizoimbwa miaka 50 hivi na kuwekwa kwenye vitabu na kisha watu waimbe. Tenzi tunazoimba za magharibi ni nzuri, ila nasi hapa tuna nyimbo nzuri na zinaendana na utamaduni wetu, kwanini tusijiongeze nasi, ili tuongeze kwenye maktaba yetu ya nyingine, vizuri vingine, tuna wataalamu wengi wa nyimbo sasa.

Na hata vitabu vya watoto, tunahitaji watu wanaopenda watoto kufanya kazi hii kwa kushirikiana. Pia umefika wakati wa 'Reverse Mission' Watu wa Amerika

ya Kusini sasa ni wainjilisti kila mahali duniani, ikiwemo magharibi kama vile Ulaya, Marekani na hata, Asia, Australia, Mashariki ya kati na Afrika! Sisi Afrika tuna Wauminin wengi kuliko Amerika ya kusini, ila bado tunaona kwamba tupate waandishi kutoka nchi zenye Wakristo wachache kuliko sisi ambao hawaandiki kwa muktadha wa mazingira yetu na watoto wetu wanaona pengine wawe na vile vitu walivyo navyo nchi zile au wawe na mwenendo kama ule mfano mdogo sana utakuwa, wanafikiri sisi ni lazima tule kimchi, taco, panzit, empanada, manicotti, tortellini, sushi, falafel, je viwanda vyetu vinatengeneza vitu hivi? Kila chakula duniani kinacholimwa hufanana tu, ila jinsi ya kukitengeneza hupishana, Mwafrika atatumia ngano kupika ugali, Mhindi chapati, Mchina Noodle, Mzungu mkate nk.

Ni kweli Kiswahili ilikuwa lugha ya kuzungumzwa na siyo ya Maandishi, ila wakati umefika maandishi kuongezwa kwenye mambo mazuri! Naelewa kwamba si utamaduni wetu kuandika, ila si utamaduni wetu kufanya mambo mengi ambayo sasa tunayafanya! Nategemea tunaiga mazuri tu! Na si kila kitabu tunachoandika ni lazima kiuzwe, vingine ni vya kusaidia jamii, wewe hautaweza kuuza kila kitu katika dunia hii kama unataka kufanya uinjilisti au kubariki watu.

Watu husema utamaduni wa mtu mweusi ni kusaidia jamaa na ndugu zake wa damu tu na wala sio taasisi. Yawezekana ni kweli ila tuna la kujifunza kutoka kwa kila mwanadamu. Wenzetu wa Nigeria wameanza kuweka vitabu vyao vya kuboresha jamii mtandaoni ili watu wasome na kufaidika katika nyanja mbalimbali kama vile uchumba, maombi ya kuondoa laana kwenye familia nk. Joel Nanauka ni mfano mzuri katika Ulimwengu wa Kiswahili kwenye kuandika na kugawia watu ujuzi wake, tumevisoma vitabu vyake vizuri ambavyo ametubariki kwa mamilioni kwenye ujasiliamali nk. Ukiwa na chochote, hata ni kama senti mbili za Mjane, ujuzi, uwezeshaji wa aina fulani tafadhali usisite kutufikia na pia kama una ujuzi wa kuandika vitabu au kufundisha wengine kuandika vitabu, tuwasiliane, maana ulimwengu wa Kiswahili una umasikini wa Maandishi yaliyoandikwa kwa muktadha wa utamaduni, nyenzo, na maisha yetu ya kila siku, tunaomba mashauri pia kwa kutumia [Email: UhamishoniUghaibuniMtandaoni@gmail.com](mailto:UhamishoniUghaibuniMtandaoni@gmail.com) a Bwana atubariki sote ili tukae Ndani Yake

YESU Anarudi! Roho na Bibi arusi waseme, "Njoo!" Kila mtu asikiaye hili, na aseme, "Njoo!" Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uzima bila malipo. Amina. Njoo Bwana

Tunawatakieni Nyote Neema Ya MUNGU Wetu Mkuu Idumu Ndani Yenu. MARANATHA Wapendwa Wa BWANA! Amina

Kila mwanadamu anahitaji maombi. Hivyo sambaza kwa wote ili tuweze kujiombea na kuombeana! Masihi anakuja, tuombe tuwe tayari kwa zawadi

ipitayo zote! Kiswahili ni Lugha ya kumi duniani, na ya tatu kwa madhehebu mengi makubwa, hivyo ombea tafsiri ya maandiko ya uzima wa milele ya Kiswahili.

Mwisho wa sura za kitabu hiki kuna nukuu toka Runinga Ya Upendo kuhusu Maombi na zaidi ya Mafungu 500 ya Maandiko yamenukuliwa humu.

UTANGULIZI

Maandiko yanatuhimiza "Kuomba bila kukoma." Hii haimaanishi kwamba tunapaswa kutumia muda wetu wote tukiwa tumepiga magoti yetu katika maombi rasmi. Bali Inamaanisha kwamba lazima tuishi na kumtumikia Bwana wetu katika mazingira ya maombi yaliyo rasmi na yasiyo rasmi (structured and unstructured), rasmi na yasiyo rasmi, yenye mpangilio na yasiyo na mpangilio, mfano ukiwa kwenye basi au safarini, ukiwa kanisani, ukiwa kibarواني, si lazima kufumba macho, ila unaweza kuinua mikono mitakatifu kama Biblia inavyoshauri ikibidi, usifikiri ni mambo ya dini fulani kuinua mikono, (1Tim2:5) hapana! Hutakuwa umekiuka sheria za Biblia kuinua mikono bila hasira wala magomvi, hata hivyo polisi akisema "mikono juu -hands up" si utaiweka? Basi kwanini usimwinulie mikono Mungu na kujisalimisha Kwake! Siku moja Kila goti litapigwa na kila ndimi itakiri Masihi ni Bwana).

Maombi ni njia ya mawasiliano kati ya nafsi zetu na MUNGU. MUNGU huzungumza nasi kupitia Neno Lake; tunamwitikia Neno Lake anapozungumza kupitia maombi yetu, Naye hutusikiliza daima. Hatuwezi kumchosha au kumlemea kwa mawasiliano yetu ya mara kwa mara ya mioyo yetu kwenda kwa moyo Wake.

Tumefika kwenye nyakati ngumu. Matukio katika ulimwengu wetu yanamuhitaji kila mfuasi wa Kristo kuwa na bidii kabisa ndani ya uhusiano wake na MUNGU. Ili kuimarisha uhusiano huu na kutosheleza mahitaji yetu ya kihisia, kijamii, kimwili, kiuchumu na pia kiroho, ni lazima tujifunze nguvu ya maombi. Ni lazima tumsihi Bwana, kama wanafunzi wa awali, tukisema, "Bwana, tufundishe kuomba." Lazima tuseme kwa kusesitiza kwamba katika nukuu hizi zote maneno mawili yametumika kupita maneno mengine nayo ni Maombi ya Dhati, na Maombi ya bidii na Usongo/ari (Earnest and Fervent Prayers). Hebu yafanyie utafiti maneno haya yana maana gani maana yamesheheni tunu kubwa, ambayo mpaka leo nasi tunajikanyaga kuyaelewa, tunaomba utuandikie na kutumegea nasi upatapo uelewa wake tafadhali sana! Mara nyingi watu hujiita Prayer Warrior wakimaanisha wapigana vita vya maombi, Sura ya Maombezi au Intercessory Prayer ni muhimu kujua tunapojiita jina Hili.

Kwamba MUNGU yuko radhi na yuko tayari kusikiliza na kujibu maombi yetu yanayotoka moyoni katika hali zote ni jambo lenye kutia moyo sana. Yeye ni Baba Mwenye upendo ambaye huzingatia wakati mambo yanaenda vizuri na wakati mabadiliko ya maisha yanapotuletea mapigo yenye kuhuzunisha, yaliyo magumu, na ya kutisha. Tunapojisikia kulia, "MUNGU, uko wapi?" Ni vizuri kujua kwamba Yeye Yupo karibu kupitia kuomba.

Mwandishi mmoja alisema, "Mambo mengi zaidi hufanywa na maombi kuliko ndoto za ulimwengu huu." Hili ni kweli pia kwa kanisa. "Uamsho wa Ucha MUNGU wa kweli miongoni mwetu ndilo hitaji kuu na la msingi kuliko mahitaji yetu yote. Kuutafuta huu inapaswa kuwa kazi yetu ya kwanza" (Selected Messages 1:121). MUNGU atatenda kwa ajili yetu tunapoomba kile ambacho hangetenda ikiwa hatukumuomba. (The Great Controversy, 525 Nafikiri hii inahusika sana uchaguzi na pambano kuu linaloendelea). Tunakubali kwamba tunahitaji kumimiwa kwa Roho Mtakatifu. Lakini hili linaweza kutimizwa tunapoomba maombi ya binafsi na ya pamoja tu. Watu wa MUNGU wanapoomba kwa bidii, kwa unyofu, mmoja mmoja, na kwa pamoja, MUNGU atajibu. Mambo makubwa yatatokea ndani na miongoni mwa watu wa MUNGU. Na ulimwengu utahisi matokeo wakati Roho Mtakatifu anakuja kuwatayarisha na kuwawezesha watu Wake.

Tunaamini kitabu hiki kitapata mapokezi kwa utayari miongoni mwa watu wa asili zote. Tunaposoma nukuu teuzi kutoka kwa RYU- Runinga ya Upendo au Roho ya Unabii juu ya somo muhimu la maombi, tutaona mioyo yetu ikiwa imechochewa kwa njia ya ajabu na changamfu. Jumbe hizi zitagusa mioyo yetu. Tutasadikishwa kwa mambo mengi yaliyoelezwa nayo yatapata nafasi ndani ya mioyo yetu, na kuibua mwitikio wa kuafiki wito wa MUNGU juu ya maisha ya maombi ya kina na mengi zaidi.

"Baba yetu wa mbinguni anasubiri kutupatia ukamilifu wa baraka Zake. Ni nafasi ya upendeleo kwetu kunywa kwa kadiri tuwezavyo kutoka kwenye chemchemi ya upendo usio na ukomo/kifani. Kinachoshangaza ni kwamba tunaomba kidogo sana. MUNGU Yuko radhi na Yuko tayari kusikia maombi ya dhati ya watoto Wake walio wanyenyekevu zaidi Kwa nini wana na binti za MUNGU wanasita kuomba, wakati maombi ndiyo ufunguo katika mkono wa imani ili kufungua ghala za mbinguni, pahali ambako zimetunzwa hazina tele za Mweza wa Yote?" (Steps to Christ, 94, 95).

Binafsi tumebarikiwa sana kukisoma kitabu hichi, hebu nawe ubarikiwe na kuviombea vitabu hivi 30 kwenye mlolongo huu vipate mhakiki-Proofreader na wataalamu wanaohusika kuvisambaza

Maranatha!

Katika kutafsiri, Mambo manne ndiyo yalikuwa kwenye mawazo yetu kuliko mengine

- Yesu Anarudi Upesi, inabidi shuhuda hizi ziwafikie watu mapema na kutayarisha tabia zetu na siku moja tusikie "Vyema mtumishi mwema, ulikuwa mwaminifu."
- Kubeba ujumbe kama ulivyo ili watu wapate kilichonuiwa, bila kupotosha neno la Mungu
- Lugha rahisi itakayoweza kusomeka Kenya, Congo, Burundi, Rwanda, Uganda na Tanzania
- Sarufi ya lugha ya Kiswahili sanifu iwe imezingatiwa. Basi tuendeleo kuyazingatia mambo 7 Muhimu kwa Kila mwanadamu
 - o Tuwamini Mungu na Kumkiri, na kuziungama dhambi zetu
 - o Tusome Maandiko Matakatiifu Kila siku
 - o Tusali kila siku bila kukoma
 - o Tutafute Ushirika unaoafuata Maandiko
 - o Mtindo wa Maisha Uendane na Maandiko Matakatiifu ambayo tunakiri kuwa ni Pumzi na barua ya Mwenyezi Mungu
 - o Huduma za Jamii, kusaidia wenye mahitaji, yatima, Wajane, masikini, wapekwe nk
 - o Tuenende ulimwengu kote na kuwaambia watu ujumbe ili wajitayarisha na Ujio wa Masihi (Share!) na hili ndilo sisi tunafanya hapa, nawe tunaomba usambaze kwa magroup yako!

Maombi yetu makuu yawe matatu ni Roho Mtakatifu, kujisalimisha kwa MUNGU na kuwa ndani Yake Naye ndani yetu. Mungu Atufungulie milango ya kuenenda ulimwenguni mwetu kwa muktadha wa utamaduni wetu. Haya manne yatakuja na baraka zote tunazozihitaji tunaposoma

SURA YA 1

MUNGU ANATUALIKA TUOMBE

Kuunganishwa Na MUNGU Kupitia Mnyororo Wa Maombi—Ni jambo la ajabu kwamba tunaweza kuomba kwa ufanisi; kwamba wanadamu tusiostahili, tunaokosea tunayo nguvu ya kutoa maombi yetu kwa MUNGU. Je! Ni nguvu gani ya juu zaidi ambayo mwanadamu anaweza kutamani kuliko hii, - kuunganishwa na kuwasiliana na MUNGU asiye na ukomo? Mtu dhaifu, mwenye dhambi ana nafasi ya kuzungumza na Muumba Wake. Tunaweza kutamka maneno ambayo yanafika kwenye kiti cha enzi cha Mfalme wa ulimwengu. Tunaweza kuongea na Yesu tunapotembea njiani, Naye anasema, Mimi Niko mkono wako wa kuume. [Pr 7.1; Maombi Aya ya 1]

Twaweza kuzungumza na MUNGU mioyoni mwetu; tunaweza kutembea katika ushirika na Kristo. Tunapofanya kazi zetu za kila siku, tunaweza kuleta matamano ya mioyo yetu, shauku isiyoweza kusikiwa na sikio la mwanadamu; lakini neno hilo haliwezi kufa kimya, wala haliwezi kupotea. Hakuna kitu kinachoweza kuzamisha shauku ya roho. Kwani hii huinuka juu ya sauti za mitaani, juu ya kelele za mashine. Ni MUNGU Ndiye ambaye tunazungumza Naye, na maombi yetu husikilizwa. [Pr 7.2; Maombi Aya ya 2]

Omba, kisha; omba, nawe utapokea. Omba unyenyekevu, hekima, ujasiri na ongezeko la imani. Kwa kila ombi la dhati jibu litakuja. Linaweza lisije vile vile unavyotamani, au kwa wakati unaolitafuta jibu hilo; lakini litakuja kwa njia na kwa wakati ambao utakidhi mahitaji yako. Maombi unayotoa katika upweke, katika uchovu, katika majaribu, MUNGU hujibu, sio kila wakati kulingana na matarajio yako, lakini kila wakati kwa faida yako. (Gospel Workers, 258) [Pr 7.3; Maombi Aya ya 3]

Yesu hutualika Kuomba—Bwana anatupatia fursa ya kumtafuta Yeye binafsi katika maombi ya bidii, ya kutua mizigo ya roho zetu Kwake, bila kumficha chochote Yeye ambaye ametualika, "Njooi Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo. Nami nitawapumzisha." Oh, tunapaswa kushukuru sana kwamba Yesu Yuko tayari na ana uwezo wa kubeba madhaifu yetu yote na kututia nguvu na kuponya magonjwa yetu yote ikiwa itakuwa kwa faida yetu na kwa utukufu Wake. - (Medical Ministry, 16) [Pr 8.1; Maombi Aya ya 4]

"Njooi Kwangu," ndio mwaliko Wake. Ikiwa una wasiwasi na majaribu yoyote, wasilisha shauri lako mbele za Bwana.— (The Desire of Ages, 329) [Pr 8.2; Maombi Aya ya 5]

Mwambie Yesu Mahitaji Yako Yote—Kuna watu wachache wanaothamani au kuboresha fursa/upendeleo wa thamani wa maombi tuliopewa na Mungu. Tunapaswa kwenda kwa Yesu na kumwambia mahitaji yetu yote. Tunaweza kumpelekea wasiwasi, masumbufu au fadhaa zetu ndogo na mashaka pamoja na shida zetu kubwa. Chochote kinachojitokeza kutusumbua au kutufadhaisha, tunapaswa kukipeleka kwa Bwana katika maombi. Tutakapohisi kuwa tunahitaji uwepo wa Kristo katika kila hatua, Shetani atakuwa na nafasi ndogo ya kupenyeza majaribu yake. Ni juhudi yake ya makusudi kutuweka mbali na rafiki Yetu bora na mwenye huruma. Hatupaswi kumfanya mtu yeyote kuwa msiri wetu ila Yesu. Tunaweza kuzungumza Naye kwa usalama, yale yote yaliyomo ndani ya mioyo yetu. —(Testimonies for the Church 5:200, 201) [Pr 8.3; Maombi Aya ya 6]

Kufungua Moyo kwa Rafiki—Maombi ni kufungua moyo kwa MUNGU kama kwa rafiki. Sio kwamba tunamjulisha MUNGU jinsi tulivyo, lakini ili kutuwezesha kumpokea. Maombi hayamshushi MUNGU kwetu, bali hutupeleka Kwake. [Pr 8.4; Maombi Aya ya 7]

Wakati Yesu alipokuwa duniani, aliwafundisha wanafunzi Wake jinsi ya kuomba. Aliwaelekeza kuwasilisha mahitaji yao ya kila siku mbele za MUNGU, na kupeleka mizigo yao yote Kwake. Na uhakikisho aliowapa ni kwamba maombi yao yatasikilizwa, ni uhakikisho pia kwetu. - (Steps to Christ, 93) [Pr 8.5; Maombi Aya ya 8]

MUNGU hutukaribisha Kwenye Chumba Chake cha kuonana Naye (mtu mmoja Pamoja na Mungu au wengi)—Tunamwendea MUNGU kwa mwaliko maalum, na Yeye anasubiri kutukaribisha kwenye chumba Chake cha kuonana Naye (chumba cha Enzi!). Wanafunzi wa kwanza waliomfuata Yesu hawakuridhika na mazungumzo ya haraka haraka pamoja Naye njiani; wakasema, "Rabi,... Wewe unakaa wapi? ... Walikuja na kuona mahali alipokuwa akiishi, wakakaa pamoja Naye siku hiyo." Yohana 1:38, 39. Kwa hivyo hata nasi tunaweza kuingizwa katika mahusiano ya karibu sana, na kuwasiliana na Mungu na kuwa na ushirika pamoja na Yeye. "Yeye aketiye mahali pa siri pa Aliye Juu atakaa chini ya uvuli wa Mwenyezi." Zaburi 91: 1. Hebu wale wanaotamani baraka za MUNGU wabishe hodi na kungojea hapo kwenye mlango wa rehema na uhakikisho thabiti, wakisema, Kwa maana Wewe, Bwana, umesema, "Kila mtu aombaye hupokea; naye atafutaye hupata; na yeye abishaye atafunguliwa." (Thoughts from the Mount of Blessings, 131) [Pr 9.1; Maombi Aya ya 9]

Upendeleo uliotukuka—Wanapopatwa na matatizo, wanaposhambuliwa na vishawishi vikali, wao [watoto wa MUNGU] wana upendeleo wa maombi. Ni fursa iliyoinuliwa kwa kiasi gani! Viumbe vyenye ukomo, ambavyo ni vumbi na majivu tu, ambao wamekubaliwa kupitia upatanishi wa Kristo, kwenye chumba cha kuonana na Yeye Aliye Juu. Katika mazoezi kama hayo roho, huletwa katika ukaribu mtakatifu na MUNGU, na hufanywa upya katika maarifa, na utakatifu wa Kweli, na kuimarishwa dhidi ya mashambulio ya adui. - (An Appeal to Mothers, 24)

[Pr 9.2; Maombi Aya ya 10]

Ombi ni hitaji la Kiroho na ni Upendeleo—Wale ambao wanakiri kwamba wanampenda Kristo, hawajaelewa uhusiano uliopo kati yao na MUNGU, ... Hawatambui upendeleo wa hali ya juu na umuhimu mkubwa wa maombi, toba, na utendaji wenye nguvu wa maneno ya Kristo.-(Selected Messages 1:134) [Pr 9.3; Maombi Aya ya 11]

Maombi Yanatuwezesha Kuishi Katika Mwanga wa Uwepo Wake—Ni fursa yetu kuifungua mioyo yetu, na kuruhusu mwangaza wa jua wa uwepo wa Kristo ndani. Kaka yangu, dada yangu, itazame nuru. Ingia katika mawasiliano halisi, na ya kibinafsi na Kristo, ili uweze kuwa na ushawishi unaoinua na kuleta uamsho. Hebu imani yenu iwe imara, yenye usafi wa moyo na thabiti. Hebu shukrani kwa MUNGU ijaze mioyo yenu. Unapoamka tu asubuhi, piga magoti kando ya kitanda chako, na umwombe MUNGU akupe nguvu ya kutimiza majukumu ya siku hiyo, na kukabiliana na majaribu yake. Mwambie akusaidie kuleta katika kazi zako za siku uzuri wa tabia ya Kristo. Mwambie akusaidie kusema maneno ambayo yatawapatia wale wanaokuzunguka matumaini na ujasiri, na kukuvuta/kukusogeza wewe karibu na Mwokozi. (Sons and Daughters of God, 199)- [Pr 9.4; Maombi Aya ya 12]

Maombi yetu siyo mzigo kwa Mungu na Yeye hachoshwi nayo kamwe—Hakuna wakati au mahali ambapo hapafai kutoa sala/maombi kwa MUNGU. Hakuna kitu kinachoweza kutuzuia kuinua mioyo yetu katika roho ya maombi ya bidii na dhati. Katika umati wa watu mitaani, katikati ya biashara au shuguli, tunaweza kutuma maombi yetu kwa MUNGU na kuomba mwongozo Kwake, kama vile Nehemia alipofanya ombi lake mbele ya Mfalme Artashasta. Ushirika wa karibu unaweza kupatikana popote tulipo. Tunapaswa kufungua mlango wa moyo kila wakati na kutoa mwaliko wetu kwenda juu ili kumwalika Yesu aje kukaa kama mgeni wa mbinguni katika mioyo yetu. [Pr 10.2; Maombi Aya ya 13]

Ingawa kunaweza kuwa na mazingira yenye mawaa ya ufisadi na yaliyoharibiwa karibu nasi, sisi hatuhitaji kuivuta hewa hiyo kwenye mapafu yetu na kupata harufu hiyo iliyo na sumu inayoharibu afya zetu, lakini tunaweza kuishi katika hewa safi ya mbinguni. Tunaweza kufunga kila mlango dhidi ya mawazo yasiyo safi na mawazo yasiyo matakatifu kwa kuinua roho mbele ya MUNGU kupitia maombi ya dhati. Wale ambao mioyo yao iko wazi kupokea msaada na baraka za MUNGU watatembea katika hali takatifu kuliko ile ya dunia na watakuwa na mawasiliano/ushirika wa mara kwa mara na mbingu. [Pr 10.2; Maombi Aya ya 14]

Tunahitaji kuwa na maoni yakinifu zaidi juu ya Yesu na ufahamu kamili wa thamani ya Ukweli wa milele. Uzuri wa utakatifu utajaza mioyo ya watoto wa MUNGU; na ili kwamba hili liweze kutimizwa, tunapaswa kutafuta mafunuo ya Bwana/mbingu kuhusiana na vitu vya mbinguni. [Pr 10.3; Maombi Aya ya 15]

Hebu roho ivutwe na kwenda juu, ili MUNGU atupe pumzi ya anga la mbinguni. Tunaweza kukaa karibu na MUNGU ili kwamba katika kila jaribu lisilotarajiwa mawazo yetu yatamgeukia Yeye kama asili ya ua ligeukiapo jua (automatik!). [Pr 10.4; Maombi Aya ya 16]

Yaweke mahitaji yako, furaha yako, huzuni yako, wasiwasi wako, na hofu yako mbele za MUNGU. Hauwezi kumlelea Yeye; huwezi Kumchosha. Yeye anayehesabu nywele za kichwa chako hapuuzii yahasuyo mahitaji ya watoto Wake. "Bwana amejaa huruma na rehema" (Yakobo 5:11). Moyo Wake wa upendo unaguswa na huzuni zetu na hata tunapozitaja Peleka Kwake kila kitu kinachotatanisha akili. Hakuna kitu kikubwa mno kwake kitakachomshinda kubeba, kwani Yeye anashikilia ulimwengu. Anatawala juu ya mambo yote ya ulimwengu. [Pr 11.1; Maombi Aya ya 17]

Hakuna jambo lolote lile linalohusu mvurugiko wa amani mioyoni mwetu ambalo ni dogo sana Kwake Yeye kutambua. Hakuna sura katika uzoefu wa maisha yetu iliyo yenye giza mno Kwake Yeye kuisoma; hakuna mifadhaiko migumu sana Kwake kuweza kuiondoa Uhusiano kati ya MUNGU na kila nafsi umetofautiana na umesheheni kana kwamba hakuna mwanadamu mwingine duniani ambaye amewahi kushiriki utunzaji Wake, ni kama vile hakuna mtu mwingine duniani ambaye kwaye alimtoa Mwanaye mpendwa isipokuwa mtu huyu mmoja tu. - (Steps to Christ, 99, 100) [Pr 11.2; Maombi Aya ya 18]

Ladha ya Mbinguni—Jipumzishe kabisa mikononi mwa Yesu. Tafakari upendo Wake mkuu, na wakati unatafakari juu ya kujikana Kwake, kafara Yake isiyo na kikomo iliyotolewa kwa niaba yetu ili tuweze kumwamini Yeye, moyo wako utajazwa na furaha takatifu, amani tulivu, na upendo usioweza kuelezeka. Tunapozungumza juu ya Yesu, tunapomwita kupitia maombi, ujasiri wetu kwamba Yeye ni Mwokozi wetu sisi Mwenye upendo, utaimarika na tabia Yake itaonekana kupendeza na kuvutia zaidi.... Tunaweza kufurahia karamu nyingi za upendo, na tunapoamini kabisa kuwa sisi ni Wake kwa kuasiliwa, tunaweza kuwa na ladha ya mbinguni. Msubiri Bwana kwa imani. Bwana huuvuta moyo katika maombi, na hutupatia sisi kuhisi upendo Wake wa thamani. Tunao ukaribu Naye, na tunaweza kufanya ushirika mzuri na Yeye. Tunapata maoni dhahiri juu ya ukarimu na huruma Yake, na mioyo yetu inavunjika na kuyeyuka na kutafakari upendo ambao tumepewa moyoni. Kweli tunapata hisia ya Kristo anayedumu katika nafsi. Hakika tunahisi Kristo anayekaa ndani ya mioyo yetu, na tunajisikia kuwa nyumbani na Yesu. Ahadi hutiririka rohoni. Amani yetu ni kama mto, wimbi baada ya wimbi la utukufu linapita ndani ya moyo, na hakika tunakula chakula cha usiku pamoja na Yesu na Yeye pamoja nasi. Tunayo hisia ya kutambua upendo wa MUNGU, na tunatulia katika upendo Wake. [Pr 11.3; Maombi Aya ya 19]

Hakuna lugha inayoweza kuielezea, ni zaidi ya maarifa. Sisi ni wamoja na

Kristo, maisha yetu yamefichwa pamoja na Kristo katika MUNGU. Tumehakikishiwa kwamba wakati Yeye ambaye ni maisha yetu atakapotokea, ndipo pia nasi tutatokea pamoja Naye katika utukufu. Kwa ujasiri mkubwa, tunaweza kumwita MUNGU Baba yetu. - (The SDA Bible Commentary 3: 1147, 1148) [Pr 12.1; Maombi Aya ya 20]

Maombi Huleta kufanywa upya kwenye Maisha ya Kiroho — Maisha yetu yanapaswa kuunganishwa na maisha ya Kristo; tunapaswa kuchota kila wakati kutoka Kwake, tukila Kwake, Mkate ulio hai ulioshuka kutoka mbinguni, tukichota kutoka kwenye chemchemi iliyo safi kila wakati, ikitoa hazina zake tele. Ikiwa tunamuweka Bwana mbele ya macho yetu daima, tukiruhusu mioyo yetu kumshukuru na kumsifu, tutakuwa na hali mpya katika maisha yetu ya kidini. Maombi yetu yatachukua mfumo wa mazungumzo na MUNGU kama ambavyo tungezungumza na rafiki. Atazungumza na sisi kuhusu mafumbo na siri Zake. Mara nyingi kutatujia hisia nzuri ya kufurahisha ya uwepo wa Yesu. Mara nyingi tutahisi mioyo yetu ikiwaka ndani yetu anapokaribia kuzungumza nasi kama alivyofanya na Henoko. Pale ambapo uzoefu huu utakuwa halisia kwenye uzoefu wa maisha ya Mkristo, maisha yake yataonyesha unyenyekevu, utulivu, upole, na moyo wa kujishusha chini, ambao utaonekana kwa wale wenzake waliomzunguka kwamba alikuwa na Yesu na kujifunza kutoka Kwake (Christ's Object Lessons, 129, 130) [Pr 12.2; Maombi Aya ya 21]

Mahali pa Kukimbilia Ambapo pako wazi daima — Njia ya kuendea kwenye kiti cha enzi cha MUNGU iko wazi kila wakati. Hauwezi kupiga magoti kila wakati kwa ajili ya maombi, lakini maombi yako ya kimya yanaweza kuendelea kupaa juu kwa MUNGU kila wakati kwa ajili ya kuwezeshwa na kuongozwa. Utakapojaribiwa, kama itakavyokuwa, unaweza kukimbilia mahali pa siri pa Aliye Juu. Mikono yake ya milele itakuwa chini yako. - (In Heavenly Places, 86) [Pr 12.3; Maombi Aya ya 22]

Siri ya Nguvu za Kiroho—Maombi ni pumzi ya roho. Ni siri ya nguvu za kiroho. Hakuna njia nyingine ya neema inayoweza kuwa mbadala na halafu afya ya roho ikawa salama. Ombi huupatia moyo mawasiliano ya haraka na Chemchemi ya uzima, na kuimarisha mishipa na misuli ya uzoefu wa kidini. Puuzia zoezi la sala, au jihusishe na maombi bila mpangilio mara hapa, au pale kama unavyoona inafaa kwako, nawe utafanya mkono wako upoteze kumshikilia MUNGU. Nguvu za kiroho hupoteza ukali wake, na uzoefu wa kidini hukosa afya na nguvu. [Pr 12.4; Maombi Aya ya 23]

Ni jambo la kushangaza kwamba kwamba sisi wanadamu tusiostahili tunaweza kuomba kwa ufanisi, kwamba sisi wakosefu tuna uwezo wa kuwasilisha maombi yetu kwa MUNGU. Je! Ni nguvu gani ya juu zaidi ambayo mwanadamu anaweza kutamani kuliko hii,- kuwa na ushirika na MUNGU asiye na kikomo (wa milele)? Mtu dhaifu, na mwenye dhambi ana upendeleo wa

kuzungumza na Muumba wake. Tunaweza kutamka maneno ambayo yanafikia kwenye kiti cha enzi cha Mfalme wa malimwengu yote. Tunaweza kuzungumza na Yesu tunapotembea njiani, na Yeye anasema, Mimi Niko mkono wako wa kuume. (Messages to Young People, 249. [Pr 13.1; Maombi Aya ya 24])

Maombi ya Siri, moyo wa Dini (moyo wa mionjo ya kiroho)— Usipuuzie maombi ya siri, kwa maana ni moyo w mambo ya kiroho. Kwa maombi ya dhati, ya bidii omba usafi wa roho. Omba kwa bidii, kwa shauku, na kwa dhati, kama ambavyo ungeliomba endapo maisha yako yangekuwa hatarini. Endeleakubakia hapo kwenye uwepo wake kumtumainia MUNGU mpaka matamania ambayo hayawezi kutamkika yatakapozaliwa ndani yako kwa ajili ya wokovu, na ushahidi mzuri wa dhambi zilizosamehewa umepatikana. —(Spiritual Gifts 2:264) [Pr 13.2; Maombi Aya ya 25]

Kila Ombi la Dhati husikika— Bado wanafunzi walikuwa hawajajua rasilimali za Mwokozi ambazo hazina ukomo. Akawaambia, "Mpaka sasa hamkuomba chochote kwa Jina Langu." Yohana 16:24. Alielezea kuwa siri ya mafanikio yao itakuwa katika kuomba nguvu na neema kwa Jina Lake. Kwamba Atakuwepo mbele za Baba kuwaomba. Maombi ya mwombaji mnyenyekevu huwasilishwa Naye kama matamania Yake Mwenyewe binafsi kwa niaba ya roho hiyo. Kila ombi la dhati husikika mbinguni. Linaweza lisiwasilishwe kwa ufasaha; lakini ikiwa linatoka moyoni kwa dhati, basi litapanda kwenda mahali Patakatifu ambapo Yesu anahudumu, naye ataliwasilisha kwa Baba bila neno moja la kuudhi/utata, lenye kigugumizi, bali kwa Neno zuri na lenye harufu nzuri ya ubani wa ukamilifu Wake Mwenyewe. [Pr 13.3; Maombi Aya ya 26]

Njia ya unyofu na uadilifu sio njia isiyo na kizuizi, lakini katika kila shida tunapaswa kuona wito wa kutoa maombi. Hakuna mtu aliye hai ambaye anayo nguvu yoyote ile ambayo hajaipokea kutoka kwa MUNGU, na chanzo zinapotoka nguvu hizo kiko wazi na huru hata kwa mwanadamu aliye dhaifu zaidi. "Nanyi mkiomba lolote kwa Jina Kangu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mkiniomba chochote kwa Jina Langu, nitafanya." [Pr 13.4; Maombi Aya ya 27]

"Kwa Jina Langu," Kristo aliwaamuru wanafunzi Wake waombe. katika Jina la Kristo wafuasi wake wanapaswa kusimama mbele za MUNGU. Kupitia thamani ya kafara iliyotolewa kwa ajili yao, wana thamani machoni pa Bwana. Kwa sababu ya haki kupitia Kristo wanahesabiwa kuwa wa thamani. Kwa ajili ya Kristo, Bwana huwasamehe wale wamchao. Haoni ubaya wa mwenye dhambi ndani yao. Anatambua mfano wa Mwanawe ndani yao, ambaye wanamuamini. - (The Desire of Ages, 667) [Pr 14.1; Maombi Aya ya 28]

Malaika hunakili Maombi yetu na kutushawishi kuelekea yale yaliyo mema—Unapoamka asubuhi, je! Unahisi kukosa kwako msaada na hitaji lako la kuwezesha kutoka kwa MUNGU? na je, kwa unyenyekevu, kwa moyo wote

unamjulisha Baba yako wa mbinguni matakwa yako? Ikiwa ndivyo, malaika hunakili maombi yako, na ikiwa maombi haya hayajatoka nje ya midomo ya unafiki/feki, wakati umo katika hatari ya kutenda mabaya bila kujua na kutoa ushawishi ambao utasababisha wengine kutenda mabaya, malaika wako mlezi atakuwa kando yako, kukufundisha kilicho bora, kukuchagulia maneno, na kuathiri matendo yako. [Pr 14.2; Maombi Aya ya 29]

Ikiwa hauhisi hatari yoyote, na ikiwa hautoi maombi ya kusihi msaada na nguvu za kupinga vishawishi, hakika utapotea; kupuuza kwako wajibu kutaandikwa katika kitabu cha MUNGU mbinguni, na utakutwa umepunguka katika siku ile ya hukumu. - (Testimonies for the Church 3: 363, 364) [Pr 14.3; Maombi Aya ya 30]

Kama Musa, Twaweza Kufurahia Ushirika wa Karibu Na MUNGU— Mkono huo ulioumba malimwengu yote (universe), Mkono huo ambao unaishikilia milima ikae katika nafasi zake, unamchukua mtu huyu aliyeumbwa kutoka kwenye mavumbi, - mtu huyu mwenye imani yenye nguvu, - na kwa rehema inamfunika katika pango la mwamba, wakati utukufu wa MUNGU na wema Wake wote ukijidhihirisha mbele zake. Je! Kweli sisi Tunaweza kushangaa kwamba "utukufu unaopita ubora wote" ulioakisiwa kutoka kwa Yeye Aliye na Nguvu zote uliangaza usoni mwa Musa na mwangaza uliosheheni kiasi kwamba watu hawakuweza kuutazama kwa macho. Alama hii ya MUNGU iliyokuwa juu yake, ikamfanya aonekane kama mmoja wa malaika wanaoang'aa kutoka kwenye kiti cha enzi. [Pr 14.4; Maombi Aya ya 31]

Uzoefu huu, tofauti na uzoefu wa hapo awali ulionyesha kwamba MUNGU atasikia maombi yake, na kwamba uwepo Wake MUNGU utamhudumia kikamilifu, na jambo hilo likawa la thamani zaidi kwa Musa kama kiongozi kuliko elimu na mafunzo yote aliyopata kwa Wamisri, au mafanikio yake yote katika sayansi ya kijeshi ya Misri. Hakuna nguvu ya kidunia au ustadi au elimu/kisomo inayoweza kuchukua nafasi ya uwepo wa MUNGU. Katika historia ya Musa tunaweza kuona ushirika wa karibu sana na MUNGU ambao ni fursa ya kila mwanadamu kuufurahia. Kwa mkosaji ni Ni jambo la kutisha kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai.. Lakini Musa hakuogopa kuwa peke yake na Mwandishi wa sheria hiyo ambayo ilikuwa imenenwa na ukuu wa kutisha vile kutoka Mlima Sinai; kwani roho yake ilikuwa katika upatanifu wa mapenzi ya Muumba wake. [Pr 15.1; Maombi Aya ya 32]

Maombi ni kuufungua moyo kwa MUNGU kama tuufunguavyo kwa rafiki. Jicho la imani litamtambua MUNGU aliye karibu sana, na mwombaji anaweza kupata ushahidi wa thamani wa upendo wa Mungu na kujali Kwake. - (Gospel Workers, 34, 35) [Pr 15.2; Maombi Aya ya 33]

Omba kwa ujasiri mtakatifu—Mkikaa ndani Yangu na maneno Yangu yakikaa ndani yenu, basi, ombeni chochote mtakacho nanyi mtapewa. "Unapoomba,

wasilisha ahadi hii. Ni fursa ya upendeleo kwetu kumwendea Yeye tukiwa na ujasiri mtakatifu. Tukiwa dhati na wanyofu tunamwomba Aache nuru Yake iangaze juu yetu, Yeye Atatusikia na kutujibu. - (Child Guidance, 499) [Pr 15.3; Maombi Aya ya 34]

Mbingu iko wazi kwa ajili ya maombi yetu, na tunaalikwa kwenda "kwa ujasiri kwenye Kiti cha Neema, ili tupate rehema, na kupata neema ya kusaidia wakati wa shida." Tunapaswa kwenda kwa imani, tukiamini kwamba tutapata vile vitu tunavyoomba Kwake. - [Pr 15.4; Maombi Aya ya 35]

Ombea Mahitaji Yetu — Kila ahadi katika Neno la MUNGU huja pamoja na jambo/mada ya kuombea, ikileta Neno la Yehova lililoahidiwa kama uthibitisho kwetu. Baraka yoyote ya kiroho tunayohitaji, tumependelewa kuiomba kupitia Yesu. Tunaweza kumwambia Bwana, tukiwa na unyenyekevu wa mtoto, kile tunachohitaji haswa. Tunaweza kumwambia mambo yetu ya muda, tukimwomba mkate, mavazi na Mkate wa Uzima na vazi la haki ya Kristo. Baba yako wa mbinguni anajua kuwa unahitaji vitu hivi vyote, na umealikwa kumuomba juu ya vyote. Ni kwa kupitia Jina la Yesu ndiyo kila neema (feva) inapokelewa. MUNGU ataheshimu Jina hilo, na atakidhi mahitaji yako kutoka katika utajiri wa ukarimu Wake. —(Thoughts from the Mount of Blessing, 133) [Pr 15.5; Maombi Aya ya 36]

Omba na Amini — Unapomwomba Bwana akusaidie, Mtukuze Mwokozi wako kwa kuamini kwamba unapokea baraka Yake. Nguvu zote, hekima zote, ziko chini ya maamuzi/uwezo wetu. Wajibu wetu sisi ni kuomba tu. [Pr 16.1; Maombi Aya ya 37]

Tembea daima katika nuru ya MUNGU. Tafakari mchana na usiku juu ya tabia Yake. Ndipo utaona uzuri Wake na kufurahi kwa wema Wake. Moyo wako utaangaziwa na hisia ya upendo Wake. Utainuliwa kana kwamba umebebwana na mikono ya milele. Ukiwa na nguvu na nuru ambayo MUNGU hutoa, unaweza kuelewa zaidi na kutimiza mengi zaidi ya ulivyoona kuwa inawezekana hapo awali. - (The Ministry of Healing, 514) [Pr 16.2; Maombi Aya ya 38]

Songa mbele, ukimtumaini MUNGU— Tunapaswa kuhimizana katika imani iliyo hai ambayo Kristo amemwezesha kila muumini kuwa nayo. Kazi inapaswa kusonga mbele wakati Bwana akiandaa njia. Anapowapitisha watu Wake katika maeneo yenye dhiki, basi ni fursa yenye upendeleo kwao kukusanyika pamoja kwa ajili ya maombi, wakikumbuka kuwa vitu vyote vinatoka kwa MUNGU. Wale ambao bado hawajapitia nyakati ngumu, ambazo zinahusu kazi katika siku hizi za mwisho hivi karibuni watalazimika kupita kwenye matukio ambayo yatajaribu sana ujasiri wao kwa MUNGU. Ni wakati ambapo watu Wake hawaoni njia ya kusonga mbele, wakati Bahari ya Shamu iko mbele yao na jeshi likiwafuata nyuma yao, hapo ndipo MUNGU anawaamuru: "Songeni mbele." kwa kufanya hivi anazijaribu imani zao. Wakati uzoefu kama huo unakujia, songa mbele, ukimtumainia Kristo. Tembea hatua kwa hatua katika njia Anayoionyesha kwa

kuiwekea alama. Majaribu yatakuja, lakini songa mbele. Hii itakupa uzoefu ambao utaimarisha imani yako kwa MUNGU na kukufaa kwa huduma ya Kweli. —(Testimonies for the Church 9:273) [Pr 16.3; Maombi Aya ya 39]

SURA YA 2

UHITAJI WETU WA MAOMBI

Maombi ni ya Muhimu Maishani kama Chakula cha Kila Siku - Maombi ya kila siku ni muhimu sana katika ukuaji wa neema, na hata kwa maisha ya kiroho yenyewe, kama vile chakula cha kidunia kwa ustawi wa mwili. Tunapaswa kujizoesha kuinua mawazo kwa MUNGU katika sala. Ikiwa akili itamangamanga, lazima tuirudishe kwa bidii isiyokoma, hatimaye mazoea yatafanya mambo kuwa rahisi. Hatuwezi hata kidogo kujitenga mbali na Kristo hata kwa nukta moja na kisha tukawa salama. Tunaweza kuwa na uwepo Wake pamoja nasi katika kila hatua tunayopiga, lakini ni kwa kuzingatia tu masharti ambayo Yeye Mwenyewe ameyaweka. — (Messages to Young People, 115) [Pr 17.2; Maombi Aya ya 40]

Maombi ni muhimu Kiroho — Ingawa Kristo alikuwa amewapa wanafunzi Wake ahadi kwamba wangepokea Roho Mtakatifu, hii haikuondoa umuhimu wa maombi. Waliomba kwa bidii zaidi; waliendelea kusali kwa moyo mmoja. Wale ambao sasa wanahusika na kazi kuu ya kuandaa watu kwa ajili ya kuja kwa Bwana, wanapaswa pia kuendelea katika maombi. (Gospel workers, 371) [Pr 17.2; Maombi Aya ya 41]

Wanafunzi wa Yesu hawakutii onyo lililorudiwa "Kesheni na mkaombe." Mwanzoni walipata tabu sana kumwona Bwana na Mwalimu wao, aliyekuwa na tabia tulivu na kutunza hadhi, na sasa akipambana mieleka na huzuni ambayo ilikuwa zaidi ya ufahamu wa kawaida. Walikuwa wameomba waliposikia kilio kikuu cha Yule Anayetaabika. Hawakuwa na nia ya kumtelekeza Mola wao, lakini walionekana kupooza kwa usingizi ambao wangeweza kuutupilia mbali ikiwa wangeendelea kumwomba MUNGU. Hawakutambua umuhimu wa kukesha na kuomba kwa bidii ili kuhimili majaribu. - (The Desire of Ages, 688) [Pr 17.3; Maombi Aya ya 42]

Uzoefu wa wanafunzi katika Bustani ya Gethsemane una somo kwa watu wa Bwana leo Hawakutambua umuhimu wa kukesha na kuomba kwa bidii ili kuyapinga majaribu. Wengi leo wamelala usingizi mzito, kama walivyokuwa wanafunzi. Hawakeshi na kuomba wasiingie katika majaribu. Hebu nasi tusome na kuchunguza mara kwa mara kwa uangalifu sehemu hizo za Maneno ya MUNGU ambazo zinarejelea siku hizi za mwisho, yakionyesha hatari ambazo zitakuwa tishio kwa watu wa MUNGU. - (In Heavenly Places, 97) [Pr 18.1; Maombi Aya ya 43]

Maombi ni uhai wa roho — Maombi ni muhimu; kwani ni uhai wa roho. Maombi ya familia, maombi ya hadhara, haya yana nafasi yake; lakini ni ushirika wetu binafsi wa siri na MUNGU ndio unaodumisha maisha ya roho. (Education, 258) [Pr 18.2; Maombi Aya ya 44]

Maombi ni muhimu kwa Afya ya Kiroho - Mara kadhaa, kila siku, nyakati bora zenye thamani, zinatakiwa kuwekwa wakfu kwa njia ya maombi na kusoma Maandiko, hata ikiwa ni kwa kuweka maandishi kwenye kumbukumbu kwa kukariri, ili maisha ya Kidini/kiroho yaweze kuwepo ndani ya roho. Maslahi anuwai ya msingi ya kazi ya Mungu huja/hutupatia chakula cha kutafakari na nguvu kwa sala zetu. Ushirika na MUNGU ni muhimu sana kwa afya ya kiroho, na hapa tu kunaweza kupatikana ile hekima na uamuzi sahihi ambao ni muhimu sana katika kutekeleza majukumu ya kila siku. —(Testimonies for the Church 4:459) [Pr 18.3; Maombi Aya ya 45]

Kielelezo cha Yesu Huonyesha Umuhimu wa Maombi—Laiti wale wapazao sauti kuu za maonyo kwa ajili ya wakati huu wangelitambua wajibu wao kwa Mungu, wangeliona umuhimu wa maombi yenye bidii. Pale miji iliponyamazishwa tuli katika usingizi wa usiku wa manane, hali kila mtu alikuwa ameenda nyumbani kwake, Kristo, Mfano wetu, Alienda Mlima wa Mizeituni, na huko katikati ya miti yenye giza nene, alikuwa akikesha usiku mzima katika maombi. Yeye, Yule ambaye hakuwa hata na doa la dhambi,- nyumba ya hazina ya baraka; ambaye sauti Yake ilisikika katika mkesho wa usiku na kisha wanafunzi wakaogopa katika ile bahari yenye dhoruba, katika baraka ya ombi toka mbinguni; na ambaye Neno Lake linaweza kuwaita wafu kutoka makaburini mwao, Yeye Ndiye

aliyeomba dua kwa kilio kizito na machozi. Yeye hakuomba kwa ajili Yake Mwenyewe, bali kwa wale ambao alikuja kuwaokoa. Alipokuwa mwombezi, Akitafuta kwenye Mkono wa Baba Yake nguvu mpya, na akatoka akiwa amepewa nguvu mpya na kama mbadala wa mwanadamu, Alijitambulisha na mateso ya ubinadamu, na akawapa mfano wa umuhimu wa maombi. [Pr 18.4; Maombi Aya ya 46]

Asili Yake haikuwa na doa au uchafu wa dhambi. Kama Mwana wa Adamu, Aliomba kwa Baba, kuonyesha kwamba asili ya kibinadamu inahitaji msaada wote wa utokao kwa Bwana, ambao mwanadamu anaweza kupata ili aweze kujiandaa kwa majukumu na kutayarishwa kwa majaribu na mitihani ya maisha. Kama Mfalme wa Uzima, alikuwa na nguvu na MUNGU, na Aliwashindia watu Wake. Mwokozi huyu, ambaye aliwaombea wale ambao waliona hawakuwa na haja ya maombi, na kulia kwa ajili ya wale ambao hawakuona haja ya kutoa machozi, sasa Yuko mbele ya kiti cha enzi, kupokea na kuwasilisha kwa Baba Yake maombi ya wale Aliwaombea duniani. Mfano wa Kristo umewekwa kwetu ili tuufuate. Maombi ni muhimu katika utendaji kazi wetu kwa wokovu wa roho za watu. MUNGU peke Yake Ndiye anayeweza kutoa ongezeko la mbegu tunazopanda.—(Gospel Workers, 28, 29) [Pr 19.1; Maombi Aya ya 47]

Yesu alihimiza Umuhimu wa Maombi — Yeye [Yesu] aliwahimiza watu umuhimu wa sala, toba, kukiri, na kuacha dhambi. Aliwafundisha uaminifu, uvumilivu, rehema, na huruma, akiwaamuru wapende sio tu wale wanaowapenda, bali hata wale wanaowachukia, ambao wanawaudhi. Kwa hili alikuwa akiwafunulia tabia ya Baba, ambaye ni mvumilivu, Mwenye huruma, na Mwenye neema, si mwepesi wa hasira, na amejaa wema na Ukweli. - (Christian Education, 74) [Pr 19.2; Maombi Aya ya 48]

Maombi yalikuwa Muhimu kwa Danieli — Danieli alikabiliwa na vishawishi vikali ambavyo vinaweza kuwashambulia vijana wa leo; na bado alikuwa imara kwa mafundisho ya kidini aliyoyapokea hapo awali katika maisha. Alikuwa amezungukwa na vishawishi vilivyodhamiria kupotosha wale ambao wangelegalega kutoka katika kanuni na mwelekeo; ila Neno la MUNGU linamwonyesha kama mtu asiye na makosa. Daniel hakuthubutu kutumainia nguvu zake mwenyewe za maadili. Maombi yalikuwa ni ya lazima kwake. Alimfanya MUNGU kuwa nguvu yake, na hofu ya Mungu ilikuwa mbele yake kila wakati katika shughuli zote za maisha yake.- (Fundamentals of Christian Education, 78) [Pr 19.3; Maombi Aya ya 49]

Kukua kiroho kunategemea Maombi - Ikiwa kungekuwa na kusali zaidi kati yetu, mazoezi zaidi ya imani hai, na kutegemea kwa udogo sana maombi ya mtu mwingine kuwa kama mbadala wa uzoefu wetu, basi tungekuwa mbali zaidi na mahali tulipo leo katika akili ya kiroho. Tunachohitaji ni uzoefu wa kina, wa moyo na roho ya mtu binafsi. Ndipo tutaweza kusema ni nini MUNGU anafanya na jinsi anavyofanya kazi. Tunahitaji kuwa na uzoefuhai katika mambo ya MUNGU; na

sisi hatuko salama mpaka tutakapokuwa na uzoefu huo. Kuna wengine ambao wana uzoefu mzuri, na wanaweza wakuambie juu yake; lakini unapokuja kuupima, unaona kuwa huo sio uzoefu sahihi, kwani hauedani na Ukweli wa “Bwana asema hivi.” Ikiwa kuna wakati katika historia yetu tuliohitaji kujinyenyekeza roho zetu binafsi mbele za MUNGU, basi ni leo. Tunahitaji kumwendea MUNGU kwa imani katika yote yaliyoahidiwa katika Neno, na kisha tutembe katika nuru na nguvu zote ambazo MUNGU anatoa. - (The Review and Herald, Julai 1, 1909) [Pr 20.1; Maombi Aya ya 50]

Maombi Yanahitajika Kila Siku — Dini lazima ianze kwa kuusafisha na kuutakasa moyo, na inapaswa kulishwa kwa sala ya kila siku. —(Testimonies for the Church 4:535) [Pr 20.2; Maombi Aya ya 51]

Inafaa, na inawezekana kabisa, na pia ni muhimu sana kwetu, kuomba mara tatu kwa siku kama ilivyokuwa kwa Danieli. Maombi ni pumzi ya roho, msingi wa ukuaji wa kiroho. Nyumbani kwako, mbele ya familia yako, na mbele ya watendakazi wako, unapaswa kushuhudia Ukweli huu. Na unapobahatika kukutana na ndugu zako kanisani, waambie juu ya umuhimu wa kuweka wazi njia ya mawasiliano kati ya MUNGU na moyo wako. Waambie kwamba ikiwa watapata moyo na sauti ya kuomba, basi MUNGU Naye atakuwa na majibu ya maombi yao. Waambie wasipuuze majukumu yao ya kidini. Wahimize ndugu kuomba. Lazima tutafute ikiwa tutapata, lazima tuombe ikiwa tutapokea, lazima tubishe hodi ikiwa tutafunguliwa mlango. - (The Signs of the Times, Februari 10, 1890) [Pr 20.3; Maombi Aya ya 52]

Katika huduma ya ukuhani wa Kiyahudi tunakumbushwa kila wakati juu ya dhabihu na maombezi ya Kristo. Wote wanaokuja kwa Kristo leo wanapaswa kukumbuka kuwa neema Yake ni uvumba unaochanganyika na maombi ya wale wanaotubu dhambi zao na kupokea msamaha na rehema na neema. Hitaji letu la maombezi ya Kristo ni la kudumu. Siku kwa siku, asubuhi na jioni, moyo mnyenyekevu unahitaji kutoa maombi ambayo yatarudishiwa majibu ya neema na amani na furaha. “Basi, kwa njia ya Yesu, tumtolee MUNGU dhabihu ya sifa daima, hayo ni matunda ya midomo yetu ikitoa shukrani kwa Jina Lake. Msisahau kutenda mema na kusaidiana, maana hizi ndizo dhabihu zinazompendeza Mungu. (SDA Bible Commentary 6:1078) [Pr 21.1; Maombi Aya ya 53]

Kama wazee wa zamani, wale wanaodai kumpenda MUNGU wanapaswa kumjengea Bwana madhabahu popote pale wanapopiga hema zao. Ikiwa kuna muda ambapo kila nyumba ilipaswa kuwa nyumba ya sala, basi ni sasa. Akina baba na mama wanapaswa kuinua mioyo yao kwa MUNGU kwa dua ya unyenyekevu kwao na kwa watoto wao. Hebu baba kama kuhani wa nyumba, aweke juu ya madhabahu ya Mungu dhabihu ya asubuhi na jioni, wakati mke na watoto wanaungana katika maombi na sifa. Katika nyumba kama hiyo Yesu atapenda kukawia kawia kutoka hapo. [Pr 21.2; Maombi Aya ya 54]

Nuru takatifu inapaswa kuangaza kutoka katika kila nyumba ya Kikristo. Upendo unapaswa kufunuliwa kwa vitendo. Nao unapaswa kutiririka katika mahusiano yote ya nyumbani, ukijionyesha katika ukarimu, upole, na adabu iliyo na uungwana usio na ubinafsi. Kuna nyumba ambazo kanuni hii hufanywa, nyumba zile ambazo MUNGU huabudiwa na upendo wa Kweli hutawala. Kutoka kwa nyumba hizi sala ya asubuhi na jioni hupanda juu kwa MUNGU kama uvumba mtamu, na rehema Zake na baraka hushuka juu ya waombaji kama umande wa asubuhi. - (Patriarchs and Prophets, 144) [Pr 21.3; Maombi Aya ya 55]

Katika kumfuata Kristo, kumtazama Yeye Mwenye kuanzisha Na kuitimiza imani yetu, utahisi kuwa unafanya kazi chini ya jicho Lake, kwamba unaathiriwa na uwepo Wake, na kwamba Anajua nia zako. Katika kila hatua utauliza kwa unyenyekevu: Je! Hii itampendeza Yesu? Je! Itamtukuza MUNGU? Asubuhi na jioni sala zako za dhati zinapaswa kupaa kwa MUNGU kwa baraka na mwongozo Wake. Maombi ya Kweli humshika Mweza na hutupatia ushindi. Kwa magoti yake, Mkristo anapata nguvu ya kuyapinga majaribu. - (Testimonies for the Church 4:615, [Pr 21.4; Maombi Aya ya 56]

Kadiri makuhani walivyoingia asubuhi na jioni mahali Patakatifu wakati wa uvumba, dhabihu ya kila siku ilikuwa tayari kutolewa juu ya madhabahu mahali pa wazi. Huu ulikuwa wakati wa kuvutia/kupendeza sana kwa washiriki waliokusanyika mahali pa kuabudia. Kabla ya kuingia katika uwepo wa MUNGU kupitia huduma ya kuhani, walipaswa kushiriki kwa bidii katika kuuchunguza moyo na kukiri dhambi. Waliungana katika sala ya kimya, nyuso zao zikielekea pahali Patakatifu. Kwa hivyo maombi yao yalipaa pamoja na wingu la ubani, huku imani ikiwa juu ya sifa za Mwokozi aliyeahidiwa, na zikiwakilisha dhabihu ya upatanisho. Saa zilizowekwa kwa ajili ya dhabihu ya asubuhi na ya jioni zilizingatiwa kuwa takatifu, na zilionekana kama wakati uliowekwa wa ibada katika taifa lote la Kiyahudi. Na wakati wa baadaye Wayahudi walitawanyika/walitawanywa kama mateka katika nchi za mbali, na bado katika ile saa iliyowekwa wakaelekeza nyuso zao kuelekea Yerusalemu na kutoa maombi yao kwa MUNGU wa Israeli. Katika desturi hii Wakristo wana mfano kuhusiana na sala ya asubuhi na jioni. Wakati MUNGU analaani milolongo ya sherehe tu, bila roho ya ibada, Yeye huwaangalia kwa furaha wale wanaompenda, wakiinama asubuhi na jioni kutafuta msamaha wa dhambi walizotenda na kuwasilisha maombi yao kwa baraka zinazohitajika.—(Patriarchs and Prophets, 353, 354) [Pr 22.1; Maombi Aya ya 57]

Maombi Hutuunganisha na Mbingu — Wale ambao watavaa silaha zote za MUNGU na kutenga muda kila siku kwa ajili ya kutafakari na kufanya maombi na kusoma Maandiko wataunganishwa na mbingu kisha watakuwa na mvuto uokoao, unaobadilisha kwa wale wanaowazunguka. Mawazo mazuri, matamanio bora, ufahamu dhahiri kuhusu Ukweli na wajibu kwa MUNGU, haya yote yatakuwa yao. Watakuwa wana shauku ya kuwa na usafi wa moyo, nuru, na upendo, na

neema zote zinazozaliwa Mbinguni. Maombi yao ya bidii kabisa yatapenya ndani ya pazia. Watu hawa watakuwa na ujasiri mtakatifu mbele ya Yeye Asiye na Kikomo. Watahisi kuwa nuru na utukufu wa mbinguni vipo kwa ajili yao, nao watasafishwa, watainuliwa, na kuboreshwa na uhusiano huu wa karibu na MUNGU. Huo ndio upendeleo walionao Wakristo wa Kweli. (Testimonies for the Church 5:112, 113) [Pr 22.2; Maombi Aya ya 58]

Maombi Yanapaswa kuwa Shughuli ya Kwanza ya Siku (mkakati wa kwanza wa siku) —Jiweke wakfu kwa MUNGU wakati wa asubuhi; fanya hilli kuwa kazi yako ya kwanza kabisa. Hebu Ombi lako liwe, "Nichukue, Ee Bwana, niwe wako kabisa. Ninaweka mipango yangu yote miguuni pako. Nitumie leo katika huduma yako. Kaa nami, na kazi yangu yote ifanyike ndani Yako." Hili ni suala la kila siku. Kila asubuhi jiweke wakfu kwa MUNGU kwa ajili ya siku hiyo. Salimisha mipango yako yote, ili itekelezwe au isitelekezwe kulingana na hekima/majaliwa Yake yatakavyoongoza. Kwa namna hiyo unakuwa umeyatoa maisha yako mikononi Mwake MUNGU, na kwa njia hiyo utaumbwa/utafinywanga na kufanana zaidi na zaidi na maisha ya Kristo. - (Steps to Christ, 70) [Pr 23.1; Maombi Aya ya 59]

Shauku ya kwanza kabisa ya roho wakati wa asubuhi inapaswa kuwa kwa ajili ya uwepo wa Yesu. "Pasipo Mimi," Anasema, "huwezi kufanya lolote." Yesu Ndiye tunayemhitaji; Nuru Yake, Maisha Yake, na Roho Yake, inapaswa kuwa wetu daima. Tunamuhitaji kila saa. Na tunapaswa kuomba wakati wa asubuhi kwamba kama jua linavyoangazia nchi, na kuweka nuru katika ulimwengu, basi vivyo hivyo Jua la Haki liangaze katika vyumba vya ubongo na moyo na kutufanya sisi sote kuwa nuru katika Bwana. Hatuwezi kufanya jambo lolote bila uwepo Wake hata nukta moja. Adui anajua pale tunapoamua kufanya mambo bila Bwana wetu, naye yupo karibu, tayari tayari kuzijaza akili zetu na mapendekezo yake ya uovu ili tushindwe kuwa thabiti; lakini ni shauku ya Bwana kwamba kila wakati tuwe ndani Yake, na kwamba tuwe wakamilifu ndani Yake. - (My Life Today, 15) [Pr 23.2; Maombi Aya ya 60]

Maombi ni Wajibu—Hakuna kitu chenye kukuza afya ya mwili na roho zaidi kuliko roho ya shukrani na sifa. Ni jukumu letu chanya na muhimu sana kuipinga roho ya huzuni, na pia mawazo na hisia za kutoridhika kama ambavyo ilivyo muhimu kuomba. - (The Ministry of Healing, 251) [Pr 23.3; Maombi Aya ya 61]

Pale Ambapo Hatujisikii Kuomba ndio Maombi yahitajika zaidi — Pale ambapo hatujisikii kuwasiliana na Yesu, ndipo tunapopaswa kuomba zaidi. Kwa kufanya hivyo tutavunja mtego wa Shetani uliojificha, kisha mawingu ya giza yatatoweka, na tutahisi uwepo wa Yesu. - (Lift Him Up, 372) [Pr 24.1; Maombi Aya ya 62]

Giza Huwafunga Wale Wanaopuuza Maombi — Ikiwa Mwokozi wa wanadamu, Mwana wa Mungu, alihisi hitaji la maombi/kusali, Je hitaji la maombi ya dhati na ya bila kukoma halitakuwa zaidi kwa wanadamu dhaifu, wanyonge, wenye

dhambi na wanaokufa?. [Pr 24.2; Maombi Aya ya 63]

Baba yetu wa mbinguni anasubiri kutupatia ukamilifu na wingi wa baraka Zake. Tumependelewa kunywa kwa kadiri tuwezavyo kutoka kwenye chemchemi ya upendo Wake usio na mipaka. Inastaajabisha kwa kiasi gani kwamba tunaomba kidogo sana! MUNGU Yupo tayari kusikia maombi ya dhiti ya watoto Wake wanyenyekevu na walio na hali duni sana, na bado kuna kusitasita kwingi kwa upande wetu kumjulisha MUNGU matakwa yetu. Malaika wa mbinguni wanaweza kufikiria nini jamani kuhusu wanadamu hawa maskini wasiojiweza, ambao wanakabiliwa na majaribu, wakati moyo wa MUNGU wenye upendo usio na kikomo unawainamia wao kwa matamanio, Naye akiwa tayari kuwapa zaidi ya vile wanavyoweza kuomba au kuwazia, lakini bado wanaomba kidogo sana na wana imani ndogo sana? Malaika wanapenda kusujudu mbele za MUNGU; wanapenda kuwa karibu Naye. Wanaona kuwa karibu na MUNGU ndiyo furaha yao kuu; lakini wanadamu waishio chini duniani, ambao wanahitaji msaada mkubwa ambao unaweza kutolewa na MUNGU tu, wanaonekana kuridhika kutembea bila nuru ya Roho Wake, bila ushirika wa uwepo Wake. [Pr 24.3; Maombi Aya ya 64]

Giza la yule mwovu linawafunga wale wanaopuza kuomba. Majaribu ambayo adui anawanong'onezea yanawashawishi kutenda dhambi; na hii yote ni kwa sababu hawatumii fursa ambazo MUNGU amewapa katika wasaa mzuri wa mihadi Naye kwa maombi. Kwa nini wana na binti za MUNGU wanasita kuomba, wakati maombi ni ufunguo katika mkono wa imani ili kufungua ghala la mbinguni, ambako zimetunzwa hazina tele, zisizo na kikomo za Mweza wa Yote? - (Steps to Christ, 94) [Pr 24.4; Maombi Aya ya 65]

Epuka Kupuuzia Maombi-Angalia/chunga, ndugu, uhafifu wa kwanza wa [25] nuru yako, kupuuzia sala kwa mara ya kwanza, dalili ya kwanza ya usingizi wa kiroho. —(Testimonies for the Church 4:124) [Pr 24.5; Maombi Aya ya 66]

Unapaswa kukesha, ili shughuli nyingi za maisha haya zisababishe upuuzie maombi wakati unapohitaji zaidi nguvu ambayo maombi yanaweza kutoa. Hali ya utauwa ipo hatarini kwa roho kuzongwa/kubanwa zaidi na shughuli za maisha haya. Ni uovu mkubwa kuinyima roho nguvu na hekima ya mbinguni ambayo inakusubiri, ambayo ipo tayari kwa ajili yako unapoiomba. Unahitaji nuru ile ambayo MUNGU pekee Ndiye anayeweza kutoa. Hakuna mtu anayeweza kufaa katika kazi yake isipokuwa awe na hekima hii.- (Testimonies for the Church 5:560) [Pr 25.1; Maombi Aya ya 67]

Shetani Huwadanganya Wale Wasiofanya Maombi—(Wale ambao hawayachunguzi maandiko kwa bidii na kusalimisha kila shauku na kusudi la maisha Kwake Yule Asiyekosea, wote ambao hawamtafuti MUNGU katika maombi kwa ajili ya kuyajua mapenzi Yake, hakika watatangatanga mbali na njia sahihi na kuangukia kwenye hila/udanganyifu wa Shetani—((Testimonies for the

Church 5: 192) [Pr 25.2; Maombi Aya ya 68]

Majaribu Hufanya Maombi Kuwa ya Lazima — Nguvu inayopatikana katika kupeleka maombi kwa MUNGU, ikiunganishwa na juhudi za mtu binafsi katika kuifundisha na kuizoeza akili kufikiri kwa kina na kuwa mwangalifu, humwandaa mtu huyo kwa ajili ya majukumu ya kila siku na hufanya roho iwe na amani katika mazingira yote, haijalishi hali ni ngumu kiasi gani. Majaribu ambayo kila siku tunaanikwa katika mazingira yake hufanya maombi kuwa jambo la lazima. Ili tuweze kulindwa na uweza wa MUNGU kwa njia ya imani, shauku za akili zinapaswa kuelekezwa mbinguni daima katika maombi ya kimya ili kupata msaada, kupata nuru, kupata nguvu, kupata maarifa. Lakini fikra na maombi hayawezi kuchukua nafasi ya kuwa na juhudi katika kuboresha utumiaji wa muda vizuri na kwa uaminifu. Kazi na sala vyote vinahitajika katika kukamilisha tabia ya Kikristo. [Pr 25.3; Maombi Aya ya 69]

Lazima tuishi maisha ya pande mbili, maisha ya kufikiri na kutenda, maisha ya maombi ya kimya na kufanya kazi kwa juhudi.... Mungu anatutaka tuwe barua hai, zinazojulikana na kusomwa na watu wote. Roho inayomgeukia Mungu kwa ajili ya kupata nguvu, sapoti/msaada, uwezo, kwa maombi ya bidii ya kila siku, itakuwa na mawazo yaliyoboreshwa, uelewa dhahiri wa ile Kweli na wajibu, malengo ya juu kwenye utendaji, na kuendelea kuwa na njaa na kiu ya haki.—(God's Amazing Grace, 317) [Pr 25.4; Maombi Aya ya 70]

Sala Inahitajika Sasa Zaidi Kuliko Siku Za Awali — Lazima tuwe katika maombi sana ikiwa tutaendelea mbele katika maisha ya ucha Mungu (Kimungu/kimbingu). Wakati ujumbe wa ile Kweli ulipotangazwa kwa mara ya kwanza, ni kwa kiasi gani tuliomba. Ni mara ngapi sauti ya maombezi ilisikika chumbani, ghalani, kwenye shamba la bustani, au kwenye vijisitu. Mara kwa mara tulitumia masaa kadhaa kwa maombi ya dhati, wawili au watatu wakiwa pamoja walidai ahadi; mara nyingi sauti ya kulia ilisikika na kisha sauti ya shukrani na wimbo wa sifa. Sasa siku ya MUNGU (yaani hukumu ya mwisho) iko karibu kuliko wakati tulipoanza kuamini, na tunapaswa kuwa na bidii, kudumu kuwa na usongo/ari, na shauku nzito zaidi kuliko siku zile za mwanzo. Hatari zetu ni kubwa sasa kuliko hapo awali. Mioyo imefanywa kuwa migumu zaidi. Tunahitaji sasa kujazwa na roho ya Kristo, na hatupaswi kupumzika mpaka tuipokee. —(Testimonies for the Church 5:161, 162) [Pr 26.1; Maombi Aya ya 71]

Mtafute Bwana kwa Moyo Wote — Maombi yetu yanapaswa kujazwa na upole, huruma na upendo. Tunapotamani ufahamu wa kina na mpana zaidi wa upendo wa Mwokozi, tutamlilia MUNGU atupatie hekima zaidi. Ikiwa kulikuwa na haja ya sala na mahubiri yanayochochea roho, ni sasa. Mwisho wa vitu vyote umekaribia. Laiti tungeweza kuona kama tunavyotakiwa, umuhimu wa kumtafuta Bwana kwa moyo wote! Basi Tungelimpata. Hebu MUNGU na awafundishe watu Wake jinsi ya kuomba. —(God's Amazing Grace, 92) [Pr 26.2; Maombi Aya ya 72]

Maombi Sio upotezaji wa muda - Kila asubuhi chukua muda kuanza kazi yako na sala. Usifikirie kuwa kufanya hivi ni upotezaji wa muda; huu ni wakati ambao utaishi milele zote (enzi zote). Kwa njia hii mafanikio na ushindi wa kiroho yataletwa. Mwili wako utaitikia mguso wa Mkono wa Mwalimu na Bwana. Hakika baraka za MUNGU zinastahili na kufaa kuombwa, na kazi haiwezi kufanywa kwa usahihi isipokuwa ina mwanzo unaofaa. Mikono ya kila mfanyakazi lazima iimarishwe, moyo wake lazima utakaswe, kabla Bwana hajamtumia kwa ufanisi zaidi.—(Testimonies for the Church 7:194) [Pr 26.3; Maombi Aya ya 73]

Wachache Wanathamini Fursa ya Maombi — Tunapaswa kukesha na kufanya kazi na kuomba kana kwamba hii ndiyo siku yetu ya mwisho ambayo tumepewa/tutapewa. Je, maisha yetu yangekuwa na bidii nzito ya kiasi gani. Kwa Kwa ukaribu wa jinsi gani tungemfuata Yesu katika maneno na matendo yetu yote. [Pr 26.4; Maombi Aya ya 74]

Kuna wachache wanaothamini au kuboresha upendeleo wa thamani wa maombi. Tunapaswa kwenda kwa Yesu na kumwambia mahitaji yetu yote. Tunaweza kumpelekea wasiwasi wetu mdogo, dhiki zetu ndogo na hata shida zetu kubwa. Chochote kinachojitokeza kutusumbua au kutufadhaisha, tunapaswa kukipeleka kwa Bwana katika maombi Tutakapohisi kuwa tunahitaji uwepo wa Kristo kwa kila hatua, Shetani atakuwa na nafasi ndogo ya kuyapenyeza majaribu yake. Ni juhudi yake ya makusudi/anayokusudia, na anayoifanyia utafiti, kutuweka mbali na rafiki Yetu bora na Mwenye huruma. Hatupaswi kumfanya mtu yeyote kuwa msiri wetu ila Yesu. Tunaweza kuzungumza na kuwasiliana Naye kwa usalama kuhusiana yote yaliyo ndani ya mioyo yetu. —(Testimonies for the Church 5:200, 201) [Pr 27.1; Maombi Aya ya 75]

Maombi Zaidi yanahitajika Mwisho Unapokaribia — Mashirikisho ya vyama yataongezeka kwa idadi na nguvu tunapokaribia mwisho wa wakati. Mashirika haya yataunda ushawishi kinzani dhidi ya ile Kweli, na kuunda miungano mipya ya wanaojiita waumini ambao wataziweka kwenye vitendo nadharia zao za udanganyifu. Uasi utaongezeka. "Wengine watajitenga na imani, wakizingatia roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani" (1 Timotheo 4: 1). Wanaume na wanawake wameungana kumpinga Bwana MUNGU wa mbinguni, na kanisa bado halijaamka ili kuitambua hali hiyo kwa ukamilifu wake. Kuna haja ya kuwa na maombi zaidi, na bidii zaidi, kati ya wale wanaodai kuwa waumini. — (Selected Messages 2:383) [Pr 27.2; Maombi Aya ya 76]

"Kama kulikuwa na wakati ambapo tunapaswa kukesha na kuomba kwa bidii, ni sasa. Kunaweza kuwa na vitu vinavyodhaniwa kwa mwonekano wake kama vitu vizuri, ila bado vinahitaji kuchujwa kwa uangalifu na maombi mengi, kwani ni vifaa maalum vya adui kuongoza roho katika njia ambayo iko karibu sana na njia ya ile Kweli ambayo itakuwa ni vigumu kutofautisha na njia inayoongoza kwenye

utakatifu na mbinguni. Lakini jicho la imani linaweza kugundua kuwa inapotosha njia sahihi, ingawa sio rahisi kujulikana. Mwanzoni inaweza kudhaniwa kuwa ni sawa, lakini baada ya muda itaonekana kuwa tofauti sana na njia salama, mbali sana na njia inayoongoza kwenye utakatifu na mbinguni. - (Testimonies to Ministers and Gospel Workers, 229) [Pr 27.3; Maombi Aya ya 77]

Ushindi Kupitia Maombi ya Kila Siku — Kupitia maombi ya kila siku kwa MUNGU, watakuwa na hekima na neema kutoka Kwake ili kumudu mizozo na hali halisi ngumu za maisha, na kisha watatokeza kama washindi. Uadilifu na utulivu wa akili unaweza kuhifadhiwa kwa kukesha na kuomba tu. (Messages to Young People, 80) [Pr 28.1; Maombi Aya ya 78]

Ushindi Unahitaji Maombi ya Dhati — Ushindi haupatikani bila maombi mengi ya bidii, bila kuijishusha nafsi kwa kujinyenyekeza katika kila hatua. Nia au mapenzi yetu hayatakiwi kulazimishwa kushirikiana na wakala wa MUNGU/Mbingu, lakini ni lazima yatolewe kwa Bwana kwa hiari yetu wenyewe.- (Thoughts from the Mount of Blessing, 142) [Pr 28.2; Maombi Aya ya 79]

Lazima tutenge muda wa Kuomba — Tunapaswa sasa kujifunza/kujizoeza kumfahamu MUNGU kwa kuthibitisha ahadi Zake. Malaika wanatunza kumbukumbu ya kila sala ambayo ni ya dhati na ya kweli (Malaika wanarekodi kila ombi). Ni bora kujitenga/ kutupilia mbali matakwa yetu ya binafsi kuliko kupuuzia ushirika na MUNGU. Umasikini wa kilindi kirefu, kujikana nafsi kwa kwa hali ya juu, vikiwa na kibali Chake, ni bora kuliko utajiri, heshima, maisha rahisi, na marafiki bila kibali Chake. Ni Lazima tuchukue muda na kuutenga kwa kwaajili ya kuomba - (The Great Controversy, 622) [Pr 28.3; Maombi Aya ya 80]

Tumia muda mwingi katika Maombi — Tumia muda mwingi katika maombi na kutafuta kwa ukaribu Neno. Hebu wote wapate Ukweli halisi wa imani katika mioyo yao kwa kuamini kwamba Roho Mtakatifu atamwagwa kwao kwa sababu wana njaa halisi na kiu ya haki...Hebu kuwe na maombi zaidi, kuamini, na kupokea, na kufanya kazi zaidi pamoja na MUNGU. —(Testimonies for the Church 6:65, 66) [Pr 28.4; Maombi Aya ya 81]

Omba kuliko ulivyowahi kuomba maishani Mwako — Mtazame Yesu kwa urahisi/usahili na imani. Mkodolee macho Yesu mpaka roho izimie chini ya nuru iliyosheheni. Hatusali hata nusu. Hatuamini hata nusu ya tunavyopaswa kuamini, tunaambiwa. "Ombeni, nanyi mtapewa." Luka 11: 9 Ombeni, aminini, na imarishaneni. Ombeni kuliko mliyowahi kuomba maishani mwenu, kwamba Bwana atawawekea mkono Wake, ili muweze kufahamu marefu na mapana na kina na kimo, na kujua upendo wa Kristo, upitao ujuzi wote, ili mjazwe utimilifu wote wa MUNGU. —(Testimonies for the Church 7:214) [Pr 28.5; Maombi Aya ya 82]

Omba, ndiyo, omba kuliko ulivyowahi kuomba maishani mwako, ili

usidanganywe na hila za Shetani, ili usipate kuangukia ugonjwa wa moyo usiokuwa na usikivu, moyo usiojali, na wenye ubatili, na kisha ujihudhulishe kwenye majukumu na shuguli za kidini kwaajili tu ya kutuliza dhamiri yako mwenyewe. – (Testimonies for the Church 2:144) [Pr 29.1; Maombi Aya ya 83]

Ombeni Daima - "Ombeni kila wakati;" hiyo ni kwamba, Daima uwe katika roho ya maombi, na hapo ndipo utakapokuwa tayari kwa Ujio wa Bwana wako. – (Testimonies for the Church 5:235) [Pr 29.2; Maombi Aya ya 84]

Hitaji la Maombi mengi – Sasa kuna hitaji la maombi mengi. Kristo anaamuru, "Ombeni bila kukoma;" yaani, ielekeze akili yako juu kwa MUNGU, Chanzo cha nguvu zote na ufanisi. – (Testimonies to Ministers and Gospel Workers, 510) [Pr 29.3; Maombi Aya ya 85]

Shughuli si mbadala wa Maombi (shughuli nyingi hayachukui nafasi ya Sala) – kadiri shughuli zinavyoongezeka na watu kufanikiwa katika kufanya kazi yoyote kwa MUNGU, kuna hatari ya kutegemea mkakati na njia za kibinadamu. Kuna tabia ya kuomba kwa udogo na kuwa na imani kidogo. Kama wanafunzi, tuko katika hatari ya kupoteza machoni mwetu utegemezi wetu kwa MUNGU wetu, na kujikita kuona shuguli zetu ndiyo mkombozi. Tunahitaji kumtazama Yesu daima, huku tukitambua kuwa ni nguvu Yake ndiyo ambayo hutenda kazi Wakati tukiendelea kufanya bidii kwa ajili ya wokovu wa wapotevu, lazima pia tutenge wakati wa kutafakari, kwa maombi, na kujifunza Neno la MUNGU. Ni ile kazi pekee iliyotekelezwa kwa maombi mengi, na kutakaswa kwa uwezo na sifa ya Kristo ndiyo mwishowe itathibitisha kuwa imefaulu kwa ufanisi kwa mema. - (The Desire of Ages, 362) [Pr 29.4; Maombi Aya ya 86]

Maombi yanahitajika ili kuwa na misimamo isiyopendwa -Inahitaji ujasiri wa kimaadili, uthabiti, kuazimia, uvumilivu, na maombi mengi kukaa katika upande ule tofauti usiopendwa na wengi. Tunashukuru kwamba tunaweza kuja kwa Kristo kama wale maskini wanaoteseka walivyomjia Kristo hekaluni. - (Evangelism, 240). [Pr 29.5; Maombi Aya ya 87]

Maombi yanahitajika ili Kufanya Kazi ya MUNGU-Maombi mengi na mazoezi ya nguvu ya akili ni muhimu ikiwa tungependa tuwe na utayari wa kuifanya kazi ambayo MUNGU atatukabidhi na atatuamini tuifanye. Wengi hawafikii nafasi ambayo wanaweza kuifikia, kwa sababu wanangojea MUNGU awafanyie yale ambayo amewapa uwezo wa kuyafanya wao wenyewe. Wote ambao wamechaguliwa kufaa utumishi katika maisha haya lazima wafundishwe kwa nidhamu kali ya kiakili na kimaadili, na kisha MUNGU atawasaidia kwa kuchanganya nguvu Zake za Kiungu/Uungu na juhudi za kibinadamu. - (Testimonies for the Church 4: 611) [Pr 30.1; Maombi Aya ya 88]

Maombi Yanahitajika ili Kuielewa ile Kweli -Mada za ukombozi ni mada muhimu na nzito mno, na ni wale tu ambao wana nia ya kiroho wanaweza

kutambua kina na umuhimu wake. Ni usalama kwetu, maisha yetu, na furaha yetu, kuishi ndani ya zile Kweli za mpango wa wokovu. Imani na maombi ni muhimu ili tuweze kuyaona mambo ya kina ya MUNGU. Fikra zetu zimefungwa sana na maoni finyu na hafifu, kiasi kwamba tunapata maoni na mitazamo michache tu ya uzoefu ambao ni upendeleo wetu kuwa nayo. Tunaelewa kwa udogo wa kiasi gani lile ombi la mtume, aliposema, "kwamba atawapatia, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu Wake, Muimarishwe kwa nguvu na roho Yake katika utu wa ndani; ili Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani; ili ninyi, mkiwa na shina, na msingi wa upendo, mpate kuweza kujua pamoja na watakatifu wote jinsi ya mapana, na marefu, na kina, na kimo; na kuujua upendo wa Kristo, upitao ujuzi, ili mjazwe utimilifu wote wa Mungu. Sasa Kwake Yeye awezaye kufanya mengi kupita yote tunayoomba au kufikiria, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu, tukufu umrudie Yeye kanisani kupitia Kristo Yesu katika vizazi vyote, milele na milele. Amina (na amina, ombi zito sana kupita yote!). The Review and Herald, Novemba 17, 1891) [Pr 30.2; Maombi Aya ya 89]

Maombi Yanahitajika Nyumbani — Upendo hauwezi kudumu, hata katika mzunguko wa nyumbani, isipokuwa kuna upatanifu na mwelekeo kwa mapenzi ya MUNGU. Vitivo na shauku zote zinapaswa kuletwa katika upatanifu na sifa za Yesu Kristo. Ikiwa baba na mama katika upendo na hofu ya MUNGU wataungana katika shauku na kuwa na mamlaka nyumbani, wataona umuhimu wa maombi mengi, na kutafakari kwa undani zaidi. Na wanapomtafuta MUNGU, macho yao yatafunguliwa kuona wajumbe wa mbinguni waliopo kuwalinda kama jibu la maombi ya imani. Watashinda udhaifu wa tabia zao na kutembea kuelekea kwenye ukamilifu. - (The Adventist Home, 315, 316) [Pr 30.3; Maombi Aya ya 90]

Maombi yanahitajika kudumisha uhusiano na MUNGU— Puuza mazoezi ya maombi, au jihusishe na maombi hapa na pale bila mtiririko wa daima, ukitenda kile kinachokuwa rahisi kwako, basi utapoteza uhusiano wako na MUNGU. Maisha ya Kikristo hugeuka kuwa makavu, na nguvu za kiroho hazina nguvu kali. Uzoefu wa kidini unakosa afya na nguvu. - (The Signs of the Times, July 31, 1893) [Pr 31.1; Maombi Aya ya]

Maombi yanahitajika ili kupata Nguvu za Kiroho — Sababu ambayo wengine hawana utulivu, ni kwamba hawaendi kwa Yeye ambaye Ndiye chanzo pekee cha Kweli cha furaha. Kila mara wanajaibu kutafuta kujifurahisha mbali na ile furaha inayopatikana ndani Kristo Yake pekee. Ndani Yake hakuna matumaini yaliyokatishwa tamaa. Oh! Ni kwa jinisi gani fursa ya thamani ya maombi imepuuziwa! Usomaji wa Neno la MUNGU huandaa akili kwa ajili ya maombi. Moja kati ya sababu kubwa ya kwa nini wengi wanajitoa kwa udogo katika kumkaribia MUNGU kwa njia ya maombi ni, kwamba wamejitenga wenyewe na kazi hii takatifu kwa kusoma hekaya zinazowavutia, ambazo zimeyasisimua mawazo na kuamsha tamaa mbaya. Neno la Mungu linakuwa lenye ladha

isiyopendeza (mionjo yao imebadilika kwa wanachokula); saa ya maombi haiwekwi mawazoni. Maombi ni nguvu ya Mkristo. Wakati yuko mwenyewe, yeye hayupo peke yake; anahisi uwepo wa Yule aliyenena, "Tazama, Mimi Niko pamoja nawe siku zote." (The Review and Herald, Machi 11, 1880) [Pr 31.1; Maombi Aya ya 91]

Maombi Yanahitajika ili Kuingia Mbinguni — Hakuna kitu kama kuingia kwetu kwenye malango ya mbinguni kupitia kujifurahisha, kujiendekeza na upumbavu, maburudisho, ubinafsi, bali tu ni kwa kukesha na kuomba bila kukoma. Kukesha kiroho kwa kila mmoja wetu ndiyo gharama/bei ya usalama. Usiegemee upande wa Shetani hata sentimita moja, asije akapata manufaa kwako na kukuteka. - (SDA Bible Commentary 6: 1094) [Pr 31.2; Maombi Aya ya 92]

Maombi hutufanya kudumu kuwa Waaminifu — Bila maombi yasiyokoma na kukesha kwa bidii, tuko katika hatari ya kuongeza uzembe, kutojali na kupotoka mbali na njia sahihi. Adui daima anatafuta kuzuia au kufunga njia ya kukifikia Kiti cha Rehema, ili kwa sala ya dhati na imani tusipate neema na nguvu ya kupinga majaribu. - (The Review and Herald, Desemba 8, 1904) [Pr 31.3; Maombi Aya ya 93]

Omba kwa ajili ya roho- Ikiwa tunataka kujifunza juu ya Kristo, lazima tuombe kama vile ambavyo mitume waliomba Roho Mtakatifu alipomwagwa juu yao. Tunahitaji ubatizo wa Roho wa MUNGU. Hatuko salama hata kwa saa moja tunaposhindwa kutoa utii kwa Neno la MUNGU.—(Fundamentals of Christian Education, 537) [Pr 32.1; Maombi Aya ya 94]

Udhaifu hugeuzwa na kuwa Nguvu Kupitia Maombi — Wao [watu wengi wa MUNGU] hawaoni umuhimu wa kuzijua nafsi zao na pia kuzitawala nafsi zao wenyewe. Hawakeshi na kuomba, ili wasije wakaingia majaribuni. Ikiwa wangekesha, wangeweza wangejelimisha kuzitambua pointi/vipengele vyao dhaifu, ambavyo vina uwezekano mkubwa kuwaingiza hatarini, na kuwashambulia kwa majaribu. Kwa kukesha na kuomba, vipengele/maeneo yao dhaifu yanaweza kulindwa vyema na hata mwishowe yakawa vipengele vyao vyenye kuwafanya wawe imara/nguvu, na wanaweza kukabiliana na majaribu bila kushindwa. Kila mfuasi wa Kristo anapaswa kujichunguza mwenyewe kila siku, ili aweze kuujua kwa ukamilifu mwenendo wake mwenyewe.—(Testimonies for the Church 2:511) [Pr 32.2; Maombi Aya ya 95]

Omba katika Hali Zote — Katika biashara yako, katika nyakati za kuburudika kwa pamoja na wengine, na katika muingiliano wa maisha, acha kila mahusiano unayoingia, yawe katika maombi ya dhati, na ya unyenyekevu. Kwa njia hiyo utaonyesha kwamba unamheshimu MUNGU, na MUNGU atakuheshimu na kukutunukia. Omba moyo unapokuwa dhaifu na kuzimia. Unapokata tamaa, funga mdomo wako kwa wanadamu (Usinyanyue mdomo wako kuwaelezea watu shida zako); usifuate njia ya wengine na kuwa kivuli chao; bali mwambie Yesu

kila kitu. Nyosha mikono yako juu na kuomba msaada. Katika udhaifu wako shikilia nguvu isiyo na kikomo. Omba unyenyekevu, hekima, ujasiri, ongezeko la imani, ili uweze kuona mwanga katika nuru ya MUNGU na ufurahie upendo Wake.
- (The Ministry of Healing, 513) [Pr 32.1; Maombi Aya ya 96]

SURA YA 3

MUNGU HUSIKIA MAOMBI

MUNGU husikia Maombi ya Wanyenyekevu — Baba yetu wa mbinguni anasubiri kutupatia ujazo/ukamilifu wa baraka Zake. Ni nafasi ya upendeleo kwetu kunywa kwa kadiri tuwezavyo kutoka kwenye chemchemi ya upendo usio

na ukomo. Inashangaza kwa kiasi gani kwamba sisi tunaomba kidogo sana! MUNGU Yuko tayari kusikia maombi ya dhati ya watoto Wake wanyenyekevu, na bado kuna kusitasita kwingi kwa upande wetu kumjulisha MUNGU yale tunayoyataka. Malaika wa mbinguni wanafikiria nini juu ya wanadamu maskini wasiojiweza, ambao wanakabiliwa na majaribu, wakati moyo wa MUNGU wa upendo usio na kikomo unawainamia kwa matamania, akiwa tayari kuwapa zaidi ya vile wanavyoweza kuomba au kufikiri, ila bado wao wanaomba kidogo sana na wana imani ndogo sana? Malaika wanapenda kusujudu mbele za MUNGU; wanapenda kuwa karibu Naye. Wanauchukulia ushirika wao na MUNGU kuwa ndiyo furaha yao kubwa kupita furaha zote; ila wanadamu, ambao wanahitaji msaada mkubwa ambao ni MUNGU tu anayeweza kuutoa, wanaonekana kuridhika kutembea bila nuru ya Roho Wake, ushirika wa uwepo Wake. —(Steps to Christ, 94) [Pr 33.1; Maombi Aya ya 1]

Wale ambao wana unyenyekevu, wamtegemeao Mungu, na kuwa moyo uliopondeka, Mungu huwakubali, na husikia maombi yao; na MUNGU anaposaidia, vikwazo vyote vitaondolewa. Ni watu wangapi wenye uwezo mkubwa wa vipaji vya asili, akili nyingi, na elimu ya hali ya juu wameshindwa walipowekwa katika nafasi za uwajibikaji, wakati wale wenye akili dhaifu, na mazingira duni, wamefanikiwa sana. Siri ilikuwa: Wale wa kwanza wenye vipaji na visomo, walijiamini wao wenyewe, wakati wale dhaifu na duni waliungana na Yeye ambaye ni Mshauri wa ajabu na hodari katika kufanya kazi ili kutimiza mapenzi Yake. —(Testimonies for the Church 4:538, 539) [Pr 33.2; Maombi Aya ya 2]

MUNGU husikia na Kujibu Maombi — MUNGU husikia maombi. Kristo amesema “Mkiniomba chochote kwa Jina Langu, Nitafanya.” Tena anasema, “Mtu yeyote Akinitumikia, Baba Yangu atamheshimu.” Yohana 14:14; Yohana 12:26. Ikiwa tunaishi kulingana na Neno Lake, kila ahadi ya thamani aliyoitoa itatimizwa kwetu. Hatustahili rehema Yake, lakini tunapojitoa kwake, Yeye hutupokea. Yeye atafanya kazi kwa ajili na kupitia wale wanao mfuata. - (The Ministry of Healing, 226, 227) [Pr 34.1; Maombi Aya ya 3]

Hakika Bwana atasikia na kujibu maombi ya watendakazi Wake ikiwa watamtafuta kwa ajili ya ushauri na mafundisho. - (Evangelism, 399) [Pr 34.2; Maombi Aya ya 4]

MUNGU husikia maombi ya wote wanaomtafuta katika Kweli. Ana nguvu ambayo sisi sote tunahitaji. Anajaza moyo kwa upendo, na furaha, na amani, na utakatifu. —(Testimonies for the Church 9:169) [Pr 34.3; Maombi Aya ya 5]

Niliona kwamba kila ombi ambalo hutolewa kwa imani kutoka katika moyo mwaminifu litasikiwa na MUNGU na kujibiwa, na yule aliyetuma ombi atapata baraka wakati anapoihitaji zaidi, na mara nyingi majibu atakayopata yatazidi matarajio yake. Hakuna ombi la mtakatifu wa kweli linalopotea ikiwa limetumwa kwa imani kutoka katika moyo mkweli/mnyofu. —(Testimonies for the Church

1:121) [Pr 34.4; Maombi Aya ya 6]

MUNGU husikiliza Kila ombi — MUNGU aliye wa milele, alisema Yesu, hufanya iwe fursa yako kumwendea Yeye kwa Jina la Baba. Hebu elewa kila kinachomaanishwa hapa. Hakuna mzazi yoyote wa duniani aliyewahi kumsihi sana mtoto aliyekosea kama Yeye Aliyekuumba anavyomsihi mkosaji. Hakuna nia ya ya upendo wa kibinadamu iliyowahi kumfuata yule asiyetaka toba kwa miito ya upole kiasi hicho. MUNGU hufanya makazi Yake kila mahali; Yeye husikia kila neno linalosemwa, husikiliza kila ombi linalotolewa, anasikia huzuni na kukatishwa tamaa kwa kila mwanadamu, Anazingatia jinsi baba, mama, dada, rafiki, na jirani wanavyotendewa. Yeye hujali mahitaji yetu, na upendo Wake na rehema na neema zake zinaendelea kububujika ili kukidhi hitaji letu.- (The Signs of the Times, Oktoba 28, 1903) [Pr 34.5; Maombi Aya ya 7]

MUNGU husikia kila Maombi ya Dhati — Biblia inatuonyesha MUNGU katika mahali Pake pa juu na Patakatifu, sio katika hali ya kutokuwa na shughuli, sio kwa ukimya na upweke, ila akiwa amezungukwa na elfu kumi mara elfu kumi na maelfu ya maelfu ya viumbe watakatifu na wenye akili (malaika), wote wakingojea kufanya mapenzi Yake. Kupitia njia ambazo hatuwezi kutambua Yeye Yuko katika mawasiliano hai na kila sehemu ya utawala Wake. Lakini ni katika sehemu hii ndogo sana kama punje tu ukilinganisha na himaya Yake, yaani dunia yetu, ambapo zipo roho ambazo alimtoa Mwanawe wa pekee ili kuziokoa, shauku Yake na masilahi ya mbinguni yote yamejikita hapo. MUNGU anainama kutoka kwenye kiti Chake cha enzi kusikia kilio cha wanaoonewa. Kwa kila ombi la dhati Anajibu, "Mimi hapa." Yeye huwainua waliofadhaika na waliodhulumiwa kwa kukanyagwakanyagwa. Katika taabu zetu zote Yeye pia anataabika. Katika kila jaribu na kila mtihani malaika wa uwepo Wake yuko karibu kuokoa. - (The Desire of Ages, 356) [Pr 35.1; Maombi Aya ya 8]

Wanafunzi walikuwa bado kujua rasilimali na nguvu za Mwokozi zisizo na kikomo. Akawaambia, "Mpaka sasa hamkuomba chochote kwa Jina Langu." Yohana 16:24. Alielezea kuwa siri ya mafanikio yao itakuwa katika kuomba nguvu na neema kwa Jina Lake. Kwamba Angelikuwepo mbele za Baba kuomba kwa niaba yao. Maombi ya mwombaji mnyenyekevu Yeye huyawasilisha kama matamania Yake mwenyewe kwa niaba ya mtu huyo (roho hiyo). Kila ombi la dhati husikika mbinguni. Linaweza lisiwasilishwe kwa ufasaha; lakini ikiwa linatoka moyoni, litapanda kwenda mahali Patakatifu ambapo Yesu anahudumu, Naye ataliwasilisha kwa Baba bila neno moja la kuudhi, lenye kigugumizi, bali kwa Neno zuri na lenye harufu nzuri ya ubani wa ukamilifu Wake Mwenyewe. [Pr 35.2; Maombi Aya ya 9]

Njia ya uaminifu na uadilifu sio kwamba inakosa kizuizi, ila katika kila shida tunapaswa kuona wito wa kuomba. Hakuna mtu aliye hai ambaye ana nguvu yoyote ambayo hajaipokea kutoka kwa MUNGU, na chanzo kinachotoka nguvu

hizo kiko wazi hata kwa mwanadamu dhaifu zaidi. “Nanyi mkiomba lo lote kwa Jina Langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mkiniomba chochote kwa Jina Langu, nitafanya.” [Pr 35.3; Maombi Aya ya 10]

Kristo aliwaagiza wanafunzi Wake waombe "Kwa Jina Langu," .Katika Jina la Kristo wafuasi wake wanapaswa kusimama mbele za MUNGU. Kupitia thamani ya kafara iliyotolewa kwa ajili yao, wana thamani machoni pa Bwana. Kwa sababu kupewa haki kupitia Kristo wanahesabiwa kuwa wa thamani. Kwa ajili ya Kristo Bwana huwasamehe wale wamchao. Haoni ubaya ndani ya wenye dhambi hao. Anatambua mfano wa Mwanawe ndani yao, ambaye wanamuamini. - (The Desire of Ages, 667) [Pr 36.1; Maombi Aya ya 11]

Hakuna Ombi la dhati linalopotea – mjulishe maombi yako Muumba wako. Hakuna aliyewahi kumwendea kwa moyo uliopondeka na akafukuzwa. Hakuna ombi hata moja la dhati lilipotea. Katikati ya nyimbo za kwaya ya mbinguni, MUNGU husikia kilio cha mwanadamu dhaifu. Tunamwaga matamania ya mioyo yetu ndani ya vyumba vyetu vya siri, tunapumua maaombi tunapotembea njiani, na maneno yetu yanafika kwenye kiti cha enzi cha Mfalme wa ulimwengu/malimwengu. Sauti zetu zinaweza zisisikike kwenye sikio lolote la mwanadamu, lakini haziwezi kufa kimyakimya tu, wala haziwezi kupotea kupitia shughuli na kelele zinazoendelea. Hakuna kitu kinachoweza kuzamisha matamania ya moyo. Haya huinuka juu ya sauti za mitaani, juu ya machafuko ya kadamnasi za watu, na kwenda hadi nyua za mbinguni. Ni MUNGU Ndiye ambaye tunaongea Naye, na maombi yetu yanasikika. Wewe ambaye unajiona hustahili kabisa, usiogope kabisa kuikabishi kesi yako inayokukabili kwa MUNGU. - (In Heavenly Places, 82) [Pr 36.2; Maombi Aya ya 12]

MUNGU husikia Maombezi ya Yesu Yaliyochanganyika na Maombi Yetu – Kristo ameahidi Mwenyewe kuwa mbadala na mdhamini wetu, na hampuuzii au kumuacha mtu yeyote. Kuna fungu/mfuko usiopungukiwa wa utii kamili unaotokana na utii Wake nao unatitirika daima. Kule mbinguni sifa Zake, kujikana Kwake Mwenyewe na kujitoa mhanga Mwenyewe, kunathaminiwa kama uvumba unaopaswa kutolewa pamoja na maombi ya watu Wake. Wakati maombi ya dhati, na ya unyenyekevu ya mwenye dhambi yanapopanda kwenye kiti cha enzi cha MUNGU, Kristo anachanganya maombi hayo na sifa za maisha Yake Mwenyewe za utii mkamilifu. Maombi yetu yafanywa kuwa na harufu nzuri na uvumba huu. Kristo ameahidi kufanya maombezi kwa niaba yetu, na siku zote Baba humsikia Mwanawe.—(Sons and Daughters of God, 22) [Pr 36.3; Maombi Aya ya 13]

MUNGU daima hujibu, ingawa wakati mwingine twaweza tusitambue- Ikiwa tunamwendea MUNGU, tukijisikia kwamba tu wanyonge, tusio na uwezo na tegemezi, kama tulivyo, na kwa imani ya unyenyekevu tukitumaini tunawasilisha matakwa yetu Kwake Yeye ambaye maarifa Yake hayana mwisho, anayeona kila kitu katika uumbaji, na ambaye anatawala kila kitu kwa mapenzi na Neno Lake, Yeye anaweza na atashughulikia kilio chetu, na ataangaza nuru mioyoni mwetu.

Kupitia maombi ya dhati tunaletwa katika muunganiko wa akili ya Yule Asiye wa milele. Labda hatuwezi kuwa na ushahidi unaoonekana na wa kustaajabisha wakati huo ambao uso wa Mkombozi wetu umeinama juu yetu kwa huruma na upendo, lakini huo ndio Ukweli wenyewe. Tunaweza tusihisi mguso Wake unaoonekana, lakini mkono Wake uko juu yetu kwa upendo na huruma ya upole.- (Steps to Christ, 97) [Pr 37.1; Maombi Aya ya 14]

Majibu ya MUNGU siku zote sio yale tunayotarajia— Omba basi; Omba, nawe utapata. Omba unyenyekevu, hekima, ujasiri, ongezeko la imani. Kwa kila ombi la dhati jibu litakuja. Linaweza lisije vile vile tunavyotamani, au kwa wakati tunalitafuta; lakini litakuja kwa njia na kwa wakati ambao litakidhi mahitaji yako kwa ubora zaidi. Maombi unayotoa kwa upweke, kwa uchovu, katika majaribio, MUNGU hujibu, sio kila wakati kulingana na matarajio yako, lakini kila wakati kwa faida yako (kwa wema kwako). — (Messages to Young People, 250) [Pr 37.2; Maombi Aya ya 15]

MUNGU husikia Maombi kwa ajili ya kuongoa Roho — Wakati wale wanaojua Ukweli wanapofanya mazoezi ya kujikana nafsi yaliyoamriwa katika Neno la MUNGU, ujumbe utaenda kwa nguvu. Bwana atasikia maombi yetu ya kuongoka kwa roho. Watu wa MUNGU wataacha nuru yao iangaze, na wale wasioamini, wakiona matendo yao mema, watamtukuza Baba yetu wa mbinguni. - (Counsels on Stewardship, 302) [Pr 37.3; Maombi Aya ya 16]

Amini kwamba MUNGU husikia maombi yako-watu wa MUNGU lazima wasonge kwa uelewa. Hawapaswi kuridhika mpaka kila dhambi inayojulikana imetubiwa; kisha ni haki na wajibu wao kuamini kwamba Yesu anawakubali. Hawapaswi kungojea mpaka wengine wapige gwaride kusonga mbele ili kuliacha giza na kupata ushindi kwaajili yao kufurahia. Furaha kama hiyo itadumu hadi mkutano utakapofungwa tu. Lakini MUNGU lazima atumikiwe kutoka kwa kanuni badala ya hisia. Asubuhi na usiku jipatieni ushindi kwaajili yenu wenyewe katika familia yenu. Usiruhusu kazi yako ya kila siku ikuzuie katika hili. Chukua muda ichanganyike na maombi yako. Unaweza usihisi jibu la haraka wakati wote; lakini basi ni kwamba imani hiyo inakuwa inajaribiwa. Unathibitishwa kuona ikiwa utamtegemea MUNGU, ikiwa una imani hai, na inayodumu. “Yeye analiyewaita ninyi atafanya hivyo kwani ni mwaminifu.” Tembea kwenye boriti nyembamba ya imani. Yaache yote juu ya ahadi za Bwana. Mtumaini MUNGU gizani. Huo ni wakati wa wewe kuwa na imani. Lakini mara nyingi mnaruhusu hisia ziwatawale. Mnaangalia kustahili ndani yenu wenyewe wakati hamuhisi kufarajiwa na Roho wa MUNGU, na mnakata tamaa kwa sababu hamuwezi kupata. Hamumtumaini Yesu vya kutosha, Yesu wa thamani. Hamfanyi kustahili kwake kuwa yote, yote. Hata mkifanya kwa ubora mnavyoweza kufanya haitaweza kustahili fadhili za MUNGU. Ni kustahili kwa Yesu ndiyo kutawaokoa, damu Yake ndiyo itakayowatakaswa. Lakini mnayo juhudi ya kufanya. Lazima ufanye kile unachoweza kwa upande wako. Uwe na bidii na kutubu, kisha mwamini. -

(Ushuhuda kwa Kanisa 1: 167) [Pr 38.1; Maombi Aya ya 17]

SURA YA 4

MAOMBI NA USHINDI WA NAFSI

Maombi ni Sehemu Muhimu ya Mafanikio katika kuongoa Roho-Ikiwa washiriki wa makanisa wangezifanyia kazi nguvu za akili walizo nazo, kwa juhudi zinazoelekezwa vizuri, katika mipango iliyokomaa vizuri, basi wangepeweza kumfanyia Kristo mara mia zaidi ya wanavyofanya sasa. Endapo wangesonga mbele kwa maombi ya dhati, kwa upole na unyenyekevu wa moyo, huku wao binafsi wakitafuta kuwapa wengine ujuzi wa wokovu, ujumbe huo unaweza kuwafikia wakazi wa dunia. - (The Review and Herald, Aprili 11, 1893). [Pr 39.1; Maombi Aya ya 1]

Tunapaswa kuja kwa MUNGU kwa imani, na kumimina dua zetu mbele Yake, tukiamini kwamba atafanya kazi kwa niaba yetu, na kwa niaba ya wale ambao tunatafuta kuwaokoa. Tunapaswa kutumia wakati mwingi kusali kwa bidii.— (SDA Bible Commentary 3: 146, 1147) [Pr 39.2; Maombi Aya ya 2]

Chagua roho nyingine na nyingine pia, kila siku ukitafuta mwongozo kutoka kwa MUNGU, ukiweka kila kitu mbele Zake kwa maombi ya bidii, na ufanye kazi

kwa hekima ya Bwana. Unapofanya hivi, utaona kwamba MUNGU atampa Roho Mtakatifu kusadikisha, na nguvu ya Ukweli kuiongoa roho. - (Medical Ministry, 245). [Pr 39.3; Maombi Aya ya 3]

Kumbuka kwamba kufaulu kwa karipio kunategemea kwa ukubwa roho ambayo kupitia kwayo onyo linatolewa. Usipuuze maombi ya dhati ili uwe na roho ya kujishusha, inayonyenyekea, na kwamba malaika wa MUNGU waende mbele yako na kufanya kazi juu ya mioyo unayojaribu kuifikia, na hivyo wailainishe kwa hisia za mbinguni ili juhudi zako zipate kuwa zenye faida. —(Testimonies for the Church 2:53) [Pr 40.1; Maombi Aya ya 4]

Ikiwa watu kadhaa wangekutana pamoja kwa nia moja, na mioyo iliyolemewa na mzigo kwa ajili ya roho zinazoangamia, na watoe maombi ya dhati, ya bidii, hakika matokeo yangekua mazuri. - (The Review and Herald, Agosti 23, 1892) [Pr 40.2; Maombi Aya ya 5]

Kuziombea roho Kutatuleta Karibu na MUNGU— Tunapotafuta kuwaleta wengine kwa Kristo, tukibeba mzigo wa roho za watu katika maombi yetu, mioyo yetu itadunda na ushawishi wenye nguvu wa kuhuishwa wa neema ya MUNGU; mapenzi yetu wenyewe yatang'aa kwa bidii zaidi ya kiungu; maisha yetu yote ya Kikristo yatakuwa halisia zaidi, yenye bidii zaidi, na ya maombi zaidi. - (Christ Object Lessons, 354). [Pr 40.3; Maombi Aya ya 6]

Pale ubinafsi unapokufa, kutakuwa na mwamko mkubwa wa matamano ya wokovu wa wengine, - hamu ambayo itasababisha kufanyika kwa juhudi za kudumu katika kutenda mema. Kutakuwa na kupanda kando ya maji yote; na sala yenye msukumo na mkazo, na maombi ya kujitolea, yataingia mbinguni kwa niaba ya roho zinazoangamia. - (Gospel Workers, 470). [Pr 40.4; Maombi Aya ya 7]

Mkutane pamoja kuombea uongoaji wa roho— Ikiwa katika sehemu moja wapo wawili tu au watatu tu ambao wanaujua Ukweli, basi na wajifanyie kikundi cha watenda kazi. Hebu watunze mshikamano/dhamana ya muungano wao usivunjike, wakivuta nyavu pamoja kwa upendo na umoja, wakitiana moyo kusonga mbele, kila mmoja akijipatia ujasiri na nguvu kutoka kwenye msaada wa wengine... Wanapoendelea kufanya kazi na kuomba kwa Jina la Kristo, idadi yao itaongezeka. —(Testimonies for the Church 7:21) [Pr 40.5; Maombi Aya ya 8]

Hebu kanisa la Los Angeles liwe na msimu maalum wa maombi kila siku kwa kazi ambayo inafanywa. Baraka ya Bwana itakuja kwa washiriki wa kanisa ambao kwayo wanashiriki katika kazi hiyo, wakikusanyika katika vikundi vidogo kila siku kuombea mafanikio yake. Na hivyo waumini watapata neema, na kazi ya Bwana itasonga mbele.—(Evangelism, 111, 112) [Pr 40.6; Maombi Aya ya 9]

Tunapaswa kufanya makongamano ya maombi, tukimwomba Bwana afungue njia ili Ukweli upate kuingia katika ngome ambazo Shetani ameweka kiti chake cha enzi, na kuondoa kivuli alichotupa katika njia ya wale ambao anatafuta

kuwadanganya na kuwaangamiza. —(Testimonies for the Church 6:80) [Pr 41.1; Maombi Aya ya 10]

Oh, kwamba sala ya dhati ya imani ipande kwenda juu kutokea kila mahali, Nipe roho zilizozikwa sasa kwenye takataka za makosa, la sivyo nife! Waleta kwenye ujuzi wa Ukweli kama ulivyo ndani ya Yesu. —(This Day With God, 171). [Pr 41.2; Maombi Aya ya 11]

Kila mtu Anaweza Kuziombea roho — Sio wote walioitwa kufanya kazi binafsi katika maeneo ya nchi za kigeni, lakini wote wanaweza kufanya kitu kwa maombi yao na zawadi zao kusaidia kazi ya umishonari. —(Testimonies for the Church 6:29) [Pr 41.3; Maombi Aya ya 12]

Kaka na dada, mmesahau kwamba sala zenu zinapaswa kutoka na kwenda nje, kama mundu kali, pamoja na watendakazi katika shamba kubwa la mavuno? —(Testimonies for the Church 3:162) [Pr 41.4; Maombi Aya ya 13]

Wale walio wa kiroho wazungumze na roho hizi. Omba pamoja nao na kwa ajili yao. Hebu muda mwingi utumike katika maombi na uchunguzaji wa karibu wa Neno kwa karibu. Hebu wote wapate Ukweli halisi wa imani katika nafsi zao kwa kuamini kwamba Roho Mtakatifu ataingia kwao kwa sababu wana njaa halisi na kiu ya haki. —(Testimonies for the Church 6:65) [Pr 41.5; Maombi Aya ya 14]

Wakati nyavu ya injili inatupwa majini, hebu kuwe na kukesha karibu na nyavu, kwa machozi na maombi ya bidii. Hebu watendakazi wadhamirie kutovunjika moyo; na wasiiachilie nyavu hadi itakapotolewa pwani, na matunda ya kazi yao. - (The Signs of the Times, Machi 16, 1882) [Pr 41.6; Maombi Aya ya 15]

Je! Tunawezaje kumheshimu MUNGU, tunawezaje kulitetea na kulithibitisha Neno Lake, pasipo kusali sana na kumwomba aonyeshe nguvu Zake kwa niaba ya wale wanaoangamia? - (The Review and Herald, Agosti 23, 1892) [Pr 42.1; Maombi Aya ya 16]

Jitihada za binafsi za kuongoa zafanikishwa kwa Maombi — Niliamua kwamba juhudi zangu hazipaswi kukoma mpaka roho hizi, nilizokuwa na matamano nazo, zimejitoa kwa MUNGU. Baadhi ya siku, katika nyakati za usiku, nilizitumia katika maombi ya dhati kwa wale ambao nilikuwa nimewatafuta na kuwaleta pamoja kwa kusudi la kuwafanyia kazi na kuomba pamoja nao. [Pr 42.2; Maombi Aya ya 17]

Katika kila moja ya mikutano yetu midogo niliendelea kuhimiza na kumwomba kila mmoja mmoja, hadi kila mmoja alipojitoa kwa Yesu, nikikiri sifa za upendo Wake unaosamehe. Kila mtu aliongolewa kuwa MUNGU.—(Testimonies for the Church 1:33, 34) [Pr 42.3; Maombi Aya ya 18]

Kuombea Roho huitoa akili katika wasiwasi wa mambo madogomadogo-

Omba sala za watu kwa ajili ya roho unazofanyia kazi; wawasilishe mbele ya kanisa kama mada za maombezi. Litakuwa ni hitaji ambalo ni muhimu kwa kanisa, kuzita akili zao kutoka kwenye shida zao ndogo ndogo, kuhisi mzigo mkubwa, kuwa na shauku binafsi, juu ya roho ambayo iko tayari kuangamia. - (Medical Ministry, 244, 245) [Pr 42.4; Maombi Aya ya 19]

Ombea Ufanisi Zaidi katika kuongoa roho-oh, na ionekane ndugu zangu, kwamba Yesu anakaa moyoni, anatia nguvu, anaimarisha, anafariji. Ni fursa yako kupewa, siku hadi siku kiwango kikubwa cha Roho Wake Mtakatifu, na kuwa na maoni mapana juu ya umuhimu na upeo wa ujumbe tunaotangaza kwa ulimwengu. Bwana Yu tayari kukufunulia mambo ya ajabu kutoka kwenye sheria Yake. Subiri mbele zake kwa unyenyekevu wa moyo. Omba kwa bidii sana ili upate ufahamu wa nyakati tunazoishi, kwa dhana kamili ya kusudi Lake, na kwa kuongezeka kwa ufanisi katika kuokoa roho. —(Testimonies to Ministers and Gospel Workers, 513, 514) [Pr 42.5; Maombi Aya ya 20]

Kuna roho nyingi zinazotamani nuru kupita maelezo, kupata uhakikisho na nguvu zaidi ya vile wanavyoweza kufahamu. Wanahitaji kutafutwa na kufanyiwa kazi kwa uvumilivu, bila kuchoka. Mwombe Bwana katika maombi ya bidii ili kupata msaada. Mwasilishe Yesu kwa watu kwasababu unamjua Yeye kama Mwokozi wako binafsi. Acha upendo Wake unaoyeyuka na laini, neema Yake nyingi, itiririke kutoka kwenye mdomo ya wanadamu. Haupaswi kuwasilisha hoja za Mafundisho makuu ya imani isipokuwa umehojiwa. Lakini chukua Neno, na kwa upendo mwororo na wenye shauku kwa ajili ya roho, waonyeshe haki ya thamani ya Kristo, ambaye Kwake Yeye, wewe na wao lazima muokolewe. - (Evangelism, 442) [Pr 43.1; Maombi Aya ya 21]

Wanafunzi waliomba kwa bidii nzito kwa ajili ya kufaa na utayari wa kuwaendea watu na katika mahusiano yao wa kila siku kuzungumza maneno ambayo yangewaongoza wenye dhambi kwa Kristo. waliweka pembeni tofauti zao zote, na hamu yote ya ukuu, wakakutana pamoja katika ushirika wa Kikristo. Wakajisogeza karibu na karibu zaidi na MUNGU, na walipofanya hivi walitambua ni upendeleo wa kiasi gani kwao kuruhusiwa kushirikiana kwa karibu na Kristo. Huzuni ilijaza mioyo yao walipofikiria ni mara ngapi walikuwa wamemhuzunisha Yeye kwa uzito wao katika kuelewa, kushindwa kwao kuelewa masomo ambayo, kwa faida yao wenyewe, alikuwa akijaribu kuwafundisha. [Pr 43.2; Maombi Aya ya 22]

Siku hizi za maandalizi zilikuwa siku za uchunguzi wa moyo kwa kina. Wanafunzi walihisi hitaji lao la kiroho na wakalia kwa Bwana kwa ajili ya upako mtakatifu ambaye angewafaa kwa kazi ya kuokoa roho. Hawakuomba baraka kwao wenyewe tu. Walielemea na mzigo wa kuongoa roho. Walitambua kwamba injili inapaswa kupelekwa ulimwenguni, nao wakadai nguvu ambayo Kristo alikuwa ameahidi. - (The Acts of the Apostles, 37) [Pr 43.3; Maombi Aya ya 23]

Maombi mengi yanahitajika ili kujua jinsi ya kuwafikishia watu Ukweli – Sio kila mtu anayeweza kufanya kazi kwa busara kwa ajili ya ukombozi wa roho. Panahitajika kuwa na kufikiri na tafakari ya kina. Hatupaswi kuingia katika kazi ya Bwana hovyoyvyo bila mikakati na kutarajia mafanikio. Bwana anahitaji watu wenye akili, watu wenye tafakari. Yesu anatoa wito ili kupata watendakazi wenza, na sio waborongaji. MUNGU anataka watu wenye mafikara sahihi na walio na akili kufanya kazi kubwa inayohitajika kwa ajili ya wokovu wa roho. [Pr 43.4; Maombi Aya ya 24]

Fundi mitambo, wanasheria, watu wa stadi mbalimbali, na taaluma zote, hujielimisha wenyewe ili waweze kuwa magwiji waliobobea katika fani zao. Je! Wafuasi wa Kristo wanapaswa kupungukiwa na ufahamu, na kisha wale wanaodai kuhusika na utumishi Wake ni wajinga (mbumbumbu) katika njia na mbinu zile wanazozitumia? Shughuli ya kupata uzima wa milele iko juu ya kila jambo la kidunia. Ili kuongoza roho kwa Yesu lazima kuwe na maarifa ya asili ya mwanadamu na kuisomea akili ya mwanadamu. Tafakari makini sana na maombi ya dhati yanahitajika kujua jinsi ya kuwafikia wanaume na wanawake juu ya mada kuu ya Ukweli. – (Testimonies for the Church 4:67) [Pr 44.1; Maombi Aya ya 25]

Maombi hutenda Zaidi Katika kuongoa roho Kuliko Maneno Peke yake—Shetani anakufuatilia kwenye njia yako. Yeye ni mpinzani mjanja, na roho mbaya yenye sumu ambayo unakutana nayo katika kazi yako vimeangaziwa na yeye. Wale ambao yeye huwaweka chini yake wanarudia mwangwi wa maneno yake. Ikiwa pazia lingeweza kuchanwa kutoka kwenye macho yao, wale waliofanya kazi hiyo wangeona Shetani akitumia sanaa yake yote kuwavuta kutoka kwenye Ukweli. Katika kuziokoa roho kutoka katika hila zake, mafanikio yatapatikana zaidi kupitia sala ya unyenyekevu kama ya Kristo kuliko kwa maneno mengi bila maombi. - (Colporteur Ministry, 81) [Pr 44.2; Maombi Aya ya 26]

MUNGU anataka vijana wenye kiasi, wenye kujistahi, wanyenyekevu, watulivu, wenye akili timamu, na wanaume wenye umri wa kukomaa, ambao wana msawaziko wa kanuni (balansi), ambao wanaweza kuomba na kuongea, ambao watainuka mbele ya wazee ili kuonyesha heshima kwao, na kuwatendea waliowazidi kwa kuwaheshimu. [Pr 44.3; Maombi Aya ya 27]

Kazi ya MUNGU inateseka kwa ajili ya upungufu wa watenda kazi wenye ufahamu na nguvu ya akili. Kaka na dada zangu, Bwana amewabariki na uwezo wa vitivo vya kiakili unaoweza kuboresheka zaidi. Kuza talanta zako kwa bidii ya kudumu. Fanya mazoezi na ifundishe akili kwa kusoma, kwa uchunguzi, kwa kutafakari.

Hauwezi kukutana na akili ya MUNGU isipokuwa umetumia kila nguvu. Uwezo wa akili utaimarika na kukuzwa ikiwa utaenda kufanya kazi kwa hofu ya MUNGU, kwa unyenyekevu, na kwa maombi ya dhati. Kusudi thabiti litatimiza maajabu.

Muwe wazi, thabiti, wakristo walioazimia. Mtukuze Yesu, zungumza juu ya upendo Wake, sema juu ya uweza Wake, na hivyo uache nuru yako iangaze kwa ulimwengu. - (Life Sketches, 275) [Pr 44.4; Maombi Aya ya 28]

Ombea Roho -Anza kuombea roho; mkaribie Kristo, karibu na upande Wake unaovuja damu. Hebu roho ya upole na utulivu ipambe maisha yenu, na ombi lenu la bidii, lililopondeka, na la unyenyekevu lipande Kwake kwaajili ya kupata hekima ili mpate kufaulu kuokoa sio nafsi zenu tu, bali na roho za wengine Omba zaidi ya uimbavyo. Je! Wewe huna hitaji kubwa la maombi zaidi kuliko kuimba? Vijana na wanawake, MUNGU anawaiteni mfanye kazi, mumfanyie kazi. Fanya mabadiliko yote katika mwenendo wako. Unaweza kufanya kazi ambayo wale wanaohudumu kwa Neno na mafundisho hawawezi kufanya. Unaweza kulifikia lile tabaka ambalu ambalo wachungaji hawawezi kulifikia.—(Testimonies for the Church 1:513. [Pr 45.1; Maombi Aya ya 29]

Hebu na tuombe kwa bidii pia kwa niaba ya wale ambao tunatarajia kuwatembelea, kwa imani hai kuwaleta, mmoja baada ya mwingine, katika uwepo wa MUNGU. - (Christian Service, 169) [Pr 45.2; Maombi Aya ya 30]

Fanya kazi miongoni mwa watu wa hali ya chini, masikini, na walioonewa. Tunapaswa kuwaombea na kuomba nao wale wanyonge, wasio na msaada ambao hawana nguvu ya kutawala hamu ya chakula au tamaa ya mwili imeiharibu. Jitihada za bidii na za kudumu lazima zifanyike kwa wokovu wa wale ambao mioyo yao imepata uamsho. —(Testimonies for the Church 6:84) [Pr 45.3; Maombi Aya ya 31]

SURA YA 5

AHADI ZA MUNGU KUHUSU MAOMBI

MUNGU Huahidi Kusikia na Kujibu Maombi – Kristo Ndiye kiunganishi kati ya MUNGU na mwanadamu. Ameahidi maombezi Yake Mwenyewe binafsi kwa kutumia Jina Lake. Anaweka fadhila yote ya haki Yake upande wa mwombaji. Kristo anamuomba mwanadamu, na mwanadamu, kwa anayehitaji msaada wa Bwana/Mungu, anajiomba Mwenyewe mbele za MUNGU, akitumia nguvu ya ushawishi wa Yule aliyetoa maisha Yake kwa ulimwengu. Tunapokiri mbele za MUNGU kuthamini na ukubali wetu wa haki na sifa ya Kristo, manukato hutolewa kwa maombezi yetu. Oh, ni nani anayeweza kuthamini rehema na upendo huu mkubwa! Tunapomkaribia MUNGU kupitia sifa ya Kristo, tumevikwa mavazi Yake ya kikuhani. Yeye hutuweka karibu Yake, akituzunguka kwa mkono Wake wa kibinadamu, wakati huo huo kwa mkono Wake wa Kiungu Yeye anashika kiti cha enzi cha Yeye Asiye na mwisho. Anaweka haki, uzuri na sifa Zake, kama uvumba mtamu, ndani ya chetezo mikononi mwetu, ili kutia moyo maombi yetu. Anaahidi kusikia na kujibu sala zetu. [Pr 46.2; Maombi Aya ya 1]

Maombi rahisi yanayoshawishiwa na Roho Mtakatifu yatapanda juu kupitia Lango lililofunguliwa, mlango ule ulio wazi ambao Kristo ametangaza: Nimefungua, na hakuna mtu anayeweza kufunga. Maombi haya, yaliyochanganywa na uvumba wa ukamilifu wa Kristo, yatapanda juu kama manukato kwa Baba, na majibu yatakuja. –(Testimonies for the Church 6:467) [Pr 46.2; Maombi Aya ya 2]

Niliona kwamba kila ombi ambalo hutolewa kwa imani kutoka katika moyo mwaminifu litasikika juu kwa MUNGU na kujibiwa, na yule aliyetuma ombi atapata baraka wakati anapoihitaji sana, na mara nyingi majibu huzidi matarajio yake. Hakuna ombi la mtakatifu wa kweli linalopotea ikiwa limetumwa kwa imani kutoka katika moyo mkweli.—(Testimonies for the Church 1:121) [Pr 47.1; Maombi Aya ya 3]

Kuomba kama Nehemia alivyoomba katika saa yake ya uhitaji ni nyenzo ya kumuongoza Mkristo katika mazingira ambapo aina nyingine za maombi zitashindikana Wanaofanya kazi zenye kutoa jasho pahali ambapo maisha yana shuguli nyingi (busy), waliosongwa nanwako karibu kuzidiwa na mifadhaiko, wanaweza kutuma ombi kwa MUNGU kwa ajili ya mwongozo Wake Bwana. Wasafiri baharini na nchi kavu, wanapotishiwa na hatari kubwa, wanaweza kujikabidhi katika ulinzi wa Mbingu. Wakati wa shida ya ghafla au hatari, moyo

unaweza kutuma kilio chake cha kuomba msaada kwa Yule ambaye ameahidi kuwasaidia waaminifu Wake, waaminio kila wanapomwita. Katika kila jambo, chini ya kila hali, nafsi iliyolemewa na huzuni na masumbufu ya maisha haya, au kushambuliwa vikali na majaribu, inaweza kupata uthibitisho, msaada, na usaidizi katika upendo usiomwangusha mtu na nguvu ya MUNGU anayeshika agano.— (Prophets and Kings, 631, 632) [Pr 47.2; Maombi Aya ya 4]

Tukimwomba, MUNGU atajibu -Ni sehemu ya mpango wa MUNGU kutupatia, kwa kujibu maombi ya imani, yale ambayo hangetoa ikiwa hatukuomba. - (The Great Controversy, 525) [Pr 47.3; Maombi Aya ya 5]

MUNGU husikia maombi. Mkiniomba chochote kwa Jina Langu, Nitafanya." Tena anasema, "Mtu yeyote Akinitumikia, Baba Yangu atamheshimu." Yohana 14:14; Yohana 12:26. Ikiwa tutaishi kulingana na Neno Lake, kila ahadi ya thamani aliyotoa itatimizwa kwetu. Sisi hatustahili rehema Yake, lakini tunapojitoa Kwake, Yeye hutupokea. Atafanya kazi kwaajili yetu na kupitia wale wanaomfuata. - (The Ministry of Healing, 226, 227) [Pr 47.4; Maombi Aya ya 6]

Unapomwomba Bwana akusaidie, Mtukuze Mwokozi wako kwa kuamini kwamba unapokea baraka Yake. Nguvu zote, hekima yote, ziko chini ya mamlaka yetu. Tunachopaswa ni kuomba tu. - (The Ministry of Healing, 514) [Pr 48.1; Maombi Aya ya 7]

MUNGU ana mbingu iliyojaa mibaraka ambayo anataka kuwapa wale ambao wanatafuta kwa bidii msaada ule ambao Bwana peke Yake ndiye anaweza kutoa.—(Sons and Daughters of God, 123) [Pr 48.2; Maombi Aya ya 8]

Yesu Huwasilisha kwa Baba Maombi Yetu Yenye Maneno Mabovu na duni - Kila ombi la dhati husikika mbinguni. Linaweza lisiwasilishwe kwa ufasaha; lakini ikiwa linatoka moyoni, litapanda kwenda mahali Patakatifu ambapo Yesu anahudumu, na ataliwasilisha kwa Baba bila hata Neno moja la kuudhi, na lenye kigugumizi, bali kwa Maneno mazuri na yenye harufu nzuri ya ubani wa ukamilifu Wake mwenyewe. [Pr 48.3; Maombi Aya ya 9]

Nguvu ya Kushinda majaribu inatolewa kwa Wale Wanaoomba- Wote wanawajibika kwa matendo yao wakiwa katika ulimwengu huu wakati mlango wa rehema haujafungwa bado. Wote wana uwezo wa kudhibiti matendo yao ikiwa watataka. Wakiwa ni dhaifu katika wema na usafi wa mawazo na matendo, wanaweza kupata msaada kutoka kwa Rafiki wa wanyonge. Yesu anauelewa udhaifu wote wa asili ya kibinadamu, na, ikiwa ataombwa, atatoa nguvu kushinda majaribu yenye nguvu zaidi. Wote wanaweza kupata nguvu hii ikiwa wataitafuta kwa unyenyekevu. - (Child Guidance, 466, 467) [Pr 48.4; Maombi Aya ya 10]

MUNGU Hujibu Maombi Yetu Wakati na Jinsi Anavyoona inafaa - Kila mtakatifu anayekuja kwa MUNGU kwa moyo wa Kweli, na kutuma kwa imani maombi yake yaliyo na unyofu Kwake, atajibiwa maombi yake. Imani yako

haipaswi kuachilia ahadi za MUNGU, ikiwa hautaona au kuhisi jibu la haraka la maombi yako. Usiogope kumtumaini MUNGU. Zitegemee ahadi Zake za Kweli: "Ombeni, nanyi mtapata." MUNGU ni Mwenye busara mno kukosea, na ni mwema sana kuwazuilia watakatifu Wake wanaotembea katika unyoofu kitu chochote kizuri. Mtu hufanya makosa, na ingawa maombi yake yanatumwa kutoka katika moyo mnyofu/mkweli, mara zote huwa haombi vitu ambavyo ni vyema kwake, au ambavyo vitamtukuza MUNGU. Wakati hili likiwa hivyo, basi Baba yetu Mwenye busara na mwema husikia maombi yetu, Naye atajibu, wakati fulani hujibu haraka -; lakini Yeye hutupatia vitu ambavyo ni kwa faida yetu na utukufu Wake Mwenyewe. MUNGU hutupatia baraka; laiti tungeangalia mpango Wake, tungeliona wazi kwamba Anajua kile kilicho bora kwaajili yetu na kwamba maombi yetu huwa yamejibiwa. Hatupewi chochote cha kutuumiza, bali baraka tunazohitaji hutolewa badala ya kitu ambacho tuliomba ambacho hakitakuwa kizuri kwetu, ambacho kingetuumiza. [Pr 48.5; Maombi Aya ya 11]

Niliona kwamba ikiwa hatuhisi majibu ya haraka ya maombi yetu, tunapaswa kushikilia imani yetu kwa ujasiri, bila kuruhusu mashaka, kwani hayo yatatutenganisha na MUNGU. Imani yetu ikitetereka, hatutapokea chochote kutoka Kwake. Imani yetu kwa MUNGU inapaswa kuwa imara; na tunapohitaji sana, baraka itatuangukia kama matone ya mvua. —(Testimonies for the Church 1:120, 121) [Pr 49.1; Maombi Aya ya 12]

MUNGU Hutoa Hekima Kwa Kujibu Maombi — Bwana ametupa ahadi hii, "Ikiwa yeyote kati yenu amepungukiwa na hekima, na aombe kwa MUNGU, ambaye huwapa watu wote kwa ukarimu, wala hakemei; naye atapewa." Ni katika utaratibu wa MUNGU kwamba wale wanaobeba majukumu mara nyingi wanapaswa kukutana pamoja ili kushauriana wao kwa wao, na kuomba kwa bidii hekima hiyo ambayo Yeye peke Yake Ndiye anaweza kutoa. Kwa pamoja mumjulishe MUNGU shida zenu. Zungumzeni kidogo; muda wa thamani unapotea katika mazungumzo ambayo hayana nuru. Ndugu waungane katika kufunga na kuomba kwa ajili ya hekima ambayo MUNGU ameahidi kuitoa kwa ukarimu na uhuru mwingi sana. (Testimonies to Ministers and Gospel Workers, 499) [Pr 49.2; Maombi Aya ya 13]

Neema ya Kristo yapatikana hata kabla ya sisi kuiomba - hata kabla ya maombi kutamkwa, ... neema kutoka kwa Kristo inaenda kukutana na neema inayofanya kazi juu ya roho ya mwanadamu.— (Christ's Object Lessons, 206) [Pr 49.3; Maombi Aya ya 14]

Tunaweza Kudai Ahadi Zake Kwa Ujasiri— "Mkikaa ndani Yangu, na maneno Yangu yakikaa ndani yenu, mtaomba kila mnachotaka, nanyi mtatendewa." Unapoomba, wasilisha ahadi hii. Ni upendeleo kwetu kumwendea Yeye tukiwa na ujasiri mtakatifu. Tukimwomba kwa dhati nuru Yake iangaze juu yetu, Atatusikia na kutujibu. Lakini lazima tuishi kulingana na maombi yetu. Kwani hayana faida yoyote ikiwa tutatembea kinyume nayo. Nimemuona baba ambaye, baada ya

kusoma sehemu ya maandiko kutoa ombi, alipoinuka tu kutoka magotini baada ya sala, alianza kuwafokea watoto wake. Je! MUNGU angeweza kujibu ombi hilo aliloomba? Na ikiwa, baada ya kukemea watoto wake, baba atasali, je, sala hiyo itawanufaisha watoto? Hapana; labda ikiwa ni maombi ya kuungama kwa MUNGU. - (Child Guidance, 499) [Pr 50.1; Maombi Aya ya 15]

Malaika Watatusaidia sisi Katika kujibu Maombi — Unapotaka kuzungumza kwa jazba/hasira, funga mdomo wako. Usitamke neno lolote. Omba kabla ya kuzungumza, na malaika wa mbinguni watakuja kukusaidia na watawarudisha nyuma malaika wabaya, ambao wangukuongoza kumvunjia MUNGU heshima, kuiletea aibu au fedheha kazi Yake Mungu, na kudhoofisha roho yako mwenyewe.—(Testimonies for the Church 2:82) [Pr 50.2; Maombi Aya ya 16]

Malaika Watakua upande Wetu katika kujibu Maombi — Uangalizi/ulinzi wa jeshi la mbinguni umetolewa kwa wote ambao watafanya kazi katika njia za MUNGU na kufuata mipango Yake. Tunaweza, kwa maombi ya dhati, yenye majuto kuwaita wasaidizi wa mbinguni upande wetu. Vikosi vya nuru na nguvu visivyoonekana vitafanya kazi na wanyenyekevu, wapole na wale waliojishusha. [Pr 50.3; Maombi Aya ya 17]

Injili itasonga mbele haraka ikiwa ni matokeo ya maombi — MUNGU angefanya kazi kwa nguvu za kushangaza kwa watu Wake leo ikiwa wangejiweka chini ya uongozi Wake kikamilifu. Wanahitaji kufungamana na Roho Mtakatifu kila wakati. Ikiwa kungekuwa na maombi zaidi katika mabaraza ya wale waliobeba majukumu, unyenyekezaji wa moyo zaidi mbele za MUNGU, tungeliona ushahidi mwingi wa uongozi wa Bwana, na kazi yetu ingelisonga mbele haraka. - (Testimonies for the Church 8: 238) [Pr 50.4; Maombi Aya ya 18]

Maombi Yataleta Uwezo wa Kushinda- Lazima tuwe na silaha zote za MUNGU na tuwe tayari wakati wowote kwa vita dhidi ya nguvu za giza. Wakati majaribu na mitihani vinatukimbilia kwa kasi, twendeni kwa MUNGU na kuteseka/kuhuzunika Naye katika maombi. Hataturudisha na mikono mitupu, lakini atatupa neema na nguvu za kushinda, na kuvunja nguvu za adui. -(Early Writings, 46) [Pr 51.1; Maombi Aya ya 19]

Baraka Zitaendana na Imani Yetu — Omba kwa imani. Na hakikisha unauleta mtindo wako wa maisha upatane na maombi yako, ili upate baraka ambazo unaziombea. Hebu imani yako isidhoofike, kwani baraka zinazopatikana zinalingana na imani inayotumika. "na iwe kwako kulingana na imani yako". Na mkiwa na imani, chochote mtakachoomba katika sala, mtapata." Mathayo 9:29; Mathayo 21:22. Omba, amini, furahi. Mwimbieni MUNGU sifa kwa sababu amejibu maombi yenu. Mchukue kwa Neno Lake. "Yeye ni mwaminifu aliyeahidi." Waebrania 10:23. Hakuna ombi hata moja la dhati litakalopotea. Mfereji upo wazi; kijito kinatiririka. Kinabeba pamoja nacho sifa za uponyaji, kinamimina umeme wa uzima, afya na wokovu. —(Testimonies for the Church 7:274) [Pr 51.2;

SURA YA 6

MAOMBI YA IMANI

Maombi ni Njia ya Mafanikio ya Mbingu katika Kuishinda Dhambi — Kuna wengi ambao, ingawa wanajitahidi kutii amri za MUNGU, wana amani kidogo au furaha. Upungufu huu katika uzoefu wao ni matokeo ya kushindwa kuizoesha imani yao. Wanatembea kana kwamba ni katika ardhi yenye chumvi, nyika iliyokauka na udongo kupasukapasuka. Wanaomba kidogo (wanadai ahadi

chache), wakati wanaweza kuomba/kudai mengi; kwani hakuna kikomo kwa ahadi za MUNGU. Hao hawawakilishi kwa usahihi utakaso unaokuja kwa kuitii ile Kweli. Bwana angependa wana na binti Zake wote wawe na furaha, amani, na utiifu. Kupitia kupata imani anaye amini anamiliki baraka hizi. Kupitia kuizoesha imani, kila upungufu wa tabia unaweza kutolewa, kila unajisi unaweza kusafishwa, kila kosa linarekebishwa, kila ubora unapata kuendelezwa. [Pr 52.1; Maombi Aya ya 1]

Maombi ni njia ya mafanikio katika vita dhidi ya dhambi na ukuaji wa tabia ya Kikristo iliyowekwa na mbingu. Ushawishi wa Bwana ambao unaokuja ili kujibu ombi la imani utatimiza katika roho ya mwombaji yote ambayo anaomba. Kwa msamaha wa dhambi, kwa Roho Mtakatifu, kwa haiba kama ya Kristo, kwa hekima na nguvu ya kufanya kazi Yake, kwa zawadi yoyote ambayo ameahidi, tunaweza kuomba; na ahadi ni, "Mtapokea." (Matendo ya Mitume, 563, 564) [Pr 52.2; Maombi Aya ya 2]

MUNGU hutamani Kutufanyia Mambo Makubwa — Fungu/kazi yetu ni kuomba na kuamini. Kesheni mkiomba. Keshi, na ushirikiane na MUNGU anayesikia maombi. Iweke akilini mwako kwamba "sisi ni watenda kazi pamoja na MUNGU." 1 Wakorintho 3: 9. Sema na tenda kwa kupatana na maombi yako. Itafanya tofauti ya milele kwako endapo jaribu litathibitisha imani yako kuwa ya kweli, au kuonyesha kwamba maombi yako ni mfumo fulani tu. [Pr 53.1; Maombi Aya ya 3]

Wakati fadhaa zinatokea, na magumu yanakukabili, usitafute msaada kwa wanadamu. Muachie na kumtegemea MUNGU kwa yote. Kitendo cha kuwaambia wengine shida zetu hutufanya tuwe dhaifu, na hakileti nguvu yoyote kwao. Kinaweka juu yao mzigo wa udhaifu wetu wa kiroho, ambao hawawezi kuutua. Tunatafuta nguvu kutoka kwa mwanadamu anayekosea, mtu mwenye mwisho, anayekufa, wakati tunaweza kuwa na nguvu ya MUNGU asiye kosea, na asiye na ukomo. [Pr 53.2; Maombi Aya ya 4]

Hauna haja ya kujipelekea au kusafiri huku na kule hadi miisho ya dunia ili kupata hekima, kwa maana MUNGU Yuko karibu nawe. Sio uwezo ulionao sasa au utakaokuwa nao mbeleni, ndio ambao utakupa mafanikio. Ni kile ambacho Bwana anaweza kukufanyia. Tunahitaji kuwa na imani ndogo sana juu ya kile mwanadamu anachoweza kufanya na ujasiri mkubwa zaidi kwa kile MUNGU anachoweza kufanya kwa kila roho inayoamini. Anatamani mno wewe umuendee kwa imani. Anatamani sana utarajie kutoka Kwake mambo makubwa mno. Anatamani kukupa ufahamu katika mambo ya kidunia na pia katika mambo ya kiroho. Anaweza kuzinoa bongo/akili zako na zikawa bora zaidi. Anaweza kutoa busara na ustadi. Weka talanta zako katika kazi hiyo, mwombe MUNGU akupe hekima, nawe utapewa. - (Christ's Object Lessons, 146) [Pr 53.3; Maombi Aya ya 5]

Maombi na Imani vitafanya Mambo ya Ajabu — Ninaogopa kwamba hakuna imani hiyo ambayo ni muhimu na nyeti kuwa nanyo. Je! Hatuvaa njuga dhidi ya kukatishwa tamaa na vishawishi hata tuvunjike moyo? MUNGU ni Mwenye rehema, na tukifurahi katika Kweli, inayotakasa, nainayoboresha maisha, tunaweza kufanya kazi nzuri na thabiti kwa MUNGU. Maombi na imani vitafanya mambo ya kushangaza. Neno lazima liwe silaha yetu ya vita. Miujiza inaweza kufanywa kupitia Neno; kwa kuwa lina faida/manufaa kwa vitu vyote. - (Evangelism, 489) [Pr 53.4; Maombi Aya ya 6]

Imani Kuchanganywa na maombi Yetu -Watu wa MUNGU lazima wasonge kwa uelewa. Hawapaswi kuridhika mpaka watakapotubu kila dhambi inayojulikana; kisha ni haki na wajibu wao kuamini kwamba Yesu anawakubali. Hawapaswi kungojea wengine washinikize kupitia gizani na kupata ushindi ili wafurahie. Furaha kama hiyo itadumu hadi mkutano utakapofungwa tu. Lakini MUNGU lazima atumikiwe kwa kanuni badala ya hisia. Asubuhi na usiku jipatieni ushindi katika familia yenu. Usiruhusu kazi yako ya kila siku ikuzuie katika hili. Kuwa na muda wa kuomba, na unapoomba, amini kwamba MUNGU anakusikia. Kuwa na imani iliyochanganywa na maombi yako. Unaweza usipate jibu la haraka wakati wote; lakini basi ni kwamba imani hiyo inakuwa inajaribiwa. Unathibitishwa kuona ikiwa utamtegemea MUNGU, ikiwa una imani hai, na inayodumu. “Yeye ni Mwaminifu ambaye awaita, Naye atafanya hivyo (kwani ni Mwaminifu). Tembea katika njia nyembamba ya imani. Yaache yote juu ya ahadi za Bwana. Mtumaini MUNGU gizani. Huo ndio wakati wa kuwa na imani. Lakini mara nyingi mnaruhusu hisia ziwatawale. Mnatafuta kustahili ndani yenu wakati hamuhisi kufarajiwa na Roho wa MUNGU, na mnakata tamaa kwa sababu hamuwezi kupata. Hamjamtumaini Yesu vya kutosha, Yesu wa thamani. Hamfanyi kustahili Kwake kuwa yote, yote. Namna bora zaidi mnayoweza kuifanya kwa uwezo wenu, bado haitazidi fadhili za MUNGU. Ni thamani ya Yesu ndiyo itakayowaokoa, damu Yake ndiyo itakayowatakasa. Lakini mnayo kazi ya kufanya. Lazima mfanye kile mnachoweza kwa upande wenu. Mwe na bidii na kutubu, kisha muamini. [Pr 54.1; Maombi Aya ya 7]

Usichanganye imani na hisia pamoja. Vipo tofauti. Tunapaswa kuwa na imani. Imani hii lazima tuifanyie mazoezi. Amini, amini. Hebu imani yako ishikilie baraka, na ni zako. Hisia zako hazina uhusiano wowote na imani hii. Imani inapoleta baraka moyoni mwako, na unafurahi katika baraka, sio imani tena, bali ni hisia. — (Testimonies for the Church 1:167) [Pr 54.2; Maombi Aya ya 8]

Sala na Imani Hushikilia Nguvu za Mungu—Imani ya Kweli na sala ya Kweli—zina nguvu ilioje! Ni kama mikono miwili ambayo mwombaji wa mwanadamu anashikilia nguvu ya Upendo usio na kikomo. Imani ni kumtegemea Mungu,— kuamini kwamba anatupenda, na anajua ni nini kilicho bora na cha manufaa kwetu. Hivyo, badala ya njia yetu wenyewe, inatuongoza kuchagua njia Yake. Badala ya ujinga wetu, inakubali hekima Yake; badala ya udhaifu wetu,

nguvu Zake; badala ya dhambi zetu, haki Yake. Maisha yetu, sisi wenyewe, tayari ni Yake Yeye; imani inakiri umiliki Wake Mungu, na inakubali baraka Zake. Ukweli, unyoofu, usafi, husondwa kidole kwamba ndiyo siri za mafanikio ya maisha. Ni imani ndiyo inatuweka katika kumiliki na kuyashika haya. Kila msukumo wajambo jema au matamaniao mema ni zawadi ya kutoka kwa Mungu; imani hupokea kutoka kwa Mungu uhai ambao pekee Yake ndiyo unaweza kutokeza ukuaji na ufanisi wa Kweli.—(Gospel Workers, 259) [Pr 54.3; Maombi Aya ya 9]

Maisha yetu Yanapaswa kuendana na Maombi Yetu — Omba kwa imani. Na hakikisha unayapatanisha maisha yako na maombi yako, ili upate baraka ambazo unaziombea. Imani yako isidhoofike, kwani baraka zinazopatikana zinalingana/zinatoshana na imani tuliyonayo. "na iwe kwako kulingana na imani yako. "Na mkiwa na imani, chochote mtakachoomba katika sala, mtapata." Mathayo 9:29; Mathayo 21:22. Omba, amini, furahi. Mwimbieni MUNGU sifa kwa sababu amejibu maombi yenu. Muendee kwa Neno Lake. "Yeye ni Mwaminifu aliyeahidi." Waebrania 10:23. Hakuna ombi hata moja la dhati litakalopotea. Mfereji upo wazi; nao mkondo unatiririka. Unabeba sifa za uponyaji, ukimimina mkondo/umeme wa uhai unaorejesha upya, afya na wokovu. —(Testimonies for the Church 7:274) (Pr 55.1; Maombi Aya ya 10]

MUNGU hukubali Maombi ya Imani - Ombi lililo na unyenyekevu, akili na imani, ambalo hutoka kwenye midomo isiyo feki/udanganyifu, linakubalika kikamilifu kwa MUNGU. Ni maombi ya kina ya moyo ndiyo ambayo husikika mbinguni na kutuzwa kwa jibu hapa duniani. "Lakini kwa mtu huyu nitamtazama, hata yeye ambaye ni maskini, na mwenye roho iliyopondeka, na anayetetemeka Neno Langu." "Kwa maana asema huyu Mkuu, aliye juu, akaaye milele, Jina Lake ni Mtakatifu; Ninakaa mahali pa juu na Patakatifu, pamoja na yeye ambaye pia ni mwenye roho iliyopondeka na mnyenyekevu, ili kufufua roho ya wanyenyekevu, na kufufua moyo wa wale waliopondeka. "Roho iliyopondeka ni Dhabihu kwa MUNGU; Moyo uliovunjika na uliopondeka, oh! MUNGU, hutaudharau." (The Signs of the Times, December 3, 1896) (Pr 55.2; Maombi Aya ya 11]

Peleka Maombi yako kwa Imani bila kukoma — MUNGU atakuwa kila kitu kwetu kama tunavyohitaji awe. Maombi yetu dhaifu, ya moyo wa nusu nusu hayatatuletea majibu kutoka mbinguni. Lo, tunahitaji kushinikiza ombi letu bila kuchoka! Omba kwa imani, subiri kwa imani, pokea kwa imani, furahiya kwa tumaini, kwani kila mtu atafutaye hupata. Uwe na bidii katika jambo hilo. Mtafute MUNGU kwa moyo wote. Watu huweka moyo mnyofu na bidii katika kila kitu wanachofanya japo ni mambo ya muda mfupi na ya kupita tu, hukazana hadi hadi jasho lao linavalishwa taji ya mafanikio. Kwa bidii kubwa jifunze stadi ya kutafuta baraka nyingi ambazo MUNGU ameahidi, na kwa uvumilivu, na juhudi zenye bidii utakuwa na nuru Yake na Ukweli Wake na neema Yake nyingi. (Pr 56.1; Maombi Aya ya 12]

Kwa unyofu wa moyo, katika njaa ya kiroho, mlilie MUNGU. Shindana na

mawakala wa mbinguni hadi upate ushindi. Wekeza mwili na Roho yako yote mikononi mwa Bwana, nafsi, mwili, na roho, na amua kuwa, wakala Wake mpendwa aliyejiweka wakfu, akiongozwa na mapenzi Yake, akidhibitiwa na akili Yake, na kujazwa na Roho Wake. (Pr 56.2; Maombi Aya ya 13]

Mwambie Yesu matakwa yako kwa unyofu wa roho yako (kwa dhati). Siyo lazima ufanye mabishano au mjadala mrefu Naye, au kumhubiria MUNGU, lakini kwa moyo wa huzuni kwaajili ya dhambi zako, sema, "Niokoe, Bwana, la sivyo nitaangamia." Kuna matumaini kwa roho kama hizo. Watatafuta, wataomba, watabisha, na watapata. Wakati Yesu ameondoa mzigo wa dhambi unayousagasaga moyo, utaburudishwa kwa baraka ya amani ya Kristo. —(Our High Calling, 131) (Pr 56.3; Maombi Aya ya 14]

MUNGU hujibu Maombi ya Imani Kwa Uweza — Wakati watu wanajitoa kama Eliya na wana imani aliyokuwa nayo, MUNGU atajifunua kama alivyofanya wakati huo. Watu watakapokuwa wanamsihi Bwana kama vile Yakobo, majibu/matokeo ambayo yalionekana wakati huo yataonekana tena. Nguvu zitatoka kwa MUNGU kujibu maombi ya imani. - (Gospel Workers, 255) (Pr 56.4; Maombi Aya ya 15]

Elewa Sayansi ya Maombi-Maombi na imani ni marafiki walioshikamana kwa karibu sana, na vyote vinahitaji kufunzwa kwa pamoja. Katika ombi la imani kuna sayansi ya Bwana; ni sayansi ambayo kila mtu ambaye anatamani kufanikisha kazi yake ya maisha lazima aelewe. Kristo anasema, "Yo yote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu." Marko 11:24. Anaweka wazi kwamba ombi letu lazima liwe kulingana na mapenzi ya MUNGU; lazima tuombe vitu ambavyo ameahidi, na chochote tunachopokea lazima kitumike katika kufanya mapenzi Yake. Masharti yakitimizwa, ahadi haizuiliki. [Pr 57.1; Maombi Aya ya 16]

Kwa ajili ya msamaha wa dhambi, kwa ajili ya Roho Mtakatifu, kwa ajili ya tabia kama ya Kristo, kwa ajili ya hekima na nguvu ya kufanya kazi Yake, kwa ajili ya zawadi yoyote ambayo Ameiahidi, tunaweza kuomba; basi tunapaswa kuamini kwamba tunapokea, na kurudisha shukrani kwa MUNGU kwamba tumepokea.—(Education, 257, 258) [Pr 57.2; Maombi Aya ya 17]

Maombi ya siri hudumisha Maisha ya Roho — Hatuna haja ya kutafuta ushahidi wa nje unaoonyesha baraka. Zawadi iko katika ahadi, na tunaweza kuendelea na kazi yetu tukiwa na hakika kwamba kile ambacho MUNGU amekiahidi Ana uwezo wa kukitekeleza, na kwamba zawadi, ambayo tayari tunayo, itadhihirika wakati tunapoihitaji zaidi. (Pr 57.3; Maombi Aya ya 18]

Kuishi kwa Neno la MUNGU kunamaanisha kusalimisha Kwake maisha yote. Kutakuwa na hisia ya kuendelea kuwa na uhitaji na utegemezi, kuuvuta moyo kumfuata MUNGU. Maombi ni lazima; kwani ni uhai wa roho. Maombi ya familia, maombi ya hadhara, yana nafasi yake; lakini ni ushirika wa siri na MUNGU ndiyo

unaodumisha maisha ya roho. (Pr 57.4; Maombi Aya ya 19]

Ilikuwa katika mlima pamoja na MUNGU ndiko ambako Musa aliona mfano wa jengo lile la ajabu ambalo lingekuwa mahali pa kukaa pa utukufu Wake. Ni katika mlima pamoja na MUNGU- mahali pa siri pa ushirika - ambapo tunapaswa kuutafakari mpango Wake wa utukufu kwa wanadamu. Ndipo tutakapowezeshwa, na hivyo kutengeneza/kuumba muundo wa tabia yetu ili ahadi Yake itimizwe kwetu, "Nitakaa ndani yao, na nitatembea kati yao, Nami nitakuwa MUNGU wao, nao watakuwa watu Wangu." 2 Wakorintho 6:16. [Pr 57.5; Maombi Aya ya 20]

Ilikuwa ni katika masaa ya maombi ya faragha ndipo ambapo Yesu alipokea hekima na nguvu katika maisha Yake ya duniani. Hebu vijana wafuate mfano Wake katika kutafuta alfajiri na jioni muda wa utulivu kwaajili ya ushirika na Baba yao aliye mbinguni. Hebu wainue mioyo yao kwa MUNGU siku nzima inapoendelea kusonga mbele. Katika kila hatua ya njia zetu anasema, 'Kwa maana Mimi, Bwana, MUNGU wako, nitakushika mkono wako wa kuume, nikikuambia, Usiogope; nitakusaidia.. Isaya 41:13. Endapo watoto wetu wangeluweza kujifunza masomo haya katika miaka yao ya mapema/awali, ni upya gani na nguvu, furaha na utamu ulioje, ambao ungeletwa maishani mwao!—(Education, 258, 259) [Pr 58.1; Maombi Aya ya 21]

Kuomba kwa Imani Huleta Baraka nyingi — Kwa maneno tunayoongea kwa watu na katika maombi tunayotoa, MUNGU anatutaka tutoe ushahidi dhahiri kwamba tuna maisha ya kiroho. Hatufurahii utimilifu wa baraka ambazo Bwana ametuandalia, kwa sababu hatumwombi/hatumwulizi Bwana kwa imani. Laiti tungeitumia imani katika Neno la MUNGU aliye hai tungelikuwa na baraka nyingi. Tunamvunjia MUNGU heshima kwa ukosefu wetu wa imani; na hivyo hatuwezi kuwapa maisha wengine kwa kutoa ushuhuda ulio hai, na wenye kuinua. Hatuwezi kutoa kile ambacho hatumiliki. —(Testimonies for the Church 6:63) [Pr 58.2; Maombi Aya ya 22]

Omba kwa Imani; Kisha Pokea — Kuna nguvu inayopatikana kutoka kwa MUNGU. Anaweza kusaidia. Anaweza kutoa neema na hekima ya mbinguni. Kama utaomba kwa imani, utapata; lakini ni lazima ukeshe katika maombi. Kisha, omba, fanya kazi, ndiyo inapaswa kuwa kauli mbiu yako. - (Testimonies for the Church 2:427) [Pr 58.3; Maombi Aya ya 23]

Imani hupokea Baraka Kabla haijatambulika wala kuhisiwa — nimeona mara kwa mara kwamba watoto wa Bwana hupuuza maombi, haswa maombi ya siri zaidi; kwamba wengi hawatumii imani hiyo ambayo ni haki yao na wajibu wao kuwa nayo, mara nyingi wakingojea hisia ambayo imani pekee inaweza kuleta. Hisia sio imani; hivi ni vitu viwili tofauti. Imani ni yetu tumepewa ili kuizoeza, lakini hisia za furaha na baraka ni MUNGU hutoa. Neema ya MUNGU huijia nafsi kupitia mkondo wa imani hai, na imani hiyo iko katika uwezo wetu kuwa kuifanyia

mazoezi, na kuwa nayo. [Pr 58.4; Maombi Aya ya 24]

Imani ya Kweli inashikilia na kudai baraka iliyoahidiwa kabla haijatambulika na kuhisiwa. Lazima tupeleke ombi letu kwa imani ndani ya pazia la pili na kuacha imani yetu ichukue baraka iliyoahidiwa na kuidai kama yetu. Kisha tunapaswa kuamini kwamba tunapokea baraka, kwa sababu imani yetu imeishikilia, na kulingana na Neno, basi ni yetu. Kristo anasema, "Yo yote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu." Marko 11:24. Hapa kuna imani, imani dhahiri, iliyo wazi kabisa, kuamini kwamba tunapokea mibaraka, hata kabla ya kuitambua. Baraka iliyoahidiwa inapogunduliwa, inapoonekana na hata kufurahiwa, basi imani inamezwa. Lakini wengi hudhani wanayo imani kubwa wanapokuwa wana ushirika kwa kiasi kikubwa na Roho Mtakatifu na kwamba hawawezi kuwa na imani isipokuwa wanahisi nguvu ya Roho. Hilo linachanganya imani na baraka ambayo huja kupitia imani. Wakati hasa wa kutumia imani ni pale tunapohisi kukosa msaada wa Roho. Wakati mawingu mazito ya giza yanaonekana kuigubika akili, basi huo ndio wakati wa kuruhusu imani iliyo hai itoboe giza na kutawanya mawingu. Imani ya Kweli inapatikana katika ahadi zilizo katika Neno la MUNGU, na ni wale tu ambao wanaolitii Neno hilo ndio ambao wanaweza kudai ahadi zake tukufu. "Mkikaa ndani Yangu na Maneno Yangu yakikaa ndani yenu, basi, ombeni chochote mtakacho nanyi mtapewa. (Yohana 15:7). na twaweza kupokea Kwake chochote tunachoomba, maana tunazitii amri Zake na kufanya yale yanayompendeza." 1 Yohana 3:22.—(Early Writings, 72, 73) [Pr 59.1; Maombi Aya ya 25]

Usizimie nguvu ikiwa Hakuna Jibu La Mpapo kwa hapo lililotolewa — Imani yako haipaswi kuachilia ahadi za MUNGU, ikiwa hautaona au kuhisi jibu la haraka la maombi yako. Usiohofu kumtumaini MUNGU. Zitegemee ahadi Zake za kweli: "Ombeni, nanyi mtapewa." MUNGU ni mwenye hekima mno kukosea, na ni mwema sana kuwazuilia watakatifu Wake wanotembea katika unyoofu kitu chochote chema- (Testimonies for the Church 1:120) [Pr 59.2; Maombi Aya ya 26]

Omba; na Kisha Matokeo mwachie MUNGU— Fanya kazi kwa imani, na mwachie MUNGU matokeo. Omba kwa imani, na mafumbo na siri ya majaliwa Yake italeta jibu lake. Kuna mwingine inaelekea kama hutaweza kufaulu. Lakini fanya kazi na uamini, ukiwekamo katika jitihada yako imani, tumaini, na ujasiri. Baada ya kufanya uwezavyo, umngojee Bwana, ukitangaza uaminifu Wake, Naye atatimiza Neno Lake. Subiri, sio kwa hofu, na wasiwasi lakini kwa imani yenye ujasiri, isiyotishika na uwe na kumtegemea Yeye kusikoyumbayumba.—(Testimonies for the Church 7:245) [Pr 59.3; Maombi Aya ya 27]

Omba kwa Ujasiri — Ni maombi ya kutoka moyoni ya imani ambayo husikika mbinguni na kujibiwa duniani. MUNGU anaelewa mahitaji ya wanadamu. Anajua kile tunachotamani hata kabla hatujamwomba. Anaona mgogoro/mzozo wa roho

na mashaka na majaribu. Anaona unyofu wa mwombaji. Atapokea fedheha na mateso ya roho. "Nitamtazama mtu huyu," anatangaza, "hata yeye aliye maskini na mwenye roho iliyopondeka, na anayetetemeka kwa Neno Langu." [Pr 60.1; Maombi Aya ya 28]

Ni fursa yetu kuomba kwa ujasiri, Roho akichochea maombi yetu. Kwa unyenyekevu tunapaswa kuelezea mahitaji yetu kwa Bwana, na kudai ahadi Yake. - (God's Amazing Grace, 92) [Pr 60.2; Maombi Aya ya 29]

Yesu Yu tayari Kusikiliza Maombi Leo Kama Alipokuwa Duniani — Hekima ya Ulimwengu inafundisha kwamba sala sio muhimu. Wanasayansi wanadai kuwa hakuna jibu halisi la ombi; kwamba hii itakuwa ukiukaji wa sheria, muujiza, na kwamba miujiza haipo. Wao husema Ulimwengu unasimamiwa na sheria zisizobadilika, na MUNGU Mwenyewe hafanyi chochote kinyume na sheria hizi. Kwa hivyo wanamwakilisha MUNGU akiwa amefungwa na sheria Zake Mwenyewe-kana kwamba utendaji wa sheria za Mungu unaondoa uhuru wa Bwana, Mwenyezi. Mafundisho hayo yanapingana na ushuhuda wa Maandiko. Je! Miujiza haikufanywa na Kristo na mitume Wake? Mwokozi Huyu Huyu Mwenye huruma anaishi hivi leo, na Yuko tayari kusikiliza maombi ya imani kama vile alipotembea miongoni mwa wanadamu na kukutana nao uso kwa uso (waziwazi kwa kuonekana). - (The Great Controversy, 525) [Pr 60.3; Maombi Aya ya 30]

Maombi ya Imani huonyesha Matakwa Rahisi ya roho— Maombi sio mpatanishi wa dhambi; hayana fadhila au sifa yake yenyewe. Maneno yote tunayoyamiliki na kuyarembesha tunapoyatoa hayalingani hata na shauku moja takatifu. Maombi yaliyopangiliwa vizuri kwa ufasaha zaidi hayana tofauti na maneno ya kubwikabwatika tu ikiwa hayaonyeshi hisia za Kweli za moyo. Lakini ombi linalotoka kwenye moyo wenye dhati na makini, wakati mahitaji sahili ya roho yanapowasilishwa, kama vile tunavyoweza kumwomba jambo rafiki wa kidunia (kuomba feva), tukitarajia tutapata-hili ni ombi la imani. MUNGU hatamani pongezi zetu za sherehe za ibada ya destruri, bali kilio kisichonenea cha moyo uliovunjika na kuhuzunishwa na hisia za dhambi na udhaifu mwingi hupata kibali kwa Baba wa rehema zote. -(Thoughts from the Mount of Blessing, 86, 87) [Pr 60.4; Maombi Aya ya 31]

Maombi humwamsha MUNGU Kutenda-Kwa maombi yako ya imani yenye bidii unaweza kufanya mkono wenye nguvu zote, unaotawala ulimwengu ujongee. Unaweza kuwafundisha watoto wako kuomba kwa ufanisi wanapopiga magoti kando yako. Hebu maombi yapande juu kwenye kiti cha enzi cha MUNGU, "Uwasamehe watu Wako, Ee Bwana, wala usiwape urithi Wako wakosaji, ili mataifa wasiwatawale; wasije kusema miongoni mwao, Yuko wapi MUNGU wao?" MUNGU Yuko kazini Akitenda. Yeye hufanya maajabu, na ingawa Yupo juu na ameinuliwa, maombi yanaweza kufikia kiti Chake cha enzi. Yeye anayegeuka na kupindua juu chini mambo au kuyatangua, Yeye anayeweza kufanya mambo ya ajabu, atazingatia maombi ya toba ya imani kutoka kwa watoto Wake

wanyenyekevu. - (The Review and Herald, Aprili 23, 1889) [Pr 61.1; Maombi Aya ya 32]

MUNGU Hawezi Kujibu Maombi Asiyooombwa — Maombi na Imani vitafanya kile ambacho hakuna nguvu yoyote duniani inaweza kutimiza. Ni nadra sana, katika hali zote, tunawekwa katika nafasi ile ile mara mbili. Tunakuwa na matukio mapya na majaribu mapya ya kuyashinda, ambapo uzoefu wetu wa zamani hauwezi kuwa mwongozo wa kutosha. Lazima tuwe na nuru siku zote inayotoka kwa MUNGU. Kristo daima hutuma ujumbe kwa wale wanaosikia sauti Yake. [Pr 61.2; Maombi Aya ya 33]

Ni sehemu ya mpango wa MUNGU kutupatia, katika kujibu maombi ya imani, kile ambacho hangeweza kutupa endapo tusingemwuliza/hatukumuomba. - (My Life Today, 15) [Pr 61.3; Maombi Aya ya 34]

Wachungaji/Watumishi Wasichoke Katika Maombi — Watumishi wanapaswa kufanya maandalizi ya moyo kabla ya kuanza kazi ya kuwasaidia wengine, kwani walei wamewatangulia wachungaji walio wengi. Wanapaswa kupigana mieleka bila kuchoka katika sala hadi Bwana awabariki. Wakati upendo wa MUNGU unawaka juu ya madhabahu ya mioyo yao, hawatahubiri ili kuonyesha busara au ujanja walio nao, bali watamwasilisha Kristo ambaye huondoa dhambi za ulimwengu. - (Testimonies for the Church 5:166) [Pr 61.4; Maombi Aya ya 35]

Tiba ya Kukata Tamaa au kufa moyo Ni Imani, Maombi, na Kazi — Kwa wale wote waliokata tamaa kuna tiba/dawa moja tu, - imani, sala, na kazi. (Testimonies for the Church 6:438) [Pr 61.1; Maombi Aya ya 36]

Maombi Ndio Silaha Ambayo kwayo Tunampinga Adui — Kristo Ndiye tumaini letu pekee. Njoo kwa MUNGU kwa Jina la Yeye aliyetoa uhai wake kwa ajili ya maisha ya ulimwengu. Tumainia ufanisi wa dhabihu Yake. Onyesha kwamba upendo Wake, furaha Yake, imo katika roho yako, na kwa sababu ya hili, furaha yako imejaa. Katika MUNGU ndiyo nguvu zetu. Omba sana. Maombi ni maisha ya roho. Ombi la imani ni silaha ambayo tunaweza kufanikiwa kupinga kila shambulio la adui. - (The Signs of the Times, Agosti 24, 1904) [Pr 62.2; Maombi Aya ya 37]

Maombi hayapotei, hata ikiwa hayajajibiwa kama tunavyotarajia — Ombi la imani halipotei kamwe; lakini kudai kuwa litajibiwa kila wakati kwa njia ileile na kwa jambo lile lile ambalo tumetarajia, ni dhana tu. - (Testimonies for the Church 1:231) [Pr 62.3; Maombi Aya ya 38]

Mfariji Huja katika kujibu Maombi ya Imani — Wakati wote na mahali pote, katika huzuni zote na shida zote, wakati hali ya nje inaonekana kuwa ni ya giza na ile ya wakati ujao inaleta mfadhaiko, nasi tunajisikia wanyonge na peke yetu, Mfariji atatumwa katika kujibu maombi ya imani. Mazingira yanaweza kututenganisha na kila rafiki wa kidunia; lakini hakuna hali/mazingira, wala

umbali, unaoweza kututenganisha na Mfariji wa mbinguni. Popote tulipo, popote tutakapoenda, Yeye yuko mkono wetu wa kuume kila wakati kutusaidia, kutudumisha, kuttuunza, na kutupa nguvu. - (The Desire of Ages, 669, 670) [Pr 62.4; Maombi Aya ya 39]

Malaika hubeba Maombi yetu kwenda Patakatifu pa Mbinguni — Malaika husikia sadaka za sifa na ombi la imani, na hubeba maombi kwa Yeye anayehudumu katika Patakatifu kwa ajili ya watu Wake, na wanasihi haki na sifa Yake kwa niaba yao. Ombi la Kweli hujitegemeza/humshikilia Yeye aliye mkuu na hutupatia ushindi. Akiwa magotini mwake, Mkristo anapata nguvu za kupinga vishawishi. - (The Review and Herald, Februari 1, 1912) [Pr 62.5; Maombi Aya ya 40]

Ombi la dhati litakanganya Jitihada kali za Shetani — Mwanadamu ni mateka wa Shetani na kwa kawaida amejikita katika kufuata maoni yake adui na kutii matakwa na amri zake. Yeye mwenyewe hana uwezo wa kupinga upinzani maridhawa wa uovu. Ni pale tu Kristo anapokaa ndani yake kwa imani hai, akiziongoza shauku zake na kumtia nguvu kwa uwezo utokao juu, ndipo mwanadamu anaweza kujitosa ili kukabiliana na adui mbaya sana. Njia nyingine yoyote ya ulinzi ni bure kabisa. Ni kupitia njia ya Kristo pekee, ndiyo kwamba nguvu ya Shetani inawekewa ukomo. Huu ni Ukweli muhimu ambao wote wanapaswa kuelewa. Shetani yuko bize kila wakati, akienda huku na huko, akitembea juu na chini katika dunia, akitafuta ambaye anaweza kummeza. Lakini ombi la dhati la imani litakanganya juhudi zake kali. Kisha chukua "ngao ya imani," ndugu, "ambayo kwayo mtaweza kuzima mishale yote ya moto ya yule mwovu." (Testimonies for the Church 5:294) [Pr 63.1; Maombi Aya ya 41]

Ombi la Imani Hushinda Dhidi ya Shetani — Ombi la imani ni nguvu kubwa ya Mkristo na hakika litamshinda Shetani. Hii ndiyo sababu yeye anasisitiza kwamba hatuna haja ya maombi. Jina la Yesu, Wakili wetu, analichukia; na tunapomwendea Kwake kwa dhati kwa ajili ya msaada, Jeshi la Shetani linaogopa. Kusudi lake linatimia vizuri ikiwa tunapuuza mazoea ya kuomba, kwa kuwa maajabu yake ya uwongo yanapokelewa kwa urahisi zaidi. - (Testimonies for the Church 1:296) [Pr 63.2; Maombi Aya ya 42]

SURA YA 7

MAOMBI NA UTII

Omba na Fanya Kazi — Hatupaswi kukaa kwa utulivu kama maji ya mtungini eti tunangojea udhalimu na dhiki vitufikie, na kukunja mikono yetu, bila kufanya chochote kuzuia maovu. Hebu vilio vyetu kwa pamoja vitumwe juu mbinguni. Omba na ufanye kazi, na fanya kazi na usali. Lakini usifanye chochote kwa kukurupuka. Jifunze kuliko wakati mwingine wowote ule kuwa lazima uwe mpole na mnyenyekevu wa moyo. -(Selected Messages 2:370, 371) [Pr 64.1; Maombi Aya ya 1]

Lazima tuombe na tufanye kazi na kuamini. Bwana Ndiye ufanisi wetu. (Evangelism, 438) [Pr 64.2; Maombi Aya ya 2]

Utalazimika kupambana mieleka na magumu, kubeba mizigo, kutoa ushauri, kupanga mikakati na kutiekeleye, ukimtazama MUNGU kila kwa ajili ya msaada. Omba na fanya kazi, fanya kazi na omba; kama wanafunzi katika shule ya Kristo, jifunzeni kuhusu Yesu. (Testimonies to Ministers and Gospel Workers, 498, 499) [Pr 64.3; Maombi Aya ya 3]

Maombi ni mkakati wa mbingu wa Mafanikio katika Kuishinda Dhambi — Kuna wengi ambao, japo wanajitahidi kuzitii amri za MUNGU, wana amani kidogo au furaha. Upungufu huu katika uzoefu wao ni matokeo ya kushindwa kupata imani. Wanatembea kana kwamba wapo katika nchi yenye chumvi, iliyo na ardhi iliyokauka na kupasuka vipandevipande. Wanaomba au kudai kidogo tu, wakati wanaweza kuomba mengi; kwani ahadi za MUNGU hazina kikomo. Hao hawawakilishi kwa usahihi utakaso unaokuja kwa kuitii ile Kweli. Bwana angependa wana na binti ake wote wawe na furaha, amani, na utiifu. Kwa kuizoesha Imani, mwamini anafikia mahali pa kuzimiliki baraka hizi. Kupitia imani, kila upungufu wa tabia unakarabatiwa, kila unajisi unasafishwa, kila kosa linarekebishwa, kila ubora unapata kuendelezwa na kuwa na ufanisi zaidi na zaidi. [Pr 64.4; Maombi Aya ya 4]

Maombi ni njia iliyowekwa na mbingu kwaajili ya mafanikio katika vita na dhambi na ukuaji wa tabia ya Kikristo. Ushawishi wa Bwana unaokuja ili kujibu ombi la imani utatimiza katika roho ya mwombaji yote ambayo anaomba. Kwa

ajili ya msamaha wa dhambi, kwaajili ya Roho Mtakatifu, kwaajili sifa na tabia kama ya Kristo, kwa hekima na nguvu ya kufanya kazi Yake, kwa zawadi yoyote ambayo ameahidi, tunaweza kuomba; na ahadi ni, "Mtapokea." (The Acts of the Apostles, 563, 564) [Pr 65.1; Maombi Aya ya 5]

Majaribu ya kila siku Hufanya Maombi Kuwa jambo la Lazima— Nguvu inayopatikana katika maombi na MUNGU, ikiunganishwa na juhudi za mtu binafsi katika kuifundisha akili kufikiri kwa kina na kuwa na uangalifu/usikivu, humwandaa mtu huyo kwa ajili ya majukumu ya kila siku na hufanya roho iwe na amani katika hali zote, haijalishi hali ni ngumu kwa kiasi gani. Majaribu ambayo tunakuwa katika mazingira yake kila siku hufanya maombi kuwa jambo la lazima (majaribu ambayo tunaanikwa kwayo kila siku, hufanya maombi kuwa jambo la lazima). Ili tuweze kulindwa na uweza wa MUNGU kwa njia ya imani, shauku za akili zinapaswa kuelekezwa mbinguni daima katika maombi ya kimya ili kupata msaada, kupata nuru, kupata nguvu, kupata maarifa. Lakini fikra na maombi hayawezi kuchukua nafasi ya kuwa dhati, na kutenda kwa juhudi katika kutumia muda vizuri kwa uaminifu. Kazi na sala zinahitajika katika kukamilisha tabia ya Kikristo. —(Testimonies for the Church 4:459) [Pr 65.2; Maombi Aya ya 6]

Maombi ya Kila siku Huguza Makosa Kuwa Ushindi — Ikiwa mtu ambaye kila siku anashirikiana na MUNGU anapotea njia kwa kutenda makosa, ikiwa anageuka kwa nukta chache kutoka kwenye kumwangukia Yesu kwa uthabiti, sio kwa sababu anatenda dhambi kwa makusudi; kwani anapoliona kosa lake, anarudi tena, na kumtazama Yesu, basi ule uhalisia kwamba amekosea, haumfanyi ashuke thamani mbele ya moyo wa MUNGU. Anajua kwamba ana ushirika na Mwokozi; na anapokemewa kwa kosa lake katika suala fulani la maamuzi yake, hatembe na jazba moyoni au, au chuki ya kimya kimya na kumlalamikia MUNGU, bali huligeuza lile kosa na kuwa ushindi. Anajifunza somo kutoka kwenye Maneno ya Mwalimu, na anachukua tahadhari ili asidanganyike au kudanganywa tena. - (The Review and Herald, Mei 12, 1896) [Pr 65.3; Maombi Aya ya 7]

Kristo Ndiye Njia Ya Maombi Kati Yetu na MUNGU— Kristo ndiye kiunganishi kati ya MUNGU na mwanadamu. Ameahidi maombezi Yake binafsi. Anaweka fadhila yote ya haki Yake upande wa mwombaji. Kristo amamuomba mwanadamu, na mwanadamu, anayehitaji msaada wa Mungu, anajiombea mbele za MUNGU, akitumia nguvu ya ushawishi wa Yule aliyetoa maisha Yake kwa ulimwengu. Tunapokiri mbele za MUNGU ukubali wetu wa uzuri wa Kristo, manukato hutolewa kwa maombezi yetu. Tunapomkaribia MUNGU kupitia fadhila ya Mkombozi, Kristo hutuweka karibu na upande Wake, akituzunguka kwa mkono Wake wa kibinadamu, wakati kwa mkono Wake wa Kiungu Yeye anashikishika kiti cha enzi cha Yule Asiye na mwisho. Yeye anaweka sifa, wema na haki Yake, kama uvumba mtamu, ndani ya chetezo mikononi mwetu, ili kutia moyo maombi

yetu. Anaahidi kusikia na kujibu maombi yetu. [Pr 66.1; Maombi Aya ya 8]

Naam, Kristo amekuwa njia ya maombi kati ya mwanadamu na MUNGU. Pia amekuwa njia ya baraka kati ya MUNGU na mwanadamu. Ameunganisha Uungu na ubinadamu. Watu wanapaswa kushirikiana Naye kwa ajili ya wokovu wa roho zao wenyewe, na kisha kufanya jitihada za bidii, za kudumu na za dhati ili kuwaokoa wale ambao wako tayari kufa. - (Testimonies for the Church 8:178) [Pr 66.2; Maombi Aya ya 9]

Wakati kuhani mkuu analinyunyiza damu iliyo na joto bado juu ya Kiti cha Rehema wakati wingu la uvumba lenye harufu nzuri likipanda mbele za MUNGU, ndivyo ambavyo wakati tunakiri dhambi zetu na kuomba ufanisi na haki ya damu ya upatanisho ya Kristo, sala zetu zinapaswa kupaa mbinguni, zikiwa na harufu nzuri na sifa za tabia ya Mwokozi wetu. Pamoja na kutostahiki/li kwetu, tunapaswa kukumbuka kwamba Yupo Yule Anayeweza kuchukua dhambi, na Ambaye Yuko tayari kufanya hivyo, Naye Anahangaika kumwoko mwenye dhambi. Kwa damu Yake Mwenyewe alilipa penalty/adhabu kwa wacosaji wote. Kila dhambi iliyowasilishwa mbele za MUNGU kwa moyo uliopondeka, ataiondoa. "Ijapokuwa dhambi zako ni nyekundu, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa ni nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama sufu." The Review and Herald, Septemba 29, 1896) [Pr 66.3; Maombi Aya ya 10]

Maombi hayana maana au faida yo yote ikiwa Kuna Uovu wa Kukusudia Moyoni- "Neema ya MUNGU iletayo wokovu imeonekana kwa watu wote, ikitufundisha kwamba, tukikataa uovu na tamaa za ulimwengu, tunatakiwa kuishi kwa kiasi, na haki, na utauwa, katika ulimwengu huu wa sasa." Basi, muwe wakamilifu kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu. Je! Maombi yako yana thamani au faida gani ukiwa unawazia au kuuzingatia uovu uliopo ndani ya mioyo yenu? Msipofanya badiliko la dhati, muda sio mrefu, mtachoka kukemewa au kupewa maonyo, kama walivyofanya wana wa Israeli; na, kama wao, mtamwasi MUNGU. Baadhi yenu manakubali kukemewa kwa maneno, lakini mioyoni mwenu hamkubali. Mnaenenda sawa na hapo awali, mkiguswa kwa udogo zaidi na ushawishi wa Roho wa MUNGU, mnazidi kupofushwa zaidi na zaidi, na kuwa hekima pungufu zaidi, kujitawala au kujizuia nafsi kwa udogo zaidi, mmepungukiwa na nguvu ya maadili zaidi, na bidii kidogo na kufurahiya uzoefu wa kidini/kiroho kwa udogo zaidi; na, msipoongoka, hatimaye mtatanga mbali na kumwacha MUNGU kabisa. Hamkufanya mabadiliko katika maisha yenu wakati karipio lilipowajia, kwa sababu hamjaona na kugundua kasoro zenu za kitabia na tofauti kubwa kati ya maisha yenu na maisha ya Kristo. Imekuwa sera yenu kujiweka katika mazingira ambayo hamtapoteza kabisa ujasiri mlio nao kwa ndugu zenu. -(Testimonies for the Church 4:332) [Pr 67.1; Maombi Aya ya 11]

Maombi hayachukui Nafasi ya Utii — Kuna masharti ya kutimizwa ahadi za MUNGU, na ombi haliwezi kuchukua mahali pa wajibu. "Ikiwa mnanipenda," Kristo anasema, "mtazishika amri Zangu." "Azipokeaye amri Zangu na kuzishika, yeye

ndiye anipendaye. Naye anipendaye Mimi atapendwa na Baba Yangu, Nami nitampenda na kujidhihirisha Kwake." Yohana 14:15, 21. Wale ambao huleta maombi yao kwa MUNGU, wakidai ahadi Zake wakati hawafuati masharti, wanamtukana Yehova (au wanamkosea heshima Mungu). Hao huleta Jina la Kristo kama mamlaka yao kwa ajili ya kutimiziwa ahadi, lakini hawafanyi mambo yale ambayo yangeonyesha imani katika Kristo na upendo Kwake Yeye. [Pr 67.2; Maombi Aya ya 12]

Wengi wanapoteza haki ya masharti ya kukubaliwa na Baba. Twahitaji kuchunguza kwa ukaribu tendo la kumtegemea Yeye wakati tunapokuwa tunamkaribia MUNGU. Ikiwa sisi si watiifu, tunamletea Bwana hundi ya kupewa malipo wakati sisi hatujatimiza masharti ambayo yangeidhinisha malipo yetu. Tunawasilisha kwa MUNGU ahadi Zake, na kumwomba azitimize, wakati kwa kufanya hivyo atalivunjia heshima Jina Lake Mwenyewe. [Pr 68.1; Maombi Aya ya 13]

Ahadi ni "Mkikaa ndani Yangu na maneno Yangu yakikaa ndani yenu, basi, ombeni chochote mtakacho nanyi mtapewa. (Yohana 15:7). Na Yohana anatangaza: "Katika hili twajua ya kuwa tunamjua Yeye, ikiwa tunazishika amri Zake. Mtu akisema kwamba anamjua, lakini hazitii amri Zake, basi mtu huyo ni mwongo, na Kweli haimo ndani yake. Bali yeye ashikaye Neno Lake, katika huyo upendo wa MUNGU umekamilika kweli kweli." 1 Yohana 2: 3-5.— (Christ's Object Lessons, 143, 144) [Pr 68.2; Maombi Aya ya 14]

Twapaswa Kuamini MUNGU Anasikia na Kisha kuyaishi Maombi Yetu — Watoto na vijana wanaweza kuja kwa Yesu na mizigo yao na mifadhaiko yao, wakifahamu kwamba Ataheshimu maombi yao Kwake, na kuwapa yale wanayohitaji. Kuwa na bidii; kuwa imara. Wasilisha ahadi ya MUNGU, na kisha uamini bila shaka hata moja. Usingoje kupata hisia maalum kabla ya kufikiria Bwana anajibu. Usikariri na kuweka alama kwamba kuna njia fulani ambayo Bwana lazima aitumie au kuifanyia kazi kwako kabla ya wewe kuamini kuwa utapokea vitu ulivyoomba Kwake; lakini amini Neno Lake, na Ukabidhi kila kitu mikononi mwa Bwana, ukiwa na imani kamili kwamba maombi yako yataheshimiwa, na jibu litakuja wakati muafaka na kwa njia ambayo Baba yako wa mbinguni anaona ni kwa faida yako; na kisha ishi maombi yako. Tembea kwa unyenyekevu na endelea kusonga mbele. -(Messages to Young People,123) [Pr 68.3; Maombi Aya ya 15]

Omba kwa ajili ya Neema ya kuyapinga majaribu-Katika maisha ya kila siku utakutana na mishangao ya ghafla, kukatishwa tamaa, na vishawishi. Neno linasema nini? "Mpingeni shetani," kwa kumtegemea Mungu kabisa, "naye atawakimbia. Mkaribieni MUNGU, Naye atawakaribia ninyi. Na ashikilie nguvu Zangu, ili afanye amani Nami; naye atafanya amani Nami." Mtazame Yesu kila wakati na kila mahali, ukitoa maombi ya kimya kutoka katika moyo mwaminifu ili ujue jinsi ya kufanya mapenzi Yake. Kisha adui anapoingia kama mafuriko, Roho

wa Bwana atakuinua kiwango chako dhidi ya adui. Unapokaribia kuanguka au kutekewa na jaribu, kupoteza uvumilivu na kuitawala nafsi, kuwa mgumu na mwenye kulaani, kutafuta makosa na kumchukia mtu, kukosoa, kufanya ujeuri, kufanya ukatili au kulaumu — huu ni wakati wako kutuma ombi mbinguni, "Nisaidie, Ee MUNGU, kupinga jaribu, kuondoa uchungu wote na ghadhabu na kunena mabaya kutoka moyoni mwangu. Nipe upole Wako, unyenyekevu Wako, uvumilivu Wako, na upendo Wako. Usiniache nimuaibishe Mkombozi wangu, nisitafsiri vibaya maneno na nia ya mke wangu, watoto wangu, na kaka na dada zangu katika imani. Nisaidie nipate kuwa mwema, mwenye moyo laini/mwororo, mwenye huruma, mwenye kusamehe. Nisaidie kuwa mfunga-nyumba (mweka nyumba sawa), yaani mlinzi wa kweli nyumbani mwangu na kuwakilisha tabia ya Kristo kwa wengine." *(mume kingereza ni husband-houseband Kamba ya kufunga nyumba yake kwa ulinzi na upendo na yale bora) (The Adventist Home, 214, 215) [Pr 68.4; Maombi Aya ya 16]

Tunajua hatari na vishawishi zinazowazinga vijana wakati huu sio chache au ndogo.....Twaishi katika wakati ambapo kupinga uovu kunahitaji kukesha na kuomba kila wakati. Neno la MUNGU lenye thamani ndiyo kiwango kwa vijana ambao watakuwa waaminifu kwa Mfalme wa mbinguni. Heb una wasome Maandiko. Hebu na waweke kwenye kumbukumbu kwa kukariri mstari baada ya mstari, na wapate ujuzi wa kile Bwana Alichosema Na katika majaribu hebu vijana watandaze Neno la MUNGU mbele yao, na kwa mioyo iliyo na unyenyekevu, na kwa imani, wamtafute Bwana kwa ajili ya hekima ili kujua njia Yake, na kwa nguvu wakanyage na kutembea ndani Yake [Pr 69.1; Maombi Aya ya 17]

Hebu vijana wetu waanzishe vita dhidi ya kila tabia ambayo ina hatari hata ile ndogo ya kuongoza roho mbali na wajibu na kujitoa wakfu. Na watenge misimu fualni kwa ajili ya maombi, bila kupuuza masaa hayo kamwe, ikiwa inaweza kuepukika. Ikiwa wataenda vitani na tabia zao mbaya walizokuwa nazo kabla ya kukiri ushirika na Kristo, wataangukia kuwa windo la hila za Shetani kwa urahisi. Lakini wakiwa wamejihami na Neno la MUNGU, wakiwa wamelithamini moyoni na akilini, watatoka bila kuumizwa na mashambulio yote ya maadui wa MUNGU au mwanadamu. - (My Life Today, 315) [Pr 69.2; Maombi Aya ya 18]

SURA YA 8

MAOMBI YALETAYO USHINDI

Usiachilie ahadi za MUNGU— Kila mtakatifu ambaye anamuendea MUNGU kwa moyo wa kweli, na kutuma maombi yake ya uaminifu Kwake kwa imani, atajibiwa maombi yake. Imani yako haipaswi kuziachilia ahadi za MUNGU, ikiwa hautaona au kuhisi jibu la haraka kwa maombi yako. Basi Usipate hofu kumtumaini MUNGU. Zitegemee ahadi Zake za Kweli: "Ombeni, nanyi mtapewa." MUNGU ni mwenye busara isiyo na ukomo kiasi kwamba hakosei, na ni mwema sana kuwazuilia watakatifu Wake wanaotembea kwa unyoofo mbele Zake kitu chochote kilicho kizuri. Mwanadamu hukosea, na japokuwa maombi yake yanatumwa kutoka katika moyo ulio mkweli, huwa haombi mara zote vitu ambavyo ni vyema kwake, au vile ambavyo vitamtukuza MUNGU. Wakati hili likiwa hivyo, Baba yetu mwenye busara na mwema husikia maombi yetu, na atajibu, wakati mwingine hujibu haraka; lakini Yeye hutupatia vitu ambavyo ni kwa faida yetu na utukufu Wake Mwenyewe. MUNGU hutupatia baraka; laiti tungeangalia mkakati Wake, tungeona kwa uwazi kwamba, Yeye Anajua kilicho bora kwaajili yetu na kwamba maombi yetu hujibiwa. Hakuna chochote cha kutuumiza tutakachopewa, ila tu baraka tunazohitaji, badala y kilea kitu tuliomba ambacho hakitakuwa kizuri kwetu, na ambacho kingetuumiza. [Pr 70.1; Maombi Aya ya 1]

Niliona kwamba ikiwa hatuhisi/hatuoni majibu ya haraka ya maombi yetu, tunapaswa kushikilia imani yetu kwa bidii, bila kuruhusu mashaka kuingia ndani yetu, kwani hayo yatatutenganisha tu na MUNGU. Endapo Imani yetu itatetereka, basi hatutapokea kitu chochote kutoka Kwake. Imani yetu kwa MUNGU inapaswa kuwa imara; na tunapokuwa na uhitaji mkubwa zaidi, baraka itatuangukia kama matone ya mvua. —(Testimonies for the Church 1:120, 121) [Pr 70.2; Maombi Aya ya 2]

Maombi yetu yanapaswa kuwa ya bidii na yasiyotikiswa— MUNGU hasemi uombe mara moja tu, na kisha utapokea. Anatumuru kuomba. Bila kuchoka tusitikisike katika maombi. Kuomba kwa imani imara humleta mwombaji kwenye mkao wa bidi, na humpatia tamano linalozidi kupokea mambo aliyoyaomba. Kristo alisema kwa Martha kaburini kwa Lazaro, "Mimi sikukwambia ya kwamba ukiamini utauona utukufu wa Mungu?" Yohana 11:40. [Pr 71.1; Maombi Aya ya 3]

Lakini wengi hawana imani iliyo hai. Hii ndio sababu hawaoni zaidi nguvu za MUNGU. Udhaifu wao ni matokeo ya kutokuamini kwao. Wana imani zaidi katika matendo yao kuliko utendaji kazi wa MUNGU kwao. Wanajipigania wenyewe (wanajitunza wenyewe). Wanapanga na kuweka mikakati, lakini husali kidogo, na hawamtumaini Mungu kwa ukubwa. Wao hufikiri kwamba wana imani, lakini kumbe ni msukumo tu wa muda mfupi. Wanashindwa kutambua uhitaji wao wenyewe, au utayari wa MUNGU kutoa, nao hawavumilii katika kuweka maombi yao mbele za Bwana. [Pr 71.2; Maombi Aya ya 4]

Maombi yetu yanapaswa kuwa ya bidii na yasiyotikiswa kama ilivyokuwa ombi

la yule rafiki masikini aliyekwenda kuomba mikate usiku wa manane. Kwa kadiri tunavyoomba kwa bidii na uthabiti, ndivyo muungano wetu wa kiroho na Kristo utakavyokuwa wa karibu zaidi. Tutapokea baraka zilizoongezeka kwa sababu tumeongezeka kiiimani. [Pr 71.3; Maombi Aya ya 5]

Fungu letu ni kuomba na kisha kuamini. kesheni mkiomba. Keshi, na ushirikiane na MUNGU anayesikia maombi. Kumbuka kwamba "sisi ni watenda kazi pamoja na MUNGU." 1 Wakorintho 3: 9. Sema na kutenda kulingana na maombi yako. Na hilo litafanya tofauti kubwa kwako pale jaribu litakapokujia ili kuhakikisha kuwa Imani yako ni ya Kweli, au kuonyesha kwamba maombi yako ni mfano tu. [Pr 71.4; Maombi Aya ya 6]

Daudi anatangaza, "Nampenda Bwana, kwa sababu amesikia sauti yangu na dua zangu. Kwa sababu amenitegea sikio lake, kwa hivyo nitamwita siku zangu zote." Wema wa MUNGU katika kusikia na kujibu maombi hutuweka chini ya jukumu zito la kutoa shukrani zetu kwa neema tulizopewa. Tunapaswa kumsifu MUNGU zaidi kuliko tunavyofanya sasa. Baraka zilizopokelewa katika jibu la maombi zinapaswa kutambuliwa mara moja. Kumbukumbu zake zinapaswa kuwekwa katika shajara yetu, ili tunapokishika kitabu mkononi, tuweze kukumbuka wema wa Bwana, na kulisifu jina Lake takatifu. - (The Review and Herald, Mei 7, 1908) [Pr 95.3; Maombi Aya ya 19]

Tabia zetu zinaweza Kubadilishwa – Mabadiliko tunayohitaji ni mabadiliko ya moyo, na yanaweza kupatikana tu kwa kumtafuta MUNGU mtu mmoja mmoja kwa ajili ya baraka Zake, kwa kumwomba Yeye kwa ajili ya nguvu Zake, kwa kuomba kwa bidii ili neema Yake itujie, na kwamba tabia zetu zinaweza kubadilishwa. Haya ndio mabadiliko tunayohitaji leo, na ili kupata uzoefu huu tunapaswa kutumia nguvu ya kudumu na kuonyesha bidii ya moyoni. Tunapaswa kuuliza kwa ukweli mtiifu, "Nifanye nini ili niokolewe?" Tunapaswa kujua ni hatua zipi tunachukua kuelekea mbinguni. - (Selected Messages 1:187) [Pr 94.4; Maombi Aya ya 20]

Uelewa wetu wa Neno la MUNGU utapanuliwa— Hakuna mtu aliye salama hata kwa siku moja au saa bila maombi. Hakika tunapaswa kumwomba Bwana kwa ajili ya hekima ya kulielewa Neno Lake. Hapa Unafunuliwa ujanja na hila zake mshawishi na zile mbinu ambazo anaweza kupingwa kwa mafanikio. Shetani ni mtaalam aliyebobea katika kunukuu Maandiko, akiweka tafsiri yake mwenyewe juu ya vifungu, ambavyo anatarajia kutufanya sisi tujikwae. Tunapaswa kujifunza Biblia kwa unyenyekevu wa moyo, bila kupoteza mtazamo wetu juu ya utegemezi wetu kwa MUNGU. Ingawa inabidi tujilinde kila wakati dhidi ya hila za Shetani, tunapaswa kuomba kwa imani daima: "Usitutie kwenye majaribu." The Great Controversy, 530) [Pr 95.1; Maombi Aya ya 21]

Biblia haifai kusomwa bila maombi. Roho Mtakatifu Ndiye peke yake anaweza kutufanya tuhisi umuhimu wa vile tunavyovisoma kueleweka, au kutuepusha kuunyagua ule Ukweli mgumu katika ufahamu ili uendane na matakwa yetu. Ni kazi ya ofisi ya malaika wa mbinguni kuandaa mioyo ili kulielewa Neno la MUNGU ili tuweze tuvutiwe na uzuri wake, tukishauriwa na maonyo yake, au kuhuishwa na kuimarishwa na ahadi zake. Tunapaswa kufanya ombi la mwandishi wa-Zaburi kuwa letu wenyewe: "Fungua macho yangu, ili nipate kuona maajabu ya sheria

Yako." Zaburi 119:18. Majaribu mara nyingi huonekana hayapingiki kwa sababu, kupitia kupuuza maombi na kusoma Biblia, mtu aliyejaribiwa hawezi kukumbuka ahadi za MUNGU kwa urahisi na kukutana na Shetani akiwa na silaha za Maandiko. Lakini malaika wanawazunguka wale ambao wako tayari kufundishwa katika mambo ya Bwana/mbingu; na wakati wa ulazima mkubwa, watawakumbusha Kweli zile ambazo zinahitajika. Kwa hivyo "wakati adui atakapokuja kama mafuriko, Roho wa Bwana atainua kiwango dhidi yake." Isaya 59: 19— (The Great Controversy, 599, 600) [Pr 95.2; Maombi Aya ya 22]

SURA YA 11

MAOMBI YALIYOJIBIWA

MUNGU Atajibu, ikiwa tutaomba- Hekima ya ulimwengu inafundisha kwamba maombi jambo la lazima. Wanasayansi wanadai kuwa hakuna jibu halisi kwa sala; kwamba hii itakuwa ukiukaji wa sheria, muujiza, na kwamba miujiza haipo. Wao husema kwamba Ulimwengu wote (universe), unasimamiwa na sheria zisizobadilika, na hata MUNGU mwenyewe hafanyi chochote kinyume na sheria hizi. Kwa hivyo wanamwakilisha MUNGU akiwa amefungwa na sheria Zake mwenyewe-kana kwamba utendaji wa sheria za Bwana unamwondolea uhuru Wake Mungu (Uungu unakosa uhuru kufanya unavyotaka). Mafundisho hayo yanapingana na ushuhuda wa Maandiko. Je! Miujiza haikufanywa na Kristo na mitume Wake? Mwokozi Huyo Huyo Mwenye huruma anaishi leo, na Yuko tayari kusikiliza maombi ya imani kama vile alipotembea waziwazi na akaonekana miongoni mwa wanadamu. Maumbile ya asilia hushirikiana na nguvu za Mungu zipitizao nguvu zote, kutenda miujiza,. Ni sehemu ya mpango wa MUNGU kutupatia sisi kwa kuyajibu maombi ya imani, yale ambayo asingetupatia kama itusingemwuliza/tusingemwomba. (The Great Controversy, 525) [Pr 96.1; Maombi Aya ya 1]

Unapopata fursa ya kukutana na ndugu zako kanisani, waambie juu ya umuhimu wa kuweka wazi mfereji wa mawasiliano kati ya MUNGU na roho/moyo. Waambie kwamba ikiwa watakuwa/watapata moyo na sauti ya kuomba, basi

MUNGU pia atapata/atakuwa na majibu kwa maombi yao. Waambie wasipuuze majukumu yao ya kidini/kiroho. Wahimize na kuwatia moyo ndugu zako kusali. Lazima tutafute ikiwa tutapata, lazima tuombe ikiwa tutapokea, lazima tubishe hodi ikiwa tutafunguliwa mlango. - (The Signs of the Times, Februari 10, 1890) [Pr 96.2; Maombi Aya ya 2]

Yesu hatuiti tumfuate, na kisha atutelekeze. Ikiwa tusalimisha maisha yetu kwa ajili ya huduma Yake, hatuwezi kamwe kuwekwa katika nafasi ambayo MUNGU hajaandaa majaliwa Yake. Katika hali yetu yoyote, tuna Mwongozo wa kuongoza njia yetu; shida zetu zozote, tunaye Mshauri wa kweli; huzuni yetu yote, kufiwa, au upweke, tunaye Rafiki anayetuhurumia. Ikiwa pasipo kujua au ujinga wetu tunafanya makosa, Kristo hatuachi [Pr 97.1; Maombi Aya ya 3]

Na mkiwa na imani, chochote mtakachoomba katika sala, mtapata." [Mathayo 21:22.] - (Gospel Workers, 263) [Pr 97.2; Maombi Aya ya 4]

Baraka za MUNGU zitakuja kama matokeo ya Imani ya Unyenyekevu - Uhusiano wa karibu na mbingu utatoa toni/mwitikio sahihi kwa uadilifu wako na utakuwa msingi wa mafanikio yako. Hisia zako za utegemezi zitakusukuma kwenye sala, na kuhisi kwako kuwajibika kutakupelekea kufanya jitihada za dharura. Maombi na bidii, bidii na maombi, vitakuwa shughuli ya maisha yako. Lazima uombe kana kwamba ufanisi na sifa zote zinategemea na utendaji wa MUNGU tu, na kufanya kazi kana kwamba jukumu ni lako wewe mwenyewe tu. Ukitaka nguvu unaweza kuwa nayo; inasubiri rasimu/amri yako tu. Mwamini MUNGU tu, muendee kwa Neno Lake, tenda kwa imani, na baraka zitakuja. [Pr 97.3; Maombi Aya ya 5]

Katika suala hili, euwzo wa akili nyingi za asili kwenye ubongo (genius), mantiki, na ufasaha/umbuji havitafaulu. Wale ambao wana unyenyekevu, wanamtegemea Mungu, na wenye moyo uliopondeka, MUNGU huwakubali, na husikia maombi yao; na MUNGU anaposaidia, vikwazo vyote vitaondolewa. Ni watu wangapi wenye uwezo mkubwa wa asili, talaluma/elimu ya hali ya juu wameshindwa walipowekwa katika nafasi za uwajibikaji, wakati wale wa akili dhaifu, na mazingira duni, wamefanikiwa sana. Siri ni: Wale wenye uwezo wa asili na elimu, walijiamini wao wenyewe, wakati wale dhaifu waliungana na Yeye ambaye ni Mshauri wa Ajabu na Jemedari hodari katika kufanya kazi kutimiza Yale ambayo amepanga kutokana na mapenzi Yake. — (Testimonies for the Church 4:538, 539) [Pr 97.4; Maombi Aya ya 6]

Maombi rahisi yamesukuwa na Roho Mtakatifu yatapanda kupitia malango wazi, mlango ulio wazi ambao Kristo ametangaza: Nimefungua [47], na hakuna mtu anayeweza kufunga. Maombi haya, yaliyochanganywa na uvumba wa ukamilifu wa Kristo, yatapanda kama manukato kwa Baba, na majibu yatakuja. —(Testimonies for the Church 6:467) [Pr 97.5; Maombi Aya ya 7]

Maombi ya Unyenyekevu na Imani kama ya Mtoto Yatajibiwa - "Ikiwa mtu yeyote ana kiu, na aje Kwangu anywe." Lakini atakayekunywa maji nitakayompa Mimi, hataona kiu milele. Maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji ya uzima na kumpatia uzima wa milele." Yohana 7:37; Yohana 4:14. [Pr 98.1; Maombi Aya ya 8]

Ikiwa, pamoja na ahadi hizi mbele yetu, tunachagua kubaki wakavu na kuwa na kiu kwa kukosa maji ya uzima, ni kosa letu wenyewe. Ikiwa tungekuja kwa Kristo tukiwa na unyenyekevu wa mtoto anavyoenda kwa wazazi wake wa kidunia, na kuomba vitu ambavyo ameahidi, tukiamini kwamba tunavipokea, hakika tutakuwa navyo. - (Testimonies for the Church 9:179) [Pr 98.2; Maombi Aya ya 9]

Omba na Amini – MUNGU hasemi, Omba mara moja, nawe utapata. Yeye anatusihi tuombe. Tuendeleo kuomba bila kupata uchovu. Kudumu katika maombi kunamleta mwombaji katika kujibidisha zaidi, na kumpa shauku ya dhati zaidi, na kuongeza shauku ya kupokea vitu anavyoomba. Kristo alimwambia Martha kwenye kaburi la Lazaro, "Ikiwa utaamini, utaona utukufu wa MUNGU." Yohana 11:40. [Pr 98.3; Maombi Aya ya 10]

Lakini wengi hawana imani hai. Hii ndio sababu hawaoni uwezo wa MUNGU zaidi. Udhaifu wao ni matokeo ya kutokuamini kwao. Wana imani zaidi katika matendo yao kuliko utendaji kazi wa MUNGU kwao. Wanajipigania na kujitunza wao wenyewe.

Wanapanga na kuweka mikakati, ila wanasali kidogo, na wana mategemeo madogo kwa MUNGU. Wao hufikiri kwamba wana imani, lakini ni msukumo tu wa kitambo kidogo tu. Wanashindwa kutambua hitaji lao wenyewe, au utayari wa MUNGU kutoa, hawana uvumilivu katika kuyaweka maombi yao mbele za Bwana. [Pr 98.4; Maombi Aya ya 11]

Maombi yetu yanapaswa kuwa ya dhati, bidii na ya kudumu hata katika wakati mgumu kama ilivyokuwa ombi la rafiki masikini aliyeomba mikate usiku wa manane. Kadiri tunavyoomba kwa bidii na uthabiti, ndivyo muungano wetu wa kiroho na Kristo utakavyokuwa karibu zaidi. Tutapokea baraka zilizoongezeka kwa sababu tumeongezeka kiimani. [Pr 98.5; Maombi Aya ya 12]

Fungu letu ni kuomba na kuamini. kesheni mkiomba. Kesho, na ushirikiane na MUNGU anayesikia maombi. Kumbuka kwamba "sisi ni watenda kazi pamoja na MUNGU." 1 Wakorintho 3: 9. Sema na tenda kulingana na maombi yako. Itafanya tofauti kubwa kwako hata utakapo jaribiwa imani yako kuhakikisha kuwa ya kweli, au kuonyesha kwamba maombi yako ni desturi au kutekeleza wajibu tu.—(Christ's Object Lessons, 145, 146) [Pr 99.1; Maombi Aya ya 13]

Omba kwa Imani na Majibu Yatakuja – Masomo ambayo MUNGU hutuma kila wakati, ikiwa yataeleweka vizuri, yataleta msaada kwa wakati unaofaa.

Wekategemeo lako kwa MUNGU Omba sana, na uamini. Kwa Kuamini, kutumaini, kutegemea, mkishikilia kwa nguvu Mkono wenye Nguvu isiyo na kipimo, mtakuwa zaidi ya washindi. [Pr 99.2; Maombi Aya ya 14]

Wafanyakazi wa kweli hutembea na kufanya kazi kwa imani. Wakati mwingine wanachoka kwa kutazama maendeleoya kazi yanavyozorota wakati vita vinapopamba moto kati ya nguvu za mema na mabaya. Lakini wakikataa kushindwa au kuvunjika moyo wataona mawingu yakitawanyika na ahadi ya ukombozi ikitimizwa. Kupitia ukungu ambao Shetani amewazunguka nao, wataona mwangaza wa miale inayong'aa ya Jua la Haki. [Pr 99.3; Maombi Aya ya 15]

Fanya kazi kwa imani, na mwachie MUNGU matokeo. Omba kwa imani, na mafumbo/siri ya majaliwa Yake italeta jibu Lake. Wakati mwingine inaweza kuonekana kuwa huwezi kufaulu. Lakini fanya kazi na uamini, ukiweka imani, tumaini, na ujasiri katika jitihada zako. Baada ya kufanya uwezavyo, mwachie Bwana, ukitangaza uaminifu Wake, Naye atatimiza Neno Lake. Subiri, sio kwa wasiwasi au kwa kukosa utulivu, lakini kwa imani imara na uaminifu usiotetereka.—(Testimonies for the Church 7:245) [Pr 99.4; Maombi Aya ya 16]

Kuna nguvu inayotakiwa kupatikana kutoka kwa MUNGU. Yeye ana uwezo wa kusaidia. Anaweza kutoa neema na hekima ya mbinguni. Kama utaomba kwa imani, utapokea; lakini ni lazima ukeshe katika maombi. Kesha, omba, fanya kazi, inapaswa kuwa kauli mbiu yako . - (Testimonies for the Church 2:427) [Pr 99.5; Maombi Aya ya 17]

MUNGU ametutuma tufanye kazi katika shamba Lake la mizabibu. Ni wajibu wetu kufanya yote tuwezayo. "Panda mbegu yako asubuhi, wala usizuie mkono wako jioni; kwa maana haujui ni nini kitafanikiwa, ama hiki au kile." Tuna imani ndogo sana. Tunamwekea mipaka Mtakatifu wa Israeli. Tunapaswa kushukuru kwamba anashuka chini kabisa na kumtumia yeyote miongoni mwetu kama vyombo vyake. Kwa kila ombi la dhati na bidii lililowekwa kwa imani, jibu litarudishwa. Linaweza lisije vile vile tulivyotarajia; lakini jibu huja wakati ambao tunalihitaji zaidi (muafaka). Mkikaa ndani Yangu na maneno Yangu yakikaa ndani yenu, basi, ombeni chochote mtakacho nanyi mtapewa. The Review and Herald, Machi 23, 1897) [Pr 99.6; Maombi Aya ya 18]

Ikiwa tupata muda wa Kuomba, MUNGU Atapata muda wa Kujibu- Kila ombi la dhati kwa ajili ya kupata neema na nguvu litajibiwa Mwombe MUNGU akufanyie mambo ambayo wewe mwenyewe huwezi kujifanyia. Mwambie Yesu kila kitu. Zianike siri za moyo wako waziwazi mbele Zake; kwani jicho Lake huchunguza vichocho vya ndani kabisa ya moyo, Naye husoma mawazo yako kama kitabu kilicho wazi. Wakati umeomba vitu ambavyo ni muhimu kwa faida ya roho yako, amini kwamba unavipokea, na utakuwa navyo. Kubali zawadi Zake kwa moyo wako wote; kwani Yesu amekufa ili vitu vya thamani vya mbinguni

vipate kuwa vyako, na mwishowe upate makao na malaika wa mbinguni katika ufalme wa MUNGU. [Pr 100.1; Maombi Aya ya 19]

Ikiwa utapata sauti na wakati wa kuomba, MUNGU Naye atapata wakati na sauti ya kujibu. - (My Life Today, 16) [Pr 100.2; Maombi Aya ya 20]

Shangilia kabisa Kwamba MUNGU Ameyajibu Maombi Yako — Omba kwa imani. Na hakikisha unayaleta maisha yako kupatana na maombi yako, ili upate baraka ambazo unaziombea. Usiache imani yako idhoofike, kwani baraka utakazopokea zinatoshana na imani uliyonayo. "na iwe kwako kulingana na imani yako". Na mkiwa na imani, chochote mtakachoomba katika sala, mtapata." Mathayo 9:29; Mathayo 21:22. Omba, amini, furahi. Mwimbieni MUNGU sifa kwa sababu amejibu maombi yenu. Mwendeeni/mchukue kwa Neno Lake. "Yeye ni mwaminifu aliyeahidi." Waebrania 10:23. Hakuna hata ombi moja la dhati linalopotea. Njia iko wazi; mkondo unabubujika. Unabeba sifa Zake za uponyaji, ukimimina mkondo unaorejesha uzima/uhai mpya, afya na wokovu. — (Testimonies for the Church 7:274) [Pr 100.3; Maombi Aya ya 21]

Uzito wa Maombi yetu ni Ahadi kwamba MUNGU Atajibu— Wakati mtu anatoa ombi dhati, ari na bidii kwa MUNGU (Yesu Kristo Ndilo Jina pekee tulilopewa chini ya mbingu ambalo Kwalo tunaweza kuokolewa), kuna ahadi katika nguvu na bidii hiyo dhati kutoka kwa MUNGU kwamba Yuko njiani kujibu hilo ombi zaidi, na juu ya yote ambayo tunaweza kuomba au kufikiria (kupiga picha kichwani). Hatupaswi kuomba kwa Jina la Yesu tu, bali kwa uvuvio na moto* wa nguvu za Roho Mtakatifu. Hii inaelezea huwa inamaanisha nini kusema, "Roho Mwenyewe hutuombea kwa kuugua/maumivu kusikoweza kutamkika." Maombi lazima yatolewe kwa imani ya dhati. Kisha yatafikia kiti cha rehema. Endelea kuomba bila kusita. MUNGU hasemi, Omba mara moja, Nami nitakujibu. Neno Lake ni omba, na kuwa mwepesi, na mwenye utayari kuomba saa yo yote, ukiamini unavyo tayari vile vitu unavyoomba, nawe utavipokea; Mimi Nitakujibu wewe. - (Gospel Herald, Mei 28, 1902. [Pr 101.1; Maombi Aya ya 22]

("kindling" ni inaweza kuwaka kwa urahisi - kwa maneno mengine, ni kitu kidogo kama vijiti ambavyo vinaweza kutumika kuwasha moto. Kwa kupendeza, Roho Mtakatifu alishuka siku ya Pentekoste katika ndimi za moto. Kwa hivyo naona kwa hapa Roho Mtakatifu ni kama dutu inayoweza kuwaka ambayo huipa maombi yetu nguvu na hutumika kama mbebaji wa maombi yetu kwenye kiti cha enzi cha Mungu)

Masharti ya Kujibiwa kwa Maombi — Kuna mazingira fulani ambayo tunaweza kutarajia kwamba MUNGU atasikia na kuyajibu maombi yetu. La kwanza kati ya sababu hizi ni kwamba tunahisi hitaji letu la msaada kutoka Kwake. Ameahidi, "Nitamwaga maji juu yake yeye aliye na kiu, na mafuriko juu ya nchi kavu." Isaya 44: 3. Wale walio na njaa na kiu ya haki, ambao wanamfuata MUNGU, wanaweza

kuwa na uhakika kwamba watajazwa. Moyo lazima uwe wazi kwa ushawishi wa Roho, la sivyo baraka ya MUNGU haiwezi kupokelewa. [Pr 101.2; Maombi Aya ya 23]

Uhitaji wetu wenyewe ni hoja kubwa tosha na inasihi kwa umbuji zaidi kwa niaba yetu. Lakini Bwana anapaswa kutafutwa ili atufanyie mambo haya. "Ombeni, nanyi mtapewa." Yeye ambaye hakumhurumia hata Mwanae wa pekee, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote. Ikiwa amefanya hivyo, je, atakosaje kutukirimia mema yote pia? Mathayo 7:7; Warumi 8:32. [Pr 101.3; Maombi Aya ya 24]

Ikiwa tunazingatia uovu mioyoni mwetu, ikiwa tunaing'ang'ania dhambi yoyote inayojulikana, basi Bwana hatatusikia; lakini ombi la mtu mwenye majuto, kupondeka moyo na toba, daima linakubaliwa. Wakati makosa yote yanayojulikana yanasahihishwa, tunaweza kuamini kwamba MUNGU atajibu maombi yetu. Uzuri au sifa yetu wenyewe haitatufanya tufae kupata upendeleo au neema ya MUNGU; ni ustahiki wa Yesu ndio ambao unatuokoa, Ni damu Yake ndiyo ambayo itatutakasa; lakini tuna kazi ya kufanya ili kutimiza masharti ya kukubaliwa. [Pr 101.4; Maombi Aya ya 25]

Kipengele kingine cha ombi linaloshinda, lenye ustahimilivu na lenye ushawishi ni imani. "Yeye amwendeaye MUNGU lazima aamini kwamba Yeye Yupo, na kwamba Yeye huwapa thawabu wale wamtafutao." (Waebrania 11:6). Kristo anasema, "Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu." Marko 11:24. Je! Tunamwendea na kumchukua kutokana na Neno Lake? [Pr 101.1; Maombi Aya ya 26]

Hakikisho letu ni pana na halina kikomo, na Yeye ni waminifu ambaye ameahidi. Wakati hatupokei yale tuliyoomba, wakati tunaomba, bado tunapaswa kuamini kwamba Bwana anasikia na kwamba atajibu maombi yetu. Sisi ni wakosefu sana na tumepungukiwa na uelewa wetu ni finyu kiasi kwamba wakati mwingine tunaomba vitu ambavyo havingekuwa baraka kwetu, na Baba yetu wa mbinguni kwa upendo hujibu maombi yetu kwa kutupatia kile kitakachokuwa kwa faida yetu ya juu zaidi - kile ambacho sisi wenyewe tungetamani tukiwa na maono/utashi yaliyoangaziwa na MUNGU tunaweza kuona vitu vyote kama vilivyo. Wakati maombi yetu yanaonekana kutojibiwa, tunapaswa kushikilia ahadi; kwani wakati wa majibu hakika utakuja, na tutapokea baraka wakati ule ambapo tunaihitaji zaidi. Lakini kudai kwamba maombi yatajibiwa kila wakati kwa njia ile ile tuliyoomba na kwa kile kile ambacho tunatamani, ni dhana (au kiburi wakati mwingine). MUNGU ni Mwenye busara mno kukosea, na ni mwema sana kuwazuilia watakatifu Wake wanaoenenda kwa unyoofu kitu chochote kizuri. Basi usiwe na woga au hofu kumtumainia, ingawa huoni jibu la maombi yako papo hapo. Tegemea ahadi Yake ya hakika, "Ombeni, nanyi mtapewa." [Pr 101.2; Maombi Aya ya 27]

Ikiwa tutachukua ushauri na mashaka na hofu mioyoni mwetu, au kujaribu kutatua kila kitu ambacho hatuwezi kuona wazi, kabla ya kuwa na imani, mashaka yatazidi kuongezeka na kuwa na kina kirefu. Ikiwa tunamwendea MUNGU, tukijisikia tu hoi bina taabani na tegemezi, kama tulivyo kihalisia, na kwa imani ya kumtegemea Yeye na tukiwasilisha matakwa yetu Kwake Yeye ambaye maarifa Yake hayana mwisho, anayeona kila kitu katika uumbaji, na ambaye anasimamia na kuongoza kila kitu kwa mapenziYake na Neno Lake, Anaweza na atashughulikia kilio chetu, na atatuangazia nuru mioyoni mwetu. Kupitia maombi ya dhati tunaletwa katika ushirika na Nia na akili ya Yule Asiye na mwisho/kikomo. Labda hatuwezi kuwa na ushahidi unaoonekana wakati huo kwamba uso wa Mkombozi wetu umeinama juu yetu kwa huruma na upendo, lakini ndiyo ukweli wenyewe. Tunaweza tusihisi mguso Wake unaoonekana, lakini mkono Wake uko juu yetu kwa upendo na huruma kubwa. [Pr 102.3; Maombi Aya ya 28]

Tunapokuja kuomba rehema na baraka kutoka kwa MUNGU tunapaswa kuwa na roho ya upendo na msamaha mioyoni mwetu. Je! Tunawezaje kuomba, "Utusamehe deni zetu, kama sisi tunavyowasamehe wadeni wetu," na bado tunaendekeza roho ya kutosamehe? Mathayo 6:12. Ikiwa tunatarajia maombi yetu wenyewe yasikilizwe lazima tusamehe wengine kwa njia ile ile na kwa kiwango kile kile tunachotarajia kusamehewa. [Pr 103.1; Maombi Aya ya 29]

Kutochoka yaani uvumilivu katika maombi kumefanywa kuwa sharti la kupokea. Lazima tuombe kila wakati ikiwa tunataka kukua katika imani na uzoefu. Tunapaswa kuwa "na utayari saa yote katika maombi," "Tunapaswa kudumu katika sala, na kukesha vikitoshana na kushukuru kwetu." Warumi 12:12; Wakolosai 4: 2. Petro anawahimiza waumini kuwa "wenye kiasi, na wakeshe katika maombi." 1 Petro 4: 7. Paulo anaelekeza, "Katika kila jambo kwa maombi na dua pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na MUNGU." (Wafilipi 4:6). "Lakini ninyi, wapenzi," anasema Yuda, "mkiomba katika Roho Mtakatifu, jilindeni katika upendo wa MUNGU." Yuda 20, 21 .— (Steps to Christ, 95-97) [Pr 103.2; Maombi Aya ya 30]

Ikiwa tutampa Yeye utii wa nusu-nusu tu, ahadi Zake hazitatimizwa kwetu. - (The Ministry of Healing, 227) [Pr 103.3; Maombi Aya ya 31]

Lazima tuishi Maombi yetu ikiwa yataenda kujibiwa — Tunapaswa kuomba na kukesha katika maombi, ili kusiwe na mapishano katika maisha yetu. Hatupaswi kukosa kuwaonyesha wengine kwamba tunaelewa kuwa kukesha katika maombi kunamaanisha kuishi maombi yetu mbele za MUNGU, ili kwamba Yeye ayajibu. — (Selected Messages 1:116, 117) [Pr 103.4; Maombi Aya ya 32]

Maombi ni kazi bure ikiwa Maisha hayashabihiani na Maombi - "Mkikaa ndani Yangu, na maneno Yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo nanyi mtapewa." Unapoomba, wasilisha ahadi hii. Ni upendeleo kwetu kumwendea tukiwa na

ujasiri mtakatifu. Kwa unyofu tukimwomba nuru Yake iangaze juu yetu, Yeye Atatusikia na kutujibu. Lakini lazima tuishi kulingana na maombi yetu. Maombi ni kazi bure, yaani hayana faida yoyote ikiwa tunatembea kinyume nayo. Nimemwona baba ambaye, baada ya kusoma sehemu ya Maandiko na kuomba, mara nyingi kabla ya kuinuka baada tu ya kupiga magoti, analianza kuwafokea watoto wake. MUNGU angewezaje kweli kujibu ombi lile alilomba? Na ikiwa, baada ya kuwagombeza watoto wake, baba anasali, je, sala hiyo inawanufaisha watoto kweli? Hapana; labda ikiwa anatoa maombi ya kuungama kwa MUNGU. - (Child Guidance, 499) [Pr 103.5; Maombi Aya ya 33]

Tunapaswa kuambatanisha sifa ikiwa tunahitaji maombi yetu yajibiwe — Je! Shughuli na uzoefu wetu wote wa ibada unapaswa kujumuisha kuomba na kupata peke yake tu? Je! Tunapaswa kufikiria kila wakati matakwa/mahitaji yetu na si faida yoyote tunayopokea? Je! Sisi Tutakuwa wapokeaji wa rehema Zake na kamwe tusitoe shukrani zetu kwa MUNGU, na wala tusimsifu kwa yale aliyotutendea? Sisi wala Hatuombi sana, ila tuna ubahili wa kutoa shukrani. Ikiwa upendo mkarimu wa MUNGU ungeleta shukrani zaidi na kumsifu Yeye, basi tungelikuwa na nguvu zaidi katika maombi. Tungependana zaidi katika upendo wa MUNGU na kuzidi kumtukiza. Wewe ambaye unalalamika kwamba MUNGU hasikii maombi yako, badilisha zoezi la utaratibu wako wa sasa na uchanganye sifa katika maombi yako. Unapozingatia wema na rehema Zake utagundua kuwa Yeye atazingatia matakwa yako. [Pr 104.1; Maombi Aya ya 34]

Omba, omba kwa bidii na bila kukoma, lakini usisahau kusifu. - (Testimonies for the Church 5:317) [Pr 104.2; Maombi Aya ya 35]

Kukosa uaminifu katika Uwakili Kunaweza Kuwa Sababu ya Maombi Kutojibiwa — Kama Mtoaji wa kila baraka, MUNGU anadai sehemu fulani ya vitu vyote tulivyo navyo. Huu ni mpango Wake wa kuendeleza kuhubiri kwa injili. Na kwa kumrudishia MUNGU, tunakuwa tumeonyesha kuthamini kwetu na shukrani zetu kwa zawadi Zake. Lakini ikiwa tunamzuilia Yeye kilicho chake, tunawezaje basi kumtarajia Yeye atuamini na kutukabidhi vitu vya mbinguni? Inawezekana kwamba hii ndio siri ya sala isiyojibiwa. — (Christ's Object Lessons, 144) [Pr 104.3; Maombi Aya ya 36]

Twamtukana Mungu na kumdhalilisha kwa kuzidai Ahadi Zake bila Kukidhi Masharti — Kuna masharti ya kutimizwa kwa ahadi za MUNGU, na maombi hayawezi kuchukua mahali nafasi ya wajibu. "Ikiwa mnanipenda," Kristo anasema, "mtazishika amri Zangu." Azipokeaye amri Zangu na kuzishika, yeye ndiye anipendaye. Naye anipendaye Mimi atapendwa na Baba Yangu, Nami nitampenda na kujidhihirisha kwake." Yohana 14:15, 21. Wale ambao huleta maombi yao kwa MUNGU, wakidai ahadi Yake wakati hawafuati masharti yake, wanamtukana/wanamdhalilisha Yehova. Wao huleta Jina la Kristo kama mamlaka yao ya kutimiziwa ahadi, lakini hawafanyi mambo ambayo yangeonyesha imani katika Kristo na upendo wao Kwake. - (Christ Object

Lessons, 143) [Pr 104.4; Maombi Aya ya 37]

Ikiwa Masharti yametimizwa, Ahadi ya Maombi yanayojibiwa haizuiliki (haina mashaka) – Maombi na imani vimeunganishwa kwa karibu (ni pacha), na vinahitaji kuchunguzwa/kusomwa kwa pamoja. Katika ombi la imani kuna sayansi ya Bwana/mbingu; ni sayansi ambayo kila mtu ambaye anatamani kufanikisha kazi yake ya maisha lazima aelewe. Kristo anasema, "Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu." Marko 11:24. Anaweka wazi kwamba ombi letu lazima liwe kulingana na mapenzi ya MUNGU; lazima tuombe vitu ambavyo ameahidi, na chochote tunachopokea lazima kitumike katika kufanya mapenzi Yake. Masharti yakitimizwa, ahadi haizuiliki (hakuna maswali yanabakia). [Pr 105.1; Maombi Aya ya 38]

Kwa msamaha wa dhambi, kwa Roho Mtakatifu, kwa hulka na tabia kama ya Kristo, kwa hekima na nguvu ya kufanya kazi Yake, kwa zawadi yoyote ambayo Yeye ameahidi, tunaweza kuomba; kisha tunapaswa kuamini kwamba tunapokea, na kurudisha shukrani kwa MUNGU kwamba tumekwishapokea. [Pr 105.2; Maombi Aya ya 39]

Hatuhitaji kutafuta ushahidi wa nje wa baraka. Zawadi iko katika ahadi, na tunaweza kwenda kuendelea na kazi yetu tukiwa na uhakikisho kwamba kile ambacho MUNGU amekiahidi, Yeye Ana uwezo wa kukitekeleza, na kwamba zawadi, ambayo tayari tunayo, itadhihirika haswa wakati tutakapokuwa tunaihitaji zaidi. – (Education, 257, 258) [Pr 105.3; Maombi Aya ya 40]

Maombi yetu Sio Amri za kumwamrisha MUNGU– Tunajua kwamba Yeye hutusikia ikiwa tunaomba kulingana na mapenzi Yake. Maombi yetu hayapaswi kuchukua mfumo wa amri, bali mfumbo wa maombezi Kwake Yeye ili afanye mambo tunayotamani kutoka Kwake. (Testimonies for the Church 2:149) [Pr 105.4; Maombi Aya ya 41]

Maombi hayajibiwi Papo hapo mara zote – MUNGU ana mbingu iliyojaa baraka kwa wale watakaoshirikiana Naye. Wote wanaomtii wanaweza kudai kwa ujasiri utimizo wa ahadi Zake. Lakini lazima tuonyeshe kumtegemea kikamilifu bila na uaminifu thabiti usiokengeuka kwa MUNGU. Mara nyingi Yeye hucheleweshwa kutujibu ili kujaribu imani yetu au kujaribu unyofu wa matamania yetu. Baada ya kuomba kulingana na Neno Lake, tunapaswa kuamini ahadi Yake na kukazana bila kuchoka katika maombi yetu kwa kunuia ambako hakutakataliwa. – (Christ's Object Lessons, 145) [Pr 105.5; Maombi Aya ya 42]

Wakati wale wanaojua Ukweli wanapofanya mazoezi ya kujinyima yaliyoamriwa katika neno la MUNGU, ujumbe utaenda kwa nguvu. Bwana atasikia maombi yetu ya kuongoa roho. Watu wa MUNGU wataruhusu nuru yao iangaze, na wasioamini, wakiona matendo yao mema, watamtukuza Baba yetu wa mbinguni. - (Messages to Young People, 315) [Pr 106.1; Maombi Aya ya 43]

Kuchelewa kwa Kristo kwa siku mbili baada ya kusikia kwamba Lazaro alikuwa mgonjwa haukuwa upuuziaji au kukataa kwa upande Wake. Lilikuwa ni kusudi Lake kubaki pale alipokuwa mpaka kifo cha Lazaro kitokee, ili aweze kuwapa watu ushahidi wa Uungu Wake, sio kwa kumponya mtu anayekaribia kufa, bali kwa kumfufua mtu aliyezikwa tayari. [Pr 106.2; Maombi Aya ya 44]

Jambo hili linapaswa kuwa faraja kwetu. Wakati mwingine tunajaribiwa kufikiri kwamba ahadi, “Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtapata; bisheni, nanyi mtafunguliwa,” haitimizwi mpaka pale ambapo jibu linatolewa mara tu ombi linapowasilishwa. Ni upendeleo kwetu kuomba baraka maalum, na kuamini kwamba tutapewa. Lakini ikiwa baraka zilizoombwa hazitolewi mara moja, hatupaswi kufikiria kwamba maombi yetu hayasikilizwi. Hakika tutapokea, hata kama jibu litacheleweshwa kwa muda. Katika kutekeleza mpango wa ukombozi, Kristo anaona mengi katika ubinadamu ya kumvunja moyo. Lakini Yeye havunjiki moyo au kukata tamaa. Kwa rehema na upendo Anaendelea kutupatia fursa na upendeleo. Kwa hivyo tunapaswa kupumzika katika Bwana, na kumngojea Yeye kwa uvumilivu. Jibu la maombi yetu linaweza lisije haraka kama tunavyotamani, na inaweza kuwa sio kile kitu ambacho tuliomba rasmi ; lakini Yeye ambaye anajua ni kipi bora kupita vyote kwa ajili ya watoto Wake atatoa mema zaidi kuliko tulivyoomba, tusipopoteza imani (au kuwa makafiri) na kuvunjika moyo. —(The Youth’s Instructor, April 6, 1899) [Pr 106.3; Maombi Aya ya 45]

Sisi sote tunatamani majibu ya haraka na ya moja kwa moja kwa maombi yetu, na tunajaribiwa kuvunjika moyo wakati jibu linapocheleweshwa au likiwa katika fumbo ambalo hatukulitazamia. Lakini MUNGU ni Mwenye busara sana na mwema kujibu maombi yetu wakati ule ule na namna ile ile tunayotamani mara zote. Yeye Atatutendea zaidi na bora kwetu, kuliko kutimiza matamania yetu yote. Na kwa sababu tunaweza kuamini hekima na upendo Wake, hatupaswi kumuomba aridhie mapenzi yetu, lakini tunapaswa kutafuta kuingia safari ya kutimiza kusudi Lake. Matamania na shauku zetu zinapaswa kuzama katika mapenzi Yake. Uzoefu huu unaojaribu imani ni kwa faida yetu. Kwao inadhihirishwa kama imani yetu ni ya Kweli na ya dhati, na inayotegemea Neno la MUNGU peke yake, au inatokana na mazingira tu, na inakuwa sio ya kutegemewa na hubadilika-badilika tu. Imani huimarishwa kwa mazoezi. Lazima tuache uvumilivu utende kazi yake kamilifu, tukikumbuka kwamba kuna ahadi za thamani katika Maandiko kwa wale wanaomsabiri Bwana. - (The Ministry of Healing, 230, 231) [Pr 107.1; Maombi Aya ya 46]

Niliona kwamba watumishi wa MUNGU na kanisa walikuwa wanavunjika moyo kwa urahisi sana. Walipomuomba Baba yao wa mbinguni vitu ambavyo walidhani kuwa wanavihitaji, na hivi havikuja mara moja, imani yao iliyumba, ujasiri wao ukatoweka, na hisia za kunung'unika zikawajaa. Niliona, hili halikumpendeza MUNGU. [Pr 107.2; Maombi Aya ya 47]

Watakatifu wote wanaomwendea MUNGU kwa moyo wa kweli, kwa imani, na

kutuma maombi yao ya kweli Kwake, watajibiwa maombi yao. Imani yao haipaswi kuachilia ahadi za MUNGU ikiwa hawaoni au hawasikii majibu ya mara moja ya maombi yao. Usiogope kumtumaini MUNGU. Zitegemee ahadi zake za kweli: Ombeni, nanyi mtapokea.' MUNGU ni mwenye busara mno hakosei, na ni mwema sana kuwazuilia watakatifu wake kitu chochote kizuri wanao tembea katika unyoofu. Mtu hukosea, na ingawa maombi yake yanatumwa kutoka katika moyo mkweli, mara zote huwa haombi vitu ambavyo ni vyema kwake, au ambavyo vitamtukuza MUNGU. Wakati hili likiwa hivyo, Baba yetu mwenye busara na mwema anasikia maombi yetu, na atajibu, wakati fulani hujibu haraka; lakini Yeye hutupatia vitu ambavyo ni kwa faida yetu na utukufu wake mwenyewe. [Pr 107.3; Maombi Aya ya 48]

Ikiwa watoto wa MUNGU wangepokea kuona mpango Wake, wangepokea kuwa Yeye huwapa kile ambacho ni kwa faida yao. Ingawa hawawezi kupokea yale mambo waliyotarajia tu, au waliyoomba, bado maombi yao yalijibiwa Hakuna chochote cha kuumiza walichopewa, bali baraka waliyohitaji zaidi, badala ya kitu ambacho walikuwa wameomba, ambacho kisingekuwa kizuri kwao, bali kingewaumiza. [Pr 107.4; Maombi Aya ya 49]

Niliona kwamba ikiwa hatuhisi majibu ya haraka ya maombi yetu, tunapaswa kushikilia imani yetu, bila kuruhusu mashaka, kwani hayo yatatutenganisha na MUNGU. Imani yetu ikitetereka, hatutapokea chochote kutoka kwake. Imani yetu kwa MUNGU inapaswa kuwa imara; na wakati tunapoihitaji sana, baraka itatuangukia kama matone ya mvua. [Pr 108.1; Maombi Aya ya 50]

Wakati watumishi wa MUNGU wanapoomba kwaajili ya Roho Wake na baraka, wakati mwingine hivi huja papo hapo; lakini sio kila wakati basi huwa hivyo. Katika nyakati kama hizo, usizimie roho. Hebu imani yako ishikilie ahadi kwamba, itakuja. Acha tumaini lako liwe kamili kwa MUNGU, na mara nyingi baraka hiyo itakuja wakati unapoihitaji zaidi, na bila kutarajia utapokea msaada kutoka kwa MUNGU, wakati unazungumza ile Kweli kwa wale wasioamini, utazungumza kwa uwazi Neno, na kwa nguvu. [Pr 108.2; Maombi Aya ya 51]

Ilionyeshwa kwangu kama watoto wakiomba baraka ya wazazi wao wa kidunia wanaowapenda. Wanaomba kitu ambacho mzazi anajua kitawaumiza; mzazi huwapa vitu ambavyo vitakuwa vyema na vyenye afya kwao, mahali pa kile ambacho mtoto alitaka/alitamani. Niliona kwamba kila ombi ambalo hutolewa kwa imani kutoka katika moyo mwadilifu litasikika juu kwa MUNGU na kujibiwa, na yule aliyetuma ombi atapata baraka wakati anapoihitaji sana/zaidi, na mara nyingi majibu yatazidi matarajio yake. Hakuna sala ya mtakatifu wa kweli inayopotea ikiwa imetumwa kutoka katika moyo wa mnyofu kwa imani. -(Spiritual Gifts 4b, 7-9) [Pr 108.3; Maombi Aya ya 52]

Baada kutoa ombi, ikiwa jibu halitakuja mara moja, usichoke kusubiri na kuwa dhaifu. Mawazo yako yasimangemange kama wimbi la bahari. Ing'ang'anie ahadi, "Yeye ni mwaminifu ambaye Awaita, Naye Atatenda" Kama mjane aliyekuwa na

bidii isiyokatishwa tamaa, peleka kesi yako kwa Mungu, ukiwa thabiti katika kusudi lako. Je! Kitu hicho ni cha muhimu na chenye matokeo makubwa kwako? Hakika ni hivyo. Basi usitetereke, kwani imani yako inaweza kujaribiwa. Ikiwa kitu unachotamani ni cha thamani kubwa, basi kinastahili juhudi imara, na yenye bidii. Una ahadi; baso kesho na uombe. Uwe imara na maombi yako yatajibiwa; kwa maana si ni Mungu Ndiye ameahidi? kama itakugharimu kukipata basi utakipa thamani zaidi wakati kitakapopatikana. Unaambiwa waziwazi kwamba ikiwa utakuwa na shaka haupaswi kufikiria kwamba utapokea chochote kutoka kwa Bwana. Tahadhari imetolewa hapa usichoke, bali utulie kwa uthabiti kwenye ahadi za Bwana. Ukiomba, Yeye atakupa kwa ukarimu na wala hutakemewa.-(Testimonies for the Church 2:131) [Pr 108.4; Maombi Aya ya 53]

“Ombeni, nanyi mtapewa.” Uhakikisho ni mpana na hauna kikomo, na Yeye ni Mwaminifu ambaye ameahidi. Wakati mwingine tunashindwa katika imani kwa sababu Hekima isiyo na kikomo haiji kwa kufuata sera au mkataba wetu. Wakati kwa sababu yoyote ile hatupokei yale tunayoomba kwa wakati tunaoomba, bado tunapaswa kuamini kwamba Bwana anasikia, na kwamba atatupatia vitu ambavyo ni bora kwetu. Utukufu Wake Mwenyewe ni sababu tosha ya wakati mwingine kuzuia kile tunachoomba, na kisha kujibu maombi yetu kwa njia ambayo hatukutarajia. Lakini tunapaswa kuikumbatia ahadi; kwani wakati wa majibu utafika, na tutapokea baraka tunazohitaji zaidi. - (The Signs of the Times, Agosti 21, 1884) [Pr 109.1; Maombi Aya ya 54]

MUNGU Hatujibu Kama Tunavyotarajia mara zote, Bali Daima Kwa Manufaa Yetu — omba, basi; omba, nawe utapokea. Omba unyenyekevu, hekima, ujasiri, ongezeko la imani. Kwa kila ombi la dhati (nyofu) jibu litakuja. Linaweza lisije vile vile unavyotamani, au kwa wakati unalitafuta; lakini litakuja kwa njia na kwa wakati ambao utakidhi mahitaji yako kwa ubora zaidi. Maombi unayotoa katika upweke, ukiwa umechoka, katika mitihani ya maisha, MUNGU huyajibu, sio kila wakati kulingana na matarajio yako, lakini mara zote kwa faida yako. —(Messages to Young People, 250) [Pr 109.2; Maombi Aya ya 55]

Wakati ulipoomba katika shida au mateso yako kwaajili ya amani katika Kristo, wingu la giza lilionekana kutia weusi kwenye akili yako. Pumziko na amani havikuja kama ulivyotarajia. Wakati mwingine imani yako ilionekana kujaribiwa kupita kiasi. Ulipotazama nyuma katika maisha yako ya zamani, uliona huzuni na kukatishwa tamaa; ulipoangalia siku zijazo, yote yakawa yasiyo na uhakika kwako. Mkono wa Bwana ulikuongoza kwa namna ya kushangaza kwa kukuleta wewe msalabani na kukufundisha kwamba hakika MUNGU alikuwa mtoa thawabu kwa wale wanaomtafuta kwauadilifu. Wale wanaoomba kwa usahihi watapokea. Yule Anayetafuta kwa imani atapata. Uzoefu unaopatikana katika tanuru la majaribu na mateso ni wa thamani zaidi kuliko usumbufu wake wote na gharama ya maumivu yake. [Pr 109.3; Maombi Aya ya 56]

Maombi ambayo ulitoa katika upweke wako, katika kuchoka kwako na majaribu, MUNGU alijibu, sio kila wakati kulingana na matarajio yako, lakini kwa faida yako. Haukuwa na maoni wazi na sahihi kuhusiana na ndugu zako, wala haukujiona katika nuru sahihi. Lakini, kwa majaliwa/mwongozo wa MUNGU, Amekuwa kazini kujibu maombi uliyotoa katika taabu yako, kwa namna ya kukuokoa na kulitukuza Jina Lake Mwenyewe. Kwa kutotambua au ujinga wako uliomba vitu ambavyo havikuwa bora kwako. MUNGU alisikia maombi yako yenye unyoofu, lakini baraka uliyopewa ilikuwa kitu tofauti sana na matarajio yako. MUNGU amekusudia, katika mipango/uongozi Wake, kukuweka moja kwa moja katika uhusiano na kanisa Lake, ili ujasiri wako uwe kwa kiasi kidogo juu yako mwenyewe na uwe mkubwa zaidi katika wengine ambao Anawaongoza kuendeleza kazi Yake mbele. [Pr 110.1; Maombi Aya ya 57]

MUNGU husikia kila ombi la dhati-lenye unyofu wa moyo. - (Testimonies for the Church 3:415, 416) [Pr 110.2; Maombi Aya ya 58]

MUNGU Hujibu Maombi kwa Wakati Wake Aliouchagua- Katika maisha yake yote ya ndoa, Zakaria alikuwa ameombea apate mtoto wa kiume. Yeye na mkewe walikuwa wamezeeka sasa, na bado maombi yao yalikuwa hayajajibiwa; lakini hakunung'unika. MUNGU hakuwa amesahau. Alikuwa na wakati Wake uliowekwa wa kujibu ombi hili, na suala hilo ilipoonekana kutokuwa na matumaini, Zakaria alipokea jibu lake. - (SDA Bible Commentary, juz. 5, 1114) [Pr 110.3; Maombi Aya ya 59]

Kwa nini majibu kwa maombi yanaweza kuchelewa-MUNGU huwa hajibu mara zote maombi yetu pale tunapomwomba kwa mara ile ya kwanza; kwani akifanya hivi, tunaweza kuichukulia kirahisi kwamba tulikuwa na haki ya mibaraka na neema zote Alizotupatia. Badala ya kuchukua muda katika tukipekua mioyo yetu ili kuona ikiwa tumeendekeza uovu wowote, au dhambi yoyote tunayoifurahia, au kufanya mambo kizembe na kisha tukashindwa kutambua utegemezi wetu Kwake, na hitaji letu la msaada Wake. - (The Review and Herald, Juni 9, 1891) [Pr 110.4; Maombi Aya ya 60]

Kuna ahadi za thamani katika Maandiko kwa wale wanaomsubiri Bwana. Sisi sote tunatamani jibu la haraka kwa maombi yetu na tunajaribiwa kuvunjika moyo ikiwa ombi letu halijajibiwa mara moja. Sasa, uzoefu wangu umenifundisha kuwa hili ni kosa kubwa. Uchelewesho ni kwa faida yetu maalum. Tuna nafasi ya kuona ikiwa imani yetu ni ya Kweli na ya dhati au inaweza kuyumbayumba kama mawimbi ya bahari. Lazima tujifunge juu ya madhabahu kwa kamba kali za imani na upendo, na kuacha uvumilivu uwe na kazi yake kamilifu. Imani inaimarika kupitia mazoezi ya kila wakati. Kusubiri huku hakumaanishi kwamba kwa sababu tumeshamwomba Bwana uponyaji, basi sasa hakuna chochote tunachopaswa kukifanya. Badala yake, tunapaswa kutumia mbinu bora kabisa ambazo Bwana kwa wema Wake ametupatia katika mahitaji yetu. - (Counsils on Health, 380, 381)

[Pr 110.5; Maombi Aya ya 61]

Dumu kuomba, Hata ikiwa Jibu haliji— Wakati mwingine majibu ya maombi yetu huja mara moja; na wakati mwingine tunalazimika kungojea kwa uvumilivu na kuendelea kuomba kwa dhati na bidii vitu tunavyohitaji, kesi zetu zikiwakilishwa kwa mfano wa mwombezi wa mkate mwenye bidii isiyochoka, aliyeingia kwa ghafla nyumbani mwa mtu usiku. "Ni yupi kati yenu ambaye atakuwa na rafiki, na atamwendea usiku wa manane," nk. Somo hili lina maana zaidi ya vile tunavyoweza kufikiria. Tunapaswa kuendelea kuomba, hata ikiwa hatuyaoni majibu ya haraka kwa maombi yetu. Kwa hiyo, ombeni, nanyi mtapewa, tafuteni, nanyi mtapata, bisheni nanyi mtafunguliwa. Maana yeyote aombaye hupewa, atafutaye hupata na abishaye hufunguliwa. Luka 11: 9, 10. [Pr 111.1; Maombi Aya ya 62]

Tunahitaji neema, tunahitaji kuangaziwa na Bwana, ili kupitia kwa Roho Wake tuweze kujua jinsi ya kuomba yale mambo ambayo tunayahitaji. Hebu Bwana na ayaandike maombi yetu kwa ufanisi na kwa ukubali Wake, na kisha ayajibu.— (Counsels on Health, 380) [Pr 111.2; Maombi Aya ya 63]

Majibu Yanacheleweshwa ili kufunua Ubinafsi Wetu — Yeye aliyembariki mtu mwenye cheo wa Kapernaumu anataka kutubariki sisi pia. Lakini kama baba aliyeteseka, mara nyingi tunaongozwa kumtafuta Yesu kwa shauku ya kujipatia mema ya kidunia; na katika kutoa ombi letu tunaweka imani yetu katika upendo Wake. Mwokozi anatamani kutupa baraka kubwa kuliko tunavyoomba; Naye huchelewesha jibu la ombi letu ili atuonyeshe uovu ulio mioyoni mwetu wenyewe, na hitaji letu kubwa la neema Yake. Anatamani tuukane ubinafsi ambao unatuongoza kumtafuta Yeye. Tukiri kutojiweza kwetu na hitaji letu chungu, tunapaswa kujidondosha kikamilifu kabisa katika upendo Wake, tukimtegemea na kumwamini Yeye. [Pr 111.3; Maombi Aya ya 64]

Mtu huyu mwenye cheo alitaka kuona utimilifu wa maombi yake kabla ya kuamini; lakini ilimbidi akubali Neno la Yesu kwamba ombi lake lilisikilizwa na baraka zikatolewa. Sisi nasi tunapaswa kujifunza somo hili pia. Sio kwa sababu tunaona au kuhisi kwamba MUNGU anatusikia ndio tunapaswa kuamini. Tunapaswa kuziamini ahadi Zake. Tunapomjia kwa imani, kila ombi huingia moyoni mwa MUNGU. Tunapokuwa tumeomba baraka Yake, tunapaswa kuamini kwamba tumeipokea, na kumshukuru kwamba tumeipokea. Halafu tunapaswa kuendelea na majukumu yetu, tukiwa na hakika kwamba baraka itapatikana wakati tutapokuwa na uhitaji zaidi. Tutakapokuwa tumejifunza kufanya hivi, tutajua kwamba maombi yetu yanajibiwa. MUNGU atatutendea kwa kupita kipimo na ukarimu "sana", "kulingana na utajiri wa utukufu Wake," na "utendaji wa nguvu Zake kuu." Waefeso 3:20, 16; Waefeso 1:19.— (The Desire of Ages, 200) [Pr 112.1; Maombi Aya ya 65]

Maombi yanayoonekana kutojibiwa Yanaweza Kuwa Kati ya Baraka Zetu

Kubwa Zaidi — Katika kujali Kwake kwa upendo na masilahi yetu, mara nyingi Yeye ambaye anatuelewa sisi vizuri zaidi ya tunavyojielewa wenyewe hukataa kuturuhusu kujiridhisha wenyewe na ubinafsi na matamania ya ukuu. Yeye hatupi leseni kuyapita majukumu matakatifu ya nyumbani ambayo yanayoonekana kuwa hayavutii ila yapo karibu nasi. Mara nyingi majukumu haya yanatoa mafunzo muhimu sana katika kututayarisha kwa kazi ya juu zaidi. Mara nyingi mipango yetu inashindwa/inafeli ili mipango ya MUNGU kwetu ifanikiwe. [Pr 112.2; Maombi Aya ya 66]

Kamwe hatujaitwa kutoa kafara halisi kwa MUNGU. Kuna vitu vingi anavyotuomba tuvisalimishe Kwakei, lakini kwa kufanya hivyo tunatoa kile kinachotuzuia katika njia ya kwenda mbinguni. Hata tunapoombwa kusalimisha vitu ambavyo kwa vyenye ni vyema, tunaweza kuwa na uhakika kwamba MUNGU anafanya kazi kwa mema mengine za juu zaidi kwetu. Mara nyingi mipango yetu hufeli ili mipango ya Mungu ifanikiwe. [Pr 112.3; Maombi Aya ya 67]

Katika maisha ya baadaye mafumbo na siri ambazo hapa zimetukasirisha au kutupa usumbufu na kutukatisha tamaa zitawekwa wazi. Tutagundua kwamba maombi yetu yaliyoonekana kutokuwa na majibu na matumaini na yaliyotukatishwa tamaa, hayo yamekuwa miongoni mwa baraka zetu kubwa. [Pr 112.4; Maombi Aya ya 68]

Tunapaswa kuzingatia kila wajibu kama ni mtakatifu, hata uwe ni wa unyenyekevu au umasikini wa kiasi gani, kwa sababu ni sehemu ya huduma ya MUNGU. Maombi yetu ya kila siku yanapaswa kuwa, “Bwana, nisaidie kufanya bidii kwa kadiri navyoweza. Nifundishe jinsi ya kufanya kazi bora. Nipe nguvu na uchangamfu. Nisaidie kuleta katika huduma yangu huduma ya upendo wa Mwokozi.” (The Ministry of Healing, 473, 474) [Pr 112.5; Maombi Aya ya 69]

Wakati mwingine MUNGU Hatupi Tunachoombea Kwa sababu Ana Kitu Bora zaidi Kwetu — Tunapokuja Kwake tunapaswa kuomba ili tuweze kuingia na kutimiza kusudi Lake, na kwamba matamania yetu na masilahi yetu yazame/yapotee ndani Yake. Tunapaswa kutambua ukubali wetu kwa mapenzi Yake, sio kumuomba akubaliane na mapenzi yetu. Ni afadhali kwetu kwamba MUNGU huwa hajibu maombi yetu kila wakati pale ambapo tunaanza kutaka kitu, na kwa namna tunayotaka. Atatufanyia zaidi, na mazuri kuliko kutimiza matakwa yetu yote, kwani hekima yetu ni upumbavu. - (Testimonies for the Church 2:148) [Pr 113.1; Maombi Aya ya 70]

Lile Ombi la dhati litokalo moyoni kwa bidii na Imani lina ufanisi, usiochoka, wenye manufaa, na msaada wa hali ya juu.. MUNGU hajibu maombi yetu kila mara kama sisi tunavyotarajia, kwani tunaweza tusiombe kile kilicho bora zaidi kwetu; bali kwa upendo na hekima Yake isiyopimika, Yeye atatupatia vile vitu ambavyo ndivyo tunavyovihitaji sana. - (Testimonies for the Church 4:531) [Pr 113.2; Maombi Aya ya 71]

Tunapaswa Kushirikiana na MUNGU Katika Kujibu Maombi Yetu — Katika Neno la MUNGU zimewasilishwa pande mbili zinazoshindana ambazo zinaathiri na kudhibiti mashirika ya kibinadamu katika ulimwengu wetu. Mara kwa mara vyama hivi vinafanya kazi na kila mwanadamu. Wale ambao wako chini ya udhibiti wa MUNGU na ambao wanaongozwa na malaika wa mbinguni, wataweza kutambua hila za nguvu zisizoonekana za giza. Wale ambao wanataka kuwa sawa na wakala wa mbinguni wanapaswa kuwa wenye bidii sana kufanya mapenzi ya MUNGU. Yabidi wasimpe nafasi yoyote Shetani na malaika zake. [Pr 113.3; Maombi Aya ya 72]

Lakini tusipokuwa macho kila wakati, tutashindwa na adui. Ingawa ufunuo makini wa mapenzi ya MUNGU juu yetu umefunuliwa kwa wote, lakini ujuzi wa mapenzi Yake hauweki kando ulazima wa kutoa maombi ya dhati Kwake kwaajili ya msaada, na kwa bidii kutafuta kushirikiana naye katika kujibu maombi yaliyotolewa. Yeye hutimiza makusudi yake kupitia vyombo vya kibinadamu. - (SDA Bible Commentary 6: 1119) [Pr 113.4; Maombi Aya ya 73]

Sala bila kuutoa moyo kikamilifu haitaleta Majibu (maombi ya moyo nusu nusu)-MUNGU Atakuwa kila kitu kwetu kwa kadiri tunavyomruhusu Awe. Maombi yetu yenye unyonge, yasiyoutoa moyo kikamilifu hayatatuletea majibu kutoka mbinguni. Oh, tunahitaji kuweka usongo/bidii katika kuwasilisha ombi letu! Omba kwa imani, subiri kwa imani, pokea kwa imani, shangilia kwa matumaini, kwani kila mtu atafutaye hupata. Kuwa na bidii na unyofu katika jambo hilo. Mtafute MUNGU kwa moyo wote. Watu huweka moyo wote na bidii katika kila kitu wanachofanya kwenye vitu vya muda mfupi vipitavyo, hadi juhudi zao zitakapofanikiwa. Kwa bidii nzito jifunze stadi na shuguli ya kutafuta baraka nyingi ambazo MUNGU ameahidi, na kwa uvumilivu, kwa juhudi zenye bidii na kuazimia, wewe utakuwa na nuru Yake na Ukweli Wake na neema Yake nyingi. [Pr 114.1; Maombi Aya ya 74]

Kwa unyofu wa moyo, katika njaa ya kiroho, mlilie MUNGU. Pigana mieleka na mawakala wa mbinguni hadi upate ushindi. Weka moyo utu wako wote mikononi mwa Bwana, nafsi, mwili, na roho, na amua kwa kuvalia njuga kwa kuwa wakala mpendwa aliyejiweka wakfu, akiongozwa na mapenzi Yake, akidhibitiwa na akili Yake, na aliyejazwa na Roho Wake. [Pr 114.2; Maombi Aya ya 75]

Mwambie Yesu matakwa yako kwa unyofu wa roho yako. Hautakiwi kufanya mazungumzo marefu na, au kutoa hubiri kwa MUNGU (usimhubiri Mungu), lakini kwa moyo wa huzuni juu ya dhambi zako, sema, "Niokoe, Bwana, la sivyo nitaangamia." Kuna matumaini kwa roho kama hizo. Watatafuta, wataomba, watabisha, na watapata. Wakati Yesu ameondoa mzigo wa dhambi unaosagasaga roho, utapata baraka ya amani ya Kristo. —(Our High Calling, 131) [Pr 114.3; Maombi Aya ya 76]

Ombi la Msamaha Daima Hujibiwa Papo hapo — Katika visa vingine vya uponyaji, Yesu hakutoa baraka iliyotafutwa pale pale. Lakini katika kisa cha ukoma, ombi lilijibiwa punde mara tu baada ya wito wa kusihi uponyaji ulipotolewa. Tunapoomba baraka za kidunia, jibu la maombi yetu linaweza kucheleweshwa, au MUNGU anaweza kutupa kitu kingine zaidi ya kile tunachoomba, lakini si hivyo pale tunapoomba ukombozi kutoka dhambini. Ni mapenzi Yake kututakasa dhidi ya dhambi, na kutufanya watoto Wake, na kutuwezesha kuishi maisha matakatifu. "Kristo alijitoa Mwenyewe kwa ajili ya dhambi zetu ili apate kutuokoa katika ulimwengu huu mbaya wa sasa, kulingana na mapenzi ya MUNGU na Baba yetu. Wagalatia 1: 4. "Tukiomba chochote sawasawa na mapenzi Yake, Atusikia; na kama tukijua kwamba asikia, tuombacho chote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba." 1 Yohana 5:14, 15. "Lakini tukiziungama dhambi zetu, basi MUNGU ni Mwaminifu na wa Kweli, Naye atatusamehe dhambi zetu na kututakasa na uovu wote." 1 Yohana 1: 9— (The Desire of Ages, 266) [Pr 114.4; Maombi Aya ya 77]

Kristo Huwasilisha Maombi Yetu Mbele ya Baba kama Ombi Lake Mwenyewe— Mara tu mtoto wa MUNGU anapokaribia kuingia kwenye Kiti cha Rehema, yeye anakuwa mteja wa Wakili mkuu. Katika kutamka kwake kwa mara ya kwanza toba na kuomba msamaha Kristo anaunga mkono kesi yake na kuifanya iwe Yake Mwenyewe, akiwasilisha ombi mbele ya Baba Yake kama ombi Lake Mwenyewe. - (Testimonies for the Church 6:364) [Pr 115.1; Maombi Aya ya 78]

Omba Kumshukuru na Kumsifu MUNGU kwa ajili ya Maombi Yaliyojibiwa—Katika sura ya pili ya 1 Samweli imeandikwa sala ya mwanamke aliyejitoa bila kuchoka, na ambaye alimtumikia na kumtukiza MUNGU. Aliomba: "Moyo wangu wamshangilia BWANA, Pembe yangu imetukuka katika BWANA, Kinywa changu kimepanuka juu ya adui zangu; Kwa kuwa naufurahia wokovu wako". Hakuna mtakatifu kama Bwana, kwa kuwa hakuna mwingine isipokuwa Yeye, wala hakuna mwamba kama MUNGU wetu." Sadaka ya Shukrani ya Hana kwa ajili ya jibu la maombi yake ni somo kwa wale ambao leo wanapokea majibu ya maombi yao. Je! Sisi tunapuuzia kurudisha sifa na shukrani kwa MUNGU kwa fadhili Zake za upendo? [Pr 115.2; Maombi Aya ya 79]

Daudi anatangaza, "Nampenda Bwana, kwa sababu amesikia sauti yangu na dua zangu. Kwa sababu amenitegea sikio lake, kwa hivyo nitamwita maadamu ninaishi." Wema wa MUNGU katika kusikia na kujibu maombi hutuweka chini ya jukumu zito la kuonyesha shukrani zetu kwa neema tulizopewa (kwa mdomo na matendo). Tunapaswa kumsifu MUNGU zaidi kuliko tunavyofanya sasa. Baraka zilizopokelewa katika jibu la maombi zinapaswa kutambuliwa mara moja kwa ushuhuda wa mdomo na katika maisha. Kumbukumbu zake zinapaswa kuwekwa katika shajara yetu, ili tunapokishika kitabu mkononi, tuweze kukumbuka wema wa Bwana, na kulisifu Jina Lake takatifu. - (The Review and Herald, Mei 7, 1908)

SURA YA 12

MAOMBI NA UAMSHO

Uamsho Utakuja Tu Kama Jibu Maombi — Uamsho wa utauwa wa Kweli miongoni mwetu ndio hitaji kubwa na la dharura kuliko mahitaji yetu yote. Kuutafuta uamsho huu inapaswa kuwa kazi yetu ya kwanza. Lazima ziwepo juhudi za dhati kujitwalia baraka ya Bwana kwetu, sio kwa sababu MUNGU Hayuko tayari kutumwagia baraka Yake, lakini kwa sababu sisi hatujajiandaa kuipokea. Baba yetu wa Mbinguni Yuko tayari kuwapatia Roho Wake Mtakatifu wale wanaomwomba, kuliko ambavyo wazazi wa hapa duniani walivyo tayari kutoa zawadi nzuri kwa watoto wao. Lakini ni kazi yetu, kwa kukiri, kujidhili, kutubu, na kutoa maombi ya dhati na biii, kutimiza masharti ambayo kwayo MUNGU ameahidi kutupa baraka Yake. Uamsho unapaswa kutarajiwa tu katika jibu la maombi.—(Selected Messages 1:121) [Pr 116.1; Maombi Aya ya 1]

Leo kuna haja ya uamsho wa dini ya Kweli ya moyoni kama ilivyokuwa kwa Israeli wa zamani. Kama wao, tunahitaji kuzaa matunda yanayofaa kwa toba, - kuondoa dhambi zetu, kusafisha hekalu lililochafuliwa la moyo ili Yesu aweze kutawala ndani. Kuna haja ya maombi - maombi ya dhati, ya bidii na ya kudumu. Mwokozi wetu ameacha ahadi za thamani kwa mwombaji atubuye kweli. Huyo hatautafuta uso Wake bure. Yeye pia kwa mfano Wake Mwenyewe ametufundisha umuhimu wa maombi. Yeye Mwenyewe, Mfalme wa Mbingu, Mara nyingi alitumia usiku kucha katika ushirika na Baba Yake. Ikiwa Mkombozi

wa ulimwengu hakujiona kuwa Yeye ni safi sana, Mwenye busara sana, au mtakatifu sana kutafuta msaada kutoka kwa MUNGU, hakika wanadamu dhaifu, wenye makosa wana kila hitaji la msaada huo wa Bwana. Kwa toba na imani, kila Mkristo wa Kweli atakuwa akitafuta daima “Kiti cha Neema, ili apate rehema, na kupata neema ya kusaidia wakati wa shida” (The Signs of the Times, January 26, 1882) [Pr 116.2; Maombi Aya ya 2]

Maombi Hutuleta katika ushirika na MUNGU - Ikiwa tunamwendea MUNGU, tukijisikia hoi, wasiojiweza na tegemezi, kama vile tulivyo kihalisia, na kwa imani ya unyenyekevu na tumaini tukiwasilisha matakwa yetu Kwake Yeye ambaye maarifa Yake hayana kikomo, Yule anayeona kila kitu katika uumbaji, na ambaye anatawala na kuongoza kila kitu kwa mapenzi na Neno Lake, Anaweza na atashughulikia kilio chetu, na ataangazia nuru mioyoni mwetu. Kupitia maombi ya dhati tunaletwa katika mwuunganiko wa ile akili ya Yule Asiye na mwisho. Pengine tunaweza tusiwe na ushahidi unaoonekana kwa namna ya ajabu na wazi wakati ule ambao uso wa Mkombozi wetu umeinama juu yetu kwa huruma na upendo, lakini huo ndio ukweli wenyewe. Tunaweza tusihisi mguso Wake kwa kuonekana uso kwa uso, yaani dhahiri lakini mkono Wake u juu yetu kwa upendo na huruma yenye sikitiko.—(Steps to Christ, 97) [Pr 117.1; Maombi Aya ya 3]

Maombi yetu hupanda mbinguni kama umande wenye unyevunyevu wa damu ya Kristo itakasayo—Huduma za kidini, kiroho, sala, sifa, kukiri dhambi kwa toba, hupanda juu kutoka kwa waumini wa kweli kama uvumba kwenda Patakatifu pa mbinguni, lakini kwa kupita katika njia ovu na fisadi za ubinadamu, hunajisiwa sana kiasi kwamba visipotakaswa kwa damu, kamwe haviwezi kuwa vya thamani kwa Mungu. Hukwea juu vikiwa na waa na madoa hivyo pasipo Mwombezi, aliye Mkono wa Kuume wa Mungu ili kuwasilisha na kutakasa vyote kwa Haki Yake, hayakubaliki kwa Mungu. Uvumba wote kutoka madhabahu za kidunia, lazima uwe na umande wa matone ya utakaso wa damu ya Kristo. Mbele Zake Baba. Anashikilia chetezo cha haki na sifa Zake Mwenyewe, ambamo ndani yake hakuna uchafu wa rushwa au ufisadi wa kidunia. Yeye Hukusanya maombi sifa na maungamo ya watu Wake ndani ya chetezo hiki na pamoja nayo huweka Haki Yake isiyo na doa. Ukiwa na harufu ya manukato ya sifa za upatanishi wa Kristo, uvumba huu huja na mbele za Mungu moja kwa moja na kwa ukamilifu tayari kwa kukubalika kabisa. Kisha, majibu yenye Neema hurudishwa. - (Selected Messages 1:344) [Pr 117.2; Maombi Aya ya 4]

Katika Maombi Twahisi Uwepo wa Yesu — Iwapo tutamweka Bwana mbele yetu daima, tukaruhusu mioyo yetu kwenda kumshukuru na kumsifu, tutafanywa upyakatika maisha yetu ya kiroho/kidini. Maombi yetu yatakuwa katika mfumo wa mazungumzo na MUNGU kama ambavyo tungezungumza na rafiki. Atazungumza nasi kuhusu mafumbo na siri Zake. Hisia nzuri za shangwe ya uwepo wa Yesu zitatuja mara kwa mara.—(Christ’s Object Lessons, 129) [Pr 118.1; Maombi Aya ya 5]

Roho Mtakatifu alikuja wakati wa Pentekoste Kama Jibu La Maombi – Roho alikuja juu ya wanafunzi wanaosubiri, wanaosali kwa utimilifu uliofikia kila moyo. Yule asiye na mwisho alijifunua katika uongozi kwa kanisa Lake. Ilikuwa kana kwamba kwa miaka mingi ushawishi huu ulikuwa umezuiliwa, na sasa mbingu ilifurahi kumwaga juu ya kanisa utajiri wa neema ya Roho. Na, chini ya ushawishi wa Roho, maneno ya toba na kukiri yalichanganywa na nyimbo za kumsifu Mungu kwa ajili ya dhambi zilizosamehewa. Maneno ya shukrani na ya unabii yalisikika. Mbingu zote ziliinama chini kutazama na kuabudu hekima ya Upendo usiolinganishwa, usioelezeka/usioeleweka na binadamu. Walipotelea katika mshangao, nao mitume wakasema, "Hapa pana upendo." Walishika na kuilewa zawadi waliyopewa. Na nini kilifuata basi? Upanga wa Roho, ukiwa umenolewa na nguvu na kusafishwa na umeme wa mbinguni, nao ulikatakata hali ya kutokuamini. Maelfu wakaongolewa siku ile.—(The Acts of the Apostles, 38) [Pr 118.2; Maombi Aya ya 6]

Tunapaswa kuomba kwa ajili ya Roho Mtakatifu kama walivyofanya Wanafunzi katika Pentekoste – Moyo lazima ukungutwe kila punje ya unajisi na kusafishwa kwa ajili ya kukaa kwa Roho. Ilikuwa kwa kuungama na kuacha dhambi, kwa kuomba kwa dhati na bidii na kujitoa wakfu kikamilifu wenyewe kwa MUNGU, ndivyo wanafunzi wa awali walivyojiandaa kwa ajili ya kumwagiwa kwa Roho Mtakatifu Siku ya Pentekoste. Kazi hiyo hiyo, lakini kwa kiwango kikubwa zaidi, lazima ifanyike sasa.... [Pr 118.3; Maombi Aya ya 7]

Pasipo kusonga mbele katika kielelezo cha fadhila za Kikristo kila siku, hatutaweza kutambua udhihirisho wa Roho Mtakatifu katika mvua ya masika. Inaweza kuwa ikianguka kwenye mioyo ya wengine kila mahali kutuzunguka, lakini sisi hatutatambua au kupokea.... [Pr 119.1; Maombi Aya ya 8]

Neema ya Mungu inahitajika mwanzoni, neema ya Bwana inahitajika katika kila hatua ya mafanikio, na neema ya Mungu pekee ndiyo inaweza kumaliza kazi hiyo. Hakuna nafasi kwetu sisi kubweteka na mielekeo ya kizembezembe. Kamwe tusingahau maonyo ya Kristo, "Kesha katika maombi," "daima.....kesha na uombe" Kuungana na wakala wa kimbangu kila nukta ni muhimu kwa maendeleo yetu. Yawezekana tuliwahi kupata kipimo fulani cha Roho wa MUNGU huko nyuma, lakini kwa maombi na imani tunapaswa kuendelea kuomba ili tuwe na Roho zaidi. —(Testimonies to Ministers and Gospel Workers, 507, 508) [Pr 119.2; Maombi Aya ya 9]

Tunapaswa kuomba kwa bidii kwa ajili ya kushuka kwa Roho Mtakatifu kama wanafunzi walivyoomba siku ya Pentekoste. Ikiwa walimhitaji wakati huo, basi sisi tunamhitaji zaidi leo. [Pr 119.3; Maombi Aya ya 10]

Bila Roho na nguvu ya MUNGU, kujitahidi kwetu kuwasilisha Ukweli itakuwa ni kazi bure tu.—((Australasian) Union Conference Record, April 1, 1898) [Pr 119.4;

Maombi Aya ya 11]

Dai Ahadi ya Roho kwa Imani — Ni kwa wale tu ambao humngojea MUNGU kwa unyenyekevu, wale ambao hutazama Uongozi na neema Yake, ndio hupewa huyo Roho. Nguvu ya MUNGU inasubiri takwa lao na mapokezi. Baraka hii iliyoahidiwa, na kudaiwa kwa imani, huleta baraka zingine zote kwenye mlolongo au treni yake. Inatolewa kulingana na utajiri wa rehema za Kristo, na Yuko tayari kuipatia kila nafsi kulingana na uwezo wa kupokea kwake. —(The Desire of Ages, 672) [Pr 119.5; Maombi Aya ya 12]

Ombea Mvua ya masika-Lazima tuombe ili MUNGU afungue chemchemi ya maji ya uzima. Na lazima sisi wenyewe tupokee maji ya uzima. Hebu sisi, kwa mioyo mikunjufu na uliopondeka, tuombe kwa bidii ili sasa, wakati wa mvua ya masika, mvua za neema ziweze kutuangukia. Katika kila mkutano tunaohudhuria sala zetu zinapaswa kupanda juu, ili wakati kamahuu MUNGU atoe joto na unyevunyevu kwenye roho zetu. Tunapomtafuta MUNGU kwa ajili ya Roho Mtakatifu, atafanya kazi ndani yetu kuwa wapole, unyenyekevu wa nia naakili, kumtegemea MUNGU kwa ajili ya kupata mvua ya masika. Ikiwa tunaombea baraka kwa imani, tutapokea kama vile MUNGU alivyoahidi. —(Testimonies to Ministers and Gospel Workers, 508) [Pr 119.6; Maombi Aya ya 13]

Uwe na ari katika Maombi na katika Uwezo wa Roho Mtakatifu — Tunachohitaji ni ushawishi wa Roho Mtakatifu wa MUNGU uhuishao. "Si kwa nguvu, wala si kwa uwezo, bali kwa Roho Wangu, asema Bwana wa majeshi." Omba bila kukoma, na kesho ukifanya kazi kulingana na maombi yako. Unapoomba, amini, mtumaini MUNGU. Ni wakati wa mvua ya masika, wakati ambao Bwana atatoa kwa kiasi kikubwa Roho Wake. Dumu katika maombi, na kesho katika Roho- (Testimonies to Ministers and Gospel Workers, 512) [Pr 120.1; Maombi Aya ya 14]

Shetani Huogopa watu wa MUNGU wanaoomba kwa ajili ya Roho mtakatifu-Hakuna kitu ambacho humogofya Shetani kama habari kuwa watu wa MUNGU watafungua njia kwa kuondoa kila kikwazo, ili Bwana aweze kumwaga Roho Wake juu ya kanisa lenye uchovu na kutaniko ambalo halijafanya toba. Ikiwa Shetani angelikuwa na njia yake, hakungekuwa na uamsho mwingine, mkubwa au mdogo, hadi mwisho wa wakati. Lakini sisi si wajinga katika kutambua hila zake. Inawezekana kuzipinga nguvu zake. Pale njia ipoandaliwa kwa ajili ya Roho wa MUNGU, baraka itakuja. Shetani hawezi kuzuia mvua ya baraka zisishuke juu ya watu wa MUNGU kama vile asivyoweza kufunga madirisha ya mbinguni ili mvua isiweze kufikia watu duniani. Watu waovu na mapepo/mashetani hawawezi kuzuia kazi ya MUNGU, ua kufungia uwepo Wake kwenye mikusanyiko ya Watu Wake, Ikiwa kwa mioyo iliyotiishwa, yenye toba na kupondeka, watakiri na kuachana na dhambi zao, na kudai ahadi Zake kwa Imani. —(Selected Messages 1:124) [Pr 120.2; Maombi Aya ya 15]

Roho Huandamana na Kila Ombi la Dhati — Dini inayotoka kwa MUNGU ndiyo

dini pekee itakayoongoza kumuelekea MUNGU. Ili kumtumikia Yeye sawasawa, lazima tuzaliwe na Roho Mtakatifu. Hii itasafisha moyo na kufanya upya akili, ikitupatia uwezo mpya wa kumjua na kumpenda MUNGU. Itatupa utii wa hiari kwa matakwa Yake yote. Hii ndio ibada ya Kweli. Ni tunda la utendaji wa Roho Mtakatifu. Kwa Roho kila sala ya dhati inaandikwa na kupewa ukubali Wake, na sala kama hiyo inakubalika kwa MUNGU. Mahali popote ambapo roho inamfuata MUNGU, hapo utendaji wa Roho unadhihirika, na MUNGU atajifunua kwa nafsi hiyo. Kwa maana Yeye Bwana anawatafuta wale wamwabuduo namna hii. Yeye anangojea kuwapokea, na kuwafanya wana na binti Zake. —(The Desire of Ages, 189) [Pr 120.3; Maombi Aya ya 16]

Maombi bila Shughuli iliyo dhati na ya Bidii kwa ajili ya watu Wengine husababisha kutumbukia katika mapokeo— MUNGU hamaainishi kwamba yeyote miongoni mwetu lazima awe mtawa aliyejitenga na watu au asiyejitenga na watu (monk/hermit) na kwamba tuukimbie ulimwengu na kujitoa masaa yote kwa ibada tu. Maisha lazima yawe kama maisha ya Kristo, katikati ya mlima na umati (akisali mlimani na akihudumu kwenye umati). Yule ambaye hafanyi chochote isipokuwa kuomba tu, ataacha kuomba hivi karibuni, au sala zake zitakuwa ni taratibu za mapokeo ya kila siku (desturi). Wakati watu wanapojiondoa katika maisha yao na jamii, mbali na uwanja wao wa wajibu wa Kikristo na kubeba msalaba; wanapoacha kufanya kazi kwa bidii kwa Bwana, ambaye alifanya kazi kwa bidii kwa ajili yao, wanapoteza mwelekeo na msingi wa maombi, na wanakosa motisha wa kujitoa wakfu kwaajili ya ibada. Maombi yao huwa yanahusu wao wenyewe na hivyo ya ubinafsi. Hawawezi kuomba kwa kuzingatia matakwa ya wanadamu au kuhusiana na kujengwa kwa ufalme wa Kristo, wakiugua kwaajili ya kupewa nguvu ya kufanya kazi.—(Steps to Christ, 101) [Pr 121.1; Maombi Aya ya 17]

Maendeleo ya Kiroho Hutegemea Maombi — Lazima tudumu katika maombi ikiwa tunahitaji kupiga hatua katika maisha ya Kiungu/mbingu. Wakati ujumbe wa ile Kweli ulipotangazwa kwa mara ya kwanza, ni kiasi gani tuliomba. Ni mara ngapi sauti ya maombezi ilisikika chumbani, ghalani, kwenye shamba la matunda, au vijisitu. Mara kwa mara tulitumia masaa kwa maombi ya dhati, wawili au watatu pamoja wakadai ahadi; mara nyingi sauti ya kulia ilisikika na kisha sauti ya shukrani na wimbo wa sifa. Sasa siku ile ya MUNGU iko karibu kuliko wakati tulipoanza kuamini, na tunapaswa kuwa na unyofu, shauku, na bidii ya kudumu zaidi kuliko siku zile za mwanzo. Hatari tulizo nazo sasa ni kubwa kuliko hapo awali.— (Testimonies for the Church 5:161, 162) [Pr 121.2; Maombi Aya ya 18]

SURA YA 13

WANAUME NA WANAWAKE WA MAOMBI

Henoko

Maombi yalikuwa Pumzi ya Nafsi Yake — kwa kuwasiliana na MUNGU, Henoka alizidi kuakisi sura ya Mungu. Uso wake ulikuwa uking'aa na nuru takatifu, hata ile nuru inayoangaza usoni mwa Yesu. Alipokuwa akitoka kwenye mawasiliano/mazungumzo haya na Bwana, hata wale wasiompanda Mungu (makafiri) walitazama kwa mshangao mkubwa mvuto (muhuri) wa mbinguni juu ya uso wake. [Pr 122.1; Maombi Aya ya 1]

Imani yake ilizidi kuimarika, upendo wake ukawa wenye shauku kali zaidi (enthusiasm), ukidumu kwa karne nyingi. Kwake maombi yalikuwa kama pumzi ya roho. Aliishi katika angahewa la mbinguni. - (Gospel Workers, 52) [Pr 122.2; Maombi Aya ya 2]

Akifadhaishwa na uovu uliokithiri wa wale wasiomcha MUNGU, na akiogopa kwamba kukosa uadilifu kwao kungeweza kupunguza kicho chake kwa MUNGU, Henoka aliepuka kushirikiana nao mara kwa mara, na alitumia muda mwingi akiwa amejitenga peke yake, akajitoa wakfu kwa tafakari na sala. Hivyo ndivyo alivyojihudhurisha mbele za Bwana, akitafuta maarifa wazi ya mapenzi Yake, kwa makusudi ya kuyatimiza. Kwake maombi yalikuwa kama pumzi ya roho; aliishi katika angahewa ya mbinguni. - (Patriarchs and Prophets, 85) [Pr 122.3; Maombi Aya ya 3]

Henoka Alitembea Na MUNGU Kupitia Maombi — Natamani ningeweza kumhimiza/kumshawishi kila mtendakazi katika kazi ya MUNGU hitaji kuu la sala ya kudumu na ya bidii. Hawawezi kupiga magoti daima, lakini wanaweza kuendelea kuinua mioyo yao kwa MUNGU. Hii ndio njia ambayo Henoka alitembea na MUNGU. - (The Review and Herald, Novemba 10, 1885) [Pr 123.1; Maombi Aya ya 4]

Wakati tunafanya kazi zetu za kila siku, tunapaswa kuinua mioyo yetu mbinguni kwa ajili ya maombi. Maombi haya ya kimyakimya, hupanda kama uvumba mbele ya kiti cha neema; na adui hupatwa na mshtuko wa fadhaa.

Mkristo ambaye moyo wake umekaa kwa MUNGU hawezi kutindikiwa. Hakuna sanaa za uovu au giza ambazo zinaweza kuharibu amani yake. Ahadi zote za Neno la MUNGU, nguvu zote za neema ya Bwana, rasilimali zote za Yehova, zimeahidiwa kama uhakikisho wa ukombozi Wake. Ilikuwa kwa jinsi hiyo ndiyo Henoka alivyotembea na MUNGU. Na MUNGU alikuwa pamoja naye, msaada ulio tele wakati wa mateso au mahitaji. - (Messages to Young People, 249) [Pr 123.2; Maombi Aya ya 5]

Watu Walimtafuta Henoka kwa ajili ya Maombi — Henoka alikua mhubiri wa haki, akiwajulisha watu kile ambacho MUNGU alikuwa amemfunulia. Wale waliomcha Bwana walimtafuta mtu huyu mtakatifu, ili ashiriki nao maagizo yake na sala zake. - (Patriarchs and Prophets, 86) [Pr 123.3; Maombi Aya ya 6]

Kadiri kazi ya Henoka ilivyozidi kuwa kubwa, ndivyo Maombi yake yalivyokuwaya dhati na bidii zaidi — Katika maisha ya kazi ya bidii, Henoka alidumisha uhusiano wake na MUNGU. Kadiri kazi yake ilivyokuwa kubwa na kupata msukumo zaidi, ndivyo maombi yake yalikuwa ya kudumu na ya bidii zaidi. Aliendelea kujitenga mwenyewe, katika vipindi fulani, mbali na jamii yote. Baada ya kukaa kwa muda kati ya watu, akitenda kazi ili kuwanufaisha kwa kuwafundisha na kutoa mfano, alijitenga, kutumia msimu katika upweke, akiwa na njaa na kiu ya maarifa ya Bwana ambayo MUNGU peke yake Ndiye anayeweza kuyatoa. - (Patriarchs and Prophets, 86, 87) [Pr 123.4; Maombi Aya ya 7]

Abrahamu

Maombi ya kila siku yanapaswa kupaa kwa MUNGU kama ubani unaonukia— Maisha ya Ibrahimu, rafiki wa MUNGU, yalikuwa maisha ya maombi. Kila mahali alipopiga hema lake, karibu naye ilijengwa madhabahu, ambayo juu yake ilitolewa dhabihu ya asubuhi na ya jioni. Wakati hema lake lilipoondolewa, madhabahu ilibaki. Na Mkanaani aliyekuwa akirandaranda au akihamahama huko na kule, alipofika kwenye madhabahu hiyo, alijua ni nani aliyekuwepo hapo. Naye huyu mkanani alipopiga hema lake aliikarabati ile madhabahu na kumwabudu MUNGU Aliye hai. [Pr 123.5; Maombi Aya ya 8]

Kwa hivyo nyumba za Wakristo zinapaswa kuwa taa ulimwenguni. Kutoka kwao, asubuhi na jioni, sala inapaswa kupanda juu kwa MUNGU kama uvumba unaonukia. Na kama umande wa asubuhi, rehema Zake na baraka zitashuka juu ya waombaji. [Pr 124.1; Maombi Aya ya 9]

Akina baba na akina mama, kila asubuhi na jioni wakusanye watoto wako karibu na wewe, na kwa dua ya unyenyekevu inua moyo kwa MUNGU kwa ajili ya msaada. Wapendwa wako wanaanikwa kwenye majaribu. Kero za kila siku zinasonga njia ya vijana na wazee. Wale ambao wataishi maisha ya uvumilivu, ya upendo, na uchangamfu lazima waombe. Ni kwa kupokea msaada wa kila wakati

kutoka kwa MUNGU ndipo tunaweza kupata ushindi juu ya nafsi yetu. [Pr 124.2; Maombi Aya ya 10]

Kila asubuhi jiwekeni wakfu kwa MUNGU na watoto wenu kwa ajili ya siku hiyo. Msifanye mahesabu ya miezi au miaka; hiyo sio yenu. Umepewa siku moja fupi. kama vile ndio siku yako ya mwisho duniani, fanya kazi kwa Bwana masaa hayo. Weka mipango yako yote mbele za MUNGU, ili ifanyike au ihahirishwe, kama vile maagizo Yake Mungu yatakavyoelekeza. Kubali mipango Yake badala mipango yako mwenyewe, hata kama kuikubali mipango Yake, kutakuhitaji wewe kuiacha miradi unayoipenda. ndipo maisha yako yatatengenezwa/yatafinyangwa zaidi na zaidi katika mfano wa Kiungu/mbingu; "Na amani ya MUNGU, ipitayo akili zote, italinda mioyo yenu na akili zenu kupitia Kristo Yesu." Wafilipi 4: 7 .— Testimonies for the Church (7:44) [Pr 124.3; Maombi Aya ya 11]

Ibrahimu aliomba kwa Imani Licha ya mazingira yenye changamoto – Ibrahimu hakuweza kuelezea mwongozo au majaliwa ya Mungu; alikuwa hajajua matokeo yatakuwaje; lakini alishikilia ile ahadi, "nitakubariki, na kulitukuza jina lako; nawe utakuwa baraka." Kwa maombi ya dhati alifikiria jinsi ya kuhifadhi maisha ya watu wake na mifugo yake, lakini hakuruhusu mazingira yale yatikisike imani yake katika Neno la MUNGU. - (Conflict and Courage, 45) [Pr 124.4; Maombi Aya ya 12]

Ibrahimu alimwomba MUNGU kwa Ujasiri wa Mtoto Akimsihi Baba Yake - Wajumbe wawili wa mbinguni waliondoka, wakimwacha Ibrahimu peke yake na Yeye ambaye sasa alijua kuwa ni Mwana wa MUNGU. Na yule mtu wa imani alisihi yaani alifanya maombezi kwa wakaaji wa Sodoma. Siku za awali alikuwa amewaokoa kwa upanga wake, na sasa alijitahidi kuwaokoa kwa sala. Lutu na nyumba yake walikuwa bado wakazi huko; na upendo usio na ubinafsi ndio uliomsukuma Ibrahimu kuwaokoa kutoka kwa Waelamu, sasa ulitafuta kuwaokoa kutoka kwenye dhoruba ya hukumu ya Bwana, ikiwa ni kwa mapenzi ya MUNGU. [Pr 124.5; Maombi Aya ya 13]

Kwa heshima kubwa na unyenyekevu alitoa ombi lake: "Nimejitolea kusema na Bwana, mimi ambaye ni mavumbi na majivu tu." Hakukuwa na kujiamini mwenyewe, wala kujisifu kwa haki yake mwenyewe. Yeye hakudai upendeleo kwa sababu ya utii wake, au dhabihu alizotoa kwa kufanya mapenzi ya MUNGU. Yeye mwenyewe akiwa mwenye dhambi, aliomba rehema kwa niaba ya mdhambi. Roho kama hiyo tunapaswa kumiliki wote tunaomkaribia MUNGU. Walakini Ibrahimu alionyesha ujasiri wa mtoto anayemwomba baba yake mpendwa. Alimkaribia Mjumbe wa mbinguni, na akahimiza ombi lake kwa bidii.... Pr 125.1; Maombi Aya ya 14]

Upendo kwa roho zinazoangamia ulimsukuma/ulimbidisha Ibrahamu kusihi. Wakati alikuwa anachukia dhambi za mji huo wenye ufisadi, matamania yake yalikuwa kwamba wenye dhambi waweze kukolewa. Kuijali kwake Sodoma kwa

kina kunaonyesha wasiwasi ambao tunapaswa kuhisi kwa wale wasiotubia dhambi zao. Tunapaswa kuichukia dhambi mioyoni mwetu, lakini kumwonea huruma na na kumpenda mwenye dhambi. - (Patriarchs and Prophets, 139, 140) [Pr 125.2; Maombi Aya ya 15]

Yakobo

Uzoefu wa Yakobo Unafundisha Umuhimu ombi linaloshinda, lisilochoka. lenye bidii na linaloleta ushawishi kwa wengine (prevailing prayer) — Yakobo alishinda kwa sababu alikuwa mvumilivu na mwenye kuazimia. Uzoefu wake unathibitisha nguvu ya sala ya kujitolea. Wakati huu ndio wa kujifunza somo hili la ombi linaloshinda na lisilochoka, na lisilokata tamaa. Ushindi mkubwa kwa kanisa la Kristo au kwa Mkristo mmoja mmoja sio ule unaopatikana kwa talanta au elimu, kwa utajiri au upendeleo wa watu. Bali ni ushindi ambao hupatikana katika chumba cha hadhira na MUNGU, wakati imani yenye bidii, yenye uchungu inashikilia mkono wa mkuu mwenye nguvu. [Pr 125.3; Maombi Aya ya 16]

Wale ambao hawataki kutelekeza kila dhambi na kutafuta kwa bidii baraka za MUNGU, basi hawatazipata. Lakini wote watakaoshika ahadi za MUNGU kama alivyofanya Yakobo, na kuwa na bidii na uvumilivu kama yeye, watafaulu kama yeye alivyofaulu. - (Patriarchs and Prophets, 203) [Pr 125.4; Maombi Aya ya 17]

Musa

Fuata Mfano wa Musa katika kuomba— Ongea kidogo (fanya magumzo kwa uchache sana); wakati wa thamani unapotea katika mazungumzo ambayo hayana nuru. Hebu ndugu waungane katika kufunga na kuombea hekima ambayo MUNGU ameahidi kutoa kwa kila mtu na kwa ukarimu. Mjulishe MUNGU shida zako. Mwambie, kama alivyofanya Musa, "Siwezi kuwaongoza watu hawa mpaka uwepo Wako utakapoenda nami." Na kisha omba zaidi; omba na Musa, "Nionyeshe utukufu wako." [Kutoka 33:18.] Utukufu huu ni nini? —Tabia na sifa ya MUNGU. Hivi ndivyo alimtangazia Musa. - (Gospel Workers, 417) [Pr 126.1; Maombi Aya ya 18]

Musa alifanya maombezi yenye Mafanikio kwa ajili ya Israeli - Agano la MUNGU na watu Wake lilikuwa limefutwa, na alimwambia Musa, "Niache, ili hasira Yangu iwake juu yao, na niwaangamize; Nami nitakufanya uwe taifa kubwa." Watu wa Israeli, haswa umati uliokuwa mseto (uliochangamana waisraeli na wamisri), walikuwa wana mwelekeo wa kumuasi MUNGU daima. Pia walilalamika dhidi ya kiongozi wao, na walimuhuzunisha kwa kutokuamini na ukaidi wao, na hivyo ingekuwa kazi ya kutoa jasho ya kujaribu roho kuwaongoza mpaka Nchi ya Ahadi. Dhambi zao tayari zilikuwa zimepoteza neema ya MUNGU, na haki ilidai waangamizwe. Kwa hiyo Bwana alipendekeza kuwaangamiza, na kumfanya Musa kuwa taifa lenye nguvu. [Pr 126.2; Maombi Aya ya ; Maombi Aya ya 19]

"Niachie Mimi,... ili niwaangamize," yalikuwa maneno ya MUNGU. Ikiwa MUNGU alikuwa amekusudia kuangamiza Israeli, ni nani angeweza kufanya maombezi kwa niaba yao? Ni wangapi kama si wachache tu ambao wangewaachia wenye dhambi kuikabili hatima yao! Ni wangapi kama si wachache wangefurahi kubadilishana na taabu nyingi na mzigo mzito na kujitoa kafara, kulipwa kwa 'shukurani ya punda mateke' na manung'uniko, kupewa nafasi ya raha na heshima, wakati ni MUNGU Mwenyewe Ndiye aliyekuwa anatoa afueni (Mungu alimruhusu Musa awe huru na uzao wake uendele! Akakataa na kuombea watu wake waisraeli). [Pr 126.3; Maombi Aya ya ; Maombi Aya ya 20]

Lakini Musa alitambua msingi wa tumaini pale ambapo palionekana panavunja moyo na ghadhabu tu. Maneno ya MUNGU, "Niache Mimi," aliyaelewa kama kutomaanisha kumkataza yeye (Musa) bali kumhamasisha afanye maombezi, Akimaanisha kuwa hakuna chochote isipokuwa maombi ya Musa yangeweza kuokoa Israeli, yaani yabidi aombe kwa niaba yao na kwa kufanya hilo, MUNGU angewasamehe watu Wake [Pr 126.4; Maombi Aya ya ; Maombi Aya ya 21]

Kadiri Musa alivyofanya maombezi kwa ajili ya Israeli, unyonge na woga wake ulipotea katika shauku yake ya kina na upendo kwa wale ambao aliwaweka mikononi mwa MUNGU, ambaye Ndiye njia ya kufanya mengi. Bwana alisikiza maombi yake, na akajibu maombi yake yasiyo ya ubinafsi. MUNGU alikuwa amemthibitisha mtumishi Wake; Alikuwa amejaribu uaminifu wake na upendo wake kwa watu hao wakosaji, wasio na shukurani, na kwa ubora na busara, Musa alivumilia jaribu. Masilahi yake kwa Israeli hayakutokana na nia ya ubinafsi. Ustawi wa watu waliochaguliwa/walioteuliwa na MUNGU ulikuwa wa kupendeza kwake kuliko heshima ya binafsi, wenye kupendeza kuliko fursa ya yeye kuwa baba wa taifa lenye nguvu. MUNGU alifurahishwa na uaminifu wake, unyenyekevu wa moyo, usahili wa moyo, na uadilifu wake, na akamkabidhi yeye, kama mchungaji mwaminifu, jukumu kubwa la kuongoza Israeli kwenda Nchi ya Ahadi. - (Patriarchs and Prophets, 318, 319) [Pr 127.1; Maombi Aya ya 22]

Musa Aliendelea kuwasilisha Maombi yake kwa MUNGU— Musa alijua upotovu na upofu wa wale ambao waliwekwa chini ya uangalizi wake; alijua shida na changamoto anazopaswa kushindana nazo. Lakini alikuwa amejifunza kwamba ili kufanikiwa kuongoza watu hao, lazima awe na msaada kutoka kwa MUNGU. Aliomba ufunuo wazi wa mapenzi ya MUNGU na uhakikisho wa uwepo Wake: "Tazama, unaniambia, Walete watu hawa: na hukunijulisha ni nani utakayemtuma pamoja nami. Lakini umesema, nakujua kwa jina lako, nawe umepata neema mbele zangu. Basi sasa, nakuomba, ikiwa nimepata neema machoni pako, nionyeshe njia yako, ili nipate kukujua, ili nipate kibali machoni Pako; na zingatia kuwa taifa hili ni watu wako. [Pr 127.2; Maombi Aya ya 23]

Jibu lilikuwa, "Uwepo Wangu utaenda nawe, Nami nitakupa raha." Lakini Musa

alikuwa bado hajaridhika. kulikuwa na shinikizo la kuogofya juu ya nafsi yake juu ya hisia ya matokeo mabaya ikiwa MUNGU angewaacha Israeli wakutane na maisha magumu na kutojutia dhambi zao. Hakuweza kuvumilia kwamba masilahi yake yatenganishwe na yale ya ndugu zake, na aliomba kwamba neema ya MUNGU irejeshwe kwa watu Wake, na kwamba ishara ya uwepo Wake iendelee kuongoza safari zao: " uwepo Wako usipoenda nami, usituchukue kutoka hapa. Kwa maana itajulikanaje hapa kuwa mimi na watu Wako tumepata neema mbele Zako? Je! si kwa sababu Wewe unaenda pamoja nasi? Basi tutatenganishwa, mimi na watu Wako, dhidi ya watu wote walio juu ya uso wa dunia. [Pr 127.3; Maombi Aya ya 24]

Bwana akasema, "Nitafanya jambo hili pia ulilolinena; kwa kuwa umepata neema mbele Zangu, na nakujua kwa jina." Bado nabii hakuacha kuomba/kusihi. Kila sala ilikuwa imejibiwa, lakini alikuwa na kiu ya ishara kubwa za upendeleo wa MUNGU. Sasa alifanya ombi ambalo hakuna mwanadamu aliyewahi kufanya hapo awali: "Ninakuomba, nionyeshe utukufu Wako." [Pr 128.1; Maombi Aya ya 25]

MUNGU halikukemea ombi lake kama la kujiamini kwa kupitiliza (au kuonyesha ukaidi au kiburi); lakini maneno ya neema yalisemwa, "Nitapitisha wema Wangu wote mbele yako." Utukufu uliofunuliwa wa MUNGU, hakuna mtu katika hali hii ya kufa anayeweza kutazama na kuishi; lakini Musa alihakikishiwa kwamba angeliangalia utukufu wa Mungu kwa kadiri atakavyoweza kuvumilia. Kisha akaitwa tena kwenye kilele cha mlima; halafu Mkono ule ulioumba ulimwengu, ule Mkono "unaoondoa milima, nao watu hawajui" (Ayubu 9: 5), ukamchukua kiumbe huyu wa mavumbi, mtu huyu hodari wa imani, na kumweka katika pango la mwamba, wakati utukufu wa MUNGU na wema Wake wote ukapita mbele yake. [Pr 128.2; Maombi Aya ya 26]

Uzoefu huu - Zaidi ya yote, ahadi ya kwamba Uwepo wa MUNGU ungemhudumia - kwake Musaulikuwa ni uhakikisho wa kufanikiwa katika kazi iliyokuwa mbele yake; na aliihesabu hili kuwa lenye thamani isiyopimika kuliko elimu yote ya Misri au mafanikio yake yote kama kiongozi wa serikali au kiongozi wa jeshi. Hakuna nguvu ya kidunia au ujuzi au ujifunzaji unaoweza kuwa mbadala wa uwepo wa MUNGU unaodumu. - (Patriarchs and Prophets, 327, 328) [Pr 128.3; Maombi Aya ya 27]

Chini ya Msongo, Maombi ya Musa yakafanana kama Malalamiko kwa kiasi fulani-Moyo wa Musa ukazama. Alikuwa ameomba kwamba Israeli wasiangamizwe, hata kama kizazi chake kingeweza kuwa taifa kubwa wakati huo. Katika upendo wake kwao alikuwa ameomba kwamba jina lake lifutwe kutoka kitabu cha uzima kuliko waisraeli waachwe na kuangamia. Alikuwa amehatarisha yote kwa ajili yao, na haya ndiyo majibu yao. Shida zao zote, hata mateso yao ya kufikirika, walimtuhumu yeye; na manung'uniko yao mabaya ulikuwa mzungu uliomlema mara mbili kwa utunzaji na uwajibikaji ambao aliubeba. Katika dhiki

yake alijaribiwa hata kutomwamini MUNGU. Maombi yake yalikuwa kama malalamiko. "Kwa nini umemtesa mtumishi Wako? Kwa nini sikupata kibali machoni Pako, hata ukaniwekea mzigo wa watu hawa wote juu yangu? ... ni wapi nitapata nyama kuwapa watu hawa wote? maana wananililia wakisema, Tupe nyama, tule. Siwezi kubeba watu hawa wote peke yangu, kwa sababu ni mzigo mzito kwangu. [Pr 128.4; Maombi Aya ya 28]

Bwana alisikiza sala yake, na akamwongoza aite wanaume sabini miongoni mwa wazee wa Israeli-wanaume sio tu walio na umri mkubwa, lakini waliokuwa na hadhi, maamuzi mazuri, hekima na uzoefu. "Na uwalete kwenye hema ya kukutania," alisema, "ili wasimame hapo pamoja nawe. Nami nitashuka na kuzungumza nawe huko; Nami nitachukua baadhi ya roho iliyo juu yako, na kuiweka juu yao; nao watabeba mzigo wa watu pamoja nawe, ili usichukue wewe peke yako." (Patriarchs and Prophets, 379, 380) [Pr 129.1; Maombi Aya ya 29]

Musa aliomba Rehema kwa ajili ya Israeli — Musa sasa akainuka na kuingia katika madhabahu ya kukutania. Bwana akamtangazia hivi, "Nitawapiga kwa tauni, na kuwazuia, na nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa zaidi." Lakini tena Musa alisihi kwa maombezi kwa ajili ya watu wake. Hangekubali waangamizwe, na yeye mwenyewe afanywe kuwa taifa lenye nguvu. Akiomba huruma ya MUNGU, alisema: "Ninakuomba, nguvu za Bwana wangu ziwe kubwa kama ulivyozungumza, ukisema, Bwana ni mvumilivu, na mwingi wa rehemawasamehe, ninakuomba Wewe, uovu wa watu hawa kulingana na ukuu wa rehema Zako, na jinsi ulivyowasamehe watu hawa, kutoka Misri hata sasa." [Pr 129.2; Maombi Aya ya 30]

Bwana aliahidi kuwaepusha Israeli na uharibifu wa haraka; lakini kwa sababu ya kutokuamini kwao na woga hakuweza kudhihirisha nguvu Zake katika kuwashinda adui zao. Kwa hiyo kwa rehema Yake aliwaamuru, kama njia pekee salama, warudi nyuma kuelekea Bahari ya Shamu. - (Patriarchs and Prophets, 390, 391) [Pr 129.3; Maombi Aya ya 31]

Maombi ya Musa yaliwaokoa Waisraeli dhidi ya Hukumu za MUNGU— watu walipomwangalia yule mtu mwenye umri mkubwa, aliyekuwa anakaribia kuchukuliwa kutoka kwao, walikumbuka, kwa shukrani mpya na ya kina, huruma yake ya 'mzazi', mashauri yake ya busara, na kazi yake isiyochoka. Ni mara ngapi, ambapo dhambi zao zilikuwa zimealika hukumu za haki za MUNGU, na sala za Musa zikaendelea bila kuchoka na kushinda pamoja Naye Mungu na kisha hawakuwaangamiza! Huzuni yao iliongezeka kwa majuto. Walikumbuka kwa uchungu kwamba upotovu wao wenyewe ulikuwa umempelekea Musa kwenye dhambi ambayo kwayo anapaswa kufa.- (Patriarchs and Prophets, 470) [Pr 129.4; Maombi Aya ya 32]

Ombi la Mwisho la Musa lililotimizwa katika Mlima wa kugeuka sura kwa Yesu kwa mng'ao usoni— hakuna muda hapo awali, mpaka ilipodhihirika katika mfano

wa dhabihu ya Kristo, ambapo haki na upendo wa MUNGU vilionyeshwa kwa kushangaza zaidi kuliko katika kushugulika Kwake na Musa. MUNGU alimfungia Musa nje ya Kanaani, ili kufundisha somo ambalo halipaswi kusahaulika kamwe— kwamba Anahitaji utii kamili, na kwamba watu wanapaswa kuwa waangalifu dhidi ya kujichukulia utukufu ambao ni wa Muumba wao tu. Hakuweza kulitimiza ombi la Musa kwamba apate kushiriki urithi wa Israeli, hata hivyo hakumsahau au kumwacha mtumishi Wake. MUNGU wa mbinguni alielewa mateso ambayo Musa alikuwa amevumilia; Alikuwa ameona kila tendo la huduma ya uaminifu kwa miaka hiyo mingi ya mizozo na majaribio/mitihani. Juu ya Pisga, MUNGU alimwita Musa kwenye urithi mtukufu zaidi kuliko Kanaani ya kidunia. [Pr 130.1; Maombi Aya ya 33]

Juu ya mlima wa mng'ao wa uso wa Yesu (transfiguration), Musa alikuwepo na Eliya, ambaye alikuwa ametwaliwa. Walitumwa kama wabebaji wa nuru na utukufu kutoka kwa Baba kwenda kwa Mwanawe. Na hivyo ombi la Musa, ililolitoa karne nyingi zilizopita, mwishowe lilitimizwa. Alisimama juu ya "mlima mzuri", ndani ya nchi ya urithi wa watu wake Israeli, akishuhudia kwake Yeye ambaye ahadi zote kwa Israeli zimejikita kwake. Hili ndilo lilikuwa tukio la mwisho alilofunuliwa Musa katika maono wakati bado akiwa na mwili unaokufa, katika historia ya mtu huyo aliyeheshimiwa sana na Mbingu. - (Patriarchs and Prophets, 479) [Pr 130.2; Maombi Aya ya 34]

Hana

Mfano wa Hana unamtia moyo Kila Mama — Kutoka Shilo, Hana alirudi kimya nyumbani kwake huko Rama, akimwacha mtoto Samweli afundishwe utumishi katika nyumba ya MUNGU, chini ya maagizo ya kuhani mkuu. Kuanzia mafunzo ya awali ya akili yake alikuwa amemfundisha mtoto wake kumpenda na kumcha MUNGU na kujiona kama yeye ni wa Bwana. Kwa kila kilichomzunguka alichokifahamu alikuwa anatarajia kuwa atapeleka mawazo yake kwa Muumba. Walipotengana na mtoto wake, upweke wa mama mwaminifu haukukoma. Kila siku Samweli alikuwa chini ya maombi yake. Kila mwaka alimtengenezea kwa mikono yake mwenyewe, joho la utumishi wake; na alipokwenda pamoja na mumewe kuabudu huko Shilo, alimpa mtoto ukumbusho huu wa upendo wake. Kila nyuzi ya vazi dogo ilikuwa imesokotwa na maombi ili awe safi, adhimu, bora na mkweli. Hakuomba ukuu wa ulimwengu kwa mtoto wake, lakini aliomba kwa bidii ili apate ukuu ambao Mbingu inathamini-ili amheshimu MUNGU na kubariki wanadamu wenzake. [Pr 130.3; Maombi Aya ya 35]

Hana alikuwa na thawabu iliyoje! Na ni mfano wa faraja ya kuita moyo kwa namna gani juu ya uaminifu wake! Kuna fursa za thamani isiyo na kifani, masilahi yenye thamani kubwa, yaliyowekwa kwa kila mama. Duru zaunyenyekavu ambazo wanawake wameziona kama kazi ya kuchosha zinapaswa kuangaliwa kama kazi kuu na bora. Ni fursa ya mama kuubariki ulimwengu kwa ushawishi

wake, na kwa kufanya hivyo ataleta furaha moyoni mwake. Anaweza kutengeneza njia zilizonyooka kwa ajili ya miguu ya watoto wake kupitia katika mwangaza wa jua na kivuli, hadi utukufu wa juu kabisa. Lakini ni wakati tu anapotafuta, katika maisha yake mwenyewe kufuata mafundisho ya Kristo, ndipo ambapo mama anaweza kutumaini kuunda tabia ya watoto wake kulingana na mfano wa Mungu/mbingu. Ulimwengu unafurika na ushawishi mbaya. Mitindo na desturi zina nguvu kubwa juu ya vijana. Ikiwa mama atashindwa katika jukumu lake la kufundisha, kuongoza, na kuzuia, watoto wake, kwa asilia/kawaida watakubali uovu, na kuachana na wema. Hebu kila mama aende mara kwa mara kwa Mwokozi wake na sala, "Tufundishe, tutamwamuru vipi mtoto, na tufanye nini kwake?" Hebu azingatie mafundisho ambayo MUNGU ametoa katika Neno Lake, naye atapewa hekima kadiri atakavyohitaji. - (Patriarchs and Prophets, 572, 573) [Pr 131.1; Maombi Aya ya 36]

Hana alikuwa Mwanamke wa Maombi — Hana hakutoa lawama kwa mumewe kuhusiana na ndoa yake isiyo na busara. Huzuni ambayo hakuweza kushiriki na rafiki wa kidunia, aliipeleka kwa Baba yake wa Mbinguni, na kutafuta faraja kutoka kwa Yeye peke yake ambaye alisema, "Niite siku ya shida, Nami nitakuokoa." Kuna nguvu kubwa katika maombi. Adui yetu mkuu anatafuta kila mara kuweka roho iliyofadhaika mbali na MUNGU. Ombi kuelekea Mbinguni la mtakatifu mnyenyekevu zaidi, hutazamwa kwa 'kuwaka moto tumbo' na Shetani kuliko sheria za mabaraza ya nchi au maagizo ya wafalme. [Pr 131.2; Maombi Aya ya 37]

Sala ya Hana haikusikiwa na sikio la mwandamu anayekufa, lakini iliingia kwenye sikio la Bwana wa majeshi. Aliomba kwa dhati na bidii kwamba kwamba MUNGU aiondoe aibu yake, na ampe kibali cha kuthaminiwa zaidi na wanawake wa umri huo, - baraka ya kuwa mama. Alipokuwa akishindana mieleka katika maombi, sauti yake haikutoa mlio (haikusikika), lakini midomo yake ilisogea na uso wake ulitoa ushahidi wa hisia za ndani za kina. Na sasa mtihani mwingine ulimngojea mwombaji huyu mnyenyekevu. Jicho la Eli kuhani mkuu lilipotua kwake, aliamua kwa haraka kwamba alikuwa amelewa. Sherehe za karamu isiyo na adabu ya ulevi na uzinzi zilikuwa zimeukanyaga utauwa wa kweli miongoni mwa watu wa Israeli. Matukio ya kukosekana kwa adabu na kutotawala nafsi kwa vileo, hata kati ya wanawake, yalitokea mara kwa mara, na sasa Eli aliazimia kusimamia kile alichokiona kuwa kinastahili kukemewa. "Utalewa mpaka lini? Ondoa divai yako." [Pr 132.1; Maombi Aya ya 38]

Hana alikuwa akiongea na MUNGU. Aliamini kwamba sala yake imesikilizwa, na amani ya Kristo iliujaza moyo wake. Haiba yake ilikuwa ya woga, upole, na nyeti, na bado hakutumbukia katika sikitiko wala hasira kwa kutuhimiwa pasipo haki na kwa hasira kwamba amelewa katika nyumba ya MUNGU. Kwa heshima kubwa kwa watiwa-mafuta wa Bwana, alituliza mashtaka hayo kwa utulivu na

kusema sababu ya hisia zake. "Hapana Bwana wangu, mimi ni mwanamke mwenye roho ya huzuni. Sikunywa divai wala kileo, lakini nimemwaga roho yangu mbele za Bwana. Usimhesabie mjakazi wako kuwa binti wa Beliali, kwa kuwa kwa sasa niliongea kwa malalamiko yangu na huzuni yangu." Akishawishika kwamba maonyo yake hayakuwa ya haki, Eli alijibu, "Nenda kwa amani, na MUNGU wa Israeli akupe ombi lako ulilomwomba." [Pr 132.2; Maombi Aya ya 39]

Katika sala yake, Hana alikuwa ameweka nadhiri kwamba ikiwa ombi lake litakubaliwa, atamtoa mtoto wake kwa ajili ya huduma kwa MUNGU. Kiapo hiki alimjulisha mumewe, na alithibitisha katika hafla adhimu ya ibada, kabla ya kuondoka Shilo. [Pr 132.3; Maombi Aya ya 40]

Sala ya Hana ilijibiwa, na akapokea zawadi ambayo alikuwa ameiomba kwa unyofu na bidii. Alipotazama ahadi ya upendeleo wa Bwana alimwita mtoto Samweli –Nilimwombwa kwa MUNGU. - (The Signs of the Times, Oktoba 27, 1881) [Pr 133.1; Maombi Aya ya 41]

Eliya

Eliya aliomba kwa ajili ya kutubu kwa Israeli – Kati ya milima ya Gileadi, mashariki mwa Yordani, katika siku za Ahabu kulikuwa na mtu wa imani na maombi ambaye huduma yake isiyo na woga ilikusudiwa kusitisha kuenea kwa uasi haraka katika Israeli. Akiwa mbali sana na mji wowote mashuhuri, na bila ya kuwa na nafasi ya juu maishani, hata hivyo Eliya mtishibi aliingia katika utume wake akiwa na ujasiri katika kusudi la MUNGU la kuandaa njia mbele yake na kumpa mafanikio tele. Neno la imani na nguvu lilikuwa juu ya midomo yake, na maisha yake yote yalikuwa ya kujitolea kwa kazi ya matengenezo. Sauti yake ilikuwa ya mtu anayelia nyikani kukemea dhambi na kuzuia wimbi la uovu lirudi nyuma. Na wakati alipoenda kwa watu kama mkemeaji wa dhambi, ujumbe wake ulitoa zeri ya Gileadi kwa roho za wagonjwa na wadhambi wote ambao walitaka kuponywa. [Pr 133.2; Maombi Aya ya 42]

Kadiri Eliya alivyoona Israeli inazidi kudumbukia chini zaidi katika ibada ya sanamu, ndivyo roho yake ilifadhaika na hasira yake ikaamka. MUNGU alikuwa amefanya mambo makubwa kwa watu Wake. Alikuwa amewaokoa kutoka utumwani na kuwapa "nchi za mataifa (pagani), ... ili wazishike amri Zake, na kuzishika sheria Zake." Zaburi 105: 44, 45. Lakini mipango ya neema ya Yehova ilikuwa imesahaulika. Kutoamini kulikuwa kunalitenganisha haraka taifa lililochaguliwa kutoka kwenye Chanzo cha nguvu zake. Akiuona uasi huu kutoka katika mfungo/kujitenga kwake mlimani, Eliya aligubikwa na huzuni. Kwa uchungu wa roho alimsihi MUNGU awakamate watu waliowahi kupendelewa katika mwenendo wao mbaya, awatembelee na hukumu, ikiwa ni lazima, ili waongozwe kuona katika nuru ya kweli kuchepuka kwao kutoka kwenye mpango wa mbingu. Alitamani kuwaona wakitubu kabla hawajazama katika maovu kiasi cha kumfanya Bwana awaangamize kabisa. [Pr 133.3; Maombi Aya ya 43]

Ombi la Eliya lilijibiwa. Wito uliorudiwa mara kwa mara, majibizano, na maonyo vilishindwa kuileta Israeli kwenye toba. Wakati ulikuwa umefika ambapo lazima MUNGU azungumze nao kwa njia ya hukumu. Japokuwa waabudu Baali walidai kwamba hazina za mbinguni, umande na mvua, havikutoka kwa Yehova, bali kutoka kwenye nguvu asilia za maumbile, na kwamba ilikuwa kupitia nishati ya uumbaji wa jua kwamba dunia ilitajirika na kufanywa kuleta mazao kwa wingi, laana ya MUNGU ilikuwa inaenda kukaa juu ya ardhi iliyonajisiwa. Makabila ya waasi wa Israeli yalipaswa kuonyeshwa upumbavu wa kuamini nguvu ya Baali kwa ajili ya mibaraka ya muda (kama mvua). Mpaka watakapomgeukia MUNGU wakiwa na toba, na kumkubali kuwa Ndiye chanzo cha baraka zote, mvua wala umande havitaanguka juu ya nchi. - (Prophets and Kings, 119, 120) [Pr 134.1; Maombi Aya ya 44]

Hofu ya MUNGU ilikuwa ikipungua kila siku katika Israeli. Ishara za kukufuru za upofu wao wa kuabudu sanamu zao zilikuwa zikionekana kati ya Israeli wa MUNGU. Hakukuwa na mtu aliyethubutu kufichua maisha yao kwa kusimama waziwazi kinyume na ibada ya sanamu yenye kukufuru iliyokuwepo. Madhabahu za Baali, na makuhani wa Baali ambao walitoa dhabihu kwa jua, mwezi, na nyota, zilikuwa maarufu kila mahali. Walikuwa wameweka wakfu mahekalu na miti, ambapo ndani yake kuliwekwa kazi ya mikono ya watu kwa ajili ya kuabudu. Manufaa ambayo MUNGU aliwapa watu hawa hazikuleta shukrani kwa Mpaji. Kwa neema zote za Mbingu, vijito vya maji, na mikondo ya maji yaliyo hai, umande mwororo, na manyunyu ya mvua kuiburudisha dunia, na kusababisha mashamba yao yatoe mazao kwa wingi, walidai ni neema ya miungu yao. [Pr 134.2; Maombi Aya ya 45]

Nafsi ya uaminifu ya Eliya ilihuzunika. Hasira yake iliwashwa, na alikuwa na wivu kwa utukufu wa MUNGU. Aliona kwamba Israeli ilikuwa imetumbukia katika uasi wa imani unaotisha. Alitindikiwa na mshangao na huzuni kwa uasi wa watu, wakati alipokumbuka mambo makubwa ambayo MUNGU alikuwa amewafanyia. Lakini hii yote ilisahaulika na watu wengi. Alikwenda mbele za MUNGU, na roho yake ikiwa imebanwa kwa uchungu, akamsihi Yeye awaokoe watu Wake ikiwa ni lazima awahukumu. Akamsihi MUNGU azuie umande, hazina za mbinguni na mvua kwa watu Wake wasio na shukrani, ili waasi wa Israeli waweze kutazama na kuona kwamba sanamu zao ni kazi bure, sanamu zao za dhahabu, mbao, na jiwe, jua, mwezi, na nyota, miungu yao, haziwezi kumwagilia ardhi na kuipatia utajiri, na kuifanya izea sana. MUNGU alimwambia Eliya alikuwa amesikia maombi yake. Naye angewazuilia watu Wake umande na mvua, mpaka wamgeukie Yeye kwa toba. - (The Review and Herald, September 16, 1873) [Pr 134.3; Maombi Aya ya 46]

Katika miaka mingi ya ukame na njaa, Eliya aliomba kwa bidii ili mioyo ya Israeli igeuzwe kutoka kwenye ibada ya sanamu na kuwa watiifu kwa MUNGU.

Kwa subira nabii huyo akangojea, wakati mkono wa Bwana ulikaa kwa uzito wa adhabu katika nchi iliyopigwa na ukame. Alipoona dalili za mateso na umasikini unazidi kila upande, moyo wake ulikuwa umefunikwa na huzuni, na alitamani nguvu ya kuleta matengenezo haraka. Lakini MUNGU mwenyewe alikuwa akifanya mkakati Wake, na yote ambayo mtumishi Wake angefanya ni kusali kwa imani na kungojea wakati wa kuchukua hatua. - (Prophets and Kings, 133) [Pr 135.1; Maombi Aya ya 47]

Eliya Mfano wa Mtu Ambaye Alishinda Kupitia Maombi ya Dhati — Tunapaswa kuwa katika maombi ya siri daima. Kristo Ndiye mzabibu, ninyi ni matawi. Ili tuweze kushamiri, lazima tuendeleo kupata maji na lishe ya utomvu kutoka kwenye Mzabibu ulio Hai; kwa kuwa tukitengwa kutoka kwa Mzabibu tutakuwa hatuna nguvu. [Pr 135.2; Maombi Aya ya 48]

Nilimuuliza malaika kwanini hakukuwa na imani na nguvu tena katika Israeli. Alisema, "Ninyi mnaachilia mkono wa Bwana mapema sana. Wasilisha maombi yako kwenye kiti cha enzi kwa ari/usongo, na ushikilie kwa imani thabiti. Ahadi ni za Kweli. Amini kwamba mnapokea mnayoomba, nanyi mtayapata." Kisha nikaelekezwa kwa Eliya. Alikuwa na haiba ya wanadamu kama sisi, na aliomba kwa dhati na bidii. Imani yake ilivumilia jaribu. Aliomba mara saba mbele za Bwana, na mwishowe wingu likaonekana. Niliona kwamba tulikuwa tumetilia mashaka ahadi za hakika, na tukamjeruhi Mwokozi kwa ukosefu wetu wa imani. Malaika alisema, "Jifunge silaha, na juu ya yote chukua ngao ya imani; kwa kuwa hiyo italinda moyo, na uzima, na mishale ya moto ya waovu." Ikiwa adui anaweza kusababisha wale waliokata tamaa kuondoa macho yao kutoka kwa Yesu, na kujitazama wenyewe, na kukita kwenye kutostahili kwao, badala ya kukaa juu ya ustahiki wa Yesu, upendo Wake, sifa Zake, na rehema Zake kuu, adui ataondoa ngao yao ya imani na kupata lengo lake; watakuwa katika hatari ya vishawishi vyake vyake vya moto mkali. Kwa hiyo wanyonge wanapaswa kumtazama Yesu, na kumwamini; hivyo huonyesha na kuizoesha imani yao. - (Early Writing, 73) [Pr 135.3; Maombi Aya ya 49]

Wajumbe wa MUNGU wasifanye haraka kuondoka mbele za Mungu bali wakae Naye kwa muda mrefu, ikiwa wangetaka kufanikiwa katika kazi yao. Kisa hiki kimesimuliwa ya mwanamke mzee wa Lancashire ambaye alikuwa akisikiliza sababu ambazo majirani zake walitoa kwa kufanikiwa kwa mchungaji wao. Walizungumza juu ya vipawa vyake, namna anavyojieleza, mtindo wake wa mahubiri, juu ya adabu zake au hulka. "La," alisema kikongwe, "nitakuambia ni nini. Mtu wako ni amejazwa sana na Mwenyezi." [Pr 136.1; Maombi Aya ya 50]

Watu watakapojitoa wakfu kama Eliya na watakapokuwa na imani aliyokuwa nayo, MUNGU atajifunua kama alivyofanya wakati ule. watakapomsihi Bwana kama vile Yakobo, matokeo ambayo yalionekana wakati huo yataonekana tena. Nguvu zitatoka kwa MUNGU kujibu maombi ya imani. - (Gospel Workers, 255) [Pr 136.2; Maombi Aya ya 51]

Maombi ya Eliya juu ya Mlima Karmeli Yalijibiwa kwa mshindo na ajabu – Akiwakumbusha watu juu ya uasi ulioendelea ambao umeamsha ghadhabu ya Yehova, Eliya aliwatolea wito wanyenyekeze mioyo yao na kumrudia MUNGU wa baba zao, Ili laana juu ya nchi ya Israeli iweze kuondolewa. Halafu, akiinama nakusujudu kwa heshima mbele ya MUNGU asiyeonekana, akainua mikono yake kuelekea mbinguni na kutoa sala rahisi. Makuhani wa Baali wamepiga kelele, wametoa povu mdomoni, na wamepata jazba na kuruka, kutoka asubuhi hadi jioni; lakini Eliya anapoomba, hakuna kelele za kugumia na mayowe yasiyo na maana yanayosikika kwenye kilele huko Karmeli. Anaomba kana kwamba anajua kuwa Yehova Yuko hapo, shahidi wa tukio hilo, msikilizaji wa ombi lake. Manabii wa Baali wameomba vikali, bila kueleweka. Eliya anasali kwa urahisi na kwa bidii, akimwomba MUNGU aonyeshe ukuu Wake juu ya Baali, ili Israeli iongozwe kumrudia Yeye. [Pr 136.3; Maombi Aya ya 52]

"Bwana MUNGU wa Ibrahimu, Isaka, na Israeli," nabii anaomba, "na ijulikane leo kuwa Wewe Ndiwe MUNGU katika Israeli, na kwamba mimi ni mtumishi wako, na kwamba nimefanya haya yote kwa Neno Lako. Nisikilize, Bwana, unisikilize, ili watu hawa wapate kujua ya kuwa Wewe Ndiwe Bwana MUNGU, na ya kuwa umeirudisha mioyo yao tena. [Pr 136.4; Maombi Aya ya 53]

Ukimya, mzito unaotesa katika ukuu wake unakaa juu ya wote. Makuhani wa Baali wanatetemeka kwa hofu. Kwa ufahamu wa hatia yao, wanatafuta kisasi cha haraka. [Pr 137.1; Maombi Aya ya 54]

Mara tu maombi ya Eliya yalipotamkwa, kukashuka miali ya moto kama umeme angavu wa radi kutoka mbinguni juu ya madhabahu iliyoinuliwa, ukiteketeza dhabihu, ukilamba maji ya mtaro, na kuteketeza hata mawe ya madhabahu. Mwangaza wa moto unaangaza mlima na kuangaza macho ya umati. Katika mabonde chini, ambapo wengi wanaangalia katika hali ya kutojua la kufanya kwa mashaka kuhusu harakati za wale walio juu, kushuka kwa moto kunaonekana wazi, na wote wanashangaa kuona. Unafanana na nguzo ya moto ambayo kwenye Bahari ya Shamu ilitenganisha watoto wa Israeli na jeshi la Wamisri. - (Prophets and Kings, 152, 153) [Pr 137.2; Maombi Aya ya 55]

Maombi ya Eliya Yalitoka kwa Imani katika Kudai Ahadi za MUNGU— Pamoja na kuuawa kwa manabii wa Baali, njia ilifunguliwa ya kuendelea na matengenezo makubwa ya kiroho kati ya makabila kumi ya ufalme wa kaskazini. Eliya alikuwa amewaonyesha watu uasi wao; alikuwa amewataka wanyenyekeze mioyo yao na kumrudia Bwana. Hukumu za Mbinguni zilikuwa zimetekelezwa; watu walikiri dhambi zao, na walimkubali MUNGU wa baba zao kama MUNGU aliye hai; na sasa laana ya Mbingu ilikuwa inaenda kuondolewa, na baraka za muda za maisha zikafanywa upya. Ardhi ilipaswa kuburudishwa na mvua. "Ondoka, ule, unywe," Eliya akamwambia Ahabu; "Kwa maana kuna sauti ya mvua nyingi." Kisha nabii akaenda juu ya mlima ili kuomba. [Pr 137.3; Maombi Aya ya 56]

Haikuwa kwa sababu ya uthibitisho wowote wa nje kwamba mvua ilikuwa karibu kunyesha, ndiyo kwamba Eliya aliweza kumwambia Ahabu kwa uhakika kwamba ajitayarisha kwa ajili ya mvua. Nabii hakuona mawingu mbinguni; hakisikia ngurumo. Alizungumza tu Neno ambalo Roho wa Bwana alikuwa amemsukuma kunena katika kuitikia imani yake yenye nguvu. Siku nzima alikuwa ametenda mapenzi ya MUNGU bila kuyumbayumba na alikuwa amedhirisha imani yake kamili katika unabii wa Neno la MUNGU; na sasa, akiwa amefanya yote ambayo yalikuwa katika uwezo wake kufanya, alijua kwamba Mbingu ingetoa kwa uhuru na ukarimu baraka zilizotabiriwa. MUNGU Yule Yule ambaye aliyekuwa ametuma ukame alikuwa ameahidi mvua tele kama malipo ya kutenda sahihi; na sasa Eliya alisubiri kumwagwa kwa ahadi. Katika mtazamo wa unyenyekevu, "uso wake katikati ya magoti yake," alifanya maombezi kwa MUNGU kwa ajili ya Israeli iliyotubu. [Pr 137.4; Maombi Aya ya 57]

Tena na tena, Eliya alimtuma mtumishi wake aende kwenye eneo lililo karibu mbalo angeweza kutazama bahari ya Mediterania, ili ajue ikiwa kulikuwa na ishara yoyote inayoonekana kuonyesha kwamba MUNGU alikuwa amesikia sala yake. Kila wakati mtumishi alirudi na neno, "Hakuna kitu." Nabii hakukosa subira au kupoteza imani, lakini aliendelea kuomba kwa bidii. Mara sita mtumishi alirudi na neno kwamba hakuna dalili ya mvua katika mawingu ya mbingu yaliyokuwa na rangi ya kahawia. Bila woga, Eliya akamtuma tena mara mora tena; na wakati huu mtumishi akarudi na neno, "Tazama, wingu dogo linatoka katika bahari ukubwa wa kiganja cha mkono wa mwanadamu." [Pr 138.1; Maombi Aya ya 58]

Hii ilitosha. Eliya hakungojea mbingu ziweze kukusanya weusi zaidi. Katika wingu hilo dogo aliona kwa imani mvua tele; naye akatenda kupatana na imani yake, akimtuma mtumishi wake haraka kwa Ahabu na ujumbe huu, "Tengeneza gari lako, ukashuke, mvua isikuzuie." [Pr 138.2; Maombi Aya ya 59]

Ilikuwa ni kwa sababu Eliya alikuwa mtu wa imani kubwa kwamba MUNGU angeweza kumtumia katika dharura na mgogoro huu mbaya katika historia ya Israeli. Alipokuwa akiomba, imani yake ilifikia na kuzishikilia kwa nguvu ahadi za Mbingu, na alidumu katika maombi hadi maombi yake yakajibiwa. Hakungoja uthibitisho kamili kwamba MUNGU alikuwa amemsikia, bali alikuwa tayari kujitosa kwa ishara hata kidogo ya upendeleo wa Bwana. Ila, kile alichowezeshwa kukifanya chini ya uwezo wa Mungu, wote tunaweza kukifanya katika nyanja yetu ya utendaji katika huduma/utumishi kwa MUNGU; Kwa maana imeandikwa hivi kuhusu nabii kutoka milima ya Gileadi: "Eliya alikuwa mtu wa tabia kama sisi, akaomba kwa bidii mvua isinyeshe; na mvua haikunyesha juu ya nchi muda wa miaka mitatu, miezi sita." Yakobo 1: 5, 17, [Pr 138.3; Maombi Aya ya 60]

Imani ya namna hii inahitajika ulimwenguni leo-imani ambayo itazishika ahadi za Neno la MUNGU na kukataa kuziacha hadi Mbingu itakaposikia. Imani kama

hii hutuunganisha kwa karibu na Mbingu, na hutuletea uwezo wa kukabiliana na nguvu za giza. Kwa imani watoto wa MUNGU“wamezitiisha falme, wametenda haki; walipata ahadi, walifunga vinywa vya simba, walizima udhalimu wa moto, waliokoka katika makali ya upanga, kutoka katika udhaifu walifanywa kuwa hodari, wakawa hodari katika vita, wakafukuza majeshi ya wageni. Waebrania 11:33, 34. Na kwa njia ya imani sisi leo tunapaswa kufikia kilele cha kusudi la MUNGU kwetu. "Ukiweza kuamini, mambo yote yanawezekana kwake yeye aaminiye." Marko 9:23. [Pr 138.4; Maombi Aya ya 61]

Imani ni jambo muhimu katika maombi yanayoshinda na yasiyochoka. "Yeye amwendeaye MUNGU lazima aamini kwamba Yeye Yuko, na kwamba Yeye huwapa thawabu wale wamtafutao." "Tukiomba chochote sawasawa na mapenzi Yake, Yeye hutusikia; na ikiwa tunajua kwamba Yeye hutusikia, lolote tuombalo, tunajua kwamba tuna maombi ambayo tulimwomba." Waebrania 11: 6; 1 Yohana 5:14, 15. Tukiwa na imani ya kudumu ya Yakobo, na uvumilivu wa Eliya, tunaweza kuwasilisha maombi yetu kwa Baba, tukidai yote ambayo ameahidi. Heshima ya kiti Chake cha enzi imo hatarini kwa utimilifu wa Neno Lake. (heshima ya Ukuu Wake imo hatarini endapo Neno Lake halitatimizwa kama vile ALIVYONENA YEYE) - (Prophets and Kings, 157, 158) [Pr 139.1; Maombi Aya ya 62]

Eliya Alidumu kwa uvumilivu Katika Maombi Hadi Jibu lilipokuja— Masomo muhimu huwasilishwa kwetu katika uzoefu wa Eliya. Akiwa juu ya mlima Karmeli aliomba maombi kwaajili ya mvua, imani yake ilijaribiwa, lakini aliendelea kumjulisha ombi lake kwa MUNGU. Aliomba kwa bidii mara sita, na bado hakukuwa na ishara kwamba ombi lake lingejibiwa, lakini kwa imani thabiti alihimiza ombi lake katika kiti cha neema. Kama angekata tamaa kwa mara ya sita, maombi yake yasingejibiwa, lakini alivumilia hadi jibu lilipokuja. Tunaye MUNGU ambaye sikio lake halijazibwa/hajaliziba kwaajili ya kupokea maombi yetu; na ikiwa tutalithibitisha Neno Lake (tutalipima na kuliona ndiyo kama anavyosema), ataheshimu imani yetu. Yeye anataka matamania yetu yote yafumwe pamoja na matamania yake, ndipo anaweza kutubariki sana; kwani hatutajivunia wakati baraka zinapokuwa zetu, lakini tutampa/tumtarudishia MUNGU sifa zote. MUNGU huwa hajibu maombi yetu mara ya kwanza tunapomuomba; kwani akifanya hivi, tunaweza kuichukulia kirahisi kwamba tuna haki ya baraka na neema zote alizotupatia. Badala ya kujitazama mioyo yetu kuona ikiwa kuna uovu wowote tunaouendekeza, au dhambi yoyote iliyoendekezwa, tunakuwa wazembe, na tunashindwa kutambua utegemezi wetu Kwake, na hitaji letu la msaada Wake. [Pr 139.2; Maombi Aya ya 63]

Eliya alijinyenyekeza mpaka alipokuwa katika hali ambayo asingejichukulia utukufu mwenyewe. Hili ndilo sharti ambalo kwalo Bwana husikia maombi, kwa kuwa tutampa sifa Yeye. Desturi ya kuwapa sifa wanadamu ndiyo inayosababisha uovu mkubwa. Mtu humsifu mwingine, na kwa hivyo mtu huyo huongozwa kuhisi kuwa utukufu na heshima ni mali yao. Unapomwinua

mwanadamu, unamwekea mtego katika nafsi yake, na kufanya kama Shetani anavyotaka ufanye. Unapaswa kumsifu MUNGU kwa moyo wako wote, roho, uwezo, akili na nguvu zote; kwa maana MUNGU peke yake Ndiye anayestahili kutukuzwa. - (SDA Bible Commentary 2: 1034, 1035) [Pr 140.1; Maombi Aya ya 64]

Mtumishi alitazama wakati Eliya akiomba. Alirudi mara sita kutoka kwenye lindo, akisema, Hakuna kitu, hakuna wingu, wala ishara ya mvua. Lakini nabii huyo hakukata tamaa kwa kuvunjika moyo. Aliendelea kupitia maisha yake, kuona ni wapi alikuwa ameshindwa kumheshimu MUNGU, kisha alikiri dhambi zake, na hivyo akaendelea kuitesa nafsi yake mbele za MUNGU, wakati akitafuta ishara kuona kwamba sala yake imeshajibiwa. Alipoendelea kuchunguza moyo wake, alionekana kuwa mdogo na amepungua, kwa makadirio yake mwenyewe na pia mbele ya MUNGU. Ilionekana kwake kuwa yeye si kitu, na kwamba MUNGU Ndiye kila kitu; na alipofikia hatua ya kujikana nafsi yake mwenyewe, huku akimshikilia kwa nguvu Mwokozi kama nguvu na haki yake pekee, basi jibu lilikuja. - (The Review and Herald, Mei 26, 1891) Herald, Mei 26, 1891) [Pr 140.2; Maombi Aya ya 65]

Daudi

Anguko la Daudi ni Onyo kwetu la Kutopuza Maombi - MUNGU alikusudia historia ya anguko la Daudi iwe kama onyo kwamba hata wale ambao Amewabariki sana na kuwapendelea hawapaswi kujisikia salama na kupuuza kukesha na maombi. Na hivyo ndivyo imedhihiriswa kwa wale ambao kwa unyenyekevu wametafuta kujifunza somo ambalo MUNGU amekusudia kufundisha. Kutoka kizazi hadi kizazi maelfu wameongozwa hivyo kutambua hatari yao wenyewe dhidi ya nguvu ya mshawishi. Kuanguka kwa Daudi, aliyeheshimiwa sana na Bwana, kumeamsha kwao, kutokujiamini. Wamehisi kwamba MUNGU pekee Ndiye awezaye kuwatunza wao kwa uwezo Wake kupitia imani. Wakajua kwamba ndani Yake kulikuwa na nguvu na usalama wao, wamekuwa na hofu ya kukanyaga mguu wao kwenye ile hatua ya kwanza kuelekea uwanja wa Shetani.-(Patriarchs and Prophets, 724) [Pr 140.3; Maombi Aya ya 66]

MUNGU alijibu Maombi ya Daudi ya Msamaha - Moja ya maombi ya dhati kabisa yaliyoandikwa katika Neno la MUNGU ni lile la Daudi wakati alipoomba, "Unda ndani yangu moyo safi, Ee MUNGU." Jibu la MUNGU kwa maombi kama haya ni, nitakupa moyo mpya. Hii ni kazi ambayo hakuna mwanadamu mwenye anayekufa anayeweza kuifanya. Wanaume na wanawake wanapaswa kuanza mwanzoni, wakimtafuta MUNGU kwa bidii zaidi kwa uzoefu wa Kweli wa Kikristo. Wanapaswa kuhisi uwezo wa uumbaji wa Roho Mtakatifu. Wanapaswa kupokea moyo mpya, ambao huwekwa laini na mkunjufu kwa neema ya mbinguni. Nafsi yenye ubinafsi inapaswa kusafishwa kutokea kwenye roho. Wanapaswa kufanya kazi kwa dhati, bidii na kwa unyenyekevu wa moyo, kila mmoja akimwangalia Yesu kwa ajili ya mwongozo na kutiwa moyo. Kisha jengo hilo, ambalo

limeundwa/limejengwa kwa pamoja, litakuwa hekalu takatifu katika Bwana. ((SDA Bible Commentary 4: 1165) [Pr 141.1; Maombi Aya ya 67]

Sulemani

Tunahitaji Kujifunza Somo Katika Maombi ya Unyenyekevu ya Sulemani – Mwanzoni mwa utawala wake, Sulemani aliomba: “Ee Bwana MUNGU wangu, Umemfanya mtumwa wako awe mfalme badala ya Daudi baba yangu: nami ni mtoto mdogo. Nami sijui namna ya kutoka au kuingia.” 1 Wafalme 3: 7. [Pr 141.2; Maombi Aya ya 68]

Sulemani alikuwa amemrithi baba yake Daudi katika kiti cha enzi cha Israeli. MUNGU alimheshimu sana, na, kama tunavyojua, alikuja kuwa mfalme mkuu, tajiri, na mwenye hekima aliyewahi kukalia kiti cha enzi duniani, katika miaka ya baadaye . Mwanzoni mwa utawala wake Sulemani alivutiwa na Roho Mtakatifu na uzito wa majukumu yake, na, ingawa alikuwa na talanta nyingi na uwezo, aligundua kuwa bila msaada wa Bwana alikuwa mnyonge kama mtoto mdogo kutenda lolote. Sulemani hakuwahi kuwa tajiri sana au mwenye busara sana au mkuu sana kama ule wakati alipomkiri Bwana kwa kusema: "Mimi ni mtoto mdogo: sijui kutoka au kuingia..... [Pr 141.3; Maombi Aya ya 69]

Na hotuba hiyo ilimpendeza Bwana, ya kwamba Sulemani alikuwa ameomba hili jambo. MUNGU akamwambia, Kwa kuwa umeomba neno hili, wala hukujitakia maisha marefu; wala hujaomba utajiri kwa ajili yako mwenyewe, wala hukutaka uhai wa adui zako; bali umejitakia ufahamu wa kupambanua hukumu; tazama, nimetenda sawasawa na maneno yako; tazama, nimekupa moyo wa hekima na wa akili; hata kabla yako hapakuwa na mtu kama wewe, wala baada yako hatainuka mtu kama wewe. Na pia nimekupa yale ambayo haujaomba, utajiri na heshima: hivi kwamba hakutakuwa na yeyote kati ya wafalme kama wewe siku zako zote.” Sasa masharti yalikuwa haya: "Na ikiwa utakwenda katika njia Zangu, ukazishika sheria Zangu na amri Zangu, kama vile baba yako Daudi alivyotembea, ndipo nitakurefushia siku zako." [Pr 141.4; Maombi Aya ya 70]

Wote wanaoshika nafasi za uwajibikaji wanahitaji kujifunza somo ambalo linafundishwa katika sala ya unyenyekevu ya Sulemani. Wanapaswa kukumbuka siku zote kwamba cheo hakitabadilisha tabia kamwe au kumzuia/kumwezesha mtu asitende dhambi tena kamwe. Kadiri mtu anavyochukua nafasi ya juu, ndivyo jukumu analobeba linavyozidi kuwa kubwa zaidi, na ndivyo ushawishi anaoshinikiza unavyokuwa mpana zaidi na ndivyo hitaji lake la kuhisi utegemezi wake juu ya hekima na nguvu za MUNGU na kustawisha tabia bora na takatifu zaidi huongezeka.— (Testimonies for the Church 9:281, 282). [Pr 142.1; Maombi Aya ya 71]

Mfano wa Sulemani - funzo La kukesha katika Maombi – ilikuwaje-kuwaje, katika kisa chake Sulemani mpaka akawa mtu dhaifu, mwenye tabia ya

kusuasua— mtu jasiri kwa kawaida, thabiti, na mwenye kuazimia — alivyotikiswa kama mwanzi katika upepo chini ya nguvu ya mshawishi! Je! Mwerezi wa Lebanoni mzee na uliokunjwa, mwaloni imara wa Bashani, ukainama mbele ya mlipuko wa majaribu! Ni somo lililoje kwa wote wanaotaka kuokoa roho zao wakeshe katika maombi daima. Ni onyo lililoje la kuweka neema ya Kristo mioyoni mwao, kupigana na uharibifu wa ndani ya moyo na majaribu ya nje.— (Manuscript Relees 21:383) [Pr 142.2; Maombi Aya ya 72]

Mfalme Hezekia

Hezekia aliwaombea masalia wa Israeli- "Siku hii ni siku ya taabu, na ya kukemea, na ya kukufuru," ndilo neno mfalme alilotuma. Huenda Bwana, MUNGU wako, atayasikia maneno yote ya amiri, ambaye mfalme wa Ashuru, bwana wake, amemtuma ili amtukane MUNGU aliye hai; naye atayakemea maneno aliyoyasikia Bwana, MUNGU wako; kwa hivyo inua maombi yako kwa masalia waliobaki." Mstari wa 3, 4. [Pr 142.3; Maombi Aya ya 73]

"Kwa sababu hii, mfalme Hezekia, na nabii Isaya mwana wa Amози, waliomba, wakalia Mbinguni." 2 Mambo ya Nyakati 32:20. [Pr 143.1; Maombi Aya ya 74]

MUNGU alijibu maombi ya waja Wake. Isaya alipewa ujumbe huu kwa ajili ya Hezekia: "BWANA asema hivi, Usiogope maneno uliyoyasikia, ambayo watumishi wa mfalme wa Ashuru wamenitukana. Tazama, nitapeleka mlipuko juu yake, naye atasikia fununu, na kuirudia nchi yake mwenyewe; na Nitamwangusha kwa upanga katika nchi yake mwenyewe." 2 Wafalme 19: 6, 7—(Prophets and Kings, 354) [Pr 143.2; Maombi Aya ya 75]

Ombi la Hezekia Lilipatana na mapenzi ya MUNGU-Wakati mfalme wa Yuda alipopokea barua ya kumtukana kwa kejeli, aliipeleka hekaluni na "kuifungua mbele za Bwana" na kuomba kwa imani thabiti msaada kutoka mbinguni, ili mataifa ya dunia yapate kujua kwamba MUNGU wa Waebrania bado yuko hai na anatawala. Mstari wa 14. Heshima ya Yehova ilikuwa hatarini; Yeye peke yake Ndiye angeweza kuleta ukombozi. [Pr 143.3; Maombi Aya ya 76]

"Ee Bwana, MUNGU wa Israeli, ukaaye kati ya makerubi," Hezekia aliomba, "Wewe Ndiwe MUNGU, Wewe peke Yako, wa falme zote za dunia; Wewe Ndiwe uliyefanya mbingu na nchi. Bwana, inamisha sikio Lako, usikie; fungua, Bwana, macho Yako, uone; na usikie maneno ya Senakeribu, aliyomtuma kumtukana MUNGU aliye hai. Kwa kweli, Bwana, wafalme wa Ashuru wameharibu mataifa na nchi zao, na wametupa miungu yao motoni; kwa kuwa hawakuwa miungu, bali kazi ya mikono ya wanadamu, miti na mawe; kwa hivyo wameiangamiza. Basi sasa, Ee Bwana, MUNGU wetu, nakuomba utuokoe na mkono wake, ili falme zote za dunia zijue ya kuwa Wewe Ndiwe Bwana MUNGU, Wewe peke yako. " 2 Wafalme 19: 15-19 [Pr 143.4; Maombi Aya ya 77]

Maombi ya Hezekia kwa niaba ya Yuda na heshima ya Mtawala wao Mkuu

yalikuwa katika umoja/upatanifu na mapenzi ya MUNGU. Sulemani, katika baraka zake wakati wa kuwekwa wakfu kwa hekalu, alikuwa amemwomba Bwana asimamie "hoja ya watu Wake Israeli wakati wote, kama itakavyohitajika: ili watu wote wa dunia wapate kujua kwamba Bwana Ndiye MUNGU, na kwamba hakuna mwingine." 1 Wafalme 8:59, 60. Bwana alikusudia kuonyesha upendeleo haswa wakati wa vita au ukandamizaji wa kijeshi, wakuu wa Israeli walipaswa kuingia katika nyumba ya sala na kuomba ukombozi. Mstari wa 33, 34. [Pr 143.5; Maombi Aya ya 78]

Hezekia hakuachwa bila tumaini. Isaya akatumwa kwake, akisema, "Bwana, MUNGU wa Israeli, asema hivi, Hilo uliloliomba dhidi ya Senakeribu mfalme wa Ashuru.—(Prophets and Kings, 355, 356, 359) [Pr 144.1; Maombi Aya ya 79]

Hezekia Aliponywa katika Jibu la Maombi — Tangu siku za Daudi, hakukuwa na mfalme aliyetawala ambaye alifanya kazi kubwa sana kwa ajili ya ujenzi wa ufalme wa MUNGU wakati wa kipindi cha uasi na kukata tamaa kama alivyofanya Hezekia. Mtawala aliyekaribia kufa alikuwa amemtumikia MUNGU wake kwa uaminifu, na alikuwa amefanya mengi kuimarisha imani ya watu kwa Yehova kama Mtawala wao Mkuu. Na, kama Daudi, sasa aliweza kusihi: "Maombi yangu na yaje mbele zako; tega sikio lako usikie kilio changu; kwa maana nafsi yangu imejaa taabu, na maisha yangu yanakaribia kaburi." "Wewe Ndiye tumaini langu, Ee Bwana MUNGU: Ndiwe tegemeo langu tangu ujana wangu. Nimeshikiliwa na wewe.... Usiniache nguvu zangu zipungukapo. Ee MUNGU, usiwe mbali nami: Ee MUNGU wangu, ufanye haraka kunisaidia Ee MUNGU, usiniache; hata nitakapoonyesha nguvu yako kwa kizazi hiki, na uweza wako kwa kila mtu atakayekuja." Zaburi 88: 2, 3; Zaburi 71: 5-18. [Pr 144.2; Maombi Aya ya 80]

Yeye ambaye "huruma Zake hazikomi" (Maombolezo 3:22) alisikia maombi ya mtumishi Wake. "Ikawa, kabla Isaya hajaenda katika ua wa katikati, Neno la Bwana likamjia, kusema, Rudi, ukamwambie Hezekia, mkuu wa watu wangu, Hivi ndivyo asemavyo Bwana, Mungu wa baba yako Daudi nimesikia ombi lako na nimeona machozi yako. Nitakuponya na baada ya siku tatu utakwenda katika nyumba ya Bwana. Nami nitakuongezea siku zako miaka kumi na tano; Nami nitakuokoa wewe na mji huu kutoka mkononi mwa mfalme wa Ashuru; Nami nitaulinda mji huu kwa ajili Yangu Mwenyewe, na kwa ajili ya mtumishi Wangu Daudi. 2 Wafalme 20: 4-6.— (The Review and Herald, Mei 6, 1915) [Pr 144.3; Maombi Aya ya 81]

Danieli

Sala ya Danieli Yenye Ufanisi, unyofu na Nguvu—Danieli alimwomba MUNGU, hakujiinua mwenyewe au kudai wema wowote: "Ee Bwana, sikia; Ee Bwana, samehe; Ee Bwana, sikiliza na utende; usichelewe, kwa mapenzi yako, Ee MUNGU wangu." Hivi ndivyo Yakobo anavyoliita ombi linalofaa, la dhati. Kuhusu Kristo

imeandikwa: "Na akiwa katika uchungu aliomba kwa bidii zaidi." Kwa kulinganisha na maombezi haya ya Mkuu wa mbinguni ni maombi dhaifu, yasiyo na moyo ambayo hutolewa kwa MUNGU. Wengi wanaridhika na huduma ya midomo, na ni wachache walio na shauku ya dhati, ya bidii, na ya upendo kwa MUNGU. -(Testimonies for the Church 4:534) [Pr 145.1; Maombi Aya ya 82]

Danieli Alidumu kuwa muaminifu Katika Maombi Licha ya Mateso — Je! Danieli aliacha kuomba kwa sababu agizo hilo lingeanza kutekelezwa! —Hapana, huo ndio wakati hasa aliohitaji kuomba. "Danieli alipojua ya kuwa maandishi yamesainiwa, aliingia nyumbani kwake; na, kwa kuwa dirisha lake lilikuwa wazi katika chumba chake kuelekea Yerusalemu, alipiga magoti mara tatu kwa siku, akasali, akashukuru mbele za MUNGU wake, kama vile alivyofanya zamani. " Danieli hakutafuta kuficha uaminifu wake kwa MUNGU. Yeye hakuomba kimya moyoni mwake, lakini kwa sauti yake, ya juu, dirisha lake likiwa wazi kuelekea Yerusalemu, alituma ombi lake mbinguni. Ndipo maadui zake wakalalamika kwa mfalme, na Danieli akatupwa ndani ya shimo la simba. Lakini Mwana wa MUNGU alikuwepo. Malaika wa Bwana alipiga kambi karibu na mtumishi wa Bwana, na mfalme alipokuja asubuhi, na kuita, "Ee Danieli, mtumishi wa MUNGU aliye hai, ni MUNGU wako, ambaye unamtumikia daima, anaweza kukuokoa simba? Ndipo Danieli akamwambia mfalme, Ee mfalme, uishi milele. MUNGU wangu amemtuma malaika Wake, na kuziba vinywa vya simba, wasinidhuru." Hakuna madhara yaliyompata, na alimtukuza Bwana MUNGU wa mbinguni. - (The Review and Herald, Mei 3, 1892) [Pr 145.2; Maombi Aya ya 83]

Sala ya Danieli yenye Bidii na Shauku—Wakati ulipokaribia mwisho wa miaka sabini ya utumwa wao (walikuwa mateka miaka 70), Akili ya Danieli ilifikiria na kuchunguza sana unabii wa Yereimia. Aliona kwamba wakati ulikuwa umefika ambapo Mungu angewapa watu Wake wateule jaribu lingine; na kwa kufunga, kujifedhehesha, na sala, alimsihi Mungu wa mbinguni kwa ajili ya Israeli, kwa maneno haya: "Ee Bwana, wewe ni Mungu mkuu na wa kuogofya. Wewe ni Mwaminifu kwa agano lako na unawafadhili wakupendao na kuzitii amri Zako. Tumetenda dhambi, tumekosa, tumetenda maovu na kukuasi. Tumezikiuka amri Zako na kanuni Zako. Hatukuwasikiliza watumishi Wako manabii, ambao kwa Jina Lako waliongea na wafalme wetu, wakuu wetu, wazee wetu na taifa letu lote." (Danieli 9:4-6) [Pr 145.3; Maombi Aya ya 84]

Danieli hatangazi uadilifu wake mwenyewe mbele za Bwana. Badala ya kudai kuwa safi na mtakatifu, nabii huyu aliyeheshimiwa anajitambulisha kwa unyenyekevu na yule mwenye dhambi kabisa wa Israeli. Hekima ambayo MUNGU alikuwa amempa ilikuwa bora zaidi kuliko hekima ya watu wakuu wa ulimwengu kama vile nuru ya jua inayoangaza mbinguni wakati wa adhuhuri inavyong'aa kuliko nyota dhaifu zaidi. Walakini tafakari maombi kutoka kwenye midomo ya mtu huyu aliyependelewa sana na Mbingu. Kwa unyonge na kujidhili kukubwa, kwa machozi na kupondeka kwa moyo, anasihi kwaajili yake mwenyewe na kwa

ajili ya watu wake. Anaiweka nafsi yake wazi mbele za MUNGU, akikiri kutostahili kwake na kukiri ukuu, utukufu na utawala wa Bwana. [Pr 146.1; Maombi Aya ya 85]

Ni unyoofu na ari iliyoje vilivyotawala dua zake! Mkono wa imani unainuliwa juu ili kushika ahadi zisizoshindwa kamwe za Yule Aliye Juu Zaidi. Nafsi yake inapigana mweleka kwa uchungu. Na ana ushahidi kuwa maombi yake yanasikika. Anajua kuwa ushindi ni wake. Ikiwa sisi kama watu tungeomba kama Danieli alivyoomba, na kupambana mieleka kama alivyopambana, tukizinyenyekeza nafsi zetu mbele za MUNGU, tunapaswa kutambua majibu ya maombi yetu kama yalivyotolewa kwa Danieli. Sikia jinsi anavyosisitiza kesi yake katika nyua za mbinguni: [Pr 146.2; Maombi Aya ya 86]

“Ee MUNGU wangu, tega sikio lako, usikie; fungua macho yako, utazame ukiwa wetu, na mji ulioitwa kwa Jina Lako; kwa maana hatutoi maombi yetu mbele Zako kwa ajili ya haki yetu, bali kwa ajili ya rehema Zako nyingi. Ee Bwana, usikie; Ee Bwana, samehe; Ee Bwana, usikie ukafanye; usicheleweshe; kwa ajili Yako, Ee MUNGU wangu, kwa maana mji Wako na watu Wako wanaitwa kwa Jina Lako” (mistari 18, 19). [Pr 146.3; Maombi Aya ya 87]

Mtu wa MUNGU alikuwa akiomba baraka za Mbinguni juu ya watu wake na ujuzi ulio wazi zaidi wa mapenzi ya MUNGU. Mzigo wa moyo wake ulikuwa kwa ajili ya Israeli, ambao hawakuishika sheria ya MUNGU kwa uthabiti kabisa. Alikubali kuwa misiba yao yote imewajia kama matokeo ya ukiukaji wao wa sheria hiyo takatifu. Anasema, “Tumetenda dhambi, tumetenda maovu Kwa sababu kwa ajili ya dhambi zetu, na maovu ya baba zetu, Yerusalemu na watu wako wamekuwa aibu kwa wote wanaotuzunguka” (mistari 15, 16). Wayahudi walikuwa wamepoteza tabia yao ya kipekee, takatifu kama watu waliochaguliwa na MUNGU. “Basi sasa, Ee MUNGU wetu, uyasikie maombi ya mtumishi wako, na dua zake, ukaangazie uso wako juu ya Patakatifu pako palipojitenga” (mistari 17). Moyo wa Danieli unageukia kwa shauku kuu kuelekea Patakatifu pa Mungu palipojitenga, yaani kwenye upweke. Anajua kwamba usitawi wake unaweza kurejeshwa pale tu Israeli watakapotubu makosa yao ya kuasi sheria ya MUNGU, na kuwa wanyenyekevu, waaminifu na watiifu. [Pr 147.1; Maombi Aya ya 88]

Wakati maombi ya Danieli yanaendelea, malaika Gabrieli anakuja akishuka kutoka nyua za mbinguni kumwambia kwamba maombi yake yamesikilizwa na kujibiwa. Malaika huyu mwenye nguvu ameagizwa kumpa ujuzi na ufahamu—kufungua mbele yake siri na mafumbo ya enzi zijazo (vizazi vijavyo). Kwa hiyo, huku akitafuta kwa bidii kujua na kuelewa Ukweli, Danieli aliletwa katika ushirika na mjumbe aliyetumwa wa Mbinguni. [Pr 147.2; Maombi Aya ya 89]

Katika kujibu ombi lake, Danieli alipokea si tu nuru na Ukweli ambao yeye na

watu wake walihitaji zaidi, bali mtazamo wa matukio makuu ya wakati ujao, hata ule ujio wa Mkombozi wa ulimwengu. Wale wanaodai kuwa wametakaswa, wakati hawana matamano/hamu ya kuchunguza Maandiko au kupigana mieleka na Mungu katika maombi ili kupata uelewa wa wazi wa ile Kweli ya Biblia, hawajui utakaso wa Kweli ni nini. (The Sanctified Life, 46-49) [Pr 147.3; Maombi Aya ya 90]

Nehemia

Ombi la Nehemia Ni Mfano kwa Watu wa MUNGU Leo—Mioyo ya wale wanaotetea jambo hili lazima ijazwe na Roho wa Yesu. Tabibu Mkuu peke yake Ndiye anayeweza kupaka zeri ya Gileadi. Hebu watu hawa wasome kitabu cha Nehemia kwa mioyo minyenyekevu iliyoguswa na Roho Mtakatifu, na mawazo yao ya uongo yatarekebishwa, na kanuni sahihi zitaonekana, na utaratibu uliopo sasa wa mambo utabadilishwa. Nehemia alimwomba MUNGU amsaidie, na MUNGU akasikia maombi yake. Bwana alifanya kazi kwenye mioyo ya wafalme wa mataifa waje kumsaidia. Wakati maadui zake walipofanya kazi kwa bidii dhidi yake, Bwana alifanya kazi kupitia wafalme kutekeleza kusudi Lake, na kujibu maombi mengi ambayo yalikuwa yakipanda kwenda Kwake kwa ajili ya msaada ambao waliuhitaji sana. - (The Review and Herald, Machi 23, 1911) [Pr 147.4; Maombi Aya ya 91]

Maombi yaliimarisha Imani na Ujasiri wa Nehemia—Kupitia wajumbe kutoka Yuda yule mzalendo Mwebrania alijua kwamba siku za majaribu zilikuwa zimefika Yerusalemu, jiji lililochaguliwa. Mateka waliorudi walikuwa wakipitia mateso na aibu. Hekalu na sehemu za mji zilikuwa zimejengwa upya; lakini kazi ya kurejesha hali ya mji na ukarabati ilikuwa inazuiliwa, huduma za hekalu zilivurugwa, na watu wakaendelea kupata mshtuko wa kuogofya kwa sababu kuta za jiji bado zilikuwa magofu kwa sehemu kubwa. [Pr 148.1; Maombi Aya ya 92]

Akiwa amezidiwa na huzuni, Nehemia hakuweza kula wala kunywa; "alilia, na kuomboleza siku kadha wa kadha, na kufunga." Katika huzuni yake alimgeukia Msaidizi wake ambaye alikuwa Mungu Mwenyewe. "Niliomba," alisema, "mbele za MUNGU wa mbinguni." Kwa uaminifu aliungama dhambi zake na dhambi za watu wake. Alisihi kwamba Mungu asimamie mambo ya Israeli, awarudishie ujasiri na nguvu, na awasaidie kujenga maeneo yaliyoharibiwa ya Yuda. [Pr 148.2; Maombi Aya ya 93]

Kadiri Nehemia alivyoomba, imani yake na ujasiri viliimarika. Kinywa chake kilijaa hoja takatifu. Alisonda kidole zile fedheha ambazo zingetupwa kwa Mungu, ikiwa watu Wake, ambao sasa wamerudi Kwake, wangeachwa katika udhaifu na mateso; naye akamsihi Bwana kutimiza ahadi Yake: "Mkinigeukia Mimi, na kuzishika Amri Zangu, na kuzifanya; ijapokuwa baadhi yenu walitupwa hata mwisho wa mbingu, lakini nitawakusanya kutoka huko, na kuwaleta mpaka mahali pale nilipochagua kuliweka Jina Langu huko." Tazama Kumbukumbu la

Torati 4: 29-3. Ahadi hii ilikuwa imetolewa kwa Israeli kupitia Musa kabla hawajaingia Kanaani, na kwa karne nyingi ilikuwa imesalia hivyo bila kubadilika. Watu wa MUNGU sasa walikuwa wamemrudia Yeye kwa toba na imani, na ahadi Yake haikushindwa. Mara nyingi Nehemia alikuwa amemwaga roho yake kwa niaba ya watu wake. Lakini sasa alipokuwa akiomba kusudi takatifu lilijenga akilini mwake. Aliazimia kwamba ikiwa angeweza kupata kibali cha mfalme, na usaidizi unaohitajika katika kupata zana na nyenzo, yeye mwenyewe angefanya kazi ya kujenga upya kuta za Yerusalemu na kurejesha nguvu za taifa la Israeli. Naye akamwomba Bwana amjalie kibali machoni pa mfalme, ili mpango huu utimie. “kufanikiwa, nakuomba, mtumishi wako leo,” akasihi, “na umpe rehema machoni pa mtu huyu.” [Pr 149.1; Maombi Aya ya 94]

Kwa miezi minne Nehemia alingoja nafasi nzuri ya kuwasilisha ombi lake kwa mfalme. Wakati huo, ingawa moyo wake ulikuwa mzito na wenye huzuni, alijitahidi kujistahi kwa uchangamfu mbele ya mfalme. Katika kumbi hizo za anasa (luxury) na fahari lazima wote waonekane wenye moyo mwepesi na wenye furaha. Mifadhaiko isiweke kivuli chake juu ya uso wa mtumishi yeyote wa kifalme. Lakini katika nyakati za Nehemia za kupumzika kutoka kibaruni, wakati ambapo alikuwa haonekani machoni pa wanadamu, sala nyingi, maungamo, machozi, yalisikiwa na kushuhudiwa na MUNGU na malaika.— (Prophets and Kings, 628- 630) [Pr 149.2; Maombi Aya ya 95]

Nehemia Alikubali Dhambi Yake Binafsi Katika Maombi Yake— Sio tu kwamba Nehemia alisema kwamba Israeli walikuwa wametenda dhambi. Ila pia alikubali kwa toba kwamba yeye na nyumba ya baba yake walikuwa wamefanya dhambi. “Tumetenda kwa ufisadi dhidi Yako,” asema, akijiweka mwenyewe miongoni mwa wale ambao walikuwa wamemvunjia MUNGU heshima kwa kutosimama kwa imara kwa ajili ya ile Kweli.... [Pr 149.3; Maombi Aya ya 96]

Nehemia alijinyenyekeza mbele za MUNGU, akimpa utukufu unaostahili Jina Lake. Ndivyo pia alivyofanya Danieli huko Babeli. Hebu tujifunze maombi ya watu hawa. Yanatufundisha kwamba tunapaswa kujinyenyekeza, lakini kwamba hatupaswi kamwe kufuta mpaka au mstari kati ya watu wa MUNGU wanaoshika amri na wale ambao hawaheshimu sheria Yake.—(SDA Bible Commentary 3:1136) [Pr 149.4; Maombi Aya ya 97]

Nehemia Aliomba, Akiwa na Uhakika Kwamba MUNGU Angetimiza Ahadi Zake—Imani yake ikishikilia sana ahadi za Bwana, Nehemia aliwasilisha kwenye Kiti cha Rehema cha mbinguni ombi lake kwamba MUNGU angedumisha kazi ya watu Wake wenye kutubu, na kurejesha nguvu zao; na kujenga mahali pao palipokuwa mahame. MUNGU alikuwa mwaminifu kwa Vitisho vyake wakati watu Wake walipojitenga Naye; Alikuwa amewatapanya kote kati ya mataifa, kulingana na Neno Lake. Naye Nehemia alipata katika Ukweli huu uhakikisho kwamba Angekuwa Mwaminifu vile vile katika kutimiza ahadi Zake (kuwarudisha).—(SDA Bible Commentary 3:1136) [Pr 150.1; Maombi Aya ya 98]

Nehemia Alifanya Sala Zake Kuendana na Mahitaji ya Wakati Huo—kumbukumbu ya hali ya Yerusalemu iliamsha huruma ya mfalme bila kuamsha chuki zake. Swali lingine lilitoa fursa ambayo Nehemia alikuwa ameingoja kwa muda mrefu: “Unataka nini? Lakini mtu wa MUNGU hakuthubutu kujibu mpaka alipotaka mwongozo kutoka kwa Aliye juu kuliko Artashasta. Alikuwa na muamana mtakatifu wa kutimiza, ambao ulihitaji msaada kutoka kwa mfalme; na alitambua kwamba mengi yalitegemea juu ya kuwasilisha kwake jambo hilo kwa njia ya kupata kibali chake mfalme na kuomba msaada wake. “Nikaomba,” alisema, “kwa MUNGU wa mbinguni.” Katika sala hiyo fupi Nehemia alisisitiza katika uwepo wa Mfalme wa wafalme na kushinda nguvu inayoweza kugeuza mioyo kama mito ya maji inavyogeuzwa. [Pr 150.2; Maombi Aya ya 99]

Maombi ya Nehemia yaliimarishwa na Kusudi Imara—Kuna hitaji la kuwa na akina Nehemia katika kanisa leo,—sio watu wanaoweza kuomba na kuhubiri tu, bali watu ambao maombi na mahubiri yao yameimarishwa kwa kusudi thabiti na lenye maazimio yenye shauku.—(The Signs of the Times, Desemba 6, 1883) [Pr 150.3; Maombi Aya ya 100]

Kama Nehemia, Tunaweza kuomba Wakati Wowote au Mahali Popote—Kuomba kama Nehemia alivyoomba katika saa yake ya hitaji ni nyenzo ya kumuongoza Mkristo katika mazingira ambapo aina nyingine za maombi zitashindikana Watenda kazi wenye bidii katika safari ya maisha, waliokuwa katika msongamano na kutindikiwa na wasiwasi au fedheha, wanaweza kutuma ombi kwa MUNGU kwa ajili ya mwongozo Wake wa Kiungu/mbingu. Wasafiri baharini na nchi kavu, wanapotishiwa na hatari kubwa, wanaweza kujikabidhi katika ulinzi wa Mbingu. Wakati wa shida ya ghafla au hatari, moyo unaweza kutuma kilio chake cha kuomba msaada kwa Yule ambaye ameahidi kuwasaidia waaminifu Wake, wale wanaoamini, kila wanapomwita. Katika kila jambo, chini ya kila hali, nafsi iliyolemewa na huzuni na masumbufu ya maisha haya, au kushambuliwa vikali na jaribu, inaweza kupata uthibitisho, msaada, na sapoti/utegemezi katika upendo usiokoma na nguvu ya MUNGU anayeshika agano. [Pr 151.1; Maombi Aya ya 101]

Katika wakati huo mfupi wa maombi kwa Mfalme wa wafalme, Nehemia alikusanya ujasiri kumwambia Artashasta kuhusu matamanio yake ya kupewa muda kutoka katika majukumu yake katika nyua za kifalme, naye akaomba mamlaka ya kujenga mahali palipokuwa ukiwa Yerusalemu na kupafanya tena kuwa jiji lenye nguvu na ulinzi. Matokeo muhimu kwa taifa la Kiyahudi yalikita kwenye ombi hili. “Na,” Nehemia atangaza, “mfalme alinipa kibali, kulingana na mkono mwema wa MUNGU wangu ulio juu yangu.” (Prophets and Kings, 631-633) [Pr 151.2; Maombi Aya ya 102]

MUNGU katika majaliwa Yake haturuhusu kuujua mwisho tangu mwanzo; bali anatupa nuru ya Neno Lake ili kutuongoza tunapopita, na anatuagiza kuweka

mawazo yetu kwa Yesu. Popote tulipo, haijalishi kazi tuliyo nayo, mioyo yetu inapaswa kuinuliwa kwa MUNGU katika maombi. Hii ni kuwa na utayarikuomba wakati wowote. Hatuhitaji kusubiri hadi tuweze kupiga magoti kabla ya kuomba. Wakati fulani, Nehemia alipofika mbele ya mfalme, mfalme aliuliza ni kwanini alionekana mwenye huzuni, na ni ombi gani aliazimia kumwambia mfalme. Lakini Nehemia hakuthubutu kujibu hapo hapo. Masilahi muhimu yalikuwa hatarini. Hatima ya taifa ilining'inia juu ya mtazamo ambao unapaswa kutengenezwa juu ya akili ya mfalme; naye Nehemia akatuma maombi kwa MUNGU wa Mbinguni, kabla hajathubutu kumjibu mfalme. Matokeo yake ni kwamba alipata yote aliyoomba au hata yale aliyotamani. - (The Signs of the Times, October 20, 1887) [Pr 151.3; Maombi Aya ya 103]

Hakuna wakati au mahali ambapo hapafai kutuma ombi kwa MUNGU. Hakuna kitu kinachoweza kutuzuia kuinua mioyo yetu katika moyo wa maombi ya bidii. Katika umati wa watu mitaani, katikati ya biashara au shuguli, tunaweza kutuma ombi kwa MUNGU na kuomba mwongozo wa MUNGU, kama alivyofanya Nehemia alipotoa ombi lake mbele ya Mfalme Artashasta. Ushirika wa karibu unaweza kupatikana popote tulipo. Tunapaswa kufungua mlango wa moyo kila wakati na mwaliko wetu kwa Yesu kwenda juu ili aje kukaa kama mgeni wa mbinguni katika nafsi zetu (mioyo yetu). [Pr 151.4; Maombi Aya ya 104]

Ingawa tunaweza kuwa na mazingira yenye uchafuzi, ufisadi, na uharibifu karibu nasi, hatuhitaji kuvuta pumzi ya harufu yake, lakini tunaweza kuishi katika hewa safi ya mbinguni. Tunaweza kufunga kila mlango kwa mawazo yasiyofaa na mawazo yasiyo matakatifu kwa kuinua roho mbele ya MUNGU kupitia maombi ya dhati. Wale ambao mioyo yao iko wazi kupokea msaada na baraka za MUNGU watatembea katika angahewa takatifu kuliko ile ya dunia na watakuwa na ushirika wa mara kwa mara na mbingu. —(Steps to Christ, 99). [Pr 152.2; Maombi Aya ya 105]

Nehemia Aliomba kwa Bidii Usiku Wote—Kwa siri na kimya, Nehemia alikamilisha mzunguko wake wa zile kuta. Anatangaza, “Watawala hawakujua nilikokwenda, wala nilikofanya; wala nilikuwa sijawaambia Wayahudi, wala makuhani, wala wakuu, wala viongozi, wala wengine waliofanya kazi hiyo.” Katika uchunguzi huu mchungu hakutaka kuvutia umakini wa marafiki au maadui, msisimko usije ukazushwa, na ripoti kuletwa na kusambaa, jambo ambalo ingeweza kufanya misheni kufeli au au kuzuia, kazi yake. Nehemia alitumia muda uliosalia wa usiku kwa maombi; asubuhi lazima kuwe na jitihada ya bidii ya kuwaamsha na kuwaunganisha watu wa nchi yake waliokata tamaa na waliogawanyika.— (Christian Service, 174) [Pr 152.3; Maombi Aya ya 106]

Mafanikio ya Nehemia Yanaonyesha Nguvu ya Maombi— Katika kazi yao, Ezra na Nehemia walijinyenyekeza mbele ya MUNGU, wakiungama dhambi zao na dhambi za watu wao, na kuomba msamahakana kwamba wao wenyewe ndio

wakosaji. Kwa subira walijitaabisha kufanya kazi, wakisali na kuteseka. Jambo ambalo lilifanya kazi yao kuwa ngumu zaidi lilikuwa sio uadui wa wazi wa watu wa mataifa (wapagani), bali upinzani wa siri wa marafiki wa kujifanya, ambao, kwa kutoa ushawishi wao kwa ajili ya huduma za uovu, waliongeza mara kumi mzigo wa watumishi wa MUNGU. Wasaliti hawa waliwapa adui za Bwana nyenzo za kutumia katika vita vyao juu ya watu Wake. Tamaa zao mbaya na nia yao ya uasi vilikuwa vikipigana daima na matakwa ya MUNGU yaliyo wazi. [Pr 152.4; Maombi Aya ya 107]

Mafanikio yanayoambatana na jitihada za Nehemia yanaonyesha kile ambacho sala, imani, hekima na utendaji wenye msukumo wa bidii unavyoweza kutimiza. Nehemia hakuwa kuhani; hakuwa nabii; hakujiifanya kuwa na cheo cha juu. Alikuwa mwanamatengenezo aliyeinuliwa kwa wakati muhimu. Lilikuwa lengo lake kuwaweka watu wake kuwa waadilifu kwa MUNGU (waweke mambo yao sawa na Mungu). Akisukumwa na kusudi kuu, alipinda/aliweka kila nguvu ya uhai wake ili kutimiza lengo hilo. Uadilifu wa hali ya juu, usiobadilika uliashiria juhudi zake. Alipokutana na uovu na upinzani katika kutenda kile kilicho haki, alichukua msimamo mkali sana kiasi kwamba watu waliamshwa kufanya kazi kwa bidii na ujasiri mpya. Hawakuwa na jinsi isipokuwa kutambua uaminifu wake, uzalendo wake, na upendo wake wa kina kwa MUNGU; na, walipoona hivyo, walikuwa tayari kufuata alikowaongoza.— (Prophets and Kings, 675, 676) [Pr 153.1; Maombi Aya ya 108]

Yohana Mbatizaji

Yohana Alitumia Muda Katika Kutafakari na Kuomba Kujua mapenzi ya MUNGU kwa ajili ya maisha yake—Maisha ya Yohana hayakutumika katika uvivu, uzembe, utawa, au kujitenga kwa ubinafsi. Mara kwa mara alienda kuchangamana na watu; na alikuwa mtazamaji makini mwenye nia ya kujua kile kilichokuwa kiendelea duniani. Akiwa kwenye pumziko lake tulivu nyikani alitazama matukio yalivyokuwa. Akiwa na maono yaliyoangaziwa na Roho wa MUNGU alisoma tabia za wanadamu, ili apate kuelewa jinsi ya kuifikia mioyo yao kwa ujumbe wa mbinguni. Mzigo wa utume wake ulikuwa juu yake. Akiwa peke yake, kwa kutafakari na kusali, alitafuta kujifunga na mshipi wa uimara kwenye nafsi yake kwa ajili ya kazi ya maisha iliyokuwa mbele yake.—(The Desire of Ages, 102) [Pr 153.2; Maombi Aya ya 109]

Maombi Yalimwezesha Yohana Kuwakabili Wafalme wa Dunia—Yohana Mbatizaji katika maisha yake ya jangwani alifundishwa na MUNGU. Alisoma mafunuo ya MUNGU katika asili. Chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu, alisoma hati-kunjo za manabii. Mchana na usiku, Kristo alikuwa somo lake, kutafakari kwake, mpaka akili na moyo na roho vilijaa maono ya utukufu. [Pr 153.3; Maombi Aya ya 110]

Alimtazama Mfalme katika uzuri Wake, na nafsi yake ikapotea (ubinafsi wake

ukaisha). Aliona ukuu wa utakatifu na akajua kwamba anapokuwa peke yake, yeye hana ufanisi na ustahiki. Ulikuwa ni ujumbe wa MUNGU ambao alipaswa kuutangaza. Ilikuwa katika uwezo wa MUNGU na haki Yake kwamba alipaswa kusimama. Alikuwa tayari kwenda kama mjumbe wa Mbinguni, bila kukatishwa tamaa na mwanadamu, kwa maana alikuwa amemtazama MUNGU. Angeweza kusimama bila woga mbele ya wafalme wa kidunia kwa sababu kwa kutetemeka alikuwa ameinama na kusujudu mbele ya Mfalme wa wafalme.— (Testimonies for the Church 8:331, 332) [Pr 154.1; Maombi Aya ya 111]

Petro

MUNGU Alijibu Sala ya Petro ya Kumfufua Dorkasi—Moyo wa mtume huyo uliguswa na huruma alipoona huzuni yao. Kisha, akielekeza kwamba marafiki waliokuwa wakilia watolewe chumbani, alipiga magoti na kusali kwa bidii kwa MUNGU amrudishie Dorkasi uhai na afya. Akaugeukia ule mwili, akasema, Tabitha, inuka. Naye akafumbua macho yake, na alipomwona Petro, akaketi.” Dorkasi alikuwa amefanya utumishi mkubwa kwa kanisa, na MUNGU aliona inafaa kumrudisha kutoka nchi ya adui, ili ustadi wake na nguvu zake zipate kuwa baraka kwa wengine, na pia kwamba kwa udhihirisho huu wa uweza Wake kusudi la Kristo lipate kuimarishwa.— (Matendo ya Mitume, 132) [Pr 154.2; Maombi Aya ya 112]

SURA YA 14

SALA YA KILA SIKU

Ni Muhimu Kama Chakula Chetu cha Kila Siku—Ikiwa tutakuza tabia ambayo MUNGU anaweza kukubali, lazima tutengeneze mazoea sahihi katika maisha yetu ya kidini. Maombi ya kila siku ni muhimu kwa ukuaji wa neema, na hata kwa maisha ya kiroho yenyewe, kama vile chakula cha muda kwa ustawi wa kimwili. Tunapaswa kujizoesha kuinua mawazo kwa MUNGU katika sala. Akili ikitangatanga, lazima tuirudishe; kwa bidii ya kudumu, tabia hatimaye itafanya iwe rahisi. Hatuwezi kujitenga mbali na Kristo hata wakati mmoja tukawa salama. Tunaweza kuwa na uwepo Wake pamoja nasi katika kila hatua, lakini kwa kuzingatia tu masharti ambayo Yeye mwenyewe ameweka. —(Messages to Young People, 115.114, 115) [Pr 155.1; Maombi Aya ya 1]

Hitaji letu la sala ya kila siku- Wote wanaokuja kwa Kristo leo wanapaswa

kukumbuka kuwa haki na sifa yake ni uvumba unaochanganyika na maombi ya wale wanaotubu dhambi zao na kupokea msamaha na rehema na neema. Hitaji letu la maombezi ya Kristo ni la mara kwa mara. Siku baada ya siku, asubuhi na jioni, moyo mnyenyekevu unahitaji kutoa maombi ambayo yatarudishiwa majibu ya neema na amani na furaha. “Basi kupitia Yeye na tutoe dhabihu ya sifa kwa MUNGU mara kwa mara, yaani, tunda la midomo yetu itoe shukrani kwa Jina Lake Lakini msisahau kutenda mema na kuwasiliana; kwa maana dhabihu za namna hii MUNGU hupendezwa nazo” (SDA Bible Commentary 6:1078) [Pr 155.2; Maombi Aya ya 2]

Anza Siku Yako Kwa Maombi—Ni upendeleo kwetu kufungua mioyo yetu, na kuruhusu mwanga wa jua wa uwepo wa Kristo uingie. Kaka yangu, dada yangu, ikabili nuru. Njoo katika mawasiliano halisi ya kibinafsi na Kristo, ili uweze kuwa na ushawishi wa kuinua na kuleta uamsho. Acha imani yako iwe imara na safi na thabiti. Hebu shukrani kwa MUNGU ijaze mioyo yenu. Unapoamka asubuhi, piga magoti kando ya kitanda chako, na umwombe MUNGU akupe nguvu ya kutimiza majukumu ya siku, na kukabiliana na majaribu yake. Mwambie akusaidie kuleta katika kazi yako utamu na uzuri wa tabia ya Kristo. Muombe akusaidie kusema maneno ambayo yatawapatia wale wanaokuzunguka tumaini na ujasiri, na kukusogeza karibu na Mwokozi. (Sons and Daughters of God, 199)- [Pr156.1; Maombi Aya ya 3]

Kila asubuhi chukua muda kuanza kazi zako kwa ombi. Usifikirie kuwa huku ni kupoteza muda; kwani ni muda ambao utaishi kwa nyakati za milele. Kwa njia hii mafanikio na ushindi wa kiroho utaletwa. Mwili wako utajibu mguso wa mkono wa Mwalimu Mkuu. Hakika kuomba baraka ya MUNGU kunastahili wakati wetu, na kazi haiwezi kufanywa kwa usahihi isipokuwa ina mwanzo sahihi.—(Testimonies for the Church 7:194) [Pr 156.2; Maombi Aya ya 4]

Ndugu na dada zangu, wazee na vijana, mnapokuwa na saa moja ya kupumzika na burudani (mnapokuwa hamna la kufanya), fungueni Biblia na mhifadhi akili zenu na Kweli zake wa thamani. Unapojishughulisha na kazi, linda akili, iache akili iendeleo kukaa kwa MUNGU, ongea kidogo, na tafakari zaidi. Kumbuka: "Kila neno lisilofaa ambalo watu watazungumza, watatoa hesabu yake siku ya hukumu." Chunga maneno yako; hii itafunga mlango dhidi ya adui wa roho. Hebu uingie katika siku yako mpya kwa maombi; fanya kazi kama upo machoni pa MUNGU. Malaika Wake huwa karibu nawe kila wakati, wakiandika maneno yako, mwenendo wako, na namna ya utendaji kazi wako. Unapoacha ushauri mzuri na kuchagua kushirikiana na wale ambao una sababu ya kuwashuku kwamba hawana mwelekeo wa mambo ya kidini/kiroho, ingawa wanadai kuwa Wakristo, hivi karibuni utakuwa kama wao. Unajiweka mwenyewe katika barabara ya majaribu, kwenye uwanja wa vita wa Shetani, na, isipokuwa umelindwa kila mara, utashindwa na hila zake.—(Testimonies for the Church 4:588, 589) [Pr

156.3; Maombi Aya ya 5]

Mwendee Bwana kila siku kwa ajili ya mafundisho na mwongozo; Mtegemee MUNGU kwa nuru na maarifa. Omba kwa ajili ya mafundisho haya na mwanga huu, hadi upate. Haitakufaa wewe kuomba, kisha ukasahau jambo uliloliombea. Weka akili yako juu ya maombi yako. Unaweza kufanya hivyo wakati unafanya kazi kwa mikono yako. Unaweza kusema, Bwana, naamini; kwa moyo wangu wote naamini Acha nguvu za Roho Mtakatifu zije juu yangu. — (Fundamentals of Christian Education, 531) [Pr 157.1; Maombi Aya ya 6]

Katika kumfuata Kristo, ukimtaazama Yeye ambaye Ndiye Mwanzilishi na Mkamilishaji wa imani yako, utahisi kuwa unafanya kazi chini ya jicho Lake, kwamba unashawishiwa na uwepo Wake, na kwamba Anajua nia zako. Katika kila hatua utauliza kwa unyenyekevu: Je! Hii itampendeza Yesu? Je! Itamtukuza MUNGU? Asubuhi na jioni sala zako za dhati zinapaswa kupaa kwa MUNGU kwa ajili ya baraka na mwongozo Wake. Maombi ya Kweli hujitegemeza kwa Muweza na hutupatia ushindi. Akiwa amepiga magoti yake Mkristo hupata nguvu za kushinda vishawishi.— Yoh.(Testimonies for the Church 4:615) [Pr 157.2; Maombi Aya ya 7]

Tenga muda kila siku kwa ajili ya maombi — Wale ambao watavaa silaha zote za MUNGU na kutenga muda kila siku kwa ajili ya kutafakari na kufanya maombi na kusoma Maandiko wataunganishwa na mbingu na watakuwa na mvuto uokoao, na unaobadilisha kwa wale wanaowazunguka. Mawazo makuu, matamania bora, ufahamu dhahiri kuhusu ile Kweli na wajibu kwa MUNGU, haya yote yatakuwa yao. Watakuwa wana shauku ya kuwa na usafi wa moyo, kuwa na nuru, kuwa na upendo, na kuwa na neema zote zitokazo mbinguni. Maombi yao ya bidii kabisa yatapenya ndani ya pazia. Kundi hili litakuwa na ujasiri mtakatifu mbele ya Yeye Asiye na kikomo. Watahisi kuwa nuru na utukufu wa mbinguni upo kwa ajili yao, na watasafishwa, watainuliwa, wataboreshana kuadilishwa na uhusiano huu wa karibu na MUNGU. Huo ndio upendeleo walionao Wakristo wa kweli. [Pr 157.3; Maombi Aya ya 8]

Kutafakari nadharia tu bila vitendo halisi haitoshi; shughuli au utendaji mwingi pia hautoshi; vyote viwili ni muhimu kwa uundaji wa tabia ya Kikristo. Nguvu inayopatikana katika maombi ya dhati, na ya siri, hututayarisha kustahimili vivutio/vishawishi vibaya kwenye jumuiya. Na bado hatupaswi kujitenga na ulimwengu, kwani uzoefu wetu wa Kikristo unapaswa kuwa nuru ya ulimwengu. Jamii ya wasioamini haitatudhuru ikiwa tutachangamana nao kwa kusudi la kuwaunganisha na Mungu na kuwa na nguvu za kutosha kiroho kuhimili ushawishi wao. - (Testimonies for the Church 5:112, 113) [Pr 158.1; Maombi Aya ya 9]

Matokeo Ya Maombi ya kila siku -Roho inayomgeukia MUNGU kwa ajili ya kupata nguvu, msaada, uwezo, kwa maombi ya dhati na bidii kila siku, itakuwa na

matamano bora, uelewa dhahiri wa ile Kweli na wajibu, malengo yaliyo ya juu katika utendaji wa kazi, na kudumu kuwa na njaa na kiu ya haki.—(God's Amazing Grace 317) [Pr 25.4; Maombi Aya ya 10]

Kwa kudumisha uhusiano na MUNGU, tutawezeshwa kusambaza kwa wengine, kupitia ushirika wetu nao, nuru, amani, utulivu, unaotawala mioyoni mwetu. Nguvu inayopatikana katika sala kwa MUNGU, ikiunganishwa na jitihada ya kudumu katika kuzoeza akili katika kufikiria na kutenda, hutayarisha mtu kwa ajili ya majukumu ya kila siku na kuiweka roho katika amani chini ya hali zote. [Pr 158.2; Maombi Aya ya 11]

Tukimkaribia Mungu, ataweka neno kinywani mwetu kusema kwa niaba yake, hata sifa kwa jina lake. Atatufundisha mkazo kutoka katika wimbo wa malaika, hata shukrani kwa Baba yetu wa mbinguni. Katika kila tendo la maisha, nuru na upendo wa Mwokozi anayeishi ndani vitafichuliwa. Shida za nje haziwezi kufikia maisha ambayo yanaishi kwa imani katika Mwana wa MUNGU.—(Thoughts from the Mount of Blessing, 85) [Pr 158.3; Maombi Aya ya 12]

Maombi yanahitajika Kila Siku Ili Kumpinga (kumsukuma) Shetani — Utakaso sio kazi ya nukta moja, saa moja au siku moja. Ni ukuaji endelevu katika neema. Hatujui hata siku moja mzozo wetu utakuwa na nguvu kiasi gani siku inayofuata. Shetani anaishi, na anafanya kazi kwa bidii, na kila siku tunahitaji kumlilia MUNGU kwa dhati ili kupata msaada na nguvu za kumpinga. Maadamu Shetani anatawala tutapaswa kutiisha ubinafsi daima, tutakuwa na usumbufu na mashambulizi ya kukabili, na hakuna mahali pa kusimama, hakuna hatua ambayo tunaweza kuifika na kusema tumeiwezea kikamilifu. — (Testimonies for the Church 1:340) [Pr 158.4; Maombi Aya ya 13]

Maombi ya Kila Siku yajumuishe Mahitaji ya Kimwili na Kiroho— Maombi ya mkate wa kila siku yanajumuisha sio tu chakula cha kutegemeza mwili, lakini mkate wa kiroho ambao utarutubisha na kulisha roho hata kwenye uzima wa milele. Yesu anatuagiza, "Msikifanyie kazi chakula chenye kuharibika, bali kile kidumucho hata uzima wa milele." Yohana 6:27. Anasema, "Mimi Ndimi mkate hai uliyoshuka kutoka mbinguni. Mtu yeyote akila mkate Huu, ataishi milele." Mstari wa 51. Mwokozi wetu ni mkate wa uzima, na ni kwa kutazama upendo Wake, kwa kuupokea rohoni, ndio tunakula mkate ulioshuka kutoka mbinguni. [Pr 159.1; Maombi Aya ya 14]

Tunampokea Kristo kupitia Neno Lake, na Roho Mtakatifu anatolewa ili kulifungua Neno la MUNGU katika ufahamu wetu, na kuleta Kweli Zake mioyoni mwetu. Tunapaswa kuomba siku baada ya siku kwamba tunaposoma Neno lake, MUNGU atume Roho Wake ili kutufunulia Ukweli ambao utaimarisha roho zetu kwa hitaji la siku. [Pr 159.2; Maombi Aya ya 15]

Katika kutufundisha kuomba kila siku kile tunachohitaji— baraka za kimwili na za kiroho—MUNGU ana kusudi la kutimiza kwa manufaa yetu. Angependa

tutambue utegemezi wetu juu ya utunzaji Wake wa kila mara, kwa kuwa anatafuta kutuvuta katika ushirika na Yeye Mwenyewe. Katika mawasiliano na ushirika huu na Kristo, kwa njia ya maombi na kujifunza zile Kweli kuu na za thamani za Neno Lake, kama roho zenye njaa tualishwa; kama wale walio na kiu, tutaburudishwa kwenye chemchemi ya uzima.—(Thoughts from the Mount of Blessing, 112, 113) [Pr 159.3; Maombi Aya ya 16]

Kama Wakristo wa awali, Tunahitaji Kuomba Kila Siku kwa Ajili ya Roho Mtakatifu—Wale ambao katika Pentekoste walivishwa nguvu kutoka juu, hawakuwekwa huru dhidi ya mitihani na majaribu siku za mbeleni. Waliposhuhudia Ukweli na haki walishambuliwa mara kwa mara na adui wa Kweli zote, ambaye alitaka kuwaibia uzoefu wao wa Kikristo. Walilazimika kujitahidi kwa nguvu zao zote walizopewa na MUNGU kufikia kiwango cha mfano wa wanaume na wanawake walio katika Kristo Yesu. Kila siku waliomba msaada mpya wa neema, ili waweze kufikia juu na juu zaidi kuelekea ukamilifu. Chini ya utendaji kazi wa Roho Mtakatifu hata wale walio dhaifu, kwa kuizoeza imani yao kwa MUNGU, walijifunza kuboresha nguvu walizokabidhiwa na kutakaswa, kusafishwa, na kuboreshwa. Kwa unyenyekevu walijitiisha chini ya ushawishi wa Roho Mtakatifu, wakapokea utimilifu wa Uungu na wakaandaliwa kwa mfano wa MUNGU. - (The Acts of the Apostles, 49, 50) [Pr 159.4; Maombi Aya ya 17]

Kupita kwa wakati hakujaleta mabadiliko katika ahadi ya Kristo alipokuwa akiondoka ya kumtuma Roho Mtakatifu kama mwakilishi Wake. Si kwa sababu ya kizuizi chochote kwa upande wa MUNGU kwamba utajiri wa neema yake havitiririki duniani kwa wanadamu. Ikiwa utimilifu wa ahadi hauonekani jinsi unavyoweza kuonekana, ni kwa sababu ahadi haithaminiwi kama inavyopaswa kuwa. Kama wote wangekubali, wote wangejazwa na Roho. Popote pale ambapo hitaji la Roho Mtakatifu ni jambo linalo fikiriwa kwa udogo sana, panaonekana kuwa na ukame wa kiroho, giza la kiroho, mporomoko wa kiroho na kifo. Wakati mambo madogo yanachukua umakini, na nguvu ya kiungu/Bwana ambayo ni muhimu kwa ukuaji na ustawi wa kanisa, na ambayo italeta baraka zingine zote kwenye treni yake, inakosekana, ingawa hutolewa kwa wingi Wake usio na kipimo. [Pr 160.1; Maombi Aya ya 18]

Kwa kuwa hii ndiyo njia ambayo kwayo tunapaswa kupokea nguvu, kwa nini hatuna njaa na kiu ya karama ya Roho? Kwa nini hatuizungumzii, hatuiombei, na kuhubiri kuhusu hiyo? Bwana Yupo tayari sana kumtoa Roho Mtakatifu kwa wale wanaomtumikia zaidi ya wazazi wavyokuwa na shauku ya kutoa zawadi bora kwa watoto wao. Kila mfanyakazi anapaswa kutoa ombi lake kwa MUNGU kwa ubatizo wa kila siku wa Roho. Vikundi vya watendakazi Wakristo vinapaswa kukusanyika ili kuomba msaada wa kipekee, kwa ajili ya hekima ya mbinguni, ili wajue jinsi ya kupanga na kutekeleza mikakati kwa hekima. Hasa wanapaswa kuomba ili MUNGU awabatize mabalozi Wake waliochaguliwa katika fildi za misheni kwa kipimo kikubwa cha Roho Wake. Uwepo wa Roho pamoja na

watenda kazi wa MUNGU utatoa nguvu juu ya utangazaji wa Ukweli ambao hakuna heshima au utukufu wote wa ulimwengu ungeweza kutoa.—(The Acts of the Apostles , 49-51) [Pr 160.2; Maombi Aya ya 19]

Ombea Neema kwa Mahitaji ya Kila Siku—Ukweli wa MUNGU uliopokelewa moyoni unaweza kukufanya uwe na hekima hata kufikia wokovu. Kwa kuiamini na kuitii utapokea neema ya kutosha kwa ajili ya majukumu, mitihani na majaribu ya leo. Hautaji Neema ya kesho. Unapaswa kuhisi kuwa unahusika na leo tu. Kushinda kwa leo; kujikana kwa leo; kuomba na kukesha kwa leo; kupata ushindi katika MUNGU leo. Hali zetu na mazingira yetu, mabadiliko ya kila siku yanayotuzunguka, na Neno lililoandikwa la MUNGU ambalo hutambua na kuthibitisha mambo yote hayo vinatosha kutufundisha wajibu wetu na kile ambacho tunapaswa kufanya, siku baada ya siku. Badala ya kuitesa akili yako kukimbia katika njia ya mawazo ambayo hutapata faida yoyote nayo, wewe unapaswa kuwa unachunguza Maandiko kila siku na kufanya kazi zile za maisha ya kila siku ambazo sasa zinaweza kuonekana ni usumbufu tupu, lakini ni zile ambazo lazima zifanywe na mtu fulani.—(Testimonies for the Church 3:333) [Pr 160.3; Maombi Aya ya 20]

Omba kila siku kwa ajili ya Uelewa wa Biblia — Wale wanaodai kumwamini Yesu, daima wanapaswa kusonga mbele kwenye nuru kwa bidii. Wanapaswa kuomba kila siku ili nuru ya Roho Mtakatifu iangaze kwenye kurasa za kitabu kitakatifu, ili waweze kuwezesha kuelewa mambo ya Roho wa MUNGU. - (Fundamentals of Christian Education, 188, 189) [Pr 161.1; Maombi Aya ya 21]

Omba Kila Siku kwa ajili ya Baraka Inayoletwa na Sabato— Wote wanaoichukulia Sabato kama ishara kati yao na MUNGU, wakionyesha kwamba Yeye Ndiye MUNGU anayewatakasa, watawakilisha kanuni za serikali Yake. Wataleta katika utendaji wao wa kila siku sheria za ufalme Wake. Itakuwa ombi lao la kila siku kwamba utakaso wa Sabato uwe juu yao. Kila siku watakuwa na ushirika wa Kristo na wataonyesha ukamilifu wa tabia Yake. Kila siku nuru yao itawaangazia wengine kwa matendo mema.— (Testimonies for the Church 6:353) [Pr 161.2; Maombi Aya ya 22]

Ombi la kila siku la Mzazi—Fanya kazi yako iwe ya kupendeza kwa nyimbo za sifa. Ikiwa ungependa kuwa na rekodi safi katika vitabu vya mbinguni, usikasirike wala kukemea. Acha sala yako ya kila siku iwe, "Bwana, nifundishe kutenda vyema. Nifundishe jinsi ya kufanya kazi bora. Nipe nguvu na uchangamfu." ... Mlete Kristo katika yote unayoyafanya. Ndipo maisha yenu yatajazwa na mwangaza na shukraniHebu na tujitahidi, tukisonga mbele kwa uchangamfu katika utumishi wa Bwana, mioyo yetu ikiwa imesheheni furaha Yake.—(Child Guidance, 148) [Pr 161.3; Maombi Aya ya 23]

Vijana waombe Kila Siku kwa ajili ya Hekima na Neema — Majaribu na ufukara ambao vijana wengi wanalalamikia, Kristo alivivumilia bila kunung'unika. Na

nidhamu hii ndiyo ule uzoefu ambao vijana wanauhitaji, na ambao utawapa uthabiti katika tabia zao, na kuwafanya wawe kama Kristo, wenye nguvu katika roho ya kupinga majaribu. Hawataweza, ikiwa watajitenga na ushawishi wa wale ambao watawapotosha na kuharibu maadili yao, kushindwa na hila za Shetani. Kupitia maombi ya kila siku kwa MUNGU, watakuwa na hekima na neema kutoka Kwake ya kubeba migogoro na uhalisia mkali wa maisha, na kuwa washindi. Uadilifu na utulivu wa akili unaweza kutunzwa tu kwa kukesha na kuomba. Maisha ya Kristo yalikuwa kielelezo cha nguvu ya kudumu, ambacho hakikuruhusiwa kudhoofishwa na lawama, dhihaka, ufukara au shida. [Pr 162.1; Maombi Aya ya 24]

Ndivyo inavyopaswa kuwa kwa vijana. Ikiwa Majaribu yataongezeka juu yao, wanaweza kujua kwamba MUNGU anajaribu na kudhihirisha uaminifu wao. Na ni katika kiwango hicho tu ambacho wanadumisha uadilifu wao wa tabia katika mazingira ya kukatishwa tamaa, ndipo uimara, ujasiri, uthabiti, na uwezo wao wa kustahimili utakapongezeka, nao watakuwa na nguvu katika roho.—(Messages to Young People, 80) [Pr 162.2; Maombi Aya ya 25]

Haja ya Mwalimu Kusali Kila Siku—Kila mwalimu anapaswa kupokea kila siku mafundisho kutoka kwa Kristo na anapaswa kufanya kazi daima chini ya uongozi Wake. Haiwezekani kwake kuelewa vizuri au kufanya kazi yake ipasavyo isipokuwa anakuwa na Mungu katika maombi mengi. Ni kwa msaada wa Bwana tu, pamoja na unyofu wa moyo, na juhudi katika kujikana, ndipo anaweza kutumaini kufanya kazi yake kwa busara na vizuri zaidi. [Pr 162.3; Maombi Aya ya 26]

Mwalimu asipotambua hitaji la maombi na kuunyenyekeza moyo wake mbele za MUNGU, atapoteza kiini hasa cha elimu. Anapaswa kujua jinsi ya kuomba na ni lugha gani aitumie katika maombi. “Mimi ni Mzabibu,” Yesu alisema, “ninyi ni matawi; akaaye ndani Yangu Nami ndani yake, huyo atazaa matunda mengi; maana pasipo Mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote.” Yohana 15: 5 Mwalimu anapaswa kuacha matunda ya imani yaonekane katika maombi yake. Anapaswa kujifunza jinsi ya kuja mbele za Bwana na kumsihi Yeye kwa sala mpaka apate uhakikisho kwamba maombi yake yamesikiwa.—(Counsels to Parents, Teachers, and Students, 231) [Pr 162.4; Maombi Aya ya 27]

Katika Nyakati za Agano la Kale, Waisraeli Waliomba Kila Siku— kadiri makuhani walipoingia asubuhi na jioni makuhani mle katika Patakatifu wakati wa uvumba, dhabihu ya kila siku ilikuwa tayari kutolewa juu ya madhabahu katika ua wa nje. Huu ulikuwa wakati wa kupendeza sana kwa washiriki waliokusanyika mahali pa kuabudia. Kabla ya kuingia katika uwepo wa MUNGU kupitia huduma ya kuhani, walipaswa kuichunguza mioyo yao kwa dhati na kukiri dhambi zao. Waliungana katika sala ya kimya, na nyuso zao zikielekea mahali Patakatifu. Hivyo maombi yao yalipanda juu pamoja na wingu la uvumba, imani yao ikiwa imeshikilia stahiki za Mwokozi aliyeahidiwa ambaye aliwakilishwa na dhabihu ya

upatanisho. Saa zilizowekwa kwa ajili ya dhabihu ya asubuhi na ya jioni zilizingatiwa kuwa takatifu, na zikaadhimishwa kama muda wa ibada katika taifa lote la Kiyahudi. Na katika nyakati za baadaye Wayahudi walipotawanywa kama mateka katika nchi za mbali, bado katika saa hiyo iliyoamriwa walielekeza nyuso zao kuelekea Yerusalemu na kutoa maombi yao kwa MUNGU wa Israeli. Katika desturi hii Wakristo wana mfano kwa ajili ya sala ya asubuhi na jioni. Ingawa MUNGU hushutumu mzunguko tu wa mapokeo ya sherehe, bila roho ya ibada, Yeye huwatazama kwa furaha sana wale wanaompenda, wakisujudu asubuhi na jioni ili kuomba msamaha wa dhambi zilizotendwa na kuwasilisha maombi yao kwa baraka zinazohitajiwa..—(Patriarchs and Prophets, 353, 354) [Pr 163.1; Maombi Aya ya 28]

Maombi ya Kila Siku Hustawisha na kuboresha Uzoefu Wetu wa Kidini/kiroho—Dini lazima ianze kwa kusafisha na kutakasa moyo, na lazima ipewe lishe kwa maombi ya kila siku.— (Testimonies for the Church 4:535) [Pr 163.2; Maombi Aya ya 29]

Maisha ya Maombi ya Kila Siku Yanahitaji Jitihada dhati— Maisha ya sala na sifa kila siku, maisha ambayo yataangazia njia ya wengine, hayawezi kudumishwa bila juhudi za dhati. Lakini bidii kama hiyo itazaa matunda ya thamani, yatakayobariki sio tu mpokeaji, bali mtoaji pia. Roho ya kufanya kazi bila ubinafsi kwa ajili ya wengine inatoa kina, uthabiti, na uzuri wa tabia kama wa Kristo kwa mhusika na huleta amani na furaha kwa yule aliye nayo. Matarajio yameinuliwa. Hakuna nafasi ya ugoigoi au ubinafsi. Wale walioonyesha neema za Kikristo watakua. Watakuwa na mishipa na misuli ya kiroho, na watakuwa na nguvu ya kufanya kazi kwa MUNGU. Watakuwa na mitazamo wazi ya kiroho, imani thabiti inayoongezeka, na nguvu za kudumu na zinazoshinda katika maombi. Wale ambao wanakesha kwaajili ya kuzilinda roho, ambao hujitolea kikamilifu kwa wokovu wa wakosaji, hakika wanafanya kazi ya wokovu wao wenyewe pia. —(Testimonies for the Church 5:607) Pr 163.3; Maombi Aya ya 30]

Malaika Hurekodi Sala ya Asubuhi—Nyinyi nyote mna ushawishi kwa wema au uovu katika akili na tabia za wengine. Na ushawishi unaoutoa au kushinikiza umeandikwa katika kitabu cha kumbukumbu mbinguni. Malaika anakutembelea na anachukua rekodi ya maneno na matendo yako. Unapoamka asubuhi, Je! Unahisi kutojiwezea kwako na hitaji lako la nguvu kutoka kwa MUNGU? na Je, kwa unyenyekevu, na kwa moyo wako wote unamjulisha Baba yako wa mbinguni matakwa yako? Ikiwa ndivyo, malaika hunakili maombi yako, na ikiwa maombi haya hayajatoka nje ya midomo ya uwongo au hila, basi wakati uko katika hatari ya kufanya makosa bila kujua na kutoa ushawishi ambao utasababisha wengine kutenda uovu, malaika wako mlezi atakuwa kando yako, kukufundisha kilicho bora, kukuchagulia maneno ili uyatumie, na kuathiri matendo yako. [Pr 164.1; Maombi Aya ya 31]

Ikiwa huhisi kwamba uko katika hatari yoyote, na ikiwa hautoi sala yoyote ya usaidizi wa nguvu za kupinga majaribu, utakuwa na uhakika wa kupotoka; Kupuuza kwako wajibu kutarekodiwa katika kitabu cha MUNGU mbinguni, nawe utaonekana kuwa umepungua katika siku ile ya hukumu.—(Testimonies for the Church 3:363, 364) [Pr 164.2; Maombi Aya ya 32]

Mazoea ya Maombi ya Kila Siku hayapaswi Kufuatwa Kiholela (bila mpangilio au kanuni) - Ibada ya Familia haipaswi kuongozwa na matukio au hali ya hewa. Haupaswi kuomba hapa na pale, kulingana na matukio fulani, na kisha wakati una kazi kubwa ya siku ya kufanya, unaacha kuomba. Kwa kufanya hivi unawaongoza watoto wako kuona kama maombi hayana matokeo yoyote maalum. Maombi yana maana kubwa sana kwa watoto wa MUNGU, na utoaji wa shukrani unapaswa kuja mbele za MUNGU asubuhi na jioni. Anasema mwandishi wa Zaburi "Njoni, tumwimbie Bwana, tumfanyie shangwe mwamba wa wokovu wetu. Tuje mbele Zake kwa shukrani, na tumfanyie shangwe kwa Zaburi. [Pr 164.3; Maombi Aya ya 33]

Akina baba na akina mama, hata kama unafanya biashara yako, usishindwe kukusanya familia yako karibu na madhabahu ya MUNGU. Omba ulinzi wa malaika watakatifu nyumbani mwako. Kumbuka kwamba wapendwa wako wanakabiliwa na vishawishi. [Pr 165.1; Maombi Aya ya 34]

Katika jitihada zetu za kuwafariji na kuwafurahisha wageni, hebu tusipuuze wajibu wetu kwa MUNGU. Saa ya maombi haipaswi kupuuzwa kwa kuzingatia jambo au mtu yeyote. Msizungumze na kujifurahisha wenyewe hadi mjichoshe na kuwa hoi kabisa kufurahia msimu wa ibada. Kufanya hivi ni kumtolea MUNGU sadaka iliyo kilema. Katika Saa ya mapema ya jioni, tunapoweza kusali bila haraka na kwa uwazi wa kuelewa mambo ubongoni mwetu vyema, tunapaswa kutoa dua zetu na kupaza sauti zetu kwa furaha na sifa ya shukrani. [Pr 165.2; Maombi Aya ya 35]

Hebu wale wote wanaowatembelea Wakristo waone kwamba saa ya maombi ni ya thamani zaidi, takatifu zaidi, na ya furaha zaidi ya siku. Misimu hii ya ibada huongeza ushawishi ulio bora, safi, na wenye kuyaelekeza mawazo juu mbinguni kwa wale wote wanaoshiriki. Huleta amani na pumziko la shukrani kwa roho .— (Child Guidance, 520, 521) [Pr 165.3; Maombi Aya ya 36]

Maombi ya Kila Siku ya Kupaa kwa MUNGU kama Uvumba Mtamu—Maisha ya Abrahamu, rafiki ya MUNGU, yalikuwa maisha ya maombi. Kila mahali alipopiga hema lake, karibu na nalo ilijengwa madhabahu, ambayo juu yake ilitolewa sadaka ya asubuhi na ya jioni. Wakati hema lake lilipoondolewa, madhabahu ilibaki. Na Mkanaani anarandaranda huko, alipofika kwenye madhabahu hiyo, alijua ni nani aliyekuwepo hapo. Nate alipopiga hema lake alitengeneza madhabahu na kumwabudu MUNGU aliye hai. [Pr 165.4; Maombi Aya ya 37]

Kwa hivyo nyumba za Wakristo zinapaswa kuwa nuru ulimwenguni. Kutoka

kwazo, asubuhi na jioni, sala inapaswa kupaa kwa MUNGU kama uvumba mtamu. Na kama umande wa asubuhi, rehema Zake na baraka zitashuka juu ya waombaji. [Pr 165.5; Maombi Aya ya 38]

Enyi akina baba na akina mama, kila asubuhi na jioni wakusanyeni watoto wenu karibu nanyi, na kwa dua ya unyenyekevu inueni moyo kwa MUNGU kwa ajili ya msaada. Wapendwa wenu wanakabiliwa na majaribu. Kero za kila siku zinasonga njia ya vijana na wazee. Wale ambao wanahitaji kuishi maisha ya uvumilivu, ya upendo, na uchangamfu lazima waombe. Ni kwa kupokea msaada wa kila wakati kutoka kwa MUNGU tunaweza kupata ushindi juu ya nafsi yetu. [Pr 166.1; Maombi Aya ya 39]

Kila asubuhi jiweke wakfu kwa MUNGU na watoto wako kwa siku hiyo. Usifanye hesabu kwa miezi au miaka; hiyo si yako. Umpewa siku moja fupi. Kana kwamba ndiyo mwisho wako duniani, fanya kazi kwa Mwalimu wakati wa saa zake. Weka mipango yako yote mbele za MUNGU, itekelezwe au kutolewa, kama vile uelekezaji Wake utakavyoonyesha. Kubali mipango Yake badala ya mipango yako mwenyewe, ingawa kukubali kwake kunahitaji kuachwa kwa miradi inayopendwa. Hivyo maisha yatafinyangwa zaidi na zaidi kufuatana na mfano wa kimungu; "Na amani ya MUNGU, ipitayo akili zote, itahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu." Wafilipi 4:7 .—(Testimonies for the Church 7:44) [Pr 166.2; Maombi Aya ya 40]

Mambo ya Kuombea Kila Siku—Tunapaswa kulitazama kila jukumu kuwa takatifu kwasababu ni sehemu ya utumishi wa Mungu, hata jukumu hilo liwe la unyenyekevu wa kiasi gani. Ombi letu la kila siku linapaswa kuwa , "Bwana, nisaidie kufanya vizuri kwa uwezo wangu wote. Nifundishe jinsi ya kufanya kazi bora. Nipe nguvu na uchangamfu. Nisaidie kuleta katika huduma yangu huduma ya upendo ya Mwokozi." (The Ministry of Healing, 474) [Pr 166.3; Maombi Aya ya 41]

Jiweke wakfu kwa MUNGU asubuhi; fanya hii iwe kazi yako ya kwanza kabisa. Ombi lako liwe, "Nitwae, Ee Bwana, niwe Wako kabisa. Ninaweka mipango yangu yote miguuni pako. Nitumie leo katika huduma Yako. Kaa nami, na kazi yangu yote ifanyike ndani Yako." Hili ni mada/suala la kila siku. Kila asubuhi jiweke wakfu kwa Mungu kwa ajili ya siku hiyo. Mkabidhi Yeye mipango yako yote, ili itekelezwe au isitelekezwe kulingana na atakavyoongoza. Kwa hivyo siku baada ya siku unayakabidhi maisha yako mikononi Mwake Mungu, na hivyo maisha yako yataundwa/yatafinyangwa zaidi na zaidi kufanana na maisha ya Kristo.—(Steps to Christ, 70) [Pr 166.4; Maombi Aya ya 42]

SURA YA 15

MFANO WA YESU KATIKA MAOMBI

Fuata Kielelezo cha Yesu kwa Kuanza Siku kwa Sala—Ilikuwa katika saa za sala ya peke yake ndipo Yesu katika maisha Yake duniani alipata hekima na nguvu. Hebu vijana wafuate mfano Wake katika kutafuta alfajiri na jua lizamapo magharibi, muda wa utulivu kwaajili ya ushirika na Baba yao aliye mbinguni. Na pia wainue mioyo yao kwa MUNGU siku nzima. Katika kila hatua ya njia zetu anasema, 'Kwa maana Mimi, Bwana, MUNGU wako, nitakushika mkono wako wa kuume, Usiogope; nitakusaidia.. Isaya 41:13. Laiti watoto wetu wanguweza kujifunza masomo haya katika miaka yao ya awali, ni upya na nguvu, furaha na utamu wa jinsi gani, ambao ungeletwa maishani mwao!—(Education, 258, 259) [Pr 167.1; Maombi Aya ya 1]

Maombi ya dhati na yenye bidii ya Yesu yanatofautiana na maombi yetu dhaifu—Kuhusu Kristo inasemwa: “Na akiwa katika uchungu mkubwa aliomba kwa bidii zaidi.” Je ni tofauti iliyoje tukilinganisha maombezi haya ya Mkuu wa mbinguni na maombi yetu dhaifu, yasiyojumuisha moyo, ambayo hutolewa kwa MUNGU. Wengi wanaridhika na huduma ya mdomo, na ni wachache walio na shauku ya dhati, ya bidii, na ya upendo kwa MUNGU. -(Testimonies for the Church 4:534) [Pr 167.2; Maombi Aya ya 2]

Ikiwa Yesu Alihitaji Kuomba Akiwa Duniani, sisi tunapaswa kusali zaidi kwa kiasi gani basi—Wakati Yesu alipokuwa hapa duniani, Aliwafundisha wanafunzi Wake jinsi ya kuomba. Aliwaelekeza kuwasilisha mahitaji yao ya kila siku mbele za MUNGU, na kumtupia/kuitwika mizigo yao yote Kwake. Na uhakikisho aliowapa kwamba maombi yao yatasikilizwa, ni uhakikisho kwetu pia. [Pr 168.1; Maombi Aya ya 3]

Yesu Mwenyewe, alipokuwa akiishimiongoni mwa wanadamu, mara nyingi alikuwa katika maombi. Mwokozi wetu alijitambua kuwa na mahitaji na udhaifu wetu, katika hilo alikuwa muhitaji, mwombaji, akitaka kutoka kwa Baba Yake nguvu mpya, ili aweze kuja kuimarishwa kwa ajili ya jukumu na jaribio. Yeye ni mfano wetu katika mambo yote. Yeye ni ndugu katika udhaifu wetu, “akijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote; lakini kama mtu asiye na dhambi asili yake ilijiepusha na uovu; Alivumilia mapambano na mateso ya nafsi katika ulimwengu wa dhambi. Ubinadamu wake ulifanya maombi kuwa jambo la lazima la muhimu. Alipata faraja na furaha katika ushirika na Baba Yake. Na ikiwa Mwokozi wa wanadamu, Mwana wa MUNGU, alihisi hitaji la maombi, ni kiasi gani watu dhaifu,

wenye dhambi wanapaswa kuhisi ulazima wa sala ya bidii na ya kudumu.—(Steps to Christ, 93, 94) [Pr 168.2; Maombi Aya ya 4]

Kristo alipambana mieleka kwa maombi ya dhati; Alitoa dua Zake kwa Baba Yake kwa kilio kikali/kizito na machozi kwa ajili ya wale ambao kwa ajili ya wokovu wao aliondoka mbinguni na kuja hapa duniani. Sasa ni sahihi kiasi gani, ndio, ni muhimu namna gani kwamba watu wanapaswa kuomba na sio kuzimia(kuzirai)!— (The Review and Herald, Aprili 1, 1890) [Pr 168.3; Maombi Aya ya 5]

Yesu Aliomba Nguvu za kustahimili Majaribu—Wachache watafuata mfano wa Mwokozi wetu kwa maombi ya bidii na ya mara kwa mara kwa MUNGU ili kupata nguvu za kustahimili majaribu, na kuweza kutekeleza majukumu ya kila siku, ya maisha haya. Kristo Ndiye Kapteni wa wokovu wetu, na kwa mateso na dhabihu Yake Mwenyewe, ametoa mfano kwa wafuasi Wake wote, kwamba kukesha kwa maombi na bidii ya kudumu ni vitu muhimu kwa upande wao ikiwa watawakilisha kwa usahihi upendo uliokaa katika kifua Chake kwa ajili ya jamii ya ubinadamu iliyoanguka.—(The Review and Herald, Februari 23, 1886) [Pr 168.4; Maombi Aya ya 6]

Nguvu ya Yesu Ilitoka katika Maombi—Nguvu ya Kristo ilikuwa katika maombi. Alikuwa ameutowa ubinadamu, na akachukua udhaifu wetu na akawa dhambi kwa ajili yetu. Kristo alitoka kwenda kwenye vijisitu/vichaka au milimani huku akijitenga na ulimwengu na mambo mengine yote (alijifungia kutoka kwenye mambo hayo yote ili apate nafasi ya kuomba). Alikuwa peke Yake na Baba Yake. Kwa dhati na bidii kubwa, Alimimina maombi yake, na kuelekeza nguvu zote za roho Yake katika kushikilia mkono wa Yeye Asiye na mwisho/kikomo. Majaribu mapya na makuu yalipokuwa mbele Yake, Yeye alijiondoa taratibu bila ya watu kujua na kuelekea mahali patulivu, kisha akawa peke Yake milimani, na kutumia usiku mzima kwa ajili ya maombi kwa Baba Yake wa Mbinguni. [Pr 169.1; Maombi Aya ya 7]

Kwa kuwa Kristo ni kielelezo chetu katika mambo yote, ikiwa tutaiga mfano Wake kwa kutochoka na kuwa na ari katika maombi, tukiwasilisha maombi kwa MUNGU ili tuweze kuwa na nguvu katika Jina Lake Yeye Ambaye hakuangukia kwenye majaribu ya hila za adui mjanja Shetani, hata sisi hatutashindwa naye mwovu (tutashinda).— (The Youth's Instructor, April 1, 1873.) Katika maisha yaliyoweka wakfu kikamilifu kwa ajili ya kuwatendea wema wengine, Mwokozi aliona ni muhimu kuchepuka kutoka katika njia alipokuwa safarini na kutoka kwenye umati uliomfuata Yeye siku baada ya siku. Ni lazima aachane na maisha ya shughuli zisizokoma kwa muda, aache kushugulika na mahitaji ya mwanadamu, na kisha atafute pumziko na pia ushirika usiovunjika na Baba Yake. Kama Mmoja pamoja nasi, mshiriki wa mahitaji na udhaifu wetu, alikuwa akimtegemea MUNGU kabisa, na katika pahali pa siri pa maombi alitafuta nguvu za Kimungu, ili aende akiwa amejipanga na kuimarishwa kwa ajili ya wajibu na

majaribu. Katika ulimwengu wa dhambi Yesu alivumilia mapambano na mateso ya nafsi. Kwa ushirika na MUNGU angeweza kutua mzigo wa huzuni zilizokuwa zikimpondaponda. Hapa Alipata faraja na furaha. [Pr 169.2; Maombi Aya ya 8]

Katika Kristo kilio cha wanadamu kilimfikia Baba wa huruma isiyo na kikomo. Kama mwanadamu aliomba kiti cha enzi cha MUNGU hadi ubinadamu Wake ulichajiwa (ulipewa nguvu) na umeme wa mbinguni ambao ulifanya mwunganiko wa ubinadamu na Uuungu. Kupitia ushirika wa daima alipokea uzima kutoka kwa MUNGU, ili aweze kuupa ulimwengu uzima. Uzoefu wake unapaswa kuwa wetu wetu. [Pr 169.3; Maombi Aya ya 9]

“Jitengeni ninyi wenyewe,” anaturalika. Ikiwa tutatii Neno Lake, tunapaswa kuwa na nguvu na wenye manufaa zaidi. Wanafunzi wakamtafuta Yesu, wakamwambia yote; na Akawatia moyo na kuwafundisha. Ikiwa leo tutatenga muda kumwendea Yesu na kumwambia mahitaji yetu, hatupaswi kukatishwa tamaa (au hatutadondoshwa).—(The Desire of Ages, 362, 363) [Pr 169.4; Maombi Aya ya 10]

Mtu wa Huzuni anamimina dua Zake kwa kilio kizito na machozi. Anaomba ili apate nguvu za kuvumilia jaribu hilo kwa niaba ya wanadamu. Ni lazima Yeye Mwenyewe apate kumshikilia vizuri Mweza wa yote, kwa kuwa ni kwa jinsi hiyo tu Anaweza kutafakari yajayo. Naye anamimina matamania ya moyo Wake kwa wanafunzi Wake, ili katika saa ya nguvu za giza imani yao isianguke. Umande ni mzito juu ya umbo Lake anaposujudu, lakini Yeye hafikirii kuhusu hili. Vivuli vya usiku vinakusanyika kumzunguka Yeye, lakini Yeye haangalii utusitusi wake (hali ya kizakiza au mawingumawingu).—(The Desire of Ages, 419, 420) [Pr 170.1; Maombi Aya ya 11]

Pale Yesu alipoingia nyikani alifungiwa ndani na utukufu wa Baba. Usikivu Wake wote ukiwa umefyonzwa katika ushirika na MUNGU, aliinuliwa juu ya udhaifu wa kibinadamu. Lakini utukufu uliondoka, na akaachwa apambane na majaribu. Alikuwa akisongwa kila dakika. Asili Yake ya kibinadamu ilisinyaa (ilitaka kuepuka) kutoka katika pambano lililomngoja. Kwa siku arobaini alifunga na kuomba. Akiwa dhaifu na na kukonda kutokana na njaa, akiwa amechoka, na kuchakaa na kudhoofika kwa maumivu ya akili, “uso Wake ulikuwa umeharibika kuliko wanadamu wote, na umbo Lake zaidi ya wanadamu” (Isaya 52:14). Sasa Shetani aliona amepata mwanya. Sasa akafikiri kwamba angeweza kumshinda Kristo.— (Selected Messages 1:227, 228) [Pr 170.2; Maombi Aya ya 12]

Kwa mtenda kazi aliyejiweka wakfu kuna faraja ya ajabu katika kujua kwamba hata Kristo wakati wa maisha Yake duniani alimtafuta Baba Yake kila siku kwa ajili ya ugavi mpya wa neema iliyohitajika; na kutokana na ushirika huu na MUNGU alienda kuwaimarisha na kuwabariki wengine. [Pr 170.2; Maombi Aya ya 13]

Kisha Mwana wa MUNGU aliinama katika maombi kwa Baba yake! Ingawa

Yeye ni Mwana wa MUNGU, Yeye huimarisha imani yake kwa maombi, na kwa ushirika na Mbingu hujikusanyia nguvu za kupinga uovu na kuhudumia mahitaji ya wanadamu. Akiwa ni ndugu mkubwa wa jamii yetu, anajua mahitaji ya wale ambao, wamezingirwa na udhaifu na wanaoishi katika ulimwengu wa dhambi na majaribu, ila bado wanashauku ya kumtumikia.[171] Anajua ya kwamba Mitume anao waona wanafaa kuwatuma ni watu wadhaifu wapotovu. lakini kwa wote wanaojitoa kikamilifu kwa ajili ya utumishi wake anaahidi msaada wa kiungu. Mfano wake mwenyewe ni uhakikisho kwamba dua ya dhati, yenye kudumu kwa MUNGU katika imani—imani inayoongoza kwenye kumtegemea MUNGU kabisa, na kujiweka wakfu bila kujibakiza kwa ajili ya kazi Yake—itafaa kuwaletae wanadamu msaada wa Roho Mtakatifu katika vita dhidi ya dhambi. [Pr 170.3; Maombi Aya ya 14]

Kila mfanyakazi anayefuata mfano wa Kristo atakuwa tayari kupokea na kutumia nguvu ambazo MUNGU ameahidi kwa kanisa lake kwa ajili ya kukomaa kwa mavuno ya dunia. Asubuhi baada ya asubuhi, watangazaji wa injili wanapopiga magoti mbele za Bwana na kufanya upya viapo vyao vya kujiweka wakfu Kwake, Yeye atawapa uwepo wa Roho Wake, pamoja na nguvu zake za kuhuisha, za kutakasa. Wanapoendelea na kazi za siku hiyo, wana uhakika kwamba wakala asiyeonekana wa Roho Mtakatifu huwawezesha kuwa “wafanya kazi pamoja na MUNGU.” 1Wakorintho 3:9.](Gospel Workers, 510, 511) [Pr 171.1; Maombi Aya ya 15]

Maombi Yalimtia Nguvu Yesu kwa Ajili ya Majaribu—Kristo Mwokozi wetu alijaribiwa katika mambo yote kama sisi, lakini hakuwa na dhambi. Alichukua asili ya mwanadamu, tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, na mahitaji Yake yalikuwa mahitaji ya mwanadamu. Alikuwa ana mahitaji ya kimwili yaliyohitaji kutimizwa, uchovu wa mwili uliopaswa kuondolewa. Ilikuwa ni kwa maombi kwa Baba Yake ndipo alipoandaliwa na kuimarishwa kwa ajili ya wajibu na kwa majaribio. Siku baada ya siku Alifuata mzunguko Wake wa wajibu, akitafuta kuokoa roho.... Naye akakesha usiku kucha akiomba kwa ajili ya wale waliojaribiwa [Pr 171.2; Maombi Aya ya 16]

Majira ya usiku ya maombi ambayo Mwokozi alitumia mlimani au jangwani yalikuwa muhimu kumtayarisha Yeye kwa ajili ya mitihani ambayo ilikuwa lazima akutane nayo katika siku zijazo. Alihisi hitaji la kuburudishwa na kutiwa nguvu rohoni na mwilini, ili aweze kukabiliana na majaribu ya Shetani; na wale wanaojitahidi kuishi maisha Yake watahisi hitaji hilo hilo.— (Maranatha, 85) [Pr 171.3; Maombi Aya ya 17]

Wakati Yerusalemu ikiwa imenyamaza kimya, na wanafunzi wakiwa wamerudi nyumbani kwao ili kupata burudisho katika usingizi ili kuweza kufanywa upya asubuhi, Yesu hakulala. Maombi yake ya kimbingu yalikuwa yakipanda kwa Baba Yake kwa ajili ya wanafunzi Wake, ili waweze kuepukana na ushawishi mbaya ambao wangekutana nao kila siku katika dunia, na ili nafsi Yake Mwenyewe

iweze kuimarishwa na kutayarishwa kwa ajili ya kazi na majaribu ya siku inayokuja.—(The Review and Herald, August 17, 1886) [Pr 171.4; Maombi Aya ya 18]

Maombi Yalimpa nguvu mpya Yesu—Siku Zake zilipita kwenye huduma kwa umati uliomsonga, na katika kufunua hila za marabi za usaliti, na kazi hii isiyokoma mara nyingi ilimwacha akiwa amechoka sana hata mama Yake, ndugu Zake, na hata wanafunzi Wake, waliogopa kwamba maisha Yake yangetolewa kafara. Lakini aliporudi kutoka katika saa za maombi zilizotamatisha siku Yake yenye taabu, mwonekano wa amani juu ya uso Wake uliweka alama usoni Mwake, hisia ya kuburudishwa ambayo ilionekana kutawala uwepo Wake. Ilikuwa ni kutoka katika saa zilizotumiwa na MUNGU kwamba Yeye alitoka, asubuhi baada ya asubuhi, kuleta nuru ya mbinguni kwa wanadamu.—(Thoughts from the Mount of Blessing, 102) [Pr 172.1; Maombi Aya ya 19]

Maombi Yalidumisha Maisha ya Kiroho ya Yesu—Haikuwa msalabani tu ambapo Kristo hakujitoa mhanga Mwenyewe kwa ajili ya wanadamu. Alipokuwa “akizunguka huku na huko akitenda mema” (Matendo 10:38), uzoefu wa kila siku ulikuwa mmiminiko wa maisha Yake. Kwa njia moja tu maisha kama hayo yangeweza kudumishwa. Yesu aliishi kwa kumtegemea MUNGU na kuwa na ushirika Naye. Mahali pa siri Pake Yeye Aliye juu, chini ya uvuli Wake Mwenyezi, watu huenda huko hapa na pale (mara zingine) na kutulia huko kwa msimu kwa muda, na matokeo yake yanadhihirika kwa matendo bora na mema. kisha imani yao inashindwa, ushirika unakatizwa, na kazi ya maisha kuharibiwa. Lakini maisha ya Yesu yalikuwa ni maisha ya imani daima, yaliyodumishwa kwa ushirika wa daima; na huduma Yake kwa mbingu na ardhi ilifanyika bila kushindwa au kuyumba (haikufeli wa kutetereka). [Pr 172.2; Maombi Aya ya 20]

Kama mwanadamu aliomba kiti cha enzi cha MUNGU hadi ubinadamu Wake ulipoongezewa nguvu (ulichajiwa) na mkondo wa umeme wa mbinguni ambao unapaswa kuunganisha ubinadamu na uungu. Akipokea uzima kutoka kwa MUNGU, Aliwapa wanadamu uzima/uhai.— (Education, 80, 81) [Pr 172.3; Maombi Aya ya 21]

Maisha ya Maombi ya Yesu Yanafichua Siri ya Nguvu za Kiroho—Maisha ya Mwokozi duniani yalikuwa maisha ya ushirika na asilia (uumbaji) na MUNGU. Katika ushirika huu alitufunulia siri ya maisha ya nguvu za kiroho.— (Counsels on Health, 162) [Pr 173.1; Maombi Aya ya 22]

Yesu Aliomba Katika Kujitayarisha kwa ajili ya Kazi maalum— Yesu, alipokuwa akijitayarisha kwa ajili ya jaribu kubwa au kazi fulani muhimu, aliondoka na kujitenga katika milima yenye utulivu na kulala usiku kucha katika sala kwa Baba Yake. Usiku wa maombi ulitangulia kuwekwa mikono/wakfu kwa mitume na Mahubiri ya Mlimani, kugeuka sura kwa mng’ao, uchungu wa jumba la hukumu, msalaba, na utukufu wa ufufuo. [Pr 173.2; Maombi Aya ya 23]

Sisi pia lazima tutenge nyakati kwa ajili ya kutafakari na kusali na kupokea burudisho la kiroho. Hatuthamini nguvu na ufanisi wa maombi jinsi tunavyopaswa.—(The Ministry of Healing, 509) [Pr 173.3; Maombi Aya ya 24]

Ubinadamu wa Yesu Ulifanya Sala Kuwa Lazima—kutokana na hali ya kuwa na ubinadamu, Alihisi hitaji Lake la nguvu kutoka kwa Baba Yake. Alikuwa na mahali pa pekee pa kuomba. Alipenda kufanya ushirika na Baba Yake kwenye upweke wa milima. Katika zoezi hili nafsi Yake takatifu, ya ubinadamu iliimarishwa kwa ajili ya kazi na majaribu ya siku hiyo. Mwokozi wetu anajitambulisha Mwenyewe na mahitaji na udhaifu wetu, katika hilo alifanyika mwombaji/mwombaji, mwombezi wa usiku, akitafuta kutoka kwa Baba Yake nguvu mpya, ili atoke akiwa ametiwa nguvu na kuburudishwa, akiwa amejifanywa imara na thabiti kwa ajili ya wajibu na majaribio. Yeye ni Mfano wetu katika mambo yote. Yeye ni ndugu katika udhaifu wetu, lakini si katika kuwa na matamano mabaya ya mwili. Akiwa Yule asiye na dhambi, asili Yake ilijepusha na uovu. Alivumilia mapambano na mateso ya nafsi katika ulimwengu wa dhambi. Ubinadamu Wake ulifanya maombi kuwa jambo la lazima na muhimu. Alihitaji usaidizi wote wa Kiungu Wenye nguvu zaidi na faraja ambayo Baba Yake alikuwa tayari kumpa Yeye, Yeye ambaye kwa faida ya mwanadamu, aliacha furaha ya mbinguni na kuchagua makao Yake katika ulimwengu wenye ubaridi na usio na shukrani. Kristo alipata faraja na furaha katika ushirika na Baba Yake. Hapa aliweza kuutua mzigo wa moyo Wake wenye huzuni zilizokuwa zikimsagasaga/zikimpondaponda. Alikuwa mtu wa huzuni na ajuaye sikitiko. [Pr 173.4; Maombi Aya ya 25]

Alitumia siku yake kufanya kazi kwa bidii na unyofu, kuwatendea wengine wema, kuwaokoa watu kutoka kwenye uharibifu. Aliponya wagonjwa, aliwafaraji walioomboleza, na kuleta uchangamfu na tumaini kwa waliokata tamaa. Aliwafufua wafu. Baada ya kazi Yake kukamilika kwa siku hiyo, Aliondoka, jioni baada ya jioni, mbali na mkanganyiko wa jiji, na mwili Wake ukainamishwa kwa kusujudu katika dua kwa Baba Yake, katika kichaka kilichokuwa kwenye upweke. Wakati fulani miale angavu ya mwezi ilianguka juu ya mwili/umbo Lake lililokuwa katika ibada akisujudu. Na kisha tena mawingu na giza vilifunga nuru yote. Umande na barafu ya usiku vilikaa juu ya kichwa Chake na ndevu zake wakati akiwa katika hali ya Mwombaji/Mwombezi. Mara kwa mara aliendelea na maombi Yake usiku kucha. Yeye ni mfano wetu. Ikiwa tungeweza kukumbuka hili, na kumwiga, tungekuwa na nguvu zaidi katika MUNGU. [Pr 174.1; Maombi Aya ya 26]

Ikiwa Mwokozi wa wanadamu, pamoja na nguvu Zake za Kiungu, alihisi hitaji la maombi, ni zaidi kiasi gani basi kwa wanadamu wanyonge, wenye dhambi wanaokufa wanapaswa kuhisi ulazima wa maombi—Sala ya bidii na ya daima! Wakati Kristo alipozingirwa na majaribu makali zaidi, Hakula chochote. Alijikabidhi kwa MUNGU na, kupitia maombi ya dhati na utii mkamilifu kwa

mapenzi ya Baba Yake, aliibuka mshindi. Wale wanaoshuhudia ile Kweli katika siku hizi za mwisho, juu ya kila tabaka jingine la wanaodai kuwa Wakristo, wanapaswa kumwiga Yule ambaye ni Kielelezo Kikuu katika maombi. [Pr 174.2; Maombi Aya ya 27]

"Inatosha mwanafunzi kuwa kama mwalimu wake, na mtumwa kuwa kama bwana wake." Meza zetu hutapakaa/hutachafuliwa mara kwa mara na anasa (luxury) zisizo za afya wala za lazima, kwa sababu tunapenda vitu hivi kuliko tunavyopenda kujinyima nafsi, kutokuwa na magonjwa, na utimamu wa akili. Yesu alitafuta kwa dhati na bidii nguvu kutoka kwa Baba Yake. Mwana Huyu wa MUNGU Mwenyewe, alionekana kuona hilo ni la thamani zaidi Kwake Mwenyewe, kuliko kuketi kwenye meza ya kifahari zaidi (luxury table). Yeye Ametupa ushahidi kwamba maombi ni muhimu ili kupokea nguvu za kushindana na nguvu za giza, na kufanya sehemu ya kazi tuliyopewa kutimiza. Nguvu zetu wenyewe ni udhaifu, lakini kile ambacho MUNGU hutoa ni chenye nguvu na uhodari mkuu na kitamfanya kila mtu anayepokea kuwa zaidi ya mshindi.—(Testimonies for the Church 2:201-203) [Pr 174.3; Maombi Aya ya 28]

Yesu Alitenga Muda kwa ajili ya Maombi Bila kujali kwamba alikuwa na Shughuli Gani au uchovu kiasi gani—Kristo hakutoa huduma yoyote yenye ubahili au isiyo na ukarimu. Hakupima utendaji kazi Wake kwa masaa. Wakati Wake, moyo Wake, nafsi Yake na nguvu, vilitolewa kufanya kazi kwa manufaa ya wanadamu. Katika siku za uchovu alijitaabisha, na kwa usiku mrefu alsujudu/aliinama katika maombi kwa ajili ya neema na uvumilivu ili aweze kufanya kazi kubwa zaidi. Kwa kilio kikali na machozi Alituma maombi Yake mbinguni, ili asili Yake ya ubinadamu ipate kuimarishwa, ili Aweze kuzingirwa na kulindwa ili kukabiliana na adui mjanja katika kazi zake zote ya udanganyifu, na kuimarishwa kutimiza utume Wake wa kumnyanyua mwanadamu juu. Kwa watenda kazi Wake anasema, "Nimewapa kielelezo, ili nanyi mfanye kama Mimi nilivyofanya." Yohana 13:15.—(Ministry of Healing, 500) [Pr 174.4; Maombi Aya ya 29]

Yesu Aliomba Mapema Asubuhi—Asubuhi na mapema mara nyingi ilimkuta katika sehemu fulani ya faragha, akitafakari, akichunguza Maandiko, au katika sala. Kwa sauti ya uimbaji alikaribisha mwanga wa asubuhi. Kwa nyimbo za shukrani alizishangilia saa zake na kuleta shangwe ya mbinguni kwa wale waliochoka na kazi zao za kila siku na waliovunjika moyo.—(Counsels on Health, 162) [Pr 175.1; Maombi Aya ya 30]

Yesu Alikuwa na Mahali Mahsusi pa kufanyia Sala—Uwe na mahali pa sala ya siri. Yesu alikuwa na maeneo teule ya ushirika na MUNGU, na sisi pia tunapaswa kuwa napo/nayo. Tunahitaji mara kwa mara kujitenga hadi mahali fulani, hata kama ni panyenyekevu pa kiasi gani, mahali ambapo tunaweza kuwa peke yetu tu na MUNGU. — (Thoughts from the Mount of Blessing, 84) [Pr 175.2; Maombi Aya ya 31]

Yesu Aliomba kwa Ajili Yetu—Mara nyingi Yesu alikuwa amechoka kutokana na taabu isiyokoma na kujikana nafsi (kujinyima), kujitoa mhanga, na kujinyima ili kubariki wanaoteseka na wahitaji. Alitumia usiku mzima katika maombi juu ya milima pweke, si kwa sababu ya udhaifu Wake na mahitaji Yake, bali kwa sababu Aliona, Alihisi, udhaifu wa asili zetu katika kupinga majaribu ya adui katika vipengele vile vile ambavyo vinatushinda sasa. Alijua kwamba tusingejali kuhusu hatari zenu na tusingehisi hitaji letu la maombi. Ilikuwa ni kwa ajili yetu ndiyo sababu Alimimina maombi Yake kwa Baba Yake kwa vilio vizito na machozi.—(Testimonies for the Church 3:379) [Pr 175.3; Maombi Aya ya 32]

Wanafunzi wa Yesu Walivutiwa na Mazoea Yake ya Kuomba— “Mwana wa Adamu hakuja kutumikiwa, bali kuhudumu.” Si kwa ajili Yake Mwenyewe, bali kwa ajili ya wengine, aliishi na kutafakari na kuomba. Kutoka katika saa alizotumia pamoja na MUNGU alitoka asubuhi baada ya asubuhi kuleta nuru ya mbinguni kwa wanadamu. Kila siku alipokea ubatizo mpya wa Roho Mtakatifu. Katika saa za mapema za siku mpya Bwana alimwamsha kutoka katika usingizi Wake, na nafsi Yake na midomo yake ilipakwa mafuta ya neema, ili aweze kuwagawia wengine. Alipokea Maneno Yake mapya kutoka katika makao mbinguni, Maneno ambayo angeweza kusema kwa majira yake kwa waliochoka na kuonewa. “Bwana MUNGU amenipa,” alisema, “ulimi wa hao waliofundishwa nipate kujua jinsi ya kumwambia Neno kwa wakati yeye aliyechoka: ananiamsha asubuhi kwa asubuhi, anaamsha sikio Langu kusikia kama waliofundishwa” [Pr 176.1; Maombi Aya ya 33]

Wanafunzi wa Kristo walivutiwa sana na maombi Yake na tabia Yake ya ushirika na MUNGU. Siku moja baada ya kutokuwepo kwa Mola wao kwa muda mfupi, walimkuta amezama katika maombi. Akionekana kutojua uwepo wao, Aliendelea kuomba kwa sauti. Mioyo ya wanafunzi iliguswa sana. Alipomaliza kuomba, wakasema, “Bwana, tufundishe kuomba.” The Review and Herald, Agosti 11, 1910) [Pr 176.2; Maombi Aya ya 34]

Sala ya Bwana inaonyesha Uzuri wa mambo kuwa rahisi/sahili— Yesu aliwafundisha wanafunzi Wake kwamba ni sala ile tu inayotoka katika midomo isiyo na unafiki/feki, ikichochewa na mahitaji halisi ya nafsi, ndiyo ya dhati, na italeti baraka za mbinguni kwa mwombaji. Alitoa sala fupi na ya kina, yaani iliyojumuisha kila jambo kwa wanafunzi Wake. Sala hii, kwa usahili wake mzuri, haina ufanani. Ni sala kamilifu kwa ajili ya maisha ya hadhara na faragha; ni ya hadhi/heshima ya hali ya juu na iliyoinuliwa, ila ni rahisi sana kiasi kwamba mtoto aliye kwenye goti la mama yake anaweza kuielewa. Watoto wa MUNGU wamerudia sala hii kwa karne nyingi, na bado mng'ao wake haujafifia. Kama vito cha thamani kubwa, imeendelea kupendwa na kuthaminiwa. Maombi haya ni uzalishaji wa ajabu. Hakuna watakaomba bure ikiwa ndani ya maombi yao zimejumuishwa hizi kanuni ndani yake. Maombi yetu ya hadharani yanapaswa kuwa mafupi, na yaeleze tu mahitaji halisi ya roho, tukiomba kwa usahili na imani

rahisi ya kuamini kwa ajili ya vile vitu tunavyohitaji. Maombi kutoka kwenye moyo mnyenyekevu, uliopondeka ni pumzi muhimu ya roho yenye kiu ya haki. - (The Signs of the Times, Desemba 3, 1896) [Pr 176.3; Maombi Aya ya 35]

Yesu Alipiga Magoti Alipoomba—Katika ibada ya hadhara na faraghani, ni fursa yetu kupiga magoti mbele ya Bwana tunapotoa maombi yetu Kwake. Yesu, mfano wetu, "alipiga magoti na kuomba." Juu ya wanafunzi Wake imerekodiwa kwamba wao pia, "walipiga magoti na kuomba." Paulo alitangaza, "Ninampigia Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo magoti." Katika kuungama mbele za MUNGU dhambi za Israeli, Ezra alipiga magoti. Danieli "alipiga magoti mara tatu kwa siku, akaomba, akashukuru mbele za MUNGU wake." Messages to Young People, 251) [Pr 177.1; Maombi Aya ya 36]

Fikiria kwa Makini Masomo ya Yesu Kuhusu maombi—masomo ya Kristo kuhusu maombi yanapaswa kuangaliwa na kuzingatiwa kwa umakini. Kuna sayansi ya Kiungu/mbingu katika maombi, na kielelezo chake kinaleta kutazama kanuni ambazo kila mwanadamu anapaswa kuzielewa. Anaonyesha kile ambacho ni roho ya Kweli ya maombi, Anafundisha hitaji la kudumu katika kuwasilisha maombi yetu kwa MUNGU, na hutuhakikishia utayari Wake wa kusikia na kujibu maombi.—(Christ's Object Lessons, 142) [Pr 177.2; Maombi Aya ya 37]

SURA YA 16

MAOMBI YA FARAGHA

Ombi la Faragha Ni Muhimu—Nafsi Haiwezi kusitawi ilhali maombi sio mazoezi maalum ya akili. Maombi ya familia au ya halaiki peke yake hayatoshi. Maombi ya siri ni muhimu sana; katika faragha nafsi inafunuliwa wazi mbele ya jicho la MUNGU lichunguzalo, na kila nia inachunguzwa kwa makini. Maombi ya siri! Yana thamani iliyoje! Nafsi inazungumza na MUNGU! Maombi ya siri yanapaswa kusikilizwa tu na MUNGU anayesikia maombi. Hakuna sikio lenye udadisi linalopaswa kupokea mzigo wa maombi hayo. Katika maombi ya siri roho haiathiriwi na ushawishi unaoizunguka, ipo huru kutokana na hisia au mihemko yenye mikanganyiko. Kwa utulivu, lakini kwa bidii, itamfikia MUNGU. Maombi ya siri mara nyingi hupotoshwa, na miundo yake mizuri hupotea, kwa maombi ya sauti kubwa. Badala ya tumaini shwari, tulivu na imani katika MUNGU, nafsi ikiwa imetolewa katika sauti ya chini, na ya unyenyekevu, sauti inapandishwa na kuwa juu, na msisimko unatiwa moyo (unashawishiwa), na sala ya siri inapoteza

ushawishi wake mtakatifu na laini. Kuna dhoruba ya hisia, dhoruba ya maneno, ambayo inapelekea kukosa uwezekano wa kutambua sauti ndogo, na tulivu inayozungumza na nafsi wakati inashiriki katika ibada yake ya siri, ya kweli, ya moyo wote. Ombi la siri, likitolewa ipasavyo, huleta manufaa makubwa Lakini ombi linalowekwa hadharani kwa familia nzima na majirani sio ombi la siri, ingawa inadhaniwa kuwa hivyo, na nguvu za Bwana hazipokelewi kutoka katika ombi hilo. Ushawishi mzuri na wa kudumu utakuwa unatoka kwa Yeye anayeona kwa siri, ambaye sikio Lake liko wazi kusikia sala inayotokana na moyo. Kwa imani tulivu, iliyo sahili, nafsi hushikilia ushirika na MUNGU na kujikusanyia yenyewe miale ya Mungu ya nuru ili kuitia nguvu na kuitegemeza kustahimili mapambano ya Shetani. Mungu Ndiye nguzo/mnara wetu wa nguvu.—(Testimonies for the Church 2:189, 190) [Pr 178.1; Maombi Aya ya 1]

Maombi ya faragha, maombi ya Familia, maombi katika mikusanyiko ya hadhara kwa ajili ya kumuabudu MUNGU, yote ni ya muhimu. Na tunapaswa kuyaishi maombi yetu. Tunapaswa kushirikiana na Kristo katika kazi Yake. (Testimonies for the Church 7:239) [Pr 179.1; Maombi Aya ya 2]

Wote tunahitaji Kukesha na Kuomba Daima—Mwanzo kabisa wa uovu ulikuwa ni kupuuza kukesha na maombi ya siri, kisha kukaja. kupuuza majukumu mengine ya kidini/kiroho, na hivyo njia ilifunguliwa kwa dhambi zote zilizofuata. Kila Mkristo ataweza kushambuliwa na vivutio vya ulimwengu, usumbufu wa asili ya tamaa za kimwili, na majaribu ya moja kwa moja ya Shetani. Hakuna aliye salama. Haijalishi uzoefu wetu umekuwaje, haijalishi kituo chetu kiko juu kiasi gani, tunahitaji kukesha na kuomba daima. Ni lazima tutawaliwe, na kudhibitiwa kila siku na Roho wa MUNGU la sivyo tutatawaliwa na Shetani.— (Testimonies for the Church 5:102) [Pr 179.2; Maombi Aya ya 3]

Sali Nyakati Zote—Jenga mazoea ya kuzungumza na Mwokozi unapokuwa peke yako, wakati unapotembea, na unaposhughulika na kazi zako za kila siku. Acha moyo uinuliwe kila wakati katika ombi la kimya la msaada, kwa ajili nuru, nguvu, na maarifa. Hebu kila pumzi unayovuta iwe sala.—(Temperance, 135) [Pr 179.3; Maombi Aya ya 4]

Njia ya kwenda kwenye kiti cha enzi cha MUNGU iko wazi kila wakati. Hauwezi kupiga magoti kila wakati kwa ajili ya maombi, lakini maombi yako ya kimya yanaweza kupaa kwa MUNGU kila wakati kwa ajili ya nguvu na mwongozo. Utakapojaribiwa, kama ambavyo huwa, unaweza kukimbilia mahali pa siri pa Aliye Juu. Mikono yake ya milele itakuwa chini yako.—(Counsels on Health, 362) [Pr 179.4; Maombi Aya ya 5]

Maombi ya faragha Yanafaa Pahali Popote, Wakati Wowote—Sali chumbani mwako, na unapoendelea na kazi yako ya kila siku acha moyo wako uinuliwe kwa MUNGU mara kwa mara. [Pr 180.1; Maombi Aya ya 6]

Ilikuwa kwa njia hiyo Henoka alitembea na MUNGU. Maombi haya ya kimya

huinuka kama uvumba wa thamani mbele ya kiti cha neema. Shetani hawezi kumshinda yule ambaye moyo wake umejitegemeza kwa MUNGU. [Pr 180.2; Maombi Aya ya 7]

Hakuna wakati au mahali ambapo hapafai kutoa ombi kwa MUNGU. Hakuna kitu kinachoweza kutuzuia kuinua mioyo yetu katika roho ya maombi ya bidii na unyofu. Katika umati wa watu waliosongamana mitaani, katikati shuguli za biashara, tunaweza kutuma ombi kwa MUNGU na kuomba mwongozo wa MUNGU, kama vile Nehemia alipofanya ombi lake mbele ya Mfalme Artashasta. Ushirika wa karibu unaweza kupatikana popote tulipo. Tunapaswa kuacha mlango wa moyo wazi daima na mwaliko wetu ukienda juu ili Yesu aje na kukaa kama mgeni wa mbinguni katika nafsi.—(Steps to Christ, 98, 99). [Pr 180.3; Maombi Aya ya 8]

Maombi hutuleta Katika Uwepo wa MUNGU Mwenyewe— Maombi, iwe yanatolewa katika mkusanyiko wa watu wote, kwenye madhabahu ya familia, au kwa siri, humweka mwanadamu moja kwa moja mbele za MUNGU. Kwa maombi ya kudumu vijana wanaweza kupata kanuni zilizo imara sana kiasi kwamba majaribu yenye nguvu zaidi hayatawavuta kutoka katika uaminifu wao kwa MUNGU.— (My Life Today, 18) [Pr 180.4; Maombi Aya ya 9]

Maombi hutufanya tuunganishwe na Kristo — Tunapaswa kuwa katika maombi ya siri/faragha. Kristo Ndiye mzabibu, sisi ni matawi. Na kama tunataka kukua na kusitawi, lazima tuendeleo kuteka utomvu (sap) na lishe kutoka kwenye Mzabibu Hai; maana kwa kutengwa na Mzabibu hatuna nguvu. [Pr 180.5; Maombi Aya ya 10]

Nilimwuliza malaika kwanini hakukuwa na imani na nguvu tena katika Israeli. Alisema, “wanaachilia mkono wa Bwana mapema sana. Peleka maombi yako kwenye kiti cha enzi kwa ari/usongo, na ungoje hapo kwa imani thabiti. Ahadi ni za Kweli.Early Writings, 73) [Pr 180.6; Maombi Aya ya 11]

Maombi ya faragha Hutegemeza Roho - Kuishi kwa kutegemea Neno la MUNGU inamaanisha kuyasalimisha Kwake maisha yetu yote. Kutakuwa na hisia zinazoendelea za hitaji letu la kumtegemea Yeye daima, moyo utavutwa kumfuata MUNGU. Maombi ni jambo la lazima; kwani ni uhai wa roho. Maombi ya familia, maombi ya hadhara, yana nafasi yake; lakini ni ushirika wa siri na MUNGU ndio unaodumisha maisha ya roho. [Pr 180.7; Maombi Aya ya 12]

Maombi ya Faragha yanahitajika Ili mmoja mmoja tumjue MUNGU wenyewe—Loo! Je, tunamjua MUNGU jinsi tunavyopaswa? Ni faraja iliyoje, furaha iliyoje, tunapaswa kuwa nayo ikiwa tungejifunza kila siku masomo ambayo Yeye anataka tujifunze! Lazima tumjue Yeye kwa uzoefu na ujuzi wa vitendo. Itakuwa faida kwetu kutumia muda mwingi katika maombi ya siri, katika kumjua binafsi Baba yetu wa mbinguni. - (Medical Ministry, 102) [Pr 181.1; Maombi Aya ya 13]

Watu wa MUNGU Hupuuzia Maombi ya faragha—Nimeona mara kwa mara kwamba watoto wa Bwana hupuuzia maombi, hasa maombi ya siri, kwa ujumla hupuuziwa kupita kiasi; kwamba wengi hawaizoeshi imani hiyo ambayo ni fursa na wajibu wao kuitumia, mara nyingi wakingojea ile hisia ambayo ni imani pekee inayoweza kuleta. Hisia sio imani; mambo haya mawili ni tofauti.—(Early Writings, 72) [Pr 181.2; Maombi Aya ya 14]

Muumba wetu hudai kujitoa kwetu kwa hali ya juu, utii wetu wa kwanza. Chochote ambacho huelekea kutishia upendo wetu kwa MUNGU, au kuingilia kati huduma inayostahili Kwake, kinakuwa sanamu. Kwa baadhi ya watu ni ardhi zao, nyumba zao, mali zao, bidhaa zao, ni sanamu. Biashara za miradi vinatendeka kwa ari, jitihada na nguvu, wakati huduma ya MUNGU inafanywa kuwa ya pili. Ibada ya familia imepuuzwa, maombi ya siri yamesahaulika.— (SDA Bible Commentary 2: 1011, 1012) [Pr 181.3; Maombi Aya ya 15]

Kupuuzia Maombi Ni Mchakato Endelevu—Jihadhari na jinsi unavyopuuzia maombi ya siri na kusoma Neno la MUNGU. Hizi ni silaha zako dhidi ya yeye ambaye anaweka jitihada ili kuzuia maendeleo yako ya kuelekea mbinguni. Kupuuzia kwa mara ya kwanza kwa maombi na kusoma Biblia hufanya iwe rahisi kufanya hivyo mara ya pili tena. Upinzani wa kwanza dhidi ya kusihi kwa Roho huandaa njia ya upinzani wa pili. Hivyo moyo unakuwa mgumu, na dhamiri inakajeruhiwa.—(Messages to Young People, 96) Pr 181.4; Maombi Aya ya 16]

Sala Za Misimu Fulani Tu Unapopenda Zitakufanya Upoteze Utegemezi Wako Kwa MUNGU—Maombi ni pumzi ya roho. Ndiyo siri ya nguvu ya kiroho. Hakuna njia nyingine ya neema inayoweza kuwa mbadala na bado kukawa na afya ya roho na kisha mambo yakawa salama. Maombi huupatia moyo mguso wa haraka kwenye Chemchemi ya uzima, na kuimarisha mishipa na misuli ya uzoefu wa kidini/kiroho. Puuza zoezi la sala, au jihusishe na maombi bila rejareja unapotaka, hapa na pale kama utakavyo, na mara zingine usiombe kutokana na unavyoona inafaa kwako wewe binafsi, nawe utapoteza ushirika/utegemezi wako kwa MUNGU. Vitivo vya kiroho hupoteza nguvu, uzoefu wa kidini/kiroho huondokewa afya na ushupavu. - (Messages to Young People, 249, 250) [Pr 182.1; Maombi Aya ya 17]

Maombi ya faragha yanapaswa kuwa ya faragha — Katika maombi ya faragha wote wana nafasi ya kuomba maadamu wanamatamanio ya kufanya hivyo na kujieleza kinagaubaga kwa Mungu kama watakavyo. Wanaweza kuwaombea ndugu na marafiki zao wote. Chumbani mwako, pale mahali pa faragha, ni mahali pa kusema shida zako zote binafsi, na mitihani, na majaribu. Mkutano wa pamoja wa kumwabudu Mungu si mahali pa kufungua mambo yetu binafsi ya moyoni.— (Testimonies for the Church 2:578) [Pr 182.2; Maombi Aya ya 18]

Katika ibada ya faragha maombi yetu hayatakiwi kufikia masikio ya yeyote ila MUNGU asikiaye maombi. Hakuna sikio lenye udadisi linalopaswa kupokea

mzigo wa maombi hayo. [Pr 182.3; Maombi Aya ya 19]

"Unapoomba, ingia chumbani kwako." Kuwa na mahali pa maombi ya siri. Yesu alikuwa na maeneo teule ya ushirika na MUNGU, na sisi pia tunapaswa kuwa nayo. Tunahitaji mara kwa mara kujitenga hadi mahali fulani, ingawa ni pa unyenyekevu, umasikini au ila pale ambapo tunaweza kuwa peke yetu na MUNGU. [Pr 182.4; Maombi Aya ya 20]

"Omba kwa Baba yako aliye sirini." Kwa Jina la Yesu tunaweza kuja mbele za MUNGU na ujasiri wa mtoto. Hakuna mwanadamu anayehitajika kufanya kazi kama mpatanishi. Kupitia Yesu tunaweza kufungua mioyo yetu kwa MUNGU kama Yule anayetujua na anayetupenda. [Pr 182.5; Maombi Aya ya 21]

Katika mahali faraghani pa sala, ambapo hakuna jicho bali la MUNGU linaloweza kuona, hakuna sikio lisikialo Ila LakeYeye anayeweza kusikia, tunaweza kumimina matamano yetuzetu yaliyojificha zaidi na shauku zetu kwa Baba wa huruma isiyo na kikomo, na katika utulivu na ukimya wa roho sauti hiyo ambayo kamwe haijawahi kushindwa kujibu kilio cha hitaji la mwanadamu itazungumza na mioyo yetu. [Pr 182.6; Maombi Aya ya 22]

"Bwana ni Mwenye huruma, na ni mwingi wa rehema." Yakobo 5:11. Anasubiri kwa upendo usiochoka kusikia maungamo ya wale waliyoiacha njia na kukubali toba yao. Anatazama kurudisha kwetu shukrani, kama wakati ule mama anavyolitazamia tabasamu la utambuzi kutoka kwa mtoto wake mpendwa. Angetutaka tuelewe jinsi moyo Wake mwororo na ulio na matamano kwetu unavyotupenda kwa dhati. Anatazama tupeleke majaribu na mitihani yetu kwenye huruma Yake, huzuni zetu kwenye upendo Wake, majeraha yetu kwenye uponyaji Wake, udhaifu wetu kwenye nguvu Zake, utupu wetu kwenye utimilifu Wake. Kamwe hakuna hata mtu mmoja aliyekatishwa tamaa aliyemjia Yeye. "Walimtazama, wakaangazwa; na nyuso zao hazikuaibika." Zaburi 34: 5. [Pr 183.1; Maombi Aya ya 23]

Wale wamtafuta MUNGU faraghani wakimwambia Bwana mahitaji yao na kuomba msaada, hawataomba bure. "Baba yako aonaye sirini, Yeye Mwenyewe atawapa thawabu." Kadiri Tunavyomfanya Kristo kuwa Mwenzi wetu wa kila siku tutahisi kuwa nguvu za ulimwengu usioonekana zikituzunguka; na kwa kumtazama Yesu tutafanana na sura Yake. Kwa kumtazama au kufanya ushirika Naye tunabadilishwa. Tabia hulainishwa, husafishwa, na kuboreshwa/kuheshimishwa kwa ajili ya ufalme wa mbinguni. Matokeo ya dhahiri ya tendo letu la ushirika na Bwana wetu yatakuwa ni ongezeko la ucha MUNGU, usafi wa moyo, na bidii. Kutakuwepo na ukuaji wa akili katika sala zetu. Tutapokea elimu ya Bwana/Kimbingu, na hili hudhihirishwa katika maisha ya uadilifu na shauku. [Pr 183.2; Maombi Aya ya 24]

Roho inayomgeukia MUNGU kwa ajili ya kupata nguvu, sapoti, msaada, na

uwezo, kwa maombi ya dhati ya kila siku, itakuwa na matamanio bora, uelewa dhahiri wa ile Kweli na wajibu, magoli ya kina katika utendaji kazi, na njaa na kiu ya haki ya daima. Kwa kudumisha muunganiko na MUNGU, tutawezeshwa kusambaza kwa wengine, kupitia ushirika wetu na wao, nuru, amani, utulivu, unaotawala mioyoni mwetu. Nguvu inayopatikana katika maombi kwa MUNGU, imeunganishwa na bidii ya kudumu katika kufundisha akili kwa makini kwa kujali na kusaidia, nayo huandaa mtu kwa ajili ya majukumu ya kila siku na huweka roho katika amani katika mazingira yote -(Thoughts from the Mount of Blessing,84, 85) [Pr 183.3; Maombi Aya ya 25]

Kuna wengine ambao nina hofu, hawapeleki shida zao kwa MUNGU katika maombi ya faragha, bali wanazilundika kwa ajili ya mkutano wa maombi, na huko wakifika hufanya maombi yao kwa siku kadhaa. Watu hao wanaweza kuitwa wauaji wa mikutano na maombi. Hawatoi nuru; hawamjengi mtu. Maombi yao marefu, yenye ubaridi ulioganda, hutupia wengine baridi ya kutetemesh mwili na giza pia, na kisha shuhuda zao ndefu za kurudi nyuma kwao huwatia watu kivuli tu. Wote hushusha pumzi kwa furaha wanapomaliza, na inakaribia kutowezekana kabisa kuondoa ubaridi unaotetemesh na giza ambalo maombi na mashauri yao huleta kwenye mkutano. Kutoka kwa nuru ambayo nimeipokea, mikutano yetu inapaswa kuwa ya kiroho na ya kijamii, na sio mirefu sana. Kujiweka mbali kwa kutokuwa na moyo wa kirafiki, kiburi, ubatili, na hofu ya mwanadamu vinapaswa kuachwa huko huko nyumbani. Tofauti ndogo na chuki tulizo nazo hatupaswi kwenda nazo kwenye mikutano hii. Kama ilivyo katika familia yenye umoja, unyenyekevu, upole, kujiamini, na upendo vinapaswa kuwepo mioyoni mwa akina kaka na dada ambao wanakutana ili kuhuishwa na kuongezewa nguvu kwa kuleta nuru zao pamoja. - (Testimonies for the Church 2: 578, 579) [Pr 184.1; Maombi Aya ya 26]

Maombi ya Faragha Hutoa Taswira au picha ya Wazi ya nafsi— Hakuna kitakachotoa maoni yaliyo wazi kama hayo kuhusu nafsi yako kama maombi ya siri. Yeye aonaye sirini na anayejua kila kitu, atakuangazia ufahamu wako na kuyajibu maombi yako. Majukumu ya wazi, na mepesi ambayo hayapaswi kupuuzwa yatafunguliwa mbele yako.—(Testimonies for the Church 5:163) [Pr 184.2; Maombi Aya ya 27]

Maombi ya Faragha Husitawisha Tabia tukufu—Katikati ya hatari za siku hizi za mwisho, usalama pekee wa vijana uko katika kukesha na maombi yanayoongezeka kila mara. Kijana anayepata furaha yake katika kusoma Neno la MUNGU, na katika saa ya maombi, atahuishwa mara kwa mara na rasimu kutoka kwenye chemchemi ya uzima. Atafikia kilele cha ubora wa maadili na upana wa mawazo ambayo wengine hawawezi hata kuuwazia. Ushirika na MUNGU hutia moyo mawazo mazuri, matamanio bora, mitazamo iliyo wazi ya ile Kweli, na makusudio makuu ya utendaji. Wale wanaojiunganisha na MUNGU wanatambuliwa Naye kama wana na binti Zake. Daima wanaendelea kufikia juu

na juu zaidi, wakipata mitazamo iliyo wazi zaidi juu ya MUNGU na ya umilele, hadi Bwana anawafanya mifereji ya nuru na hekima kwa ulimwengu. [Pr 184.3; Maombi Aya ya 28]

Lakini maombi hayaeleweki kama yanavyopaswa kueleweka. Maombi yetu hayapaswi kumpa habari MUNGU juu ya mambo ambayo hayajui. Bwana anajua siri za kila roho. Maombi yetu hayapaswi kuwa marefu na yenye sauti kubwa. MUNGU husoma wazo lililofichwa. Tunaweza kuomba kwa siri, na Yeye anayeona sirini atasikia, na atatujazia thawabu waziwazi. [Pr 185.1; Maombi Aya ya 29]

Maombi ambayo hutolewa kwa MUNGU na kumweleza juu ya dhambi na unyonge wetu wote pamoja na sikitiko letu, wakati hatujisikii wanyonge hata kidogo, ni maombi ya unafiki. Ni maombi ya toba ambayo Bwana anayaangalia. "Kwa Maana Yeye aliye juu, aliyetukuka, akaaye milele; ambaye Jina Lake ni Mtakatifu; Ninakaa mahali pa juu na Patakatifu, pamoja na yeye ambaye pia ni mwenye roho iliyopondeka na mnyenyekevu, ili kufufua roho ya wanyenyekevu, na kufufua moyo wa wale waliopondeka." The Youth's Instructor, August 18, 1898) [Pr 185.2; Maombi Aya ya 30]

Nguvu ya kiroho huja kupitia maombi ya Faragha— Wale ambao watavaa silaha zote za MUNGU na kutenga muda kila siku kwa ajili ya kutafakari na kufanya maombi na kusoma Maandiko wataunganishwa na mbingu na watakuwa na mvuto uokoao, na unaobadilisha kwa wale wanaowazunguka. Mawazo mazuri, matamanio bora, ufahamu dhahiri kuhusu Ukweli na wajibu kwa MUNGU, haya yote yatakuwa yao. Watakuwa na matamanio ya usafi wa moyo, kuwa na nuru, kuwa na upendo, na kuwa na neema zote zinazozaliwa na mbingu. Maombi yao ya bidii kabisa yatapenya ndani ya pazia. Kundi la watu hawa litakuwa na ujasiri mtakatifu mbele ya Yeye Asiye na Mwisho/kikomo. Watahisi kuwa nuru na utukufu wa mbinguni ni kwaajili yao, na watasafishwa, watainuliwa, wataboreshwa na kuadilishwa na uhusiano huu wa karibu sana na MUNGU. Huo ndio upendeleo walionao Wakristo wa kweli. [Pr 185.3; Maombi Aya ya 31]

Kutafakari kwa nadharia tu bila vitendo halisi hakutoshi; shughuli au utendaji mwingi hautoshi; vyote viwili ni muhimu kwa uundaji wa tabia ya Kikristo. Nguvu inayopatikana katika maombi ya dhati, na ya siri, hututayarisha kustahimili vishawishi vya jamii. Na bado hatupaswi kujitenga na ulimwengu, kwani uzoefu wetu wa Kikristo unapaswa kuwa nuru ya ulimwengu. Jamii ya wasioamini haitatudhuru ikiwa tutachangamana nao kwa kusudi la kuwaunganisha na Mungu na kuwa na nguvu za kutosha kiroho kuhimili ushawishi wao. - (Testimonies for the Church 5:112, 113) [Pr 185.4; Maombi Aya ya 32]

MUNGU Hukubali Maombi ya Kimyakimya—Bwana atakubali hata ombi la kimya la moyo uliolemewa. - (The SDA Bible Commentary 2: 1014) [Pr 186.1; Maombi Aya ya 33]

Kushuhudia Kunapaswa Kutanguliwa na Maombi—Jitihada binafsi kwa wengine zinapaswa kutanguliwa na maombi mengi ya siri; kwani inahitajika hekima kubwa kuelewa sayansi ya kuokoa roho. Kabla ya kuwasiliana na wanadamu, wasiliana na Kristo, Kwenye kiti cha enzi cha neema ya mbinguni pata maandalizi ya kuhudumia watu. - (Christ Object Lessons, 149) [Pr 186.2; Maombi Aya ya 34]

Ni sharti tupokee nuru na baraka, ili tuwe na kitu cha kutoa. Ni fursa ya kila mtendakazi kuzungumza na MUNGU kwanza katika mahali pa siri pa maombi na kisha kuzungumza na watu kama kinywa cha MUNGU. Wanaume na wanawake wanaowasiliana na MUNGU, walio na Kristo adumuye, huifanya angahewa kuwa takatifu, kwa sababu wanashirikiana na malaika watakatifu. Ushuhuda wa namna hiyo unahitajika kwa wakati huu. —(Testimonies for the Church 6:52) [Pr 186.3; Maombi Aya ya 35]

Kazi na maombi Sharti Vifungamanishwe- Lazima tuishi maisha ya pande mbili, maisha ya kufikiri na kutenda, maisha ya maombi ya kimya na kufanya kazi kwa dhati na bidii....Roho inayomgeukia MUNGU kwa ajili ya kupata nguvu, msaada (sapoti), na uwezo kwa maombi ya bidii ya kila siku, itakuwa na matamanio bora, uelewa dhahiri wa Ukweli na wajibu, malengo ya hali ya juu katika utendaji wa kazi, na njaa na kiu ya haki ya kudumu.—(Testimonies for the Church 4:459, 460) [Pr 186.4; Maombi Aya ya 36]

Ikiwa tutaruhusu kuharakia kwenye majukumu ns kutuondoa kwenye kusudi letu la kumtafuta Bwana kila siku, tutatenda makosa makubwa zaidi; na kujipatia hasara, kwa kuwa Bwana hatakuwa pamoja nasi. Tumefunga mlango ili asipate nafasi kufikia roho zetu. Lakini ikiwa tunaomba, hata wakati mikono yetu inatenda kazi, sikio la Mwokozi liko wazi kusikia maombi yetu....MUNGU anakutunza mahali ambapo ni wajibu wako kuwepo hapo. Lakini hakikisha, mara nyingi, kwa kadiri iwezekanavyo kwenda mahali ambapo sala inazoeleka kufanywa (mahali pa maombi).— (Medical Ministry, 216) [Pr 186.5; Maombi Aya ya 37]

Tumia Lugha Rahisi katika Maombi-Lugha yenye misamiati migumu au mingi, yenye madoido mengi, yenye sauti ya juu ya kujifanya na yenye maelezo mengi haifai katika maombi, iwe ombi hilo linatolewa kwenye mimbari, kwenye mzunguko wa familia, au kwa siri. Hasa yule anayetoa ombi la hadharani anapaswa kutumia lugha rahisi, ili wengine waelewe yanayosemwa na kuungana na ombi hilo. [Pr 187.1; Maombi Aya ya 38]

Ni sala inayotoka moyoni kwa imani, ndiyo ambayo husikika mbinguni na kujibiwa duniani.—(Gospel Workers, 177) [Pr 187.2; Maombi Aya ya 39]

Ni Fursa yetu Kupiga Magoti Tusalipo- tunapokuwa katika umma na katika ibada binafsi ni fursa yetu kusujudu kwa kupiga magoti mbele za MUNGU tunapotoa maombi yetu Kwake. Yesu, mfano wetu, "alipiga magoti na kuomba."

Luka 22:41. Juu ya wanafunzi Wake imeandikwa kwamba wao pia, "walipiga magoti na kuomba." Matendo 9:40. Paulo alitangaza, "Ninampigia Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo magoti." Waefeso 3:14. Katika kuungama mbele za MUNGU dhambi za Israeli, Ezra alipiga magoti. Tazama Ezra 9: 5. Danieli "alipiga magoti mara tatu kwa siku, akasali, akashukuru mbele za MUNGU wake." Danieli 6:10.—(Prophets and Kings, 48) [Pr 187.3; Maombi Aya ya 40]

Usijihusishe na maburudisho yanayokufanya Usistahili Maombi ya Faragha—Starehe yoyote ambayo unaweza kujihusisha nayo na bado ukaomba baraka za MUNGU kupitia hiyo kwa imani, haitakuwa yenye hatari. Lakini starehe yoyote ile inayokufanya usiweze kufanya maombi ya siri, au usifanye ibada kwenye madhabahu ya maombi, au kushiriki katika mkutano wa maombi, hakika sio salama, bali ni hatari.—(Messages to Young People, 386) [Pr 187.4; Maombi Aya ya 41]

MUNGU Hutuona Katika Mahali Petu pa Maombi ya Faragha— Kama Nathanaeli, tunahitaji kujifunza Neno la MUNGU sisi wenyewe, na kuomba kwa ajili ya kuangaziwa na Roho Mtakatifu. Yeye aliyemwona Nathanaeli chini ya mtini atatuona mahali pa siri pa maombi. Malaika kutoka katika ulimwengu wa nuru wako karibu na wale ambao kwa unyenyekevu wanatafuta mwongozo wa Bwana/mbingu.—(The Desire of Ages, 141) [Pr 187.5; Maombi Aya ya 42]

Maombi Yetu Hayawezi Kupotea—Ni jambo la ajabu kwamba tunaweza kuomba kwa ufasaha na ufanisi; yaani kwamba, sisi wanadamu tusiostahili, tunaokufa na wakosefu, tunao uwezo wa kutoa maombi yetu kwa MUNGU. Je! Ni nguvu gani ya juu zaidi ambayo mwanadamu anaweza kiutamani kuliko hii basi, kuwa na ushirika na MUNGU asiye na kikomo? Mtu dhaifu, na mwenye dhambi ana nafasi na upendeleo wa kuzungumza na Muumba wake. Tunaweza kutamka maneno ambayo yanakifikia kiti cha enzi cha Mfalme wa ulimwengu (sayari zote-Universe). Tunaweza kuongea na Yesu tunapotembea njiani, Naye anasema, Mimi Niko mkono wako wa kuume. [Tazama Zaburi 16: 8.] [Pr 187.6; Maombi Aya ya 43]

Twaweza kuzungumza/kuwasiliana na MUNGU mioyoni mwetu; tunaweza kutembea katika ushirika na Kristo. Tunapofanya kazi yetu ya kila siku, tunaweza kupumua matamano ya mioyo yetu, yasiyoweza kusikiwa na sikio la mwanadamu; lakini neno au ombi hilo haliwezi kufa kimya, wala haliwezi kupotea. Hakuna kitu kinachoweza kuzamisha shauku ya roho. Huinuka juu ya sauti za mitaani, juu ya kelele za mashine. Ni MUNGU Ndiye ambaye tunazungumza Naye, na maombi yetu husikilizwa. [Pr 188.1; Maombi Aya ya 44]

Omba, kisha; omba, nawe utapokea. Omba unyenyekevu, hekima, ujasiri, ongezeko la imani. Kwa kila ombi la dhati jibu litakuja. Linaweza lisije vile vile unavyotamani, au kwa wakati unaolitafuta; lakini litakuja kwa njia na kwa wakati ambao utakidhi mahitaji yako kwa ubora zaidi. Maombi unayotoa katika upweke,

katika uchovu, katika majaribio, MUNGU hujibu, sio kila wakati kulingana na matarajio yako, lakini daima kwa faida yako. - (Gospel Workers, 258) [Pr 188.2; Maombi Aya ya 45]

Wote wanaoteswa au kutumiwa isivyo haki, wamlilie MUNGU. Jiepushe na wale ambao mioyo yao ni kama chuma, na umjulishe Muumba wako maombi yako. Kila aliyemwendea Yeye kwa moyo uliopondeka, hakuna kati yao aliyewahi kupigwa teke au kuchukiwa Naye. Hakuna ombi hata moja la dhati linalopotea. Katikati ya nyimbo zinazoinua moyo za kwaya ya mbinguni, MUNGU husikia kilio cha mwanadamu dhaifu zaidi. Tunamwaga matamania ya moyo wetu katika vyumba vyetu, tunapumua maombi tunapotembea njiani, na maneno yetu yanafika kwenye kiti cha enzi cha Mfalme wa ulimwengu. Yanaweza yasikike kwenye sikio lolote la mwanadamu, lakini hayawezi kufa kimya, wala hayawezi kupotea kupitia mchakato wa shuguli zinazoendelea. Hakuna kitu kinachoweza kuzamisha shauku ya roho. Huinuka juu ya sauti za mitaani, juu ya machafuko ya umati, hadi nyua za mbinguni. Ni MUNGU Ndiye ambaye tunazungumza Naye, na sala yetu husikilizwa. - (Christ Object Lessons, 174) [Pr 188.3; Maombi Aya ya 46]

SURA YA 17

MAOMBI KATIKA MZUNGUKO WA NYUMBANI

Familia zapaswa kuomba Pamoja Kila Asubuhi na Jioni —Ibada ya Familia haipaswi kuongozwa na mazingira ya namna fulani (mfano shida imeingia). Haupaswi kuomba kulingana na matukio fulani au wakati fulani, na kisha wakati una kazi kubwa ya siku ya kufanya, unaacha. Kwa kufanya hivi unawaongoza watoto wako kuona maombi kama hayana matokeo yoyote maalum. Maombi yana maana kubwa sana kwa watoto wa MUNGU, na utoaji wa shukrani unapaswa kuja mbele za MUNGU asubuhi na jioni. Anasema mwandishi Zaburi"Njoni, tumwimbie Bwana, tumfanyie shangwe mwamba wa wokovu wetu. Tuje mbele Zake kwa shukrani, na tumfanyie shangwe kwa Zaburi. [Pr 189.1; Maombi Aya ya 1]

Akina baba na akina mama, haijalishi shuguli zako ziwe za kushinikiza kwa kias gani, usishindwe/usifeli kukusanya familia yako karibu na madhabahu ya MUNGU. Omba ulinzii wa malaika watakatifu nyumbani kwako. Kumbuka kwamba wapendwa wako wanakabiliwa na vishawishi. [Pr 189.2; Maombi Aya ya 2]

Katika jitihada zetu za kuwafariji, kuwahudumia na kuwafurahisha wageni, hebu tusipuuze wajibu wetu kwa MUNGU. Saa ya maombi haipaswi kupuuzwa kwa kuzingatia jambo au mtu yeyote. Msizungumze na kujifurahisha wenyewe hadi mchoshwe kabisa kufurahia msimu wa ibada. Kufanya hivi ni kumtolea MUNGU sadaka iliyo kilema. Saa za mapema za jioni, wakati ambapo tunapoweza kuomba bila harakaharaka na tukiwa katika ufahamu wetu (akili inafanya kazi vyema), tunapaswa kuwasilisha dua zetu na kupaza sauti zetu kwa furaha, tukimsifu Mungu na kumpa shukrani zetu. [Pr 189.3; Maombi Aya ya 3]

Hebu wote wanaowatembelea Wakristo waone kwamba saa ya maombi ni ya thamani zaidi, takatifu zaidi, na saa ya furaha zaidi ya siku. Misimu hii ya ibada huwa na uboreshaji, usafishaji, ushawishi unaoinua juu ya wote wanaoshiriki. Huleta amani na pumziko la shukrani kwa roho .—(Child Guidance, 520, 521) [Pr 190.1; Maombi Aya ya 4]

Bwana ana maslahi maalum katika familia za watotoWake hapa chini. Malaika hutoa moshi wa ubani wenye harufu nzuri kwa watakatifu wanaoomba. Basi katika kila familia acha maombi yapande juu mbinguni asubuhi na saa ya baridi jua lituapo, kwa niaba yetu tukiwasilisha mbele za MUNGU sifa na haki ya Mwokozi. Asubuhi na jioni ulimwengu wa mbinguni huandika katika kitabu cha kumbukumbu kila kaya inayoomba. - (My Life Today, 29) [Pr 190.2; Maombi Aya ya 5]

Asubuhi na jioni ulimwengu wa mbinguni unaitazama kila kaya inayoomba, na

malaika aliye na ubani, akiwakilisha damu ya upatanisho, hutafuta njia ya kumfikia MUNGU. - (SDA Bible Commentary, vol. 7, 971) [Pr 190.3; Maombi Aya ya 6]

Asubuhi mawazo ya kwanza ya Mkristo yanapaswa kuwa juu ya MUNGU. Kazi ya kidunia na masilahi ya kibinafsi vinapaswa kuwa sehemu ya pili. Watoto wanapaswa kufundishwa kuheshimu na kuwa na kicho kwa saa ya maombi Ni wajibu wa wazazi Wakristo, asubuhi na jioni, kwa sala ya dhati na imani yenye kudumu, kuwajengea ua watoto wao. Wanapaswa kuwafundisha kwa subira—kwa fadhili na bila kuchoka jinsi ya kuishi ili kumpendeza MUNGU.— (Child Guidance, 519) [Pr 190.4; Maombi Aya ya 7]

Katika kila nyumba ya Kikristo Mungu anapaswa kuheshimiwa kwa dhabihu za asubuhi na jioni za maombi na sifa. Watoto wanapaswa kufundishwa kuheshimu na kuhusudu saa ya maombi. Ni wajibu wa wazazi Wakristo, asubuhi na jioni, kwa maombi ya dhati na imani yenye kudumu, kuwajengea wigo watoto wao. [Pr 190.5; Maombi Aya ya 8]

Kanisani, nyumbani watoto wanapaswa kujifunza kuomba na kumtegemea MUNGU. Wafundishe kurudia sheria ya MUNGU. Waisraeli waliagizwa hivi kuhusu amri: “Uwafundishe watoto wako kwa bidii, na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo;” Kumbukumbu la Torati 6:7. Njoo kwa unyenyekevu, na moyo mwororo, na kwa hisia za majaribu na hatari mbele yako na watoto wako; kwa imani uwafunge madhabahuni, na kuwaandaa kwa ajili ya huduma ya Bwana. Wafunze watoto kutoa maneno yao sahili/rahisi ya maombi. Waambie kwamba MUNGU anafurahi kuwafanya wamwite Yeye.— (Counsels to Parents, Teachers, and Students, 110) [Pr 191.1; Maombi Aya ya 9]

Kabla ya kuondoka nyumbani kwa ajili ya kazi, familia yote inapaswa kuitwa pamoja; na baba, au mama wakati baba hayupo, wanapaswa kumsihi MUNGU kwa bidii ili awahifadhi kwa siku nzima. Njoo kwa unyenyekevu, na moyo uliosheheni wema, upendo na upole, na kwa hisia moyoni za majaribu na hatari zilizo mbele yako na watoto wako; kwa imani uwafunge madhabahuni, na kuomba kwa bidii na moyo wote kwa ajili ya utunzaji wa Bwana. Malaika wanaohudumu watawalinda watoto ambao wamewekwa wakfu kwa MUNGU kwa namna hiyo.—(Child Guidance, 519) [Pr 191.2; Maombi Aya ya 10]

Familia Zinapaswa Kuwa na Nyakati za Maombi Zilizowekwa Asubuhi na Jioni—Katika kila familia kunapaswa kuwe na wakati uliowekwa wa ibada ya asubuhi na jioni. Ni jambo la kufaa kwa kiasi gani kwa wazazi, kukusanya watoto wao pamoja nao kabla ya kifungua kinywa, kumshukuru Baba wa mbinguni kwa ulinzi Wake wakati wa usiku, na kumwomba msaada Wake na mwongozo, pamoja uangalizi Wake wakati wa mchana! Ni jambo linalofaa kiasi gani, wakati wa jioni unapofika pia, wazazi na watoto wakusanyike tena mbele Zake Bwana na kumshukuru kwa baraka za siku iliyopita!—(Child Guidance, 520) [Pr 191.3;

Maombi Aya ya 11]

Maombi ya Familia ni ya muhimu - Maombi ya faragha, maombi ya familia, maombi katika mikusanyiko ya hadhara/umma kwa ajili ya ibada ya MUNGU—yote ni muhimu. Na tunapaswa kuyaishi maombi yetu. Tunapaswa kushirikiana na Kristo katika Kazi Yake.—(Testimonies for the Church 7:239) [Pr 192.1; Maombi Aya ya 12]

Hakuna kitu Cha Kusikitisha Kama Nyumba isiyo na Maombi — Sijui chochote kinachonisababishia huzuni kubwa kama nyumba isiyo na maombi. Sijisikii salama katika nyumba kama hiyo hata kwa usiku mmoja; na isingekuwa kwa tumaini la kuwasaidia wazazi kutambua hitaji lao na upuuziaji wao unaohuzunisha, nisingebakia ndani ya nyumba hiyo. Watoto wanaonyesha matokeo ya upuuziaji huko, kwa maana hofu ya MUNGU haiko mbele yao.—(Child Guidance, 518) [Pr 192.2; Maombi Aya ya 13]

Kila Nyumba iwe Nyumba ya Maombi—Kama kumewahi kuwa na wakati ambapo kila nyumba inapaswa kuwa nyumba ya maombi ni sasa. (Testimonies for the Church 7:42) [Pr 192.3; Maombi Aya ya 14]

Maombi ya Familia Hutuweka Katika Uwepo wa MUNGU wa Moja kwa Moja—Sala, iwe Inatolewa katika kusanyiko hadhara ya watu wote, liwe kwenye madhabahu ya familia, au kwa siri, humweka mwanadamu moja kwa moja mbele za MUNGU. Kwa maombi yasiyokoma vijana wanaweza kupata kanuni zilizo imara sana kiasi kwamba majaribu yenye nguvu zaidi hayatawavuta kutoka katika uaminifu wao kwa MUNGU.— (My Life Today, 18) [Pr 192.4; Maombi Aya ya 15]

Maombi ya Familia huleta Nguvu na Baraka — Tunapaswa kuomba kwa MUNGU zaidi kuliko tunavyofanya. Kuna nguvu kubwa na baraka katika kuomba pamoja katika familia zetu, kuomba pamoja na kwa ajili ya watoto wetu. Wakati watoto wangu wamefanya makosa, na nimezungumza nao kwa upole na kisha nikaomba nao, sijawahi kuona kuwa ni lazima baada ya hapo kuwaadhibu. Mioyo yao iliyeyuka kwa upole, na wema mbele ya Roho Mtakatifu aliyekuja kujibu maombi. - (Child Guidance, 525) [Pr 192.5; Maombi Aya ya 16]

Lugha Rahisi Ndiyo Inafaa Zaidi kwa Maombi— Lugha yenye misamiati migumu au mingi, yenye madoido mengi, yenye sauti ya juu ya kujifanya na yenye maelezo mengi haifai katika maombi (high-flown). iwapo ombi linatolewa kwenye mimbari, katika mzunguko wa familia, au kwa siri. Hasa yule anayehusika na kutoa ombi la hadharani, anapaswa kutumia lugha rahisi, ili wengine waelewe yanayosemwa na kuungana na ombi hilo. [Pr 192.6; Maombi Aya ya 17]

Ombi la imani linalotoka moyoni ndilo ambalo husikika mbinguni na kujibiwa duniani.—(Gospel Workers, 177) [Pr 193.1; Maombi Aya ya 18]

Wafundishe Watoto Wako kuheshimu Wakati wa Maombi— Watoto wako

wanapaswa kuelimishwa kuwa wenye fadhili, wenye kufikiria wengine, wapole, waungwana, rahisi kusihiwa, na, zaidi ya yote, kuheshimu mambo ya kidini/kiroho na kuhisi umuhimu wa madai ya MUNGU. Wanapaswa kufundishwa kuheshimu saa ya maombi; wanatakiwa kuamka asubuhi ili waweze kuwa kwenye ibada ya familia. - (Child Guidance, 521) [Pr 193.2; Maombi Aya ya 19]

Maombi kwa Ajili ya Familia Yetu Ni vyema yanapofanywa/yanapooombewa Nyumbani — Hatupaswi kwenda kwenye nyumba ya MUNGU kuomba familia zetu isipokuwa hisia za ndani zitatuongoza wakati Roho wa MUNGU anashawishi. Kwa ujumla, mahali sahihi pa kuomba familia zetu ni kwenye madhabahu ya familia. Wakati mada za maombi yetu ziko mbali (watu tunaowaomba etc wapo mbali na pale kanisani), mahali pa siri ni mahali pazuri pa kumsihi kwa bidii MUNGU kwa ajili ya mada hizo. Tunapokuwa katika nyumba ya MUNGU, tunapaswa kuomba baraka ya hapo tulipo na tunapaswa kutarajia MUNGU kusikia na kujibu maombi yetu. Mikutano kama hiyo itakuwa hai, yenye uchangamfu na ya kuvutia.—(Testimonies for the Church 1:145, 146) [Pr 193.3; Maombi Aya ya 20]

Bwana Hakubali Ibada ya Familia Ambayo Imekuwa ya mazoea (ni mfano tu au desturi) —Mara nyingi ibada ya asubuhi na jioni ni zaidi kidogo ya mazoea, ni duni (inaboesha), inachosha kwa semie za kujirudiarudia, ambamo roho ya shukrani au hisia ya uhitaji wao Mungu hazidhiriki. Bwana hakubali huduma kama hiyo. Lakini maombi ya moyo mnyenyekevu na roho iliyopondeka Yeye hatayadharau/hatayapuza. Kufungua mioyo yetu kwa Baba yetu wa mbinguni, kutambua na kukiri utegemezi wetu wote Kwake, kutanabaisha mahitaji yetu, ibada ya upendo wenye shukrani— ndiyo ombi la Kweli.— (Child Guidance, 518) [Pr 193.4; Maombi Aya ya 21]

Wazazi Wanahitaji Kuomba Hekima Ili kuwafunza/kuwalea Watoto Wao Kwa hekima—Kila familia inapaswa kuinua madhabahu yake ya maombi, ikitambua kwamba kumcha Bwana ndiyo chanzo cha hekima. Ikiwa kuna watu duniani wanahitaji nguvu na faraja ambayo dini hutoa, basi ni wale ambao wanawajibika kwa malezi na mafunzo ya watoto. Hawawezi kufanya kazi yao kwa njia inayokubalika kwa MUNGU huku kielelezo chao cha kila siku kinawafundisha wale wanaotazamia kupata mwongozo kutoka kwao kwamba wanaweza kuishi bila MUNGU. Ikiwa wanawafundisha watoto wao kuishi kwa ajili ya maisha haya tu, hawatafanya maandalizi yoyote kwa ajili ya umilele. Watakufa kama walivyoishi bila MUNGU, na wazazi wao watawajibika kwa ajili ya kupoteza roho zao. Akina baba, akina mama, mnahitaji kumtafuta MUNGU asubuhi na jioni kwenye madhabahu ya familia, ili mpate kujifunza jinsi ya kuwafundisha watoto wenu kwa hekima, kwa upole, kwa wema na kwa upendo.— (Child Guidance, NW;517) [Pr 194.1; Maombi Aya ya 22]

Mmewaleta watoto katika ulimwengu ambao hawakuwa na sauti au maamuzi kuhusiana na uwepo wao. Mmejifanya wenyewe kuwajibika kwa kiwango

kikubwa kuhusu furaha yao ya baadaye, na ustawi wao wa milele. Jukumu liko juu yenu, iwe mnalihisi hili au la, kuwafundisha na kuwalea watoto hawa kwa MUNGU, kuwatunza kwa uangalifu wenye wivu mara tu adui mjanja anapotokezea na kuweka hatua yake ya kwanza, na kisha muwe tayari kuinua kiwango dhidi yake. Jenga ngome ya maombi na imani juu ya watoto wako, na ufanye bidii kukesha humo. Hauko salama hata kidogo dhidi ya mashambulio ya Shetani. —(Testimonies for the Church 2:397, 398) [Pr 194.2; Maombi Aya ya 23]

Hebu wazazi wamtafute MUNGU kwa ajili ya mwongozo katika kazi zao. Wakiwa wamepiga magoti mbele Yake watapata ufahamu wa kweli wa wajibu wao mkuu na huko wanaweza kuwakabidhi watoto wao kwa Yule ambaye hakosei kamwe katika ushauri na mafundisho.—(The Adventist Home, 321) [Pr 194.3; Maombi Aya ya 24]

Kwa maombi ya dhati na ya bidii wazazi wanapaswa kuwawekea ulinzi watoto wao. Wanapaswa kuomba kwa imani kamili kwamba MUNGU atakaa pamoja nao, na kwamba malaika watakatifu watawalinda wao na watoto wao dhidi ya nguvu katili za Shetani.— (Testimonies for the Church 7:42, 43) [Pr 194.4; Maombi Aya ya 25]

Kwa subira, kwa upendo, kama mawakili waaminifu wa neema anuwai ya Kristo, wazazi wanapaswa kufanya kazi yao waliyoagizwa. Wanatarajiwa kukutwa waaminifu. Kila kitu kifanyiike kwa imani. Ni lazima waombe daima bila kuchoka ili MUNGU awapatie neema yake watoto wao. Kamwe hawapaswi kuchoka, kukosa subira, au kukasirika katika kazi zao. Lazima washikamane kwa karibu na watoto wao na MUNGU. Wazazi wakifanya kazi kwa subira na upendo, wakijitahidi kwa dhati na bidii kuwasaidia watoto wao kufikia kiwango cha juu zaidi cha usafi wa moyo, adabu, kujistahi na kiasi, watafaulu.—(The Adventist Home, 208) [Pr 195.1; Maombi Aya ya 26]

Bila juhudi za kibinadamu jitihada za Bwana/mbingu ni bure. MUNGU atafanya kazi kwa nguvu wakati wazazi wanamtegemea na kumtumainia Yeye, wakati ule ambapo wazazi watakapoamka kwa ajili ya jukumu lao takatifu lililo juu yao, na kutafuta kuwafunza na kuwalea watoto wao ipasavyo. Atashirikiana na wazazi ambao huwaelimisha watoto wao kwa uangalifu na kwa maombi, wakifanyia kazi wokovu wao na wa watoto wao. Atafanya kazi ndani yao, kunia na kutenda mapenzi Yake mema.—(The Adventist Home, 206, 207) [Pr 195.2; Maombi Aya ya 27]

Wazazi, Je! mnafanya kazi kwa bidii isiyochona na uvumilivu kwa niaba ya watoto wenu? MUNGU wa mbinguni anaona kujali kwako, kazi yako ya bidii, kukesha katika ulinzi kwako jwa kila wakati. Anasikia maombi yako. Kwa uvumilivu na upole wafunze watoto wako kwa ajili ya Bwana. Mbingu yote inapendezwa na kazi yako. Malaika wa nuru wataungana nawe unapojitahidi kuwaongoza watoto wako kwenda mbinguni. MUNGU ataungana nawe, akiwekea

taji juhudi zako kwa mafanikio. Kristo anafurahi kuiheshimu familia ya Kikristo; kwa kuwa familia kama hiyo ni ishara ya familia iliyo mbinguni. - (The Review and Herald, Januari 29, 1901) [Pr 195.3; Maombi Aya ya 28]

Umuhimu Mkuu wa Maombi ya Mama—Wale wanaoshika sheria ya MUNGU huwatazama watoto wao kwa hisia zisizoelezeka— za matumaini na hofu, wakijiuliza watawajibika kwa upande gani katika pambano kuu lililo mbele yao. Mama mwenye wasiwasi anauliza, "watakuwa na msimamo gani? Je! Ninaweza kufanya nini kuwaandaa kutenda vizuri sehemu yao, ili wawe wapokeaji wa utukufu wa milele? Wajibu mkubwa umelala juu yenu, akina mama. Ingawa huwezi kusimama katika mabaraza ya kitaifa, .. unaweza kufanya kazi kubwa kwa ajili ya MUNGU na nchi yako. Unaweza kuwaelimisha watoto wako. Unaweza kuwasaidia kukuza tabia ambazo hazitayumbishwa/hazitapindishwa au kushawishiwa kufanya uovu, lakini utashawishi na kushawishi wengine kutenda haki. Kwa maombi yako ya bidii na ya imani unaweza kuusogeza ule Mkono unaoongoza na kuusogeza ulimwengu.—(The Adventist Home, 264) [Pr 195.4; Maombi Aya ya 29]

Ushawishi wa mama anayeomba, na kumcha MUNGU utadumu milele. Anaweza kufa, lakini kazi yake itadumu. —(Testimonies for the Church 4:500) [Pr 196.1; Maombi Aya ya 30]

Endapo wakina mama wangetambua umuhimu wa utume wao, wangeshinda kwenye maombi ya siri, wakiwaleta watoto wao kwa Yesu, wakiomba baraka Zake juu yao, na kuomba hekima ya kutekeleza ipasavyo majukumu yao matakatifu. Hebu mama aboreshe kila fursa ya kuunda na kutengeneza tabia, mazoea na haiba za watoto wake. Hebu na atazame kwa uangalifu ukuaji wa tabia, akizuia mienendo inayojitokeza kwa ukubwa, akiwatia moyo wale walio na upungufu. Hebu afanye maisha yake mwenyewe kuwa mfano safi na mzuri kwa uongozi wake wa thamani. [Pr 196.2; Maombi Aya ya 31]

Mama anapaswa kuanza kazi yake kwa ujasiri na nishati/nguvu, akitegemea mara kwa mara msaada wa Bwana katika juhudi zake zote. Hapaswi kamwe kupumzika kwa kuridhika hadi aone katika watoto wake mwinuko wa tabia ya kwenda juu unaoeleweka, hadi wawe na lengo la juu zaidi maishani kuliko kujitafutia raha zao wenyewe. [Pr 196.3; Maombi Aya ya 32]

Haiwezekani kabisa kukadiria nguvu ya ushawishi wa mama anayesali. Anamkiri MUNGU katika njia zake zote. Anawachukua watoto wake mbele ya kiti cha neema na kuwakabidhi kwa Yesu, akiomba baraka Zake juu yao. Ushawishi wa maombi hayo ni "chemchemi ya uzima." kwa watoto hao. Maombi haya, yanayotolewa kwa imani, ni msaada na nguvu ya mama Mkristo. Kupuuza wajibu wa kuomba pamoja na watoto wetu ni kupoteza mojawapo ya baraka kuu zaidi zilizo karibu nasi, mojawapo ya silaha kuu katikati ya mashaka, masumbufu ya maisha, wasiwasi, na mizigo ya kazi yetu ya maisha. [Pr 196.4; Maombi Aya ya 33]

Nguvu ya maombi ya wakina mama haiwezi kukadiriwa kwa juu sana kama ilivyo. Yule anayepiga magoti kando ya mtoto wake wa kiume na wa kike kupitia mabadiliko na misukosuko ya utotoni, kupitia hatari za ujana, hatajua mpaka hukumu ifikapo ushawishi wa maombi yake juu ya maisha ya watoto wake. Ikiwa ameunganishwa kwa imani na Mwana wa MUNGU, mkono mwororo wa mama waweza kumzuia mwanawe dhidi ya nguvu za majaribu, unaweza kumzuia binti yake asiendekeze dhambi. Wakati tamaa za mwili zinapigania ustadi, nguvu za upendo, zenye kuzuia, zilizo dhati na zenye bidii za ushawishi wa mama ulioazimiwa, unaweza kuiegemeza roho upande wa haki. - (The Adventist Home, 265, 266) [Pr 197.1; Maombi Aya ya 34]

Maombi ya akina mama Wakristo hayapuuzwi na Baba wa wote, Yeye aliyemtuma Mwanawe duniani ili akomboe watu kwa ajili Yake. Hatayakataa maombi yako na kukuacha wewe na wako kwenye makombora ya Shetani katika siku ile kuu ya pambano la mwisho. Ni juu yako kufanya kazi kwa usahili na uaminifu, Naye MUNGU ataimarisha kazi ya mikono yako.—(Child Guidance, 526) [Pr 197.2; Maombi Aya ya 35]

Maombi ya Familia Ni Muhimu, Lakini Aina Nyingine za Maombi Zinahitajika Vilevile—Maombi ya Familia au ya hadhara pekee hayatoshi. Maombi ya siri ni muhimu sana; katika upweke nafsi inafunuliwa na kuanikwa wazi mbele ya jicho la MUNGU lichunguzalo, na kila nia inapekuliwa kwa karibu na kikamilifu. Maombi ya siri! Ni ya thamani sana! Nafsi inazungumza/inawasiliana na MUNGU! Maombi ya siri yanapaswa kusikilizwa na MUNGU tu anayesikia maombi. Hakuna sikio la udadisi litakalopokea mzigo wa maombi kama hayo.—Testimonies for the Church 2:189, 190. [Pr 197.3; Maombi Aya ya 36]

SURA YA 18

MAOMBI NA IBADA

Maombi na Ibada ni Muhimu kwa ajili ya Ukuaji wa Kiroho—Tafuta kila fursa ya kwenda mahali ambapo maombi yamezoeleka kufanywa (wana ratiba ya kufanya maombi). Wale ambao kweli wanatafuta ushirika na MUNGU wataonekana katika mkutano wa maombi, watakuwa waaminifu katika kufanya wajibu wao na kwa bidii na shauku kuvuna faida zote wanazoweza kuzipata. Wataboresha kila fursa ya kujiweka mahali ambapo wataweza kupokea miale ya nuru kutoka mbinguni. - (Steps to Christ, 98) [Pr 198.1; Maombi Aya ya 1]

Maombi ya faragha, maombi ya Familia, maombi katika mikusanyiko ya hadhara kwa ajili ya kumuabudu MUNGU, haya yote ni ya muhimu. Na tunapaswa kuyaishi maombi yetu. Tunapaswa kushirikiana na Kristo katika kazi Yake.—(Testimonies for the Church 7:239) [Pr 198.2; Maombi Aya ya 2]

Katika mikutano yetu ya ibada au kujitoa wakfu kwa Mungu, sauti zetu zapasa

zidhihirishe kwa maombi na kumsifu Mungu ibada yetu kwa Baba wa mbinguni, ili wote wajue kwamba tunamwabudu Mungu kwa urahisi/usahili na Kweli, na kwa uzuri wa utakatifu.— (Counsels to Parents, Teachers, and Students, 245) [Pr 198.3; Maombi Aya ya 3]

Makundi madogo na yajikusanye jioni, mchana au asubuhi na mapema ili kujifunza Biblia. Hebu wawe na msimu wa maombi, ili waweze kuimarishwa, kuangaziwa, na kutakaswa na Roho Mtakatifu. Kazi hii Kristo anataka kuifanya moyoni mwa kila mfanyakazi. Ikiwa ninyi wenyewe mtafungua mlango wa kuipokea, baraka kubwa itakuja kwenu. Malaika wa MUNGU watakuwa katika kusanyiko lenu. Mtakula majani ya mti wa uzima. Ni ushuhuda gani unaoweza kubeba juu ya mguso wa upendo uliofanywa na watendakazi wenzako katika misimu hii ya thamani wakati wa kutafuta baraka ya MUNGU. Hebu kila mmoja aeleze uzoefu wake kwa maneno rahisi. Hii italeta faraja na furaha zaidi katika nafsi kuliko vyombo vyote vya kupendeza vya ala za muziki vinavyoweza kuletwa makanisani. Kristo atakuja mioyoni mwenu. Ni kwa njia hii pekee ndipo unaweza kudumisha uadilifu wako.—(Testimonies for the Church 7:195) [Pr 198.4; Maombi Aya ya 4]

Jitayarishe kwa maisha ya mbinguni kwa ari na bidii ambayo bado hujawahi kuoionyesha maishani mwako mwote. Ielimishe akili yako kupenda Biblia, kupenda mkutano wa maombi, kupenda saa ya kutafakari, na zaidi ya yote, saa ambayo nafsi inawasiliana na MUNGU. Kuwa na mawazo ya kimbingu ikiwa siku moja utaungana na kwaya ya mbinguni katika majumba ya juu. —(Testimonies for the Church 2:267) [Pr 199.1; Maombi Aya ya 5]

Pale Roho wa MUNGU atakapofanya kazi juu ya moyo, akilisafisha hekalu la nafsi na unajisi/ushafu wake wa mambo ya kidunia na kupenda anasa, wote wataonekana katika mkutano wa maombi, wakiwa waaminifu kufanya wajibu wao na kwa dhati, ari, jitihada na shauku ya kuvuna faida zote wanazoweza kupata. Mfanyakazi mwaminifu kwa Bwana ataboresha kila fursa ya kujiweka moja kwa moja chini ya miale ya nuru kutoka katika kiti cha enzi cha MUNGU, na nuru hii itaakisiwa juu ya wengine.—(Testimonies for the Church 4:461) [Pr 199.2; Maombi Aya ya 6]

Uwepo wa MUNGU Hufanya Nyakati za Maombi na Ibada ya Hadhara Kuwa jambo takatifu—Uchaji wa kweli kwa MUNGU huchochewa na hisia ya ukuu Wake usio na kikomo na utambuzi wa uwepo Wake. Kwa hisia hii ya Yule Asiyeonekana, moyo wa kila mtoto unapaswa kuvutiwa sana. Saa na mahali pa maombi na huduma za ibada ya hadhara mtoto anapaswa kufundishwa kuona kuwa ni takatifu kwa sababu MUNGU Yuko pale. Na kadiri kicho kinavyoonyeshwa katika mtazamo na mwenendo, hisia inayoichochea itazidishwa. —(Education, 242, 243) [Pr 199.3; Maombi Aya ya 7]

Maombi ya hadhara Hutuleta Katika Uwepo wa MUNGU Mwenyewe –

Haijalishi ikiwa Maombi yatatolewa katika mkutano wa hadhara, kwenye madhabahu ya familia, au kwa siri, daima humweka mtu moja kwa moja mbele za MUNGU. Kwa maombi ya kudumu vijana wanaweza kupata kanuni zilizo thabiti/imara sana kiasi kwamba majaribu yenye nguvu zaidi hayatawavuta kutoka katika uaminifu wao kwa MUNGU.— (My Life Today, 18) [Pr 200.1; Maombi Aya ya 8]

Maombi ya Hadhara Hayapaswi Kuwa Marefu na makavu—Kama watoto wa Mfalme wa mbinguni, mnapaswa kujielimisha wenyewe kutoa ushuhuda kwa sauti iliyo wazi, inayotambulika, maneno yakitamkwa vizuri na kueleweka, na kwa namna ambayo mtu yeyote asiweze kuwa na hisia kwamba mnasitasita kuzungumza juu ya rehema za Bwana. Katika mkutano wa kijamii, sala inapaswa kutolewa ili wote waweze kujengwa, na wale wanaoshiriki katika zoezi hili wanapaswa kufuata mfano tuliopewa katika sala nzuri ya Bwana kwa ulimwengu. Sala ya Yesu ni rahisi/sahili, wazi, ya kina kwa kujumuisha kila kitu, lakini sio ndefu kiasi cha kukosa joto la kiroho (spiritless) kama yalivyo maombi makavukavu ambayo mara nyingi hutolewa hadharani. Maombi haya yasiyo na roho ndani yake bora yasitamkwe; kwani yanashindwa kubariki au kujenga, na ni mfumo tu bila nguvu muhimu. - (Christian Education, 129) [Pr 200.2; Maombi Aya ya 9]

Maombi yanayotolewa hadharani yanapaswa kuwa mafupi na kwenda kwenye vipengele vinavyohusika. MUNGU hatuhitaji tufanye msimu wa ibada kuwa wa kuchosha kwa maombi marefu.....Dakika chache zinatoshwa kwa sala yo yote ya kawaida kwenye halaiki. - (Evangelism, 146) [Pr 200.3; Maombi Aya ya 10]

Maombi yetu na mikutano ya kijamii vinapaswa kuwa nyakati za msaada maalum na kutia moyo. Kila mmoja ana kazi ya kufanya ili mikusanyiko hii iwe ya kupendeza na yenye faida iwezekanavyo. Hii inaweza kufanywa vizuri kwa kuwa na uzoefu mpya kila siku katika mambo ya MUNGU, na kwa kutosita kusema juu ya upendo Wake katika makusanyiko ya watu Wake. Msiporuhusu giza au ukafiri kuingia mioyoni mwenu, havitadhihirika katika mikutano yenu. [Pr 200.4; Maombi Aya ya 11]

Mikutano yetu inapaswa ifanywe kuwa ya kuvutia sana. Inapaswa na angahewa la manukato ya mbinguni. Wala kusiwe na hotuba ndefu, kavukavu na maombi ya mazoea, kwa sababu tu ya kutimiza muda . - (Christian Service, 211) [Pr 201.1; Maombi Aya ya 12]

Katika ibada ya familia hebu waachie watoto washiriki sehemu. Acha wote walete Bibilia zao na kila mmoja asome mstari mmoja au miwili. Kisha wimbo au tenzi fulani inayojulikana iimbwe, ikifuatiwa na maombi. Kwa hili, Kristo ametoa mfano. Sala ya Bwana haikukusudiwa kurudiwa tu kama mfumo au desturi fulani, lakini ni kielelezo cha jinsi maombi yetu yanavyopaswa kuwa-sahili/rahisi, ya bidii, na ya kina. Katika ombi rahisi mwambie Bwana mahitaji yako na onyesha

shukrani kwa rehema Zake. Kwa hivyo unamwalika Yesu kama mgeni aliyekaribishwa ndani ya nyumba na moyo wako. Katika familia maombi marefu kuhusu vitu vya mbali hayapaswi kuwepo. Vinafanya saa ya maombi kuwa ya kuchosha, wakati inapaswa kuzingatiwa kama fursa na baraka. Fanya msimu uwe wa kupendeza na wa kufurahisha. —(Child Guidance, 524) [Pr 201.2; Maombi Aya ya 13]

Mazungumzo ya muda mrefu na maombi marefu hayafai mahali popote, na haswa katika mkutano wa kijamii. Yanawachosha malaika, na vile vile watu wanaoyasikiliza. Maombi yetu yanapaswa kuwa mafupi, na ya moja kwa moja kwenye mada/pointi. Hebu Roho wa MUNGU iaae mioyoni mwa waabudio, Naye atafutilia mbali desturi zote na mambo duni (yanayoboesha).—Review and Herald, October 10, 1882) [Pr 201.3; Maombi Aya ya 14]

Dakika moja au mbili ni ndefu za kutosha kwa maombi yoyote ya kawaida. (Testimonies for the Church 2:581) [Pr 201.4; Maombi Aya ya 15]

Maombi marefu hufanya Ibada ichoshe — Katika kila familia kuwe na wakati uliowekwa wa ibada ya asubuhi na jioni. Inafaa kama nini kwa wazazi kukusanya watoto wao pamoja nao kabla ya chakula cha asubuhi, kumshukuru Baba wa mbinguni kwa ulinzi Wake wakati wa usiku, na kumwomba msaada Wake na mwongozo na utunzaji Wake wakati jua limetokezea kwa siku nzima! Inafaa kiasi gani, pia, jioni inapofika, kwa wazazi na watoto kukusanyika tena mbele Yake na kumshukuru kwa baraka za siku iliyopita! [Pr 201.5; Maombi Aya ya 16]

Baba, au, akiwa hayupo, mama, anapaswa kuongoza ibada, akichagua sehemu ya Maandiko yenye kupendeza na kueleweka kwa urahisi. Huduma inapaswa kuwa fupi. Wakati sura ndefu inasomwa na maombi ya muda mrefu yakatolewa, huduma hufanywa kuwa ya kuchosha (kuboesha), na katika kumalizika kwake hisia ya unafuu/afueni husikika. MUNGU huaibishwa na kukosewa heshima wakati saa ya ibada inapofanywa kuwa kavukavu na ya kuwakasirisha (kuwasumbua moyoni) wana familia, inapokuwa kama shuguli nzito sana, ikapungukiwa na shauku, kiasi kwamba hata watoto wanaiogopa kwa kuifikiria kabla hata hawajaitwa kuja kushiriki. [Pr 202.1; Maombi Aya ya 17]

Akina baba na akina mama, fanyeni saa ya kuabudu ipendeze sana. Hakuna sababu kwa nini saa hii isiwe ya kupendeza na kufurahisha zaidi ya siku hiyo. Kutafakari kwa kiasi kunakofanywa katika maandalizi yake kutakuwezesha kuifanya iwe kamilifu, ya kuvutia na ya faida. Mara kwa mara huduma iwe na utofauti (mambo anuwai). Maswali yanaweza kuulizwa kwenye sehemu ya Maandiko yaliyosomwa, na majibu machache ya dhati, ya wakati unaofaa yanaweza kutolewa. Wimbo wa sifa unaweza kuimbwa. Ombi linalotolewa linapaswa kuwa fupi na la moja kwa moja (lisipindepinde). Katika maneno rahisi, na yaliyo dhati, basi yule anayeongoza katika maombi amsifu MUNGU kwa wema Wake na amwombe msaada. Kadiri hali inavyoruhusu, hebu watoto wajiunge

katika usomaji na sala. [Pr 202.2; Maombi Aya ya 18]

Ulimwengu ujao, mbinguni ndio pekee utakaofunua wema ambao majira hayo ya ibada yamejazwa na huo. —(Testimonies for the Church 7:43, 44) [Pr 202.3; Maombi Aya ya 19]

Maombi yetu hadharani yanapaswa kuwa mafupi, na yaeleze tu matakwa halisi ya roho, tukiomba katika urahisi na kwa imani rahisi ya kuamini kwa ajili ya vitu tunavyohitaji. Maombi kutoka kwenye moyo mnyenyekevu, uliopondeka ni pumzi muhimu ya roho iliyo na kiu ya haki. - (The Signs of the Times, Desemba 3, 1896) [Pr 202.4; Maombi Aya ya 20]

Kutokana na nuru niliyonayo juu ya suala hili, nimefikia maamuzi kuwa MUNGU katika ibada yake tunapokusanyika, hahitaji ziwe nyakati ndefu, zisizopendeza (zinazoboesha), za kuchosha kwa watu kubaki wameinama kwa muda mrefu wakisikiliza maombi kadhaa marefu. Wenye afya dhaifu hawawezi kuvumilia usumbufu wa namna hii bila kuchoka sana na hata kuishiwa nguvu. Mwili huchoka kwa kuendelea kuinama kwa muda mrefu; na mbaya zaidi ni kwamba, akili huchoshwa na zoezi hilo la maombi endelevu yasiyotoa burudisho la kiroho na mkutano wa namna hiyo ni mbaya kuliko mtu aliyepata hasara. Watu huchoka kiakili na kimwili na hawajapata nguvu za kiroho. [Pr 202.5; Maombi Aya ya 21]

Mikutano ya makongamano na maombi isifanywe kuwa ya kuchosha. Ikiwezekana, yote inapaswa kuzingatia saa iliyowekwa; na ikiwa kuna watu wanaopenda kujichelewesha chelewesha na kupoteza muda, wale ambao huchelewa kwa nusu saa au hata dakika kumi na tano nyuma ya wakati, hawapaswi kusubiriwa. Ikiwa wako hata watu wawili tu, hawa wanaweza kuanza mkutano kwa kudai ahadi. [Pr 203.1; Maombi Aya ya 22]

Mkutano unapaswa kufunguliwa kwenye saa iliyopangwa kadiri inavyowezekana, iwe wamehudhuria wengi au wachache. Desturi au mapokeo na ubaridi uliokakamaa unapaswa kuwekwa kando, na wote wanapaswa kuwajibika katika jukumu. Katika matukio ya kawaida kusiwe na maombi ya zaidi ya dakika kumi. Baada ya kuwepo mabadiliko la nafasi, na zoezi la uimbaji au mashauri limefurahiwa sawa, basi, ikiwa yeyote anahisi mzigo wa ombi, basi na aombe. [Pr 203.2; Maombi Aya ya 23]

Wote wanapaswa kuhisi kuwa ni jukumu la Mkristo kuomba kwa kifupi. Mwambie Bwana kile unachotaka, bila kurandaranda/kumangamanga ulimwenguni kote. Katika maombi ya faragha wote wana nafasi ya kuomba kadiri ya matamanio yao na kuwa wazi kama watakavyo. Wanaweza kuwaombea ndugu zao na marafiki. Chumbani au mahali pa faragha, ni mahali pa kusema shida zao zote za binafsi, na mitihani/magumu, na majaribu. Mkutano wa pamoja wa kumwabudu MUNGU si mahali pa kufungua mambo ya kibinafsi ya moyoni. [Pr 203.3; Maombi Aya ya 24]

Lengo la kukusanyika pamoja ni nini? Je! Ni kumjulisha MUNGU, kumfundisha kwa kumwambia yote tunayojua katika maombi? Tunakutana pamoja ili kujengana sisi kwa sisi kwa kubadilishana mawazo na hisia, kukusanya nguvu, na mwanga, na ujasiri kwa kufahamiana sisi kwa sisi kuhusu matumaini na matarajio ya kila mmoja wetu; na kwa sala zetu dhati, za bidii, na za kutoka moyoni zinazotolewa kwa imani, tunapata burudisho na nguvu kutoka kwenye Chanzo cha nguvu zetu. Mikutano hii inapaswa kuwa misimu ya thamani zaidi na inapaswa kufanywa iwe ya kuvutia kwa wote ambao wana shauku yoyote ya mambo ya kidini. [Pr 203.4; Maombi Aya ya 25]

Kuna wengine, nina hofu kwamba hawapeleki shida zao kwa MUNGU katika maombi ya faragha, lakini wanayahifadhi au kuyalimbikiza kwa ajili ya mkutano wa maombi, na hapo hufanya maombi yao kwa siku kadhaa. Watu hao wanaweza kuitwa wauaji wa mikutano na maombi (prayer and conference killers). Hawatoi nuru; hawamjengi mtu. Maombi yao ya baridi na marefu, yaliyoganda barafu na shuhuda zao ndefu, za kurudi kwao nyuma zinawekea watu kivuli. Wote wanafurahi wanapomaliza, na ni vigumu kuutupilia mbali ubaridi na giza ambalo maombi, hotuba au mawasiliano yao huleta kwenye mkutano. Kutoka katika nuru ambayo nimeipokea, mikutano yetu inapaswa kuwa ya kiroho na ya kijamii (kirafiki na mahusiano-social), na sio mirefu sana. Kukosa roho ya urafiki au kuwaweka watu mbali nawe, kiburi, ubatili, na hofu kwa mwanadamu vinapaswa kuachwa nyumbani. Tofauti ndogo na chuki haipaswi kwenda nasi kwenye mikutano hii. Kama ilivyo katika familia yenye umoja, usahili, unyenyekevu, upole, ujasiri, na upendo vinapaswa kuwepo mioyoni mwa akina kaka na dada ambao wanakutana ili kuburudishwa na kuongezewa nguvu kwa kuleta mianga yao pamoja. - (Testimonies for the Church 2: 578, 579) [Pr 203.5; Maombi Aya ya 26]

Maombi ya Hadhara yanapaswa kutamkwa kwa upekee na Kwa Uwazi—Hebu wale wanaoomba na wale wanaozungumza wayatamke maneno yao kwa upekee ili kuyatofautishanisha na kusema kwa uwazi, kwa upekee, bila kuchanganya maneno, na kwa sauti yenye toni nzuri. Ombi, Likitolewa ipasavyo, ni nguvu ya mema. Ni njia mojawapo inayotumiwa na Bwana kuwasilisha kwa watu hazina muhimu za Ukweli. Lakini Ombi haliwi kama linavyopaswa kuwa, kwa sababu ya sauti zenye kasoro za wale wanaolitamka. Shetani hufurahi wakati maombi yanayotolewa kwa MUNGU yanatolewa kwa sauti ya chini, na hivyo maneno kutoeleweka au kusikika. Hebu watu wa MUNGU wajifunze jinsi ya kuongea na kuomba kwa njia ambayo itawakilisha ipasavyo zile Kweli kuu walizonazo. Hebu shuhuda zilizobebwa na maombi yaliyotolewa viwe wazi na neno kwa neno litofautianishwe. Na kisha MUNGU atatukuzwa. —(Testimonies for the Church 6:382) [Pr 204.1; Maombi Aya ya 27]

Tumia Lugha Rahisi Unapoomba Hadharani—Lugha ya madoido mengi, misamiati mipya mingi, sauti ya juu yenye kujieleza sana na ya kutia chumvi haifai katika sala (highflown), iwe ombi hilo linatolewa mimbarani, katika

mzunguko wa familia, au kwa siri. Hasa kwa yule anayetoa ombi la hadharani anapaswa kutumia lugha rahisi, ili wengine waelewe yanayosemwa na kuungana katika ombi hilo. [Pr 204.2; Maombi Aya ya 28]

Ni ombi la imani linalotoka moyoni ambalo husikika mbinguni na kujibiwa duniani.—(Gospel Workers, 177) [Pr 204.3; Maombi Aya ya 29]

Maombi yetu yanapaswa kuwa ya utaratibu - Nimeona kwamba machafuko hayampendezi Bwana, na kwamba kuwe na utaratibu katika kuomba na pia katika kuimba. Hatupaswi kwenda nyumbani kwa MUNGU kuziombea familia zetu isipokuwa hisia za ndani zitatuongoza wakati Roho wa MUNGU anawasadikisha wale wanaoombewa kule waliko. Kwa ujumla, mahali sahihi pa kuomba familia zetu ni kwenye madhabahu ya familia. Wakati mada za maombi yetu ziko mbali, mahali pa siri ni mahali pazuri pa kumuomba MUNGU kwa ajili ya mada hizo. Tunapokuwa katika nyumba ya MUNGU, tunapaswa kuomba baraka iliyopo na tunapaswa kutarajia MUNGU kusikia na kujibu maombi yetu. Mikutano kama hiyo itakuwa ya uchangamfu na ya kuvutia.— (Testimonies for the Church 1:145, 146) [Pr 204.4; Maombi Aya ya 30]

Mungu Anapaswa kukaribiwa kwa kicho Katika Sala— Wengine hufikiri kuwa ni alama ya unyenyekevu kusali kwa MUNGU kwa njia ya mazoea au ya kawaida, kama vile wanavyozungumza na mwanadamu wenzao. Wanalichafua Jina Lake kwa kuchanganya pamoja bila ulazima na bila kicho sala zao maneno, “MUNGU Mwenyezi,” Maneno matakatifu ya kutisha, ambayo hayapaswi kamwe kutoka midomoni mwao isipokuwa kwa sauti iliyotiishwa na kwa hisia ya kicho, inayohisi utukufu na utakatifu wa Mungu.— (Gospel Workers, 176) [Pr 205.1; Maombi Aya ya 31]

Ni Fursa Yetu Kupiga Magoti Tunapoomba Hadharani—Katika ibada ya hadhara na faraghani ni wajibu wetu kupiga magoti mbele za MUNGU tunapotoa maombi yetu Kwake. Tendo hili linaonyesha utegemezi wetu kwa MUNGU.—(Selected Messages 2:312) [Pr 205.2; Maombi Aya ya 32]

Kulingana na nuru ambayo imeletwa kwangu, ingempendeza MUNGU kwa wahudumu kupiga magoti mara tu wanapoingia kwenye mimbari, na kwa kicho waombe msaada kutoka kwa MUNGU. Je, hilo lingeleta hisia ya namna gani? Kungekuwa kicho na angahewa yenye utakatifu na mshangao juu ya watu. Mhudumu wao anazungumza na MUNGU; anajitoan wakfu kwa MUNGU kabla hajathubutu kusimama mbele ya watu. Utii upo juu ya watu, na malaika wa MUNGU wanaletwa karibu sana. Wahudumu wanapaswa kumtazama MUNGU kwanza wanapoenda kwenye kibweta, na hivyo kuwaambia wote: MUNGU Ndiye chanzo cha nguvu zangu. — (Testimonies for the Church 2:612) [Pr 205.3; Maombi Aya ya 33]

Pale mhudumu anaingia, yapaswa kuwe na heshima, na kicho katika mwenendo na mwonekano. Anapaswa kuinama katika sala ya kimya mara tu

atakapoingia kwenye mimbari, na kuomba kwa bidii msaada wa MUNGU. Ni hisia gani italetwa na jambo hili! Kutakuwa na taadhimu na utukufu kwenye angahewa la watu. Mhudumu wao anazungumza na MUNGU; anajitoa wakfu kwa MUNGU kabla hajathubutu kusimama mbele ya watu. Kicho kinatawala juu ya watu, na malaika wa MUNGU wanaletwa karibu sana. Kila mmoja katika kusanyiko, pia, anayemcha MUNGU anapaswa kuungana naye kwa kuinamisha kichwa chake katika sala ya kimya ili MUNGU atoe neema Yake kwa kutano hilo kwa uwepo wake na kuupa nguvu Ukweli Wake unaotangazwa/unaohubiriwa kutoka katika midomo ya wanadamu. Mkutano unapofunguliwa kwa maombi, kila goti linapaswa kupigwa mbele ya Yule Mtakatifu, na kila moyo unapaswa kupaa kwa MUNGU katika ibada ya kimya. Maombi ya waumini waaminifu yatasikilizwa, na huduma ya Neno itathibitika kuwa yenye ufanisi. Mtazamo usio na uhai wa waumini katika nyumba ya MUNGU ni sababu moja kuu ya sababu ya huduma kukosa matokeo mazuri zaidi. Sauti ya wimbo, unaomiminwa kutoka katika mioyo mingi katika usemi ulio wazi na wa kipekee, ni mojawapo ya nyenzo za MUNGU katika kazi ya kuokoa roho. Huduma zote zinapaswa kuendeshwa kwa kicho na utii, kana kwamba tu mbele ya Yule Mkuu wa makusanyiko. —(Testimonies for the Church 5:492, 493) [Pr 205.4; Maombi Aya ya 34]

Hadharani na katika ibada binafsi ni fursa yetu kupiga magoti mbele za MUNGU tunapotuma maombi yetu. Yesu, mfano wetu, "alipiga magoti na kuomba." Luka 22:41. Juu ya wanafunzi Wake imeandikwa kwamba wao pia, "walipiga magoti na kuomba." Matendo 9:40. Paulo alitangaza, "Ninampigia Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo magoti." Waefeso 3:14. Katika kuungama mbele za MUNGU dhambi za Israeli, Ezra alipiga magoti. Tazama Ezra 9: 5. Danieli "alipiga magoti mara tatu kwa siku, akasali, na akashukuru mbele za MUNGU wake." Danieli 6:10.—(Prophets and Kings, 48) [Pr 206.1; Maombi Aya ya 35]

Maombi ya halaiki ni muhimu lakini hayajitoshelezi yenyewe- sala ya familia au ya umma tu haitoshi. Maombi ya siri ni muhimu sana; katika upweke nafsi inafunuliwa wazi mbele ya jicho la MUNGU lichunguzalo, na kila nia inapekuliwa na kuchunguzwa. Maombi ya siri! Yana thamani iliyoje! Nafsi inazungumza na MUNGU! Maombi ya siri yanapaswa kusikilizwa tu na MUNGU anayesikia maombi. Hakuna sikio lenye udadisi linalopaswa kupokea mzigo wa maombi kama hayo (hakuna mmbeya anayepaswa kusikia ya wengine pia!).—Testimonies for the Church 2:189, 190. [Pr 206.2; Maombi Aya ya 36]

SURA YA 19

MTAZAMO KATIKA MAOMBI

Mkao inayofaa kwa ajili ya Maombi ya hadhara— Nimepokea barua zinazoniuliza kuhusiana na mkao mzuri wa kuchukuliwa na mtu anayetoa ombi kwa Mfalme wa ulimwengu (universe). Ndugu zetu wamepata wapi wazo kwamba wanapaswa kusimama kwa miguu yao wakati wa kuomba kwa MUNGU? Mtu ambaye amesomea/ameshomeshwa kwa takribani miaka mitano huko Battle Creek aliombwa aongoze kwa ombi kabla Dada White hajazungumza na watu. Lakini nilipomwona amesimama wima kwa miguu yake wakati midomo yake ilikuwa karibu kufunguka katika kutoa maombi kwa MUNGU, roho yangu ilisumbuliwa sana ndani kumpa karipio la wazi. Basi nikamwita kwa jina, na kumwambia, "Piga magoti." Huu ndio msimamo (mkao) sahihi wa mwili kila wakati [Pr 207.1; Maombi Aya ya 1]

Kupiga magoti wakati wa kuomba kwa MUNGU ndio mtazamo/tabia inayofaa kuwa nayo. Tendo hili la ibada lilitakiwa kwa wale mateka watatu wa Kiebrania kule Babeli Lakini tendo kama hilo la ibada, lilipaswa kutolewa kwa MUNGU peke yake— Mtawala Mkuu wa ulimwengu, Mtawala wa ulimwengu wote mzima (mbingu na sayari zote); na hawa Waebrania watatu walikataa kutoa heshima hiyo kwa sanamu yoyote ijapokuwa ilifanyizwa kwa dhahabu safi. Kwa kufanya hivyo, wangukuwa, kwa nia na makusudio yote, wamemsujudia mfalme wa Babeli. Kwa kukataa kufanya kama mfalme alivyoamuru, walipata adhabu, na wakatupwa ndani ya tanuru inayowaka moto. Lakini Kristo alikuja Mwenyewe na kutembea pamoja nao kwenye moto, nao hawakupata madhara yoyote. [Pr 207.2; Maombi Aya ya 2]

Hadharani na katika ibada binafsi, pote hapa ni wajibu wetu kupiga magoti mbele za MUNGU tunapotuma maombi yetu Kwake. Tendo hili linaonyesha utegemezi wetu kwa MUNGU [Pr 208.1; Maombi Aya ya 3]

"Ni wapi Ndugu H alipata elimu yake?" Huko Battle Creek. Je, inawezekana kwamba kwa nuru yote ambayo MUNGU amewapa watu Wake juu ya somo la uchaji na kicho, kwamba wahudumu, wakuu, na walimu katika shule zetu, kwa kanuni na mifano, wafundishe vijana kusimama wima katika ibada kama

walivyofanya Mafarisayo? Je! Tulitazame hili jambo muhimu katika linaloashiria kujitosheleza kwao wenyewe na kujithamini wenyewe kwamba wao ndiyo bora? Je, sifa hizi zinapaswa kuonekana wazi na kukuzwa zaidi? [Pr 208.2; Maombi Aya ya 4]

Tunatumaini kwamba ndugu zetu hawataonyesha heshima na kicho kidogo wanapomkaribia MUNGU wa pekee wa Kweli na Aliye Hai kuliko wapagani wanavyoitendea na kujidhihirisha kwa miungu yao ya sanamu, la sivyo watu hawa watakuwa waamuzi wetu katika siku ya hukumu ile ya mwisho. Ngingezungumza na wote wanaoshika nafasi ya waalimu katika shule zetu. Wanaume na wanawake, msimdharau MUNGU kwa kutomheshimu kwenu kwa kujigamba, huku mkijionyesha ufahari na umuhimu wenu. Usisimame katika Ufarisayo wako na kutoa maombi yako kwa MUNGU. Usiamini nguvu zako mwenyewe. Usizitegemee; lakini mara kwa mara pigeni magoti mbele za MUNGU, na mmwabudu Yeye. [Pr 208.3; Maombi Aya ya 5]

Na mnapokusanyika kumwabudu Mwenyezi MUNGU, hakikisheni mnapiga magoti. Hebu tendo hili lishuhudie kwamba nafsi yote, mwili, na roho ziko chini ya Roho wa Kweli. Ni akina nani ambao wamechunguza Neno kwa ukaribu kuona mifano na mwelekeo katika suala hili? Je! Ni akina nani tunaoweza kuwaamini kama waalimu katika shule zetu Amerika na nchi za nje? Baada ya miaka ya mafunzo, wanafunzi watarudi katika nchi yao wenyewe wakiwa na mawazo ya ukengeufu/potofu kuhusiana na adabu, kicho na staha anayopaswa kupewa MUNGU, na kisha wasijisikie kuwa hawako chini ya wajibu wa kuheshimu wale watu wenye mvi (wazee), watu wenye uzoefu, watumishi waliochaguliwa na MUNGU ambao wameunganishwa na kazi ya MUNGU kwa takribani miaka yote ya maisha yao? Ninashauri wote wanaosoma shule za Marekani au mahali pengine popote, wasiidake roho ya kukosa kicho. Hakikisha wewe mwenyewe unaelewa fika ni aina gani ya elimu unayohitaji, ili uweze kuelimisha wengine wapate kufaa kwa tabia ambayo itahimili mtihani ambao utawajia upesi wale wote wanaoishi duniani. Shirikiana na Wakristo wenye hekima na maadili mema kupita wote. Usiwachague wakufunzi au wanafunzi wenye kujifanya (feki), bali wale wanaoonyesha utauwa wa ndani kabisa, wale walio na roho ya ufahamu katika mambo ya MUNGU. [Pr 208.4; Maombi Aya ya 6]

Twaishi katika nyakati za hatari. Waadventista wa Sabato wanasemekana ni watu wa MUNGU wanaotunza amri Zake; lakini wanapoteza roho yao ya ibada (pia roho ya kujitoa wakfu). Roho hiyo ya kuwa na kicho kwa MUNGU huwafundisha wanadamu jinsi ya kumkaribia Muumba wao—kwa utakatifu na kicho kupitia imani, si ndani yao wenyewe, bali kwa kupitia Mpatanishi. Kwa hivyo mwanadamu huwekwa imara, chini ya hali yoyote ambayo anakutana nayo. Mwanadamu lazima apige magoti, kama mnufaika wa neema, mwombaji aliye chini ya kiti cha rehema. Na anapoendelea kupokea rehema za kila siku kutoka katika mkono wa MUNGU, daima anapaswa kutunza shukrani moyoni mwake, na

kuionyesha au kuidhihirisha kwa maneno ya shukrani na sifa kwa ajili ya neema hizi asizostahili. Malaika wamekuwa wakilinda njia yake katika maisha yake yote, na mitego mingi iliyojificha ambayo yeye ameepushwa dhidi yake hajaiona. Na kwa ajili ya uangalizi huu na ulinzi wa macho ambayo hayasinzii wala hayalali kamwe, anapaswa kutambua katika kila ombi utumishi wa MUNGU kwa ajili yake.—(Selected Messages 2:311-315) [Pr 209.1; Maombi Aya ya 7]

Kupiga Magoti Katika Maombi Hufunza Heshima na Kumcha MUNGU na kustaajabia Utukufu Wake— Hebu MUNGU na awafundishe watu Wake jinsi ya kuomba. Hebu walimu katika shule zetu na wahudumu katika makanisa yetu, wajifunze kila siku katika shule ya Kristo. Ndipo wataomba kwa bidii, na maombi yao yatasikilizwa na kujibiwa. Ndipo Neno litatangazwa kwa nguvu. [Pr 209.2; Maombi Aya ya 8]

Kote hadharani na katika ibada binafsi ni wajibu wetu kupiga magoti mbele za MUNGU tunapoyaleta maombi yetu Kwake. Yesu, mfano wetu, "alipiga magoti na kuomba." Juu ya wanafunzi Wake." Imelandikwa kwamba wao pia, "walipiga magoti na kuomba." Paulo alitangaza, "Ninampigia Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo magoti." Katika kuungama mbele za MUNGU dhambi za Israeli, Ezra alipiga magoti. Danieli "alipiga magoti mara tatu kwa siku, akasali, na kushukuru mbele za MUNGU wake." [Pr 209.3; Maombi Aya ya 9]

Kumcha MUNGU katika kweli kunachochewa na hisia ya ukuu Wake usio na kipimo na utambuzi wa uwepo Wake. Kwa hisia hii ya Yule Asiyeonekana, kila moyo unapaswa kuvutiwa sana. Saa na mahali pa maombi ni vitakatifu, kwa sababu MUNGU Yupo; na kadiri heshima na kicho inavyodhihirika katika tabia na mwenendo, hisia inayovichochea itazidishwa." Jina Lake ni takatifu na la kuogopwa," mwandishi wa zaburi anatangaza. Malaika, wanaponena Jina hilo, hufunika nyuso zao. Kwa heshima gani, basi, sisi ambao tumeanguka na ni wenye dhambi, tunapaswa kulichukua kwenye midomo yetu! [Pr 209.4; Maombi Aya ya 10]

Naam Ingekuwa vema kwa wazee na vijana kutafakari Maneno hayo ya Maandiko yanayoonyesha jinsi mahali palipotiwa alama ya uwepo wa pekee kwa MUNGU panavyopaswa kuzingatiwa. "Vua viatu vyako miguuni mwako," Alimwamuru Musa kwenye kichaka kinachowaka moto, "kwa kuwa mahali hapo uilipo simama ni ardhi takatifu." Yakobo, baada ya kuona maono ya malaika, akasema, "Bwana Yuko mahali hapa; na sikuijua Hapa si mahali pengine bali nyumba ya MUNGU, na hili ndilo lango la mbinguni." Gospel Workers, 178, 179) [Pr 210.1; Maombi Aya ya 11]

Unyenyekevu wa Sulemani wakati alipoanza kubeba mizigo ya serikali, alipokiri mbele za MUNGU, "Mimi ni mtoto mdogo tu" (1 Wafalme 3:7), upendo wake wa ajabu kwa MUNGU, kicho na heshima yake kuu kwa mambo ya Bwana, kutojamini kwake ndani ya nafsi yake, na kumwinua kwake Muumba wa yote

asiye na kikomo— mienendo yote hii ya tabia, zinazostahili kuigwa sana, zilifichuliwa wakati huduma ya ibada zilizounganishwa na ukamilishaji wa ujenzi wa hekalu, wakati wa maombi yake ya kuweka wakfu hekalu alipiga magoti katika mkao/nafasi ya unyenyekevu ya mwombaji. Wafuasi wa Kristo leo wanapaswa kujilinda dhidi ya mwelekeo wa kupoteza roho ya staha na hofu ya kimungu. Maandiko huwafundisha wanadamu jinsi wanavyopaswa kumwendea/kumsogelea Muumba wao—kwa unyenyekevu na kicho, kupitia imani katika Mpatanishi wa Kiungu.—(Prophets and Kings, 47, 48) [Pr 210.2; Maombi Aya ya 12]

"Katikati mwa ua" wa hekalu alikuwa ameweka "jukwaa la shaba," au jukwaa, "urefu wa mikono mitano, na upana wa mikono mitano, na urefu wa mikono mitatu." Juu yake Sulemani alisimama na kwa mikono iliyoinuliwa alibariki umati mkubwa mbele yake. "Na mkutano wote wa Israeli wakasimama." 2 Mambo ya Nyakati 6:13, 3. [Pr 210.3; Maombi Aya ya 13]

"Asifiwe Bwana, Mungu wa Israeli," Sulemani akasema, "ambaye kwa mikono yake ametimiza kile alichosema kwa kinywa chake kwa baba yangu Daudi, akisema, Nimeichagua Yerusalemu, ili Jina Langu liwe hapo." Aya ya 4-6. [Pr 210.4; Maombi Aya ya 14]

Ndipo Sulemani akapiga magoti juu ya jukwaa la shaba, na katika usikivu wa watu wote alitoa ombi la kuweka wakfu hekalu. Akiinua mikono yake mbinguni, huku kutaniko likiwa limeinama kifudifudi (sura zao zikiwa kwenye sakafu), mfalme alisihi: "Bwana, MUNGU wa Israeli, hakuna MUNGU kama Wewe mbinguni, wala duniani; ushikaye maagano, na kuwarehemu watumishi Wako, waendao mbele Zako kwa mioyo yao yote.—(Prophets and Kings, 39, 40) [Pr 211.1; Maombi Aya ya 15]

Mfalme Sulemani alisimama juu ya jukwaa la shaba mbele ya madhabahu na kuwabariki watu. Kisha akapiga magoti na, akiwa ameinua mikono yake juu, akamimina sala ya dhati na kujitoa wakfu kwa MUNGU huku makutano wakiwa wameinamisha nyuso zao chini kwenye ardhi. Baada ya Sulemani kumaliza sala yake, moto wa miujiza ukatoka mbinguni na kuteketeza dhabihu hiyo.—(The Story of Redemption, 194) [Pr 211.2; Maombi Aya ya 16]

Mmepewa akili ili muweze kuelewa jinsi ya kufanya kazi. Mmepewa macho ili muweze kuwa makini katika kuzitambua fursa mlizopewa na MUNGU. Masikio yenu yasikilize maagizo ya MUNGU. Magoti yenu yanapaswa kupigwa mara tatu kwa siku katika maombi yanayoyotoka moyoni. Miguu yenu na itembee katika njia ya amri za MUNGU.—(Testimonies for the Church 6:297) [Pr 211.3; Maombi Aya ya 17]

Wahudumu wapige Wagoti kuomba kabla ya Kuhubiri- Kulingana na nuru ambayo nimepewa, ingempendeza MUNGU kwa wahudumu kupiga magoti mara tu wanapoingia kwenye mimbari, na kwa dhati kuomba msaada kutoka kwa

MUNGU. Je, hilo lingeleta hisia za ajabu namna gani? Kungekuwa kicho na hofu ya utukufu wa Mungu juu ya watu. Mhudumu wao anawasiliana na MUNGU; anajitoa wakfu kwa MUNGU kabla hajathubutu kusimama mbele ya watu. Kicho kinahisiwa juu ya watu, na malaika wa MUNGU wanaletwa karibu sana. Wahudumu wanapaswa kumtazama MUNGU, mara tu wanapoingia kwenye kibweta, na hivyo kuwaambia wote: MUNGU Ndiye chanzo cha nguvu zangu.— (Testimonies for the Church 2:612) [Pr 211.4; Maombi Aya ya 18]

Wakati mhudumu anaingia, yapaswa kuwe na kicho, taadhima na hadhi/heshima. Mhubiri anapaswa kuinama na kupiga magot katika sala ya kimya mara tu atakapoingia kwenye mimbari, na kuomba msaada kwa MUNGU kwa bidii. Ni hisia ya namna gani italetwa kwa watu kwa kufanya jambo hili! Kutakuwa na kicho na hofu ya Mungu juu ya watu. Mhudumu wao anazungumza na MUNGU; anajitoa kwa MUNGU kabla hajathubutu kusimama mbele ya watu. Kicho kitahisiwa juu ya watu, na malaika wa MUNGU wanaletwa karibu sana. Kila mmoja katika kusanyiko pia, anayemcha MUNGU anapaswa kuungana naye kwa kuinamisha kichwa chake katika sala ya kimya ili MUNGU ajaze neema kutano hilo kwa uwepo Wake na kuupa nguvu Ukweli Wake unaotangazwa kutoka katika midomo ya wanadamu. Mkutano unapofunguliwa kwa maombi, kila goti linapaswa kupigwa mbele ya Yule Aliye Mtakatifu, na kila moyo unapaswa kupanda juu kwa MUNGU katika ibada ya kimya. Maombi ya waumini waaminifu yatasikilizwa, na huduma ya Neno itathibitika kuwa yenye ufanisi. Mtazamo usio na uhai wa waumini katika nyumba ya MUNGU ni sababu moja kuu ya kwa nini huduma inakosa matunda mazuri zaidi. Sauti ya wimbo, unaomiminwa kutoka katika mioyo mingi katika usemi ulio wazi, unaoleweka maana yake mtu atamkapo maneno na wa kipekee, ni mojawapo ya vifaa vya MUNGU katika kazi ya kuokoa roho. Huduma zote zifanyike kwa kicho na hofu, kama ni katika uwepo dhahiri wa Bwana wa makutano.—(Testimonies for the Church 5:492, 493) [Pr 211.5; Maombi Aya ya 19]

Kupiga Magoti si lazima mara zote Wakati wa kuomba— Hatuwezi daima kuwa magotini katika sala, lakini njia ya kuelekea kiti cha rehema iko wazi sikuzote. Tunapoendelea na kazi ya inayoshugulisha sana, tunaweza kuomba msaada; na tumeahidiwa na Yule ambaye hatatudanganya, "Mtapokea." Mkristo anaweza na atapata muda wa kuomba. Danieli alikuwa Kiongozi wa taifa; majukumu mazito yalikuwa juu yake; lakini alimtafuta MUNGU mara tatu kwa siku, na Bwana akampa Roho Mtakatifu. Kwa hiyo leo wanadamu wanaweza kukimbilia kwenye hema takatifu la Yeye Aliye Juu Zaidi na kuhisi uhakikisho wa ahadi Yake, "Watu Wangu watakaa katika mkao wa amani, na katika maskani zilizo salama, na mahali pa kupumzika penye utulivu." Isaya 32:18. Wote wanaotamani wanaweza kupata mahali pa ushirika na MUNGU, ambapo hakuna sikio linaloweza kusikia ila Lile lililo wazi kwa ajili ya vilio vya wasiojiweza, wenye huzuni na wahitaji—Yule anayeona hata kuanguka kwa shomoro (ndege wadogo

wenye rangi nyeupe, nyeusi, kijivu na kahawia ambao rangi hayo haivutii sana-sparrow). Anasema, "Ninyi ni wa thamani kuliko shomoro wengi." Mathayo 10:31.—(Counsels on Health, 423, 424) [Pr 212.1; Maombi Aya ya 20]

Sababu kwa nini wengi wameachwa peke yao katika maeneo ya majaribu ni kwamba hawakumweka Bwana mbele yao daima. Tunaporuhusu ushirika wetu na MUNGU uvunjwe, ulinzi wetu unatoweka kwetu. Siyo madhumuni yako yote mazuri na nia njema ndiyo vitakuwezesha kuhimili uovu. Lazima muwe wanaume na wanawake wa maombi. Maombi yenu hayapaswi kuzimia, kuwa ya msimu hapa na pale unapoamua, na ya kuzimiana kuamka kama kifafa, bali ya bidii, ya kudumu, na ya daima. Si lazima kila wakati kupiga magoti ili kuomba. Kuza tabia ya kuzungumza na Mwokozi unapokuwa peke yako, unapotembea, na unapokuwa na shughuli nyingi zinazohusiana na kazi zako ya kila siku. Acha moyo uinuliwe kila wakati katika ombi la kimya la msaada, kwa ajili nuru, nguvu, ufahamu na maarifa. Hebu kila pumzi na iwe sala.—(The Ministry of Healing, 510, 511) [Pr 213.1; Maombi Aya ya 21]

Katika kazi ya kutunza mioyo ni lazima tuwe na utayari katika sala, bila kuchoka katika kukiomba kiti cha neema kwa ajili ya msaada. Wale ambao huchukua jina la "Mkristo" wanapaswa kumjia MUNGU kwa dhati na unyenyekevu, wakisihia msaada. Mwokozi ametuambia tuombe bila kukoma. Mkristo hawezi kuwa katika mkao wa kuomba kila wakati, lakini mawazo na matamania yake yanaweza kupanda kuelekea juu kila wakati. Kujiamini nafsi zetu wenyewe kungetoweka, kama tungeongea kidogo na kuomba zaidi.—(Sons and Daughters of God, 99) [Pr 213.2; Maombi Aya ya 22]

Njia ya kwenda kwenye kiti cha enzi cha MUNGU iko wazi kila wakati. Hutaweza kupiga magoti kila wakati kwa ajili ya maombi, lakini maombi yako ya kimya yanaweza kupaa juu kwa MUNGU kila wakati kwa ajili ya nguvu na mwongozo. Utakapojaribiwa, kama itakavyokuwa, unaweza kukimbilia mahali pa siri Pake Yeye Aliye Juu. Mikono Yake ya milele itakuwa chini yako. Acha maneno haya yakutie nguvu, "Lakini wako wachache huko Sardi ambao hawakuyachafua mavazi yao; nao watakwenda pamoja nami wakiwa wamevaa mavazi meupe, kwa maana wamestahili." Ufunuo 3:4.— (Counsels on Health, 362) [Pr 213.3; Maombi Aya ya 23]

Ikiwa watendakazi wetu wote wangukuwa katika hali ambayo wanaweza kutumia saa chache kila siku katika kazi za nje, na kujisikia huru kufanya hivi, ingekuwa baraka kwao; wangeweza kutekeleza kwa ufanisi zaidi majukumu ya wito wao. Kama hawana muda wa kutosha kupumzika, wangeweza kuweka mikakati na kuomba waendelea kufanya kazi kwa mikono yao, na hivyo wangeweza kurudi kwenye kazi yao wakiwa wameburudishwa katika mwili na roho—(Gospel Workers, 240) [Pr 213.4; Maombi Aya ya 24]

Ombi la dhati Halitegemei Wakati au Mahali au Hali/Mazingira— Omba

chumbani mwako au mahali pa faragha, na unapoendelea na kibarua chako cha kila siku, acha moyo wako uinuliwe kwa MUNGU mara kwa mara. [Pr 214.1; Maombi Aya ya 25]

Ilikuwa kwa namna hiyo Henoko alipotembea na MUNGU. Maombi haya ya kimya huinuka kama uvumba wa thamani mbele ya kiti cha neema. Shetani hawezi kumshinda yule ambaye moyo wake umejitegemeza kwa MUNGU. [Pr 214.2; Maombi Aya ya 26]

Hakuna wakati au mahali ambapo haifai kutuma ombi kwa MUNGU. Hakuna kitu kinachoweza kutuzuia kuinua mioyo yetu katika roho ya maombi ya bidii. Katika msongamano wa watu mitaani, katikati ya biashara au shuguli, tunaweza kutuma ombi kwa MUNGU na kusihi mwongozo wa MUNGU, kama vile Nehemia alipotoa ombi lake mbele ya Mfalme Artashasta. Ushirika wa karibu na faragha unaweza kupatikana popote tulipo. Mara zote tunapaswa kuacha mlango wa moyo ukiwa wazi na kutuma mwaliko wetu kwenda juu ili Yesu aje akae nasi kama mgeni kutoka mbinguni kwenye nafsi zetu –(Steps to Christ, 98, 99) [Pr 214.3; Maombi Aya ya 27]

Popote tuwapo, bila kujali shughuli zetu, mioyo yetu inapaswa kuinuliwa kwa MUNGU katika maombi. Hii ni kuwa na utayari katika maombi wakati wowote. Hatuhitaji kusubiri hadi tuweze kupiga magoti kabla ya kuomba. Wakati fulani, Nehemia alipofika mbele ya mfalme, mfalme aliuliza ni kwanini alionekana kuwa mwenye huzuni, na ni ombi gani alikuwa anataka kutoa kwa mfalme. Lakini Nehemia hakuthubutu kujibu hapo hapo. Masilahi muhimu yalikuwa hatarini. Hatima ya taifa ilining'inia juu ya mtazamo ambao unapaswa kutengenezwa juu ya akili ya mfalme; naye Nehemia akatuma maombi kwa MUNGU wa Mbinguni, kabla hajathubutu kumjibu mfalme. Matokeo yakawa kwamba alipata yote aliyoomba au hata kutamani.—(The Signs of the Times, October 20, 1887) [Pr 214.4; Maombi Aya ya 28]

Madhumuni yako yote mema na dhamira njema havitakuwezesha kustahimili mitihani ya majaribu. Lazima muwe watu wa maombi. Maombi yenu hayapaswi kuzimia, kuwa ya msimu yaani, hapa na pale bila kanuni, na ya mihemko, bali ya bidii, ya dhati, ya kudumu, na ya mara kwa mara (au daima). Sio lazima uwe peke yako, au upige magoti kuomba; lakini katikati ya shuguli zenu, nafsi zenu zinaweza kuinuliwa mara kwa mara kwa MUNGU, zikishikilia nguvu Zake; ndipo mtakapokuwa watu wa kusudi la juu, bora, takatifu, na waadilifu ambao hawatageuzwa kwa namna yoyote kutoka katika ile Kweli, na njia sahihi, na haki.—(Testimonies for the Church 4:542, 543) [Pr 214.4; Maombi Aya ya 29]

Ni lazima tuombe daima, kwa akili ya unyenyekevu na roho ya upole na unyenyekevu. Hatuhitaji kusubiri nafasi ya kupiga magoti mbele ya MUNGU. Tunaweza kuomba na kuongea na Bwana popote tulipo.— (Selected Messages 3:266) [Pr 214.5; Maombi Aya ya 30]

Maombi ya Hadhara yanapaswa Kuwa mafupi nayo yaambatane na Sauti ya asili—Badhi ya Maombi marefu yanayotolewa na wahudumu yamekuwa yasiyo na mafanikio (yamefeli). Kuomba sala refu kama wengine wanavyofanya sio sawa, kwani sio mahali pake. Wanaumiza koo na viungo vya sauti, na kisha wanazungumza juu ya kuvunjika afya kwa kazi yao ngumu. Wanajiumiza wenyewe wakati haipaswi kuwa hivyo. Wengi huhisi kwamba kusali huumiza viungo vyao vya sauti zaidi kuliko kuzungumza. Hili ni tunda la kuweka mwili kwa mkao usio wa kawaida, na jinsi ya kichwa kinavyowekwa. Wanaweza kusimama na kuzungumza, na wasijisikie kujeruhiwa. Mkao wa maombi (position) unapaswa kuwa ya asili kabisa. Kuomba kwa muda mrefu kunachosha, na si kwa mujibu wa injili ya Kristo. Nusu au hata robo ya saa ni ndefu sana. Muda wa dakika chache unatosha kuleta haja zako mbele za MUNGU na kumwambia kile unachotaka; na unaweza kuwachukua watu pamoja nawe na bado usiwachoshe na kupunguza hamu yao katika ibada na sala. Wanaweza kuburudishwa na kuimarishwa, badala ya kuchoka. [Pr 215.2; Maombi Aya ya 31]

Kosa limefanywa na wengi katika mazoezi yao ya kidini katika kuomba kwa muda mrefu na kuhubiri kwa muda mrefu, kwa kupayuka au kutumia sauti ya juu sana, kwa sauti ya kulazimisha, kwa mkazo usio wa asili na sauti isiyo ya asili.—(Testimonies for the Church 2:617) [Pr 215.3; Maombi Aya ya 32]

Zungumza kwa Uwazi na toa sala kwa Uwazi—Kwa kielelezo chako mwenyewe wafundishe watoto wako kusali kwa sauti iliyo wazi na iliyo tofauti. Wafundishe kuinua vichwa vyao kutoka kwenye kiti na kamwe wasifunike nyuso zao kwa mikono yao. Kwa kufanya hivyo wanaweza kutoa maombi yao sahili, wakirudia sala ya Bwana kwa pamoja.—(Child Guidance, 522, 523) [Pr 215.4; Maombi Aya ya 33]

Izoeze akili kuwa makini Wakati wa kuomba—Maombi ya kila siku ni muhimu katika ukuaji wa neema, na hata kwa maisha ya kiroho yenyewe, kama vile chakula cha muda cha hapa duniani, tunachokula kwa ustawi wa kimwili. Tunapaswa kujizoesha kuinua mawazo kwa MUNGU katika sala. Akili ikimangamanga huko na kule, lazima tuirudishe; kwa jitihada za dhati na zenye uvumilivu, mazoea hatimaye yatafanya iwe rahisi.—(The Sanctified Life, 93) [Pr 216.1; Maombi Aya ya 34]

Ombi halihitaji Kuwa refu au kuwa la sauti kubwa—Kusali hakueleweki jinsi inavyopaswa. Maombi yetu hayapaswi kumjulisha MUNGU juu ya kitu ambacho hajui. Bwana anajua siri za kila roho. Maombi yetu hayapaswi kuwa marefu na yenye sauti kubwa. MUNGU anasoma mawazo yaliyofichika. Tunaweza kuomba kwa siri, na Yeye anayeona katika siri atasikia, na atatupatia thawabu hadharani.—(Messages to Young People, 247) [Pr 216.2; Maombi Aya ya 35]

Hatupaswi Kujaribu Kumwamuru MUNGU Katika Maombi—Maombi yetu hayapaswi kuwa katika namna ya amri, bali yawe ni ya maombezi, Kwake Yeye, ili

Ayafanye mambo tunayotamani kutoka Kwake.—(Counsels on Health, 379) [Pr 216.3; Maombi Aya ya 36]

Omba kwa Imani—Omba kwa imani. Hakikisha unayapatanisha maisha yako na maombi yako, ili upate kupokea baraka ambazo unaziombea. Usiache Imani yako isidhoofike, kwani baraka zinazopokelewa zinalingana na imani iliyopo, yaani inayozoezwa. "na iwe kwako kulingana na imani yako". Na mkiwa na imani, chochote mtakachoomba katika sala, mtapata."Mathayo 9:29; Mathayo 21:22. Omba, amini, furahi. Mwimbieni MUNGU sifa kwa sababu amejibu maombi yenu. Muendee kwa Neno Lake. "Yeye ni Mwaminifu aliyeahidi." Waebrania 10:23. Hakuna ombi hata moja la dhati linalopotea. Njia iko wazi; na mkondo unabubujika. Umebeba miliki ya uponyaji, ukimimina mawimbi ya kurudisha uzima, afya na wokovu. (Testimonies for the Church 7:274) [Pr 216.4; Maombi Aya ya 37]

Hebu uaminifu na imani viwe sifa ya maombi yako. Bwana yu tayari kutufanyia "mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo." Waefeso 3:20. Zungumza hilo; liombea hilo. Usiongee kuhusu kutokuamini. Hatuwezi kumuacha Shetani aone kwamba ana uwezo wa kuzitia nyuso zetu giza na kuhuzunisha maisha yetu.—(Testimonies for the Church 7:273) [Pr 216.5; Maombi Aya ya 38]

SURA YA 20

KUOMBA KATIKA JINA LA YESU

Jina la Yesu Ndio Kiungo Kiunganishi Katika Maombi Kati ya Ubinadamu wote na MUNGU—Katika Jina la Kristo maombi yetu yanapanda juu kwa Baba. Yeye hutuombea, na kututetea kwa niaba yetu na Baba anazianika wazi hazina zote za neema Yake kwa ajili ya kutumegea sisi, ili sisi tufurahie na kuwagawia wengine. "Ombeni kwa Jina Langu," Kristo asema. Sisemi kwamba nitawaombea kwa Baba; kwa maana Baba Mwenyewe anawapenda ninyi. Litumieni Jina Langu mpate manufaa. Hii itayafanya maombi yenu yawe na ufanisi, na Baba atawapa utajiri wa neema Yake. Kwa hiyo ombeni, nanyi mtapata, ili furaha yenu iwe timilifu." [Pr 217.1; Maombi Aya ya 1]

Kristo Ndiye kiungo kinachomwunganisha MUNGU na mwanadamu. Ameahidi maombezi Yake binafsi. Anaweka fadhila yote ya haki Yake upande wa mwombaji. Kristo amamwomba mwanadamu, na mwanadamu, anayehitaji msaada wa Bwana, anasihi kwaajili yake mwenyewe mbele za MUNGU, akitumia nguvu ya ushawishi wa Yule aliyetoa maisha Yake kwa ulimwengu. Tunapokiri mbele za MUNGU ukubali wetu wa sifa na haki ya Kristo, uvumba wa manukato hutolewa kwa ajili ya maombezi yetu. Tunapomkaribia MUNGU kupitia fadhila ya haki na sifa za Mkombozi, Kristo hutuweka karibu na upande Wake, akituzunguka kwa mkono Wake wa kibinadamu, wakati kwa mkono Wake wa Kiungu Yeye anashika kiti cha enzi cha Yule Asiye na kikomo. Anaweka sifa na haki yake, kama uvumba mtamu wa manukato, ndani ya chetezo mikononi mwetu, ili kutia moyo maombi yetu. Anaahidi kusikia na kujibu maombi yetu. [Pr 217.2; Maombi Aya ya 2]

Ndio, Kristo amekuwa njia ya maombi kati ya mwanadamu na MUNGU (kiwambaza cha kati). Pia amekuwa njia ya baraka kati ya MUNGU na mwanadamu. Ameunganisha Uungu na ubinadamu. Watu wanapaswa kushirikiana Naye kwa ajili ya wokovu wa roho zao wenyewe, na kisha kufanya bidii, na jitihada za dhati zenye kudumu ili kuokoa wale ambao wako tayari kufa. - (Testimonies for the Church 8:178) [Pr 218.1; Maombi Aya ya 3]

Bado wanafunzi walikuwa hawajui rasilimali na nguvu za Mwokozi zisizo na kikomo. Akawaambia, "Mpaka sasa hamkuomba chochote kwa Jina Langu." Yohana 16:24. Alielezea kuwa siri ya mafanikio yao itakuwa katika kuomba nguvu na neema kwa Jina Lake. Kwamba Yeye Atakuwepo mbele za Baba kuwaomba. Maombi ya mwombaji mnyenyekevu huwasilishwa Naye kama matamania Yake Mwenyewe kwa niaba ya roho hiyo. Kila ombi la dhati husikika mbinguni. Linaweza lisiwasilishwe kwa ufasaha/umbuji; lakini ikiwa linatoka moyoni, litapanda kwenda mahali Patakatifu ambapo Yesu anahudumu, na ataliwasilisha kwa Baba bila hata Neno moja lisilopendeza, lenye kuudhi, gumu au lenye kigugumizi, bali kwa Neno zuri na lenye harufu nzuri ya ubani wa ukamilifu Wake Mwenyewe.—(The Desire of Ages, 667) [Pr 218.2; Maombi Aya ya 4]

Wanafunzi walipaswa kuendeleza kazi yao katika jina la Kristo. Kila neno na tendo lao lilipaswa kukazia fikira juu ya Jina Lake, kama lililo na nguvu muhimu ambayo kwayo wenye dhambi wanaweza kuokolewa. Imani yao ilikuwa ni kujikita ndani yake ambaye ni chanzo cha rehema na nguvu. Katika jina Lake walipaswa kuwasilisha maombi yao kwa Baba, na walipokea majibu. Walipaswa kubatiza kwa jina la Baba, la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Jina la Kristo lilipaswa kuwa ulinzi wao, kitambulisho cha utofauti wao, kifungo chao cha muungano, mamlaka ya mwenendo wao, na chanzo cha mafanikio yao.— (The Acts of the Apostles, 28) [Pr 218.3; Maombi Aya ya 5]

Patakatifu pa patakatifu naliona sanduku; juu na pande zake ilikuwa dhahabu

safi. Kila mwisho wa sanduku kulikuwa na kerubi mwenye kupendeza, na mabawa yake yametandazwa juu yake. Nyuso zao zilielekeana, na wakatazama chini. Kati ya malaika hao kulikuwa na chetezo cha dhahabu. Juu ya sanduku, pale waliposimama malaika, palikuwa na utukufu ung'aao sana, ukionekana kama kiti cha enzi alipokaa MUNGU. Yesu alisimama kando ya sanduku, na sala za watakatifu zilipomjia, uvumba ndani ya chetezo ukatoka moshi, na Yeye alitoa sala zao pamoja na moshi wa uvumba kwa Baba Yake.—(Early Writings, 32) [Pr 218.4; Maombi Aya ya 6]

Ina maana gani kuomba Katika Jina la Yesu—Kuomba katika jina la Kristo kunamaanisha mengi. Inamaanisha kwamba tunapaswa kukubali tabia yake, kudhihirisha roho yake, na kufanya kazi zake. Ahadi ya Mwokozi inatolewa kwa masharti. “Mkinipenda,” Anasema, “mtazishika amri Zangu.” Yeye huwaokoa wanadamu, si katika dhambi, bali kutoka katika dhambi; na wale wanaompenda wataonyesha upendo wao kwa utii.—(The Desire of Ages, 668) [Pr 219.1; Maombi Aya ya 7]

Yesu alisema, “Ninyi mtaomba kwa jina langu; na siwaambii, kwamba nitaomba kwa Baba kwa ajili yenu: kwa maana Baba mwenyewe anawapenda.” Nimewachagua: ... ili chochote mtakachomwomba Baba kwa jina langu, awapatie.” Yohana 16:26, 27; Yohana 15:16. Lakini kuomba katika jina la Yesu ni jambo zaidi ya kutaja tu jina hilo mwanzoni na mwisho wa ombi. Ni kuomba katika akili na roho ya Yesu, huku tukiamini ahadi Zake, kutegemea neema Yake, na kufanya kazi Zake.—(Steps to Christ, 100, 101) [Pr 219.2; Maombi Aya ya 8]

MUNGU Anatualika Kuja Kwake katika Jina la Yesu—Unaalikwa kuja, kuomba, kutafuta, kubisha; na umehakikishiwa kwamba hautatoka mtupu. Yesu anasema, “Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtapata; bisheni, nanyi mtafunguliwa; kwa maana kila aombaye hupokea; naye atafutaye hupata; na yeye abishaye atafunguliwa.” Mathayo 7:7, 8. [Pr 219.3; Maombi Aya ya 9]

Kristo anaonyesha nia ya MUNGU kubariki kwa utayari wa baba kutimiza ombi la mtoto wake. Anasema, “Je, kuna yeyote miongoni mwenu ambaye mtoto wake akimwomba mkate, atampa jiwe?” au akimwomba samaki atampa nyoka badala ya samaki? Na kama akimwomba yai, je, atampa ng'e? Ikiwa basi ninyi, mlio waovu, mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, si zaidi sana Baba yenu wa mbinguni atawapa Roho Mtakatifu hao wamwombao? Luka 11:11-13. [Pr 219.4; Maombi Aya ya 10]

Tunamwendea MUNGU katika Jina la Yesu kwa mwaliko maalum, Naye anatukaribisha kwenye chumba Chake cha faragha cha kusikiliza maombi. Anaikabidhi ile nafsi iliyonyenyekea, iliyotubu, ile imani katika Kristo ambayo kwayo anahesabiwa haki. Yesu anafuta uovu wake kama wingu zito, na moyo uliofarijiwa unapaza sauti kwa kushangilia, “Ee Bwana, nitakusifu; ingawa

ulinikasirikia, hasira Yako imegeuka, na umenifariji. Isaya 12:1.— (Counsels to Parents, Teachers, and Students, 242) [Pr 220.1; Maombi Aya ya 11]

Omba katika Jina la Yesu na kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu — Wakati mtu anatoa ombi la dhati kwa MUNGU (Yesu Kristo Ndilo Jina pekee tulilopewa chini ya mbingu litupasalo kuokolewa), katika ile nguvu na unyofu kuna ahadi kutoka kwa MUNGU kwamba Yupo karibu kujibu hilo ombi na zaidi, juu ya yote tunayoweza kumuomba au kufikiri. Hatupaswi kuomba tu katika Jina la Yesu, bali kwa uvuvio na uwepo wa joto la Roho Mtakatifu. Hii inaelezea kuwakuna maana gani kusema, "Roho Mwenyewe hutuombea kwa maumivu/kuugua kwingi kusikoweza kutamkika." Maombi lazima yatolewe kwa imani ya dhati. Kisha yatafikia kiti cha rehema. Endelea kuomba bila kusita au kuchoka. MUNGU hasemi, Omba mara moja, Nami nitakujibu. Neno Lake ni omba, kuwa mwepesi kuomba yaani uwe na utayari wa kutoa sala wakati wowote, ukiamini kwamba umeshavipokea vile vitu ambavyo umeviomba, nawe utavipokea; Mimi Nitakujibu. - (Gospel Herald, Mei 28, 1902) [Pr 220.2; Maombi Aya ya 12]

Twaweza Kumkaribia MUNGU kwa Ujasiri Kupitia Jina la Yesu—Unyenyekevu na ucha Mungu vinapaswa kubainisha tabia ya wote wanaokuja katika uwepo wa MUNGU. Kwa Jina la Yesu tunaweza kwenda mbele Zake kwa ujasiri, lakini hatupaswi kumkaribia kwa ujasiri wa kiburi (au kudhania), kana kwamba Yupo ngazi moja na sisi. Kuna wale ambao wanazungumza na MUNGU mkuu na Mwenye nguvu zote na mtakatifu, ambaye anakaa katika nuru isiyoweza kufikiwa, kama wanavyoweza kuongea na mtu wanayelingana naye, au hata mtu duni kuliko wao. Kuna wale wanaotenda katika nyumba Yake Mungu kwa namna ambayo hawazezi kufanya katika chumba cha kuonania na mtawala wa kidunia. Hawa wanapaswa kukumbuka kuwa wako machoni Pake Yeye Yule ambaye maserafi humwabudu, mahali ambapo malaika hufunika nyuso zao mbele Yake.- (Patriarchs and Prophets, 252) [Pr 220.3; Maombi Aya ya 13]

Kwa Jina la Yesu tunaweza kwenda mbele za uwepo wa MUNGU na ujasiri wa mtoto. Hakuna mtu anayehitajika kufanya kazi kama mpatanishi. Kupitia Yesu tunaweza kufungua mioyo yetu kwa MUNGU kama kwa Yule anayetujua na kutupenda sisi.—(Thoughts from the Mount of Blessing, 84) [Pr 221.1; Maombi Aya ya 14]

MUNGU Ataliheshimu Jina la Yesu Katika Maombi yetu—Kila ahadi katika Neno la MUNGU hutupatia jambo la kuombea, ikiwasilisha Neno la Yehova aliloahidi kama uhakikisho wetu. Haijalishi baraka yoyote ya kiroho tunayoihitaji, tumependelewa kuidai kupitia Yesu. Tunaweza kumwambia Bwana, kwa unyenyekevu na usahili wa mtoto kile tunachohitaji haswa. Tunaweza kumwambia mambo yetu ya muda mfupi, tukamwomba mkate na mavazi na Mkate wa Uzima na joho la haki ya Kristo. Baba yako wa mbinguni anajua kuwa unahitaji vitu hivi vyote, na umealikwa kumuomba kuhusiana na hivi vyote. Ni kupitia Jina la Yesu kwamba kila neema inapokelewa. MUNGU ataheshimu Jina

hilo, na atakidhi mahitaji yako kutoka katika utajiri wa ukarimu Wake (anatoa kwa uhuru mkubwa). —(Thoughts from the Mount of Blessing, 133) [Pr 221.2; Maombi Aya ya 15]

Hatupaswi kuomba tu katika Jina la Kristo, bali kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu. Hii inaelezea kuwa ina maana gani kusema, "Roho Mwenyewe hutuombea kwa kuugua na maumivu yasiyoweza kutamkika." Warumi 8:26 MUNGU hufurahia kujibu maombi kama hayo. Tuonapotoa ombi katika Jina la Kristo kwa dhati na nguvu, kuna ahadi yenye nguvu kutoka kwa MUNGU kwamba Yu karibu kujibu ombi letu "kwa wingi zaidi ya yote tunayoomba au kufikiri." Waefeso 3:20. [Pr 221.3; Maombi Aya ya 16]

Kristo amesema, "Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu. Marko 11:24. "Nanyi mkiomba lolote kwa Jina Langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Yohana 14:13. Naye Yohana mpendwa, chini ya uvuvio wa Roho Mtakatifu, anena kwa uwazi na uhakikisho ulio mkuu: "Tukiomba chochote sawasawa na mapenzi Yake, Yeye hutusikia; na ikiwa tunajua kwamba Yeye hutusikia, lo ote tuombalo, tunajua kwamba tuna maombi ambayo tulimwomba." 1 Yohana 5:14, 15. Basi wasilisha maombi yako kwa ujasiri na msukumo kwa Baba katika Jina la Yesu. MUNGU ataliheshimu Jina hilo.—(Christ's Object Lessons, 147, 148) [Pr 221.4; Maombi Aya ya 17]

SURA YA 21

MWONGOZO WA BWANA KUPITIA MAOMBI

Tunaweza Kujifunza Mapenzi ya MUNGU Kwetu Kupitia Maombi—Bwana hafanyi kazi bila kanuni. Mtafuteni kwa dhati na bidii sana katika maombi. Ataivuvia akili, na atatoa ulimi na usemi. Watu wa MUNGU wanapaswa kuelimishwa kutotegemea mavumbuzi ya mwanadamu na mitihani isiyo na uhakika kama njia ya kujifunza mapenzi ya Mungu kuhusu wao. Shetani na mawakala wake daima wako tayari kuingia katika mpenyo wowote utakaopatikana ambao utawaongoza watu kutoka kwenye kanuni safi za Neno la MUNGU. Watu wanaoongozwa na kufundishwa na MUNGU hawatatoa nafasi kwa mawazo ambayo kwayo hakuna "Bwana asema hivi." (Selected Messages 2:326) [Pr 222.1; Maombi Aya ya 1]

Omba kwa ajili ya Mwongozo wa MUNGU—Lazima ujene maamuzi yako ili yasiwe dhaifu, yasio na ufanisi na yasiyofaa. Ni lazima uombe kwa ajili ya uongozi, na kuweka njia zako mbele za Bwana. Ni lazima uufunge moyo wako dhidi ya upumbavu na dhambi zote, na kuufungua kwa kila mvuto wa mbinguni. Ni lazima utumie vyema wakati na fursa zako, ili kukuza tabia linganifu.—(Fundamentals of Christian Education, 302) [Pr 222.2; Maombi Aya ya 2]

Katika kila familia inapaswa kuwe na wakati uliowekwa wa ibada ya asubuhi

na jioni. Inafaa kwa kiasi gani kwa wazazi kuwakusanya watoto wao pamoja nao kabla ya kula kifungua kinywa kuanza, kumshukuru Baba wa mbinguni kwa ulinzi Wake wakati wa usiku, na kumwomba msaada Wake na mwongozo na utunzaji Wake wakati wa mchana! Inafaa kwa kiasi gani pia, jioni ifikapo, kwa wazazi na watoto kukusanyika kwa mara nyingine mbele Zake na kumshukuru kwa baraka za siku ambayo imepita!— (Testimonies for the Church 7:43) [Pr 223.1; Maombi Aya ya 3]

Jitoe wakfu kwa MUNGU asubuhi; fanya hii iwe kazi yako ya kwanza kabisa. Ombi lako na liwe, “Nichukue, Ee Bwana, niwe wako kabisa. Ninaweka mipango yangu yote miguuni Pako. Nitumie leo katika huduma yako. Kaa nami, na kazi yangu yote ifanyike ndani Yako.” Hili ni suala la kila siku. Kila asubuhi jitoe wakfu kwa MUNGU kwa ajili ya siku hiyo. Mkabidhi Yeye mipango yako yote, ili itekelezwe au ifanyike kulingana na jinsi Majaliwa Yake yatakavyoongoza. Kwa namna hiyo unakuwa unayatoa maisha yako mikononi mwa MUNGU siku kwa siku, na kwa njia hiyo maisha yako yatafanywa kuumbwa zaidi na zaidi kufanana na maisha ya Kristo. - (Steps to Christ, 70) [Pr 223.2; Maombi Aya ya 4]

Lazima ujifunze kuona kwa akili yako na pia macho yako. Lazima uyaelimishe maamuzi yako ili yasiwe dhaifu, yasiyo na ufanisi au yasiyofaa. Ni lazima uombe kwa ajili ya uongozi, na kuweka njia yako kwa Bwana. Ni lazima uufunge moyo wako dhidi ya upumbavu na dhambi zote, na kuufungua kwa kila mvuto/ushawishi wa mbinguni. Ni lazima utumie vizuri wakati na fursa zako, ili kusitawisha tabia yenye ulinganifu.—(Sons and Daughters of God, 283) [Pr 223.3; Maombi Aya ya 5]

Ombi kwa Ajili ya Mwongozo wa MUNGU linaweza Kutolewa Wakati Wowote, na mahali Popote—Hakuna wakati au mahali ambapo haifai kutoa ombi kwa MUNGU. Hakuna kitu kinachoweza kutuzuia kuinua mioyo yetu kwa roho ya maombi ya dhati. Katika umati wa watu mitaani, katikati ya shuguli au biashara, tunaweza kutuma ombi kwa MUNGU na kuomba mwongozo wa MUNGU, kama vile Nehemia alipotoa ombi lake mbele ya Mfalme Artashasta. Ushirika wa karibu unaweza kupatikana popote tulipo. Tunapaswa kuacha mlango wa moyo wazi daima na mwaliko wetu kwa Masihi ukiendelea kupanda juu ili Yesu aje na kukaa ndani yetu kama Mgeni wa mbinguni katika nafsi.—(Steps to Christ, 98, 99). [Pr 223.4; Maombi Aya ya 6]

Kuomba kama Nehemia alivyoomba katika saa yake ya uhitaji ni nyenzo ya kumuongoza Mkristo katika mazingira ambapo aina nyingine za maombi zinaweza kushindikana Wanaohenyeka katika vibarua vyeshe shuguli nyingi maishani, waliojawa na msongo na karibu kuzidiwa au kutindikiwa na fedheha, wanaweza kutuma ombi kwa MUNGU kwa ajili ya kupata mwongozo wa Wake. Wasafiri baharini na nchi kavu, wanapotishiwa na hatari kubwa, wanaweza kujikabidhi katika ulinzi wa Mbingu. Wakati wa shida ya ghafla au hatari, moyo unaweza kutuma kilio chake cha kuomba msaada kwa Yule ambaye ameahidi

Mwenyewe kuwasaidia waaminifu Wake wale waaminio kila wanapomwita. Katika kila jambo au mazingira, chini ya kila hali, nafsi iliyolemewa na huzuni na masumbufu ya maisha haya, au kushambuliwa vikali na jaribu, inaweza kupata uthibitisho, msaada, sapoti, na usaidizi katika ule upendo usiokoma na nguvu ya MUNGU Anayeshika agano.— (Prophets and Kings, 631, 632) [Pr 224.1; Maombi Aya ya 7]

Malaika Wako Karibu sana Kusaidia Tunapoomba Mwongozo wa MUNGU—Kama Nathanaeli, tunahitaji kujifunza Neno la MUNGU kwaajili yetu wenyewe, na kusali kwa ajili ya kuangaziwa na Roho Mtakatifu. Yeye aliyemwona Nathanaeli chini ya mtini atatuona sisi mahali pa sirini pa maombi. Malaika kutoka katika ulimwengu wa nuru wako karibu na wale ambao kwa unyenyekevu wanatafuta mwongozo wa Bwana.—(The Desire of Ages, 141) [Pr 224.2; Maombi Aya ya 8]

Ulimwengu unaoonekana na usioonekana upo katika mawasiliano ya karibu. Ikiwa pazia lingeondolewa, tungeliwaona malaika waovu wakisukuma giza lao kutuzunguka na kufanya kazi kwa uwezo wao wote kudanganya na kuharibu. Watu waovu wamezingirwa, wanashawishiwa, na kusaidiwa na roho waovu. Mtu wa imani na maombi ameitoa nafsi yake kwenye mwongozo wa Bwana, na malaika wa MUNGU huleta Kwake nuru na nguvu kutoka mbinguni.— (Testimonies for the Church 5:199) [Pr 224.3; Maombi Aya ya 9]

Ujuzi wa Ukweli haitegemei sana nguvu ya akili kama ilivyo juu ya usafi wa kusudi la moyo, usahili wa imani ya dhati inayomtegemea Mungu. Kwa wale ambao kwa unyenyekevu wa moyo, wanaotafuta mwongozo wa MUNGU, malaika wa MUNGU huwakaribia (karibu). Roho Mtakatifu ametolewa ili kuwafungulia hazina nyingi za ile Kweli.—(Christ's Object Lessons, 59) [Pr 225.1; Maombi Aya ya 10]

Cho chote Tunachohitaji, Twaweza Kudai Katika Ombi—Kila ahadi katika Neno la MUNGU hutupatia mada kwa ajili ya ombi (kila ahadi hutupa jambo la kuombea, zipo ahadi zaidi ya 4000 kwenye Biblia!), ikiwasilisha Neno la Yehova lililoahidiwa kuwa uhakikisho wetu. Haijalishi baraka yoyote ya kiroho tunayoihitaji, sisi tumependelewa kuiomba kupitia Yesu. Tunaweza kumwambia Bwana, kwa usahili na unyenyekevu wa mtoto, kile tunachohitaji haswa. Tunaweza kumwambia mambo yetu ya muda mfupi yanayopita, tukimwomba mkate na mavazi na Mkate wa Uzima na joho la haki ya Kristo. Baba yako wa mbinguni anajua kuwa unahitaji vitu hivi vyote, na umealikwa kumwomba juu ya vyote. Ni kupitia Jina la Yesu kwamba kila neema inapokelewa. MUNGU ataheshimu Jina hilo, na atakidhi mahitaji yako kutoka katika utajiri wa ukarimu Wake. —(Thoughts from the Mount of Blessing, 133) [Pr 225.2; Maombi Aya ya 11]

Wazazi waombe Mwongozo wa MUNGU—Wazazi, nyenyekezeni mioyo yenu mbele za MUNGU. Anza kazi kamilifu kwa watoto wako. Msihi Bwana

akusamehe kulipuuzia kwako Neno Lake katika kutojali kuwazoeza watoto wako katika njia wanayopaswa kuiendea. Omba nuru na mwongozo, dhamiri nyororo, na maamuzi/utambuzi ulio wazi ili uone makosa na kufeli kwako. MUNGU atasikia maombi kama hayo kutoka kwenye moyo mnyenyekevu na uliopondeka. - (Child Guidance, 557) [Pr 225.3; Maombi Aya ya 12]

Wale walio tayari Kuongozwa Wanaweza Kujua Mapenzi ya MUNGU— Bwana hufunua mapenzi Yake kwa wale walio na bidii ya dhati na wanaotamani kuongozwa Naye. Sababu ya kukosa kwako ufanisi ni kwamba umeacha wazo la kujua na kuyafanya mapenzi ya MUNGU, na hivyo haujui chochote katika mtazamo chanya. - (Ushuhuda kwa Kanisa 3: 466) [Pr 225.4; Maombi Aya ya 13]

Yachunguze Maandiko kwa Sala kwa ajili ya Uongozi wa Bwana — Wale ambao hawataki kukubali ule Ukweli ulio wazi, unaokatakata, na ulio thabiti wa Biblia, daima wakaendelea kutafuta hekaya za kupendeza ambazo zitatuliza au kunyamazisha dhamiri zao. kadiri ya mafundisho yanavyokuwa na upungufu wa mionjo ya kiroho, kujikana nafsi, kujidhili au kujinyenyekeza, ndivyo yanavyopokelewa kwa upendeleo mkubwa zaidi. Watu hawa wanapunguza nguvu za kiakili kutumikia tamaa zao za mwili. Hujiona wenye busara sana katika mawazo yao wenyewe yenye kiburi hata wasitafute Maandiko na kutubu kwa roho na maombi ya moyo uliopondeka na maombi dhati kwa ajili ya mwongozo wa Bwana, hawana ngao dhidi ya udanganyifu. Shetani yuko tayari kutimiza matamania ya moyo wao, naye anaingiza udanganyifu wake aliushika mkoni mwake mahali pa ile Kweli na hivyo kuwatawala kirahisi sana.—(The Great Controversy, 523) [Pr 226.1; Maombi Aya ya 14]

Mtumaini MUNGU Naye Ataongoza Njia Yako — Wengi wanashindwa kupanga mipango dhahiri ya siku zijazo. Maisha yao hayajatulia. Wanashindwa kutambua matokeo ya mambo, na hii mara nyingi huwajaza wasiwasi na machafuko. Hebu na Tukumbuke kwamba maisha ya watoto wa MUNGU katika ulimwengu huu ni maisha ya safari ya hija (wasafiri na wapitaji). Sisi hatuna hekima ya kupanga maisha yetu wenyewe. Sio juu yetu kutengeneza au kuyaumba maisha yetu ya baadaye. “Kwa imani Abrahamu alimtii MUNGU alipoitwa aende katika nchi ambayo MUNGU angempa iwe yake. Ingawa hakujua alikokuwa anakwenda, Abrahamu alienda. Waebrania 11: 8. [Pr 226.2; Maombi Aya ya 15]

Kristo katika maisha Yake humu duniani hakujifanyia/hakujipangia mikakati ya maisha Yake Yeye Mwenyewe. Alikubali mipango ya MUNGU Kwake, na siku hadi siku Baba aliifunua mipango Yake. Ndivyo nasi tunavyopaswa kumtegemea MUNGU, ili maisha yetu yaweze kuwa na utekelezaji rahisi yaani mtelemko unaoelekea kwenye mapenzi Yake. Tunapomkabidhi njia zetu, Yeye ataziongoza hatua zetu. [Pr 226.3; Maombi Aya ya 16]

Wengi sana, katika kupanga maisha mazuri ya baadaye, huishia kushindwa

kabisa. Mwachie MUNGU akupangie. Kama mtoto mdogo, tumaini mwongozo Wake Yeye ambaye "atashika miguu ya watakatifu Wake." 1 Samweli 2: 9. Mungu kamwe hawaongozi watoto Wake tofauti na vile ambavyo wangechagua kuongozwa, ikiwa wangeweza kuona mwisho tangu mwanzo na kutambua utukufu wa kusudi ambalo wanalitimiza kama watenda kazi pamoja Naye.— (The Ministry of Healing, 478, 479) [Pr 226.4; Maombi Aya ya 17]

Ikiwa umejitoe kwa MUNGU kuifanya kazi Yake, hauna haja ya kuwa na wasiwasi juu ya kesho. Yeye ambaye wewe ni mtumishi Wake, anajua mwisho tangu mwanzo. Matukio ya kesho, ambayo yamefichwa machoni pako, yako wazi machoni Pake Yeye aliye na nguvu zote. [Pr 226.5; Maombi Aya ya 18]

Tunapojichukulia mikononi yetu usimamizi wa vitu ambavyo tunapaswa kufanya, na kutegemea hekima yetu wenyewe kwa ajili ya mafanikio, tunajitwika mzigo ambao MUNGU hajatupatia, na tunajaribu kuubeba bila msaada Wake. Tunachukua jukumu ambalo ni la MUNGU, na kwa hivyo tunajiweka wenyewe katika nafasi Yake (GOD's syndrome). Tunaweza kujiletea na wasiwasi na kutarajia hatari na hasara, kutupata kwa hakika. Lakini wakati tunaamini kabisa kwamba MUNGU anatupenda na ana kusudi la kututendea mema tutakoma kuwa na wasiwasi juu ya siku zijazo. Tutamtumaini MUNGU kama vile mtoto anavyomwamini mzazi wake mwenye upendo. Ndipo shida zetu na mateso yatatoweka, kwani mapenzi yetu yamemezwa katika mapenzi ya MUNGU. —(Thoughts from the Mount of Blessing, 100, 101) [Pr 227.1; Maombi Aya ya 19]

Eliezeri Aliomba kwa ajili ya—na Akapokea—Mwongozo wa MUNGU—Akikumbuka maneno ya Abrahamu, kwamba MUNGU atamtuma malaika Wake pamoja naye, alisali kwa dhati na bidii ili kupata mwongozo chanya. Katika familia ya bwana wake alikuwa amezoea mazoezi ya mara kwa mara ya fadhili na ukarimu, na sasa aliomba kwamba kitendo cha ukarimu wa mwenyeji wake kiweze kuonyesha na msichana ambaye MUNGU alimchagua. [Pr 227.2; Maombi Aya ya 20]

Punde baada ya kutolewa maombi na jibu lipatikana papo hapo. Miongoni mwa wanawake ambao walikuwa wamekusanyika kwenye kisima, adabu ya mmoja wao ikawa imemvutia. Yule msichana alipokuwa akitoka kisimani, yule mgeni alikwenda kumlaki, akiomba maji kwenye mtungi ulio begani mwake. Ombi hilo lilipokelewa kwa jibu zuri, na ofa ya kuteka maji kwa ajili ya ngamia pia ikatamkwa na msichana huyu, huduma ambayo ilikuwa ni desturi kwa wageni hata kwa binti za wakuu kufanya kwa ajili ya mifugo na makundi ya baba zao. Kwa hivyo ishara iliyotarajiwa ilitolewa/ilionyeshwa na (Rebeka). - (Patriarchs and Prophets, 172) [Pr 227.3; Maombi Aya ya 21]

SURA YA 22

MAOMBI KWA AJILI YA WAGONJWA

Maombi yanapaswa Kutolewa kwa ajili ya Wagonjwa kwa Imani tulivu—Nilionyeshwa kwamba katika suala la ugonjwa, pale ambapo njia iko wazi kwa ajili ya kutoa ombi kwa ajili ya wagonjwa, jambo hili linapaswa kukabidhiwa kwa Bwana kwa imani tulivu, si kwa dhoruba ya msisimko. Yeye peke yake Ndiye anafahamu maisha ya zamani ya mtu huyo na Ndiye anayejua kesho yake itakuwaje. Yeye anayefahamu mioyo ya watu wote anajua ikiwa mtu huyo, ikiwa ataponywa na kisha atoke kitandani mwake, atalitukuza Jina Lake au atamvunjia heshima kwa kurudi nyuma na kuasi. Yote tunayotakiwa kufanya ni kumwomba MUNGU awaponye wagonjwa ikiwa ni sawa na mapenzi Yake, tukiamini kuwa Yeye husikia sababu tunazowasilisha na maombi ya bidii yanayotolewa. Ikiwa Bwana ataona itamtukuza zaidi, Yeye atajibu maombi yetu. Lakini kusesitiza au kulazimisha apone bila kujisalimisha kwenye mapenzi Yake sio sawa. - (Testimonies for the Church 2:147, 148) [Pr 228.1; Maombi Aya ya 1]

Pamoja na matibabu yetu yote tunayowapa wagonjwa, maombi rahisi na ya bidii yanapaswa kutolewa kwa ajili ya baraka za uponyaji. Tunapaswa kuwaelekeza wagonjwa kwa Mwokozi Mwenye huruma, na nguvu Yake ya kusamehe na kuponya. —(Selected Messages 3:296). [Pr 228.2; Maombi Aya ya 2]

Wale ambao hufanya kazi ya nyumba kwa nyumba watapata fursa za huduma katika namna nyingi (anuwai). Wanapaswa kuwaombea wagonjwa na wanapaswa kufanya yote katika uwezo wao kuwaondoa katika mateso. —(Testimonies for the Church 6:83, 84). [Pr 229.1; Maombi Aya ya 3]

Mwokozi angetutaka tuwatie matumaini wagonjwa wasio na tumaini, walio na shida ya maumivu au mateso, kushikilia nguvu Zake. Kupitia imani na maombi chumba cha wagonjwa kinaweza kubadilishwa kuwa Betheli (nyumba ya Mungu kama pale Yakobo alipita). - (The Ministry of Healing, 226) [Pr 229.2; Maombi Aya

ya 4]

Ikiwa tuna udhaifu wa mwili, kwa kweli ni sawa kumtumainia Bwana, tukiomba dua kwa MUNGU wetu katika kesi yetu, na ikiwa tunajisikia kuwaomba wengine ambao kupitia wao tunao ujasiri wa kuungana nao kwa ajili ya maombi kwa Yesu ambaye ni Tabibu hodari, hakika msaada utakuja ikiwa tutaomba kwa imani. - (Medical Ministry, 16) [Pr 229.3; Maombi Aya ya 5]

Tulituma maombi yetu ya unyenyekevu kwa ajili ya yule aliye mgonjwa na aliyesumbuliwa, ambaye alikuwa njiani kupoteza maisha haya. Tulipowasilisha jambo hii mbele ya Bwana, tulihisi uhakikisho wa upendo wa MUNGU hata katika shida hii.—(The Review and Herald, October 11, 1887) [Pr 229.4; Maombi Aya ya 6]

Tulimuweka wakfu mtoto na kuomba juu yake, tukiamini kwamba Bwana atawapa mama na mtoto amani. Ikawa hivyo. Kilio cha mtoto kilikoma, na tukawaacha wakiendelea vizuri. —(Spiritual Gifts 2:110, 111) [Pr 229.5; Maombi Aya ya 7]

Wagonjwa wataongozwa kwa Kristo kwa uangalifu wa wauguzi ambao wanayawazia mahitaji yao, na ambao huinama katika ombi na kumwomba Mmishonari Mkuu wa Tiba kumtazama kwa huruma mgonjwa anayeteseka na kuruhusu ushawishi unaotuliza wa neema Yake usikike na urejesho wa nguvu Zake udhihirike. - (Medical Ministry, 191, 192) [Pr 229.6; Maombi Aya ya 8]

Wauguzi wa kimishonari wanapowajali wagonjwa na kupunguza shida za maskini, watapata fursa nyingi za kuomba pamoja nao, kuwasomea Neno la MUNGU, kuzungumza juu ya Mwokozi Wanaweza kuleta mwanga wa tumaini katika maisha ya walioshindwa na waliokata tamaa. (Medical Ministry, 246, 247) [Pr 229.7; Maombi Aya ya 9]

Ikiwa maombi zaidi yangetolewa katika vyumba vyetu vya Sanitarium vya wagonjwa wa muda mrefu kwa ajili ya uponyaji wa wagonjwa, nguvu kuu ya Mponyaji ingeonekana. Wengine wengi wangeimarishwa na kubarikiwa, na magonjwa mengi ya dharura (papo hapo) yangeponywa. —(Selected Messages 3:295) [Pr 230.1; Maombi Aya ya 10]

Ningeenda mbele za Bwana na ombi hili: “Bwana, hatuwezi kusoma moyo wa mgonjwa huyu, lakini unajua huenda ni kwa faida ya roho yake na kwa utukufu wa Jina Lako kumuinua kiafya. Kwa wema Wako mkubwa, ulirehemu jambo hili (mhurumie mgonjwa), na ruhusu hatua za kiafya zifanyike katika mfumo. Kazi lazima iwe Yako Mwenyewe kabisa.” (Healthful Living, 239). [Pr 230.2; Maombi Aya ya 11]

Hebu sauti ya maombi isikike katika taasisi zetu kwa niaba ya wagonjwa ili waweze kujiweka mahali ambapo wanaweza kushirikiana na Yeye ambaye anaweza kuponya mwili na roho pia. [Pr 230.3; Maombi Aya ya 12]

Hapo awali tulibarikiwa na taasisi ambazo wagonjwa wangeweza kupata

msaada dhidi ya mateso, kwa matibabu ya uadilifu na sala za dhati katika imani kwa MUNGU, tulibeba kesi ambazo zilionekana kukosa matumaini kufanikiwa. Leo Bwana anawaalika wanaoteseka kuwa na imani katika Yeye. Hitaji la mwanadamu ndiyo fursa ya MUNGU kutenda (Man's necessity is God's opportunity). —(Selected Messages 3:295, 296). [Pr 230.4; Maombi Aya ya 13]

Yote ambayo yanaweza kufanywa katika kuwaombea wagonjwa ni kumsihi tu MUNGU kwa dhati na bidii, na bila kuchoka kwa niaba yao, na kwa ujasiri kamili kabidhi suala hilo mikononi Mwake. Ikiwa tunazingatia uovu mioyoni mwetu Bwana hatatusikia. Yeye Anaweza kufanya apendavyo na watu Wake Mwenyewe.— (Testimonies for the Church 2:148) [Pr 230.5; Maombi Aya ya 14]

Mara nyingi imekuwa upendeleo wangu kuomba na wagonjwa. Tunapaswa kufanya hivi mara nyingi zaidi kuliko tunavyo fanya. —(Selected Messages 3:295) [Pr 230.6; Maombi Aya ya 15]

Ni jukumu letu kuwasilisha wagonjwa na wanaoteseka kwa Kristo mikononi mwa imani yetu Tunapaswa kushikilia ahadi Yake, na kuomba kwa ajili ya udhihirisho wa nguvu Zake. Kiini cha injili ni urejesho/kurejeshwa, na Mwokozi angetutaka tuwaombea wagonjwa, wasio na tumaini, na wenye shida washizishikilie nguvu Zake. - (The Desire of Ages, 824, 825) [Pr 231.1; Maombi Aya ya 16]

Maombi kwa ajili ya Wagonjwa Ni Muhimu Sana hivyo yasishughulikiwe kwa Uzembe—Kuhusu kuombea wagonjwa, ni jambo la maana mno kiasi kwamba hatupaswi kushughulikia pasipo kujali. Ninaamini tunapaswa kupeleka kila kitu kwa Bwana, na kumjulisha MUNGU udhaifu wetu wote na kutaja shida zetu zote anuwai. - (Medical Ministry, 16) [Pr 231.2; Maombi Aya ya 17]

Maombi kwa ajili ya Wagonjwa yanafaa Leo kama katika Nyakati za Biblia—Mponyaji wa Kimungu/Mbinguni Yuko katika chumba cha wagonjwa; Anasikia kila neno la maombi yanayotolewa Kwake katika usahili wa imani ya kweli. Wanafunzi Wake leo wanapaswa kuwaombea wagonjwa, kama walivyofanya wanafunzi wa kale. Na kutakuwa na uponyaji; kwani "ombi la imani litawaokoa wagonjwa." (Gospel Workers, 215) [Pr 231.3; Maombi Aya ya 18]

Mungu Yuko tayari kurejesha afya ya wagonjwa sasa kama vile Roho Mtakatifu aliposema Maneno haya kupitia mwandishi wa- Zaburi. Na Kristo Ndiye yule yule daktari/tabibu mwenye huruma sasa kama alivyokuwa wakati wa huduma Yake hapa duniani. Ndani Yake kuna zeri ya uponyaji kwa kila ugonjwa, nguvu ya uponyaji kwa kila udhaifu. Wanafunzi Wake kwa wakati huu wanapaswa kuwaombea wagonjwa kweli kama vile wanafunzi wa zamani walivyoomba. Na uponyaji utafuata; kwani "ombi la imani litawaokoa wagonjwa." Tunayo nguvu ya Roho Mtakatifu, uhakika mtulivu wa imani, ambao unaweza kudai ahadi za MUNGU. Ahadi ya Bwana, "Wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya" (Marko 16:18), hili ni la kuaminika sasa kama katika siku zile za mitume.

Inaonyesha fursa ya watoto wa MUNGU, na imani yetu inapaswa kushikilia yote ambayo tungeweza kuyashikilia. Watumishi wa Kristo ndio mfereji wa utendaji Wake, na kupitia kwao anatamani kutumia nguvu Zake za uponyaji. Ni jukumu letu kuwasilisha wagonjwa na wanaoteseka Kwake Mungu, kwenye mikono ya imani yetu. Tunapaswa kuwafundisha kuamini katika Mponyaji Mkuu. - (The Ministry of Healing, 226) [Pr 231.4; Maombi Aya ya 19]

Maombi kwa ajili ya Wagonjwa Yapasa Kuzingatia Mapenzi ya MUNGU— Katika sala kwa ajili ya wagonjwa yapasa ikumbukwe kwamba “hatujui tunalopaswa kuomba jinsi itupasavyo.” Warumi 8:26 Hatujui kama baraka tunayotaimani itakuwa bora au la. Kwa hivyo maombi yetu yanapaswa kujumuisha wazo hili: 'Bwana, unajua kila siri ya roho. Wewe unawafahamu watu hawa. Yesu, Wakili wao, ulitoa uhai Wako kwa ajili yao. Upendo Wako kwao ni mkubwa kuliko wetu unavyoweza kuwa. Ikiwa, ni kwa ajili ya utukufu Wako na mema ya wale wanaoteseka, tunaomba, kwa Jina lako Yesu, kwamba waweze kupona. Ikiwa sio mapenzi Yako kwamba waweze kurejeshewa afya zao, tunaomba kwamba neema Yako iwafariji na uwepo Wako uwaimarishe na kuwasaidia katika mateso yao. [Pr 232.1; Maombi Aya ya 20]

“MUNGU anajua mwisho tangu mwanzo. Anajua mioyo ya watu wote. Anasoma kila siri ya roho. Anajua kama wale ambao wanaombewa wangeweza au wasingeweza kustahimili majaribu ambayo yangewajia wanapoendelea kuishi. Anajua kama maisha yao yatakuwa mbaraka au laana kwao wenyewe na kwa ulimwengu. Hii ni sababu moja kwa nini, wakati tunawasilisha ombi letu kwa bidii, tunapaswa kusema, "Walakini sio mapenzi yangu, bali Yako yatimizwe." Luka 22:42. (Ministry of Healing, 229, 230) [Pr 232.2; Maombi Aya ya 21]

Katika kuwaombea wagonjwa, tunapaswa kuomba kwamba ikiwa ni mapenzi ya MUNGU basi waponywe wawe na afya; lakini ikiwa vinginevyo kwamba awape neema Yake ya kuwafariji, na uwepo Wake uwadumishe katika mateso yao. Wengi wanaopaswa kuweka nyumba zao sawa, yaani katika mpangilio, hupuuza kufanya hivyo wakati wana tumaini kwamba watainuliwa kiafya katika kujibiwa maombi. Wakichochea na tumaini la uwongo, hawahisi hitaji la kutoa maneno ya mawaidha na ushauri kwa watoto wao, wazazi, au marafiki, na ni bahati mbaya sana. Wakikubali uhakikisho wa kwamba wangeponywa wakati wa kuombewa, hawathubutu kutaja jinsi mali zao zitakaavyogawiwa, jinsi familia yao inavyopaswa kutunzwa, au kueleza matamania yoyote kuhusu mambo ambayo wangezungumza ikiwa walidhani wangeondolewa na kifo. Kwa njia hii majanga huletwa kwenye familia na marafiki; kwa maana mambo mengi ambayo yanapaswa kueleweka yameachwa bila kutajwa au kuzungumziwa, kwa sababu wanaogopa kuwa kujieleza juu ya mambo haya itakuwa ni kuikana imani yao. Wakiadini watainuliwa kiafya kwasababu ya maombi, wanashindwa kutumia njia au kanuni za afya, au usafi ambazo ziko katika uwezo wao, wakihofia kuwa kutenda hilo ni kuikana imani yao. —(General Conference Daily Bulletin, February

26, 1897) [Pr 232.3; Maombi Aya ya 22]

"Tumeungana katika maombi ya dhati karibu na vitanda vya wagonjwa waume, na wake, na watoto, nasi tumehisi kuwa walirudishwa kwetu kutoka katika kifo kama jibu la maombi yetu ya dhati. Katika maombi haya tulifikiri lazima tuwe na mtazamo chanya, na ikiwa tuna imani, ni lazima tuombe kwaajili ya uhai tu. Hatukuthubutu kusema, "Ikiwa itamtukuza MUNGU," tukiogopa kuwa ingekuwa sawa na kuwa na shaka. Tumewaangalia kwa wasiwasi wale ambao wamerudishwa kwetu kama wale waliotoka kifoni. Tumeona baadhi ya hawa, haswa vijana, wakirejeshewa afya, nao wakamsahau MUNGU, wakawa wenye tabia mbaya maishani, wakisababisha huzuni na uchungu kwa wazazi na marafiki, na wamekuwa aibu kwa wale ambao waliogopa kuomba mapenzi ya Mungu yatimizwe. Waliishi kwa kutomheshimu na kumtukuza MUNGU, bali kumlaani kwa maisha yao ya uovu. [Pr 233.1; Maombi Aya ya 23]

"Hatutengenezi njia tena wala kutafuta kumleta Bwana katika matamano yetu. Ikiwa maisha ya wagonjwa yanaweza kumtukuza Yeye, tunaomba kwamba waishi, hata hivyo, si kama sisi tutakavyo bali kama Yeye atakavyo. Imani yetu inaweza kuwa imara, na ya uhakika kwa kuyakabidhi matamano yetu kwa MUNGU Mwenye hekima yote, na, bila wasiwasi au homa, na kwa ujasiri mkamilifu, tukimwamini Yeye. Tunayo ahadi. Tunajua kwamba Yeye hutusikia ikiwa tunaomba kulingana na mapenzi Yake.— (Counsels on Health, 378, 379) [Pr 233.2; Maombi Aya ya 24]

Mungu Hujibu Maombi kwa ajili ya Wagonjwa — Hakuna nguvu ya kibinadamu inayoweza kuokoa wagonjwa, lakini, kupitia maombi ya imani, Mponyaji Mkuu ametimiza ahadi Yake kwa wale ambao wameliitia jina Lake.— (Selected Messages 3:295). [Pr 233.3; Maombi Aya ya 25]

Hebu tufanye kama mitume wa Kristo walivyofanya; hebu tufanye maombi kwaajili ya wagonjwa, kwani wapo wengi ambao hawawezi kufaidika na vituo vyetu vya Sanitarium (tiba rahisi). Bwana ataondoa udhaifu katika kujibu maombi. - (Medical Ministry, 242) [Pr 233.4; Maombi Aya ya 26]

Kudumu katika Maombi ni Muhimu Wakati Tunaombea Wagonjwa — Katika kuwaombea wagonjwa, ni muhimu kuwa na imani; kwani kufanya hivyo ni kulingana na Neno la MUNGU. "Maombi ya bidii ya mwenye haki yanafaa sana." Yakobo 5:16. Kwa hivyo hatuwezi kutupilia mbali kuombea wagonjwa, na tunapaswa kusikitika sana ikiwa tungekosa fursa ya kumkaribia MUNGU, kuweka mbele Zake udhaifu wetu wote na ugonjwa wetu, kumweleza Mwokozi Mwenye huruma juu ya mambo haya, tukiamini kwamba Yeye husikia maombi yetu. Wakati mwingine majibu ya maombi yetu huja mara moja; wakati mwingine tunalazimika kungojea kwa uvumilivu na kuendelea kuomba kwa bidii vitu tunavyohitaji, mahitaji yetu yakiwasiliswa na mahitaji ya mwombaji asiyechoka aliyeenda kuomba mkate usiku. "Ni yupi kati yenu ambaye atakuwa na rafiki, na

atamwendea usiku wa manane," nk. Somo hili lina maana zaidi ya vile tunaweza kufikiria. Tunapaswa kuendelea kuomba, hata ikiwa hatuyajatambua majibu ya haraka ya maombi yetu. "Ninawaambia, ombeni, nanyi mtapewa, tafuteni, nanyi mtapata, bisheni nanyi mtafunguliwa. Maana yeyote aombaye hupewa, atafutaye hupata na abishaye hufunguliwa. Luka 11: 9, 10. [Pr 234.1; Maombi Aya ya 27]

Tunahitaji neema, tunahitaji mwangaza kutoka kwa BWANA, ili kupitia Roho Mtakatifu tuweze kujua jinsi ya kuomba mambo hayo ambayo hakika tunayahitaji. Maombi yetu yakizingatiwa na Bwana yatajibiwa .— (Counsels on Health, 380) [Pr 234.2; Maombi Aya ya 28]

Dhambi Lazima Iwekwe Mbali ikiwa Maombi ya Uponyaji Yapasa Kujibiwa— Kwa wale wanaotamani maombi ya kurejeshewa afya, inapaswa kuwekwa wazi kuwa ukiukaji wa sheria ya MUNGU, ziwe za asili au za kiroho, ni dhambi, na ili wao waweze kupokea baraka Yake, lazima dhambi ikiriwe na kutupiliwa mbali. [Pr 234.3; Maombi Aya ya 29]

"Maandiko yanatuambia," Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa." Yakobo 5:16. Kwa yule anayefanya maombi, hebu mawazo kama haya yawasilishwe: 'Hatuwezi kusoma moyo wako, au kujua siri za maisha yako. Hizo zinajulikana kwako mwenyewe tu na kwa MUNGU. Ukizikiri dhambi zako, ni wajibu wako kuziungama. 'The Ministry of Healing, 228) [Pr 234.4; Maombi Aya ya 30]

Kujiamini Kupita Kiasi Huonekana Kama Imani katika Kuombea Wagonjwa— Nimeona mambo mengi sana, katika kuwaombea wagonjwa yanayochukuliwa kwa kupitiliza (ushabiki), hadi nikahisi kwamba sehemu hii ya uzoefu wetu inahitaji mawazo thabiti, yaliyotakaswa, tusije kufanya ushabiki fulani kwa kudhania kwamba ni imani, na hata tukaiita ni imani, kumbe si chochote zaidi ya dhana. Watu waliochoka na shida ya ugonjwa wanahitaji kushauriwa kwa busara, ili wasonge kwa busara na hivyo kutoharibu mambo au kujiabisha; na wakati wanajiweka mbele za MUNGU kuombewa ili waponywe, hawapaswi kuchukua msimamo kwamba njia za urejeshaji wa afya kulingana na sheria za asili zinapaswa kupuuzwa. (tiba mbadala zinazofanya kazi, sisi tunapaswa kuwa na busara kuzitumia, ila kwenda hospitali na kuchunguzwa, kuchukua vipimo, maabara au xray ni muhimu kwenye dharura au hali tete, ila tunapaswa kujua jinsi ya kuzitumia tiba rahisi 8 Mungu alizotoa). [Pr 235.1; Maombi Aya ya 31]

Ikiwa watachukua msimamo kwamba katika kuombea uponyaji lazima wasitumie tiba rahisi zilizotolewa na MUNGU ili kupunguza maumivu na kuisaidia asili katika kazi yake, hebu isije ikaonekana kwamba ni kuikana imani, wanachukua msimamo usiofaa. Huku siko kuikana imani; Inaendana kabisa na mipango ya MUNGU. Hezekia alipokuwa mgonjwa, nabii wa MUNGU alimletea ujumbe kwamba lazima afe. Alimlilia Bwana, na Bwana akamsikia mtumishi Wake na kufanya muujiza kwa niaba yake, akampelekea ujumbe kwamba miaka

kumi na mitano ingeongezwa kwenye maisha yake. Sasa hapa Mungu angetumia Neno moja tu, na kisha angetibiwa kwa kuguswa mara moja tu kwa kidole cha Bwana, lakini maagizo maalum yalitolewa kuchukua tini na kuiweka kwenye sehemu iliyoathiriwa, na Hezekia akarejeshewa afya, yaani uzima wake ukarudishwa. Katika kila jambo tunahitaji kuenanda na mstari wa mipango na majaliwa ya MUNGU. [Pr 235.2; Maombi Aya ya 32]

Wakala wa kibinadamu unapaswa kuwa na imani na unapaswa kushirikiana na uwezo wa Bwana, mtu akitumia kila namna ya nyenzo, akichukua faida ya kila kitu ambacho kulingana na akili yake ni cha manufaa, akifanya kazi kwa kupatana na sheria za asili; basi kwa kufanya hivyo haikani wala hazuii imani.— (Counsels on Health, 381, 382) [Pr 235.3; Maombi Aya ya 33]

Katika Neno la MUNGU tuna maagizo yanayohusiana na maombi maalumu ya kuponya wagonjwa. Lakini utoaji wa ombi kama hilo ni tendo la wakfu kabisa na halipaswi kuchukuliwa bila kuzingatiwa kwa uangalifu. Katika visa vingi vya kuomba uponyaji wa wagonjwa, ile inayoitwa imani si kitu kingine tofauti na dhana. [Pr 235.4; Maombi Aya ya 34]

Watu wengi hujiletea magonjwa kwa kujifurahisha au kujiendekeza kwao wenyewe. Hawajaishi kulingana na sheria ya asili au kanuni za usafi wa moyo thabiti. Wengine wamepuuza sheria za afya katika tabia zao za kula na kunywa, kuvaa, au kufanya kazi. Mara nyingi aina fulani ya uovu ndiyo sababu ya udhaifu wa akili au mwili. Ikiwa watu hawa wangepata baraka ya afya, wengi wao wangeendelea kufuata njia ile ile ya uasi wa kutozingatia sheria za asili na za kiroho za MUNGU, wakifikiri kwamba ikiwa MUNGU atawaponya katika kujibu maombi yao, basi wao wako huru kuendelea na mazoea yao mabaya na yasiyofaa na kuendeleza kujifurahisha na tamaa za mwili potovu bila kujizuia Ikiwa MUNGU angefanya muujiza kuwarudishia watu hawa afya, angekuwa akiwatia moyo kuitenda dhambi. [Pr 235.5; Maombi Aya ya 35]

Ni kazi iliyopotea kuwafundisha watu kumtazama MUNGU kama mponyaji wa udhaifu wao, pasipo kuwafundisha pia kuacha mazoea yasiyofaa, yale ambayo yanapingana na afya. Ili kupokea baraka Yake katika kujibu maombi, lazima waache kufanya uovu na kujifunza kutenda vyema. Mazingira yao lazima yawe safi, mwenendo wao wa maisha uwe sahihi. Lazima waishi kwa kupatana na sheria ya MUNGU, asili na kiroho. - (The Ministry of Healing, 227, 228) [Pr 236.1; Maombi Aya ya 36]

Maombi ya Uponyaji wa Kimwujiza Yanaweza Kusababisha Ushupavu (au kupitiliza kiasi) - "Kwa nini," mmoja baada ya mwingine hujiuliza, "je, maombi hayatolewi kwa ajili ya uponyaji wa kimwujiza, badala yake hutolewa kwa ajili ya vituo vingi vya afya vya Sanitarium vilivyoanzishwa?" Hili likifanyika, ushupavu mkubwa utazuka katika vituo vyetu. Wale wanaojiamini kupita kiasi wangeanza kufanya mabadiliko.—(Evangelism, 594, 595) [Pr 236.2; Maombi Aya ya 37]

Kuzingatia Maelekezo ya Tabibu Sio Kuikana Imani Katika Maombi ya Uponyaji—Wengi wanaotafuta rehema ya uponyaji wa Bwana wanafikiri kwamba lazima wawe na jibu la moja kwa moja na la haraka kwa maombi yao au imani yao ina hitilafu. Kwa sababu hii, wale ambao wamedhoofishwa na magonjwa wanahitaji kushauriwa kwa busara, ili watende kwa hekima. Hawapaswi kupuuza wajibu wao kwa marafiki ambao wanaweza kuwasaidia kuishi, au kupuuza kutumia wakala wa asili (au tiba mbadala) kwaajili ya urejeshaji wa afya. [Pr 236.3; Maombi Aya ya 38]

Mara nyingi kuna hatari ya kukosea hapa. Kwa kuamini kwamba wataponywa katika jibu la maombi, wengine wanaogopa kufanya chochote kile ambacho kinaweza kuonekana kwamba kinaashiria ukosefu wa imani kwa upande wao. Lakini hawapaswi kupuuza kuyaweka mambo yao sawa kama wanavyotamani kufanya ikiwa kuna tarajio la wao kuondolewa kwa kifo. Wala hawapaswi kuogopa kusema maneno ya kutia moyo au ushauri ambao wangetamani kuuotoa katika saa ya kuagana kwa wapendwa wao. - (The Ministry of Healing, 231) [Pr 237.1; Maombi Aya ya 39]

Lakini baada ya kuwaombea kwa bidii wagonjwa nini kifuata basi? Je, ninaacha kufanya yote niwezayo kwa ajili ya kupona kwao?—Hapana, ninafanya kazi kwa bidii zaidi, kwa maombi mengi kwamba Bwana apate kubariki njia ambayo mkono Wake Mwenyewe umetoa; ili aweze kutoa hekima iliyotakaswa kwa ajili ya kushirikiana Naye katika kuwaponya wagonjwa.— (Healthful Living, 240, [1897, 1898]). [Pr 237.1; Maombi Aya ya 40]

Matibabu ya Dawa Yanapaswa Kutumiwa Pamoja na Maombi Kwa ajili ya Uponyaji—Wale wanaotafuta uponyaji kwa maombi hawapaswi kupuuza kutumia tiba rahisi (au tiba mbadala) ambayo ipo karibu nao, na wanaweza kuipata kwa urahisi, nayo ikawa na matokeo mazuri tu. Kutumia tiba zile ambazo MUNGU amezitoa katika kupunguza maumivu na kusaidia asili/mwili katika kazi yake ya urejeshaji afya sio kuikana imani. Kushirikiana na MUNGU, na kujiweka katika hali rafiki inayoleta uponyaji siyo kukana imani. MUNGU ameweka ndani ya uwezo/uwezekano wa kujipatia ujuzi wa sheria za uhai/uzima. Maarifa haya yamewekwa ndani ya maeneo yetu ya karibu, ili tuweze kuyafikia, kwaajili ya matumizi/kuyatumia. Tunapaswa kutumia kila miundombinu kwaajili ya urejeshaji wa afya, tukitumia kila fursa inayowezekana, kwa kufanya kazi kwa kulingana na sheria za asili. Wakati tumesali ili wagonjwa wapone, tunaweza kufanya kazi kwa nguvu nyingi zaidi, tukimshukuru MUNGU kwamba tunao upendeleo wa kushirikiana Naye, na kuomba baraka Zake juu ya njia ambazo Yeye Mwenyewe ametuandalia/ametujalia.—(The Ministry of Healing, 231, 232) [Pr 237.2; Maombi Aya ya 41]

Mtumaini MUNGU bila kujali Matokeo Ya Maombi Yatakuwaje—Tunapomba kwa ajili ya kupona kwa wagonjwa, haijalishi matokeo ya jambo hilo, hebu tusipoteze imani kwa MUNGU. Ikiwa tutaitwa kukutana na msiba, hebu tukubali

kikombe chenye uchungu, tukikumbuka kwamba mkono wa Baba unakishikilia kwenye midomo yetu. Lakini ikiwa afya itarejeshwa, haipaswi kusahaulika kwamba mpokeaji wa rehema ya uponyaji anawekwa chini ya wajibu uliofanywa upya kwa Muumba. - (The Ministry of Healing, 233) [Pr 237.3; Maombi Aya ya 42]

SURA YA 23

MAOMBI KWA AJILI YA MSAMAHA

Ombi la Msamaha Daima Hujibiwa haraka yaani papo hapo— Tunapoomba baraka za kidunia, jibu la ombi letu linaweza kucheleweshwa, au MUNGU anaweza kutupa kitu kingine tofauti na tunachoomba, lakini si hivyo tunapoomba ukombozi kutoka katika dhambi. Ni mapenzi Yake kutusafisha dhambi, kutufanya sisi watoto Wake, na kutuwezesha kuishi maisha matakatifu. Masihi “alijitoa nafsi Yake kwa ajili ya dhambi zetu, ili atukomboe na ulimwengu huu mbovu wa sasa, kama yalivyo mapenzi ya MUNGU Baba yetu.” Wagalatia 1:4. “Na huu ndio ujasiri tulio nao Kwake, ya kuwa, tukiomba kitu chochote sawasawa na mapenzi Yake, Yeye anatusikia; na kama tukijua ya kuwa anatusikia, tuombalo lo lote, twajua ya kuwa tunazo haja tulizojiomba Kwake.” 1 Yohana 5:14, 15. “Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni Mwaminifu na wa haki hata atuondolee

dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote. 1 Yohana 1:9 .— (The Desire of Ages, 266) [Pr 238.1; Maombi Aya ya 1]

Mara tu mtoto wa MUNGU anapokaribia Kiti cha Rehema ndipo anakuwa mteja wa Wakili mkuu. Katika tamko lake la kwanza la toba na ombi la msamaha Kristo hutetea kesi yake na kuifanya iwe Yake Mwenyewe, akiwasilisha ombi hilo mbele ya Baba Yake kama ombi Lake Mwenyewe.—(Testimonies for the Church 6:364) [Pr 238.2; Maombi Aya ya 2]

Mwambie Yesu mahitaji yako kwa unyofu wa nafsi yako. Hautakiwi kushikilia mdahalo au hoja/mabishano marefu, au kuhubiri mahubiri kwa Mungu, bali kwa moyo wa huzuni kwa ajili ya dhambi zako, sema, “Niokoe, Bwana, la sivyo nitaangamia.” Kuna tumaini kwa roho kama hizo. Watatafuta, wataomba, watabisha, na watapata. Wakati Yesu anakapokuwa ameuondoa mzigo wa dhambi unayoiponda nafsi, utapata baraka za amani ya Kristo.— (Our High Calling, p. 131) [Pr 239.1; Maombi Aya ya 3]

Tunapoonza ubaya wa dhambi, tunaanguka bila msaada mbele ya msalaba, tukiomba msamaha na nguvu, maombi yetu yanasikika na kujibiwa. Wale wanaowasilisha maombi yao kwa MUNGU katika Jina la Kristo hawataachwa kamwe. Bwana asema, “Yeye ajaye Kwangu sitamtupa kamwe.” “Atayatazama maombi ya aliye mkiwa.” Msaada wa Maombi yetu ya Msamaha unatoka kwa Yeye ambaye anashikilia vitu vyote mikononi Mwake. Amani anayotuma ni uhakikisho wa upendo Wake kwetu. [Pr 239.2; Maombi Aya ya 4]

Hakuna kitu kinachoweza kuwa kisicho cha msaada na kisichoweza kushindwa zaidi kuliko roho inayohisi kutokuwa na kitu (utupu wake), na hivyo kuzitegemea kabisa sifa za Mwokozi aliyesulubiwa na kufufuka (kujidondosha kabisa kwa Mwokozi). MUNGU atatuma kila malaika mbinguni kumsaidia yule anayeweka tegemeo lake lote kwa Kristo, badala ya kumruhusu kushindwa.— (The Signs of the Times, Oktoba 29, 1902) [Pr 239.3; Maombi Aya ya 5]

Wale Wanaotafuta Msamaha Lazima Wenyewe Wawe na Tabia ya Kusamehe—Tunapokuja kuomba rehema na baraka kutoka kwa MUNGU tunapaswa kuwa na roho ya upendo na msamaha katika mioyo yetu wenyewe. Tunawezaje kuomba basi, “Utusamehe deni zetu, kama sisi tunavyowasamehe wadeni wetu,” na bado tuwe na roho ya kutosamehe? Mathayo 6:12. Ikiwa tunatazamia sala zetu kusikiwa ni lazima tuwasamehe wengine kwa namna ile ile na kwa kiwango kile kile tunachotamani kusamehewa.—(Steps to Christ, 97) [Pr 239.4; Maombi Aya ya 6]

Baada ya kumaliza Sala ya Bwana, Yesu aliongeza hivi: “Mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi; bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu. Mathayo 6:14, 15. Yeye asiyesamehe anafunga/anafunga kila mfereji ambao kwa huo peke yake anaweza kupokea rehema kutoka kwa

MUNGU. Hatupaswi kufikiri kwamba wale waliotuumiza wasipokiri kosa lao, sisi tuna haki ya kuwanyima msamaha wetu. Ni sehemu ya wajibu wao, bila shaka, kunyenyekeza mioyo yao kwa toba na maungamo; lakini tunapaswa kuwa na roho ya huruma kwa wale ambao wametukosea, haijalishi kamawameungama makosa yao kwetu au la.—(The Faith I Live By, p. 131) [Pr 239.5; Maombi Aya ya 7]

Katika sala ambayo Kristo aliwafundisha wanafunzi Wake kulikuwa na ombi: Utusamehe makosa yetu kama sisi tunavyowasamehe wanaotukosea. Hatuwezi kurudia sala hii kutoka moyoni na kuthubutu kuwa watu tusiosamehe, kwani tunamwomba Bwana atusamehe makosa yetu dhidi Yake kama vile sisi tunavyowasamehe wanaotukosea. Lakini ni wachache wanaotambua umuhimu wa kweli wa sala hii. Ikiwa wale wasiosamehe wangeelewa kina cha maana yake wasingethubutu kuirudia hii sana na kumwomba MUNGU awashughulikie kama wanavyoshughulika na wanadamu wenzao wafao.— (Testimonies for the Church 3:95). [Pr 240.1; Maombi Aya ya 8]

Tunahitaji kuchunguza mioyo yetu kama matayarisho ya kwenda mbele za MUNGU katika maombi, ili tujue sisi ni wa roho ya namna gani. Ikiwa hatutawasamehe wale waliotukosea, maombi yetu ya msamaha hayatasikilizwa. "Utusamehe deni zetu, kama sisi tunavyowasamehe wadeni wetu." Sisi kama wadhambi tunapokaribia Kiti cha Rehema, hatuwezi kueleza hisia ya ombi hili bila msamaha mioyoni mwetu kwa wale wote ambao wametuumiza. Juu ya ombi hili Yesu anatoa maelezo: "Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi; bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu." (The Signs of the Times, August 21, 1884) [Pr 240.2; Maombi Aya ya 9]

Kuungama Lazima Kuwe Mahususi (taja jambo lile kwa jina lake)—maungamo ya kweli daima ni ya tabia maalum, na hukiri dhambi fulani. Yanaweza kuwa ya namna ya kuletwa mbele za MUNGU tu na sio kwa binadamu wengi, yanaweza kuwa makosa ambayo yanapaswa kuungama mbele ya watu ambao wameumizwa majereraha kupitia kwazo, au yanaweza kuwa ya aina ya jumla ambayo yanapaswa kujulikana katika kusanyiko la watu. Lakini maungamo yote yanapaswa kuwa mahususi na mtu anapasa kwenda kwenye pointi/kipengele, yakikiri dhambi zote ambazo una hatia nazo.—(Testimonies for the Church 5:639) [Pr 240.3; Maombi Aya ya 10]

Yesu Anasikia Ombi Rahisi la Msamaha—Sio lazima kwamba wote wataweza kubainisha kwa uhakika wakati dhambi zao ziliposamehewa. Somo la kufundishwa kwa watoto ni kwamba dhambi na makosa yao vinapaswa kuletwa kwa Yesu katika maisha yao ya utotoni. Wafundishe kuomba msamaha Wake kila siku kwa kosa lolote walilofanya, na kwamba Yesu anasikia sala rahisi ya moyo uliotubu na wenye huzuni, Naye atasamehe, na kuyapokea, kama vile alivyowapokea watoto walioletwa Kwake alipokuwa duniani.—(Child Guidance, 494, 495) [Pr 241.1; Maombi Aya ya 11]

Kisha, watoto, njooni kwa Yesu. Mpe MUNGU sadaka ya thamani kuliko zote uwezavyo kutoa; mpe moyo wako. Anazungumza nawe akisema, “Mwanangu, binti yangu, Nipe moyo wako. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, nitazifanya nyeupe kama theluji; kwa maana nitawatakasa kwa damu yangu mwenyewe. Nitawafanya ninyi wanachama wa familia Yangu— watoto wa Mfalme wa mbinguni. Pokeeni msamaha Wangu, Amani Yangu ninayowapa ninyi bure. Nitawavika ninyi kwa haki Yangu, vazi la harusi, na kuwafanya mstahili karamu ya harusi ya Mwana- Kondoo. Mnapovikwa haki Yangu, kwa maombi, kwa kukesha, kupitia kujifunza Neno Langu kwa bidii, mtaweza kufikia kiwango cha juu. Mtaelewa Ukweli, na tabia yenu itaundwa/itafinyangwa na ushawishi wa Bwana; “Ombeni kwa ajili ya Msamaha kwani haya ni mapenzi ya MUNGU, hata kutakaswa kwenu.” (The SDA Bible Commentary 3:1162) [Pr 241.2; Maombi Aya ya 12]

Ni muhimu sana kwamba tunapaswa kuomba ili tupate nguvu kutoka juu ya kuyaona na kuyapinga majaribu ya adui; lakini Shetani hutafuta siku zote kuwazuia watu wasiombe, kwa kuujaza muda wao kwa biashara, biashara au starehe, au kwa kuwaongoza katika uovu wa namna hiyo hata wasiwe na hamu ya kuomba. Bwana Yesu amefanya mbingu ifikike kwa wote wanaoenda Kwake, na anawaalika watoto na vijana waje Kwake. Akisema, “Waacheni watoto wadogo waje kwangu, wala msiwazuie; kwa maana ufalme wa MUNGU ni wao.” Yesu angetaka watoto na vijana waje Kwake wakiwa na ujasiri ule ule wanaoenda nao kwa wazazi wao. Kama vile mtoto anavyomuomba mama yake au baba yake chakula akiwa na njaa, ndivyo Bwana anavyotaka ninyi muombe kile mnachohitaji. Ikiwa dhambi zako ni nzito juu ya moyo wako, unapaswa kwenda kwa MUNGU na kusema, “Kwa ajili ya Masihi, nisamehe dhambi zangu.” Kila sala ya unyoofu itasikiwa mbinguni, na kila ombi la dhati na bidii la neema na nguvu litajibiwa.—(The Youth’s Instructor, July 7, 1892) [Pr 241.3; Maombi Aya ya 13]

Ombi la Msamaha Lazima Lionyeshwe Kuwa la Unyofu (litoke moyoni)— “Usinitenge na uso wako, wala usimwondoe Roho wako Mtakatifu.” Toba pamoja na msamaha ni zawadi ya MUNGU kupitia Masihi. Ni kupitia ushawishi wa Roho Mtakatifu ndipo tunasadikishwa kuhusu dhambi, na kuhisi hitaji letu la msamaha. Hakuna wanaosamehewa isipokuwa wale walio na moyo uliopondeka; lakini ni neema ya Bwana ifanyayo moyo kutubu. Anafhamu udhaifu na mapungufu yetu wote, Naye atatusaidia. Atasikia maombi ya imani; lakini unyoofu wa sala unaweza kuthibitishwa tu kwa jitihada zetu za kujileta kwenye mapatano na kile kiwango kikuu cha maadili ambacho kitapima tabia ya kila mtu (Amri Zake Kumi). Tunahitaji kufungua mioyo yetu kwa ajili ya ushawishi wa Roho, na kupata uzoefu wa nguvu Zake zinazobadilisha.—(The Review and Herald, June 24, 1884) [Pr 242.1; Maombi Aya ya 14]

“Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni nanyi mtapata; bisheni, nanyi mtafunguliwa,” Kwa nini hatumwendei MUNGU kwa Neno Lake? kuomba na kupokea

vimeunganishwa kwa karibu. Ikiwa utaomba kwa imani mambo ambayo MUNGU ameahidi, utapokea. Mwangelie Yesu kwa ajili ya mambo unayohitaji. Mwombe msamaha wa dhambi, na unapoomba kwa imani moyo wako utalainishwa, na utawasamehe wale waliokuumiza, na maombi yako yatakwenda kwa MUNGU yakiwa na harufu nzuri ya upendo. Pamoja na kuomba huja kukesha katika maombi, na kila wazo na neno na tendo vitaambatana na ombi lako la dhati kwa ajili ya matengenezo katika maisha. Maombi ya imani yataleta huleta matunda stahiki. Lakini kutamka aina ya maneno tu kwa desturi, bila unyofu wa dhati na matamano ya dhati ya msaada, bila kutarajia utapokea, haitakufaa kitu. Mwombaji wa namna hii asidhani ya kuwa atapokea kitu kwa Bwana. Wale wanaokuja kwa MUNGU lazima waamini kwamba Yeye yuko, na kwamba Yeye ni mtoa thawabu wa wale wanaomtafuta kwa bidii.—(The Review and Herald, March 28, 1912) [Pr 242.2; Maombi Aya ya 15]

SURA YA 24

MAOMBI YA KUOMBEA WENGINE- MAOMBEZI

Waombeeni Wengine—Hebu na tujitahidi kutembea katika nuru kama Kristo alivyo katika nuru. Bwana aligeuza utumwa wa Ayubu alipoomba, si kwa ajili yake tu, bali kwa ajili ya wale waliokuwa wakimpinga. Wakati Alipohisi kutamani sana kwamba roho zilizomkosea zipate kusaidiwa, yeye mwenyewe alipata msaada. Tuombe, sio kwa ajili yetu tu, bali kwa wale ambao wametuumiza, na wanaoendelea kutuumiza. Omba, omba, hasa katika akili yako. Usimpe Bwana pumziko; kwa maana masikio Yake yako wazi ili kusikia maombi yenye unyoofu, yasichoka na yenye kusihi, wakati nafsi inaponyenyekezwa/inapojidhili mbele Zake.— (The SDA Bible Commentary 3:1141) [Pr 244.1; Maombi Aya ya 1]

Unapaswa kuwa wakala ambaye kupitia Kwake MUNGU atazungumza na Roho. Mambo ya thamani yataletwa kwenye ukumbusho wako, na kwa moyo unaofurika kwa upendo wa Yesu, utazungumza Maneno ya kupendeza na muhimu. Usahili wako na unyofu wako utakuwa umbuji/ufasaha wa hali ya juu zaidi, na maneno yako yataandikwa katika vitabu vya mbinguni kuwa maneno yanayofaa, ambayo ni kama tufaha za dhahabu katika picha za fedha. MUNGU atayafanya kuwa mafuriko ya uponyaji ya mvuto wa mbinguni, yakiamsha kusadikishwa na shauku, na Yesu ataongeza maombezi Yake kwenye maombi yako, na kudai kwa ajili ya mwenye dhambi zawadi ya Roho Mtakatifu, na kuimwaga juu ya nafsi yake. Na kutakuwa na shangwe mbele ya malaika wa MUNGU kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja anayetubu.— (Sons and Daughters

of God, 274) [Pr 244.2; Maombi Aya ya 2]

Kuna wale wanaokuzunguka ambao wana huzuni, ambao wanahitaji maneno ya huruma, upendo, na laini, na maombi yetu ya unyenyekevu, yenye kuonyesha sikitiko. — (Testimonies for the Church 3:530) [Pr 245.1; Maombi Aya ya 3]

Katika kumwita MUNGU Baba yetu, tunatambua watoto Wake wote kama ndugu zetu. Sisi sote ni sehemu ya mtandao mkuu wa ubinadamu, sote ni washiriki wa familia moja. Katika maombi yetu tunapaswa kujumuisha majirani zetu na sisi wenyewe. Hakuna anayeomba kwa njia ifaayo ambaye anajitafutia baraka yeye peke yake.— (Sons and Daughters of God, 267) [Pr 245.2; Maombi Aya ya 4]

Tunapotafuta kuwaleta wengine kwa Kristo, tukibeba mzigo wa roho katika maombi yetu, mioyo yetu itapatwa na ushawishi wa kuhuisha wa neema ya MUNGU; mapenzi yetu yatang'aa zaidi kwa jitihada za Bwana; maisha yetu yote ya Kikristo yatakuwa ya kweli na halisi zaidi, yenye bidii zaidi, na ya maombi zaidi. - (Christ Object Lessons, 354). [Pr 245.3; Maombi Aya ya 5]

Kuna nafsi ambazo zimepoteza ujasiri wao; zungumza nao, uwaombee. Kuna wanaohitaji Mkate wa Uzima. Wasomee kutoka katika Neno la MUNGU. Kuna ugonjwa wa roho ambao hakuna zeri inayoweza kuugusa, hakuna dawa inayoweza kuponya. Waombee hawa, na uwalete kwa Yesu Kristo. Na katika kazi yako yote Kristo atakuwepo kufanya ushawishi kwenye mioyo ya wanadamu.— (Welfare Ministry, 71) [Pr 245.4; Maombi Aya ya 6]

Hebu wale walio wa kiroho wazungumze na nafsi hizi. Omba nao na kwa ajili yao. Hebu muda mwingi utumike katika maombi na kulichunguza Neno kwa karibu. Hebu wote wapate mambo ya halisi na ya kweli ya imani katika nafsi zao wenyewe kwa njia ya imani kwamba Roho Mtakatifu atakabidhiwa kwao kwa sababu wana njaa na kiu ya Kweli ya haki.— (Testimonies for the Church 6:65). [Pr 245.5; Maombi Aya ya 7]

Wakati Ubinafsi unapokufa, kutakuwa na uamsho wa hamu kubwa kuhusiana na wokovu wa wengine, - matamania ambayo yatasababisha juhudi za kudumu na zenye uvumilivu katika kutenda mema. Kutakuwa na kupanda kando ya maji yote; na dua ya dhati, zizochoka, maombi ya kudumu, yataingia mbinguni kwa ajili ya nafsi zinazoangamia.—(Gospel Workers, 470). [Pr 246.1; Maombi Aya ya 8]

Oh, jamani kama sala ya dhati na ya imani ingetokezea kila mahali, Nipe roho zilizozikwa sasa kwenye uchafu wa makosa, la sivyo nife! Walete kwenye ujuzi wa Ukweli kama ulivyo ndani ya Yesu.—(This Day With God, 171). [Pr 246.2; Maombi Aya ya 9]

Anzeni kuombea roho; njooni karibu na Kristo, karibu na ubavu Wake unaotoka damu. Hebu roho ya upole na utulivu iyapambe maisha yenu, Hebu maombi yenu ya dhati na bidii, yaliyopondeka, ya unyenyekevu yapande Kwake kwa ajili ya

hekima ili mpate kufanikiwa katika kuokoa sio nafsi zenu tu, bali na nafsi za wengine.— Testimonies for the Church 1 :513) [Pr 246.3; Maombi Aya ya 10]

Kuna wengi ambao matumaini yamewatoka. Warudishie mwanga wa jua hawa. Wengi wamepoteza ujasiri wao. Zungumza nao maneno ya furaha na ya kuwachangamsha. Omba kwa ajili yao.—(Prophets and Kings, 719) [Pr 246.4; Maombi Aya ya 11]

Nafsi zinapaswa kutafutwa, kuombewa, kufanyiwa kazi. Rufaa za dhati zinapaswa kufanywa. Maombi ya dhati yanapaswa kutolewa. Maombi yetu dhaifu, yasiyo na roho yanapaswa kubadilishwa kuwa maombi ya dhati na bidii sana.—(Testimonies for the Church 7:12). [Pr 246.5; Maombi Aya ya 12]

Kazi hii inakuhitaji uzilinde roho kama yule ambaye lazima utazitolea hesabu. Upole wa Kristo lazima uujaze moyo wa Mfanyakazi wa Sala ya Maombezi. Ikiwa una upendo kwa roho utaonyesha kujali kwa dhati kwa ajili yao. Utatoa maombi ya unyenyekevu, ya dhati, ya kutoka moyoni kwa wale unaowatembelea. Harufu ya upendo wa Kristo itadhihirishwa katika kazi yako. Yeye ambaye alitoa maisha Yake kwa ajili ya maisha ya ulimwengu atashirikiana na mtenda kazi asiye na uchoyo au ubinafsi kuweka msukumo juu ya mioyo ya wanadamu.—(Testimonies for the Church 6:75, 76) [Pr 246.6; Maombi Aya ya 13]

Hebu na tuufanyie kazi mpango huu, na tuombeane, tukipelekana moja kwa moja katika uwepo wa MUNGU kwa imani iliyo hai.—(The Review and Herald, August 28, 1888) [Pr 247.1; Maombi Aya ya 14]

Omba Upate Baraka Ili Kuwabariki Wengine—Maombi yetu hayapaswi kuwa maombi ya uchoyo au ubinafsi, kwa faida yetu wenyewe tu. Tunapaswa kuomba ili tuweze kutoa. Kanuni ya maisha ya Kristo lazima iwe kanuni ya maisha yetu. “Kwa ajili yao,” Yeye alisema, akizungumza juu ya wanafunzi Wake, “Najiweka wakfu, ili nao watakaswe.” Yohana 17:19. Kujitoa huko huko, kujitolea nafsi kwa namna ile ile, utiifu uleule wa madai ya Neno la MUNGU, ambao ulidhihirika katika Kristo, lazima uonekane kwa watumishi Wake.

Utume au misheni yetu kwa ulimwengu sio kujitumikia wenyewe, au kujifurahisha wenyewe; tunapaswa kumtukuza MUNGU kwa kushirikiana Naye katikakuwaokoa wenye dhambi. Tunapaswa kuomba baraka kutoka kwa MUNGU ili tuweze kuwasilisha kwa wengine. Uwezo wa kupokea huhifadhiwa kwa kutoa tu (tunapokea tu tukitoa). Hatuwezi kuendelea kupokea hazina ya mbinguni bila kuwasiliana na wale wanaotuzunguka.— (Christ's Object Lessons, 142, 143) [Pr 247.2; Maombi Aya ya 15]

Tunapomba, “Utupe leo mkate wetu wa kila siku,” tunaomba kwa ajili ya wengine na pia sisi wenyewe. Na tunakubali kwamba kile ambacho MUNGU anatupa si kwa ajili yetu wenyewe tu. MUNGU hutukabidhi kama amana, ili tuwalishe wenye njaa.—(Thoughts from the Mount of Blessing, 111, 112) [Pr

247.3; Maombi Aya ya 16]

Waombee Wengine Katika Ombi la faragha—Katika ombi la faragha wote wana fursa ya kuomba kadiri wapendavyo na kuwa wazi wapendavyo. Wanaweza kuomba kwa ajili ya jamaa na marafiki zao wote. Chumbani ni mahali pa kueleza shida zao zote binafsi, na mitihani, na majaribu. Mkutano wa pamoja wa kumwabudu MUNGU si mahali pa kufungua mambo binafsi au siri za moyoni.—(Testimonies for the Church 2:578) [Pr 247.4; Maombi Aya ya 17]

Ombea Wale Wanaohubiri na Kuhudumu—Miongoni mwa watu wa MUNGU kunapaswa kuwa na misimu ya mara kwa mara ya maombi ya dhati na ya bidii. Akili inapaswa kuwa katika mkao/mtazamo wa maombi kwa kiasi kikubwa. Nyumbani na kanisani hebu kuwe na maombi ya dhati na bidii na yatolewe kwa niaba ya wale ambao wamejitoa katika kuhubiri Neno.—(In Heavenly Places, 87) [Pr 247.3; Maombi Aya ya 18]

Wakati vijana wanapoenda kuhubiri Ukweli, mnapaswa kuwa na majira ya maombi kwa ajili yao. Omba kwamba MUNGU awaunganishe na Yeye Mwenyewe na awape hekima, neema, na maarifa. Ombeni ili waweze kulindwa na mitego ya Shetani iliyojificha na kuwekwa safi katika mawazo na utakatifu wa moyo. Ninawasihi ninyi mnaomcha Bwana, msipoteze wakati katika mazungumzo yasiyofaa, au katika kazi isiyo na maana, ili kujipatia kiburi, au kuridhisha tamaa ya chakula au ya mwili. Hebu wakati unaopatikana utumike katika kupambana mieleka na MUNGU kwa ajili ya wachungaji/wahudumu wenu. Inueni mikono yao kama Haruni na Huri walivyoifanya mikono ya Musa.—(Testimonies for the Church 5:162) [Pr 248.1; Maombi Aya ya 19]

Omba kwa ajili ya Vijana wa Kanisa — Hebu wale walio wazee katika uzoefu waangalie vijana; na wanapowaona wakijaribiwa, wawachukue kando, na waombe nao na kwa ajili yao. —(Messages to Young People, 18). [Pr 248.2; Maombi Aya ya 20]

Walimu wa Shule ya Sabato Ombeeni Washiriki wa Darasa Lenu—Kama wafanyakazi wa MUNGU tunahitaji zaidi kuwa kama Yesu na kupunguza ubinafsi. Tunapaswa kuwa na mzigo zaidi kwa ajili ya nafsi, na tunapaswa kuomba kila siku kwamba nguvu na hekima ziweze kutolewa kwa ajili ya Sabato. Waalimu, kutaneni na madarasa yenu. Omba pamoja nao, na uwafundishe jinsi ya kuomba. Hebu moyo ulainishwe, na maombi yawe mafupi na mepesi, lakini ya dhati na bidii.—(Counsels on Sabbath School Work, 125) [Pr 248.3; Maombi Aya ya 21]

Wanafunzi waombe kwaajili ya Walimu-Wanafunzi wanapaswa kuwa na nyakati zao za maombi, ambapo wanaweza kutoa maombi ya kudumu, marahisi ili MUNGU ambariki rais wa shule kwa nguvu za mwili, akili timamu, nguvu ya maadili, na utambuzi wa kiroho, na kwamba kila mwalimu astahili kwa neema ya MUNGU kufanya kazi yake. — (Fundamentals of Christian Education, 293) [Pr 248.4; Maombi Aya ya 22]

Omba kwa ajili ya Wakristo Wenzako—Mara nyingi sana tunasahau kwamba watenda kazi wenzetu wanahitaji nguvu, faraha na uchangamfu. Katika nyakati za wasiwasi fulani na mzigo, kuweni makini kuwahakikishia kujali kwenu na huruma. Wakati mnapojaribu kuwasaidia kwa maombi yenu, wajulishe kwamba mnaifanya hivyo. Muambatanishe ujumbe wa MUNGU kwa wafanyakazi Wake: “Iweni hodari na moyo wa ushujaa.” Yoshua 1:6.—(Testimonies for the Church 7:185) [Pr 249.1; Maombi Aya ya 23]

Wazazi wawaombee Watoto Wao—MUNGU ameahidi kuwapa hekima wale wanaomba kwa imani, Naye Atafanya kama vile Yeye alivyosema. Yeye Anapendezwa na imani inayomuendea kupitia Neno Lake. Mama Augustine aliomba kwa ajili ya uongofu wa mwanaye. Hakuona ushahidi wowote kwamba Roho wa MUNGU alikuwa akiushawishi moyo wake, lakini hakuvunjika moyo. Aliweka kidole chake kwenye maandiko, akiwasilisha mbele za MUNGU Maneno Yake Mwenyewe, na kusihi kama mama awezavyo kusihi. Kujidhili kwake kwa dhati, kusihi kwake kwa bidii bila ya kuchoka, imani yake isiyoyumbayumba, ilishinda, na Bwana akampa haja ya moyo wake. Hata hivi leo Yuko tayari kusikiliza maombi ya watu Wake. “Mkono Wake si mfupi hata usiweze kuokoa wala sikio Lake si zito hata lisiweze kusikia”; na wazazi wakikristo wakimtafuta kwa bidii, Yeye atajaza vinywa vyao hoja, na, kwa ajili ya Jina Lake, atafanya kazi kwa nguvu kwa ajili yao katika wongofu wa kwa watoto wao.— (Testimonies for the Church 5:322, 323. [Pr 249.2; Maombi Aya ya 24]

Tunapaswa kuomba kwa MUNGU zaidi ya tunavyoomba. Kuna nguvu nyingi na baraka katika kuomba pamoja katika familia zetu, kuomba pamoja na watoto wetu na pia kuwaombea tukiwa wenyewe.—(Child Guidance, 525). [Pr 249.3; Maombi Aya ya 25]

Hebu Kristo akupatie mkono Wake wa msaada ili kutekeleza makusudi Yake. Kwa maombi unaweza kupata uzoefu ambao utafanya huduma yako kwa watoto wako iwe na mafanikio kamili.— (Child Guidance, 69) [Pr 249.4; Maombi Aya ya 26]

Haukuona kuwa ni kazi ngumu au mzigo ikiwa njia ingefunguka ili uweze kuwatunza watoto wako na kuwakinga kutokana na uovu ulioenea katika nyakati hizi za ulimwengu. Ulikuwa mzigo wa moyo wako kuwaona wao wakimgeukia Bwana. Uliomba mbele za MUNGU kwa ajili ya watoto wako kwa vilio vikali na machozi. Ulitamani sana uongofu wao. Wakati fulani moyo wako ulikata tamaa na kuzimia, na ukaogopa kwamba maombi yako yasingejibiwa; lakini ukawaweka tena wakfu watoto wako kwa MUNGU, na moyo wako wenye shauku uliwaweka upya juu ya madhabahu. [Pr 249.4; Maombi Aya ya 27]

Walipoingia jeshini, maombi yako yaliwafuata. Walihifadhiwa kwa ajabu dhidi ya madhara. Wao waliita kuwa ni bahati nzuri; lakini maombi ya mama kutoka

kwenye nafsi yenye wasiwasi, yenye kulemewa na mzigo, alipohisi hatari ya watoto wake na hatari ya kukatiliwa mbali katika ujana wao bila tumaini kwa MUNGU yalikuwa na mengi ya kufanya juu ya kuhifadhiwa kwao. Ni maombi mangapi yaliingia mbinguni ili wana hawa wahifadhiwe ili wamtii MUNGU, na kisha wayatoe maisha yao kwa utukufu Wake! Katika mahangaiko yako kwa ajili ya watoto wako ulimsihi MUNGU awarudishe kwako tena, na ulitafuta kwa bidii zaidi kuwaongoza katika njia ya utakatifu.—(Testimonies for the Church 2:274, 275) [Pr 250.1; Maombi Aya ya 28]

Yeye [MUNGU] hatakataa kusikia maombi ya dhati na bidii ya wazazi, ambayo yanaungwa mkono na bidii ya kudumu, ili watoto wao wapate baraka kutoka Kwake, na kuwa wafanyakazi waaminifu katika kazi Yake. Wazazi wanapofanya wajibu wao kwa njia iliyowekwa na MUNGU, wanaweza kuwa na uhakika kwamba maombi yao ya msaada Wake katika kazi yao ya nyumbani yatakubaliwa.—(The Signs of the Times, May 4, 1888) [Pr 250.2; Maombi Aya ya 29]

Kesha kila wakati ili kukata mkondo na kurudisha nyuma uzito wa uovu ambao Shetani anausukuma juu ya watoto wako. Watoto hawawezi kufanya hiliwenyewe. Wazazi wanaweza kufanya mengi. Kwa ombi la dhati na bidii na imani iliyo hai, ushindi mkubwa utapatikana.—(Spiritual Gifts 4b, 139) [Pr 250.3; Maombi Aya ya 30]

Kufanya kazi yake inavyopaswa kufanywa kunahitaji talanta na ustadi na uvumilivu wenye umakini mkubwa. Inahitaji kutojiamini nafsi na kuomba kwa bidii. Hebu kila mama na ajitahidi kwa bidii katika kutimiza wajibu wake. Hebu awalete watoto wake wadogo kwa Yesu kwa mikono ya imani, akimwambia Yeye hitaji lake kubwa, na kuomba hekima na neema.— (Counsels to Parents, Teachers, and Students, 128) [Pr 250.4; Maombi Aya ya 31]

Juhudi zenye bidii na zenye maumivu, maombi na imani, vikiunganishwa na mfano sahihi, havitakosa matunda. Walete watoto wako kwa MUNGU kwa imani, na utafute kushawishi akili zao kupata hisia ya wajibu wao kwa Baba yao wa mbinguni.— (Temperance, 157, 158) [Pr 251.1; Maombi Aya ya 32]

Usitarajie badiliko lifanyike kwa watoto wako pasipo subira, kazi ya dhati, iliyochanganyika na maombi ya bidii. Kusoma na kuelewa tabia zao mbalimbali, na siku baada ya siku kuwafinyanga kulingana na Kielelezo cha Bwana, ni kazi inayohitaji bidii kubwa na ustahimilivu, na maombi mengi, pamoja na imani yenye kudumu katika ahadi za MUNGU.— (The Signs of the Times, May. 4, 1888) [Pr 251.2; Maombi Aya ya 33]

Hata mtoto mchanga mikononi mwa mama yake anaweza kukaa chini ya uvuli wa Mwenyezi kwa imani ya mama anayeomba. - (The Desire of Ages, 512) [Pr 251.3; Maombi Aya ya 34]

Akina baba na akina mama, je, hamtashikilia kazi yenu kwa nguvu, uvumilivu,

na upendo? Panda mbegu ya thamani kila siku, kwa maombi ya dhati ili MUNGU aimwagilie kwa umande wa neema, na kukupa mavuno mengi sana. Mwana wa MUNGU alikufa ili kukomboa jamii ya bindamu yenye dhambi na iliyoasi. Je, tujiepushe na taabu, kujitoa kujitoa mhanga au dhabihu yoyote ili kuokoa watoto wetu wapendwa?—(The Signs of the Times, November 24, 1881) [Pr 251.4; Maombi Aya ya 35]

Baada ya kufanya wajibu wako kwa uaminifu kwa watoto wako, basi wabebe na uwapeleke kwa MUNGU na umwombe akusaidie. Mwambie kwamba umetimiza sehemu yako ya Sala ya Maombezi, kisha kwa imani umwombe MUNGU afanye sehemu Yake, ambayo wewe hauwezi kuifanya.—(Child Guidance, 256) [Pr 251.5; Maombi Aya ya 36]

SURA YA 25

MALAIKA NA MAOMBI

Malaika Huweka katika kumbukumbu Kila Ombi la Dhati— Tunapaswa

kumfahamu MUNGU sasa kwa kuthibitisha ahadi Zake. Malaika huweka katika rekodi kila ombi ambalo ni la dhati na lenye bidii. Afadhali tutupilie mbali kuuridhisha ubinafsi kuliko kupuuza ushirika na MUNGU. Umaskini mkubwa zaidi, kujikana zaidi pamoja na kibali Chake, ni bora kuliko utajiri, heshima, urahisi wa maisha, na urafiki bila kibali Chake. Ni lazima tuwe na muda wa kuomba. (The Great Controversy, 622) [Pr 252.1; Maombi Aya ya 1]

Hebu malaika wanaotunza kumbukumbu waandike historia ya mapambano matakatifu na migogoro ya watu wa MUNGU, hebu na waandike maombi yao na machozi; lakini hebu MUNGU asidharauliwe kwa madai kutoka katika midomo ya wanadamu, yanayosema, “Mimi sina dhambi. Mimi ni mtakatifu.” Midomo iliyotakaswa haitatamka kamwe maneno hayo yenye kiburi au dhana potofu.—(The Signs of the Times, May 23, 1895) [Pr 252.2; Maombi Aya ya 2]

Malaika Wanaweza Kusikia Maombi yetu— kama wanadamu wangeweza kuona kwa maono ya mbinguni, basi wangeona makundi ya malaika walio na nguvu nyingi zaidi wakiwa na wale ambao wameshika Neno la subira ya Kristo. Kwa upole wenye huruma, malaika wameona taabu yao. Pr 252.3; Maombi Aya ya 3]

Malaika Hupeleka Maombi yetu Mbinguni—Familia iliyo na nidhamu njema, inayompenda na kumtii MUNGU, itakuwa na furaha na uchangamfu. Baba anaporudi kutoka katika kazi yake ya kila siku, hataleta mashaka au misongo yake nyumbani kwake. Atahisi kuwa nyumba, na mzunguko wa familia, ni vitakatifu sana kiasi kwamba haviwezi kuharibiwa na mifadhaiko isiyofurahisha. Alipoondoka nyumbani kwake, hakumuacha nyuma Mwokozi wake na dini yake. Vyote viwili vilikuwa katika ushirika naye. Ushawishi mzuri wa nyumba yake, baraka ya mke wake, na upendo wa watoto wake, vinafanya mizigo yake kuwa myepesi; na anarudi akiwa na amani moyoni mwake, na maneno ya uchangamfu, yenye kutia moyo kwa mke wake na watoto, ambao wanangoja kwa shangwe kukaribisha ujio wake. Anapoinama pamoja na familia yake kwenye madhabahu ya sala ili kutoa shukrani zake kwa MUNGU kwa ajili ya utunzaji Wake kwake pamoja na wapendwa wake siku nzima, malaika wa MUNGU anakuwa kwenye chumba hicho akizunguka , na kubeba maombi ya bidii ya wazazi wanaomcha MUNGU mbinguni, kama uvumba mzuri, ambao hujibiwa kwa baraka zinazorudi.— (Selected Messages 2:439, 440) [Pr 253.1; Maombi Aya ya 4]

Malaika husikia sifa zinazotolewa na ombi la imani, na hupeleka maombi kwa Yeye ambaye huhudumu katika Patakatifu kwa ajili ya watu Wake, na kuombea wema na haki Yake kwa niaba yao. Ombi la Kweli humshikilia Mweza wa yote, na huwapa wanadamu ushindi. kwa kupiga magoti yake, Mkristo hupata nguvu za kukinzana na vishawishi.—(The Review and Herald, February 1, 1912) [Pr 253.2; Maombi Aya ya 5]

MUNGU hawaachi watoto Wake wapotovu walio dhaifu katika imani, na

wanaofanya makosa mengi. Bwana husikiliza na kusikia maombi yao na ushuhuda wao. Wale wanaomtazama Yesu siku kwa siku na saa kwa saa, wanaokesha kwa maombi, wanamkaribia Yesu. Malaika walio na mbawa zilizochanuliwa hungoja kupeleka sala zao za toba kwa MUNGU, na kuzisajili katika vitabu vya mbinguni.—(The SDA Bible Commentary 4:1184) [Pr 253.3; Maombi Aya ya 6]

Malaika Hungoja Kujibu Maombi Yetu—Mara nyingi katika kujali wanaoteseka, uangalifu mwingi unatolewa juu ya mambo madogomadogo, huku hitaji la wagonjwa la zile Kweli zote kuu za wokovu wa injili, ambazo zitahudumu kwenye roho na mwili, zimesahaulika. Unapopuuza kuwaombea wagonjwa, unawanyima baraka kubwa; kwa maana malaika wa MUNGU wanangoja kuhudumu kwenye nafsi hizi katika kuitikia maombi yako.—(Medical Ministry, 195) [Pr 253.4; Maombi Aya ya 7]

Kabla ya kuondoka nyumbani kwa ajili ya kazi, familia yote inapaswa kuitwa pamoja; na baba, au mama wakati baba hayupo, anapaswa kumwomba MUNGU kwa bidii ili awahifadhi kwa siku nzima. Njoo kwa unyenyekevu (kwa Bwana), kwa moyo mwororo, na kwa hisia ya majaribu na hatari mbele yanayowazunguka ninyi na watoto wenu; kwa imani uwafunge juu ya madhabahu, na kuwaombea utunzaji wa Bwana. Malaika wanaohudumu watawalinda watoto ambao wamewekwa wakfu kwa namna hiyo na MUNGU.—(Child Guidance, 519) [Pr 254.1; Maombi Aya ya 8]

Malaika Mahsusi Huteuliwa Kujibu Maombi—Viumbe wa Mbinguni wameteuliwa kujibu maombi ya wale wanaofanya kazi bila ubinafsi kwa ajili ya kazi ya MUNGU. Malaika wa juu kabisa katika nyua za mbinguni wameteuliwa kufanyia kazi maombi ambayo hupanda kwa MUNGU kwa ajili ya kuendeleza kazi ya MUNGU. Kila malaika ana shuguli/wadhifa wake maalum wa kazi, ambapo haruhusiwi kuondoka kwenda mahali pengine popote. Kama angeondoka, nguvu za giza zingepata nafasi.... [Pr 254.2; Maombi Aya ya 9]

Siku baada ya siku mzozo kati ya wema na uovu unaendelea. Kwa nini wale ambao wamepata fursa nyingi na manufaa hawatambui uzito mkubwa wa kazi hii? Wanapaswa kutumia akili katika suala hili. MUNGU Ndiye Mtawala. Kwa uweza Wake mkuu Yeye huwadhibiti na kuwaongoza watawala wa kidunia. Kupitia mawakala Wake Anafanya kazi ambayo iliamriwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. [Pr 254.3; Maombi Aya ya 10]

Kama binadamu hatuelewi jinsi tunavyopaswa kuelewa lile pambano kuu linaloendelea kati ya mashirika yasiyoonekana, pambano kati ya malaika waaminifu na wasio waaminifu. Malaika waovu wanafanya kazi kila mara, wakipanga safu yao ya mashambulizi, wakitawala kama makamanda, wafalme, na viongozi, wa majeshi ya wanadamu wasio waaminifu...Ninatoawito kwa wahudumu wa Kristo kushinikiza nyumbani juu ya uelewa wa wote wanaoweza

kufikiwa na sauti zao, Ukweli wa huduma ya malaika. Msijiingize katika dhana za kufikirika zinazopendezesha moyo. Neno lililoandikwa ndio usalama wetu pekee. Ni lazima tuombe kama Danieli, ili tulindwe na viumbe vyenye akili vya mbinguni (malaika). Kama roho watumikao, malaika hutumwa kuwahudumia wale watakaorithi wokovu. Ombeni, ndugu zangu, ombeni kuliko mliyowahi kuomba kabla. Hatuko tayari kwa ajili ya ujio wa Bwana. Tunahitaji kufanya kazi kamilifu kwa ajili ya umilele.—(The SDA Bible Commentary 4:1173) [Pr 254.4; Maombi Aya ya 11]

MUNGU ameweka malaika wanaofanya mapenzi yake kujibu maombi ya wanyenyekevu wa dunia, na kuwaongoza watumishi Wake kwa ushauri na maamuzi. Mawakala wa mbinguni wanatafuta kila mara kutoa neema na nguvu na ushauri kwa watoto waaminifu wa MUNGU, ili waweze kutenda sehemu yao katika kazi ya kuwasilisha nuru kwa ulimwengu.—(Testimonies to Ministers and Gospel Workers, 484) [Pr 255.1; Maombi Aya ya 12]

Malaika wanaohudumu wanangojea karibu na kiti cha enzi kutii mara moja agizo la Yesu Kristo la kujibu kila ombi linalotolewa kwa imani hai iliyo ya bidii.—(Selected Messages 2:377) [Pr 255.2; Maombi Aya ya 13]

Laiti sote tungeweza kutambua ukaribu wa mbingu na dunia! Watoto waliozaliwa duniani hawalijui hili, kwamba wana malaika wa nuru kama webzu ba walinzi wao; kwa maana wajumbe wa mbinguni wanatumwa kuwahudumia wale ambao watakuwa warithi wa wokovu. Shahidi wa siri hulinda kila nafsi inayoishi, akitafuta kushinda na kuivuta kwa Kristo. Malaika hawamwachi kamwe yule anayejaribiwa kuwa mawindo kwa adui ambaye ataangamiza roho za watu ikiwa ataruhusiwa kufanya hivyo. Maadamu kuna tumaini, mpaka watakapompinga Roho Mtakatifu kwa uharibifu wao wa milele, wanadamu wanalindwa na walinzi wa mbinguni. [Pr 255.3; Maombi Aya ya 14]

Oh jamani! Kama wote wangeweza kumwona Mwokozi wetu wa thamani kama alivyo, Mwokozi. Hebu mkono Wake uvute pazia ambalo huficha utukufu Wake dhidi ya macho yetu. Itamwonyesha Yeye katika mahali Pake pa juu na Patakatifu. Je! Tunaona nini? Mwokozi wetu, si katika hali ya ukimya na kutotenda. Amezungukwa na viumbe wa mbinguni wenye utashi (malaika), makerubi, na maserafi, elfu kumi mara elfu kumi ya malaika. Viumbe hawa wote wa mbinguni wana kitu kimoja juu ya vingine vyote, ambacho wanapendezwa nacho sana —kanisa Lake katika ulimwengu wa uharibifu Wanafanya kazi kwa ajili ya Kristo chini ya agizo Lake, ili kuwaokoa kabisa wote wamtazamao na kuamini ndani Yake. [Pr 255.4 15]

Malaika wa mbinguni huagizwa kuwatazama kondoo wa malisho ya Kristo. Wakati Shetani akiwa na mitego yake yenye udanganyifu ambayo angewapotosha ikiwezekana hata wale wateule, malaika hawa walianzisha mkakati/operesheni ambayo itaokoa roho zilizojaribiwa ikiwa watalitii Neno la

Bwana, watambue hatari yao, na kusema, “La, sitaingia katika mpango huo wa Shetani. Nina Ndugu yangu mkubwa kwenye kiti cha enzi mbinguni, ambaye ameonyesha kwamba ana nia ya upole na wema kwangu, na sitauhuzunisha moyo Wake wa upendo.” [Pr 256.1; Maombi Aya ya 16]

Tukiwa tunaishi katikati ya nguvu hizi zinazopingana (uovu na wema), kupitia kuizoesha imani yetu na maombi, tunaweza kuita msafara wa malaika wa mbinguni kuja upande wetu na kutusindikiza, na hao watatulinda dhidi ya kila ushawishi wenye uovu.— (Our High Calling, 23.) [Pr 256.2; Maombi Aya ya 17]

Malaika Huzingatia na Kuyatia Alama maombi yetu, Kisha Hutoa Msaada—Unapoamka asubuhi, Je! unahisi kutokuwa na uwezo kwako, na uhitaji wako wa nguvu kutoka kwa MUNGU? Na je, wewe humjulisha Baba yako wa mbinguni mambo unayotaka kwa unyenyekevu na kutoka moyoni? Ikiwa ni hivyo, Malaika huzingatia maombi yako, na ikiwa maombi haya hayakutoka katika midomo ya kinafiki, unapokuwa katika hatari ya kufanya makosa bila kujua, na kusukuma ushawishi ambao utawaongoza wengine kufanya maovu, malaika wako mlezi atakuwa upande wako, kukuelekeza kwenye njia bora zaidi, kukuchagulia maneno yako, na kuathiri/kushawishi matendo yako. [Pr 256.3; Maombi Aya ya 18]

Ikiwa hauhisi hatari yo yote, na ikiwa haufanyi maombi ya msaada na nguvu ya kupinga vishawishi, hakika utapotea; kupuuza kwako wajibu kutaandikwa katika kitabu cha MUNGU mbinguni, na utakutwa umepunguka katika siku ile mbaya ya hukumu. - (Testimonies for the Church 3: 363, 364) [Pr 256.4; Maombi Aya ya 19]

MUNGU Hutuma majeshi ya Malaika wa Kuthibiti na Kutusaidia Katika Kujibu maombi—Ikiwa Shetani anaona kwamba yuko katika hatari ya kupoteza nafsi moja, atajitahidi kadiri ya uwezo wake wote kuihifadhi hiyo moja. Na mtu huyo anapoamshwa kwenye hatari yake, na, kwa dhiki na bidii, akamtazama Yesu ili kupata nguvu, Shetani anaogopa kwamba atampoteza mfungwa, naye anaita majeshi ya malaika zake kudhibiti mambo na kuifunga roho hiyo maskini, na kuunda ukuta wa giza kumzunguka, ili nuru ya mbinguni isimfikie. Lakini ikiwa yule aliye hatarini anavumilia, na katika hali ya kutokuwa na uwezo wake akijisalimisha juu ya wema wa damu ya Kristo, Mwokozi wetu husikiliza ombi la dhati la imani, na kutuma jeshi la wale malaika wenye uwezo mkubwa kumkomboa. Shetani hawezi kuvumilia kuona mpinzani wake Mwenye nguvu anategemewa na kusihiwa wakati wa hii dharura. Majeshi ya malaika waovu kwani anaogopa na kutetemeka mbele ya nguvu na ukuu Wake. Kwa sauti ya ombi la bidii, jeshi zima la Shetani hutetemeka. Anaendelea kuita majeshi ya malaika waovu ili kutimiza lengo lake. Na wakati malaika, wenye uwezo wote, waliovikwa silaha nzito za mbinguni, wanapokuja kusaidia nafsi iliyozimia, inayofuatiliwa kama mawindo, Shetani na jeshi lake wanarudi nyuma, wakijua vema kwamba wameshindwa katika vita yao. Raia wa Shetani ni waaminifu (mapepo), watenda kazi hodari, na wameunganishwa katika kitu kimoja. Na

ingawa wanachukiana na kupigana wao kwa wao, bado wanaboresha kila fursa ili kuendeleza maslahi yao ya pamoja. Lakini Kamanda Mkuu mbinguni na duniani amewekea mipaka nguvu za Shetani.- (Testimonies for the Church 1:345, 346) [Pr 256.5; Maombi Aya ya 20]

Ulinzi wa jeshi la mbinguni umetolewa kwa wote ambao watafanya kazi katika njia za MUNGU na kufuata mipango Yake. Tunaweza katika ombi la dhati, la toba na moyo uliopondeka, kuwaita wasaidizi wa mbinguni upande wetu. Majeshi yasiyoonekana ya nuru na yenye nguvu yatafanya kazi pamoja na wanyenyekevu, wapole, wale wa hali ya chini na wanaojishusha.— (Selected Messages 1:97) [Pr 257.1; Maombi Aya ya 21]

Niliona baadhi, wakiwa na imani yenye nguvu na vilio vya uchungu, wakimsihi MUNGU. Nyuso zao zilikuwa zimedhoofu na zilikuwa na wasiwasi mwingi, zikionyesha mapambano yaliyo ndani yao. Uthabiti na bidii kubwa ilionyeshwa katika nyuso zao; matone makubwa ya jasho yakaanguka kutoka kwenye vipaji vya nyuso zao. Nyuso zao ziling'aa hapa na pale kwa alama za kibali cha MUNGU, na tena ule mwonekano wa umakini mzito wa dhati, na wa wasiwasi ukaja tena juu yao. [Pr 257.2; Maombi Aya ya 22]

Malaika waovu walikusanyika kuwazunguka, wakitandaza giza juu yao ili kumzinga Yesu wasimwone, ili macho yao yavutwe kwenye giza lililowazunguka, na hivyo kuongozwa kutomwamini MUNGU na kumnung'unikia. Usalama wao pekee ulikuwa katika kuelekeza macho yao juu. Malaika wa MUNGU walikuwa na mamlaka juu ya watu Wake, na anga lililojawa na malaika waovu liliposogezwa karibu na hawa wenye wasiwasi, malaika wa mbinguni walikuwa wakipepea mbawa zao juu yao ili kulitawanya giza nene. [Pr 257.3; Maombi Aya ya 23]

Waombaji walipokuwa wakiendelea na kilio chao cha dhati, nyakati fulani mwali wa nuru ya Yesu uliwajia, ili kutia moyo mioyo yao na kuangaza nyuso zao. Baadhi, niliwaona, hawakushiriki katika kazi hii ya kulia kwa uchungu na kusihi. Walionekana kutozingatia na kutojali. Hawakuwa wakipinga giza lililowazunguka, na liliwafunga kama wingu zito. Malaika wa MUNGU waliwaacha hawa na kwenda kusaidia wale walio na bidii ya dhati, wanaosali. Niliona malaika wa MUNGU wakiharakisha kuwasaidia wale wote waliokuwa wakihangaika kwa uwezo wao wote kuwapinga malaika waovu na kujaribu kujisaidia wenyewe kwa kumwita MUNGU kwa ustahimilivu. Lakini malaika Wake waliwaacha wale ambao hawakufanya jitihada yoyote ya kujisaidia, nao wakapotea katika upeo wa macho yangu.—(Early Writings, 269, 270) [Pr 258.1; Maombi Aya ya 24]

Maombi Marefu Huwachosha Malaika—Mazungumzo marefu yenye kujirudia-rudia, yasiyo na umuhimu na sala ndefu havifai mahali popote, na hasa kwenye mikutano ya halaiki. Huwachosha malaika pamoja na watu wanaowasikiliza. Maombi yetu yanapaswa kuwa mafupi, na yanayogusa dhima moja kwa moja.—(The Review and Herald, October 10, 1882) [Pr 258.2; Maombi Aya ya 25]

Malaika Watatufundisha Jinsi ya Kuomba—Washiriki wa Kanisa, vijana kwa wazee, wanapaswa kuelimishwa ili kwenda kutangaza ujumbe huu wa mwisho kwa ulimwengu. Wakienda kwa unyenyekevu, malaika wa MUNGU watakwenda pamoja nao, wakiwafundisha jinsi ya kuinua sauti katika sala, jinsi ya kuinua sauti katika nyimbo, na jinsi ya kutangaza ujumbe wa injili kwa ajili ya wakati huu.—(Messages to Young People , 217) [Pr 258.3; Maombi Aya ya 26]

Malaika Hushangaa Kwamba Wanadamu Huomba Kidogo Sana—Je, Malaika wa mbinguni wanaweza kufikiria nini juu ya wanadamu dhaifu wasiojiweza, ambao wako chini ya majaribu, wakati moyo wa MUNGU wa upendo usio na kikomo una matamaniao nao, tayari kuwapa zaidi ya wawezavyo kuomba au kufikiria, na bado wanaomba kidogo sana, na wana imani ndogo sana? Malaika hupenda kusujudu mbele za MUNGU; wanapenda kuwa karibu Naye. Wanaona ushirika na MUNGU kuwa furaha yao kuu; na bado watoto wa dunia, ambao wanahitaji sana msaada ambao MUNGU pekee Ndiye anayeweza kutoa, wanaonekana kutosheka kutembea bila nuru ya Roho Wake na ushirika wa uwepo Wake.—(Steps to Christ, 94) [Pr 258.4; Maombi Aya ya 27]

SURA YA 26

MAOMBI BANDIA

Usimkaribie MUNGU kwa Mazoea katika Maombi—Unyenyekevu na uchaji vinapaswa kuujenga mwenendo wa wote wanaoenda mbele za MUNGU. Katika Jina la Yesu tunaweza kwenda mbele Zake kwa ujasiri, lakini hatupaswi kumkaribia kwa ujasiri wa kiburi (au dhana zetu), kana kwamba Yeye Yuko sawa na sisi. Kuna wale wanaozungumza na MUNGU Mkuu na Mwenye uwezo wote na mtakatifu, ambaye anakaa katika nuru isiyoweza kufikiwa, kama ambavyo wangezungumza na mtu aliye sawa nao, au hata yule wanayefikiria ni duni kwao. Kuna wale wanaojiendesha au kutenda katika nyumba Yake jinsi wasivyoweza kufanya katika chumba cha kumwona mtawala wa kidunia. Hawa wanapaswa kukumbuka kwamba wako mbele za macho Yake ambapo maserafi wanaabudu, ambapo mbele Yake malaika hufunika nyuso zao.—(Patriarchs and Prophets, 252) [Pr 259.1; Maombi Aya ya 1]

Maombi ya Unafiki—Maombi yanayotolewa kwa MUNGU ili kumwambia unyonge wetu wote, wakati hatujisikii kutofaa au unyonge wetu hata kidogo, ni

maombi ya unafiki. Ni maombi ya moyo uliopondeka pekee ndiyo ambayo Bwana anajali. “Kwa maana Yeye aliye juu, aliyetukuka, akaaye milele, ambaye Jina Lake ni Mtakatifu, asema hivi; mimi nakaa mahali palipoinuka, palipo patakatifu, tena pamoja naye aliye na roho iliyotubu na kunyenyekea, ili kuzifufua roho za wanyenyekevu, na kuifufua mioyo yao waliotubu.” [Pr 259.2; Maombi Aya ya 2]

Maombi hayakusudii kufanya mabadiliko yoyote kwa MUNGU; ila yanatuleta katika mapatano na MUNGU. Hayachukui mahali pa wajibu.—(Messages to Young People, 247, 248) [Pr 260.1; Maombi Aya ya 3]

Maombi Yanayoleta Kivuli Mwanana— Kuna baadhi, nina wasiwasi, ambao hawapeleki shida zao kwa MUNGU katika maombi ya faragha, bali wanazirundika kwa ajili ya mkutano wa maombi, na kisha huko huyafyatua/hufanya maombi yao kwa siku kadhaa. Watu hao wanaweza kuitwa wauaji wa mikutano na wauaji wa maombi. Hawatoi nuru; hawamjengi mtu. Maombi yao baridi, yaliyoganda na shuhuda ndefu, za kurudi nyuma kwao zinatia watu kivuli. Wote hufurahi wanapomaliza, na ni vigumu kukung’uta ubaridi unaotetemesha na giza ambalo maombi na kuamrisha kwao katika sala kunaleta kwenye mkutano. Kutoka katika nuru ambayo nimepokea, mikutano yetu inapaswa kuwa ya kiroho na ya kijamii, na sio mirefu sana. Kujiweka mbali na watu (kutokuwa na moyo wa kirafiki), kiburi, ubatili, na hofu kwa mwanadamu vinapaswa kuachwa nyumbani. Tofauti ndogo na chuki havipaswi kubebwa nasi kwenye mikutano hii. Kama familia iliyongana, usahili, utulivu, upole, ujasiri, na upendo vinapaswa kuwepo katika mioyo ya akina kaka na akina dada wanaokutana ili kufanywa upya na kutiwa nguvu kwa kuleta taa/mwangaza wao pamoja.— Testimonies for the Church 2:578, 579) [Pr 260.2; Maombi Aya ya 4]

Kutarajia Kwamba Maombi Yetu Yatajibiwa Daima Kwa Njia ile Tunayotaka Ni Kujiamini Kupita Kiasi— Maombi ya Imani hayapotei kamwe; lakini kudai kuwa yatajibiwa kila wakati kwa njia ile ile na kwa jambo fulani maalum ambalo tumetarajia, ni dhana.(Testimonies for the Church 1:231) [Pr 260.3; Maombi Aya ya 5]

Maombi yetu yanapoonekana kutojibiwa, tunapaswa kung’ngania ahadi; kwani wakati wa kujiiwa hakika utakuja, na tutapokea baraka tunazohitaji zaidi. Lakini kudai kwamba maombi daima yatajibiwa kwa njia ile ile na kwa jambo fulani maalumu tunalolitamani, ni dhana (au kiburi). MUNGU ni Mwenye hekima sana hata asikosee, na ni mwema sana hata asiweze kuwanyima kitu chochote kizuri wale waendao kwa unyofu. Basi msilogope kumwamini, ijapokuwa hamuoni jawabu la haraka la maombi yenu. Tegemea ahadi Yake ya hakika, “Ombeni, nanyi mtapewa.” (Steps to Christ, 96) [Pr 260.4; Maombi Aya ya 6]

Maombi ndani Yake pekee, Hayana thawabu ya kuosha Dhambi—Wapagani waliona maombi yao kama yenye kustahili na kuwa yana sifa na haki ya upatanisho wa dhambi ndani yao. Kwa hiyo kadiri maombi yanavyozidi kuwa marefu ndivyo ubora na haki yao inavyokuwa kubwa zaidi. Ikiwa wangeweza

kuwa watakatifu kwa juhudi zao wenyewe wangukuwa na kitu ndani yao cha kufurahia, sababu fulani ya kujigamba. Wazo hili kwamba sala ni utimilifu wa kanuni ya utakaso lipo kwenye msingi wa mifumo yote ya dini za uwongo. Mafarisayo walikuwa wameiga wazo hili la kipagani la sala, na halijapotea hata kidogo katika siku zetu, hata miongoni mwa wale wanaodai kuwa Wakristo. Kurudiwa kwa misemo ya kawaida kama destruri, wakati moyo hauhisi haja ya MUNGU, ni tabia sawa na "marudio ya bure" ya wapagani. [Pr 261.1; Maombi Aya ya 7]

Maombi si utakaso wa dhambi; hayana haki wala sifa ndani yake yenyewe. Maneno yote ya madoido tunayoweza kuyatoa ndani ya amri yetu hayapatani na haja takatifu. Maombi yenye ufasaha zaidi ikiwa hayaonyeshi hisia za kweli za moyo ni kazi bure tu. Lakini maombi yatokayo katika moyo wa dhati na bidii, pale yale mahitaji ya nafsi yanapowasilishwa, kama vile ambavyo tungemwomba rafiki wa kidunia atupe msaada wake, tukitarajia kuupokea—haya ndiyo maombi ya imani. MUNGU hataki kumsifia kwetu kwa maonyesho, bali kilio kisichotamkwa cha moyo uliovunjika na kutiishwa na hisia ya dhambi yake na udhaifu mkubwa hupata njia Yake kwa Baba wa rehema zote.—(Thoughts from the Mount of Blessing, 86, 87) [Pr 261.2; Maombi Aya ya 8]

Maombi Sio Ushahidi wa Kuongoka Ikiwa Maisha Hayajabadilishwa—Shetani huwaongoza watu kufikiri kwamba kwa sababu wamehisi unyakuo wa hisia, basi wao wameongoka. Lakini uzoefu wao haujabadilika. Matendo yao ni sawa na hapo awali. Maisha yao hayaonyeshi matunda mazuri. Wanaomba mara kwa mara na kwa muda mrefu, na daima wanarejelea hisia walizokuwa nazo wakati fulani. Lakini hawaishi maisha mapya. Hawa wamedanganyika. Uzoefu wao hauzami ndani zaidi kuliko hisia zao. Wanajenga juu ya mchanga, na upepo mkali unapokuja, nyumba yao inafagiliwa mbali. [Pr 261.3; Maombi Aya ya 9]

Nafsi dhaifu za walio wengi zinapapasa gizani, zikitafta hisia ambazo wengine wanasema wamekuwa nazo katika uzoefu wao. Wanapuuza ukweli kwamba mwumini katika Kristo lazima aifanyie kazi wokovu wake mwenyewe kwa hofu na kutetemeka. Mwenye dhambi aliyesadikishwa ana jambo la kufanya. Ni lazima atubu na aonyeshe imani ya kweli. [Pr 262.1; Maombi Aya ya 10]

Wakati Yesu anapozungumza juu ya moyo mpya, anamaanisha akili, utu wote, nafsi yote. Kuwa na badiliko la moyo ni kuondoa mapenzi kutoka katika ulimwengu, na kuyafunga kwa Kristo. Kuwa na moyo mpya ni kuwa na akili mpya, makusudio mapya, nia mpya. Ni nini ishara ya moyo mpya?—Maisha yaliyobadilika. Kila siku, kila saa kuna kufa kwa ubinafsi, uchoyo na kiburi.—(Messages to Young People, 71,72) [Pr 262.2; Maombi Aya ya 11]

Maombi Hayachukui Nafasi ya Utiifu—Wanaume na wanawake, katika kukabili amri chanya zaidi za MUNGU, Hufuata mwelekeo wao wenyewe, na kisha kuthubutu kuliombea jambo hilo, ili kumshawishi MUNGU ili akubali kuwaruhusu

kwenda kinyume na mapenzi Yake Mwenyewe aliyoyasema. MUNGU hapendezwi na maombi hayo. Shetani anakuja upande wao, kama alivyofanya kwa Hawa katika Edeni, na kuwavutia, nao wanapata mguso fulani akilini, na hilo wanasimulia kuwa tukio la ajabu sana ambalo Bwana amewapa.— (The Review and Herald, July. 27, 1886) [Pr 262.3; Maombi Aya ya 12]

Ushirika na MUNGU huipa nafsi ujuzi wa ndani wa mapenzi Yake. Lakini wengi wanaokiri imani hawajui uongofu wa Kweli ni nini. Hawana uzoefu katika ushirika na Baba kwa njia ya Yesu Kristo, na hawajawahi kuhisi nguvu ya neema ya Bwana ya kutakasa moyo. Huomba na kutenda dhambi, hutenda dhambi na kuomba, maisha yao yamejaa uovu, udanganyifu, hila, husuda, wivu, kijicho na kujipenda wenyewe. Maombi ya tabaka hili ni chukizo kwa MUNGU. Maombi ya kweli hushirikisha nguvu za roho na huathiri maisha. Yeye anayemimina mahitaji yake mbele za MUNGU anahisi utupu wa kila kitu kilicho chini ya mbingu.—(Testimonies for the Church 4:534, 535) [Pr 262.4; Maombi Aya ya 13]

Kuna masharti ya kutimizwa kwa ahadi za MUNGU, na maombi kamwe hayawezi kuchukua nafasi ya wajibu. “Mkinipenda,” Kristo asema, “mtazishika amri zangu.” “Yeye aliye na amri Zangu, na kuzishika, yeye ndiye anipendaye; naye anipendaye atapendwa na Baba Yangu, Nami nitampenda na kujidhihirisha kwake.” Yohana 14:15, 21. Wale wanaoleta maombi yao kwa MUNGU, wakidai Ahadi Yake huku hawatimizi masharti, wanamtukana Yehova. Wanaleta Jina la Masihi kama mamlaka yao kwa ajili ya utimilifu wa ahadi, ila hawafanyi mambo yale ambayo yangeonyesha imani katika Kristo na upendo Kwake.— (Christ's Object Lessons, 143) [Pr 263.1; Maombi Aya ya 14]

Kuomba ni kufungua moyo kwa MUNGU kama kwa rafiki. Jicho la imani litatambua MUNGU Kwa Ukaribu sana, na mwombaji anaweza kupata uthibitisho wenye thamani wa upendo na utunzaji wa Bwana kwake. Lakini kwa nini maombi mengi sana hayajibiwi? Anasema Daudi: “Nilimlilia kwa kinywa changu, Naye alitukuzwa na ulimi wangu. Nikiuangalia uovu moyoni mwangu, Bwana hatanisikia.” kupitia nabii mwingine Bwana anatupa ahadi: “Mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote.” Tena, anazungumza kuhusu wengine ambao “hawajanililia kwa mioyo yao.” Maombi kama hayo ni maombi ya mazoea ni mfano tu, ibada ya midomo tu, ambayo Bwana hakubali.—(Testimonies for the Church 4:533) [Pr 263.2; Maombi Aya ya 15]

Maombi ya Haraka, Ya Nyakati Fulani tu Si Ushirika Halisi na MUNGU—Mbingu haijafungwa dhidi ya maombi ya bidii ya wenye haki. Eliya alikuwa mwanadamu mwenye hisia kama sisi, lakini Bwana alisikia na akajibu maombi yake kwa njia ya kushangaza zaidi. Sababu pekee ya kukosa kwetu nguvu na MUNGU inapatikana ndani yetu wenyewe. Ikiwa maisha ya ndani ya wengi wanaokiri Ukweli yangewasilishwa mbele yao, basi wasingedai kuwa wao ni Wakristo. Hawakui katika neema. Ombi la haraka linatolewa hapa na pale, lakini hakuna ushirika wa kweli na MUNGU. [Pr 263.3; Maombi Aya ya 16]

Ni lazima tudumu sana katika maombi ikiwa tunakusudia kufanya maendeleo katika maisha ya Kiungu/mbingu. Ujumbe wa kweli ulipotangazwa kwa mara ya kwanza, tuliomba sana. Ni mara ngapi sauti ya maombezi ilisikika chumbani, ghalani, kwenye miti ya bustani, kwenye vijisitu au shambani. Mara kwa mara tulitumia saa nyingi katika maombi ya bidii, wawili au watatu pamoja tukidai ahadi; mara nyingi sauti ya kilio ilisikika na kisha sauti ya shukrani na wimbo wa sifa.—(Testimonies for the Church 5:161, 162) [Pr 263.4; Maombi Aya ya 17]

MUNGU Huchukia Maombi ya Wenye Ubinafsi—Niliona kwamba kulikuwa na watu kama Yuda Iskariote miongoni mwa wale wanaodai kuwa wanamngoja Bwana wao. Shetani anawadhibiti, lakini wao hawajui. MUNGU hawezi kuridhia kiwango hata kidogo cha tamaa au ubinafsi, na Anachukia maombi na kuhimiza kwa wale wanaojiingiza katika tabia hizi ovu. Shetani anavyoona kwamba wakati wake ni mfupi, huwaongoza wanadamu kuwa wabinafsi na wenye tamaa zaidi na zaidi, na kisha hufurahi anapowaona wakiwa wamejifungia ndani yao wenyewe (wanajifikiria wenyewe), ni bahili, wasio na faida, wachoyo, na wenye ubinafsi. Ikiwa macho ya hao yangefumbuliwa, wangemwona Shetani akiwa katika ushindi wa kuzimu, akishangilia juu yao na kuucheka upumbavu wa wale wanaokubali madokezo yake na kuingia katika mitego yake.— (Early Writings, 268) [Pr 264.1; Maombi Aya ya 18]

Maombi Makavu, Malegevu Hayasaidii Mtu yeyote—Kanisa linahitaji uzoefu mpya, na hai wa washiriki ambao wana mazoea ya ushirika na MUNGU. Ushuhuda mkavu, uliochakaa na maombi, bila udhihirisho wa Kristo ndani yake, havina msaada kwa watu. Ikiwa kila mtu anayedai kuwa mtoto wa MUNGU angejazwa na imani na nuru na uzima, ni ushahidi wa ajabu jinsi gani ungetolewa kwa wale wanaokuja ili kusikia ile Kweli! Na ni roho ngapi zinaweza kuokolewa kwa Kristo!—(Testimonies for the Church 6:64) [Pr 264.2; Maombi Aya ya 19]

Hazina zote za mbinguni zilikabidhiwa kwa Yesu Kristo, ili aweze kutoa karama hizi za thamani kwa mtafutaji mwenye bidii, aliye mvumilivu. Yeye “Amemfanya Yeye kuwa hekima yetu, haki yetu na utakaso na ukombozi.” 1 Wakorintho 1:30. Lakini hata maombi ya wengi ni ya mazoea sana kiasi kwamba hayana ushawishi wowote kwa ajili ya wema. Sio manukato au harufu iletayo uzima (2Wakorintho 2:16). [Pr 264.3; Maombi Aya ya 20]

Ikiwa walimu wangenyenyekeza mioyo yao mbele za MUNGU na kutambua jukumu ambalo wamekubali katika kuwasimamia vijana wakiwa kwa lengo la kuwaelimisha kwa ajili ya maisha yajayo ya umilele, badiliko kubwa lingekana upesi katika mtazamo wao. Maombi yao yasingekuwa makavu na yasiyo na uhai, bali wangeomba kwa bidii kwaajili ya nafsi zinazohisi hatari zao.— (Counsels to Parents, Teachers, and Students, 371, 372) [Pr 265.1; Maombi Aya ya 21]

Onyo Juu ya Maombi Ambayo Yana ubinafsi kama Kiini Chake—Maombi yetu kwa MUNGU hayapaswi kutoka katika mioyo iliyojaa matamania binafsi. MUNGU anatusihi tuchague karama ambazo zitaongezeka kwenye utukufu Wake.

Angetaka tuchague ya mbinguni badala ya yale ya duniani. Anatufungulia na kutudhihirishia mbele zetu uwezekano na manufaa ya uchumi wa mbinguni. Anatia moyo malengo yetu ya juu zaidi, usalama katika hazina yetu iliyo bora zaidi. Wakati mali ya kidunia itafagiliwa mbali, muumini atafurahi katika hazina yake ya mbinguni, utajiri ambao hauwezi kupotea katika maafa yoyote ya kidunia. – (Sons and Daughters of God, 188) [Pr 265.2; Maombi Aya ya 22]

Maombi ya Kweli na ya Bandia Yalinganishwa—Yule mtoza ushuru maskini aliyeomba, “MUNGU unirehemu mimi mwenye dhambi” (Luka 18:13), alijiona kuwa mtu mwovu sana, na wengine walimtazama katika nuru hiyo hiyo; lakini alihisi hitaji lake, na kwa mzigo wake wa hatia na aibu alienda mbele ya MUNGU, akiomba rehema Yake. Moyo wake ulikuwa wazi kwa ajili ya Roho wa MUNGU kufanya kazi Yake ya ukarimu na neema na hivyo kumweka huru dhidi ya nguvu za dhambi. Ombi la farisayo la kujigamba, la kujihesabia haki lilionyesha kwamba moyo wake ulikuwa umefungwa dhidi ya ushawishi wa Roho Mtakatifu. Kwa sababu ya umbali wake kutoka kwa MUNGU, hakuwa na hisia ya unajisi wake mwenyewe, tofauti na ukamilifu wa utakatifu wa Bwana. Yeye hakuona hitaji/uhitaji, naye hakupokea chochote.—(Steps to Christ, 30, 31) [Pr 265.3; Maombi Aya ya 23]

Kuna aina mbili za maombi - maombi ya mazoea na mfano tu na maombi ya imani. Kurudiwa kwa kundi la sentensi za mazoea, wakati moyo hauhisi haja ya MUNGU, ni maombi ya mazoea....Tunapaswa kuzingatia sana katika maombi yetu yote kunena matakwa ya moyo na kusema kile tunachomaanisha tu. Maneno yote ya madoidodoido mengi ambayo yamo kwenye uwezo wetu kutoa, hayalingani na shauku moja takatifu. Maombi yenye ufasaha zaidi ni marudio ya bure kama hayaonyeshi hisia za kweli za moyo. Lakini maombi yatokayo katika moyo mnyofu, pale matakwa rahisi ya nafsi yanapoonyeshwa kama ambavyo tungeomba upendeleo kwa rafiki wa duniani, tukitazamia kwamba tutapewa—hili ndilo ombi la imani. Mtoza ushuru aliyepanda kwenda hekaluni kuomba ni kielelezo kizuri cha mwumini mnyoofu, aliyejitoa kikamilifu. Alihisi kwamba alikuwa mtenda-dhambi, na uhitaji wake mkubwa ulipelekea mlipuko wa tamanio lenye shauku, “MUNGU unirehemu mimi mwenye dhambi.”— (My Life Today, 19) [Pr 265.4; Maombi Aya ya 24]

Imesemwa juu ya Kristo: "Na akiwa katika dhiki, Aliomba kwa bidii zaidi." ni tofauti ya jinsi gani kuhusu maombezi haya ya Mkuu wa mbinguni na maombi duni, yasiyo na moyo ambayo hutolewa kwa MUNGU. Wengi wameridhika na maudhui ya midomo (huduma za mdomo tu, maneno matupu bila matendo au moyo ndani yake), na ni wachache walio na hamu ya dhati, ya bidii, na ya upendo kwa MUNGU. [Pr 266.1; Maombi Aya ya 25]

Ushirika na MUNGU huipa nafsi ujuzi wa ndani wa mapenzi Yake. Lakini wengi wanaokiri imani hawajui uongofu wa kweli ni nini. Hawana uzoefu katika ushirika na Baba kwa njia ya Yesu Kristo, na hawajawahi kuhisi nguvu ya neema ya

Mungu inayotakasa moyo. Kuomba na kutenda dhambi, kutenda dhambi na kuomba, maisha yao yamejaa udanganyifu, hila, husuda, chuki, wivu, na kujipenda wenyewe. Maombi ya tabaka hili ni chukizo kwa MUNGU. Maombi ya kweli hushirikisha nguvu za roho na huathiri maisha. Yeye anayemimina mahitaji yake mbele za MUNGU anahisi ubatili/utupu wa kila kitu chini ya mbingu. "Shauku yangu yote i mbele Zako," akasema Daudi, "na kuugua kwangu hakufichiki Kwako." "Nafsi yangu ina kiu ya MUNGU, MUNGU Aliye hai, ni lini nitakuja nionekane mbele za MUNGU?" "Ninapokumbuka mambo haya, naimimina nafsi yangu iliyo ndani yangu."—(Testimonies for the Church 4:534, 535) [Pr 266.2; Maombi Aya ya 26]

SURA YA 27

SHETANI NA MAOMBI

Shetani Anajaribu Kuziba njia ili Maombi yetu Yasimfikie MUNGU—Giza la yule mwovu linawafunika wale wanaopuuzia kuomba. Majaribu yanayonong'onwa na adui yanawavuta wao kutenda dhambi; na yote ni kwa sababu hawatumii upendeleo ambao MUNGU amewapa katika mihadi mitakatifu Naye, kupitia Maombi. Kwa nini basi wana na binti za MUNGU wawe wenye kusitasita kuomba, wakati maombi ndiyo ufunguo katika mkono wa imani ili kufungua ghala za hazina za mbinguni, ambako kunatunzwa rasilimali zenye thamani isiyo na kikomo, za Yule ambaye ni Mweza wa yote? Bila maombi na kukesha daima kwa uadilifu tuko katika hatari ya kuongeza kutojali na kukengeuka kutoka katika njia iliyo sawa. Adui anatafuta daima kuifunga njia ya kuelekea kwenye Kiti cha Rehema, ili tukileta maombi ya dhati na imani tusipate neema na uwezo wa kuyapinga majaribu.— (Steps to Christ, 94, 95) [Pr 267.1; Maombi Aya ya 1]

Kuna nguvu kuu katika maombi. Adui wetu mkuu anatafuta daima kuiweka nafsi inayopitia dhoruba mbali na MUNGU. Ombi la kwenda mbinguni la yule mtakatifu aliye mnyenyekevu zaidi ndilo linaloogopwa zaidi na Shetani kuliko sheria za bunge mamlaka ya wafalme.— (The SDA Bible Commentary 2:1008) [Pr 267.2; Maombi Aya ya 2]

Adui huwazuia wengi wenu msiombe, kwa kuwaambia kwamba hamhisi roho ya maombezi ndani yenu, na kwamba ingefaa mngoje mpaka roho ya maombezi iwajie ili maombi yenu yasije yakawa ni dhihaka. Lakini unapaswa kumwambia Shetani, "Imeandikwa" kwamba "wanadamu wanapaswa kuomba siku zote, na wala wasizimie." Tunapaswa kuomba mpaka tuwe na mzigo wa mahitaji yetu juu ya nafsi zetu; na tukivumilia tutapata. Bwana atatujaza Roho Wake Mtakatifu. Bwana anajua, na Ibilisi anajua, kwamba hatuwezi kupinga majaribu ya Shetani bila nguvu kutoka juu. Kwa sababu hii yule mwovu anatafuta kutuzuia tusimshike

Yeye aliye na uwezo Mkubwa wa kuokoa. Bwana wetu alifanya hili kuwa ni wajibu wetu, pamoja na upendeleo wetu, kuunganisha udhaifu wetu, ujinga wetu, hitaji letu, nguvu, na nguvu Zake. Yeye anaunganisha nguvu Zake zisizo na kikomo na juhudi za viumbe wenye ukomo, ili wawe zaidi ya washindi katika vita na adui wa nafsi zao. [Pr 268.1; Maombi Aya ya 3]

Mtu yeyote asivunjike moyo, maana Yesu Yu hai ili atuombee. Kuna mbingu ya kupata, na jehanamu ya kutoroka, na Kristo anapendezwa na ustawi wetu (maslahi yetu). Atawasaidia wale wote wamwitao. Ni lazima tuchanganye imani na maombi yetu yote. Hatuwezi kumshusha Kristo chini, lakini, kupitia njia ya imani, tunaweza kujiinua wenyewe hadi katika umoja na mshikamano kwa kiwango kamili cha haki. Tuna adui mdanganyifu wa kukutana naye na kumshinda, lakini twaweza kufanya hivyo katika Jina la Mwenye Nguvu.—(The Review and Herald, October 30, 1888) [Pr 268.2; Maombi Aya ya 4]

Usiruhusu Mapendekezo ya Shetani yakuzuie Kuomba— Hatupaswi kulemewa sana na mawazo ya dhambi na makosa yetu kiasi kwamba tukaacha kuomba. Wengine hutambua udhaifu wao mkuu na dhambi, na kukata tamaa. Shetani anaweka kivuli chake cheusi kati yao na Bwana Yesu, aliye dhabihu yao ya upatanisho. Wanasema, Haina faida kwangu kuomba. Maombi yangu yamechanganyika na mawazo maovu kiasi kwamba Bwana hatayasikia. [Pr 268.3; Maombi Aya ya 5]

Mapendekezo haya yanatoka kwa Shetani. Katika ubinadamu Wake Kristo alikutana na kupinga jaribu hili, na Anajua jinsi ya kuwasaidia wale wanaojaribiwa hivyo. Kwa niaba yetu, “alitoa maombi na dua pamoja na kilio kikuu na machozi” (Waebrania 5:7). [Pr 268.4; Maombi Aya ya 6]

Wengi, bila kuelewa kwamba mashaka yao yanatoka kwa Shetani, wanakata tamaa na kuzimia na kisha kushindwa katika pambano hilo. Usiache kuomba kwa sababu mawazo yako ni maovu. Kama tungeweza kwa hekima na nguvu zetu kuomba ipasavyo, tungeweza pia kuishi sawa, na hivyo tusingehitaji dhabihu ya upatanisho. Lakini kutokamilika kupo juu ya ubinadamu wote. Ielimishe na uifundishe akili ili uweze kumwambia Bwana kwa usahili/urahisi kile unachohitaji. Unapotoa maombi yako kwa MUNGU, ukitaleta msamaha wa dhambi, angahewa ya usafi wa moyo na takatifu zaidi itaizunguka nafsi yako.—(In Heavenly Places, 78) [Pr 269.1; Maombi Aya ya 7]

Maombi yanafadhaisha na kupumbaza Juhudi Zenye Nguvu Zaidi za Shetani—Mwanadamu ni mateka wa Shetani na kwa asili ana mwelekeo wa kufuata mapendekezo yake na kutenda maagizo/matakwa yake. Yeye mwenyewe ndani yake hana uwezo wa kusukumilia mbali kwa ufanisi upinzani dhidi ya uovu. Ni pale tu Kristo atakapokaa ndani yake kwa imani hai, akishawishi matamania yake na kumtia nguvu kwa zile nguvu zitokazo juu, ndipo mwanadamu ataweza kujitosa kumkabili adui huyu wa kutisha sana. Njia

nyingine zozote za ulinzi ni bure kabisa. Ni kwa njia ya Kristo pekee ndiyo nguvu za Shetani zinadhibitiwa (zinawekewa mipaka). Huu ni ukweli mzito (mlima wa ukweli) ambao wote wanapaswa kuuelewa. Shetani yupo kazini akishugulika kwa bidii sana(busy) kila dakika, akienda huku na huko, akitembea juu na chini katika nchi, akitafuta mtu ammeze. Lakini maombi ya bidii ya imani yatazuia juhudi zake zenye nguvu. Kisha chukueni “ngao ya imani,” ndugu zangu , “ambayo kwayo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu.”(Testimonies for the Church 5:294) [Pr 269.2; Maombi Aya ya 8]

Maombi Huzuia Mashambulizi ya Shetani—Maombi hutuunganisha sisi kwa sisi pia pamoja na MUNGU. Maombi humleta Yesu kando yetu, na kuipa roho iliyozimia, iliyofadhaika nguvu mpya ya kuushinda ulimwengu, mwili, na shetani. Maombi huzuia mashambulizi ya Shetani.—(Christ's Object Lessons, 250) [Pr 269.3; Maombi Aya ya 9]

Ni lazima tuvae silaha zote za MUNGU na kuwa tayari wakati wowote kwa ajili ya mapambano na nguvu za giza. Majaribu na mitihani vinapotujia, tumwendee MUNGU na tumlilie kwa uchungu katika maombi. Hatatuambia turudi tukiwa watupu, bali atatupa neema na nguvu za kushinda, na kuvunja nguvu za adui.—(Early Writings, 46) [Pr 269.4; Maombi Aya ya 10]

Shetani Hutetemeka akisikia Sauti ya Maombi—Wakati Shetani anapoona kwamba yuko katika hatari ya kupoteza nafsi moja, atajitahidi kadiri ya uwezo wake wote kuihifadhi. Na mtu huyo anapoamshwa kwenye hatari yake, na, kwa dhiki na bidii na usongo, akamtazama Yesu ili kupata nguvu, Shetani anaogopa kwamba atampoteza mateka wake, naye anaita majeshi ya malaika wake ili kuizunguka roho hiyo dhaifu, na kuunda ukuta wa giza kumzunguka, ili nuru ya mbinguni isimfikie. Lakini ikiwa yule aliye hatarini anastahimili bila kuchoka, na katika hali yake ya kutokuwa na uwezo akajisalimisha juu ya wema na sifa za damu ya Kristo, Mwokozi wetu husikiliza ombi la dhati la imani, na kutuma jeshi la wale malaika wenye uwezo mkubwa ili kumkomboa. Shetani hawezi kuvumilia kuona mpinzani wake mwenye nguvu anaitwa/anasihiwa, kwa kuwa anaogopa na kutetemeka mbele ya nguvu na ukuu Wake. Kwa sauti ya ombi la dhati, jeshi zima la Shetani hutetemeka bila kujizuia. Anaendelea kuita majeshi ya malaika waovu ili kutimiza lengo lake. Na wakati malaika, wenye uwezo wote, waliovikwa la silaha za mbinguni, wanapokuja kusaidia nafsi iliyozimia, inayofuatiliwa kama mawindo, Shetani na jeshi lake wanarudi nyuma na kuanguka chini, wakijua vema kwamba wameshindwa katika vita yao. Raia (Wahanga) waliojitolea kwa Shetani ni waaminifu, watenda kazi wenye bidii, na wameunganishwa katika kusudi lao moja. Na ingawa wanachukiana na kupigana wao kwa wao, huwa wanaboresha kila fursa ili kuendeleza maslahi yao ya pamoja. Lakini Kamanda mkuu mbinguni na duniani amewekea mipaka nguvu za Shetani.— (Testimonies for the Church 1:345, 346) Pr 270.1; Maombi Aya ya 11]

Shetani Anaogopa Maombi ya Mtakatifu Mnyenyekevu Zaidi— Kuna nguvu kuu

katika maombi. Adui wetu mkuu anatafuta mara kwa mara kuiweka nafsi yenye shida mbali na MUNGU. Ombi la kwenda mbinguni la mtakatifu mnyenyekevu zaidi huogopwa zaidi na Shetani kuliko maagizo ya mabaraza au maagizo ya wafalme.— (The SDA Bible Commentary 2:1008) Pr 270.2; Maombi Aya ya 12]

Maombi ni Silaha Dhidi ya Shetani—Jihadhari jinsi unavyopuuza maombi ya siri na kujifunza Neno la MUNGU. Hizi ni silaha zako dhidi ya yeye ambaye anajitahidi kuzuia safari yako ya mbinguni. Kupuuza kwa mara ya kwanza maombi na kusoma Biblia hurahisisha kupuuzia kwa mara ya pili. Upinzani wa kwanza dhidi ya kusihi kwa Roho hutayarisha njia ya upinzani wa pili. Hivyo moyo unafanywa kuwa mgumu, na dhamira inachomwa ili isiwe nyeti.— (Messages to Young People, 96) Pr 270.3; Maombi Aya ya 13]

Maombi Huvunja Mtego uliojificha wa Shetani—Pale tunapohisi kwamba hatujisikii sana kuzungumza na Yesu, basi na tuombe zaidi. Kwa kufanya hivyo tutavunja mtego wa Shetani uliojificha, mawingu ya giza yatatoweka, nasi tutatambua uwepo mzuri wa Yesu.— (Lift Him Up, 372) [Pr 271.1; Maombi Aya ya 14]

Maombi Yanashinda Dhidi ya Shetani—Ombi la imani ndiyo nguvu kuu ya Mkristo, na hakika litashinda dhidi ya Shetani. Ndiyo maana anadokeza ushauri kwamba hatuna haja ya maombi. Jina la Yesu, Mwombezi wetu, yeye analichukia sana; na tunapomwendea kwa dhati ili kupata msaada, jeshi la Shetani hufadhaika na kupata mshtuko. Kusudi lake linatimia vyema ikiwa tutapuuzia zoezi la kuomba, kwa maana basi maajabu yake ya uwongo yatapokelewa kwa urahisi zaidi.— (Testimonies for the Church 1:296) [Pr 271.2; Maombi Aya ya 15]

Maombi Ni Muhimu Hasa Katika tete na za dharura katika Mapambano Yetu dhidi ya Shetani—Katika pambano na mashirika ya kishetani kuna nyakati za maamuzi ambazo zitaamua ushindi ama kwa upande wa MUNGU au upande wa mtawala wa ulimwengu huu. Ikiwa wale wanaohusika katika vita hii hawako makini na macho kabisa, wakiweka bidii na uangalifu, wakiomba kwa dhati hekima, wakikeshwa katika maombi, ... Shetani ataibuka kama mshindi, wakati angeweza kushindwa na majeshi ya Bwana...Walinzi waaminifu wa MUNGU hawapaswi kuzipa nguvu za uovu manufaa au mwanya wowote—(The SDA Bible Commentary 6:1094) [Pr 271.3; Maombi Aya ya 16]

Shetani Anakasirishwa na Maombi yenye bidii kubwa—Shetani huwaongoza watu wengi kuamini kwamba maombi kwa MUNGU ni bure na ni deturi tu. Anajua vizuri jinsi kutafakari na kuomba kunavyohitajika ili kuwafanya wafuasi wa Kristo waendeleo kuamshwa usingizini ili kuupinga ujanja na udanganyifu wake. Kwa hila zake hugeuza akili kutoka kwenye mazoezi haya muhimu, ili nafsi isiegemee msaada wa Yule Mwenye Nguvu na kupata nguvu kutoka Kwake za kupinga mashambulizi yake. Nilielekezwa kwenye maombi ya bidii na yenye matokeo/matunda ya watu wa MUNGU wa kale. “Eliya alikuwa mtu mwenye tabia

kama sisi, naye aliomba kwa bidii.” Danieli alimwomba MUNGU wake mara tatu kwa siku. Shetani anakasirishwa na sauti ya ombi lenye shauku kubwa kwa kuwa anajua kwamba atajipatia hasara kubwa.—(Testimonies for the Church 1:295) [Pr 271.4; Maombi Aya ya 17]

Shetani Hufurahi Maombi yanaponenwa bila kutamkwa kwa Uwazi —Hebu wale wanaoomba na wale wanaotamka wayatamke maneno yao ipasavyo na kusema kwa uwazi, dhahiri, kwa toni isiyo ya juu au chini sana au yenye utulivu. Ombi likitolewa ipasavyo, ni nguvu ya wema. Ni mojawapo ya njia mojawapo zinayztumiwa na Bwana kuwajulisha watu hazina za Kweli za thamani. Lakini ombi haliwi linavyopaswa kuwa, kwa sababu ya sauti zenye kasoro za wale wanaolitamka. Shetani anafurahi wakati maombi yanayotolewa kwa MUNGU yanakaribia kutosikika masikioni mwa watu. Hebu watu wa MUNGU wajifunze jinsi ya kusema na kuomba kwa njia ambayo itawakilisha ipasavyo zile Kweli kuu walizonazo. Hebu shuhuda zinazotolewa na sala zinazonenwa viwe wazi na kusikika vyema neno kwa neno. Na Hivyo MUNGU atatukuzwa.—(Testimonies for the Church 6:382) [Pr 272.1; Maombi Aya ya 18]

Shetani Hujaribu Kutusadikisha Kwamba Kuomba Si Lazima (sala siyo jambo la lazima)— Wazo la kwamba maombi si la lazima ni mojawapo ya mbinu za Shetani zenye ufanisi zaidi za kuharibu nafsi. Maombi ni ushirika pamoja na MUNGU, Chemchemi ya hekima, Chanzo cha nguvu, na amani, na furaha.—(Child Guidance, 518) [Pr 272.2; Maombi Aya ya 19]

Shetani anaona watumishi wa Bwana wamelemewa kwasababu ya giza la kiroho linalowafunika watu. Naye huyasikia maombi yao ya dhati kwa ajili ya neema ya Bwana na uwezo wa kuvunja uchawi wa kutojali, uvivu na kutokuwa makini. Kisha nia iliyofanywa upya anaikobeka sanaa yake. Yeye huwajaribu watu kuendekeza uchu wa tamaa ya chakula au namna nyingine ya tamaa ya mwili ya kujiridhisha, na hivyo kuzifisha hisia zao hata washindwe kusikia mambo yale ambayo wanahitajika sana kujifunza. [Pr 272.3; Maombi Aya ya 20]

Shetani anajua vyema kwamba wote wale ambao yeye anaweza kuwaongoza kwenye kupuuzia maombi na kuyachunguza Maandiko, watatekewa/watazidiwa na mashambulizi yake. Kwa hivyo yeye huvumbua kila nyenzo inayowezekana ili kuishugulisha na kuiteka akili. Daima kumewahi kuwa na tabaka la watu wanaokiri kumcha MUNGU, ambao, badala ya kufuata ili kuijua ile Kweli, wanaifanya dini yao kuwa ni kutafuta kasoro fulani ya tabia au makosa fulani ya kiimani kwa wale ambao hawakubaliani nao. Hao ndio wasaidizi wa mkono wa kulia wa Shetani. Washitaki wa ndugu si wachache, na daima wapo kibaruani wakati MUNGU anapofanya kazi na watumishi Wake wanaomtolea ibada ya Kweli. Wataweka rangi za uwongo juu ya maneno na matendo ya wale wanaoipenda na kuitii ile Kweli. Watawashutumu watumishi wa Kristo walio waaminifu zaidi, wenye bidii na wanaojikana nafsi zao kama waliodanganyika au wadanganyifu. Ni kazi yao kupotosha nia ya kila tendo la Kweli na bora/adhimu,

kusambaza maneno ya hiana, na kuibua mashaka katika akili za wasio na uzoefu. Kwa kila njia inayowezekana watatafuta kufanya kile kilicho safi na cha haki au uadilifu, kionekane kuwa najisi, kichafu na cha udanganyifu.—(The Great Controversy, 519) [Pr 273.1; Maombi Aya ya 21]

SURA YA 28

MAOMBI KATIKA SIKU ZA MWISHO

Wale Wanaoishi hasa Katika Siku za Mwisho Wanahitaji Kuomba—Ikiwa

Mwokozi wa wanadamu, na nguvu Zake takatifu, alihisi hitaji la maombi, ni kiasi gani watu wanyonge, wenye dhambi wanapaswa kuhisi umuhimu wa maombi—maombi ya bidii na ya kudumu! Wakati Kristo alipopatwa na majaribu makali zaidi, Hakula chochote. Alijikabidhi kwa MUNGU, na kupitia maombi ya dhati, na kujitiisha kikamilifu kwenye mapenzi ya Baba Yake, Naye aliibuka kama mshindi. Wale wanaoukiri na kuushuhudia Ukweli kwa ajili ya siku hizi za mwisho, zaidi ya jamii nyingine yoyote ya wanaodai kuwa Wakristo, wanapaswa kumwiga Yeye Yule aliye Kielelezo Kikuu katika maombi.— (Counsels on Diet and Foods, 52, 53) [Pr 274.1; Maombi Aya ya 1]

Watu wa MUNGU Wana Wajibu wa Kuomba kwa ajili ya Miaka Michache Zaidi ya Neema Kabla Mwisho haujafika—Lazima kuwe na hali ya kiroho zaidi, kujitolea wakfu kwa kina zaidi kwa MUNGU, na usongo/ari katika kazi Yake ambayo haijapata kufikiwa bado. Muda mwingi utumike katika maombi, ili mavazi yetu ya utu yasafishwe na kufanywa meupe katika damu ya Mwana-Kondoo. [Pr 274.2; Maombi Aya ya 2]

Tunapaswa kuwa na imani isiyoyumba haswa, tunapaswa kumtafuta MUNGU ili neema na nguvu zitolewe kwa watu Wake sasa. Hatuamini kwamba wakati umetimia wa kuwekwa vikwazo juu ya uhuru wetu. Nabii aliona “malaika wanne wamesimama katika pembe nne za dunia, wakizuia pepo nne za dunia, upepo usivume juu ya nchi, wala juu ya bahari, wala juu ya mti wowote. Malaika mwingine, akipanda kutoka mashariki, akawalilia, akisema, Msiidhuru nchi, wala bahari, wala miti, hata tutakapokwisha kuwatia muhuri watumishi wa MUNGU wetu katika vipaji vya nyuso zao.” Hii inasonda kazi tunayopaswa kufanya sasa. Wajibu mkubwa umekabidhiwa kwa wanaume na wanawake wa maombi katika nchi nzima kuomba ili MUNGU afagilie mbali wingu la uovu na kutoa miaka michache zaidi ya neema ya kufanya kazi kwa ajili ya Bwana. Hebu tumlilie MUNGU ili malaika wazizuie pepo nne hadi wamishonari watakapotumwa katika sehemu zote za ulimwengu na kutangaza onyo dhidi ya kutotii sheria ya Yehova.— (Testimonies for the Church 5:717, 718. [Pr 274.3; Maombi Aya ya 3])

Maombi Katika Nyakati za Amani yatawatayarisha Watu wa MUNGU kwa ajili ya Nyakati za Taabu Mwishoni—Watumishi wa Kristo hawakupaswa kutayarisha maelezo au hotuba yoyote ya kutoa watakapofikishwa mahakamani. Maandalizi yao yalipaswa kufanywa siku baada ya siku katika kuzitunza Kweli za thamani za Neno la MUNGU, na kwa njia ya maombi kuimarisha imani yao. Watakapofikishwa mahakamani, Roho Mtakatifu atawakumbusha zile Kweli ambazo zitahitajika haswa. [Pr 275.1; Maombi Aya ya 4]

Juhudi za kila siku za dhati za kumjua MUNGU, na Yesu Kristo ambaye amemtuma, zitaleta nguvu na ufanisi kwenye nafsi. Ujuzi unaopatikana kwa kuchunguza Maandiko kwa bidii uliangaziwa katika kumbukumbu kwa wakati ufaao. Lakini kama kuna yeyote ambaye alikuwa amepuuza kujizoeza na kujifahamisha na Maneno ya Kristo, endapo hawakupata kamwe uwezo wa

neema Yake katika majaribu, basi wasingeweza kutarajia kwamba Roho Mtakatifu angeleta Maneno Yake kwenye kumbukubu zao. Walipaswa kumtumikia MUNGU kila siku kwa upendo usiogawanyika, na kisha kumtumaini Yeye.—(The Desire of Ages, 355) [Pr 275.2; Maombi Aya ya 5]

Tunaishi katika kipindi kigumu zaidi cha historia ya ulimwengu huu. Hatima ya umati wa watu duniani inakaribia kuamuliwa. Ustawi wetu wenyewe wa wakati ujao, na pia wokovu wa roho nyingine, unategemea njia tunayofuata sasa. Tunahitaji kuongozwa na Roho wa Kweli. Kila mfuasi wa Kristo anapaswa kuomba na kuuliza kwa bidii, “Bwana, wataka mimi nifanye nini?” Tunahitaji kujinyenyekeza mbele za Bwana, kwa kufunga na kuomba, na kutafakari sana Neno Lake, hasa kuhusiana na matukio ya hukumu. Inatupasa sasa kutafuta uzoefu wa kina na ulio hai katika mambo ya MUNGU. Hatuna muda wa kupoteza. Matukio ya muhimu sana yanafanyika karibu nasi; tuko kwenye ardhi ya Shetani iliyorogwa.—(The Great Controversy, p. 601) [Pr 275.3; Maombi Aya ya 6]

Majira ya dhiki na uchungu mbele yetu yatahitaji imani inayoweza kustahimili uchovu, uchelewesho/kukawia, na njaa— imani ambayo haitazimia ingawa imejaribiwa vikali. Muda wa rehema umetolewa kwa wote kujiandaa kwa ajili ya wakati huo. Yakobo alishinda kwa sababu alivumilia, aliazimia na kujizatiti. Ushindi wake ni ushahidi wa nguvu ya maombi ya yasiyochoka na yenye bidii. Wote watakaoshikilia ahadi za MUNGU, kama yeye Yakobo, na kuwa dhati na wavumilivu kama alivyokuwa, watafanikiwa kama alivyofaulu. Wale ambao hawako tayari kujikana nafsi, kuteseka mbele ya MUNGU, kuomba kwa muda mrefu na kwa bidii kwa ajili ya baraka Zake, hakika hawataipata. Kushindana mweleka na MUNGU (mfano wa Yakobo na Malaika)—ni wachache kiasi gani wanaojua ina maana gani! Ni wachache kiasi gani wamewahi kuvutiwa roho zao kumfuata Mwenyezi MUNGU kwa matamanio makubwa kiasi cha kunyumbulisha kila nguvu. Wakati mawimbi ya kukata tamaa ambayo hakuna lugha inayoweza kueleza yanapomkumba mwombaji, ni wachache kiasi gani wanaoshikamana na imani isiyobadilika kwenye ahadi za MUNGU.— (The Great Controversy, 621) [Pr 276.1; Maombi Aya ya 7]

Maombi yawe ulinzi hata Mwisho—Hadi pambano hilo litakapokoma, kutaendelea kuwa na wale ambao watamwacha MUNGU. Shetani atatengeneza mazingira kiasi kwamba tusipotunzwa na uwezo wa Bwana, yatakaribia kuharibu ngome za nafsi bila kujua. Tunahitaji kuomba katika kila hatua, “Je, hii ndiyo njia ya Bwana?” kadiri tunavyoishi, kutakuwa na haja ya kulinda mapenzi na shauku kwa kusudi thabiti. Hakuna hata dakika moja tunayoweza kuwa salama isipokuwa tunategemea MUNGU, maisha yaliyofichwa pamoja na Kristo. Kukesha na maombi ni ulinzi wa usafi wa moyo. [Pr 276.2; Maombi Aya ya 8]

Wote wanaoingia katika Jiji la MUNGU wataingia kupitia mlango mwembamba tu— kwa bidii kubwa; kwa maana “hakitaingia humo chochote kilicho najisi. Ufunuo 21:27. Lakini hakuna yeyote aliyeanguka anayehitaji kukata tamaa.

Wazee, ambao hapo awali waliheshimiwa na MUNGU, wanaweza kuwa walitia unajisi roho zao, wakitoa mhanga wema katika madhabahu ya tamaa za mwili; lakini wakitubu, na kuacha dhambi, na kumgeukia MUNGU, bado kuna matumaini kwao. Yeye atangazaye, "Uwe mwaminifu hata kufa, Nami nitakupa taji ya uzima," pia anatoa mwaliko, "Mtu mbaya na aache njia yake, na mtu asiye haki aache mawazo yake, amrudie Mwenyezi-MUNGU apate kumhurumia, amwendee MUNGU wetu maana atamsamehe kabisa." Ufunuo 2:10; Isaya 55:7. MUNGU anachukia dhambi, lakini anampenda mwenye dhambi. "Nitaponya uasi wao," asema; "Nitawapenda kwa ukunjufu wa moyo." Hosea 14:4.— (Manabii na Wafalme, 83, 84.) [Pr 276.3; Maombi Aya ya 9]

Kundi dogo Litakuwa Likiombea Kanisa Katika Wakati wa Hatari Yake Kubwa Zaidi—Chachu ya utauwa haijapoteza nguvu zake kabisa. Wakati ambapo hatari na mfadhaiko wa kanisa ni mkubwa zaidi, kundi dogo ambalo limesimama kwenye nuru litakuwa likiugua na kulia kwa ajili ya machukizo yanayofanywa katika nchi. Lakini zaidi sana maombi yao yatainuliwa kwa niaba ya kanisa kwa sababu washiriki wake wanafanya kulingana na namna ya ulimwengu. [Pr 277.1; Maombi Aya ya 10]

Maombi ya bidii ya waaminifu hawa wachache hayataenda bure. Wakati Bwana atakapokuja kama muhukumu, atakuja pia kama mlinzi wa wale wote ambao wameilinda imani katika usafi wake na kujilinda wenyewe bila mawaa dhidi ya ulimwengu. Ni wakati huu ndio ambao MUNGU ameahidi kulipiza kisasi kwa niaba ya wateule Wake ambao humlilia mchana na usiku, ingawa Yeye huchukuliana nao na kuwavumilia kwa muda mrefu — (Testimonies for the Church 5:209, 210) [Pr 277.2; Maombi Aya ya 11]

Omba kwa ajili ya Roho Wakati wa Mvua ya Masika—Hatuwezi kutegemea mazoea au taasisi za nje. Tunachohitaji ni ushawishi wa kuhuisha wa Roho Mtakatifu wa MUNGU. "Si kwa nguvu, wala si kwa uwezo, bali kwa Roho Wangu, asema Bwana wa Majeshi." Ombeni bila kukoma, na kesheni kwa kufanya kazi sawasawa na maombi yenu. Unapoomba, amini, mtumaini MUNGU. Ni wakati wa mvua ya masika, ambapo Bwana atatoa Roho Wake kwa wingi. Uwe na bidii na ari/usongo katika maombi, na ukeshe katika Roho.—(The Review and Herald, March 2, 1897) [Pr 277.3; Maombi Aya ya 12]

Maombi ndio Usalama wa Mkristo katika siku za Mwisho— Niliona baadhi, wakiwa na imani yenye nguvu na vilio vya uchungu, wakimsihi MUNGU. Nyuso zao zilikuwa zimedhoofu na zilikuwa zina alama ya wasiwasi mwingi, zikionyesha mapambano yao ya ndani. Uthabiti na bidii kubwa vilionyeshwa katika nyuso zao; matone makubwa ya jasho yakaanguka kutoka kwenye vipaji vya nyuso zao. Mara kwa mara nyuso zao ziling'aa kwa alama za ukubalio/kibali cha MUNGU, na tena ule mwonekano ule mzito, wa dhati, na wa wasiwasi ukakaa juu yao. [Pr 278.1; Maombi Aya ya 13]

Malaika waovu walikusanyika kuwazunguka, wakisukuma giza juu yao ili kumfungia Yesu asionekane nao, ili macho yao yavutwe kwenye giza lililowazunguka, na hivyo kuongozwa kutomwamini MUNGU na kumnung'unikia. Usalama wao pekee ulikuwa katika kuelekeza macho yao juu. Malaika wa MUNGU walikuwa na mamlaka juu ya watu Wake, na anga hewa lenye sumu ya malaika waovu iliposogezwa karibu na hawa wenye wasiwasi, malaika wa mbinguni walikuwa wakipepea mbawa zao juu yao ili kulitawanya giza nene. [Pr 278.2; Maombi Aya ya 14]

Waombaji walipokuwa wakiendelea na kilio chao cha dhati, nyakati fulani nuru ya Yesu iliwajia, ili kutia moyo mioyo yao na kuangaza nyuso zao. Baadhi, niliwaona, hawakushiriki katika kazi hii ya kuteseka na kusihi. Walionekana kutozingatia na kutojali. Hawakuwa wakipinga giza lililowazunguka, na liliwafunga kama wingu zito. Malaika wa MUNGU waliwaacha hawa na kwenda kusaidia wale walio na bidii, wanaosali. Niliona malaika wa MUNGU wakiharakisha kuwasaidia wale wote waliokuwa wakihangaika kwa uwezo wao wote kuwapinga malaika wabaya na kujaribu kujisaidia wenyewe kwa kumwita MUNGU kwa ustahimilivu. Lakini malaika Wake waliwaacha wale ambao hawakufanya jitihada yoyote ya kujisaidia, nao wakapotea katika upeo wa macho yangu.—(Early Writings, 269) [Pr 278.3; Maombi Aya ya 15]

Watu wa MUNGU Wataomba na Kushinda Mwishoni Kama Alivyofanya Yakobo—Yakobo na Esau wanawakilisha matabaka mawili; Yakobo mwenye haki, na Esau mwovu. Kufadhaika kwa Yakobo alipojua kwamba Esau alikuwa anakuja dhidi yake akiwa na gwaride la watu mia nne, hii inawakilisha taabu ya wenye haki wakati amri inapotoka ya kuwaua, kabla tu ya kuja kwa Bwana. Waovu wanapokusanyika kuwazunguka, watajawa na mateso ya akili na mwili, kwani hawawezi kuona njia ya kuyaponya maisha yao kama Yakobo. Malaika akajiweka mbele ya Yakobo, naye akamshika malaika huyo, na kumng'ang'ania, na akashindana Naye mieleka usiku kucha. Vivyo hivyo na wenye haki, wakati wa taabu na dhiki zao, watahindana mweleka na MUNGU katika maombi, kama vile Yakobo alivyoshindana mweleka na malaika. Yakobo katika dhiki yake aliomba usiku kucha kwa ajili ya ukombozi kutoka kwenye mkono wa Esau. Wenye haki katika uchungu wao wa kiakili watamlilia MUNGU mchana na usiku ili awakomboe kutoka katika mkono wa waovu wanaowazunguka. [Pr 278.4; Maombi Aya ya 16]

Yakobo alikiri kutostahili kwake. "Sistahili hata kidogo rehema Zako zote, na Kweli yote uliyonionyesha mtumishi wako." Wenye haki, katika dhiki yao, watakuwa na hisia ya kina ya kutostahili kwao, na kwa machozi mengi watakiria kutostahili kwao kabisa, na kama vile Yakobo wataomba ahadi za MUNGU kwa njia ya Kristo, zilizofanywa kwa ajili ya wadhambi kama hao wategemezi, wasiojiweza, wenye dhambi wanaotubu. [Pr 279.1; Maombi Aya ya 17]

Yakobo akamng'ang'ania huyo Malaika katika shida yake, wala hakumruhusu

aende zake. Alipokuwa akiomba dua kwa machozi, Malaika huyo alimkumbusha makosa yake ya zamani, na akajaribu kumtoroka Yakobo, ili kumjaribu na kumthibitisha. Ndivyo hivyo wenye haki, katika siku ya dhiki yao, watapimwa, na kuthibitishwa, na kujaribiwa, ili kudhihirisha nguvu zao za imani, ustahimilivu wao na ujasiri usiotikisika katika uwezo wa MUNGU wa kuwakomboa. [Pr 279.2; Maombi Aya ya 18]

Yakobo hakuweza kugeuzwa. Alijua kwamba MUNGU ni mwenye rehema, na aliomba rehema Yake. Aliangalia nyuma kwenye huzuni yake ya zamani na toba ya makosa yake, na akashinikiza ombi lake la ukombozi dhidi ya mkono wa Esau. Hivyo ombi lake lisilochoka na lenye msukumo likaendelea usiku kucha. Alipopitia upya makosa yake ya zamani, ilimfanya kukaribia kukata tamaa. Lakini alijua kwamba lazima apate msaada kutoka kwa MUNGU au aangamie. Akamshika yule malaika, akashinikiza ombi lake kwa kilio cha uchungu, cha bidii, hata akashinda. Ndivyo itakavyokuwa kwa watu wema. Wanapopitia matukio ya maisha yao ya zamani, matumaini yao yatakaribia kuzama. Lakini wanapotambua kwamba ni jambo la uzima au kifo, watamlilia MUNGU kwa bidii, na kumsihi kuhusiana na huzuni yao ya zamani na toba ya unyenyekevu ya dhambi zao nyingi, na kisha watarejea kwenye ahadi yake, “Hebu ashike nguvu zangu, na afanye amani nami, naye atafanya amani nami.” Hivyo maombi yao ya bidii yatatolewa kwa MUNGU mchana na usiku.—(Spiritual Gifts 3:131- 133) [Pr 279.3; Maombi Aya ya 19]

SURA YA 29

FURSA YA MAOMBI -UPENDELEO WA MAOMBI

UPENDELEO WA MAOMBI

Kupitia asili na ufunuo, kupitia majaliwa na uongozi Wake Bwana, na kwa ushawishi wa Roho Wake, Mungu huzungumza nasi. Lakini haya hayatoshi; sisi tunahitaji pia kumimina mioyo yetu Kwake Yeye Bwana. Ili tuweze kuwa na uzima wa maisha ya kiroho na nguvu, ni lazima tuwe na ushirika na uhusiano halisi na Baba yetu wa mbinguni. Akili zetu zinaweza kuvutwa kumwelekea Yeye; tunaweza kutafakari kazi Zake, rehema Zake, baraka Zake; lakini hii sio kwa maana kamili, kuwa na ushirika Naye. Ili kuwasiliana na

Mungu, ni lazima tuwe na kitu cha kumwambia Yeye kuhusu maisha yetu halisi-[yale yanayotendeka kila siku]. {SCsw 93.1}

Maombi ni kufungua moyo kwa Mungu kama kwa rafiki. Sio kwamba ni lazima kumjulisha Mungu, kuwa sisi tukoje au tulivyo, bali ili kutuwezesha kumpokea Yeye. Maombi hayamshushi Mungu chini, bali yanatunyanyua juu Kwake. {SCsw 93.2}

Yesu alipokuwa duniani, aliwafundisha wanafunzi Wake jinsi ya kuomba. Aliwaelekeza kuwasilisha mahitaji yao ya kila siku mbele za Mungu, na kumtwika Yeye mahangaiko yao yote. Na uhakikisho aliowapa kwamba maombi yao yatasikilizwa na Yeye, ni uhakikisho wetu pia. {SCsw 93.3}

Yesu Mwenyewe, alipokuwa akiishi miongoni mwa wanadamu, mara nyingi alikuwa katika maombi. Mwokozi wetu alijitambulisha na mahitaji na udhaifu wetu, katika hilo, Yeye akawa mwombaji, mtu Anayesihi kwa niaba yetu, akitafuta kutoka kwa Baba Yake nyongeza ya nguvu mpya, ili apate kwenda akiwa imara, mwenye utayari na aliyejiandaa kabisa, kwa ajili ya kazi, majukumu na majaribu. Yeye ni mfano wetu katika mambo yote. Yeye ni ndugu katika udhaifu wetu, "katika mambo yote alijaribiwa kama sisi;" lakini kama Yule asiye na dhambi, asili yake ilijiepusha na uovu; Alivumilia mapambano na mateso ya roho katika ulimwengu wa dhambi. Ubinadamu Wake ulifanya maombi kuwa jambo la lazima, kipaumbele, upendeleo na fursa. Alipata faraja na furaha katika ushirika na Baba Yake. Na ikiwa Mwokozi wa wanadamu, Mwana wa Mungu, alihisi hitaji la maombi, Je, ni kwa kiasi gani, wanadamu wanyonge, dhaifu na wenye dhambi wanapaswa kuhisi ulazima wa maombi ya bidii, yenye ari na ya kudumu. {SCsw 93.4}

Baba yetu wa mbinguni anatusubiri ili atupe ukamilifu wa baraka Zake. Ni fursa yetu kunywa kwa kiasi kikubwa, kwenye chemchemi ya upendo usio na mipaka. Inashangaza sana kwamba tunaomba kidogo sana! Mungu ameridhia na Yuko tayari kusikia maombi ya dhati ya mtoto Wake aliye

mnyenyekevu zaidi, na bado kuna kusita-sita sana kwa upande wetu, kumjulisha Mungu mahitaji/matakwa yetu. Malaika wa mbinguni wanaweza kufikiria nini kuhusu wanadamu dhaifu na maskini wasiojiweza, ambao wanakabiliwa na majaribu, wakati moyo wa Mungu wa upendo usio na kifani, una shauku kwao, ukiwahitaji, na uko tayari kuwapa zaidi ya vile wanavyoweza kuomba au kufikiria, na bado wao wanaomba kidogo sana na wana imani ndogo sana? Malaika hupenda kusujudu mbele za Mungu; wanapenda kuwa karibu Naye. Huona ushirika na Mungu kama ndiyo furaha yao kuu; na bado watoto wa dunia, ambao wanahitaji msaada tele, ambao Mungu pekee Ndiye anayeweza kutoa, wanaonekana kutosheka, kutembea bila nuru ya Roho Wake, kuandamana na uwepo Wake. {SCsw 94.1}

Giza la yule mwovu huwafunika wale wanaopuuza kuomba. Majaribu ya adui yanayonong'oneza, huwashawishi wanadamu kutenda dhambi; na yote ni kwa sababu hawatumii upendeleo ambao Mungu amewapa katika miadi na Mungu katika maombi. Kwa nini wana na binti za Mungu wasitake kuomba, wakati maombi ndiyo ufunguo katika mkono wa imani kufungua ghala la mbinguni, ambapo hazina zisizo na kikomo za Mwenyezi Mungu zimehifadhiwa? Bila maombi yasiyokoma na (kukeshwa) maombi yasiyochoka, na ya bidii, tuko katika hatari ya kuwa wazembe na kupotoka kutoka kwenye njia sahihi. Adui anatafuta daima kufunga njia ya kwenda kwenye kiti cha rehema, ili tusipate neema na nguvu za kupinga majaribu kwa bidii, kwa maombi na imani. {SCsw 94.2}

Kuna masharti fulani ambayo tunaweza kutarajia kwamba Mungu atasikia na kuyajibu maombi yetu. Mojawapo ya haya ni kwamba tunahisi hitaji letu la msaada kutoka Kwake. Yeye Ameahidi, ***"Kwa maana nitamimina maji juu yake aliye na kiu, na vijito vya maji juu ya mahali pakavu. Isaya 44:3*** Wale wenye njaa na kiu ya haki, wenye matamanio na Mungu (wenye shauku na Mungu), wanaweza kuwa na uhakika kwamba watajazwa-wataashibishwa. Moyo

lazima uwe wazi kwa ushawishi wa Roho, la sivyo baraka za Mungu haziwezi kupokelewa. {SCsw 95.1}

Haja yetu kuu yenyewe, ni hoja tosha na inasihi kwa kujieleza kwa umbuji/ufasaha zaidi kwa niaba yetu. Lakini Bwana anapaswa kutafutwa ili afanye haya mambo kwa niaba yetu. Bwana Anasema, *ombeni, nanyi mtapewa; Yeye asiyemwachilia Mwana Wake Mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja Naye?* Mathayo 7:7, Warumi 8:32 {SCsw 95.2}

Tukiendekeza au kuzingatia uovu mioyoni mwetu, tukishikilia/tukishikamana na dhambi yoyote inayojulikana, Bwana hatatusikia; lakini sala ya mtu aliyetubu, na kukiri hukubaliwa daima. Wakati makosa yote yanayojulikana yanaporekebisha, tunaweza kuamini kwamba Mungu atajibu maombi yetu. Haki na Sifa zetu wenyewe hazitatufanya kamwe "tukubaliwe na Mungu; ni haki na sifa ya Yesu tu, ndiyo ambazo" zitatuokoa, damu Yake itatusafisha; lakini tuna kazi ya kufanya kwa kuzingatia masharti ya kukubalika. {SCsw 95.3}

Kipengele kingine cha maombi yanayoshinda, na yanayoendana na mapenzi ya Mungu na yasiyochoka ni Imani *"kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba Yeye Yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao. Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu. Waebrania 11:6, Marko 11:24"* Je, tunamkubali na kumwendea Bwana kama asemavyo, katika Neno Lake? {SCsw 96.1}

Uhakikisho ni mpana na hauna kikomo, na Yeye Aliye Mwaminifu ambaye ameahidi, atatenda. Tusipopokea mambo bainishi tuliyoomba, wakati tunapoomba, bado tunapaswa kuamini. Sisi ni wakosefu sana na hivyo hatuoni mbali kiasi kwamba, wakati mwingine huwa tunaomba mambo ambayo hayatakuwa baraka kwetu, na Baba yetu wa mbinguni kwa upendo, hujibu maombi yetu kwa kutupa kile ambacho kitakuwa kwa faida yetu kuu zaidi—kile ambacho sisi wenyewe tungetamani tukipate, ikiwa tungeangaziwa na maono yenye nuru ya Kiungu na kuweza kuona mambo yote

kama yalivyo kweli. Wakati maombi yetu yanapoonekana kutojibiwa, tunapaswa kuishika ahadi kwa kuing'ang'ania; kwani wakati wa kujibiwa hakika utakuja, na tutapokea baraka tunayohitaji zaidi. Lakini kudai kwamba maombi yetu daima yatajibiwa kwa njia ileile tuliyotaka na kwa jambo fulani maalum tunalotamani na kuomba, ni dhana/ujuvi tu (presumption). Mungu ni Mwenye hekima sana, hata asiweze kamwe kukosea, na ni mwema sana, hata asiweze kuwanyima kitu chochote chema wale wanaotembea kwa unyoofu. Basi usiogope kumwamini Bwana, ingawa hauoni majibu ya haraka kwa maombi yako. Tegemea ahadi Yake ya uhakika, "Ombeni, nanyi mtapewa." {SCsw 96.2}

Tukiruhusu mashaka na hofu zetu kutushauri na kutuongoza, kwamba zijaribu kutatua kila tatizo au kitu ambacho hatuwezi kukiona waziwazi, kabla hatujawa na imani, matatizo yataongezeka tu na kuzidi kuwa makubwa. Lakini tukimjia Mungu, tukihisi hatuna msaada na tegemezi, kama tulivyo, na kwa imani ya unyenyekevu na ya kumtumaini, tunamjulisha Yeye ambaye ujuzi Wake hauna kikomo, ambaye anaona kila kitu katika uumbaji, na anayetawala kila kitu kwa mapenzi na Neno Lake, Anaweza na Atasikiliza kilio chetu, na Ataacha nuru iangaze mioyoni mwetu. Kupitia maombi ya dhati tunaunganishwa na akili isiyo na ukomo. Huenda tusiwe na ushahidi wa ajabu wakati huo kwamba uso wa Mkombozi wetu unainama juu yetu kwa huruma na upendo, lakini hata hivyo, ndivyo ilivyo. Huenda tushisi mguso Wake unaoonekana na kuhisiwa, lakini mkono Wake uko juu yetu kwa upendo, sikitiko na huruma nyororo, na kujali. {SCsw 96.3}

Tunapokuja kuomba rehema na baraka kutoka kwa Mungu tunapaswa kuwa na roho ya upendo na msamaha mioyoni mwetu. Tunawezaje kuomba, ***"utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu"*** wakati bado tuna roho ya kutosamehe? **Mathayo 6:12**. Tukitarajia maombi yetu yasikilizwe, ni lazima tuwasamehe wengine kwa njia ile ile na kwa upana/kiwango kile kile tunachotumaini kusamehewa. {SCsw 97.1}

Uvumilivu katika maombi umefanywa kuwa sharti la kupokea. Lazima tuombe kila wakati ikiwa tunataka kukua katika imani na uzoefu. Tunapaswa kuwa “wenye kukesha *katika kusali, Dumuni sana katika kuomba, mkikesha katika kuomba huku na shukrani*; Warumi 12:12, Wakolosai 4:2. Petro anawasihi waumini kuwa *iweni na akili, mkeshe katika sala. 1 Petro 4:7* Paulo anaelekeza, *bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Wafilipi 4:6*. “Lakini ninyi, wapenzi,” Yuda anasema, *na kuomba katika Roho Mtakatifu, jilindeni katika upendo wa Mungu. Yuda 1:20-21*. Maombi yasiyokoma ni muungano usiovunjika wa roho na Mungu, ili uhai kutoka kwa Mungu utiririke katika maisha yetu; na kutoka kwenye maisha yetu, usafi na utakatifu utiririke kwa Mungu. {SCsw 97.2}

Kuna ulazima wa bidii na uadilifu katika maombi; hebu usiruhusu chochote kikuzuie. Fanya kila juhudi kuweka wazi ushirika kati ya Yesu na nafsi yako. Tafuta kila fursa ya kwenda mahali ambapo maombi yamezoeleka kufanywa. Wale wanaotafuta ushirika na Mungu wataonekana katika mkutano wa maombi, wakiwa waaminifu kufanya wajibu wao na wenye bidii na hamu ya kuvuna faida zote wanazoweza kupata. Wataboresha kila fursa ya kujiweka mahali ambapo wanaweza kupokea miale ya nuru kutoka mbinguni. {SCsw 98.1}

Tunapaswa kuomba katika mzunguko wa familia, na zaidi ya yote hatupaswi kupuuza maombi ya siri, kwani haya ndiyo uzima wa nafsi. Haiwezekani roho kustawi huku maombi ya faragha yamepuuzwa. Sala ya familia au ya hadharani pekee yake haitoshi. Katika upweke ruhusu roho yako inanikwe wazi kwa jicho la ukaguzi la Mungu linalochunguza. Maombi ya siri yanapaswa kusikilizwa na Mungu tu, anayesikia maombi. Hakuna sikio la udadisi linalopaswa kupokea mzigo wa maombi kama hayo. Katika maombi ya siri, nafsi inakuwa huru kutokana na ushawishi unaoizunguka, huru dhidi ya msisimko. Kwa utulivu, lakini kwa bidii, yatamfikia Mungu. Mvuto utakaotoka Kwake Yeye

aonaye sirini, utakuwa mzuri na wa kudumu, Yeye ambaye sikio Lake liko wazi kusikia maombi yanayotoka moyoni. Kwa imani tulivu na iliyo sahili, roho hushirikiana na Mungu na kukusanya miale ya nuru ya Bwana ili kuiimarisha na kuitegemeza katika pambano na Shetani. Mungu Ndiye ngome yetu ya nguvu. {SCsw 98.2}

Omba chumbani kwako, na unapoendelea na kazi yako ya kila siku ruhusu moyo wako uinuliwe juu kwa Mungu, mara nyingi. Ndivyo Henoko alivyotembea na Mungu. Maombi haya ya kimya-kimya huinuka kama uvumba wa thamani mbele ya kiti cha neema. Shetani hawezi kumshinda yeye ambaye moyo wake umesimama na kujitegemeza kwa Mungu. {SCsw 98.2}

Hakuna wakati au mahali ambapo haifai kutoa ombi kwa Mungu. Hakuna kitu kinachoweza kutuzuia kuinua mioyo yetu kwa roho ya maombi ya dhati. Katika umati wa watu barabarani, katikati ya shughuli za kibiashara, tunaweza kutuma ombi kwa Mungu na kuomba mwongozo wa Bwana, kama Nehemia alivyofanya alipoomba mbele ya Mfalme Artashasta. Chumba cha ushirika kinaweza kupatikana popote tulipo. Tunapaswa kuendelea kuacha mlango wa moyo ukiwa wazi kila wakati na mwaliko wetu ukiendelea kupanda juu ili Yesu aje, na kukaa ndani ya moyo kama mgeni wa mbinguni katika nafsi. {SCsw 99.1}

Ingawa kunaweza kuwa na mazingira machafu na yaliyoharibika yanayotuzunguka, hatuhitaji kupumua hewa yake chafu, na yenye harufu mbaya, lakini tunaweza kuishi katika hewa safi ya mbinguni. Tunaweza kufunga kila mlango kwa fikra chafu na mawazo yasiyo matakatifu kwa kuinua roho mbele za Mungu kupitia maombi ya dhati. Wale ambao mioyo yao iko wazi kupokea usaidizi na baraka za Mungu watatembea katika angahewa takatifu zaidi kuliko ile ya dunia na watakuwa na ushirika wa kudumu na mbingu. {SCsw 99.2}

Tunahitaji kuwa na mitazamo na maoni dhahiri, na bainishi zaidi kuhusu Yesu na ufahamu kamili wa thamani wa uhalisia wa milele. Uzuri wa utakatifu unapaswa kuijaza

mioyo ya watoto wa Mungu; na ili hili liweze kutimizwa, tunapaswa kutafuta mafunuo ya Bwana yahusuyo mambo ya mbinguni. {SCsw 99.3}

Hebu nafsi ivutwe nje na kwenda juu, ili Mungu atupe pumzi ya angahewa ya mbinguni. Tunaweza kukaa karibu sana na Mungu kiasi kwamba katika kila jaribu lisilotazamiwa, mawazo yetu yatamgeukia Yeye kama asili, yaani kama kawaida ya ua linavyoligeukia jua (phototropism). {SCsw 99.4}

Weka matakwa yako, furaha yako, huzuni zako, wasiwasi wako, na hofu zako mbele za Mungu. Huwezi kumlelea Bwana; huwezi kumchosha Mwenyezi Mungu. Yeye ahesabuye nywele za kichwa chako hayupo kinyume cha matakwa ya watoto Wake. ***"Bwana ni mwingi wa rehema, Mwenye huruma."*** Yakobo 5:11 Moyo Wake wa upendo huguswa na huzuni zetu na hata na matamshi yetu. Mpelekee Bwana kila kitu kinachosumbua akili. Hakuna kitu kikubwa sana Kwake kukibeba, kwa maana Yeye hushikilia ulimwengu, Anatawala mambo yote ya ulimwengu. Hakuna kitu ambacho kwa namna yoyote kinahusu amani yetu ambacho ni kidogo sana Kwake kukiona. Hakuna sura katika uzoefu wetu iliyo giza sana Kwake kusoma; hakuna mkanganyiko ambao ni mgumu sana Kwake kuutatua. Hakuna msiba unaoweza kumpata hata mmoja wa watoto Wake wadogo, hakuna wasiwasi unaosumbua roho, hakuna furaha ya furaha, hakuna sala ya dhati inayotoka midomoni, ambayo Baba yetu wa mbinguni haoni, au ambayo hataonyesha kujali mara moja (upeseli). Yeye ***"Huwaponya waliopondeka moyo, Na kuziganga jeraha zao. Zaburi 147:3."*** Mahusiano kati ya Mungu na kila mtu ni bainishi na dhahiri, nayo yamesheni kana kwamba hakuna nafsi nyingine duniani, inayoshiriki uangalizi Wake, hakuna roho nyingine kwa ajili yake ambayo Yeye alimtoa Mwanawe mpendwa. {SCsw 100.1}

Yesu alisema, ***"mtaomba kwa Jina Langu, wala siwaambii ya kwamba Mimi nitawaombea kwa Baba; kwa maana Baba Mwenyewe awapenda kwa kuwa ninyi"***

*mmenipenda Mimi, na kusadiki ya kwamba Mimi nalitoka kwa Baba-bali ni Mimi niliyewachagua ninyi; Nami nikawaweka mwende mkazae matunda; na matunda yenu yapate kukaa; ili kwamba lolote mmwombalo Baba kwa Jina Langu awapeni.*Yohana 16:26-27, 15:16 Lakini kuomba katika Jina la Yesu ni zaidi ya kutaja tu Jina hilo mwanzoni na mwisho wa sala. Ni kuomba katika akili na roho ya Yesu, huku tukiamini ahadi Zake, tukitegemea neema Yake, na kutenda kazi Zake. {SCsw 100.2}

Mungu hamaanishi kwamba yeyote kati yetu awe mtawa au awaepe watu kwa kujitenga na ulimwengu, ili kujitoa wakfu kwa matendo na shuguli za ibada. Maisha lazima yawe kama maisha ya Kristo—kati ya mlima na umati. Yeye ambaye hafanyi chochote isipokuwa kuomba, hivi karibuni ataacha kuomba, au vinginevyo maombi yake yatakuwa ya kaida na ratiba tu. Wanadamu wanapojiondoa katika maisha ya kijamii, mbali na nyanja ya wajibu wa Kikristo na kubeba msalaba; wanapoacha kufanya kazi kwa bidii kwa ajili ya Bwana, aliyewafanyia kazi kwa bidii, wanapoteza mada ya maombi na hawana motisha wa ibada au kujiweka wakfu. Maombi yao huwa yanawahusu wao tu na ya ubinafsi. Hawawezi kuomba kuhusu matakwa ya ubinadamu au ujenzi wa ufalme wa Kristo, hawataomba nguvu ya kufanya kazi ya Bwana. {SCsw 101.1}

Tunajipatia hasara kwa kuzembea kuchangamkia fursa ya kujumuika pamoja ili kuimarishana na kutiana moyo na wenzetu, katika kumtumikia Mungu-[huduma kwa kazi ya Mungu]. Kweli za Neno Lake Bwana hupoteza uwazi, picha zenye hisia na kumbukumbuku angavu, uhai na umuhimu wake katika bongo zetu. Mioyo yetu inaacha kuangazwa na kuzinduliwa kwa ushawishi ule unaotakasa, na tunashuka kwenda chini katika hali mionjo ya kiroho. Katika ushirikiano wetu kama Wakristo, tunapoteza mengi kwa kukosa huruma kwa kila mmoja wetu. Yeye anayejifungia mwenyewe, huwa hajazi nafasi ambayo Mungu alikusudia kuitimiza. Ukuzaji sahihi wa vipengele vya kijamii katika asili yetu hutuleta katika huruma na wengine na ni njia ya maendeleo na nguvu

kwetu katika huduma/utumishi wa Mungu. {SCsw 101.2}

Ikiwa Wakristo wangeshirikiana pamoja, wakisemezana kuhusu upendo wa Mungu na Ukweli wa thamani wa ukombozi, mioyo yao wenyewe ingeburudishwa kwa kufanywa upya na wao kwa wao wenyewe pia wangewasaidia wenzao kuburudishwa, na kufanywa upya. Tunaweza kujifunza zaidi kuhusu Baba yetu wa mbinguni kila siku, tukipata uzoefu mpya wa neema Yake; ndipo tutatamani kuzungumza juu ya upendo Wake; na tunapofanya hivi, mioyo yetu wenyewe itapata joto-joto na kutiwa moyo. Kama tungewaza na kumzungumzia zaidi Yesu, badala yetu sisi wenyewe, tungekuwa na uwepo Wake tele zaidi. {SCsw 101.3}

Ikiwa tungemfikiria Mungu mara nyingi kadiri tunavyopata ushahidi wa ulinzi na utunzaji Wake kwetu, tungeweza kumweka Yeye katika mawazo yetu kila wakati na ndipo tutajikuta tunafurahia kuzungumza kumhusu Yeye na kumsifu. Tunazungumzia mambo ya kidunia yanayopita kwa sababu tunapendezwa nayo. Tunazungumzia kuhusu marafiki zetu kwa sababu tunawapenda; furaha na huzuni zetu zimefungana pamoja nao. Ila sisi tuna sababu kubwa zaidi ya kumpenda Mungu kuliko hata kuwapenda marafiki zetu wa kidunia; inapaswa kuwa jambo la kawaida zaidi duniani kumfanya Bwana awe wa kwanza katika mawazo yetu yote, kuzungumza kuhusu wema Wake na kusimulia nguvu Zake.

Zawadi nyingi za thamani, alizotupa Yeye, hazikukusudiwa kufyonza mawazo na upendo wetu kiasi kwamba tunakosa kitu chochote cha kumpa Mungu; hizi zawadi zinapaswa kutukumbusha kuhusu Yeye kila wakati na kutufunga katika vifungo vya upendo na moyo wa shukrani kwa Mfadhili wetu wa mbinguni. Tunaishi karibu sana na nyanda za chini za dunia. Hebu na Tuyainue macho yetu kuelekea mlango ulio wazi wa Patakatifu pa juu mbinguni, ambapo nuru ya utukufu wa Mungu inang'aa kwenye uso wa Kristo, ambaye "aweza kuwaokoa kabisa"

wote wanaomjia Mungu kwa Yeye. Waebrania 7:25. {SCsw 102.1}

Tunahitaji kumsifu Mungu zaidi *"kwa fadhili Zake, na maajabu Yake kwa wanadamu. Zaburi 107:8* Mazoezi yetu ya ibada hayapaswi kuhusisha kuomba na kupokea peke yake. Hebu tusiwe tunafikiria mahitaji/matakwa yetu tu daima, na kamwe tusifikirie maslahi/faida tunazopokea. Hatuombi sana, nasi tunaacha kutoa shukrani kwa Mungu. Sisi ndio "wapokeaji wa rehema za Mungu kila mara, na bado ni shukrani ndogo kiasi gani tunayoonyesha, ni mara chache kiasi gani, sisi tunamsifu Bwana kwa yale ambayo ametufanyia." {SCsw 102.2}

Hapo awali, Bwana aliwaagiza Israeli, walipokutana pamoja kwa ajili ya huduma Yake, *"mtakula mbele za Bwana, Mungu wenu, nanyi furahini katika yote mtakayotia mikono yenu, ninyi na wa nyumbani mwenu, aliyokubarikia Bwana, Mungu wako. Kumbukumbu la Torati 12:7* Kile kinachofanywa kwa utukufu wa Mungu kinapaswa kufanywa kwa furaha, kwa nyimbo za sifa na shukrani, sio kwa huzuni, masikitiko na uchungu. {SCsw 103.1}

Mungu wetu ni Baba mpole, Mwenye mapenzi, anayejali na Mwenye huruma nyororo. Huduma Yake haipaswi kuchukuliwa kama zoezi gumu la kuhenyesha na la kusononesha moyo na kuleta msongo. Inapaswa kuwa furaha kumwabudu Bwana na kushiriki katika kazi Yake. Mungu hangetaka watoto Wake, ambao wokovu mkuu umetolewa kwao, watende kana kwamba Yeye ni msimamizi mgumu, mnyapara mkali, asiye na huruma, Mwenye kutubebesha majukumu mazito. Yeye Ndiye rafiki yetu/yao mkubwa; na tunapomwabudu, Yeye anatazamia kuwa pamoja nasi, kutubariki na kutufariji, akijaza mioyo yetu kwa furaha na upendo. Bwana anatamani watoto Wake tufarijike katika huduma Yake na kupata raha zaidi, kuliko shida na ugumu katika kazi Yake. Yeye Anatamani kwamba wale tunaokuja kumwabudu Yeye, tutarudi tukiwa na mawazo ya thamani ya ulinzi, utunzaji na upendo Wake, ili tuweze kuchangamshwa na kushangilia katika shuguli zote za

maisha ya kila siku, ili tupate neema ya kutenda kwa uadilifu/kiukweli na uaminifu katika mambo yote. {SCsw 103.2}

Ni lazima tukusanyike kuzunguka msalaba. Kristo na Yeye aliyesulubiwa anapaswa kuwa mada ya kutafakari, mazungumzo, na hisia zetu za furaha na shangwe zaidi. Tunapaswa kuweka katika mawazo yetu, kumbukumbu ya kila baraka tunayopokea kutoka kwa Mungu, na tunapotambua upendo Wake mkuu tunapaswa kuwa tayari kuamini, kwa kuweka kila kitu kwenye ule mkono uliopigiliwa misumari msalabani kwa ajili yetu. {SCsw 103.3}

Nafsi inaweza kupaa karibu na mbingu kwa mabawa ya sifa. Mungu anaabudiwa kwa wimbo na muziki katika makao ya juu, na tunapoonyesha shukrani zetu, basi tunakaribia ibada ya majeshi ya mbinguni. *"Atoaye dhabihu za kushukuru, Ndiye anayenitukuza. kushukuru, na sauti ya kuimba. Zaburi 50:23, Isaya 51:3* {SCsw 104.1}

Sura hii inaonekana katika Steps to Christ, 93-104

SURA YA 30

SALA YA BWANA

“Basi ninyi salini hivi.” Mathayo 6:9.

Sala ya Bwana ilitolewa mara mbili na Mwokozi wetu, kwanza mbele ya umati katika Mahubiri ya Mlimani, na kisha, miezi kadhaa baadaye kwa wanafunzi peke yao. Wanafunzi walikuwa wamekaa mbali kwa muda mfupi na Bwana wao, nao waliporudi walimkuta amezama/ametekewa katika ushirika/mawasiliano na MUNGU. Akiwa ameonekana kwao kwamba hajui uwepo wao, Aliendelea kuomba kwa sauti. Uso wa Mwokozi ulin’gaa, ukimulikwa na mwangaza wa mbinguni. Waliona kama Yupo mbele Zake kabisa Yeye Yule Asiyeonekana (Mungu BABA), na kulikuwa na nguvu hai katika Maneno Yake kama ya mtu anayezungumza na MUNGU. [Pr 289.1; Maombi Aya ya 1]

Mioyo ya wanafunzi waliokuwa wakisikiliza ilitekewa/iliguswa sana. Walikuwa wamehesabu ni mara ngapi Alikuwa ameenda kwa muda mrefu katika upweke kwenye ushirika na Baba Yake. Siku zake zilipita katika huduma kwa makutano waliomsonga, na katika kufunua hila za udanganyifu wa viongozi wa kidini, na kazi hii isiyokoma mara nyingi ilimfanya awe hoi kwa kuchoka sana hata mama Yake na ndugu Zake na pia wanafunzi Wake waliogopa kwamba ingemgarimu maisha (afya Yake ingetolewa mhanga). Lakini aliporudi kutoka katika saa za maombi zilizofunga siku ile yenye taabu, walishuhudia mwonekano wa amani juu ya uso Wake, hisia ya kuburudishwa ambayo ilionekana kutawala uwepo Wake. Upya na hali hii kwa ujumla vilitokana na saa alizotumia na MUNGU ndipo alienda, asubuhi baada ya asubuhi, kuleta nuru ya mbinguni kwa wanadamu. Wanafunzi Wake wakafikia hatima ya kuzihusisha saa Zake za maombi na nguvu za Maneno Yake na kazi Zake. Sasa, walipokuwa wakisikiliza ombi Lake, mioyo yao ilipata woga mtakatifu, kwa ule utukufu, na kisha wakanyenyekea. Alipomaliza kuomba tu, ilikuwa ni kwa usadikisho wa hitaji lao la ndani ndipo walipopaza sauti kusihi, “Bwana, tufundishe sisi kusali.” Luka 11:1. [Pr 289.2; Maombi Aya ya 2]

Yesu hawapi aina mpya ya ombi. Yale Aliyowafundisha hapo awali Anayarudia,

kana kwamba Angesema, Mnahitaji kuelewa kile nilichokwisha kutoa. Kina maana ya kina ambayo bado hamjaielewa. [Pr 290.1; Maombi Aya ya 3]

Mwokozi, hata hivyo, hatuzui kutumia maneno haya kama yalivyo. Akiwa mmoja na ubinadamu, Anawasilisha wazo Lake la maombi yaliyo bora, maneno mepesi sana kiasi kwamba yanaweza kukaririwa na mtoto mdogo, lakini yanafunika kila kitu na yanaeleweka sana kiasi kwamba umuhimu wake hauwezi kamwe kueleweka kikamilifu, hata na akili za werevu zaidi (**genius**). Tunafundishwa kumwendea MUNGU na zawadi yetu ya shukrani, kumweleza mahitaji yetu, kuungama dhambi zetu, na kudai rehema Zake kwa mujibu wa ahadi Zake. [Pr 290.2; Maombi Aya ya 4]

"Mnaposali, semeni Baba Yetu." Luka 11:2.

Yesu anatufundisha kumwita Baba Yake, Baba yetu. Yeye haoni haya kutuita ndugu Zake. Waebrania 2:11. Moyo wa Mwokozi kwa matamano makubwa uko tayari kutukaribisha kama wanachama wa familia ya MUNGU, ndio sababu katika Maneno Yake ya utambulisho Wake wa kwanza kabisa, tumeambiwa tupasavyo kuyatumia katika kumwendea/kumsogelea MUNGU, Yeye ameweka humo uhakikisho wa uhusiano wetu wa Kiungu Naye (na Mungu), "Baba yetu." [Pr 290.3; Maombi Aya ya 5]

Hili ni tangazo la Ukweli huo wa ajabu, Ukweli unaotia moyo na faraja mno, kwamba MUNGU anatupenda jinsi anavyompenda Mwanawe. Hivi ndivyo Yesu alisema katika sala yake ya mwisho kwa ajili ya wanafunzi Wake, "Umewapenda wao kama ulivyonipenda Mimi." Yohana 17:23. [Pr 290.4; Maombi Aya ya 6]

Ulimwengu ambao Shetani amedai kuuchukua na kuwa wake na kisha kuutawala kwa jeuri yenye ukatili, Mwana wa MUNGU, kwa ushindi mmoja mkubwa, ameuzingira katika upendo Wake na kuunganisha tena pamoja na kiti cha ufalme cha Yehova. Makerubi na maserafi, na majeshi yasiyohesabika ya ulimwengu (universe) wote usioanguka, waliimba nyimbo za sifa kwa MUNGU na Mwana-Kondoo wakati ushindi huu ulipohakikishiwa. Walifurahi kwamba njia ya wokovu ilikuwa imefunguliwa kwa jamii iliyoanguka na kwamba dunia ingekombolewa kutoka katika laana ya dhambi. Je! ni shangwe ya ajabu kiasi gani basi, inapaswa kuwabubujikia wale ambao ndio walengwa wa upendo huo wa ajabu! [Pr 290.5; Maombi Aya ya 7]

Je, tunawezaje basi kuwa katika mashaka na kutokuwa na uhakika, na kuhisi kwamba sisi ni yatima? Ilikuwa ni kwa niaba ya wale ambao walikuwa wameivunja sheria ndipo Yesu akachukua juu Yake asili ya ubinadamu; Akawa kama sisi, ili tuwe na amani ya milele na uhakikisho. Tunae Wakili mbinguni, na yeyote anayemkubali kama Mwokozi wake binafsi haachiwi kamwe kama yatima kubeba mzigo wa dhambi zake mwenyewe. [Pr 291.1; Maombi Aya ya 8]

"Wapenzi, sasa tu wana wa MUNGU." "Na ikiwa ni watoto, basi tu warithi;

warithi wa MUNGU, warithio pamoja na Kristo; ikiwa tukiteswa pamoja naye, ili tupate kutukuzwa pamoja naye." "Bado haijadhihirika tutakavyokuwa; lakini twajua ya kuwa atakapodhihirishwa tutafanana naye; kwa maana tutamwona jinsi alivyo." 1 Yohana 3:2; Warumi 8:17. [Pr 291.2; Maombi Aya ya 9]

Hatua ya kwanza kabisa ya kumkaribia MUNGU ni kujua na kuamini upendo alionao kwetu (1 Yohana 4:16); kwa maana ni kupitia kuvutiwa na upendo Wake ndipo tunapoongozwa kwenda Kwake. [Pr 291.3; Maombi Aya ya 10]

Kuusikia, kuhuhisi na kuuishi upendo wa MUNGU hufanya kazi katika kuukana ubinafsi. Katika kumwita MUNGU Baba yetu, tunawatambua watoto Wake wote kama ndugu zetu. Sisi sote ni sehemu ya mtandao mkuu wa ubinadamu, sote ni washiriki wa familia moja. Katika maombi yetu tunapaswa kujumuisha majirani zetu na sisi wenyewe. Hakuna anayeomba kwa usahihi ambaye anatafuta baraka kwa ajili yake peke yake. [Pr 291.4; Maombi Aya ya 11]

MUNGU wa milele yaani Yeye Yule Asiye na kikomo, alisema Yesu ameifanya iwe fursa kwetu sisi, kumwita Yeye kwa Jina la Baba. Elewa yote ambayo hii inamaanisha. Hakuna mzazi wa duniani aliyewahi kusihi kwa ajili ya mtoto Wake mwenye makosa kwa bidii kama Yeye Alituumba anavyotukaribisha na anavyosihi kwa ajili ya sisi wapotovu. Hakuna maslahi ya upendo wa kibinadamu yaliyowahi kuwafuata wasiotubu kwa mialiko hiyo ya huruma. MUNGU anakaa katika kila makazi; Yeye husikia kila neno linalonenwa, husikiliza kila ombi linalotolewa, huonja huzuni na kukatishwa tamaa kwa kila nafsi, huangalia jinsi anavyotendewa baba, mama, dada, rafiki na jirani. Anajali mahitaji yetu, na upendo Wake na rehema na neema vinaendelea kumiminika daima ili kutosheleza hitaji letu. [Pr 291.5; Maombi Aya ya 12]

Lakini mkimwita MUNGU Baba yenu mwaafikiana kuwa ninyi ni watoto Wake, na mu tayari kuongozwa na hekima Yake na kuwa watiifu katika mambo yote, mkijua kwamba upendo Wake haubadiliki. Mtakubaliana na mpango Wake kwa ajili ya maisha yenu. Kama watoto wa MUNGU, mtaishikilia hadhi Yake, heshima Yake, tabia Yake, familia Yake, kazi Yake, kama mambo ya shauku yenu ya juu zaidi. Itakuwa furaha yenu kutambua na kuheshimu uhusiano wenu na Baba yenu na kwa kila mwanafamilia Yake. Mtafurahi kufanya tendo lolote, hata liwe la unyenyekevu kwa kiasi gani, litakalopelekea kuleta utukufu Wake Mungu au ustawi wa ndugu zetu au udugu wetu (binadamu sote). [Pr 292.1; Maombi Aya ya 13]

"Uliyeko juu mbinguni." Yeye ambaye Kristo anatubidisha tumtazame kama "Baba yetu" "Yuko mbinguni: Yeye amefanya yale yote yanayompendeza." Katika utunzami na ulinzi Wake tunaweza kupumzika kwa usalama, tukisema, "Wakati ninaoogopa, nitakutumaini Wewe." Zaburi 115:3; Zaburi 56:3. [Pr 292.2; Maombi Aya ya 14]

"Jina lako litukuzwe." Mathayo 6:9.

Kulitukuza Jina la Bwana kunahitaji kwamba maneno ambayo tunazungumza juu ya Aliye Mkuu Zaidi yatamkwe kwa heshima. “Jina lake ni takatifu na lenye kuheshimiwa.” Zaburi 111:9. kamwe hatupo katina nafasi ya kuchukulia kwa wepesi vyeo au majina ya Uungu. Katika maombi tunaingia kwenye chumba cha kuonana na Aliye Juu; nasi tunapaswa kwenda mbele zake kwa kicho kitakatifu. Malaika hufunika nyuso zao mbele yake. Makerubi na maserafi angavu na watakatifu wanakaribia kiti Chake cha enzi kwa heshima kuu. Je! ni zaidi kiasi gani kwetu sisi, viumbe wenye kikomo, wenye dhambi, tunapaswa kwenda kwa njia ya uchaji mbele za Bwana, Muumba wetu! [Pr 292.3; Maombi Aya ya 15]

Lakini kulitakasa Jina la Bwana kunamaanisha mengi zaidi ya haya. Tunaweza, kama Wayahudi wa siku za Kristo, tukadhihirisha heshima kubwa zaidi ya nje kwa MUNGU, na bado tunachafua jina Lake sikuzote. “Jina la Bwana” ni “mwenye huruma na neema, mvumilivu, na mwingi wa fadhili na kweli, ... mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi.” Kutoka 34:5-7. Imeandikwa hivi kuhusu kanisa la Kristo: “Na mji huo utaitwa ‘Mwenyezi-MUNGU ni Ukombozi Wetu’.” Yeremia 33:16. Jina hili limewekwa kwa kila mfuasi wa Kristo. Ni urithi wa mtoto wa MUNGU. Familia inaitwa kwa jina la Baba. Nabii Yeremia, katika wakati wa taabu na dhiki kuu za Israeli, aliomba, “Tumeitwa kwa jina lako; usituache.” Yeremia 14:9. [Pr 292.3; Maombi Aya ya 16]

Jina hili linatukuzwa na kusujudiwa na malaika wa mbinguni, na wakazi malimwengu yasiyoanguka. Unapoomba, “Jina lako litukuzwe,” unapoomba kwamba litukuzwe katika ulimwengu huu, litukuzwe ndani yako. Mwenyezi MUNGU amekukiri wewe mbele za watu na Malaika kwamba u mtoto Wake; ombea ili usilikufuru na kuvunja heshima kwa “Jina lile jema tuliloitiwa.” Yakobo 2:7. MUNGU anakutuma ulimwenguni kama mwakilishi Wake. Katika kila tendo la maisha unatakiwa kudhihirisha Jina la MUNGU. Ombi hili linakutaka tumiliki tabia Yake. Hatuwezi tukalitukuza Jina Lake, hatuwezi kumwakilisha kwenye ulimwengu, isipokuwa katika maisha na tabia tnawakilisha maisha na tabia ile ile ya MUNGU (tabia Yake Mwenyewe). Hili unaweza kufanya tu kwa kukubali neema na haki ya Kristo. [Pr 293.1; Maombi Aya ya 17]

“Ufalme wako uje.” Mathayo 6:10.

MUNGU ni Baba yetu, anayetupenda na kutujali kama watoto Wake; Yeye pia Ndiye Mfalme mkuu wa malimwengu yote. Maslahi ya ufalme Wake ni masilahi yetu, na tunapaswa kufanya kazi kwa ajili ya kuujenga huo ufalme. [Pr 293.2; Maombi Aya ya 18]

Wanafunzi wa Kristo walikuwa wanatazamia ujio wa haraka wa ufalme Wake wa utukufu, lakini katika kuwapa ombi hili Yesu alifundisha kwamba ufalme usingesimikwa wakati huo. Walipaswa kuombea ujio Wa Ufalme huo kama tukio la wakati ujao. Lakini ombi hili pia lilikuwa uhakikisho kwao. Japo wasingeweza

kuuona ujio wa ufalme huo katika siku zao, uhakika wa kwamba Yesu aliwaambia wauombee ni uthibitisho kwamba katika wakati aliouweka MUNGU Mwenyewe, hakika utakuja. [Pr 293.2; Maombi Aya ya 19]

Ufalme wa neema ya MUNGU sasa unasimikwa, siku baada ya siku mioyo ambayo imejaa dhambi na uasi inajitoa na kujisalimisha kwenye ukuu wa upendo Wake. Lakini kusimamishwa kikamilifu kwa ufalme wa utukufu Wake hakutafanyika mpaka ujio wa pili wa Kristo katika ulimwengu huu. "Ufalme, utawala na ukuu wa falme zote duniani" watapewa "watu wa watakatifu wa MUNGU Mkuu." Danieli 7:27. Wataurithi ufalme uliotayarishwa kwa ajili yao "tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu." Mathayo 25:34. Naye Kristo atajitwalia uweza Wake mkuu na kutawala. [Pr 293.3; Maombi Aya ya 20]

Malango ya mbinguni yatainuliwa tena, na pamoja na elfu kumi mara elfu kumi na maelfu ya maelfu ya watakatifu, Mwokozi wetu atakuja kama Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana. Yehova Imanueli "atakuwa Ndiye mfalme pekee wa dunia yote; Naye atakuwa Ndiye Mwenyezi-MUNGU pekee, Mmoja tu, na Jina Lake litakuwa ndilo Jina pekee." "Maskani ya MUNGU" Itakuwa pamoja na wanadamu, "Naye atakaa pamoja nao, nao watakuwa watu Wake, na MUNGU Mwenyewe atakuwa pamoja nao, na atakuwa MUNGU wao." Zekaria 14:9; Ufunuo 21:3 [Pr 294.1; Maombi Aya ya 21]

Lakini kabla ya kuja huko, Yesu alisema, "Injili hii ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote kuwa ushuhuda kwa mataifa yote." Mathayo 24:14. Ufalme Wake hautakuja mpaka habari njema ya neema Yake ifikishwe duniani kote. Kwa hiyo, tunapojitoa kwa MUNGU, na kuleta nafsi nyingine kwake, tunaharakisha ujio wa ufalme Wake. Ni wale tu wanaojitoa kwa ajili ya utumishi Wake, wakisema, "Mimi hapa; nitume" (Isaya 6:8), kufungua macho ya vipofu, kuwaongoa watu "kutoka gizani hadi kwenye nuru na kutoka katika nguvu za Shetani na kumwelekea MUNGU, ili wapate ondoleo la dhambi na urithi miongoni mwao waliotakaswa" (Matendo 26:18)—wao pekee wanaomba kwa uaminifu, "Ufalme wako uje." [Pr 294.2; Maombi Aya ya 22]

"Mapenzi yako yafanyike duniani kama huko mbinguni." Mathayo 6:10.

Mapenzi ya MUNGU yanaonyeshwa katika kanuni za sheria Yake takatifu, na kanuni za sheria hii ni kanuni za mbinguni. Malaika wa mbinguni hawapati ujuzi wa juu zaidi kuliko ule wa kuyajua mapenzi ya MUNGU, na kuyafanya mapenzi Yake ndiyo huduma ya juu zaidi kabisa ambayo wao wanaweza kuzihusisha nguvu zao. (Mapenzi ya Mungu ndiyo sheria Yake na sheria Yake ndiyo Mapenzi Yake, malaika wao hawataki kujua chochote isipokuwa yale yaliyokuwa kwenye duru ya mapenzi ya Mungu tu-hawataki uovu kwa ufupi!) [Pr 294.3; Maombi Aya ya 23]

Lakini mbinguni, huduma haitolewi katika roho ya kisheria. Shetani alipoasi

sheria ya Yehova, wazo la kwamba kulikuwa na sheria lilikuja kwa malaika kama ufahamu wa wazo ambalo wao hawakuwa kulifikiria. Katika huduma yao malaika si kama watumishi, bali kama wana. Kuna umoja kamili kati yao na Muumba wao. Utii kwao sio jukumu au kongwa zito. Upendo wao kwa MUNGU hufanya utumishi wao uwe wenye shangwe yaani wa kushangilia. Kwa hiyo katika kila nafsi ambayo iko ndani ya Kristo, tumaini la utukufu, hutamalaki, Maneno Yake hurudiwa kama mwangwi tena na tena, “Kuyafanya mapenzi Yako, Ee MUNGU wangu, ndiyo furaha yangu; Naam, sheria Yako imo moyoni mwangu..” Zaburi 40:8. [Pr 294.4; Maombi Aya ya 24]

Ombi, “Mapenzi yako yatimizwe duniani kama huko mbinguni,” ni sala ya kusihi kwamba utawala wa uovu humu duniani uweze kukomeshwa, ili dhambi iteketezwe milele, na ufalme wa haki usimamishwe. Kisha duniani kama vile ilivyo mbinguni, patasheheni “raha yote ya wema Wake.” 2 Wathesalonike 1:11. [Pr 295.1; Maombi Aya ya 25]

"Utupe leo mkate wetu wa kila siku." Mathayo 6:11.

Nusu ya kwanza ya ombi ambalo Yesu ametufundisha inahusu jina na ufalme na mapenzi ya MUNGU—ili Jina Lake liheshimiwe, ufalme Wake usimikwe, na mapenzi Yake yatimizwe. Unapofanya utumishi wa MUNGU kuwa jambo kipaumbele cha Kwanza kwako, unaweza kuomba kwa uhakika na ujasiri kwamba mahitaji yako mwenyewe yaweze kutimizwa. Ikiwa umejinyima na kuikana na nafsi yako na kujitoa kwa Kristo, wewe ni mwanachama wa familia ya MUNGU, na kila kitu ndani ya nyumba ya Baba ni kwa ajili yako. Hazina zote za MUNGU zimefunguliwa kwako, yaani za ulimwengu uliopo sasa na ule ujao. Huduma ya malaika, karama ya Roho Wake, kazi ya watumishi Wake—zote zipo hapo kwaajili yako. Dunia, yenye kila kitu ndani yake, ni yako kwa kadiri inavyoweza kukutendea wema/fadhila. Hata uadui wa waovu utathibitika kuwa baraka kwa kukunidhamisha kwa ajili ya mbingu. Ikiwa “ninyi ni wa Kristo,” “vitu vyote ni vyenu.” 1 Wakorintho 3:23, 21. [Pr 295.2; Maombi Aya ya 26]

Lakini wewe ni kama mtoto ambaye bado hajawekwa kuutawala/kuudhibiti urithi wake. MUNGU hakukabidhi mali yako ya thamani, Shetani asije akakudanganya kwa ujanja wake, kama alivyowafanyia ile jozi ya watu wa kwanza kule Edeni. Kristo anashikilia urithi kwa ajili yako kwa usalama ili usifikiwe na mharibifu. Kama mtoto, utapokea siku baada ya siku kile kinachokidhi mahitaji lyako ya kila siku. Kila siku unatakiwa kuomba, “Utupe leo mkate wetu wa kila siku.” Usifadhaike ikiwa hauna vya kutosha kwa ajili ya kesho. Una uhakika wa ahadi Yake, “Basi mtakaa katika ardhi, na hakika mtalishwa.” Daudi anasema, “Nalikuwa kijana nami sasa ni mzee; lakini sijamwona mwenye haki ameachwa, wala watoto wake wakiombaomba chakula. Zaburi 37:3, 25. Yule MUNGU aliyetuma kunguru kumlisha Eliya karibu na kijito Kerithi hatampita mmoja wa watoto Wake mwaminifu na wenye kujitoa. Imeandikwa hivi kuhusu

yeye aendaye kwa haki: “Mkate atapewa; maji yake yatadumu.” “Hawataaibishwa wakati wa uovu; na siku za njaa watashiba. “Yeye hakumhurumia Mwanawe, bali alimtoa kwa ajili yetu sote, atakosaje basi kutupatia vitu vyote kwa ukarimu pamoja Naye?” Isaya 33:16; Zaburi 37:19; Warumi 8:32. Yeye ambaye alipunguza mizigo na mahangaiko ya mama Yake mjane na kumsaidia kwa kuleta riziki nyumbani kule Nazareti, anamhurumia kila mama katika jitihada zake za kuwaandalia watoto wake chakula. Yeye ambaye alikuwa na huruma kwa umati kwa sababu “walichoka na kutawanyika” (Mathayo 9:36), bado ana huruma kwa maskini wanaoteseka. Mkono Wake umenyooshwa kuelekea kwao katika kubariki; na katika ombi lile lile alilowapa wanafunzi Wake, anatufundisha kuwakumbuka maskini. [Pr 295.3; Maombi Aya ya 27]

Tunapoomba, “Utupe leo mkate wetu wa kila siku,” tunaomba kwa ajili ya wengine na sisi wenyewe pia. Na tunakubali kwamba kile ambacho MUNGU anatupa si kwa ajili yetu wenyewe. MUNGU hutukabidhi sisi kama amana, ili tuwalishe wenye njaa. Kwa wema Yeye Wake amewaandalia maskini. Zaburi 68:10. Naye anasema, “Ufanyapo chakula cha usiku au cha jioni, usiwaite rafiki zako, wala ndugu zako, wala jamaa zako, wala jirani zako matajiri.....Bali ufanyapo karamu, waite maskini, na vilema, viwete, vipofu, nawe utabarikiwa; kwa maana wao hawana cha kukulipa; kwa maana utalipwa katika ufufuo wa wenye haki.” Luka 14:12-14. [Pr 296.1; Maombi Aya ya 28]

“MUNGU aweza kuwajaza kila neema kwa wingi; ili ninyi, mkiwa na riziki za kila namna siku zote, mpate kuzidi sana katika kila tendo jema.” “Apandaye haba atavuna haba; na apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu.” 2 Wakorintho 9:8, 6. [Pr 296.2; Maombi Aya ya 29]

Ombi la mkate wa kila siku halijumuishi tu chakula cha kutegemeza mwili, bali mkate wa kiroho ambao utailisha roho hata uzima wa milele. Yesu anatuagiza, “Msikifanyie kazi chakula chenye kuharibika, bali kile kidumucho hata uzima wa milele.” Yohana 6:27. Anasema, “ Mimi ni Mkate wa Uzima uliotoka mbinguni. Mtu ye yote akiula mkate huu ataishi milele. Kifungu cha 51. [Pr 297.1; Maombi Aya ya 30]

Mwokozi wetu Ndiye mkate wa uzima, na ni kwa kuutazama upendo Wake, kwa kuupokea ndani ya roho, ndipo tunakuwa tukila mkate ulioshuka kutoka mbinguni. [Pr 297.2; Maombi Aya ya 31]

Tunampokea Kristo kupitia kwenye Neno Lake, na Roho Mtakatifu anatolewa ili kufungua Neno la MUNGU katika ufahamu wetu, na kuleta kwetu ile Kweli Yake kwenye mioyo yetu. Tunapaswa kuomba siku baada ya siku kwamba tunaposoma Neno Lake, MUNGU atume Roho Wake ili kutufunulia Ukweli ambao utaimarisha roho zetu kwa mahitaji ya siku hiyo. [Pr 297.3; Maombi Aya ya 32]

Katika kutufundisha kuomba kila siku kile tunachohitaji— baraka za kimwili za muda mfupi na zile za kiroho—MUNGU ana kusudi la kutimiza kile ambacho ni

kwa manufaa yetu wenyewe. Anatutaka tutambue kutegemea kwetu daima ulinzi Wake, kwa kuwa anatafuta kutuvuta katika ushirika Naye Mwenyewe. Katika ushirika huu na Kristo, kwa njia ya maombi na kujifunza zile Kweli kuu na za thamani za Neno Ilke, kama roho zenye njaa tutalishwa; kama wale walio na kiu, tutaburudishwa kwenye chemchemi ya uzima. [Pr 297.4; Maombi Aya ya 33]

“Utusamehe dhambi zetu kwa kuwa na sisi tunawasamehe wote wanaotukosea.” Luka 11:4.

Yesu anafundisha kwamba tunaweza kupokea msamaha kutoka kwa MUNGU pale tu tunapowasamehe wengine. Upendo wa MUNGU ndio unaotuvuta Kwake, na upendo huo hauwezi kugusa mioyo yetu bila kuumba upendo kwa ndugu zetu. [Pr 297.5; Maombi Aya ya 34]

Baada ya kumaliza Sala ya Bwana, Yesu aliongeza hivi: “Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi. Bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu. Yeye asiyesamehe hukata njia ambayo kwayo pekee anaweza kupokea rehema kutoka kwa MUNGU. Hatuna haki kufikiri kwamba wale ambao wametuumiza wasipokiri kosa lao kwetu basi sisi tuna haki ya kuwanyima msamaha wetu. Hakika na bila shaka, ni sehemu yao kunyenyekeza mioyo yao kwa toba na maungamo; lakini tunapaswa kuwa na roho ya huruma kwa wale ambao wametukosea, endapo wanakiri makosa yao au la. Haijalishi wametujeruhi vibaya kiasi gani, hatupaswi kuthamini kutotendewa haki kwetu na kujihurumia wenyewe kuhusiana na majeraha yetu; lakini kama tunavyotarajia kusamehewa makosa yetu dhidi ya MUNGU tunapaswa kuwasamehe wote wale waliotutendea sisi uovu. [Pr 297.6; Maombi Aya ya 35]

Lakini msamaha una maana pana kuliko wengi wanavyodhani. MUNGU anapotoa ahadi kwamba “atasamehe kabisa,” anaongeza, kana kwamba maana ya ahadi hiyo inapita yote tunayoweza kuelewa kwa utashi wetu: “Mawazo Yangu si kama mawazo yenu, wala njia zenu si kama njia Zangu, asema Bwana. Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia Zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo Yangu kuliko mawazo yenu.” Isaya 55:7-9. Msamaha wa MUNGU si tu tendo la haki ambalo kwalo Yeye hutuweka huru dhidi ya hukumu. Sio tu msamaha wa dhambi, bali ni ukombozi kutoka katika dhambi. Ni ububujikaji wa upendo unaokomboa, unaogeza moyo. Daudi alikuwa na dhana ya Kweli ya msamaha alipoomba, “Uniumbie moyo safi, ee MUNGU, uweke ndani yangu roho mpya na thabiti.” Zaburi 51:10. Na tena anasema, “Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi.” Zaburi 103:12. [Pr 298.1; Maombi Aya ya 36]

MUNGU katika Kristo alijitoa kwa ajili ya dhambi zetu. Aliteseka kwa kifo cha kikatili cha msalabani, alitubebea mzigo wa hatia, “wenye haki kwa wasio haki,” ili aweze kutufunulia upendo Wake na kutuvuta Kwake. Naye anasema, “Iweni

wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na MUNGU katika Kristo alivyowasamehe ninyi. Waefeso 4:32, Hebu Kristo, Aliye maisha matakatifu, akae ndani yako na kupitia kwako adhihirishe upendo uliozaliwa mbinguni ambao utahuisha tumaini kwa wasio na tumaini na kuleta amani ya mbinguni kwenye moyo uliosumbuliwa na kupipigwa-pigwa na dhambi. Tunapomwendea MUNGU, hili ndilo sharti tunalokutana nalo kwenye kizingiti, kwamba, tukipokea rehema kutoka Kwake, basi nasi tunajitoa ili kudhihirisha neema Yake kwa wengine. [Pr 298.2; Maombi Aya ya 37]

Jambo moja la muhimu kwetu ili tuweze kupokea na kutoa kwa wengine upendo huu wa Mungu wa kusamehe, ni kuujuu na kuuamini upendo Yeye alionao kwetu. 1 Yohana 4:16. Shetani anafanya kazi kwa kila udanganyifu anaoweza kuuamuru, ili tusiweze kuutambua upendo huo. Atatuongoza kufikiri kwamba makosa na maovu yetu yamekuwa ya kutisha na kuhuzunisha sana kiasi kwamba Bwana hataheshimu maombi yetu na hatatubariki na kutuokoa. Ndani yetu wenyewe hatuwezi kuona chochote ila udhaifu, hakuna kitu cha kutupatia haki mbele za MUNGU (hatuna CV ya kufaa), na Shetani anatuambia haisaidii kitu, kwani hatuwezi kurekebisha kasoro zetu za tabia. Tunapojaribu kumwendea MUNGU, adui atanong'ona kwetu, Haifai kitu kwako kuomba; Je, haukufanya ubaya huo kweli? Je! haujamtenda MUNGU dhambi na kukiuka dhamiri yako mwenyewe? Lakini tunaweza kumwambia adui kwamba “damu ya Yesu Kristo Mwanawe inatutakasa dhambi zote.” 1 Yohana 1:7. Tunapohisi kwamba tumetenda dhambi na hivyo hatuwezi kuomba, basi huo ni wakati wa kuomba haswa. Tunaweza kuona aibu usoni na kuona tumenyenyekezwa sana, lakini lazima tuombe na kuamini. “Neno hili ni la kuaminiwa, tena lastahili kukubalika kabisa, ya kwamba Kristo Yesu alikuja ulimwenguni kuwaokoa wenye dhambi; ambao mimi ni mkuu wao.” 1 Timotheo 1:15. Msamaha, upatanisho na MUNGU, huja kwetu, si kama haki au thawabu kwaaajili ya matendo yetu, hautolewi kwa sababu ya wema wa sifa yetu au haki yetu sisi wenye dhambi, bali ni zawadi kwetu, iliyokita kwenye msingi wa utoaji kutoka katika ile Haki isiyo na mawaa ya Kristo. [Pr 298.3; Maombi Aya ya 38]

Hatupaswi kujaribu kupunguza hatia yetu kwa kutolea udhuru dhambi. Ni lazima tukubali makadirio ya MUNGU ya dhambi (jinsi anavyoipima), nayo ni mazito kweli kweli. Kalvari pekee yake, ndiyo inaweza kudhihirisha ukubwa wa kuogofya wa dhambi. Kama ingebidi tuibebe hatia yetu wenyewe, basi ingetusagasaga kabisa. Lakini Yule asiye na dhambi amechukua mahali petu; Japokuwa hastahili, amebeba maovu yetu. “Tukiziungama dhambi zetu,” MUNGU “ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.” 1 Yohana 1:9. Kweli tukufu!— Mwenye haki na Mwaminifu juu ya sheria Yake Mwenyewe, na bado ni Mwenye kuwahesabia haki wote wanaomwamini Yesu. “Ee MUNGU, ni nani aliye kama Wewe? Wewe wasamehe dhambi za watu wako waliobaki, wala huyaangalii makosa yao. Hasira Yako

haidumu milele, ila wapendelea zaidi kutuonesha fadhili Zako.” Mika 7:18. [Pr 299.1; Maombi Aya ya 39]

"Usitutie majaribuni, bali utuokoe na yule mwovu." Mathayo 6:13, R.V.

Majaribu ni ushawishi wa kutenda dhambi, na huu hautoki kwa MUNGU, bali kwa Shetani na kutoka kwenye uovu wa mioyo yetu wenyewe. "MUNGU hawezi kujaribiwa na maovu, wala Yeye Mwenyewe hamjaribu mtu." Yakobo 1:13 R.V. [Pr 300.1; Maombi Aya ya 40]

Shetani anatafuta kutuingiza katika majaribu, ili ubaya wa tabia zetu udhihirishwe mbele ya wanadamu na malaika, ili apate kudai na kutuchukua kama wake. Katika unabii wa ishara wa Zekaria, Shetani anaonekana amesimama mkono wa kuume wa Malaika wa Bwana, akimshtaki Yoshua, kuhani mkuu, ambaye amevaa mavazi machafu, na akipinga kazi ambayo Malaika anatamani kumfanyia. Hii inawakilisha mtazamo wa Shetani kwa kila nafsi ambayo Kristo anatafuta kuivuta Kwake. Adui hutuongoza katika dhambi, na kisha anatushtaki mbele ya anga la mbinguni kuwa hatustahili upendo wa MUNGU (hatustahili kupendwa na Mungu). Lakini "Mwenyezi-MUNGU na akulaani, ewe Shetani! Naam, Mwenyezi-MUNGU aliyeuteua mji wa Yerusalemu na akulaani! Je! hiki si kama kinga kilichonyakuliwa kutoka motoni?" Naye akamwambia Yoshua, Tazama, nimekuondolea uovu wako, Nami nitakuvika mavazi ya thamani; Zekaria 3:1-4. [Pr 300.2; Maombi Aya ya 41]

MUNGU katika upendo Wake mkuu anatafuta kukuza ndani yetu neema za thamani za Roho Wake. Anaturuhusu tukabiliane na vikwazo, mateso, na magumu, si kama laana, bali kama baraka kuu zaidi maishani mwetu. Kila jaribu linalopingwa, kila mtihani unaobebwa kwa ujasiri, hutupatia uzoefu mpya na hutukuza katika kazi ya kujenga tabia. Nafsi ambayo kwa uwezo wa Bwana inapinga majaribu inaudhihirishia ulimwengu na anga la mbinguni ufanisi wa neema ya Kristo. [Pr 300.3; Maombi Aya ya 42]

Lakini huku tukiwa hatupaswi kufadhaishwa na majaribu, hata yawe na uchungu wa kiasi gani, sisi tunapaswa kuomba ili MUNGU asituruhusu tupelekwe mahali ambapo tutavutwa mbali na tamaa za mioyo yetu wenyewe yenye uovu. Katika kutoa ombi ambalo Kristo ametupatia, tunajisalimisha katika uongozi wa MUNGU, tukimwomba atuongoze katika njia salama. Hatuwezi kutoa ombi hili kwa dhati, na bado tukaamua kutembea katika njia yoyote tunayoichagua sisi wenyewe. Tutasubiri mkono Wake utuongoze; tutaikiliza sauti Yake, ikisema, "Njia ni hii, ifuateni." Isaya 30:21. [Pr 300.4; Maombi Aya ya 43]

Si salama kwetu kujikawiza kwa kutafakari manufaa tunayoweza kujichumia kwa kukubali madokezo ya Shetani. Dhambi maana yake ni fedheha na balaa kwa kila nafsi inayojiendekeza nayo; lakini inapofusha na inadanganya katika asili yake, na itatuvutia kwa maonyesho ya kubembebeza na udanganyifu. Ikiwa

tutajitosa kwenye ardhi ya Shetani hatuna uhakika wa kulindwa dhidi ya uwezo wake. Kwa kadiri ilivyo ndani yetu, tunapaswa kufunga kila njia ambayo kwayo mjaribu yanaweza kupata mpenyo wa kutufikia. [Pr 300.5; Maombi Aya ya 44]

Ombi kwamba, “Usitutie majaribuni,” lenyewe ni ahadi. Tukijikabidhi kwa MUNGU tuna uhakika, Yeye “hataruhusu tujaribiwe kupita nguvu zenu, ila pamoja na majaribu, Yeye atawapeni pia nguvu ya kustahimili na njia ya kutoka humo salama.” 1 Wakorintho 10:13. [Pr 301.1; Maombi Aya ya 45]

Kinga pekee dhidi ya uovu ni kutamalaki kwa Kristo ndani ya moyo kupitia imani katika haki yake. Ni kwa sababu ubinafsi upo ndani ya mioyo yetu ndiyo maana majaribu yana nguvu juu yetu. Lakini tunapouona upendo mkuu wa MUNGU, ubinafsi unaonekana kwetu katika tabia yake kutisha na ya kuchukiza, na tunatamani ufukuzwe kutoka katika nafsi. Roho Mtakatifu anapomtukuza Kristo, mioyo yetu inalainika na kutiishwa, majaribu yanapoteza nguvu zake, na neema ya Kristo inabadilisha tabia. [Pr 301.2; Maombi Aya ya 46]

Kristo hataiacha kamwe nafsi ambayo Yeye ameifia. Nafsi inaweza kumwacha Yeye na kulemewa na majaribu, lakini Kristo hawezi kamwe kugeuka na kumwacha yule mtu ambaye amemlipia gharama ya maisha Yake Mwenyewe. Ikiwa maono yetu ya kiroho yangeweza kuhuishwa, tungeweza kuziona nafsi zilizoinama chini ya ukandamizaji na kulemewa na mizigo ya huzuni, zikisukumwa kama mkokoteni chini ya miganda na tayari kufa kwa kuvunjika moyo. Tunapaswa kuona malaika wakiruka kwa upesi ili kuwasaidia hawa waliojaribiwa, ambao wamesimama kama ukingoni mwa kilele cha mwamba. Malaika kutoka mbinguni huyarudisha nyuma majeshi ya mwovu ambayo yanazingira roho hizi, na kuziongoza kusimika miguu yao juu ya msingi thabiti na wenye hakika. Vita vinavyopiganwa kati ya majeshi hayo mawili ni halisi sawa na vile vinavyopiganwa na majeshi ya ulimwengu huu, na kuhusu suala la mzozo huu wa kiroho, hatima za milele zimejiegemeza huko. [Pr 301.3; Maombi Aya ya 47]

Kwetu sisi, kama kwa Petro, Neno hili linazungumzwa, “Shetani ameomba ili awapepete kama ngano; lakini nimekuombea wewe ili imani yako isipotee. Luka 22:31, 32. Namshukuru MUNGU, hatujaachwa peke yetu. Yeye ambaye “aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele” (Yohana 3:16), hatatuacha katika vita vya adui wa MUNGU na wanadamu. Naye Anasema, “Tazama, nimewapa uwezo wa kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakachowadhuru. Luka 10:19. [Pr 301.4; Maombi Aya ya 48]

Ishi kwa kuwasiliana pamoja na Kristo aliye hai, Naye atakushikilia kwa nguvu kwa mkono ambao hautaweza kukuacha kamwe. tambueni na kuamini upendo Mungu alio nao kwetu, nanyi mmekuwa salama; kwamba upendo ni ngome isiyoweza kushindwa au kupenyeka na udanganyifu na mashambulizi yote ya

Shetani. "Jina la Bwana ni ngome imara; Mwenye haki hulikimbilia, akawa salama." Mithali 18:10. [Pr 302.1; Maombi Aya ya 49]

"Ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu." Mathayo 6:13.

Sentensi ya mwisho kama sentensi ya kwanza ya Sala ya Bwana, inaelekeza kwa Baba yetu kama aliye juu ya nguvu zote na mamlaka na kila jina linalotajwa. Mwokozi aliona miaka iliyokuwa inakuja mbele ya wanafunzi Wake, kwamba haikuwa kama walivyoiotea, wakiwa wamelala kwenye mwanga wa jua wa mafanikio na heshima ya ulimwengu, bali katika giza na tufani za chuki ya kibinadamu na ghadhabu ya shetani. Katikati ya vita na uharibifu wa kitaifa, hatua za wanafunzi zilisongwa na hatari, na mara nyingi mioyo yao ilikandamizwa na woga. Wangeiona Yerusalemu ikiwa ukiwa, hekalu likifagiliwa mbali, ibada yake ikikoma milele, na Israeli ikitawanywa katika nchi zote, kama mabaki kwenye ufuo wa jangwa. Yesu alisema, "Mtasikia habari za vita na tetesi za vita. "Taifa litaondoka kupigana na taifa, na ufalme kupigana na ufalme; kutakuwa na njaa, na tauni, na matetemeko ya ardhi sehemu mbalimbali. Yote hayo ndiyo mwanzo wa uchungu." Mathayo 24:6-8. Hata hivyo, wafuasi wa Kristo hawakupaswa kuogopa kwamba tumaini lao limepotea au kwamba MUNGU alikuwa ameitelekeza dunia. Nguvu na utukufu ni Vyake Yeye ambaye makusudi Yake makuu yangeendelea bila kuzuiliwa kuelekea utimilifu wake. Katika sala inayotoa pumzi ya matakwa yao ya kila siku, wanafunzi wa Kristo walielekezwa kupeleka nguvu zote juu ya mambo yote ya utawala wa uovu, kwa Bwana MUNGU wao, ambaye ufalme Wake unatawala juu ya yote na ambaye ni Baba yao na Rafiki wa milele. [Pr 302.2; Maombi Aya ya 50]

Kuangamia kwa Yerusalemu ilikuwa ishara ya uharibifu wa mwisho ambao ungeufadhaisha ulimwengu. Unabii uliotimizwa kiasi fulani katika kupinduliwa kwa Yerusalemu unahusiana moja kwa moja na mambo ya siku za mwisho. Sasa tumesimama kwenye mlango wa matukio makubwa na mazito. Mgogoro tete ulio mbele yetu ambao ulimwengu haujawahi kushuhudia uko mbele yetu. Habari njema kwetu, kama kwa wanafunzi wa kwanza, unakuja uhakikisho kwamba ufalme wa MUNGU unatawala juu ya yote. Mpango wa matukio yanayokuja uko mikononi mwa Muumba wetu. Mkuu wa mbinguni Ana hatima ya mataifa, pamoja na maslahi ya kanisa Lake, chini ya uwezo Wake Mwenyewe. Mwalimu wa Kiungu anamwambia kila wakala katika utimilifu wa mipango Yake, kama vile alivyomwambia Koreshi, "Nilikutia nguvu, ingawa haukunijua." Isaya 45:5. [Pr 303.1; Maombi Aya ya 51]

Katika maono ya nabii Ezeieli kulikuwa na kuonekana kwa mkono chini ya mabawa ya makerubi. Hii ni kuwafundisha waja Wake kwamba ni uweza wa Mungu ndio unaowapa mafanikio. Wale ambao MUNGU huwaajiri kama wajumbe Wake wasihisi kwamba kazi Yake inawategemea wao. Viumbe wenye ukomo hawakuachwa kubeba mzigo huu wa wajibu. Yeye asiyesinzia, ambaye daima

anafanya kazi kwa ajili ya kutimiza makusudi Yake, ataendeleza kazi Yake Mwenyewe. Bali makusudi ya watu waovu huyasukumilia mbali, na kuyavuruga/kuyakanganyisha mashauri ya wale wanaopanga mabaya juu ya watu Wake. Yeye aliye Mfalme, Bwana wa majeshi, aketiye juu ya makerubi, na katikati ya migogoro na ghasia za mataifa huwalinda watoto Wake. Yeye Anayetawala mbinguni ni Mwokozi wetu. Yeye hupima kila jaribu, hulinda moto wa tanuru ambao lazima ujaribu kila nafsi. Ngome za wafalme zitakapopinduliwa, mishale ya hasira itakapoingia mioyoni mwa adui Zake, watu Wake watakuwa salama mikononi Mwake. [Pr 303.2; Maombi Aya ya 52]

“Ee Bwana, ukuu ni Wako, na uweza, na utukufu, na kushinda, na enzi; maana vitu vyote vilivyo mbinguni na duniani ni Vyako.... uwezo na nguvu vimo mkononi Mwako. ; na mkononi Mwako wawakuza uwapendao, na huwaimarisha wote.” 1 Mambo ya Nyakati 29:11, 12. [Pr 303.3; Maombi Aya ya 53]

Sura hii inaonekana katika (Thoughts from the Mount of Blessing, 102-122)

SURA YA 31

KUOMBA ILI KUTOA

Kristo alikuwa akipokea daima kutoka kwa Baba ili aweze kuwasiliana nasi. “Neno hilo mnalolisikia,” alisema, “si Langu, bali ni la Baba aliyenituma.” Yohana 14:24. “Mwana wa Adamu hakuja kutumikiwa, bali kutumika.” Mathayo 20:28. Si kwa ajili Yake Mwenyewe, bali kwa ajili ya wengine, aliishi na kufikiria na kuomba. Kutoka katika saa alizotumia pamoja na MUNGU alitoka asubuhi baada ya asubuhi kupeleka nuru ya mbinguni kwa wanadamu. Kila siku alipokea ubatizo mpya wa Roho Mtakatifu. Katika saa za mapema (alfajiri) za siku mpya Bwana alimwamsha kutoka katika usingizi Wake, na nafsi Yake na midomo Yake ilipakwa neema, ili aweze kuwagawia wengine. Alipatiwa Maneno mapya kutoka kwenye nyua za mbinguni, Maneno ambayo angeweza kuzungumza katika msimu unaofaa kwa waliochoka na kuonewa. “Bwana MUNGU amenipa,” alisema, “ulimi wa hao wafundishwao, nipate kumtegemeza kwa Neno yeye aliyechoka, huniamsha asubuhi baada ya asubuhi; huniamsha, sikio langu lipate kusikia kama watu wafundishwao.” Isaya 50:4. [Pr 304.1; Maombi Aya ya 1]

Wanafunzi wa Kristo walivutiwa sana na maombi Yake na mazoea Yake ya ushirika na MUNGU. Siku moja baada ya kutokuwepo kwa Mola wao kwa muda mfupi, walimkuta ametekewa/amezama katika dua. Akionekana kutojua uwepo

wao, Aliendelea kuomba kwa sauti. Mioyo ya wanafunzi iliguswa sana. Alipoacha kuomba, wakapaza sauti kwa shauku kubwa, “Bwana, tufundishe kuomba.” [Pr 304.2; Maombi Aya ya 2]

Katika kujibu, Kristo alirudia sala ya Bwana, kama alivyokuwa ameitoa katika mahubiri ya mlimani. Kisha katika kisa alitoa mfano wa somo alilotaka kuwafundisha. [Pr 305.1; Maombi Aya ya 3]

“Ni nani kwenu,” akasema, “aliye na rafiki, naye atamwendea usiku wa manane, na kumwambia, Rafiki, nikopeshe mikate mitatu; kwa maana rafiki yangu amekuja kwangu katika safari yake, nami sina kitu cha kumpatia? Naye aliye ndani ajibu, na kusema, Usinisumbue; mlango sasa umefungwa, na watoto wangu wako pamoja nami kitandani; siwezi kuinuka na kukupa. Nawaambia, ijapokuwa hataamka kumpa kwa kuwa ni rafiki yake, lakini kwa sababu ya kuisitiza kwake ataamka na kumpa kadiri ya haja yake.” [Pr 305.2; Maombi Aya ya 4]

Hapa Kristo anamwakilisha mwombaji anayesihi/anayebembebeza kama yule anayeomba kwa makusudi ya kutoa tena. Ni lazima apate mkate, la sivyo hawezi kumpatia msafiri aliyechoka, aliyechelewa. Ijapokuwa jirani yake hayuko tayari kusumbuliwa, hataacha kushinikiza ombi lake; rafiki yake lazima asaidiwe; na hatimaye ombi lake linajibiwa, mahitaji yake yanatimizwa. [Pr 305.3; Maombi Aya ya 5]

Katika namna ifananayo na hiyo, wanafunzi walipaswa kutafuta baraka kutoka kwa MUNGU. Katika kulisha makutano na katika mahubiri yahusuyo mkate kutoka mbinguni, Kristo alikuwa amewafungulia kazi yao kama wawakilishi Wake. Walipaswa kuwapa watu mkate wa uzima. Yeye aliyewapa kazi yao, aliona ni mara ngapi imani yao itajaribiwa. Mara nyingi walitupwa katika mazingira yasiyotarajiwa, na walitambua upungufu wao wa kibinadamu. Nafsi zilizokuwa na njaa ya mkate wa uzima ziliwajia, na walijiona kuwa maskini na wasio na msaada. Ni lazima wapokee chakula cha kiroho, la sivyo wasingekuwa na chochote cha kuwapa wengine. Lakini hawakupaswa kuiacha nafsi hata moja kurudi kwao bila kulishwa. Kristo anawaelekeza kwenye chanzo cha usambazaji. Mtu ambaye rafiki yake alienda kwake kwa ajili ya kuburudishwa/burudani, hata saa isiyofaa ya usiku wa manane, yeye hakumfukuza. Hakuwa na kitu cha kumpa, lakini alimwendea mmoja aliyekuwa na chakula na kuisitiza ombi lake mpaka jirani akamtimizia haja yake. Na je, MUNGU, ambaye alikuwa ametuma watumishi Wake kulisha wenye njaa, Je, asingeweza kuyatosheleza mahitaji yao ya kazi Yake Mwenyewe? [Pr 305.4; Maombi Aya ya 6]

Lakini jirani mwenye ubinafsi katika mfano huo haiwakilishi tabia ya MUNGU (mifano huwa haiwakilishi vipengele vyote vyema!). Somo limetolewa/limehotwa, si kwa kulinganisha, bali kwa kutofautisha. Mtu mwenye ubinafsi ataitikia na kulitenda ombi lililotolewa kwa haraka, ili kujiepusha na mtu

anayesumbua pumziko lake. Lakini MUNGU anafurahia kutoa. Yeye ni mwingi wa huruma, na anatamani sana kutimiza maombi ya wale wanaomjia kwa imani. Anatupa sisi ili tuweze kuwahudumia wengine na hivyo kuwa kama Yeye. [Pr 306.1; Maombi Aya ya 7]

Yesu anasema, “Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtapata; bisheni, nanyi mtafunguliwa; kwa maana kila aombaye hupokea; naye atafutaye hupata; na yeye abishaye atafunguliwa.” [Pr 306.2; Maombi Aya ya 8]

Mwokozi anaendelea: “Je, kuna yeyote miongoni mwenu ambaye mtoto wake akimwomba mkate, atampa jiwe? Au je, akimwomba samaki, atampa nyoka? Kama basi nyinyi, ingawa ni waovu, mwajua kuwapa watoto wenu vitu vizuri, Je! Baba yenu wa mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?” [Pr 306.3; Maombi Aya ya 9]

Ili kuimarisha tumaini na ujasiri wetu kwa MUNGU, Kristo anatufundisha kumwita kwa Jina Jipya, Jina lililoambatanishwa na ushirika wa dhati zaidi wa moyo wa mwanadamu. Anatupa fursa ya kumwita MUNGU ambaye hana kikomo Baba yetu. Jina hili, Linapotamkwa Kwake na kuhusu Yeye, ni ishara ya upendo na uaminifu wetu Kwake, na ahadi ya kujali katika mahusiano Yake Nasi/kwetu. Linapotamkwa Kwake wakati wa kuomba upendeleo (feva) au baraka Zake, ni kama muziki masikioni Mwake. Ili tusifikirie kuwa ni kujiamini kwa kupitiliza kumwita kwa Jina hili (au kuwa na kiburi), amerudia tena na tena. Anatamani tulitambue na kujizoeza na Jina hilo. [Pr 306.4; Maombi Aya ya 10]

MUNGU anatuona sisi ni watoto Wake. Ametukomboa kutoka katika ulimwengu usiojali na ametuchagua tuwe washiriki wa familia ya kifalme, wana binti za Mfalme wa mbinguni. Anatualika tumtumaini Yeye tukiwa na matumaini na imani yenye kina na yenye nguvu zaidi kuliko ile ya mtoto kwa baba yake wa duniani. Wazazi wanawapenda watoto wao, lakini upendo wa MUNGU ni mkubwa, mpana, na wa kina zaidi kuliko upendo wa kibinadamu unavyoweza kuwa. Upendo Wake hauna kipimo. Basi ikiwa wazazi wa kidunia wanajua kuwapa watoto wao zawadi nzuri, je! Baba yetu aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu wale wamwombao? [Pr 306.5; Maombi Aya ya 11]

Masomo ya Kristo kuhusu maombi yanapaswa kuzingatiwa kwa uangalifu. Kuna sayansi ya Bwana katika maombi, na mfano Wake unaleta mtazamo wa kanuni ambazo wote tunapaswa kuelewa. Anaonyesha kile ambacho ni roho ya Kweli ya maombi, Anafundisha umuhimu wa kudumu katika kuwasilisha maombi yetu kwa MUNGU, na anatuhakikishia nia Yake ya kusikia na kujibu maombi. [Pr 307.1; Maombi Aya ya 12]

Maombi yetu hayapaswi kuwa maombi yenye ubinafsi, ya kujipatia vitu faida yetu wenyewe tu. Tunapaswa kuomba ili tuweze kutoa. Kanuni ya maisha ya Kristo lazima iwe kanuni ya maisha yetu. “Kwa ajili yao,” Yeye alisema, akizungumza juu ya wanafunzi Wake, “Najiweka wakfu, ili nao watakaswe.”

Yohana 17:19. Kujitoa vile vile, kujia mhanga kwa namna ile ile, utiifu uleule wa madai ya Neno la MUNGU, ambao ulidhihirika katika Kristo, lazima uonekane kwa watumishi Wake. Utume wetu kwa ulimwengu sio kujitumikia au kujifurahisha wenyewe; tunapaswa kumtukuza MUNGU kwa kushirikiana Naye kuwaokoa wenye dhambi. Tunapaswa kuomba baraka kutoka kwa MUNGU ili tuweze kuwasiliana na wengine. Uwezo wa kupokea kutoka Kwake au kupewa Naye, huhifadhiwa au unakuwepo tu kwa kutoa. Hatuwezi kuendelea kupokea hazina ya mbinguni bila kuwasiliana na wale wanaotuzunguka.— (Christ's Object Lessons, 142, 143) [Pr 307.2; Maombi Aya ya 13]

Katika kisa cha mfano cha aliyeomba/mwombaji, ni kwamba alikataliwa tena na tena, lakini hakuliacha kusudi lake. Kwa hiyo maombi yetu mara zingine hayaonekani kupata jibu la haraka; lakini Kristo anafundisha kwamba hatupaswi kuacha kuomba. Dhumuni la maombi si kumbadilisha MUNGU au kuleta mabadiliko Kwake; bali ni kutuleta katika upatanifu na MUNGU. Tunapomwomba Yeye, anaweza kuona kwamba ni muhimu kwetu kuipeleleza mioyo yetu na kutubu dhambi. Kwa hiyo anatuingiza katika majaribu na mitihani, hutupitisha kwenye njia ya kujidhili na unyenyekevu, ili tupate kuona kile kinachozuia utendaji wa Roho Wake Mtakatifu kupitia kwetu. [Pr 307.3; Maombi Aya ya 14]

Kuna masharti ya kutimizwa kwa ahadi za MUNGU, na maombi hayawezi kamwe hayawezi kuchukua nafasi ya wajibu. “Mkinipenda,” Kristo asema, “mtazishika amri Zangu.” “Yeye aliye na amri Zangu, na kuzishika, Yeye Ndiye anipendaye; naye anipendaye atapendwa na Baba Yangu, Nami nitampenda na kujidhihirisha kwake.” Yohana 14:15, 21. Wale wanaoleta maombi yao kwa MUNGU, wakidai ahadi Yake huku wao hawaendani na masharti, wanamtukana Yehova. Wanaleta Jina la Kristo kama mamlaka yao ya utimizo wa ahadi, lakini hawatendi mambo yale ambayo yangeonyesha imani katika Kristo na upendo Kwake. [Pr 307.4; Maombi Aya ya 15]

Wengi wanapoteza haki ya kukubalika na Baba. Tunahitaji kuchunguza kwa makini tendo la kumtumaini Mungu, tunapokuwa tunamkaribia Yeye. Ikiwa sisi si watiifu, tunamletea Bwana hundi ya kulipwa wakati hatujatimiza masharti ambayo yangetufanya tulipwe. Tunawasilisha kwa MUNGU ahadi Zake, na kumwomba au kumwuliza azitimize, wakati kwa kufanya hivyo angelikosea heshima Jina Lake Mwenyewe. [Pr 308.1; Maombi Aya ya 16]

Ahadi ni “Ninyi mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa.” Yohana 15:7. Naye Yohana anatangaza hivi: “Katika hili twajua ya kuwa tumemjua Yeye, ikiwa tunashika amri Zake. Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki amri Zake, ni mwongo, wala Kweli haimo ndani yake. Bali yeye alishikaye Neno Lake, ndani yake huyo pendo la MUNGU limekamilika hakika.” 1 Yohana 2:3-5. [Pr 308.2; Maombi Aya ya 17]

Mojawapo ya amri za mwisho za Kristo kwa wanafunzi Wake ilikuwa

“Mpendane kama nilivyowapenda ninyi.” Yohana 13:34. Je, tunatii amri hii, au tunafurahia na tunaendekeza sana tabia zisizo za Kikristo? Ikiwa kwa namna yoyote tumehuzunisha au kuwajeruhi wengine, ni jukumu letu kuungama kosa letu na kutafuta upatanisho. Haya ni maandalizi muhimu ili tuweze kwenda mbele za MUNGU kwa imani, katika kuomba baraka Zake. [Pr 308.3; Maombi Aya ya 18]

Kuna jambo lingine ambalo mara nyingi hupuuzwa na wale wanaomtafuta Bwana katika maombi. Je, umekuwa mwaminifu na mkweli kwa MUNGU? Kupitia nabii Malaki Bwana anatangaza, “Tangu siku za baba zenu mmeziacha amri Zangu, wala hamkuzishika. Nirudieni Mimi, Nami nitawarudia ninyi, asema Bwana wa majeshi. Lakini ninyi mwasema, Turudi kwa namna gani? Je, mwanadamu atamwibia Mungu? Lakini ninyi mmeniibia Mimi. Lakini ninyi mwasema, Tumekuibia kwa jinsi gani? Mmeniibia zaka na dhabihu.” Malaki 3:7, 8. [Pr 308.4; Maombi Aya ya 19]

Kama Mpaji wa kila baraka, MUNGU anadai sehemu fulani ya vyote tulivyo navyo. Hili ni fungu lililo katika mpango Wake ili kuendeleza mahubiri ya injili. Na kwa kumrudishia MUNGU, tunakuwa tumeonyesha kuthamini kwetu zawadi Zake. Lakini tukimzuilia kile ambacho ni Chake Mwenyewe, tunawezaje kudai baraka Zake? Ikiwa sisi ni mawakili wasio waaminifu wa mambo ya duniani, tunawezaje kumtarajia Yeye kutuamini kwa kutukabidhi vitu vya mbinguni? Huenda ikawa hapa ndio siri ya maombi yasiyojibiwa. [Pr 309.1; Maombi Aya ya 20]

Lakini Bwana katika rehema Zake kuu yu tayari kusamehe, Naye asema, “Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba Yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo, ... kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha kuipokea. Nami kwa ajili yenu nitamkemea yeye alaye, wala hataharibu matunda ya ardhi yenu; wala mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake kabla ya wakati wake katika shamba Na mataifa yote watawaiteni heri; maana mtakuwa nchi ya kupendeza sana, asema Bwana wa majeshi. Malaki 3:10-12. [Pr 309.2; Maombi Aya ya 21]

Ndivyo ilivyo kwa kila takwa au sharti jingine la MUNGU. Zawadi Zake zote zimeahidiwa kwa sharti la utii. MUNGU ana mbingu iliyojaa baraka kwa wale watakaoshirikiana Naye. Wote wanaomtii wanaweza kudai kwa ujasiri kutimizwa kwa ahadi Zake [Pr 309.3; Maombi Aya ya 22]

Lakini ni lazima tuonyeshe tumaini thabiti na lisilokengeuka kwa MUNGU. Mara nyingi Yeye huchelewesha kutujibu ili kujaribu imani yetu au kujaribu unyofu/ukweli wa shauku yetu. Baada ya kuomba kulingana na Neno Lake, tunapaswa kuamini ahadi Yake na kusesitiza maombi yetu kwa mtazamo wenye kuazimia kwamba hayatakataliwa. [Pr 309.4; Maombi Aya ya 23]

MUNGU hasemi, Ombeni mara moja, nanyi mtapata. Anatubidisha tuombe. Dumu katika maombi bila kuchoka. Kuomba kwa bidii humleta mwombaji katika

mtazamo wa dhati zaidi, na kumpa shauku kubwa ya kupokea mambo ambayo anaombea. Kristo alimwambia Martha kwenye kaburi la Lazaro, “Kama ukiamini, utaona utukufu wa MUNGU.” Yohana 11:40. [Pr 309.5; Maombi Aya ya 24]

Lakini wengi hawana imani iliyo hai. Na hii ndiyo sababu hawazioni nguvu zaidi ya MUNGU. Udhaifu wao ni matokeo ya kutokuamini kwao. Wana imani zaidi katika juhudi zao wenyewe kuliko katika utendaji wa MUNGU kwao. Wamejiweka katika kujitunza na kujishugulikia wenyewe. Wanapanga na kufikiri, lakini wanaomba kidogo, na wana imani ndogo ya Kweli kwa MUNGU. Wanafikiri wana imani, lakini ni msukumo tu wa wakati huo. Kwa kushindwa kutambua hitaji lao wenyewe, au nia ya MUNGU kuwapa, hawadumu katika kuweka maombi yao mbele za Bwana. [Pr 310.1; Maombi Aya ya 25]

Maombi yetu yanapaswa kuwa ya dhati na yasiyochoka kama yalivyokuwa maombi ya yule rafiki mhitaji aliyeomba mikate usiku wa manane. Kadiri tunavyoomba kwa bidii na uthabiti, ndivyo muungano wetu wa kiroho na Kristo utakavyokuwa karibu zaidi. Tutapokea baraka nyingi kwa sababu tumeongeza imani. [Pr 310.2; Maombi Aya ya 26]

Sehemu yetu ni kuomba na kuamini. Kesheni katika maombi. Kesha, na ushirikiane na MUNGU asikiaye maombi. Kumbuka kwamba “sisi ni watenda kazi pamoja na MUNGU.” 1 Wakorintho 3:9. Zungumza na kutenda kulingana na maombi yako. Itafanya tofauti ya kudumu kwako hata jaribu litaipima imani yako kuwa ya kweli, au itaonyesha kuwa maombi yako ni ya desturi/mazoea au mfano tu. [Pr 310.3; Maombi Aya ya 27]

Wakati mashaka yanapotokea, na matatizo yanakukabili, usitafute msaada kwa wanadamu. Tumainia yote kwa MUNGU. Mazoea ya kuwaambia wengine magumu yetu hutufanya tu kuwa dhaifu, na hayaleti nguvu kwao. Yanaweka juu yao mzigo wa udhaifu wetu wa kiroho, ambao hawawezi kuutatua au kutuletea afueni. Tunatafuta nguvu za mwanadamu mwenye dhambi, anayekosea, na mwenye kikomo, wakati tunaweza kuwa na nguvu za MUNGU asiyekosea, asiye na mwisho. [Pr 310.4; Maombi Aya ya 28]

Hauhitaji kwenda kwenye miisho ya dunia kwa ajili ya hekima, kwa maana MUNGU Yuko karibu. Sio uwezo ulionao sasa au utakaowahi kuwa nao wakati wowote ule, ndio utakaokupa mafanikio. Ni yale ambayo Bwana anaweza kukufanyia. Tunahitaji kuwa na imani ndogo sana katika kile ambacho mwanadamu anaweza kufanya na kuwa na ujasiri zaidi katika kile ambacho MUNGU anaweza kufanya kwa kila nafsi inayoamini. Anatamani kukufanya wewe umfikie Yeye kwa imani. Anatamani sana wewe utarajie mambo makubwa kutoka Kwake. Anatamani kukupa ufahamu katika mambo ya kimwili, yaani yale ya muda mfupi na yale kiroho. Anaweza akazinoa akili. Anaweza kutoa busara na ujuzi. Weka talanta/vipawa vyako kazini, na kisha mwombe MUNGU hekima, nawe utapewa. [Pr 310.5; Maombi Aya ya 29]

Lichukue Neno la Kristo kama uhakikisho wako. Kwani Yeye hajakualika wewe uje Kwake? Usijiruhusu kamwe kuzungumza kwa njia isiyo na matumaini, iliyovunjika moyo. Ukifanya hivyo utapoteza sana. Kwa kutazama mwonekano na kulalamika shida na shinikizo vinapokujia, unatoa uthibitisho wa imani yenye ugonjwa na iliyodhoofika. Ongea na tenda kana kwamba imani yako haiwezi kushindwa. Bwana ni tajiri wa mali; Anamiliki dunia. Tazama mbinguni kwa imani. Mwangelie Yeye aliye na nuru na uwezo na ufanisi. [Pr 311.1; Maombi Aya ya 30]

Katika imani ya kweli kuna uchangamfu, uthabiti wa kanuni, na uimara wa kusudi ambao hakuna wakati wala taabu inayoweza kudhoofisha. "Hata vijana watafifia na kulegea; naam, wataanguka kwa uchovu. Lakini wote wanaomtumainia Mwenyezi MUNGU, watapata nguvu mpya. Watapanda juu kwa mabawa kama tai; watakimbia bila kuchoka; watatembea bila kulegea." Isaya 40:30, 31, [Pr 311.2; Maombi Aya ya 31]

Kuna wengi wanaotamani kuwasaidia wengine, lakini wanahisi kwamba hawana nguvu za kiroho au nuru ya kuwapa wengine. Hebu wawasilishe maombi yao kwenye kiti cha neema. Omba kwa ajili ya Roho Mtakatifu. MUNGU anasimama nyuma ya kila ahadi Yake aliyoitoa (uhakika). Ukiwa na Biblia yako mikononi mwako sema, nimefanya kama ulivyosema. Ninawasilisha ahadi Yako, "Ombe, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtapata; bisheni, nanyi mtafunguliwa." [Pr 311.3; Maombi Aya ya 32]

Hatupaswi kuomba kwa Jina la Kristo tu, bali kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu. Hii inafafanua kile kinachomaanishwa inaposemwa kwamba Roho "hufanya maombezi kwa ajili yetu kwa uchungu usioweza kuelezeka." (kuugua kusikotamkika) Warumi 8:26. Ombi kama hilo MUNGU hufurahia kulijibu. Tunapotoa ombi katika jina la Kristo kwa bidii na mkazo, kuna ahadi kubwa kutoka kwa MUNGU kwamba atajibu ombi letu "kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo." Waefeso 3:20. [Pr 311.4; Maombi Aya ya 33]

Kristo amesema, "Yo yote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu. Marko 11:24. "Nanyi mkiomba lolote kwa Jina Langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana." Yohana 14:13. Naye Yohana mpendwa, chini ya uvuvio wa Roho Mtakatifu, anasema kwa uwazi na uhakikisho mkubwa: "Tukiomba kitu sawasawa na mapenzi Yake, anatusikia; na kama tukijua ya kuwa atusikia, tumwombalo lo ote, twajua ya kuwa tunazo haja tulizomwomba." 1 Yohana 5:14, 15. Kisha wasilisha ombi lako kwa Baba katika Jina la Yesu. MUNGU ataliheshimu Jina hilo. [Pr 311.5; Maombi Aya ya 34]

Upinde wa mvua unaokizunguka kiti cha enzi ni uthibitisho kwamba MUNGU ni Kweli/Mkweli, kwamba ndani Yake hakuna kubadilikabadilika, wala kugeuka kama kivuli. Tumemtenda dhambi na hatustahili rehema Zake. lakini Yeye Mwenyewe ameweka katika midomo yetu maombi yale ya ajabu sana, "Usitutupe, kwa heshima ya Jina Lako; usikidharau kiti chako cha enzi kitukufu. Ukumbuke

agano ulilofanya nasi, wala usilivunje. Yeremia 14:21. Tunapoenda kKwake tukiungama kutostahili na dhambi zetu, Yeye amejitolea kukisikiliza kilio chetu. Heshima ya kiti Chake cha enzi imo hatarini kwa ajili ya utimilifu wa Neno Lake kwetu (heshima Yake ipo hatarini Neno Lake lisipotimia). [Pr 312.1; Maombi Aya ya 35]

Kama Haruni, aliyefananishwa na Kristo, Mwokozi wetu anabeba majina ya watu Wake wote moyoni Mwake katika Patakatifu. Kuhani wetu Mkuu anakumbuka Maneno yote ambayo kwayo ametutia moyo kuyatumaini. Daima Yeye hukumbuka na kujali Agano Lake. [Pr 312.2; Maombi Aya ya 36]

Wote wamtafutao watapata. Wote wanaobisha watafunguliwa mlango. Udhuru hautatolewa, Usinisumbue; mlango umefungwa; Sitaki kufungua. Kamwe hataambiwa mtu, 'siwezi kukusaidia'. Wale wanaoomba mkate usiku wa manane ili kulisha roho zenye njaa watafanikiwa. [Pr 312.3; Maombi Aya ya 37]

Katika kisa cha Mfano, cha yule anayeomba mkate kwa ajili ya mgeni, hupokea "kwa wingi kadiri ya haja yake." Na ni kwa kipimo gani basi MUNGU atatugawia ili tuwagawie wengine? "Kwa kadiri ya kipimo cha kipawa cha Kristo." Waefeso 4:7. Malaika wanatazama kwa maslahi mazito kuona jinsi mwanadamu anavyoshughulika na wanadamu wenzake (anavyodili). Wanapoona mtu akidhihirisha huruma kama ya Kristo kwa wakosaji, wanajongea kwa karibu sana naye na kuleta kwenye kumbukumbu yake maneno ya kusema ambayo yatakuwa kama Mkate wa Uzima kwenye nafsi hiyo "MUNGU atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri Wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu." Wafilipi 4:19. Ushuhuda wako katika Ukweli na uhalisia wake, atafanya kuwa na nguvu katika uwezo ya maisha yajayo. Neno la Bwana litakuwa kinywani mwako kama Kweli na haki. [Pr 312.4; Maombi Aya ya 38]

Juhudi binafsi kwa wengine zinapaswa kutanguliwa maombi mengi ya siri; kwa maana inahitaji hekima kubwa kuelewa sayansi ya kuokoa roho. Kabla ya kuwasiliana na wanadamu, fanya ushirika na Kristo. Katika kiti cha enzi cha neema ya mbinguni pata maandalizi ya kuwahudumia watu. [Pr 313.1; Maombi Aya ya 39]

Hebu moyo wako uvunjike kwaajili ya matamania uliyo nayo kwa MUNGU, kwa MUNGU aliye hai. Uhai wa Kristo umeonyesha kile ambacho binadamu anaweza kufanya kwa kuwa mshiriki wa asili ya Uungu. Yote ambayo Kristo alipokea kutoka kwa MUNGU sisi pia tunaweza kuwa nayo. Kisha omba na upokee. Kwa imani yenye kudumu ya Yakobo, pamoja na ustahimilivu wa Eliya, omba mwenyewe yote ambayo MUNGU ameahidi. [Pr 313.2; Maombi Aya ya 40]

Hebu mawazo yenye utukufu ya MUNGU yatawale akili yako. Hebu maisha yako yasukwe na miunganiko iliyofichika ya maisha ya Yesu. Yeye aliyeamuru nuru iangaze kutoka gizani, Yuko tayari kuangaza moyoni mwako, na kukupa nuru ya elimu ya utukufu wa MUNGU katika uso wa Yesu Kristo. Roho Mtakatifu

atachukua mambo ya MUNGU na kukuonyesha, akiyafikisha kama nguvu iliyo hai ndani ya moyo mtiifu. Kristo atakuongoza hadi kwenye mlango wa Asiye na mwisho. Unaweza kuuona utukufu uliopo nyuma ya pazia, na kuwafunulia watu utoshelevu Wake Yeye anayeishi sikuzote kufanya maombezi kwa ajili yetu. [Pr 31z.3; Maombi Aya ya 41]

Sura hii inaonekana katika Christ's Object Lessons, pages 139-149

SURA YA 32
IMANI NA MAOMBI

Imani ni kumtumaini MUNGU—kuamini kwamba Yeye anatupenda, Naye anajua zaidi kile ambacho ndicho cha manufaa kwetu. Na Hivyo, badala ya kuchagua njia au mawazo yetu wenyewe, tunaongozwa kuchagua njia Yake. Katika mahali pa ujinga wetu, tunaikubali hekima Yake; badala ya udhaifu wetu, nguvu Zake; badala ya dhambi zetu, haki Yake. Maisha yetu sisi wenyewe, tayari ni ya Kwake; imani inakiri umiliki Wake na kukubali baraka Zake. Ukweli, unyoofu, usafi wa moyo, vimetajwa/vimesondwa kuwa siri za mafanikio ya maisha. Ni imani ndiyo inayotuweka katika umiliki wa kanuni hizi. [Pr 314.1; Maombi Aya ya 1]

“Kila msukumo mzuri au matamanio ni zawadi ya MUNGU; imani hupokea kutoka kwa MUNGU maisha ambayo ndiyo hayo pekee yanayoweza kuzalisha ukuaji wa Kweli na ufanisi. [Pr 314.2; Maombi Aya ya 2]

Namna ya kuizoesha imani yapaswa kuwekwa wazi sana. Kwa kila ahadi ya MUNGU kuna masharti. Ikiwa tuko tayari kufanya mapenzi Yake, Nguvu na uwezo Wake wote ni wetu. Karama yoyote anayoahidi, iko katika ahadi yenyewe. “Mbegu ni Neno la MUNGU.” Luka 8:11. “Kwa hakika kama vile mwaloni ulivyo katika mche, ndivyo karama ya MUNGU ilivyo katika ahadi Yake. Ikiwa tunapokea ahadi, tunayo zawadi.” [Pr 314.3; Maombi Aya ya 3]

Ile Imani inayotuwezesha kupokea karama za MUNGU, yenyewe hiyo ni zawadi, ambayo kila mwanadamu mwanadamu amepewa kwa kipimo fulani. Nayo inakua kadiri inavyotumiwa kwa usahihi wa Neno la MUNGU. Ili kuimarisha imani, ni lazima tuiunganishe mara mara na Neno Lake. [Pr 314.4; Maombi Aya ya 4]

Katika ujifunzaji wa Biblia mwanafunzi anapaswa kuongozwa kuona nguvu ya Neno la MUNGU. Katika uumbaji, Yeye “Akanena, ikawa; Akatoa amri, nayo ikasimama hivyo.” Yeye “huamuru vitu ambavyo havipo viwepo.” (Zaburi 33:9; Warumi 4:17); kwa maana anapoviamuru, huwa papo hapo. [Pr 315.1; Maombi Aya ya 5]

Ni mara ngapi wale walioamini Neno la Mungu, ingawa wao wenyewe binafsi hawana msaada au uwezo kabisa, wamepinga nguvu za ulimwengu wote — Henoka, mwenye moyo safi mtakatifu katika mtindo wa maisha, akishikilia sana imani yake katika ushindi wa haki dhidi ya kizazi kiovu na chenye watu waliojaa dhihaka; Nuhu na nyumba yake dhidi ya watu wa wakati wake, watu wenye nguvu kubwa ya mwili na akili na maadili yenye uchafu/ufisadi zaidi; watoto wa Israeli kwenye Bahari ya shamu, umati wa watumwa wasio na msaada, na wenye hofu, dhidi ya jeshi lenye nguvu zaidi la taifa lenye nguvu duniani; Daudi, kijana mchungaji, aliye na ahadi ya MUNGU ya kiti cha ufalme, dhidi ya Sauli, mfalme aliyewekwa rasmi, aliazimia kuzishikilia nguvu Zake Mungu; Shadraka na wenzake katika moto, na Nebukadreza kwenye kiti cha enzi; Danieli kati ya simba, maadui zake katika nafasi za hadhi ya hali ya juu katika ufalme; Yesu msalabani, na makuhani wa Kiyahudi na watawala wakimlazimisha hata gavana wa Kirumi

kufanya mapenzi yao; Paulo akiwa amefungwa minyororo akiwa amehukumiwa kifo cha mhalifu, na Nero dikteta/dhalimu wa himaya ya ulimwengu. [Pr 315.2; Maombi Aya ya 6]

Mifano kama hiyo haipatikani katika Biblia pekee. Imejaa katika kila rekodi ya maendeleo ya mwanadamu. Wavaudois na Wahuguenoti, Wycliffe na Huss, Jerome na Luther, Tyndale na Knox, Zinzendorf na Wesley, pamoja na umati wa wengine, wameshuhudia nguvu ya Neno la MUNGU dhidi ya nguvu na sera za binadamu katika kuunga mkono uovu. Hawa ndio waaminifu wa Kweli wa ulimwengu. Huu ni msururu/mstari Wake wa watiifu. Katika mstari huu vijana wa leo wanaitwa kuchukua nafasi zao. [Pr 315.3; Maombi Aya ya 7]

Imani inahitajika katika madogo na isipungue katika mambo makubwa zaidi ya maisha. Katika masilahi na kazi zetu zote za kila siku nguvu ya kudumisha ya MUNGU inakuwa halisi kwetu kupitia imani ya kudumu. [Pr 315.4; Maombi Aya ya 8]

Yakitazamwa kutoka katika upande wake wa kibinadamu, maisha ni njia ambayo hakuna mtu yeyote aliyewahi kupita. Ni njia ambayo, kwa kuzingatia uzoefu wetu wa kina, kila mmoja hupita peke yake. Katika maisha yetu ya ndani hakuna mwanadamu mwingine anayeweza kuingia kikamilifu. Mtoto mdogo anapoanza katika safari hiyo ambayo, mapema au baadaye, ni lazima achague njia yake mwenyewe, yeye mwenyewe akiamua masuala ya maisha ya umilele, ni jitihada ya bidii kiasi gani basi inapaswa kutumika kuelekeza imani yake kwa Kiongozi na Msaidizi wa hakika! [Pr 315.5; Maombi Aya ya 9]

Kama ngao dhidi ya majaribu, msukumo wa usafi wa moyo na Ukweli, hakuna ushawishi mwingine unaoweza kuwa sawa na hisia ya uwepo wa MUNGU. “kila kitu kimefunuliwa wazi mbele ya macho Yake Yeye ambaye Kwake tutapaswa kutoa hoja ya matendo yetu” Yeye ni “mtakatifu kabisa, hawezi kutazama uovu, hawezi kustahimili kamwe kuona mabaya.” Waebrania 4:13; Habakuki 1:13. Wazo hili lilikuwa ngao ya Yusufu kati ya ufisadi na uchafu wa Misri. Juu ya vivutio vya majaribu jibu lake lilikuwa thabiti: “Ninawezaje kufanya uovu huu mkuu, na kumtendea MUNGU dhambi?” Mwanzo 39:9. Imani, ikiwa itatunzwa, italeti ngao kama hiyo juu ya kila roho. [Pr 316.1; Maombi Aya ya 10]

Utambuzi tu wa uwepo wa MUNGU pekee unaweza kukomesha hofu ambayo, kwa mtoto mwenye woga ungemfanyia maisha kuwa mzigo. Hebu aweke katika kumbukumbu yake ahadi, “Malaika wa Bwana hufanya kituo, Akiwazunguka wamchao, na kuwaokoa.” Zaburi 34:7. Hebu asome Kisa kile cha ajabu cha Elisha katika mji ulio mlimani, na, kati yake na majeshi ya maadui wenye silaha, kikosi chenye nguvu cha malaika wa mbinguni kikiwazunguka. Hebu asome jinsi Petro, Akiwa gerezani na kuhukumiwa kifo, malaika wa MUNGU alimtokea; jinsi, alivyowapita walinzi wenye silaha, milango mikubwa na lango kubwa la chuma lenye makufuli yake na makomeo, malaika alimwongoza mtumishi wa MUNGU

nje kwa usalama. Hebu asome juu ya tukio lile la baharini, wakati wale askari-jeshi na mabaharia waliokuwa wakirushwa na tufani, wakiwa wamechoshwa na kazi ngumu na kukesha na kufunga kwa muda mrefu, Paulo mfungwa, akiwa njiani kuelekea kwenye hukumu na kuuawa, aliposema Maneno yale makuu ya ujasiri na tumaini: " Jipeni moyo; kwa maana hakuna mtu kati yenu atakayepoteza maisha yake.....Kwa maana usiku huu Malaika wa MUNGU ambaye mimi ni Wake na ninayemtumikia alisimama karibu nami, akisema, Usiogope, Paulo; imekupasa kuletwa mbele ya Kaisari; na tazama, MUNGU amekupa wote wasafirio pamoja nawe." Kwa imani ya ahadi hii Paulo aliwahakikishia wenzake, "Hapataanguka hata unywele mmoja wa kichwa cha mmoja wenu." Na ikawa. Kwa sababu ndani ya merikebu hiyo kulikuwa na mtu mmoja ambaye kupitia kwake MUNGU angeweza kufanya kazi, shehena yote ya meli ya askari wa kipagani na mabaharia ilihifadhiwa. "Walivuka wote hadi nchi kavu salama." Matendo 27:22-24, 34, 44. [Pr 316.2; Maombi Aya ya 11]

Mambo haya hayakuandikwa ili tusome tu na kushangaa- shangaa (kustaajabu), bali ili imani ile ile iliyotenda kazi ndani ya watumishi wa MUNGU wa zamani ifanye kazi ndani yetu pia. Kwa namna isiyopungua ya yale aliyoyafanya wakati huo, Yeye Atafanya kazi sasa popote palipo na mioyo ya imani iwe mifereji ya nguvu Zake. [Pr 317.1; Maombi Aya ya 12]

Hebu wasiojiamini, ambao upungufu wa kutojitegemea kwao unawapelekea kuzama mbali na kujali na kuwajibika, wafundishwe kumtegemea MUNGU. Hivyo wengi ambao la sivyo wangukuwa tu watu duni ulimwenguni (sifuri), pengine mizigo tu isiyo na msaada, wataweza kusema pamoja na mtume Paulo, "Nayaweza mambo yote katika Yeye anitiaye nguvu." Wafilipi 4:13. [Pr 317.2; Maombi Aya ya 13]

Kwa mtoto ambaye pia ni mwepesi kuchukizwa na majeraha ya chuki au visasi moyoni, kwake imani ina masomo ya thamani. Mwelekeo wa kupinga uovu au kulipiza kisasi mara nyingi huchochewa na hisia kali ya kujali haki na roho ya kutenda na yenye bidii. Hebu mtoto wa namna hiyo afundishwe kwamba MUNGU Ndiye mlinzi wa haki wa milele zote. Ana ulinzi maridhawa kwa viumbe ambao Amewapenda sana kiasi cha kumtoa Mwanaye Mpendwa kuokoa. Atashughulika kikamilifu na kila anayetenda uovu. [Pr 317.3; Maombi Aya ya 14]

"Kwa maana Yeye awagusaye ninyi aigusa mboni ya jicho Lake." Zekaria 2:8. [Pr 317.4; Maombi Aya ya 15]

"Mkabidhi Mwenyezi maisha yako; mtumainie Yeye Naye atafanya kitu. Ataufanya wema wako ung'ae kama mwanga, na uadilifu wako kama jua la adhuhuri." Zaburi 37:5, 6. [Pr 317.5; Maombi Aya ya 16]

"Bwana Naye atakuwa kimbilio kwa walioonewa, kimbilio wakati wa taabu. Nao wakujua Jina Lako watakutumaini Wewe, kwa maana Wewe, Bwana, hukuwaacha wakutafutao." Zaburi 9:9, 10. [Pr 317.6; Maombi Aya ya 17]

Huruma ambayo MUNGU anaonyesha kwetu, Yeye anatubidisha tuionyeshe kwa wengine. Hebu wenye hasira, mihemko, wenye kujitumaini nafsi, wenye kulipiza kisasi, wamtazame Yeye Aliye mpole na mnyenyekevu, akiongozwa kama kondoo anayekwenda kuchinjwa, bila kulipiza kisasi kama kondoo mbele ya mkata manyoya wake.. Wamtazame Yeye ambaye dhambi zetu zimemchoma na huzuni zetu zimemlelea, nao watajifunza kuvumilia, kustahimili, na kusamehe. [Pr 317.7; Maombi Aya ya 18]

Kupitia imani, kila upungufu wa tabia unaweza kutolewa (kujazwa na kukawa na ukamilifu), kila unajisi kusafishwa, kila kosa kurekebishwa, kila ubora unapata kuendelezwa. [Pr 318.1; Maombi Aya ya 19]

“Nyinyi mmekamilika katika Yeye.” Wakolosai 2:10. [Pr 318.2; Maombi Aya ya 20]

Maombi na imani vina uhusiano wa karibu (pacha), na vinahitaji kujifunzwa/kuchunguzwa pamoja. Katika maombi ya imani kuna sayansi ya Mbingu/Bwana; ni sayansi ambayo kila mtu ambaye anahitaji kuifanya kazi yake ya maisha ifanikiwe lazima aielewe. Kristo anasema, “Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu. Marko 11:24. Anaweka wazi kwamba maombi yetu lazima yapatane na mapenzi ya MUNGU; lazima tuombe mambo ambayo ameahidi, na chochote tunachopokea lazima kitumike katika kufanya mapenzi Yake. Masharti yakitimizwa, ahadi haizuiliki. [Pr 318.3; Maombi Aya ya 21]

Kwa msamaha wa dhambi, kwa Roho Mtakatifu, kwa hulka na tabia kama ya Kristo, kwa hekima na nguvu ya kufanya kazi Yake, kwa zawadi yoyote ambayo ameahidi, tunaweza kuomba; kisha tunapaswa kuamini kwamba tutapokea, na kurudisha shukrani kwa MUNGU kwamba tumepokea. [Pr 318.4; Maombi Aya ya 22]

Hatuhitaji mwonekano wa wote wa nje wa ushahidi wa kubarikiwa. Zawadi ipo katika ahadi, na tunaweza kuendelea na kazi yetu tukiwa na hakika kwamba kile ambacho MUNGU amekiahidi Ana uwezo wa kukitekeleza, na kwamba zawadi, ambayo tayari kabisa tunayo, itadhihirika wakati tunaipoihitaji sana. [Pr 318.5; Maombi Aya ya 23]

Kuishi hivyo kwa Neno la MUNGU maana yake ni kusalimisha Kwake maisha yote. Kutakuwa na hisia endelevu ya hitaji na utegemezi, kuvutwa kutoka moyoni kumtafuta MUNGU. Maombi ni lazima; maana ni uhai wa nafsi. Maombi ya familia, maombi ya hadhara, yana nafasi yake; lakini ni ushirika wa siri na MUNGU unaotegemeza uhai wa nafsi. [Pr 318.6; Maombi Aya ya 24]

Ilikuwa katika mlima pamoja na MUNGU ndipo ambapo Musa aliona kielelezo cha jengo lile la ajabu ambalo lilipaswa kuwa makao ya utukufu Wake. Ni katika mlima pamoja na MUNGU—katika mahali pa siri pa ushirika—ndimo tunapaswa

60. Nehemia kwaajili ya msaada (maneno 31; [Neh 6:14](#)).

61. Israeli-ungamo la dhambi (maneno 1,205-sala ndefu zaidi; [Neh 9:5-38](#)).

62. Nehemia kwa baraka (maneno 29; [Neh 13:14](#)).

63. Nehemia kwa baraka (maneno 18; [Neh 13:22](#)).

64. Nehemia kwa hukumu (maneno 21; [Neh 13:29](#)).

65. Nehemia kwa baraka (maneno 7).

Marejeleo ya maombi ([Neh 2:4](#) ; [4:9](#) ; [8:6](#)).

Maombi saba katika Ayubu:

66. Ayubu-sala ya shukrani na kuacha malalamiko na kuelewa mambo (maneno 30; [Ayubu 1:20-22](#)).

67. Ayubu katika malalamiko na kwaajili ya kitulizo na msamaha (maneno 114; [Ayubu 7:17-21](#)). Akajibu ([Ayubu 42:10](#)).

68. Ayubu katika malalamiko na msaada (maneno 571; [Ayubu 9:25-10:22](#)). Akajibu ([Ayubu 42:10](#)).

69. Ayubu katika malalamiko na kwaajili ya maisha na msamaha (maneno 198; [Ayubu 14:13-22](#)). Akajibu ([Ayubu 42:10](#)).

70. Ayubu kwaajili ya hukumu ya haki (maneno 48; [Ayubu 23:3-5](#)). Akajibu (Ayubu 38-42).

71. Ayubu, maombi ya kuungama (maneno 34; [Ayubu 40:3-5](#))

72. Ayubu, sala ya toba (maneno 87; [Ayubu 42:1-6](#)). Akajibu ([Ayubu 42:10](#)).

Sala sabini na mbili katika Zaburi:

73-123. Daudi. Katika Zaburi 50 za maombi aliomba baraka mbalimbali, nyingi kati ya hizo zikijibiwa kwa sababu ya imani katika ahadi za Mungu (Zaburi 3-7; 9; 12:1-13:6; 16:1-17:15; 19:1-20:9; 22; 25:1-31:24; 35:1; 35:1; 35:1; 35:1; 35:1; 35:1-3; 51:1-61:8; 69:1-70:5; Yale ambayo hayajajibiwa yatajibiwa kwa wakati ufaao kwa Daudi hata alisali kuhusu matukio ya wakati ujao.

124-138. Mtunga Zaburi asiyejulikana (labda Daudi) aliomba aina nyingi za baraka, ambazo zilitolewa au zitatolewa (Zaburi 10; 33; 43:1-44:26; 71; 85; 88; 102; 106; 118; 120; 123; 123; 125; 125;

139-143. Asafu alimwomba Mungu maombi mengi (katika maombi 5) kwa ajili ya aina mbalimbali za baraka ambazo zilitolewa au ambazo bado zitatolewa (Zaburi 74; 79:1-80:19; 82:1-83:18).

144. Musa anamwomba Mungu (Zaburi 90).

145. Ethani alimwomba Mungu akumbuke shutuma za watumishi wake (Zaburi 89).

Kwa hiyo, katika zaburi 72 kati ya 150 kuna maombi ya kibinafsi kwa Mungu, na kuyafanya kuwa Zaburi za sala. Wachache kati ya 78 wengine wanaweza pia kuzingatiwa kwa sababu ya hali ya jumla ya mada. Hata katika zaburi za sala zilizoorodheshwa masomo mengi ni bora zaidi kuliko sala. Tazama maelezo juu ya zaburi hizi.

Maombi matatu katika Isaya:

146. Isaya kwaajili ya kutakaswa (maneno 38; [Isa 6:5](#)). Akajibu ([Isa 6:6-7](#)).

147. Hezekia kwaajili ukombozi (maneno 133; [Isa 37:16-20](#)). Akajibu ([Isa 37:36](#)).

148. Hezekia kwa uponyaji na urefu wa siku (maneno 30; [Isa 38:3](#)). Akajibu ([Isa 38:5](#)).

Marejeleo ya maombi ([Isa 1:15](#) ; [7:11](#) ; [16:12](#) ; [26:16](#) ; [55:6-7](#)). Pia kuna maombi ambayo Israeli watafanya wakati wa kurejeshwa kwao kama taifa (Isa 12; 64).

Maombi kumi na moja katika Yeremia:

149. Yeremia, ungamo la kutoweza kumtii Mungu (maneno 12; [Yer 1:6](#)).

150. Yeremia, akimshitaki Mungu (maneno 24; [Yer 4:10](#)).

151. Yeremia kwaajili hukumu (maneno 80; [Yer 10:23-25](#)). Akajibu (Dan 5).

152. Yeremia, akimhoji Mungu (maneno 133; [Yer 12:1-4](#)).

153. Yeremia kwaajili ya msaada kwa ajili ya Yuda (maneno 95; [Yer 14:7-9](#)).

154. Yeremia kwaajili ya msaada kwa ajili ya Yuda (maneno 81; [Yer 14:20-22](#)).

155. Yeremia, hukumu (maneno 118; [Yer 15:15-18](#)).

156. Yeremia kwaajili hukumu (maneno 158; [Yer 17:13-18](#)).

157. Yeremia kwaajili hukumu (maneno 174; [Yer 18:19-23](#)).

158. Yeremia kwaajili hukumu (maneno 214; [Yer 20:7-12](#)).

159. Yeremia, kuhusu uhamisho wa Yuda (209 maneno; [Yer 32:17-25](#)).

Marejeleo ya maombi ([Yer 7:16](#) ; [11:14](#) ; [14:11](#) ; [21:2](#) ; [29:7](#) , [12](#) ; [37:3](#) ; [42:2](#) , [4](#) , [20](#)).

Maombi manne katika maombolezo:

160. Yeremia kwaajili hukumu (maneno 108; [Maombolezo 1:20-22](#)).

161. Yeremia afikiriwe (maneno 113; [Maombolezo 2:20-22](#)).

162. Yeremia kwaajili hukumu (maneno 158; [Maombolezo 3:55-66](#)).

163. Yeriaia kwaajili ya watu wa Yuda walioonewa (maneno 300; Maombolezo 5).

Yeriaia angeweza kuitwa nabii mwombezi na pia nabii Mlizi. Ana sala 15 zilizorekodiwa.

Maombi matatu katika Ezeieli:

164. Ezeieli akipinga kile ambacho Mungu alitaka afanye (maneno 41; [Eze 4:14](#)).

165. Ezeieli kwaajili ya masalia (maneno 20; [Eze 9:8](#)).

166. Ezeieli kwa mabaki (maneno 14; [Eze 11:13](#)).

Maombi mawili katika Danieli:

167. Danieli kwaajili ya msamaha wa dhambi na utimizo wa unabii (maneno 550; [Dan 9:1-19](#)).

168. Danieli kwaajili ya ufunuo (maneno 11; [Dan 12:8](#)).

Marejeleo ya maombi ([Dan 2:17-18](#) ; [6:10](#)).

Maombi mawili katika Amosi:

169. Amosi kwaajili ya msamaha (maneno 16; [Amosi 7:2](#)).

170. Amosi kwaajili ya msaada (maneno 16; [Amosi 7:5](#)).

Maombi matatu katika Yona:

171. Mabaharia kwaajili ya rehema (maneno 33; [Yona 1:14](#)).

172. Yona kwaajili ya kukombolewa kutoka kuzimu (maneno 198; [Yona 2:1-9](#)).

173. Yona kwaajili ya kifo (maneno 70; [Yona 4:2-3](#)).

Maombi matatu katika Habakuki:

174. Habakuki ili Mungu atende (maneno 75; [Hab 1:1-5](#)).

175. Habakuki kwaajili ya hukumu (maneno 156; [Hab 1:12-17](#)).

176. Habakuki kwaajili ya uamsho (maneno 474; [Hab 3:2-19](#)).

Maombi kumi na saba katika Mathayo:

177. Yesu, maombi ya Bwana (maneno 66; [Mt 6:9-13](#)).

178. Mwenye ukoma kwa uponyaji (maneno 9; [Mt 8:2](#)). Akajibu ([Mt 8:3](#)).

179. Akida kwa ajili ya uponyaji wa mtumishi wake (maneno 73; [Mt 8:6-9](#)). Akajibu ([Mt 8:13](#)).

180. Wanafunzi kupata msaada ili wasizame (maneno 5; [Mt 8:25](#)). Akajibu ([Mt 8:26](#)).

181. Pepo kupata uhuru wa muda (maneno 37; [Mt 8:29-31](#)). Akajibu ([Mt 8:32](#)).

182. Mtawala kwaajili ya uponyaji (maneno 18; [Mt 9:18](#)). Akajibu ([Mt 9:25](#)).

183. Mwanamke kwaajili ya uponyaji (maneno 11; [Mt 9:21](#)). Akajibu ([Mt 9:22](#)).

184. Vipofu wawili kwaajili ya kuponywa (maneno 8; [Mt 9:27](#)). Akajibu ([Mt 9:29-30](#)).

185. Yesu akitoa shukrani kwa Mungu (maneno 38; [Mt 11:25](#)).

186. Petro kutembea juu ya maji (maneno 13; [Mt 14:28](#)). Akajibu ([Mt 14:29](#)).

187. Petro kwaajili ya msaada wa kutozama (maneno 3; [Mt 14:30](#)). Akajibu ([Mt 14:31](#)).

188. Mwanamke kwa ajili ya uponyaji wa binti yake (maneno 36; [Mt 15:22-27](#)). Akajibu ([Mt 15:28](#)).

189. Baba kwaajili ya uponyaji wa mwanawe (39 maneno; [Mt 17:15-16](#)). Akajibu ([Mt 17:18](#)).

190. Mama kwa ajili ya kuinuliwa vyeo kwa wanawe 2, Yakobo na Yohana (maneno 23; [Mt 20:21](#)). Kutojibiwa kwa sababu ya nia mbaya na kutopatana na mpango wa Mungu ([Mt 20:23](#)).

191. Vipofu wawili kuponywa (maneno 27; [Mt 20:30-33](#)). Akajibu ([Mt 20:34](#)).

192. Yesu kuokolewa na kifo katika bustani kabla ya kufa msalabani (maneno 62; [Mt 26:39-44](#)). Akajibu ([Ebr 5:7](#)).

193. Yesu msalabani (maneno 9; [Mt 27:46](#)).

Marejeleo ya maombi ([Mt 6:5-13](#) ; [7:7-11](#) ; [Mt 14:23](#) ; [18:19-20](#) ; [21:22](#) ; [23:14](#)).

Maombi mawili katika Marko:

194. Pepo kwaajili yakupewa muda wawe huru (maneno 31; [Marko 1:23-24](#)).

195. Yesu katika kuponya bubu kiziwi (maneno 2-sala fupi zaidi; [Mk 7:34](#)). Akajibu ([Marko 7:35](#)).

Marejeleo ya maombi ([Marko 1:35](#) ; [6:41](#) , [46](#) ; [9:23](#) ; [11:22-24](#)).

Maombi saba katika Luka:

196. Simeoni katika kumbariki Yesu (maneno 43; [Luka 2:29-32](#)).

197. Tajiri akiomba atoke kwenye moto wa jeha (maneno 80; [Luka 16:24-31](#)).

198. Wakoma kumi kwa ajili ya uponyaji (maneno 5; [Luka 17:13](#)). Akajibu ([Luka 17:14](#) , [19](#)).

199. Mfarisayo katika kujivunia haki yake (maneno 34; [Lk 18:11-12](#)). Isiyo na haki ([Luka 18:14](#)).

200. Mtoza ushuru kwaajili ya rehema (maneno 7; [Luka 18:13](#)). Akajibu, amehesabiwa haki ([Luka 18:14](#)).

201. Yesu msalabani (maneno 10; [Luka 23:34](#)).

202. Yesu msalabani (maneno 8; [Luka 23:46](#)).

Marejeleo ya maombi ([Luka 3:21-22](#) ; [5:16](#) ; [6:12](#) ; [9:28-29](#) ; [11:1-13](#) ; [18:1-18](#) ; [22:31-32](#)).

Maombi matano katika Yohana:

203. Mtu mwenye nyadhifa kwaajili ya uponyaji wa mtoto (maneno 7; [Yohana 4:49](#)). Akajibu ([Yohana 4:50](#)).

204. Watu kwaajili ya mkate wa uzima (maneno 6; [Yohana 6:34](#)).

205. Yesu kwaajili ya ufufuo wa Lazaro (maneno 40; [Yohana 11:41-43](#)). Akajibu ([Yohana 11:44](#)).

206. Yesu kwa ajili ya kutukuzwa (maneno 19; [Yohana 12:27-28](#)). Akajibu ([Yohana 12:28](#)).

207. Yesu kwaajili wanafunzi (maneno 638; Yohana 17).

Marejeleo ya sala ([Yohana 7:37-39](#) ; [14:12-15](#) ; [15:7](#) , [16](#) ; [16:23-26](#)).

Maombi sita katika Matendo:

208. Wanafunzi kwaajili ya mrithi wa Yuda (maneno 41; [Matendo 1:24-25](#)). Akajibu ([Matendo 1:26](#)).

209. Petro kwaajili ya uponyaji wa kiwete (maneno 12; [Matendo 3:6](#)). Akajibu ([Matendo 3:7-8](#)).

210. Wanafunzi kwaajili ujasiri na uwezo (maneno 178; [Matendo 4:24-30](#)). Akajibu ([Matendo 4:31-33](#)).

211. Stefano kwa ajili ya maadui (maneno 13; [Matendo 7:59-60](#)).

212. Paulo kwa mafundisho (maneno 12; [Matendo 9:5-6](#)). Akajibu ([Matendo 9:5-6](#)).

213. Petro kwa ufufuo wa Tabitha (maneno 2; [Matendo 9:40](#)). Akajibu ([Matendo 9:40-41](#)).

Marejeleo ya maombi ([Matendo 1:14](#) ; [3:1](#) ; [6:4](#) ; [8:22](#) , [24](#) , [34](#) ; [10:9](#) , [31](#) ; [12:5](#) ; [16:13-16](#)).

Ombi Moja katika 3 Yohana:

214. Ili sisi wasomaji tufanikiwe na kuwa na afya kadri nafsi zetu zinavyofanikiwa (maneno 18; 3 Yoh.

Sala nane katika Ufunuo:

215. Wazee katika ibada (maneno 27; [Ufu 4:11](#)).

216. Malaika katika ibada (maneno 22; [Ufu 5:12](#)).

217. Viumbe vyote katika ibada (maneno 22; [Ufu 5:13](#)).

218. Wafia imani kwaajili ya kulipiza kisasi (maneno 22; [Ufu 6:10](#)).

219. Umati mkubwa katika ibada (maneno 13; [Ufu 7:10](#)).

220. Malaika katika ibada (maneno 23; [Ufu 7:12](#)).

221. Watakatifu waliotukuzwa katika ibada (maneno 56; [Ufu 19:1-6](#)).

222. Yohana kwaajili kuja kwa Yesu Kristo mara ya pili, maneno 5 ([Ufu 22:20](#)).

Kando na sala halisi zilizo katika vitabu hivi 31 vya Biblia, kuna mafungu vilevile katika baadhi ya vile vitabu 35 ambavyo havina sala, vinavyotoa maagizo mengi kuhusu sala. Inafikiriwa na wengine kwamba kuna idadi ya sala kadhaa katika nyaraka, lakini kwa kweli, vitabu hivi vina maneno tu kwa Wakristo, kuhusu mitume kuwaombea ili Mungu awabariki, au hutoa maagizo kwa Wakristo kuomba na kuwaambia nini cha kuomba. Tunavyoona haya sio maombi halisi yanayoelekezwa kwa Mungu, hata hivyo ([Rum 1:8-10](#) ; [16:20](#) ; [Efe 1:15-20](#) ; [3:13-21](#) ; [Flp 1:2-7](#) ; [Kol 1:3-14](#) ; [1 Wathesalonike 1:2-3](#) ; [3:9-13](#) ; [3:1-13](#) ; [3:3-13](#) ; [3:1-13](#) ; [4:14-18](#) ; [Yakobo 5:13-18](#)).

Vitabu Thelathini na tano Ambapo neno Sala halijatajwa Moja kwa Moja

1. Mambo ya Walawi
2. Ruthu
3. Esta
4. Methali
5. Mhubiri
6. Wimbo Ulio Bora
7. Hosea
8. Yoeli
9. Obadia
10. Mika
11. Nahumu
- 12.
- Sefania 13. Hagai

14.
Zekaria
14. Zekaria
1
Wakorintho 15.]
19. Wagalatia
20. Waefeso
21. Wafilipi
22. Wakolosai
23. 1 Wathesalonike
24. 2 Wathesalonike
25. 1Timotheo
26. 2Timotheo
27. Tito
28. Filemoni
29. Waebrania
30. Yakobo
31. 31. 2 Yohana
32.
1 Yohana
32. 2 Yohana 3 Petro.

Muhtasari wa Kitabu Njia Salama-Ninawezaje Kuja Kwa Kristo? **Sehemu ya Kwanza**

Asili na ufunuo wa Mungu kwa wanadamu, vyote kwa pamoja hushuhudia upendo wa Mungu. Ni uvunjaji (uasi) wa Sheria ya Mungu, Sheria ya upendo, ndio imeleta misiba na kifo. Lakini hata katikati ya mateso yanayotokana na dhambi, upendo wa Mungu unafunuliwa. “Mungu ni upendo” imeandikwa juu ya kila chipukizi, juu ya kila unyasi unaochipuka.

Masihi alikuja kuishi miongoni mwa wanadamu ili kudhihirisha upendo wa Mungu usio na kikomo. Upendo, rehema, na huruma zilikuwa zimefunuliwa katika kila tendo la maisha Yake; Moyo Wake ulikwenda kwa huruma nyororo, mapenzi mwanana, na kujali, kwa watoto wa wanadamu. Alichukua asili ya mwanadamu, ili Aweze kufikia matakwa ya mwanadamu. Maskini na wanyenyekevu zaidi hawakuogopa kumkaribia Yeye. Hiyo ndiyo tabia ya Kristo kama inavyofunuliwa katika maisha Yake. Hii ndiyo tabia ya Mungu.

Ilikuwa ni kwa ajili ya kutukomboa ndiyo maana Yesu aliishi, aliteseka,

na kufa. Alifanyika “Mtu wa Huzuni,” ili sisi tupate kufanywa washirika wa furaha ya milele. Lakini dhabihu hii kuu haikutolewa ili kuunda katika Moyo wa Baba upendo kwa mwanadamu, sio kumfanya awe tayari kutuokoa. Hapana, hapana! “Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe pekee.” Yohana 3:16. Baba anatupenda, sio kwa sababu ya upatanisho mkuu, bali Yeye Alitoa upatanisho kwa sababu anatupenda. Hakuna mwingine ila Mwana wa Mungu Ndiye Ambaye angeweza kutimiza ukombozi wetu.

Hii inaweka thamani iliyoje kwa mwanadamu! Kupitia uasi, wana wa wanadamu wanakuwa raia wa Shetani. Kupitia imani katika dhabihu ya upatanisho ya Kristo, wana wa Adamu wanaweza kuwa wana wa Mungu. Upendo usio na kifani wa Mungu kwa ulimwengu ambao haukumpenda! Mawazo yana nguvu ya kutiisha juu ya nafsi na huleta akili katika utumwa wa mapenzi ya Mungu.

Mwanadamu hapo awali alijaliwa uwezo bora na akili iliyo na utimamu mzuri. Alikuwa mkamilifu katika nafsi yake, na mapatano na Mungu. Mawazo yake yalikuwa safi, malengo yake yalikuwa matakatifu. Lakini kwa kutokutii, nguvu zake zilipotoshwa, na ubinafsi ukachukua nafasi ya upendo. Asili yake ilidhoofika sana kupitia dhambi ambayo haikuwezekana kwake, kwa nguvu zake mwenyewe, kupinga nguvu za uovu.

Haiwezekani sisi, naam, sisi wenyewe, kuepuka shimo la dhambi ambalo tumezama ndani yake. Mioyo yetu ni miovu, na hatuwezi kujibadilisha. Lazima kuwe na nguvu inayofanya kazi kutoka ndani, maisha mapya kutoka juu, kabla ya sisi wanadamu kubadilishwa kutoka katika dhambi hadi utakatifu. Nguvu hiyo ni Kristo. Neema Yake pekee ndiyo inayoweza kuhuisha uwezo usio na uhai wa nafsi, na kutuvuta kwa Mungu, kwa utakatifu. Kwa wote, kuna jibu moja tu, Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu.” Yohana 1:29. Hebu na tuikubali njia hii iliyotolewa kwa ajili yetu ili tuweze kugeuzwa na kufanana Naye, na kurejeshwa katika ushirika na malaika wanaohudumia, kwa maelewano na ushirika na Baba na Mwana.

Mtu atakuwaje mwenye haki mbele za Mungu? Mwenye dhambi atafanywaje kuwa mwadilifu? Ni kwa njia ya Kristo pekee tunaweza kuletwa katika mapatano na Mungu, kwa utakatifu; lakini tunawezaje kumwendea Kristo?

Toba ni pamoja na huzuni kwa ajili ya dhambi na kuiacha. Hatutaacha dhambi mpaka tuone ubaya wake; mpaka tuiache kwa moyo, hakutakuwa na mabadiliko ya kweli katika maisha. Lakini moyo unapokubali kuongozwa na Roho wa Mungu, dhamiri itahuishwa, na mwenye dhambi atatambua jambo fulani la kina, na utakatifu wa Sheria takatifu ya Mungu, na msingi Wa serikali Yake mbinguni na duniani. Kisha usadikisho hushika akili na moyo.

Ombi la Daudi, baada ya anguko lake, linaonyesha asili ya huzuni ya kweli kwa ajili ya dhambi. Toba yake ilikuwa ya dhati na ya kina. Hakukuwa na jitihada za kutuliza hatia yake; hakuwa na hamu ya kutoroka hukumu inayomtishia ila aliongozwa katika maombi yake. Daudi aliona ukubwa wa kosa lake; aliona unajisi wa nafsi yake; yeye aliichukia dhambi yake. Haikuwa kwa ajili ya msamaha tu kwamba aliomba, lakini kwa ajili ya usafi wa moyo. Alitamani furaha ya utakatifu, kurejeshwa katika maelewano na ushirika na Mungu. Toba kama hii haiwezi kufikiwa na uwezo wetu wenyewe na kuikamilisha; bali hupatikana tu kutoka Kristo.

Kristo Yuko tayari kutuweka sisi huru kutokana na dhambi, lakini halazimishi nia hiyo. Tukikataa, Je, Yeye anaweza kufanya nini zaidi? Jifunze Neno la Mungu kwa maombi. Unapona ukubwa wa dhambi maishani mwako, kama unavyojiona jinsi ulivyo, usikate tamaa kwa kupoteza matumaini. Ni wenye dhambi ndio ambao Kristo alikuja kuwaokoa. Shetani anapokuja kukuambia kuwa wewe ni mwenye dhambi mkuu, wewe mtazame Mkombozi wako na uongee juu ya wema Wake. Ikiri dhambi yako, lakini mwambie adui kwamba “Kristo alikuja ulimwenguni kuwaokoa wenye dhambi” ili mimi nipate kuokolewa (1 Timotheo 1:15).

“Afichaye dhambi zake hatafanikiwa, bali yeye aziungamaye na kuziacha atapata rehema.” Mithali 28:13. Masharti ya kupata rehema ya Mungu ni rahisi na ya haki na busara. Ungameni dhambi zenu kwa Mungu, Ambaye peke Yake Ndiye anayeweza kuwasamehe, na msameheane makosa yenu ninyi kwa ninyi. Wale ambao hawajanyenyekesha nafsi zao mbele za Mungu, kwa kukiri hatia yao, bado hawajatimiza hatua ya kwanza ya kukubalika, kwani sharti tuwe tayari kuinyenyekesha mioyo yetu na kufuata masharti ya Sheria ya Neno la Kweli. Kukiri ambako kunamiminiwa kwa roho ya ndani hupata njia yake kwa Mungu wa huruma Asiye na kikomo. Kuungama kwa kweli

siku zote huwa na tabia maalum, na hukubali dhambi fulani. Maungamo yote yanapaswa kuwa ya uhakika na ya kulenga jambo mahususi. Imeandikwa, “Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.” 1John 1:9.

Ahadi ya Mungu ni, “Mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa mioyo yenu yote.” Yeremia 29:13. Moyo wote sharti utolewe, au mabadiliko hayawezi kamwe kufanywa ndani yetu ambayo kwayo tunapaswa kurejeshwa kwa mfano Wake Bwana.

Vita dhidi ya nafsi ni vita kubwa zaidi kuwahi kupiganwa. Kujitolea kwa nafsi, kusalimisha Mapenzi yetu yote kwa Mungu, kunahitaji mapambano; lakini nafsi inapaswa kunyenyekea kwa Mungu kabla ya kufanywa upya katika utakatifu. Katika kujitoa kwa Mungu, ni lazima kuacha yote ambayo yangetutenganisha Naye. Kuna wale wanaodai kumtumikia Mungu huku wakitegemea juhudi zao wenyewe kutii Sheria Yake, ili kuunda tabia sahihi na kupata wokovu. Mioyo yao haiguswi na hisia yoyote ya kina ya upendo wa Kristo, lakini wanatafuta kutekeleza majukumu ya maisha ya Kikristo kama vile ambavyo Mungu anataka kutoka kwao ili kuipata mbingu. Dini kama hiyo haina thamani.

Kristo akikaa ndani ya moyo, roho itajawa na upendo Wake, na furaha ya kuungana Naye, kwamba roho itashikamana Naye; na katika kumfikiria Yeye, nafsi itasahauliwa. Upendo kwa Mwenyezi Mungu utakuwa chemchemi ya kila wazo na tendo. Mambo hayo hayalengi viwango vya chini kabisa, bali hulenga kupatana kikamilifu na Mapenzi ya Mkombozi wao.

Je, unahisi kwamba ni dhabihu kubwa sana kwako kutoa yote kwa Kristo? Jiulize swali, “Ni nini Kristo ametoa kwa ajili yangu?” Mwana wa Mungu alitoa maisha yake yote, kwa upendo na akapitia mateso kwa ajili ya ukombozi wetu. Je, sisi, tusiostahili, ambao ni walengwa wa upendo mkuu hivyo, tutazuia mioyo yetu Kwake? Je, Tunatoa nini zaidi wakati tunatoa yote? Ni Moyo uliochafuliwa na dhambi tu, ndiyo tunatoa na hakuna lingine la thamani tunalolitoa kwa Mungu, tunautoa moyo huu, ili Yesu ausafishe, ausafishe kwa damu Yake Mwenyewe, na kutuokoa kwa upendo Wake usio na kifani. Na ajabu ni kwamba, bado watu wanafikiri ni vigumu kuacha yote! (na kumbe kile tunachokiacha ni moyo mchafu tu). Mungu hataki tutoe chochote ambacho ni cha manufaa kwetu ili tubaki salama. Katika yote anayofanya, Yeye ana maslahi ya

watoto Wake katika mtazamo Wake.

Wengi wanauliza, “Nifanyeje ili kujisalimisha kikamilifu kwa Mungu?” Unatamani kujitoa Kwake, lakini u dhaifu katika uwezo wa kimaadili, kisha una utumwa wa mashaka, na unatawaliwa na tabia za maisha ya dhambi. Ahadi na maazimio yako ni kama kamba za mchanga. Huwezi kudhibiti mawazo yako, misukumo yako, na mapenzi yako. Ujuzi ulio nao kuhusu ahadi zako zilizovunjwa na ahadi ulizopoteza hudhoofisha kujiamini kwako katika unyofu wako mwenyewe, na kukufanya uhisi kwamba Mungu hawezi kukukubali; lakini huna haja kukata tamaa.

Unachohitaji kuelewa ni nguvu ya kweli ya uthubutu (uchaguzi). Hii ndiyo nguvu inayotawala katika asili ya mtu, nguvu ya uamuzi, au ya kuchagua. Kila kitu kinategemea hatua sahihi ya uthubutu. Nguvu ya uhuru wa kuchagua ambao Mungu amewapa wanadamu; ni juu ya hii unapaswa kuifanyia mazoezi. Huwezi kubadilisha moyo wako, na huwezi kujibadili wewe mwenyewe, kwahiyo mpe Mungu mapenzi (matamano) ya moyo wako; lakini unaweza kuchagua kumtumikia. Unaweza kumpa mapenzi yako; Naye Atafanya kazi ndani yako, kunia na kutenda sawasawa na mapenzi Yakemema. Kwa hivyo asili yako yote itaweza kuletwa chini ya udhibiti wa Roho wa Kristo; mapenzi yako yataelekezwa Kwake, mawazo yako yatakuwa sawa na Yeye.

Matamano ya kuwa na wema na utakatifu ni sawa kadiri yanavyokwenda; lakini ukiishia hapa, hautafaidika kwa chochote. Wengi watapotea huku wakitumaini na kutamani kuwa Wakristo. Hawafikii hatua ya kuweka mapenzi yao kwa Mungu. Hawachagui sasa kuwa Wakristo.

Kupitia mazoezi sahihi ya uthubutu, mabadiliko yote yanaweza kufanywa katika maisha yako. Utakuwa na nguvu kutoka juu ili kukuweka imara, na hivyo kupitia kuendelea kujitoa daima kwa Mungu utawezeshwa kuishi maisha mapya, hata maisha ya imani.

Kwa vile dhamiri yako imehuishwa na Roho Mtakatifu, umeona kitu juu ya uovu/ubaya wa dhambi, na nguvu zake, hatia yake, na majanga yake; na sasa unaitazama dhambi kwa chuki. Ni amani ndiyo unayohitaji. Umeungama dhambi zako, na kuziweka mbali na moyo wako. Umeamua kujitoa kwa Mungu. Sasa nenda Kwake, na umwombe kwamba akuoshe dhambi zako na kukupa moyo mpya.

Basi amini kwamba Yeye Anafanya hivi kwa sababu ameahidi hivyo.

Zawadi ambayo Mungu anatuahidi, ni sharti tuamini kwamba tunaipokea, na kwamba ni zetu. Wewe ni mwenye dhambi. Huwezi kulipia dhambi zako zilizopita; huwezi kuubadili moyo wako na kujifanya kuwa mtakatifu. Lakini Mungu anaahidi kufanya haya yote kwa ajili yako kupitia Kristo. Wewe amini tu ahadi hiyo. Tubu dhambi zako na kujitoa kwa Mungu. Utapenda kumtumikia. Vile vile unapofanya hivi, hakika Mungu atatimiza Neno Lake kwako. Ikiwa unaamini katika ahadi hiyo, Mungu anaitoa kwako kweli (kiuhalisia). Usisubiri mpaka uhisi kuwa umefanywa mzima, lakini sema, “Naamini; ni hivyo, si kwa sababu ninaihisi, bali kwa sababu Mungu “Aliahidi.”

Sehemu ya Pili

Je, ninawezaje Kubaki Mkweli kwa Kristo?

Yesu anasema, “Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.” Marko 11:24. Kuna sharti kwa ahadi hii - kwamba tuombe sawasawa na Mapenzi ya Mungu. Lakini ni Mapenzi ya Mungu kutusafisha na dhambi zetu, kutufanya watoto Wake, na kutuwezesha kuishi maisha matakatifu. Hivyo tunaweza kuomba baraka hizi, na kuamini kwamba tunazipokea, na kumshukuru Mungu kwamba tumepokea ahadi hizo.

Tangu sasa ninyi si mali yenu wenyewe; mmenunuliwa kwa bei kubwa. Kupitia tendo hili rahisi la kumwamini Mungu, Roho Mtakatifu amezaa maisha mapya ndani ya moyo wako. Wewe ni mtoto aliyezaliwa katika familia ya Mungu, na Yeye anakupenda kama vile anavyompenda Mwanawe.

Sasa kwa kuwa umejitoa kwa Yesu, usirudi nyuma tena, usijiondoe Kwake, lakini siku baada ya siku sema, “Mimi ni wa Kristo, nimejitoa Kwake,” na umwombe Akupe Roho Wake ili Akutunze kwa neema Yake. Kama ilivyo, unapojitoa kwa Mungu, na kumwamini, basi, unakuwa mtoto Wake, ndivyo na wewe wanapaswa kuishi ndani Yake.

Hapa ndipo maelfu wanaposhindwa; hawaamini kwamba Yesu anasamehe kila nafsi, yaani mtu mmoja mmoja. Hawamtilii maanani Mungu katika Neno Lake. Ni fursa ya wote wanaotii masharti kujua wenyewe kwamba msamaha unatolewa kwa kila dhambi. Ondoa shaka kwamba ahadi za Mungu hazikukusudiwa kwa ajili yako. Ahadi za Mungu zipo kwa ajili ya kila nafsi inayotubu. Inueni macho juu, ninyi

wenye mashaka na kutetemeka; kwa maana Yesu Yu hai ili atuombee. Mshukuruni Mungu kwa ajili ya zawadi ya Mwanawe mpendwa.

“Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya, ya kale yamepita; tazama, mambo yote yamekuwa mpya.” 2 Wakorintho 5:17. Huenda mtu asiweze kutaja wakati au mahali hasa, au kufuatilia mlolongo wote kwamba mambo yalikuwaje katika huu mchakato wa uongofu; lakini hii haithibitishi kuwa wewe haujaongoka.

Mabadiliko yataonekana katika mwenendo, tabia, na utendaji wako. Tofauti itakuwa wazi na kuamuliwa kati ya vile ambavyo ulivyo sasa na ulivyokuwa. Nani ana moyo wako? Mawazo yetu yanamilikiwa na nani? Je, tunapenda kuzungumza juu ya nini au nani? Ni nani aliye na upendo wetu makini na nguvu zetu bora zaidi? Ikiwa sisi ni wa Kristo, mawazo yetu yapo pamoja Naye. Hakuna uthibitisho wa toba ya kweli isipokuwa inafanya kazi ya matengenezo.

Uzuri wa tabia ya Kristo utaonekana kwa wafuasi Wake. Ilikuwa furaha Yake Masihi kufanya Mapenzi ya Mungu. Kuna makosa mawili ambayo watoto wa Mungu hasa wanatakiwa kujilinda nayo: La kwanza ni lile la kujivunua kazi zao wenyewe, kujiamini kuwa wao wanaweza kufanya kitu fulani, ili kuweza kujileta wenyewe katika mapatano na Mungu. Yote ambayo mwanadamu anaweza kufanya bila Kristo yamechafuliwa na ubinafsi na dhambi. Ni neema ya Kristo pekee, kwa njia ya imani, ndiyo ambayo inaweza kutufanya watakatifu.

Kosa la pili lililo kinyume na la hatari ni kwamba watu huamini kwamba imani katika Kristo huwaachilia wanadamu kutoka katika kuishika Sheria ya Mungu; kwamba kwa kuwa na imani pekee tunakuwa washiriki wa neema ya Kristo, matendo yetu hayana la kufanya katika suala la ukombozi wetu.

Utii ni tunda la imani. Haki inafafanuliwa kwa kiwango cha Sheria takatifu ya Mungu, kama inavyoonyeshwa katika zile Amri kumi (Kutoka 20:3-20). Kile kinachoitwa imani katika Kristo ambacho kinadai kuachilia watu kutoka katika wajibu wa utii kwa Mungu, sio imani, lakini ni kiburi na uelewa ulio na makosa. Sharti la uzima wa milele, kama lilivyo sasa ndivyo lilivyokuwa siku zote - kama ilivyokuwa katika edeni (au paradiso) kabla ya anguko la wazazi wetu wa kwanza, sharti hilo ni Utii mkamilifu kwa Sheria ya Mungu, ambayo ndiyo uadilifu mkamilifu.

Ikiwa uzima wa milele ungetolewa kwa sharti lolote pungufu ya hili, basi ni furaha ya sayari zote na mbingu imo hatarini. Njia ingelifunguliwa

wazi kwa ajili ya dhambi, pamoja na msururu wake wote wa misiba na taabu, hata kama watu hawafi.

Kristo anabadilisha moyo. Anakaa moyoni mwetu kwa imani. Tunapaswa kudumisha uhusiano huu na Kristo kwa imani na kujitoa daima kwa mapenzi yetu Kwake; na mradi unafanya hivi, Yeye atafanya kazi ndani yake kutaka na kutenda kulingana na mapenzi Yake mema.

Kadiri unavyomkaribia Masihi, ndivyo utakavyoona ulivyo na makosa zaidi machoni pako; maana maono yako yatakuwa wazi zaidi. Huu ni ushahidi kwamba udanganyifu wa Shetani unapoteza nguvu zake. Hakuna upendo wa kina kwa Yesu unaoweza kukaa katika moyo ambao hautambui dhambi yake wenyewe. Nafsi inayogeuzwa kwa neema ya Kristo itapendezwa na tabia Yake Mungu. Mtazamo wa dhambi zetu unasukuma na Yeye anayeweza kusamehe; na wakati nafsi, inatambua unyonge wake, na kumfikia Kristo, Yeye atajidhihirisha kwa uwezo Wake. Kadiri hisia za kumhitaji zinavyotusukuma Kwake na kwa Neno la Mungu, ndivyo tutakavyokuwa na mitazamo iliyotukuka zaidi juu ya tabia Yake, na kwa ukamilifu zaidi tutaiakisi sura Yake.

Badiliko la mioyo ambalo kwalo tunafanyika kuwa wana wa Mungu linapatikana katika Biblia kama kuzaliwa. Tena linalinganishwa na kuota kwa mbegu nzuri iliyopandwa na mkulima. Ni Mungu Ndiye anayeleta chipukizi la majani kutokea na kisha ua, na mwishowe matunda. Ni kwa uwezo Wake mbegu hukua. Kama vile Ua linavyoligeukia jua, ili miale yake angavu isaidie katika ukamilifu mzuri na ulinganifu wake; ndivyo sisi tutakiwavyo kuligeukia Jua la Haki, ili nuru ya mbinguni iangaze juu yetu, ili tabia zetu ziweze kukuzwa katika kufanana na Kristo.

Je, unauliza, "Ninawezaje kukaa ndani ya Kristo?" Kama jinsi ulivyompokea Kristo hapo kwanza. "Basi kama mlimpokea Kristo Yesu, Bwana, enendeni vivyo hivyo katika Yeye." Wakolosai 2:6. Kwa imani wewe ukawa Wake Kristo; na kwa imani unapaswa kukua ndani Yake kwa kutoa na kupokea. Unapaswa kutoa yote, moyo wako, mapenzi yako, huduma yako, hebu jitoe Kwake ili kutii matakwa Yake yote; nawe sharti uvibebe vyote, yaani umchukue Kristo (Ambaye Ndiye vyote), Ambaye ni utimilifu wa baraka zote, Naye Akae moyoni mwako, Awe nguvu yako, Awe haki yako, na Msaidizi wako wa milele wa kukupa uwezo wa kutii.

Jiweke wakfu kwa Mungu asubuhi; fanya hii iwe kazi yako ya kwanza kabisa. Ombi lako liwe, Nitwae, Ee Bwana, niwe Wako kabisa. Ninaweka

mipango yangu yote miguuni Pako. Nitumie leo katika huduma Yako. Kaa nami, na kazi yangu yote na itimizwe ndani yako.” Niepushe kuyafanya yale ambayo sipaswi kuyafanya, na kuyafanya yale ambayo napaswa kufanya. Hili ni jambo la kila siku. Kila asubuhi jiweke wakfu kwa Mungu kwa ajili ya siku hiyo. Peleka mipango yako yote Kwake, ili itekelezwe au iache kutokana na majaliwa Yake yatakavyoonyesha. Hivyo siku baada ya siku unaweza kuendelea ku yatoa maisha yako mikononi mwa Mungu, na hivyo maisha yako yatafinyangwa zaidi na zaidi kufanana na maisha ya Kristo.

Maisha ndani ya Kristo ni maisha ya utulivu. Kunaweza kuwa hakuna furaha yenye mihemko ya hisia, lakini kunapaswa kuwa na uvumilivu wa kuendelea kudumu katika Imani yenye matumaini. Wakati akili inapokaa juu ya ubinafsi, inageuzwa mbali na Kristo, Aliye chanzo cha nguvu na uhai. Kwa hivyo, ni juhudi ya mara kwa mara ya Shetani kutoa usikivu kutoka kwa Mwokozi na hivyo kuzuia muungano na ushirika wa roho na Kristo.

Kristo alipotwaa asili ya mwanadamu juu Yake, Aliufungamanisha ubinadamu Kwake kwa kifungo cha upendo ambacho hakiwezi kamwe kuvunjwa na mamlaka yoyote, isipokuwa chaguo la mwanadamu mwenyewe. Shetani ataendelea kuweka vivutio vya kutushawishi kuvunja uhusiano huu yaani kuchagua kujitenga na Kristo. Lakini wacha tuendeleo kuinua macho yetu kumtazama Kristo, Naye atatuhifadhi. Tukimtazama Masihi, tuko salama. Hakuna kinachoweza kutung'oa kutoka mkononi Mwake. Yote ambayo Kristo alikuwa kwa wanafunzi, anatamani yawe kwa watoto Wake leo.

Yesu alituombea, na aliomba kwamba tuwe na umoja Naye, kama vile Yeye alivyo mmoja na Baba. Huu ni muungano wa thamani kiasi gani! Hivyo, tukimpenda na kukaa ndani Yake, “Tutakua hata tumfikie Yeye katika yote, Yeye Aliye kichwa, Kristo.” Waefeso 4:15.

Mungu Ndiye chanzo cha uhai na nuru na furaha kwa ulimwengu. Popote uzima wa Mungu unapokuwepo ndani ya mioyo ya watu, uzima huo utatiririka kwa wengine kwa upendo na baraka.

Furaha ya Mwokozi wetu ilikuwa katika kuinuliwa na ukombozi wa wanadamu walioanguka. Kwa hili hakuyahesabu maisha Yake kuwa ya thamani Kwake Yeye Mwenyewe, bali aliustahimili msalaba na kuidharau aibu. Wakati upendo wa Kristo umo ndani ya moyo, ni kama

manukato au harufu nzuri isiyoweza kufichwa. Upendo kwa Yesu utadhihirika katika hamu ya kufanya kazi kama Yeye alivyofanya kazi kwa ajili ya baraka na kuinuliwa kwa ubinadamu. Upendo kwa Kristo huleta mwitikio wa upendo, rehema, na huruma yenye mguso kwa viumbe vyote ambavyo Baba yetu wa mbinguni Anavitunza. Wale walio washiriki wa neema ya Kristo watakuwa tayari kutoa dhabihu yoyote, ili wengine aliowafia wapate kushiriki zawadi ya mbinguni. Watafanya yote wawezayo kufanya duniani, ili dunia iwe mahali bora zaidi katika kukaa kwao humo. Roho hii ndiyo chanzo cha uhakika cha nafsi iliyoongoka kweli kweli. Mara tu mtu anapokuja kwa Kristo ndipo unazaliwa ndani ya moyo wake, hamu ya kufanya Kristo ajulikane kwa wengine na kwamba ni urafiki wa thamani gani ameupata kwa Yesu (In Jesus I found a friend). Ikiwa tumeonja na kuona kwamba Bwana ni mwema, tutakuwa na kitu cha kusema. Tutajaribu kuwasilisha kwa wengine vivutio vya Kristo na mambo yasiyoonekana ya ulimwengu ujao. Kutakuwa na nguvu yenye matamano makubwa katika kufuata njia ambayo Yesu aliipita.

Na jitihada za kuwabariki wengine zitaleta mwitikio wa baraka juu yetu wenyewe. Wale ambao wanakuwa washiriki katika kazi ya upendo, huletwa karibu zaidi na Muumba wao. Roho ya kufanya kazi bila ubinafsi kwa ajili ya wengine hutoa kina, uthabiti, na kuwa na tabia ya kupendeza kama Kristo kwa mhusika, na kisha huleta amani na furaha kwa mhusika (mtoaji). Nguvu huja kwa kujizoeza. Hatuhitaji kwenda katika nchi za kipagani, au hata kuacha mazingira ya nyumba zetu, ikiwa hapo ni pale ambapo wajibu wetu uko, ili kufanya kazi kwa ajili ya Kristo. Kwa roho ya upendo tunaweza kufanya kazi kwa unyenyekevu katika maisha “kwa Bwana.” Wakolosai 3:23. Ikiwa upendo wa Mungu umo moyoni, utadhihirika katika maisha yetu. Haupaswi kungojea hafla nzuri au kutarajia uwezo wa ajabu kabla ya kwenda kufanya kazi kwa ajili ya Mungu. Wanafunzi wanyenyekevu na maskini zaidi wa Yesu wanaweza kuwa baraka kwa wengine wakati wote.

Kuna njia nyingi ambazo Mungu anatafuta kujitambulisha kwetu na kutuleta katika ushirika pamoja Naye. Ikiwa tutasikiliza tu, Asili huzungumza na hisia zetu bila kukoma. Kazi zilizoumbwa na Mungu zitatufundisha masomo ya thamani ya utii na uaminifu.

Hakuna machozi yanayotolewa ambayo Mungu hayatambui. Hakuna mwenendo asioutia alama. Kama tungeweza kumwamini kikamilifu,

mahangaiko yote yasiyofaa yangetupiliwa mbali. Maisha yetu yasingejazwa na kukata tamaa kama ilivyo sasa; kwa maana kila kitu, kiwe kikubwa ama kidogo, kingeachwa mikononi mwa Mungu.

Mungu huzungumza nasi kupitia kazi Zake na majaliwa na kupitia ushawishi wa Roho Wake juu ya moyo yetu. Mungu anazungumza nasi katika Neno Lake. Hapa tunayo mistari iliyo wazi zaidi ya ufunuo wa tabia Yake, kushughulika Kwake na wanadamu, na kazi kuu ya ukombozi. Jaza moyo wote kwa Neno la Mungu. Neno ni maji yaliyo hai, yakizima kiu yako iwakayo. Neno ni mkate wa uzima kutoka mbinguni.

Siri ya ukombozi ni jambo ambalo malaika wanatamani kuliangalia na kulijua ila ni fumbo na siri; ukombozi wa mwanadamu itakuwa ndiyo sayansi na wimbo wa waliokombolewa katika enzi zote zisizo na kikomo za milele. Kama ni hivyo, Je, haifai basi tufikirie sasa kwa makini na kujifunza leo hii? Tunapotafakari juu ya Mwokozi, kutakuwa na njaa na kiu ya nafsi ya kuwa kama Yeye Ambaye tunamwabudu.

Biblia iliandikwa kwa ajili ya watu wa kawaida. Kweli kuu zinazohitajika kwa wokovu zinafanywa wazi kama mchana. Hakuna kitu kinachohesabiwa kuimarisha akili kuliko kujifunza Maandiko Matakatifu. Lakini kuna faida kidogo inayopatikana kwa kusoma Biblia haraka-haraka. Fungu moja likisomwa kwa makini hadi tukagundua umuhimu kwa akili zetu na uhusiano wake, na mpango wa wokovu ukawa dhahiri, huu ndio usomaji wa thamani zaidi kuliko usomaji wa sura nyingi bila malengo dhahiri na hakuna maagizo chanya yaliyopatikana.

Weka Biblia yako pamoja nawe. Upatapo nafasi, isome; yaweke maandishi kwenye kumbukumbu yako. Hatuwezi kupata hekima bila uangalifu wa dhati na kujifunza kwa sala.

Kamwe Biblia haipaswi kusomwa bila maombi. Kabla ya kufungua kurasa Zake, tunapaswa kuomba nuru ya Roho Mtakatifu, nayo itatolewa. Malaika kutoka katika ulimwengu wa nuru watakuwa pamoja na wale ambao kwa unyenyekevu wa moyo wanatafuta mwongozo wa Mwenyezi Mungu. Je, ni kwa jinsi gani Mungu anawathaminiwanadamu? Yeye alimtoa Mwanawe ili afe kwa ajili yao na anamtuma Roho Wake Mtakatifu kuwa mwalimu wa mwanadamu, Naye ni kiongozi wa kudumu!

Kupitia asili na ufunuo, kupitia majaliwa Yake, na kwa ushawishi wa Roho Wake, Mungu anazungumza nasi. Lakini haya hayatoshi; tunahitaji pia kumimina mioyo yetu Kwake. Ili kuwasiliana na Mungu, sharti tuwe

na kitu cha kumwambia kuhusu maisha yetu halisi, maisha ya kila siku. Maombi ni kufungua moyo kwa Mungu kama kwa rafiki. Sio kwamba ni sharti tumjulisha Mungu mambo yalivyo kwetu, bali ni ili Atuwezeshe kumpokea Yeye mioyoni mwetu. Maombi hayamshushi Mungu kwetu, lakini maombi hutupeleka juu Kwake.

Baba yetu wa mbinguni anasubiri kutupa utimilifu wa baraka Zake. Inashangaza kiasi gani kwamba sisi tunaomba kidogo sana! Mungu Yuko tayari kutubariki na Anawiwa kusikia maombi ya dhati ya watoto Wake walio wanyenyekevu zaidi. Malaika wa mbinguni wanashangaa wanapofikiria juu ya wanadamu maskini wasiojiweza, ambao wako chini ya majaribu, nao wanaomba kidogo sana na wana imani ndogo sana, wakati Moyo wa Mungu wenye upendo usio na kikomo una matamano nao, Naye Yupo tayari kuwapa zaidi ya vile wanavyoweza kuomba au kufikiria.

Giza la mwovu linawafunika wale wanaopuuza kuomba. Majaribu ya kunong'ona ya adui huwashawishi wanadamu kutenda dhambi; na yote ni kwa sababu hawatumii fursa ya maombi. Walakini maombi ndio ufunguo katika mkono wa imani kufungua ghala ya mbinguni, ambapo rasilimali zisizo na kikomo za Mweza wa yote zinatunzwa.

Kuna masharti fulani ambayo kwayo tunaweza kutarajia kwamba Mungu atasikia na kujibu maombi yetu: Moja ni kwamba tunahisi hitaji letu la msaada kutoka Kwake. Tukiwaza maovu mioyoni mwetu, tukishikamana na dhambi yoyote tuijuayo; Bwana hatatusikia; lakini sala ya mtu aliyetubu na aliyeungama hukubaliwa daima. Wakati wote makosa yanayojulikana yanaposahihishwa, tunaweza kuamini kwamba Mungu atajibu maombi yetu.

Kipengele kingine cha maombi yenye nguvu ni imani. Wakati maombi yetu yanaonekana kutojibiwa, tunapaswa kushikilia kwa bidii ahadi Zake; kwani wakati wa kujibiwa utakuja hakika, na tutapokea baraka tunazozihitaji zaidi. Lakini kudai kwamba maombi daima yatajibiwa kwa namna tutakavyo na kila kitu tunachokitamani ni dhana za kufikirika.

Tunapokuja kwa Mungu katika maombi, tunapaswa kuwa na roho ya upendo na msamaha ndani ya mioyo yetu wenyewe. Kuendelea kudumu katika maombi kumefanywa kuwa sharti la kupokea majibu yetu. Sharti tuombe kila wakati ikiwa tunataka kukua katika imani na uzoefu.

Tunapaswa kuomba katika mzunguko wa familia, na zaidi ya yote

hatupaswi kupuuza maombi ya siri, kwa maana haya ndiyo maisha ya kiroho. Sala ya familia au ya hadhara pekee yake haitoshi. Maombi ya siri yanasikika kwa Mungu Ajibuye maombi.

Hakuna wakati au mahali pasipofaa kutoa ombi kwa Mungu. Katika umati wa watu mtaani, katikati ya shughuli za kibiashara, tunaweza kutuma ombi kwa Mungu na kumsihi Mungu Atupe mwongozo wa Kiungu.

Hebu roho na ivutwe na kwenda juu, ili Mungu atupe pumzi ya anga la mbinguni. Sisi tunaweza kuwa karibu sana na Mungu kiasi kwamba katika kila jaribu lisilotarajiwa mawazo yetu yatamgeukia Yeye kwa ile kawaida ya ua linavyoligeukia jua. Weka mahitaji yako, furaha yako, huzuni zako, wasiwasi wako, na hofu zako mbele za Mungu.

Wewe huwezi kumlelea; huwezi kumchosha. Yeye hachoshwi na matakwia ya watoto Wake.

Tunapata hasara tunapopuuza fursa ya kujumuika pamoja ili kuimarishana na kutiana moyo sisi kwa sisi katika utumishi kwa Mungu. Ikiwa Wakristo watashirikiana pamoja, wakisemezana kuhusu upendo wa Mungu na Kweli za thamani za ukombozi, mioyo yao wenyewe ingeburudishwa na wangeburudishana wao kwa wao.

Ni sharti tukusanyike pamoja kwa ajili ya msalaba. Kristo na Yeye aliyesulubiwa vinapaswa kuwa mada ya kutafakari, mada ya mazungumzo, na hisia zetu za furaha zaidi. Tunapaswa kuweka katika mawazo yetu kila baraka tunayoipokea kutoka kwa Mungu, na tunapotambua upendo Wake mkuu tunapaswa kuwa tayari kuamini kila kitu kilicho katika mikono ile iliyotundikwa msalabani kwa ajili yetu.

Nafsi inaweza kupaa karibu na mbingu kwa mbawa za sifa kwa Mungu. Tunapoonyesha shukrani zetu, ndivyo tukaribiavyo kuabudu na majeshi ya mbinguni. Wengi nyakati fulani wanatatizwa na mapendekezo ya kutilia shaka kuhusu Mungu. Mungu kamwe hatuambii tuamini bila kutoa uthibitisho wa kutosha wa kujenga imani yetu. Tunaweza kuficha uhalisia au ukweli Kwa namna tuwezavyo, ila sababu halisi ya shaka na kutokuamini, katika hali nyingi, ni kupenda dhambi. Ni sharti tuwe na nia ya dhati ya kujua Ukweli na utayari wa moyo kuitii.

Kabla ya kuingia kwa dhambi, Adamu alifurahia ushirika wa wazi na Muumba wake; lakini tangu mwanadamu alipojitenga yeye mwenyewe kutoka kwa Mungu kwa kutenda dhambi, jamii ya kibinadamu

imekatiliwa mbali na upendeleo huu mkuu. Kwa mpango wa ukombozi, hata hivyo, njia imefunguliwa ambayo kwayo wakaaji wa dunia wanaweza bado kuwa na uhusiano na Mbingu. Mungu amewasiliana na wanadamu kwa Roho Wake, na nuru ya Bwana imekuwa ikipandikizwa ulimwenguni kwa mafunuo, kupitia watumishi Wake wateule. “Watu watakatifu wa Mungu walinena kama walivyokuwa wakiongozwa na Roho Mtakatifu.” 2 Petro 1:21.

Wakati wa karne ishirini na tano za kwanza za historia ya mwanadamu, hapakuwa na ufunuo ulioandikwa (Musa aliishi miaka 2500 hivi baada ya Adamu kuumbwa, na ndiye mwandishi wa kwanza). Wale ambao walikuwa wamefundishwa na Mungu, waliwasilisha ujuzi wao kwa wengine, na maarifa haya yalipitishwa kutoka kwa baba kwenda kwa mwana, kupitia vizazi vilivyofuatana. Maandalizi ya Neno lililoandikwa yalianza wakati wa Musa.

Mafunuo yaliyovuviwa yalijumuishwa katika kitabu kilichovuviwa. Kazi hii iliendelea kwa muda mrefu kipindi cha miaka elfu na mia sita (1600), kutoka kwa Musa, mwanahistoria wa uumbaji na Sheria, hadi Yohana, mwandishi wa Kweli kuu za injili (takribani Kutoka 1500 KK hadi 100 BK).

Biblia inaelekeza kwa Mungu kama mwandishi Wake; lakini iliandikwa kwa mikono ya wanadamu; na kwa mtindo wake tofauti vitabu vyake mbalimbali vinawasilisha sifa za waandishi kadhaa. Kweli zilizofunuliwa zote “hutolewa kwa pumzi ya Mungu” (2 Timotheo 3:16); lakini zinaonyeshwa kwa maneno ya wanadamu, kwani si imla, ila walipewa njozi na ndoto na wakaandika kwa maneno yao. Roho Mtakatifu ametoa nuru katika akili na mioyo ya watumishi Wake. Amewapa ndoto na maono, alama na takwimu; na wale waliofunuliwa Kweli hizi, wameonyesha wenyewe mawazo hayo katika lugha ya kibinadamu.

Amri kumi zilinenwa na Mungu Mwenyewe, na ziliandikwa kwa mkono Wake Mwenyewe. Amri Kumi ni za Mungu Mwenyewe. Tunatakiwa tuwe waangalifu sana, kwani amri za mataifa yetu tunazitilia maanani, na tunapozivunja tunapata shida, sembuse Amri za Mwenyezi Mungu? Hakuna awezaye kushika sheria na kutembea na Mwenyezi Mungu isipokuwa amepata msaada kutoka Kwake, na Kila mwanadamu aombaye msaada huo, Mungu Yupu tayari kumpa.

Ngazi ya Kufika Mbinguni - Mwongozo wa Kujiifunzia

Kitabu cha Ngazi ya Kufika mbinguni, ambacho kimetafsiriwa kutoka kwenye Kingereza 'Steps to the Messiah' ni mojawapo ya vitabu vyenye mionjo ya kiroho zaidi, vinavyozingatia Masihi na kazi Yake ya ukombozi na jinsi anavyotufikisha mbinguni. Nakala ya kwanza ilichapwa mwaka wa 1891. Kitabu hiki kimetafsiriwa kwenye lugha zaidi ya 160 (hadi Mei 1985).